HUDUMA YA UPONYAJI
TIBA 8 ZA ASILI
1 Lishe Bora
2 Mazoezi
3 Maji Safi
4 Miale ya Jua
5 Kiasi
6 Hewa Safi
7 Pumziko
8 Kumwamini Mungu
Jopo la RYU

Mwito kwa Mpendwa Msomaji

Jiunge na darasa la Uandishi, Ukalimani, Kutafsiri na Uhariri WhatsApp!

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu , ushauri, na kisha Maombi yako msomaji. Kumbuka pia huduma zingine za machapisho kwa kila lugha, taifa na jamaa. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window' Sambaza Biblia popote ndiyo kauli mbiu ya muumini, Sambaza Neno la Mungu kote. Jiunge nasi katika kuandika vitabu vya kuboresha watu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ombi letu, ni unapochapa, usibadilishe chochote labda typos tu, tuwasilane kama kuna kosa la dhana au lugha! Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa rasilimali, mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Ila hapa Kwetu Afrika Mashariki, sisi tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu kwenye mada za afya, lishe, mahusiano kati ya wazazi au ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake, haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandano ya magharibi na ni mema tu, ila kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwasababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine. Kwanini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe. Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu, kwanini tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu ya nyingine, vizuri vingine, tuna wataalamu wengi wa nyimbo sasa.

Na hata vitabu vya watoto, tunahitaji watu wanaopenda watoto kufanya kazi hii kwa kushirikiana. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata, Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Wauminin wengi kuliko Amerika ya kusini, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule, mfano mdogo sana utakuwa, wanafikiri sisi ni lazima tule kimchi, taco, panzit, empanada, manicotti, tortellini, sushi, falafel, je viwanda vyetu vinatengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana, Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk. Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! Naelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya! Nategemea tunaiga mazuri tu! Na si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii, wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu, vingine vitakudodea. Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio taasisi. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao vya kuboresha jamii mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake, tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwa mamilioni kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani tafadhali usisite kutufikia na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, tuwasiliane, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa ***Maandishi*** yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku, tunaomba mashauri pia kwa kutumia

email UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au
simu -1 -908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

n

a

Huduma ya Vitabu Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

Tukishirikianana na Huduma ya ‘Mungu Anajali‘ ya Dr Mtango na Mwinjilisti Oola

Tuko Njiani kuingia kwenye Youtube tukisaidiwa na Dr Mtango kwa Maelezo ya tiba sahili -Jukwaa la Afya au Afya talk, Inspiration talk.

Samaritan Laymen Ministries of New Jersey

ELLEN G. WHITE

YALIYOMO

DIBAJI 4

SEHEMU YA 1—MMISHENARI WA KWELI WA MATIBABU/TIBA 5

SURA YA 1

KIELELEZO CHETU 6

SURA YA 2

SIKU ZA HUDUMA 12

SURA YA 3

PAMOJA NA ASILI NA PAMOJA NA MUNGU 24

SURA YA 4

MGUSO WA IMANI 28

SURA YA 5 38

UPONYAJI WA ROHO 38

SURA YA 6

KUOKOLEWA ILI KUTUMIKA 50
SEHEMU YA 2—KAZI YA TABIBU 60
SURA YA 7
USHIRIKIANO WA UUNGU NA UBINADAMU 61
SURA YA 8
DAKTARI, MWELIMISHAJI 71
SEHEMU YA 3—WAMISHONARI TIBA NA KAZI ZAO 84
SURA YA 9
KUFUNDISHA NA KUPONYA 85
SURA YA 10
KUSAIDIA WALIOJARIBIWA 100
SURA YA 11
KUFANYA KAZI NA WATU WASIO NA KIASI 108
SURA YA 12
KUSAIDIA WATU WASIO NA AJIRA/KAZI NA WASIO NA MAKAZI 118
SURA YA 13
MASKINI WASIOJIWEZA 133
SURA YA 14
HUDUMA KWA WALIO MATAJIRI 140
SEHEMU YA 4—UANGALIZI WA WAGONJWA 147
SURA YA 15
KATIKA CHUMBA CHA WAGONJWA 148
SURA YA 16
MAOMBI KWA AJILI YA WAGONJWA 152
SURA YA 17
MATUMIZI YA TIBA RAHISI 159
SURA YA 18
KUIPONYA AKILI 165
SURA YA 19
KUWASILIANA NA ASILI 182
SEHEMU YA 5—KANUNI ZA AFYA 188

SURA YA 20
USAFI WA JUMLA 189
SURA YA 21
USAFI MIONGONI MWA WAISRAELI 195
SURA YA 22
MAVAZI 202
SURA YA 23
LISHE NA AFYA 209
SURA YA 24
NYAMA KAMA CHAKULA 223
SURA YA 25
LISHE ILIYOPITILIZA 228
SURA YA 26
VICHOCHEO NA MADAWA YA KULEVYA 233
SURA YA 27
USAFIRISHAJI WA VILEO NA MAKATAZO AU MARUFUKU YALIYOWEKWA KWENYE UTUMIAJI 245
SEHEMU YA 6—NYUMBANI 254
SURA YA 28
HUDUMA YA NYUMBANI 255
SURA YA 29
WAJENZI WA NYUMBA 260
SURA YA 30
CHAGUO NA MAANDALIZI YA NYUMBA 266
SURA YA 31
MAMA 271
SURA YA 32
MTOTO 276
SURA YA 33
USHAWISHI WA NYUMBANI NA ATHARI ZAKE 284
SURA YA 34 289

ELIMU YA KWELI, MAFUNZO YA UMISHONARI 289
SEHEMU YA 7—MAARIFA MUHIMU 299
SURA YA 35
MAARIFA HALISI YA KUMJUA MUNGU-ELIMU YA KWELI 300
SURA YA 36
HATARI KATIKA UJUZI WA KUDHANIA 315
SURA YA 37
ELIMU YA UONGO NA ELIMU YA KWELI 328
SURA YA 38
UMUHIMU WA KUTAFUTA UJUZI WA KWELI 339
SURA YA 39
MAARIFA YANAYOPATIKANA KUPOKELEWA KUPITIA NENO LA MUNGU 346
SEHEMU YA 8—HITAJI LA MTENDAKAZI 354
SURA YA 40
KUFAANA KATIKA MAISHA YA KILA SIKU 355
SURA YA 41
KUWASILIANA NA WENGINE 365
SURA YA 42
MAENDELEO NA HUDUMA 376
SURA YA 43 .....
UZOEFU WA JUU 381

Waliofanikisha Kazi

(Watafsiri, Wahariri, Washauri, Wana maombi, Watu wa Teknolojia, na wengine wote waliofanikisha kazi hii). Watu elfu moja wote wataamini siku moja kwa ule ujumbe wa kimya! Sambaza kwa Marafiki, ndugu jamaa, jirani na kila mtu -Samaritan Laymen Ministries

Grace Momadi-Masaka—New Jersey, Marekani

Bahati na Ben Geliga—Boston, Marekani

Daniel Masaka—Kisii, Kenya

Sandra Barron—Kentucky, Marekani

Musa Budodi—Shinyanga, Tanzania

Niwaeli Mburuja—Suji, Tanzania

Sala Jackson—Kombeo na Umishenari TV

Paul Nsulwa—Mafinga, Tanzania

Cindy Tustch—Washington, Marekani

Mbusi Mpagalushu—Bariadi, Tanzania

Mohammed Mboi—Nairobi, Kenya

David Masaka—Pennslyvania, Marekani

Tabori Mugeta-Mara, Tanzania

Ezekiel Ojwang—Kiterere, Tanzania

Judi Mmari Mugane—Siha, Tanzania

John Mugane—Nakuru, Kenya

Grace Naka Otieno-Tennessee

Group—Vitabu vya msaada Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni na Majumbani (Swahili Self Help Books)

Faustine Momadi Mkama—Dar Es Salaam, Tanzania

Denis Chilala Momadi—Masasi, Tanzania

Petro and Elodia Tumaini—Iringa, Tanzania

Paul Momadi Masaka, New Jersey, Marekani

Faustin Tryphone Mkama—Dar, Tanzania

Gerard Makori Nyafanga—Shirati, Tanzania

Email: UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com

Maneno ya Wafasiri na Wawezeshaji Wote

Katika toleo la Kiswahili la kitabu hiki, mpangilio wa namba za Aya uko hivi; ukiachana na maelezo mengine bali kwa kuanzia hasa kwenye sura zenyewe za kitabu, kila Sura ina idadi ya Aya ambapo mwishoni mwa kila Aya kuna mafungu mawili ya namba:

- Fungu la awali ni namba ya Aya kulingana na mpangilio wa Aya katika toleo la Kiingereza (**mfano; MH 132.3**) na
- Fungu la pili ni namba ya Aya kulingana na mfuatano wa Aya toka mwanzo wa Sura hadi mwisho wa Sura hiyo (**mfano; HU Aya ya 8**).

Hivyo, ukiwa unataka kunukuu aya yo yote, anza na jina la kitabu, inafuata sura ya kitabu ilipo aya hiyo na kisha anza kuhesabu aya zote toka mwanzoni mwa sura mpaka utakapoifikia aya unayotaka kuinukuu. Hii itarahisisha kuhifadhi kumbukumbu na itakuwa rahisi kumshirikisha mtu kuhusiana na aya hiyo.

Mpangilio huu ni tofauti na kunukuu kwa kufuata ukurasa kwani utafsiri hutofautiana kwa mtu mmoja na mwingine, lakini pia uongezeaji wa maelezo fulani hufanya yaliyomo kutofautiana katika kurasa yalipo..

Aidha, katika tafsiri ya kitabu hiki, kuna maneno ambayo yametumika kwa ajili ya kuleta ufasaha zaidi ambayo wakati mwingine tumeyatumia kwa mbadilishano:

“**Aghalabu**” badala ya “**mara nyingi/mara kwa mara**,” ingawa si mara zote tumetumia neno “**aghalabu**” bali wakati mwingine tumetumia maneno “**mara kwa mara**” au “**mara nyingi**.”

Badala ya kutumia neno, “K**iungu**” yaani “**Divine**,” tumependekeza kutumia maneno, “**Mungu**, **Mwenyezi Mungu** au **Mbinguni**” ili kuleta ufasaha na heshima zaidi ya mamlaka hiyo, iliyo Kuu sana.

Wakati mwingine tumetumia maneno, **“Umishenari wa Kitabibu**,” yaani “**Medical Missionary**” kwa mbadilishano na maneno “**Umeshanari wa Tiba**)

Neno “**Must**” limetafsiriwa kama “**sharti** (kivumishi)” au “**lazima**,” hivyo tafsiri zote mbili zimetumika kwa kubadilishana

Neno “**Masaibu**” limetumika kwa kubadilishana na neno “**maafa**” au “**majanga**”

Neno “**Pure**” limetafsiriwa mahali mahali kama “**usafi**” au “**usafi wa moyo**” au “**ukamilifu**” hivyo tafsiri zote hizo zimetumika kwa kubadilishana.

Neno “**Ignorance**” limetafsiriwa kama “**ukosefu wa elimu/maarifa**” na mahali pengine limeachwa hivyo hivyo na ukali wake yaani, “Ujinga” ili kuonyesha msisitizo hasa.

Neno “**Physician**” limetafsiria kama “**tabibu**” au “**daktari**,” hivyo tafsiri zote mbili zimetumika kwa kubadilishana.

Neno, “**will** (nomino),” limetafsiriwa kama “**dhamiri**,” “**nia**,” na “**kusudi**,” na tafsiri hizi zote zimetumika kwa kubadilishana ili kuleta maana iliyo sahihi zaidi.

VIFUPISHO:

MH—Ministry of Healing

HU—Huduma ya Uponyaji

DIBAJI

Ulimwengu unaugua, na mateso yanaendelea kuzidi popote pale watoto wa wanadamu wanapofanya makazi. Kila upande watu wanatafuta faraja. MH 7.1

Si kusudi la Muumba kwamba mwanadamu walemewe na mzigo wa maumivu, kwamba utendaji wake upunguzwe au kuhafifishwa na magonjwa, kwamba nguvu zake zipungue, na maisha yake yakatiliwe mbali na magonjwa. Lakini mara nyingi sana sheria zilizowekwa na Mungu kuyathibiti na kuyaongoza maisha huvunjwa waziwazi; dhambi huingia moyoni, na mwanadamu hupoteza mtazamo wa kumtegemea Mungu, ambaye Ndiye Chanzo cha uzima na afya. Kinachofuata ni adhabu za uasi ambazo ni-maumivu, magonjwa, na kifo. MH 7.2

Kuzielewa sheria za asili zinazoongoza mwili na kuleta mazoea ya mtindo wa maisha kupatana na sheria hizi ni jukumu la kipaumbele cha kwanza kwa mwanadamu. Kuna hitaji la kuelewa mambo mengi yanayochangia furaha ya kweli—ikihusisha, nyumba yenye uchangamfu, utii wa sheria za uhai, na uhusiano ufaao na wanadamu wenzako. MH 7.3

Ugonjwa unapokuja, ni muhimu kwamba tutumie mawakala mbalimbali ambao, kwa ushirikiano na juhudi za asili, hivi vitajenga mwili na kurejesha afya. Kuna swali kubwa na la maana zaidi— nalo ni lile la uhusiano wetu na Muumba ambaye hapo awali alimpa mwanadamu uhai wake, ambaye alifanya kila mpango kwa ajili ya furaha yake yenye uendelevu, na ambaye hata leo anapendezwa mwanadamu akiwa na hali njema. MH 7.4

Katika kitabu hiki, mwandishi, kwa uwezo wa Roho ya Unabii, mwenye tajriba kubwa katika masuala ya kivitendo ya maisha, na ambaye anapendwa na wengi, na mwenye ufahamu na ujuzi adimu, ameweza kumfikia kila baba na mama kwa undani, kila mwanamume na mwanamke, walei na watu wa taaluma, hazina kubwa ya habari juu ya uhai na sheria zake, juu ya afya na matakwa yake, juu ya magonjwa na tiba zake, juu ya ugonjwa wa nafsi na zeri ya uponyaji ya Gileadi. MH 7.5

Kitabu kimeandikwa kwenye lugha iliyo wazi, sahili, nzuri, yenye kufundisha, yenye matumaini kwa waliokata tamaa, yenye kuwatia moyo na kuwashangilia wagonjwa, na yenye utulivu kwa waliochoka. Kwa miongo kadhaa amefikisha ujumbe wake wenye kusaidia mamilioni, kama ilivyotolewa mara ya kwanza na kutolewa tena katika nchi nyingi, na katika lugha kadhaa zinazoongoza ulimwenguni. MH 8.1

Ili kazi hii ambayo inatoa njia bora zaidi, itufunulie maisha sahili, matamu zaidi, yaliyojaa furaha na shangwe, yenye nafasi kwa ajili ya huduma hii ya msaada ambayo “ni heri kutoa kuliko kupokea,” iweze kutimiza misheni yake kikamilifu na matumaini ya dhati ya wachapishaji na MH 8.2

Wadhamini wa Roho ya Unabii, **Maryland, Marekani**

SEHEMU YA 1—MMISHENARI WA KWELI WA TIBA/MATIBABU

“Kuwahubiri wanyenyekevu habari njema;...kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia wafungwa uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao; kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa; ... kuwafariji wote wanaoomboleza.”

SURA YA 1

KIELELEZO CHETU

Bwana wetu Yesu Kristo alikuja katika ulimwengu huu kama mtumishi asiyechoka ili kukidhi hitaji la mwanadamu. Ali—"utwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa yetu," ili aweze kuhudumia kila hitaji la wanadamu. Mathayo 8:17. Mzigo wa ugonjwa na unyonge na dhambi, alikuja kuviondoa. Ulikuwa ni utume Wake kuwarejesha wanadamu kikamilifu; Alikuja kuwapa hao afya na amani na ukamilifu wa tabia. [MH 17.1; HU Aya ya 1]

Hali na mahitaji ya wale walioomba msaada Wake vilikuwa vya namna tofauti-tofauti, na hakuna yeyote aliyekuja Kwake akaondoka bila msaada. Kutoka Kwake ulitiririka mkondo wa nguvu za uponyaji, na watu walifanywa kuwa wazima kwenye miili na akili na roho zao. [MH 17.2; HU Aya ya 2]

Kazi ya Mwokozi haikuzuiliwa na mipaka ya muda au mahali. Huruma Yake haikujua kikomo. Kwa kiwango kikubwa sana aliendesha kazi Yake ya kuponya na kufundisha kwa mtindo huu, nao watu wakajazana kiasi kwamba hapakuwa na jengo lolote katika Palestina lililokuwa kubwa vya kutosha kupokea umati wa watu waliosongamana karibu Yake. Juu ya miteremko ya milima ya kijani kibichi ya Galilaya, katika njia za kusafiri, kando ya bahari, katika masinagogi, na kila mahali ambapo wagonjwa wangeweza kuletwa Kwake, kulikuwa na hospitali Yake hapo. Katika kila jiji, kila mji, kila kijiji, alikopita, aliweka mikono Yake juu ya wale waliokuwa wakiteseka, Naye akawaponya. Po pote palipokuwa na mioyo iliyo tayari kupokea ujumbe Wake, aliwafariji hao kwa hakikisho la pendo la Baba yao wa mbinguni. Mchana kutwa aliwahudumia wale waliomjia; jioni aliwajali wale ambao walilazimika kuhangaika na vibarua mchana ili kupata pesa kidogo kwa ajili ya mahitaji ya familia zao. [MH 17.3; HU Aya ya 3]

Yesu alibeba uzito wa kutisha wa wajibu kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Alijua kwamba kusipokuwa na badiliko thabiti katika kanuni na makusudi ya jamii ya kibinadamu, wote wangepotea. Huu ulikuwa ni mzigo wa nafsi Yake, na hakuna aliyeweza kuutambua vyema uzito uliokuwa juu Yake. Utotoni, ujanani, na katika utu uzima alitembea peke Yake. Hata hivyo mbingu ilikuwa katika uwepo Wake. Siku baada ya siku alikutana na mitihani na majaribu; siku baada ya siku alikutana na uovu na akashuhudia nguvu za huo uovu juu ya wale

ambao alikuwa akitafuta kuwabariki na kuwaokoa. Hata hivyo hakushindwa au kukata tamaa. [MH 18.1; HU Aya ya 4]

Katika mambo yote aliyaacha kikamilifu mapenzi Yake kwa muda ili ajikite kwenye utume Wake. Aliyatukuza maisha Yake kwa kufanya kila kitu ndani Yake kuwa chini ya mapenzi ya Baba Yake. Katika ujana Wake mama Yake, alipomkuta katika shule ya marabi, alisema, “Mwanangu, mbona umetutenda hivi?” Yeye Alijibu,—na jibu Lake hili ndio msingi wa kazi Yake ya maisha,—“Kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba Yangu?” Luka 2:48, 49. [MH 19.1; HU Aya ya 5]

Maisha Yake daima yalikuwa katika kujitoa dhabihu nafsi Yake. Hakuwa na makazi katika dunia hii isipokuwa pale majaliwa ya Mungu yalipotoa wema kupitia marafiki waliomkaribisha Yeye kama msafiri kwa miguu. Kwa niaba yetu alikuja kuishi maisha ya mtu fukara zaidi, na kutembea na kufanya kazi miongoni mwa wahitaji na watu watesekao. Bila kutambuliwa na kutukuzwa, aliingia na kutoka miongoni mwa watu ambao Yeye alikuwa amewafanyia mengi zaidi. [MH 19.2; HU Aya ya 6]

Siku zote alikuwa mvumilivu na mchangamfu, na wale wataabikao walimsifu kama Mjumbe wa uzima na amani. Aliona mahitaji ya wanaume na wanawake, watoto na vijana, na kwa wote hao aliwapatia mwaliko, “Njoni Kwangu.” [MH 19.3; HU Aya ya 7]

Wakati wa huduma Yake, Yesu alitumia muda mwingi zaidi kuponya wagonjwa kuliko kuhubiri. Miujiza na maajabu Yake, vilishuhudia ukweli wa Maneno Yake, kwamba hakuja kuharibu, bali kuokoa. Po pote alipokwenda, habari za rehema Yake zilimtangulia kabla ya Yeye kuwasili huko. Pale alipokuwa amepita, walengwa wa huruma Yake walikuwa wakifurahia katika uzima na kufanya majaribio (uhakikisho) wa nguvu zao mpya walizozipata. Umati ulikuwa unawazunguka wale walioponywa ili kusikia toka midomoni mwao matendo ambayo Bwana alikuwa ameyafanya. Sauti Yake ilikuwa sauti ya kwanza kabisa ambayo wengi walikuwa wameisikia (baada ya masikio kuponywa), Jina Lake lilikuwa ndilo neno la kwanza walilopata kutamka, uso Wake ndio ulikuwa wa kwanza kabisa waliowahi kuuona (kuutazama). Kwa nini basi wasimpende huyu Yesu, na kutamka sifa Zake? Alipopitia kwenye miji na majiji alikuwa kama mkondo wa maji (nishati), ukitawanya uzima na furaha. [MH 19.4; HU Aya ya 8]

“Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali,

Njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani,

Galilaya ya mataifa, Watu wale waliokaa katika giza

Wameona mwanga mkuu,

Nao waliokaa katika nchi na uvuli wa mauti

Mwanga umewazukia.” Mathayo 4:15, 16. [MH 20.1; HU Aya ya 9]

Mwokozi alifanya kila kazi ya uponyaji kuwa nafasi na tukio la kupandikiza kanuni takatifu katika akili na roho. Hili ndilo lilikuwa kusudi la kazi Yake. Alitoa baraka za kidunia, ili apate kuelekeza mioyo ya watu kuipokea injili ya neema Yake. [MH 20.2; HU Aya ya 10]

Kristo angeweza kuchukua nafasi ya juu zaidi miongoni mwa walimu wa taifa la Kiyahudi, ila Yeye alipendelea zaidi kupeleka injili kwa maskini. Alikwenda mahali hadi mahali, ili wale walio katika njia kuu na vinjia vidogo, mahali pale watu wasipoweza kufikiwa kwa urahisi, ili wapate kusikia yale maneno ya kweli. Kando ya bahari, milimani, na katika njia za mji, na katika sinagogi, sauti Yake ilisikika ikifafanua Maandiko. Mara nyingi alifundisha katika ua wa nje wa hekalu, ili watu wa mataifa wapate kusikia maneno Yake. [MH 20.3; HU Aya ya 11]

Maelezo Yake Kristo kuhusiana na Maandiko Yalikuwa tofauti na yale yaliyotolewa na waandishi na Mafarisayo, na hilo likavuta usikivu wa watu. Marabi walijikita kwenye mapokeo, juu ya nadharia za wanadamu na uvumi (nadharia zisizo na ushahidi). Mara nyingi kile ambacho wanadamu walikuwa wamefundisha na kuandika kuhusu Maandiko kiliwekwa mahali pa Maandiko yenyewe. Somo kuu la mafundisho ya Kristo lilikuwa Neno la Mungu. Daima alikabiliana na waulizaji maswali, kwa maneno ya wazi, “Imeandikwa” “Je, Maandiko yasemaje?” “Wasomaje?” Katika kila fursa wakati hamu ilipoamshwa na aidha rafiki au adui, alilinena Neno kwao. Kwa uwazi na nguvu alitangaza ujumbe wa injili. Maneno Yake yalitoa mafuriko ya mwanga juu ya mafundisho ya wazee wa imani na manabii, kisha wanadamu waliyaona Maandiko kama ufunuo mpya. Wasikilizaji Wake hawakuwahi kamwe kutambua ndani ya Neno la Mungu maana ya kina namna hii. [MH 21.1; HU Aya ya 12]

Kamwe hakukuwahi kuwapo mwinjilisti kama Kristo. Alikuwa Mkuu wa enzi ya mbinguni, lakini alijinyenyekeza akachukua asili yetu, ili apate kukutana na wanadamu pale walipokuwa. Kwa watu wote, matajiri na maskini, walio huru na waliofungwa, Kristo, Mjumbe wa agano, alileta habari za wokovu. Umaarufu Wake kama Mponyaji Mkuu ulienea Palestina yote. Wagonjwa walikwenda kumngoja mahali pale ambapo angepita, ili waweze kumwomba msaada. Huku wengi wakija wakiwa na matamanio ya kusikia Maneno Yake na kupokea mguso wa mkono Wake. Hivyo alikwenda mji na mji, akihubiri injili na kuponya wagonjwa—Mfalme wa utukufu akiwa katika vazi la hadhi ya chini la ubinadamu. [MH 22.1; HU Aya ya 13]

Alihudhuria kwenye maadhimisho ya sherehe kuu za kila mwaka za taifa, na kwa umati uliomezwa na shughuli za maadhimisho ya mwonekano wa nje, alinena mambo ya mbinguni, akiuleta umilele (maisha ya milele baada ya dhambi) karibu yao. Kwa wote aliileta hazina toka katika ghala la hekima. Alizungumza nao kwa lugha rahisi sana kiasi kwamba hawakuweza kushindwa

kuelewa. Kwa njia Zake zilizokuwa zenye upekee, aliwasaidia wote waliokuwa katika huzuni na mateso. Kwa huruma, uungwana wenye neema, aliihudumia kila nafsi iliyokuwa na ugonjwa wa dhambi, kwa kuiletea uponyaji na nguvu. [MH 22.2; HU Aya ya 14]

Mkuu Huyu wa waalimu wote, alitafuta njia ya kuwafikia watu kupitia kuleta kwao mambo waliyoyajua vyema. Aliihubiri kweli kwa njia ambayo baada ya hapo ilikuwa rahisi kwa wasikilizaji Wake kuifungamanisha na kumbukumbu zao takatifu zaidi na huruma. Alifundisha kwa njia ambayo iliwafanya kuhisi ukamilifu wa utambulisho Wake pamoja na matamanio yao na furaha. Maagizo Yake yalikuwa ya moja kwa moja, vielelezo vyake vilikuwa vya kufaa sana, maneno Yake yalikuwa ya huruma na uchangamfu, kiasi kwamba wasikilizaji Wake walivutiwa. Urahisi na unyofu ambao aliwahubiri wahitaji, ulitakasa kila neno. [MH 23.1; HU Aya ya 15]

Ni maisha gani hayo yenye shughuli nyingi ambayo Kristo aliishi! Siku baada ya siku aliweza kuonekana akiingia kwenye makazi yenye hadhi ya chini, yenye uhitaji na huzuni, akitamka tumaini kwa watu waliolemewa na shida na amani kwa wenye huzuni. Mwokozi Mwenye neema, mpole, mwenye huruma, alizunguka huku na kule akiwainua waliolemewa na mizigo ya masumbufu na kuwafariji walio na huzuni. Po pote alipokwenda, alibeba baraka. [MH 24.1; HU Aya ya 16]

Alipokuwa akiwahudumia maskini, Yesu alijifunza pia kutafuta njia za kuwafikia matajiri. Alitafuta kufahamiana na yule Mfarisayo tajiri na huyu Myahudi mwungwana na pia mtawala mrumi. Alikubali mialiko yao, akahudhuria karamu zao, akitafuta kutambua shauku zao na kazi zao, ili apate kuifikia mioyo yao, na kuwafunulia ule utajiri usioharibika. [MH 24.2; HU Aya ya 17]

Kristo alikuja katika ulimwengu huu ili kuonyesha kwamba kwa kupokea nguvu toka juu, mwanadamu anaweza kuishi maisha yasiyochafuliwa (yenye usafi wa moyo). Kwa uvumilivu usiochoka na huruma yenye msaada, alikutana na watu katika mahitaji yao. Kwa mguso mtulivu wa neema alifukuza wasiwasi na mashaka toka kwenye mioyo ya watu, akibadilisha uadui kuwa upendo, na kutoamini kuwa na imani na ujasiri. [MH 25.1; HU Aya ya 18]

Aliweza kuzungumza na yule aliyependezwa Naye, “Nifuate,” na yule aliyeambiwa alisimama na kumfuata. Mvuto wa kuupenda na kuufurahia ulimwengu ulivunjwa. Kwa kusikika sauti Yake, roho ya uchoyo na matamanio ya ukuu yalikimbia toka moyoni, na watu hawa walisimama, wakiwa huru, kumfuata Mwokozi. [MH 25.2; HU Aya ya 19]

Upendo wa Kidugu

Kristo hakuwa na ubaguzi kwa kutofautisha watu kutokana na taifa, wadhifa au imani. Waandishi na Mafarisayo walitamani kuzifanya karama za mbinguni kuwa za maeneo yao na kwa taifa lao tu, na kuwatenga ulimwenguni wengine

ambao ni sehemu ya familia ya Mungu. Lakini Kristo alikuja kubomoa kila ukuta wa utengano. Alikuja kuonyesha kwamba zawadi Yake ya rehema na upendo, kama ilivyo hewa, mwanga, au matone ya mvua yaburudishayo dunia, haiwekewi mipaka aukufungiwa kwa watu fulani tu. [MH 25.3; HU Aya ya 20]

Maisha ya Kristo yalianzisha dini ambayo ndani yake kulikuwa hakuna matabaka, dini ambayo kwayo Myahudi na Mtu wa mataifa, yule aliye huru ama mfungwa, wanaunganishwa katika udugu wa pamoja, nao wanakuwa sawa mbele za Mungu. Hakuna suala la sera lililoathiri harakati Zake. Hakuwatendea watu kwa ubaguzi, na hivyo hakuweka tofauti kati ya majirani na wageni, marafiki na maadui. Kile kilichovutia moyo Wake ilikuwa ni roho yenye kiu ya maji ya uzima. [MH 25.4; HU Aya ya 21]

Hakumpita mwanadamu ye yote kwa kumwona kuwa hana thamani, bali alitafuta kutumia tiba yenye uponyaji kwa kila roho. Katika kundi lo lote lile alilokuwamo, alitoa somo linalolingana na hali, tukio na mazingira. Kila upuuziaji au matusi yaliyoonyeshwa na wanadamu kwa wanadamu wenzao vilimfanya tu Yeye kutambua kwa kina zaidi hitaji lao la huruma Yake ya Kiungu na Kibinadamu. Alitafuta kuwatia moyo kwa kuwapa tumaini, wale waliokuwa wakatili na wasiofaa, akiweka mbele yao hakikisho kwamba wanaweza kuwa watu wasio na lawama na wasiodhuru wengine, wakijipatia tabia ambayo ingewadhihirisha kuwa wana wa Mungu. [MH 25.5; HU Aya ya 22]

Mara nyingi alikutana na wale ambao walikuwa wametumbukia chini ya udhibiti wa Shetani, na ambao hawakuwa na uwezo wa kutoka kwenye mtego wake. Kwa mtu kama huyo, aliyevunjika moyo, mgonjwa, aliyejaribiwa, aliyeanguka, Yesu angezungumza maneno ya huruma nyororo, maneno ambayo yalihitajika na ambayo yangeweza kueleweka. Alikutana na wengine waliokuwa wakipigana vita vya ukaribu na adui wa roho. Hawa aliwatia moyo kuwa wavumilivu, akiwahakikishia kwamba watashinda; kwa maana malaika wa Mungu walikuwa upande wao nao wangewashindia. [MH 26.1; HU Aya ya 23]

Aliketi kama mgeni mtukufu katika meza ya watoza ushuru, kwa huruma na ukarimu Wake katika mahusiano na jamii akionyesha kwamba alitambua hadhi ya ubinadamu; na watu wakatamani kustahili kupata ujasiri Wake kwao. Mioyoni mwao yenye kiu maneno Yake yalianguka yakiwa na nguvu takatifu yenye kuleta uzima. Misukumo mipya iliamshwa, na kwa watu hawa waliotengwa na jamii, kwao ulifunguka mlango wa uwezekano wa maisha mapya. [MH 26.2; HU Aya ya 24]

Ingawa alikuwa Myahudi, Yesu alifungamana kwa uhuru pamoja na Wasamaria, akipinga na kutojali desturi za Kifarisayo katika taifa Lake. Akikabiliana na chuki yao alikubali ukarimu wa watu hawa waliokuwa wanadharauliwa (wanatwezwa). Alilala pamoja nao sakafuni, alikula pamoja nao mezani mwao,—akila chakula kilichoandaliwa na kuletwa na wao—alifundisha vijijini

mwao, na aliwatendea kwa ukarimu wa juu na wa heshima. Na akiwa anaivuta mioyo yao Kwake kwa njia ya kuwahurumia, neema Zake za mbinguni ziliwaletea wokovu ambao Wayahudi waliukataa. [MH 26.3; HU Aya ya 25]

Huduma Binafsi

Kristo hakupuuza fursa yo yote ya kutangaza injili ya wokovu. Hebu sikiliza maneno Yake ya kushangaza kwa mwanamke yule wa Samaria. Alikuwa ameketi kando ya kisima cha Yakobo, alipokuja mwanamke kuteka maji. Kwa mshangao wake mwanamke, alimwomba msaada. Akasema, “Nipe maji ninywe,” Alitaka kutuliza kiu, na pia alitamani kufungua njia ambayo kwayo angeweza kumpa mwanamke maji ya uzima huyu mlengwa. “Imekuwaje,” akasema yule mwanamke, “Wewe uliye Myahudi waomba maji kwangu, nami ni mwanamke Msamaria? kwa maana Wayahudi hawachangamani na Wasamaria.” Yesu akajibu, “Kama ungalijua karama ya Mungu, na ni nani akuambiaye maneno haya, Nipe ninywe; ungalimwomba, Naye angalikupa maji yaliyo hai.... Kila atakayekunywa maji haya ataona kiu tena: lakini yeyote atakayekunywa maji nitakayompa Mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele.” Yohana 4:7-14. [MH 27.1; HU Aya ya 26]

Kristo alionyesha shauku kubwa kiasi gani kwa mwanamke huyu mmoja! Jinsi gani maneno Yake yalivyokuwa ya dhati na fasaha! Pale huyu mwanamke aliposikia hayo, aliuacha mtungi wake, na akaenda mjini, akiwaambia rafiki zake, Njoni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda; huyu siye Kristo? Tunasoma kwamba “wengi wa Wasamaria wa mji huo wakamwamini.” Mstari wa 29, 39. Na ni nani anayeweza kukadiria ushawishi uliofanywa na maneno haya ya Kristo kwa ajili ya kuokoa roho tangu siku hiyo alipozungumza na mwanamke msamaria kisimani, mpaka leo? [MH 28.1; HU Aya ya 27]

Po pote ambapo mioyo imefunguliwa ili kupokea ile kweli, Kristo Yu tayari kuwafundisha watu hao. Anawafunulia Baba kwao, na huduma inayokubalika Kwake Yeye asomaye moyo. Kwa watu kama hawa, Hatumii mifano/vielelezo. Kwao, kama kwa mwanamke huyu kisimani, huwaambia, “Mimi ninayesema nawe Ndiye. [MH 28.2; HU Aya ya 28]

SURA YA 2

SIKU ZA HUDUMA

Katika nyumba ya mvuvi huko Kapernaumu, mama wa mke wa Petro, yaani mkwewe, amelala akiugua “homa kali,” na “Nao wakamwambia habari zake.” Yesu “akamgusa mkono, na homa ikamwacha,” na akasimama na akaenda kumtumikia Mwokozi na wanafunzi Wake. Luka 4:38; Marko 1:30; Mathayo 8:15. [MH 29.1; HU Aya ya 1]

Habari hizi zilisambaa kwa kasi. Muujiza ulikuwa umefanyika siku ya Sabato, na kwa kuwaogopa marabi watu hawakuthubutu kuja kuponywa mpaka pale jua lilipozama. Ndipo baada ya hapo wakaaji wa jiji hilo walitoka majumbani, madukani, sokoni, nao wakasonga mbele kuelekea kwenye makao ya hali ya chini ambayo yalimsitiri Yesu. Wagonjwa waliletwa Kwake wakiwa kwenye machela, wengine walikuja wakiwa wanajikongoja na fimbo, au, wakisaidiwa kujongea na marafiki, walijikongoja kwa unyonge kuelekea alipo Mwokozi. [MH 29.2; HU Aya ya 2]

Saa baada ya saa walikuja na kwenda; kwa maana hakuna aliyeweza kujua kama kesho yake wangemkuta Yule Mponyaji akiwa angali bado yu kati yao. Kapernaumu ilikuwa haijawahi kamwe kushuhudia siku kama hii. Angahewa lilijaa sauti ya ushindi na kelele za kufunguliwa. [MH 29.3; HU Aya ya 3]

Yesu hakukoma kazi Yake mpaka mgonjwa wa mwisho alipoponywa (alipopata ahueni). Ilikuwa ni usiku sana wakati umati ulipotawanyika, na ukimya ukatanda kwenye nyumba ya Simoni. Siku hiyo ndefu yenye kusisimua ikapita, na Yesu akatafuta pumziko. Lakini jiji lilipokuwa limegubikwa na usingizi, Mwokozi, “kesho yake alfariji, kabla hapajapambazuka,” “akaamka na akaenda mahali pa faragha, akasali.” Marko 1:35. [MH 29.4; HU Aya ya 4]

Asubuhi na mapema Petro na wenzake walimwendea Yesu, wakimwambia kwamba tayari watu wa Kapernaumu walikuwa wanamtafuta. Kwa mshangao walisikia maneno ya Kristo, “Imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa

Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nalitumwa” Luka 4:43. [MH 30.1; HU Aya ya 5]

Katika msisimko ambao ulienea Kapernaumu kulikuwa na hatari kwamba lengo la utume Wake lingepoteza mwelekeo. Yesu hakutosheka kuwavutia watu Kwake kama tu mtenda maajabu/miujiza au kama tu mponyaji wa magonjwa ya kimwili. Alikuwa akitafuta kuwavuta watu Kwake kama Mwokozi wao. Japokuwa watu walikuwa na matamanio ya kuamini kwamba Yeye alikuwa amekuja kama mfalme ili kusimamisha utawala wa kidunia, Yeye alitamani kugeuza mawazo yao kutoka katika mambo ya kidunia na kwenda kwenye yale yaliyo ya kiroho. Mafanikio ya kidunia peke yake yangeizuia kazi Yake. [MH 31.1; HU Aya ya 6]

Ule mshangao mkubwa wa umati usiojali uliikera roho Yake. Hakuna kujitukuza kulikochanganyika na maisha Yake. Heshima ambayo ulimwengu unatoa kwa wenye cheo, mali, au talanta ilikuwa ngeni kwa Mwana wa Adamu. Yesu hakutumia mbinu yo yote ile ambayo wanadamu hutumia ili kupata utii au kuamrisha heshima. Karne nyingi kabla ya kuzaliwa Kwake ilikuwa imetabiriwa kuhusiana na Yeye, “Hatalia, wala hatapaza sauti Yake, wala hatatoa sauti Yake katika njia kuu. Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima; ataitokeza hukumu kwa Kweli.” Isaya 42:2, 3. [MH 31.2; HU Aya ya 7]

Mafarisayo walitafuta kujulikana kwa kujitofautisha wenyewe na wengine kwa taratibu zao za kidini zenye umakini na ibada za kujionyesha na misaada yao kwa wahitaji. Walithibitisha bidii yao kwa ajili ya dini kwa kuifanya kuwa mada ya mjadala. Migogoro kati ya madhehebu yenye kupingana ilikuwa mikubwa na ya muda mrefu, na haikuwa jambo la ajabu kusikia mitaani sauti ya mabishano yenye hasira kutoka kwa wasomi wa sheria. [MH 32.1; HU Aya ya 8]

Maisha ya Yesu yalikuwa tofauti kabisa na watu wengine. Hakuna tendo lililofanyika katika maisha, la mabishano yenye makelele, la ibada ya kujionyesha, hayakuwa, la kupigiwa makofi au kushangiliwa na watu. Kristo alifichwa ndani ya Mungu, na Mungu alifunuliwa katika tabia ya Mwanawe. Ni kwa ufunuo huu ndio Yesu alitamani akili za watu zielekezwe. [MH 32.2; HU Aya ya 9]

Jua la Haki halikuchomoza ulimwenguni kwa ufahari, ili kuzishtua na kuzishangaza hisia za watu kwa utukufu Wake. Kuhusiana na Kristo imeandikwa “kutokea Kwake ni yakini kama asubuhi.” Jua huchomoza taratibu, likitawanya giza na kuuamsha ulimwengu kutoka usingizini. Ndivyo Jua la Haki lilivyochomoza, “likiwa na uponyaji katika mbawa Zake.” Malaki 4:2. [MH 32.3; HU Aya ya 10]

“Tazama mtumishi Wangu nimtegemezaye; mteule wangu, ambaye nafsi Yangu imependezwa naye; nimetia roho Yangu juu yake; naye atawatolea mataifa hukumu.”

Isaya 42:1. [MH 33.1; HU Aya ya 11]

“Maana Umekuwa ngome ya maskini,

Ngome ya mhitaji katika dhiki yake,

Mahali pa kukimbilia wakati wa tufani, Kivuli wakati wa hari.”

Isaya 25:4. [MH 33.2; HU Aya ya 12]

“Mungu Bwana anena,

Yeye aliyeziumba mbingu, na kuzitandaza;

Aliyeitandaza nchi na mazao yake; Yeye awapaye pumzi watu walio juu yake;

Yeye awapaye pumzi watu walio juu yake,

Na roho kwa hao waendao ndani yake;

Mimi, Bwana, nimekuita katika haki,

Nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu. Nuru ya Mataifa;

Kuyafunua macho ya vipofu,

Kuwatoa gerezani waliofungwa,

Kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa.

Isaya 42:5-7. [MH 33.3; HU Aya ya 13]

“Nitawaleta vipofu katika njia wasiyoijua;

Nitawaongoza katika mapito wasiyoyajua;

Nitafanya giza kuwa nuru mbele yao,

Na mahali palipopotoka kuwa pamenyoka.

Mambo haya nitawatenda, wala sitawaacha.”

Kifungu cha 16. [MH 33.4; HU Aya ya 14]

"Mwimbieni Bwana wimbo mpya,

Na sifa Zake tokea miisho ya dunia,

Ninyi mshukao baharini, na vyote vilivyomo;

Visiwa, na wakaao humo.

Jangwa na miji yake na ipaze sauti zao,

Vijiji vinavyokaliwa na Kedari;

Na waimbe wenyeji wa Sela,

Wapige kelele toka vilele vya milima.

Na wamtukuze Bwana,

Na kutangaza sifa Zake visiwani.." Mafungu ya 10-12. [MH 33.5; HU Aya ya 15]

"Imbeni, enyi mbingu; kwa kuwa Bwana ametenda hayo;

Pigeni kelele, enyi pande za chini za nchi;

Pazeni nyimbo, enyi milima,

Nawe msitu, na kila mti ulio ndani yake;

Kwa kuwa Bwana amemkomboa Yakobo,

Na atajitukuza katika Israeli.

Isaya 44:23. [MH 33.6; HU Aya ya 16]

Kutoka kwenye gereza la chini ya ardhi la Herode, akiwa katika hali ya kukata tamaa na kufadhaika kuhusu kazi ya Mwokozi, Yohana Mbatizaji alitazama na kungojea, kisha akawatuma wanafunzi wake wawili kwa Yesu na ujumbe huu: MH 34:1; HU Aya ya 17]

"Je! Wewe Ndiye Ujaye, au tumtazamie mwingine?" Mathayo 11:3. [MH 34.2; HU Aya ya 18]

Mwokozi hakujibu mara moja swali la wanafunzi. Walipokuwa wakisimama na kustaajabia ukimya Wake, wale waliokuwa wanateseka na wenye shida

walikuwa wanaendelea kumjia. Sauti ya Mponyaji Mkuu (Tabibu Mkuu) ilipenya kwenye sikio la kiziwi. Neno, na mguso wa mkono Wake, vikafungua macho ya vipofu ili watazame nuru ya mchana, mandhari ya uumbaji wa Mungu, nyuso za marafiki, na uso wa Mwokozi. Sauti Yake ilifika masikioni mwa wafu, nao wakaamka wakiwa na afya njema na nguvu. Wenye pepo waliopooza na kushindwa kujongea walitii Neno Lake, wenda wazimu wao ukawatoka, nao wakamwabudu. Wakulima maskini na vibarua wa kazi, ambao waliepukwa na kukataliwa na marabi kama watu najisi, walikusanyika kumzunguka, Naye alizungumza nao maneno ya uzima wa milele. [MH 34.3; HU Aya ya 19]

Nayo siku ikasogea mbele, wanafunzi wa Yohana walikuwa wakiona na kusikia yote. Hatimaye Yesu akawaita Kwake, akawaagiza waende kumwambia Yohana yale waliyoyaona na kuyasikia, akiongeza, “Heri mtu yeyote asiyechukizwa Nami. Kifungu cha 6. Wanafunzi wakabeba ujumbe huo, nao ulitosha. [MH 35.1; HU Aya ya 20]

Yohana alikumbuka unabii kuhusu Masihi, “BWANA amenitia mafuta kuwahubiri wanyenyekevu habari njema; Amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao; kutangaza mwaka wa Yehova aliyekubaliwa, na ... kuwafariji wote wanaoomboleza” Isaya 61:1, 2. Yesu wa Nazareti Ndiye Aliyeahidiwa. Ushahidi wa Uungu Wake ulionekana katika huduma Yake kwa mahitaji ya wanadamu wanaoteseka. Utukufu Wake ulionyeshwa kwa kujishusha Kwake ili kufikia hali yetu ya chini. [MH 35.2; HU Aya ya 21]

Kazi za Kristo hazikumtangaza Yeye kama Masihi tu, bali zilionyesha ni kwa namna gani ufalme Wake ungesimikwa na kuthibitika. Kwa Yohana ulifunuliwa ukweli ule uliomjia Eliya kule jangwani, pale “upepo mkubwa na wenye nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo huo tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika tetemeko hilo; na baada ya tetemeko hilo kukawa na moto; lakini Bwana hakuwamo ndani ya moto ule.” na baada ya moto, Mungu alizungumza na nabii huyo kwa sauti ndogo, tulivu. 1 Wafalme 19:11, 12. Ndivyo Yesu alipaswa kufanya kazi Yake, si kwa kupindua viti vya enzi na falme, si kwa fahari na kujionyesha kwa nje, bali kwa kunena mioyoni mwa watu kwa maisha ya rehema na kujitoa sadaka (kujidhabihu). [MH 36.1; HU Aya ya 22]

Ufalme wa Mungu hauji kwa kuchunguza au maonyesho ya nje. Bali huja kwa njia ya upole wa uvuvio wa Neno Lake, kupitia utendaji kazi wa ndani wa Roho Wake, ushirika wa roho pamoja na Yeye aliye uzima wa hiyo roho. Udhihirisho mkuu zaidi wa uweza Wake unaonekana katika asili ya mwanadamu inayoletwa kwenye ukamilifu wa tabia ya Kristo. [MH 36.2; HU Aya ya 23]

Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa nuru ya ulimwengu; lakini Mungu hawaagizi kwamba watie jitihada ili waweze kuangaza. Hakubaliani na jitihada

zo zote za kuwaridhisha wenyewe katika kufanya maonyesho (kujionyesha) ya wema wa hali ya juu. Anatamani kwamba nafsi zao zijazwe na kanuni za mbinguni; na ndipo, wanapokutana na ulimwengu, wataiangaza nuru iliyo ndani yao. Uaminifu wao ulio thabiti katika kila tendo la maisha utakuwa njia ya kuangaza. [MH 36.3; HU Aya ya 24]

Utajiri au cheo cha juu, vifaa vya gharama, majengo au samani, si muhimu katika kuendeleza kazi ya Mungu; wala mafanikio ambayo yanashangiliwa kwa makofi na wanadamu na kuleta ubatili. Maonyesho ya kilimwengu, hata yawe makubwa au ya kushangaza kwa kiasi gani, hayana thamani machoni pa Mungu. Juu ya yale yaonekanayo kwa macho na ya muda, Yeye huthamini yale yasiyoonekana na ya milele. Ya kwanza ni ya thamani ikiwa tu yanaelezea yale ya mwisho. Maonyesho bora zaidi ya sanaa hayana uzuri unaoweza kulinganishwa na uzuri wa tabia, ambao ni tunda la utendaji kazi wa Roho Mtakatifu ndani ya roho. [MH 36.4; HU Aya ya 25]

Mungu alipomtoa Mwanawe kwa ulimwengu wetu, aliwajalia wanadamu utajiri usioharibika—utajiri ambao ukilinganisha na ule wa hazina ya wanadamu tangu mwanzo ni ubatili. Kristo alikuja duniani na kusimama mbele ya watoto wa wanadamu akiwa na upendo uliosheheni wa milele, na hii ndiyo hazina ambayo, kwa kuunganishwa kwetu Naye, hatuna budi kupokea, kuangaza, na kutoa. [MH 37.1; HU Aya ya 26]

Juhudi za kibinadamu zitakuwa na ufanisi katika kazi ya Mungu, sawasawa na kujitoa wakfu kwa mtenda kazi—kwa kudhihirisha uweza wa neema ya Kristo kuyabadilisha maisha. Hatuna budi kutofautishwa na ulimwengu kwa sababu Mungu ameweka muhuri Wake juu yetu, kwa sababu anadhihirisha ndani yetu tabia Yake Mwenyewe ya upendo. Mkombozi wetu hutufunika kwa haki Yake. [MH 37.2; HU Aya ya 27]

Katika kuchagua wanaume na wanawake kwa ajili ya utumishi Wake, Mungu hawaulizi kama wana mali ya dunia, elimu, au ufasaha. Yeye huuliza, “Je, wanatembea kwa unyenyekevu hata nipate kuwafundisha njia Yangu? Je, Ninaweza kuyaweka maneno Yangu katika vinywa vyao? na Je, wataniwakilisha Mimi?” [MH 37.3; HU Aya ya 28]

Mungu anaweza kumtumia kila mtu kwa kadiri tu anavyoweza kuweka Roho Wake katika hekalu la roho. Kazi ile ambayo ataikubali ni ile kazi inayoakisi sura Yake. Wafuasi Wake wanapaswa kubeba, kama vitambulisho vyao kwa ulimwengu, sifa zisizoweza kufutika au kusahulika, za kanuni Zake za kutokufa. [MH 37.4; HU Aya ya 29]

“Atawakusanya Wana-Kondoo Kwa Mkono Wake”

Yesu alipokuwa anaendelea kuhudumu kwenye barabara za miji, akina mama waliokuwa na watoto wagonjwa na waliokuwa wanakaribia kufa mikononi mwao, walisogea mbele katikati ya umati, wakitafuta kufika mahali ambapo Yeye angewaona. [MH 38.1; HU Aya ya 30]

Watazame wakina mama hawa, nyuso zao zikiwa zimepauka, kwa kukosa afya, na wakiwa wamechoka, na karibu kukata tamaa, lakini wamedhamiria, nao wanajikaza na kuvuta subira. Wakiwa wamebeba mzigo wao wa mateso, wanamtafuta Mwokozi. Wanaposongamana nyuma kutokana na umati unaoongezeka, Kristo anawajia hatua kwa hatua, mpaka anafika karibu yao. Matumaini yanabubujika mioyoni mwao. Machozi yao ya furaha yanaanguka pale Yesu anapowajali, na kuyaona macho Yake yakionyesha huruma na upendo. [MH 38.2; HU Aya ya 31]

Akimchagua mmoja katika kundi, Mwokozi anashawishi ujasiri wa huyo, kwa kusema, “unataka nikutendee nini wewe?” yule mama akalia kwa uchungu kuhusu hitaji lake kubwa, “Bwana, Yaani kama Wewe ungemponya mtoto wangu.” Kristo akamchukua mtoto mdogo kutoka mikononi mwake yule mama, na ugonjwa unakimbia kwa kuguswa Naye. Ukungu wa mauti umetoweka; mkondo wa uzima unapitia mishipani; misuli inakuwa na nguvu. Maneno ya faraja na amani yananenwa kwa huyu mama; na kisha kesi nyingine yenye umuhimu pia, inapelekwa Kwake. Mara nyingine Kristo anatumia uweza Wake wa kuhuisha, na wote wanampa sifa, utukufu na heshima Yeye afanyaye mambo ya ajabu. [MH 38.3; HU Aya ya 32]

Sisi wanadamu huwa tunafikiri sana juu ya ukuu wa maisha ya Kristo. Twazungumza juu ya mambo ya ajabu aliyoyatimiza, na miujiza aliyoifanya. Lakini umakini Wake kwa mambo ambayo kwa kawaida yanahesabiwa kuwa ni madogo, ndio uthibitisho wa juu zaidi kuhusu ukuu Wake. [MH 39.1; HU Aya ya 33]

Miongoni mwa Wayahudi ilikuwa ni desturi yao, kuwaleta watoto wao kwa rabi fulani, ili aweke mikono yake juu yao na kuwabariki; lakini wanafunzi walifikiri kwamba kazi Yake Mwokozi ni muhimu sana, nayo haikupaswa kukatizwa kwa kufanya hivyo. Pale akina mama walipokuja wakitaka Yesu awabarikie watoto wao wadogo, wanafunzi waliwatazama kwa kutopendezwa na jambo hili. Walifikiri kuwa watoto hawa walikuwa wachanga sana kunufaika kwa ujio wao kwa Yesu, na wakahitimisha kwamba Yeye angechukizwa na uwepo wa hawa watoto. Lakini Mwokozi alielewa utunzaji, masumbufu na mzigo wa akina mama ambao walikuwa wakitafuta kuwalea watoto wao kufuatana na Neno la Mungu. Alikuwa amesikia maombi yao. Yeye Mwenyewe aliwavuta ili wawe kwenye uwepo Wake binafsi. [MH 40.1; HU Aya ya 34]

Mama mmoja pamoja na mtoto wake walitoka nyumbani kwao na kwenda kumtafuta Yesu. Akiwa njiani kulekea huko, alimwambia jirani shughuli inayomtoa nyumbani kwake, naye jirani akatamani Yesu awabariki watoto wake

pia. Ndivyo wakina mama kadhaa walikuja pale kwenye mkutano pamoja, na watoto wao wadogo. Baadhi ya watoto walikuwa wamevuka umri wa utoto uchanga hadi utoto na sasa walikuwa kwenye ujana. Pale akina mama walipotangaza matamanio yao, Yesu, hali moyo wake ukiwa umejaa huruma na majonzi, alilisikia ombi lao. Lakini alingoja kuona wanafunzi watawatendeaje watu hawa. Alipowaona wanafunzi wakiwakemea akina mama na kuwaambia waondoke zao, wakifikiri wanamfanyia Yeye wema, Yeye aliwaonyesha kosa lao, akisema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie; kwa maana ufalme wa Mungu ni wao.” Marko 10:14. Naye akawachukua watoto mikononi Mwake, akiweka mikono Yake juu yao, na kuwapa baraka ambazo walikuja kuzitafuta. [MH 41.1; HU Aya ya 35]

Akina mama walifarijika. Walirudi majumbani mwao wakiwa wameimarishwa na kubarikiwa na maneno ya Kristo. Walitiwa moyo kubeba mzigo wao kwa uchangamfu mpya na kufanya kazi kwa matumaini kwa ajili ya watoto wao. [MH 41.2; HU Aya ya 36]

Kama maisha ya baadaye ya kundi hilo dogo yangefunuliwa mbele yetu, tungewaona akina mama hawa wakiwakumbusha watoto wao tukio la siku hiyo, na kurudia kwao maneno ya upendo ya Mwokozi. Twapaswa kuona jinsi ambavyo kumbukumbu ya maneno haya ilivyojirudia kwenye akili zao mara kwa mara, ikiwalinda dhidi ya kutoka katika njia iliyowekwa kwa ajili ya wale waliokombolewa na Bwana. [MH 41.3; HU Aya ya 37]

Hata hivi leo Kristo ni Mwokozi Mwenye huruma sawa na wakati ule alipotembea kati ya wanadamu. Yeye ni msaidizi wa akina mama sasa kama siku zile alipowakusanya watoto mikononi Mwake huko Yudea. Watoto walio majumbani mwetu wamenunuliwa kwa damu Yake vivyo hivyo kama ilivyokuwa kwa watoto wale zamani zile. [MH 41.4; HU Aya ya 38]

Yesu ajua mzigo wa moyo wa kila mama. Yeye aliyekuwa na mama aliyehangaika na umaskini na ufukara, anamhurumia kila mama katika shughuli zake. Yeye aliyefunga safari ndefu ili kuutuliza moyo wa mwanamke Mkananayo, atafanya mengi kama alivyofanya siku zile alipokuwa duniani, kwa ajili ya akina mama wa siku hizi. Yeye aliyemrudishia mjane wa Naini mwanawe wa pekee, na hata katika maumivu ya uchungu Wake pale msalabani alimkumbuka mama Yake Mwenyewe, leo anaguswa na huzuni ya mama. Katika kila huzuni na kila hitaji, atafariji na kusaidia. [MH 42.1; HU Aya ya 39]

Wakina mama na waje kwa Yesu wakiwa na fadhaa zao. Nao watapata neema ya kutosha kuwasaidia katika malezi ya watoto wao. Malango yako wazi kwa kila mama ambaye ataweka mizigo yake miguuni pa Mwokozi. Yeye aliyesema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie” (Marko 10:14), bado anawaalika akina mama kuwaleta watoto wao wadogo ili wabarikiwe Naye. [MH 42.2; HU Aya ya 40]

Kwa watoto walioletwa karibu Naye, Yesu aliona ndani yao, wanaume na wanawake ambao wangekuja kuwa warithi wa neema Yake na raia wa ufalme Wake, na baadhi yao wangekuwa wafia imani kwa ajili Yake. Alijua kwamba watoto hawa wangemsikiliza na kumkubali Yeye kama Mkombozi wao kwa utayari zaidi kuliko ambavyo wangekuwa watu wazima, ambao wengi wao wangelikuja kuwa wenye hekima ya kilimwengu na wenye mioyo migumu. Katika kufundisha, alishuka chini hata kuwa sawa na wao kwa hadhi. Yeye, Mkuu na enzi ya mbinguni, alijibu maswali yao na kurahisisha masomo Yake muhimu ili kukidhi ufahamu wao wa kitoto. Alipanda akilini mwao mbegu za ile kweli, ili baada ya miaka mingi zije kuchipuka na kuzaa matunda ya uzima wa milele. [MH 42.3; HU Aya ya 41]

Yesu alipowaambia wanafunzi wasiwazuie watoto kuja Kwake, alikuwa akizungumza na wafuasi Wake katika vizazi na zama zote—kwa maofisa wa kanisa, wachungaji, wasaidizi, na Wakristo wote. Yesu anawavuta watoto Kwake, Naye atuamuru leo, “Waacheni waje Kwangu, wala msiwazuie”; ni kana kwamba anamaanisha kwamba, Watakuja Kwangu tu, ikiwa ninyi hamtawazuia. [MH 42.4; HU Aya ya 42]

Usiiruhusu tabia yako isiyo kama ya Kristo imwakilishe Yesu vibaya. Usiwaweke watoto wadogo mbali Naye kwa mzizimo na ukali wako (hasira, ukatili au manyanyaso). Kamwe usiwape sababu ya kuhisi kwamba mbinguni hapatakuwa mahali pazuri kwao ikiwa wewe ungekuwa huko. Usizungumzie dini kama kitu ambacho watoto hawawezi kukielewa (mambo ya kiroho), au kutenda kana kwamba wao hawatarajiwi kumkubali Kristo katika utoto wao. Usiwafanye wawaze vibaya kwamba dini ya Kristo ni dini ya huzuni, na ya kwamba katika kuja kwao kwa Mwokozi ni lazima wayaache mambo yote ambayo huyafanya maisha kuwa ya furaha. [MH 43.1; HU Aya ya 43]

Kadiri Roho Mtakatifu anavyogusa mioyoni mwa watoto, waunge mkono kwa kushirikiana na kazi Yake. Wafundishe kwamba Mwokozi anawaita, kwamba hakuna kitu kinachoweza kumpa furaha kubwa Bwana kuliko wao kujitoa Kwake katika miaka ile wanayoongezeka kwa kimo na kupendeza (kuchanua, yaani miaka yao ya ujanani). [MH 44.1; HU Aya ya 44]

Wajibu wa Mzazi

Mwokozi, kwa huruma isiyokuwa na kikomo, anajali sana roho ambazo amezinunua kwa damu Yake. Wao ndio humfanya ajidai kwa upendo Wake. Huwatazama kwa shauku isiyotamkika. Moyo Wake huvutiwa, si tu na wale watoto waliolelewa na kufunzwa vyema na wanaovutia bali pia na wale ambao, kwa kurithi na kwa kupuuzwa wana sifa za tabia zinazochukiza. Wazazi wengi hawaelewi ni kwa kiasi gani wanahusika katika tabia hizi kwa watoto wao, hawalijui jukumu lao juu ya tabia za watoto wao. Hawana huruma na hekima ya kushughulika na wakosaji hawa ambao wazazi wenyewe ndio wamesababisha

hali waliyo nayo watoto. Lakini Yesu awatazama watoto hawa kwa huruma. Anaona kutoka chanzo hadi matokeo. [MH 44.2; HU Aya ya 45]

Mtendakazi Mkristo anaweza kuwa wakala wa Kristo katika kuwavuta watoto hawa walio na hitilafu na kasoro kwa Mwokozi. Kwa hekima na busara anaweza kuwafunga watoto hawa moyoni mwake, aweza kuwapa ujasiri na tumaini, na kwa neema ya Kristo atashuhudia kwa macho yake wakigeuzwa tabia, ili kwamba maneno haya yatimizwe na kusemwa kwao, “Ufalme wa Mungu ni wao.” [MH 44.2; HU Aya ya 46]

Mikate Mitano Midogo ya Shayiri Yalisha Umati Mkubwa.

Siku nzima watu walikuwa wamejazana kwenye miguu ya Kristo na kwa wanafunzi Wake alipokuwa akifundisha kando ya bahari. Walikuwa wamesikiliza maneno Yake yaliyojawa neema, yaliyokuwa rahisi na ya wazi sana kiasi kwamba yalikuwa kama zeri (tiba/kitulizo) ya Gileadi nafsini mwao. Uponyaji wa mkono Wake wa kiungu ulikuwa umeleta afya kwa wagonjwa na uzima kwa waliokufa. Siku hiyo ilionekana kwao kama mbingu duniani, nao wakasahau wamekaa muda gani bila kula chakula chochote. [MH 45.1; HU Aya ya 47]

Jua lilikuwa linazama upande wa magharibi, na bado watu walikawia kutoka hapo. Hatimaye wanafunzi walimwendea Kristo, nao wakasisitiza kwamba kwa ajili ya umati wenyewe, ni vyema watu hawa waambiwe waende makwao. Wengi walikuwa wametoka mbali na walikuwa hawajala chochote tangu asubuhi. Wanafunzi wakasema kwamba watu hawa wangeweza kupata chakula katika miji na vijiji vinavyozunguka. Lakini Yesu akasema, “Wapeni ninyi chakula.” Mathayo 14:16. Kisha, akimgeukia Filipo, alimwuliza, “Tununue wapi mikate ili watu hawa wapate kula?” Yohana 6:5. [MH 45.2; HU Aya ya 48]

Filipo alitazama juu na kuona vichwa vingi vya watu vikienea sehemu kubwa kama bahari, naye akaanza kufikiria jinsi jambo hilo lisivyowezekana kuupatia chakula umati huu mkubwa sana. Naye akajibu kwamba mikate ya fedha ya dinari 200 haiwatoshi watu hawa hata kama kila mmoja atapata kipande kidogo tu!” [MH 45.3; HU Aya ya 47]

Yesu akauliza kiasi gani cha chakula kingeweza kupatikana miongoni mwa watu waliokuwa hapo. Andrea akasema “Yupo hapa mtoto, yuna mikate mitano ya shayiri na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa?" Kifungu cha 9. Yesu akaagiza chakula hicho kiletwe Kwake. Kisha akawaambia wanafunzi wawaketishe watu kwenye nyasi. Hilo lilipokamilika, alikitwaa kile chakula, “akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano. Wakala wote wakashiba; wakayaokota masazo ya vipande vya mikate, vikapu kumi na viwili, vimejaa.” Mathayo 14:19, 20. [MH 45.4; HU Aya ya 48]

Ilikuwa ni kwa muujiza wa uweza wa Kiungu ndiyo Kristo aliweza kulisha umati; hata hivyo ni jinsi gani chakula kile kilichotolewa, kilikuwa cha hali ya chini—samaki na mikate ya shayiri peke yake, chakula cha kawaida cha kila siku kwa wavuvi wa Galilaya. [MH 47.1; HU Aya ya 49]

Kristo angaliweza kuwaandalia watu mlo wenye fahari, lakini chakula kinachotayarishwa kwa ajili ya kukidhi tu hamu ya chakula, kisingekuwa na somo lolote kwa manufaa yao. Kupitia muujiza huu Kristo alitamani kufundisha somo la ustawi. Ikiwa watu leo wangekuwa na mazoea sahili katika mitindo yao ya maisha, wakiishi kupatana na sheria za asili, kama Adamu na Hawa walivyofanya hapo mwanzo, kungekuwa na ugavi mwingi kwa ajili ya mahitaji ya familia ya ubinadamu. Lakini ubinafsi na kuendekeza uchu wa kula vimeleta dhambi na taabu, kwa upande wa wenye chakula kingi kupita kiasi, na kwa upande mwingine wenye upungufu wa chakula. [MH 47.2; HU Aya ya 50]

Yesu hakutafuta kuwavuta watu Kwake kwa kutosheleza hamu yao ya chakula cha bei ya gharama kubwa (chenye ufahari/anasa). Kwa umati huo mkubwa, uliochoka na wenye njaa baada ya siku ile ndefu na ya kusisimua, chakula hicho rahisi kilikuwa hakikisho wa nguvu Zake na utunzaji Wake mwororo kwao katika mahitaji ya kawaida ya maisha yao ya kila siku. Mwokozi hajawaahidi wafuasi Wake anasa za ulimwengu huu; sehemu yao inaweza kufungwa na umaskini; lakini Neno Lake limeahidiwa kwao kwamba mahitaji yao yatatoshelezwa, na ameahidi kile kilicho bora kuliko mema ya hapa duniani—faraja ya kudumu ya uwepo Wake Mwenyewe. [MH 47.3; HU Aya ya 51]

Baada ya umati kulishwa, chakula kilibaki kingi. Yesu akawaamuru wanafunzi Wake, “Kusanyeni vipande vilivyosalia, kisipotee cho chote.” Yohana 6:12. Maneno haya yalikuwa na maana zaidi ya kukiweka kile chakula kwenye vikapu. Somo hili lilikuwa na mafunzo mawili. Hakitakiwi cho chote kutupwa. Hatupaswi kuruhusu au kuachia faida ya muda ituponyoke mikononi mwetu. Hatupaswi kupuuza chochote ambacho kingemnufaisha mwanadamu. Hebu kila ambacho kitasaidia kutoa unafuu kwa mahitaji ya mwanadamu, kikusanywe kwa ajili ya wahitaji na watu wenye njaa duniani. Kwa uangalifu huo huo twapaswa kuthamini hazina ya mkate kutoka mbinguni, ili kuyalisha na kuyatosheleza mahitaji yetu ya kiroho. Twapaswa kuishi kwa kila Neno litokalo kwa Mungu. Cho chote alichosema Mungu kisipotee bure. Hata Neno moja linalohusu wokovu wetu wa milele lisipuuzwe. Neno hata moja na lisianguke chini bure. [MH 48.1; HU Aya ya 52]

Muujiza wa mikate unatufundisha kumtegemea Mungu. Kristo alipowalisha watu elfu tano, hakukuwa na chakula karibu yao. Yaonekana pia pesa hazikuwa kwenye mamlaka Yake. Alikuwa amesimama hapo nyikani pamoja na wanaume elfu tano, bila ya kuhesabu wanawake na watoto, machoni Pake. Hakuwa ameualika umati huo kumfuata huko. Watu hawa wakiwa na shauku ya kuwa katika uwepo Wake, walikuwa wamekuja bila mwaliko au kushurutishwa; lakini

alijua kwamba baada ya kusikiliza maagizo Yake siku nzima walikuwa wamepata njaa na kuhisi udhaifu wa mwili. Walikuwa mbali na nyumbani, na usiku ulikuwa unakaribia. Wengi wao hawakuwa na uwezo wa kununua chakula. Yule ambaye Yeye Mwenyewe alikuwa amefunga siku arobaini jangwani kwa ajili yao, hakuwaacha wanadamu warudi majumbani mwao wakiwa wamefunga. [MH 48.2; HU Aya ya 53]

Majaliwa ya Mungu yalikuwa yamemweka Yesu mahali alipokuwa, Naye alimtegemea Baba Yake wa mbinguni kwa mbinu na uwezo kutatua hitaji hilo. Tunapoletwa katika maeneo yenye shida, twapaswa kumtegemea Mungu. Katika kila dharura twapaswa kutafuta msaada kutoka Kwake, ambaye ana rasilimali zisizo na ukomo chini ya amri Yake. [MH 48.3; HU Aya ya 54]

Katika muujiza huu, Kristo alipokea kutoka kwa Baba; Naye akawagawia wanafunzi, nao wanafunzi wakawapa watu, na watu mmoja baada ya mwingine. Kwa hiyo kila aliyeunganishwa na Kristo atapokea kutoka Kwake mkate wa uzima, na kuwapa watu wengine. Wanafunzi Wake ndio njia iliyowekwa kwa ajili ya mawasiliano kati ya Kristo na watu. [MH 49.1; HU Aya ya 55]

Wanafunzi waliposikia maelekezo ya Mwokozi, “Wapeni ninyi chakula,” magumu yote yaliibuka katika akili zao. Nao wakauliza, “Je, twende vijijini kununua chakula?” Lakini Kristo alisema nini? “Wapeni *ninyi* chakula.” Wanafunzi walimletea Yesu chakula chote walichokuwa nacho; lakini Yeye hakuwaalika wao kula kile chakula. Aliwapa maagizo wawahudumie watu. Chakula kilichoongezeka mikononi Mwake, na mikononi mwa wanafunzi, walipomfikia Kristo, wao hakikuwatindikia. Ghala ndogo ya chakula ilitosha kuwalisha watu wote. Umati ulipokwisha kulishwa, wanafunzi walikula pamoja na Yesu chakula cha thamani, kilichotolewa na mbingu. [MH 49.2; HU Aya ya 56]

Tunapoona mahitaji ya maskini, wajinga, na watu wanaoteseka, ni mara ngapi mioyo yetu huzama. Nasi twauliza “Ni nini kitakachowezekana kwa nguvu zetu hizi dhaifu na rasilimali ndogo, kukidhi mahitaji haya ya kutisha? Je, haitakuwa vyema kumngojea mtu fulani mwenye uwezo mkubwa zaidi au tajiri aongoze kazi, au kufanya utaratibu fulani wa kuunda shirika litakaloshughulikia jambo hili?” Kristo asema, “Wapeni *ninyi chakula*.” Tumieni mali, muda, na uwezo mlio nao. Mletee Yesu mikate yako ya shayiri. [MH 49.3; HU Aya ya 57]

Ingawa rasilimali zako haziwezi kutosha kulisha maelfu, zaweza kutosha kulisha mtu mmoja. Mikononi mwa Kristo, malighafi ndogo zaweza kuwalisha watu wengi. Kama wanafunzi, wewe toa kile ulicho nacho mkononi. Naye Kristo atazidisha karama. Atatunuku uaminifu, utegemezi rahisi Kwake. Kile ambacho kilionekana kuwa chakula kidogo kwetu kitathibitika kuwa karamu yenye utajiri (meza itajaa). [MH 49.4; HU Aya ya 58]

“Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu...Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na

riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema; kama ilivyoandikwa. [MH 50.1; HU Aya ya 59]

"Ametawanya, amewapa maskini;
Haki yake yadumu milele. [MH 50.2; HU Aya ya 60]

"Na Yeye ampaye mpanzi mbegu, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, Naye atayaongeza matunda ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote umpatiao Mungu shukrani kwa kazi zenu. 2 Wakorintho 9:6-11. [MH 50.3; HU Aya ya 61]

SURA YA 3

PAMOJA NA ASILI NA PAMOJA NA MUNGU

Maisha ya Mwokozi duniani yalikuwa maisha ya kuwasiliana na kutafakari asili pamoja na Mungu. Katika ushirika huu, Yeye alitufunulia siri ya maisha yenye nguvu. [MH 51.1; HU Aya ya 1]

Yesu alikuwa mtendakazi aliyefanya kazi daima kwa dhati, ari na bidii. Kamwe hakujawahi kuishi mtu aliyebebeshwa majukumu mazito kama Yeye. Hakuna mwingine aliyewahi kubeba mzigo mzito wa huzuni na dhambi ya ulimwengu. Kamwe hakuna mwingine aliyejitaabisha mwenyewe kwa ari iliyochukua muda na umakini wake wote kwa ajili ya mema ya wanadamu isipokuwa Yeye. Hata hivyo maisha Yake yalikuwa maisha yenye ukamilifu. Kimwili na kiroho aliwakilishwa na mwana-kondoo aliyetolewa dhabihu, "asiye na hila na asiye na doa." 1 Petro 1:19. Katika mwili Wake, kama alivyo rohoni, Yeye alikuwa kielelezo cha kile ambacho Mungu alikusudia jamii yote ya wanadamu iwe kupitia utii kwa sheria Zake. [MH 51.2; HU Aya ya 2]

Watu walipomtazama Yesu, waliona uso ambao ndani yake huruma ya Mungu ilichanganyika na nguvu ya fahamu za mwanadamu. Alionekana kuzungukwa na angahewa ya maisha ya kiroho. Ingawa tabia Zake zilikuwa za upole na zisizo na majivuno, aliwavutia watu kwa utambuzi wa uweza ambao ulikuwa umefichwa ndani Yake, ila haukuweza kusitirika kabisa. [MH 51.3; HU Aya ya 3]

Wakati wa huduma Yake alikuwa akifuatiliwa mara kwa mara na wenye hila na wanafiki ambao walikuwa wakitafuta maisha Yake. Wapelelezi walikuwa wakimfuata kila alipokanyaga hatua Zake, wakifuatilia maneno, ili kupata sababu fulani dhidi Yake. Watu hodari na wenye elimu za juu zaidi wa taifa, walitafuta kumshinda katika mijadala au mabishano. Lakini kamwe hawakuweza kujipatia ushindi. Mwishowe walilazimika kwenda kupumzika kwa kuondoka eneo la tukio, wakiwa wamekanganyikiwa na kuaibishwa na Mwalimu mnyenyekevu na mwenye hali ya chini (masikini) kutoka Galilaya. Mafundisho ya Kristo yalikuwa na upya na nguvu ambayo wanadamu hawakuwahi kuitambua hapo awali. Hata adui Zake walilazimika kukiri, “Hajanena kamwe mtu ye yote kama huyu anavyonena.” Yohana 7:46. [MH 51.4; HU Aya ya 4]

Maisha ya Yesu ya utoto yakiwa ni ya kimaskini, hayakupotoshwa na tabia za bandia za zama zile za upotovu. Akifanya kazi kwenye meza ya useremala (karakana), akibeba mizigo ya maisha ya nyumbani, akijifunza masomo ya utii na masumbufu ya maisha, alipata burudiko katikati ya mandhari ya asili (kitabu cha Mungu cha uumbaji), akikusanya maarifa na kutafuta kuelewa siri za uumbaji. Alijifunza Neno la Mungu, na saa Zake za shangwe kuu zilikuwa wakati alipoweza kuacha kando eneo Lake la kazi na kwenda mashambani, kutafakari katika mabonde tulivu, kufanya ushirika na Mungu kando ya mlima au katikati ya miti ya msituni. Saa za asubuhi mapema mara nyingi zilimkuta katika mahali pa faragha, akitafakari, akichunguza Maandiko, au katika maombi. Alipaza sauti Yake kwa kuimba, akiukaribisha mwanga wa asubuhi. Alizichangamsha saa zake za kazi kwa nyimbo za shukrani na kuileta furaha ya mbinguni kwa wale waliochoshwa na suluba na kuvunjika moyo. [MH 52.1; HU Aya ya 5]

Muda mrefu wa maisha Yake ya huduma aliutumia nje ya nyumba. Safari zake kutoka mahali hadi mahali zilifanywa kwa miguu, na mafundisho Yake mengi yalitolewa kwenye eneo la wazi. Ili kuwafundisha wanafunzi Wake, mara nyingi aliondoka kutoka katika mkanganyiko wa mji hadi kwenye utulivu wa mashambani, kama ilivyopatana kwa ubora zaidi na masomo Yake ya unyenyekevu, imani, na kujikana nafsi aliyotamani kuwafundisha. Ilikuwa ni chini ya vivuli vya miti iliyokuwa kando ya mlima, mbali kidogo kutoka Bahari ya Galilaya, ambapo wale Kumi na Wawili waliitwa kwenye utume na Hubiri la Mlimani lilitolewa katika eneo hilo. [MH 52.2; HU Aya ya 6]

Kristo alipenda kuwakusanya watu kumzunguka chini ya anga wazi, kwenye mwinuko wenye nyasi, au kwenye ufukwe kando kando ya ziwa. Hapa, akizungukwa na kazi za uumbaji Wake Mwenyewe, angeweza kugeuza mawazo

yao kutoka kwenye ubunifu bandia hadi kwenye asili kamilifu. Katika ukuaji wa vile vilivyoumbwa Naye na maendeleo ya asili, kanuni za ufalme Wake zilifunuliwa hapo. Wanadamu wanapoyainua macho yao kwenye vilima vya Mungu na kutazama kazi za ajabu zilizoumbwa na mkono Wake, basi, wangeweza kujifunza masomo ya thamani ya ukweli wa mbinguni. Katika siku za usoni masomo haya ya Mwalimu wa Kiungu yangerudiwa kwao kupitia uumbaji huu wa asili. Akili zao zingeinuliwa na moyo ungepata pumziko. [MH 54.1; HU Aya ya 7]

Yesu aliwapa muda wa kurudi majumbani mwao wale wanafunzi ambao walikuwa wakishirikiana Naye katika kazi Yake ili wapate kutembelea familia zao na kupumzika; ila juhudi zao za kumvuta Yeye mbali na kazi Zake hazikufaulu. Siku nzima alihudumia umati uliomjia kwa kushonana, na jioni, au asubuhi na mapema, alikwenda mahali alipopatenga kama Patakatifu milimani kwa ajili ya mawasiliano na Baba Yake. [MH 55.1; HU Aya ya 8]

Mara nyingi kazi Yake isiyokoma na makabiliano na uadui na mafundisho ya uongo ya marabi vilimwacha akiwa amechoka hoi, kiasi kwamba mama Yake na ndugu Zake, na hata wanafunzi Wake, waliogopa kwamba maisha Yake yangekoma mapema. Lakini aliporejea kutoka zile saa Zake za maombi ambazo zilikamilisha siku Yake ile yenye taabu, ziliacha alama ya mwonekano wa amani juu ya uso Wake, uchangamfu na uzima na nguvu vilionekana kutawala nafsi Yake yote. Kutoka kwenye zile saa alizokaa peke Yake na Mungu, alikuja, asubuhi baada ya asubuhi, kuwaletea wanadamu nuru ya mbinguni. [MH 55.2; HU Aya ya 9]

Baada tu ya kurejea kutoka kwenye safari yao ya kwanza ya umishenari, Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mkapumzike kidogo. Wanafunzi walikuwa wamerejea, wakiwa wamejawa na furaha ya kufaulu kwao kama watangazaji wa injili, hapo ndipo habari za kifo cha Yohana Mbatizaji kwa mkono wa Herode zilipowafikia. Lilikuwa jambo la huzuni, fadhaa na kuvunja moyo. Yesu alijua kwamba kwa kumwacha Yohana Mbatizaji afe gerezani alikuwa ameijaribu sana imani ya wanafunzi. Kwa upole wenye huruma alizitazama nyuso zao zenye huzuni, na zilizojaa machozi. Machozi yalikuwa machoni Pake Mwenyewe, aliponyanyua sauti Yake na kusema “Njooni ninyi peke yenu kwa faragha mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo.” Marko 6:31. [MH 56.1; HU Aya ya 10]

Karibu na Bethsaida, kaskazini mwa Bahari ya Galilaya, palikuwa na eneo tulivu, lenye kupendeza na la kijani kibichi cha majira ya kuchipua mimea, ambalo lilitoa mandhari ya faragha kwa Yesu na wanafunzi Wake. Walianza safari kuelekea mahali hapa kwa mashua yao kuvuka ziwa. Hapa wangeweza kupumzika, bila ya kubughudhiwa na mkanganyiko wa umati. Wanafunzi waliweza kusikiliza maneno ya Kristo hapa bila ya kubughudhiwa na maneno ya

hasira na shutuma toka kwa Mafarisayo. Hapa walitarajia kufurahia kipindi kifupi cha ushirika katika uwepo wa Bwana wao. [MH 56.2; HU Aya ya 11]

Yesu aliweza kuwa na faragha na wapendwa Wake kwa muda mfupi tu, lakini majira haya mafupi yalikuwa na thamani iliyoje kwao. Walizungumza pamoja kuhusu kazi ya injili na uwezekano wa kufanya kazi yao iwe yenye ufanisi zaidi katika kuwafikia watu. Yesu alipokuwa akiwafungulia hazina za ile kweli, wanafunzi walitiwa nguvu kwa uweza wa Bwana na kuhuishwa kwa tumaini na ujasiri. [MH 56.3; HU Aya ya 12]

Lakini muda si mrefu, umati ukaanza kumtafuta tena. Wakidhania kwamba alikuwa ameenda mahali pake pa kila mara pa kupumzikia, watu hao walimfuata huko. Matumaini yake ya kupata hata saa moja ya kupumzika yalikatishwa. Lakini ndani ya kina cha moyo Wake mkamilifu na wenye huruma, Mchungaji Mwema wa kondoo alikuwa tu na upendo na huruma kwa ajili ya roho hizi zenye hangaiko na kiu. Siku nzima alihudumia mahitaji yao, na wakati wa jioni aliwaaga, akawaambia waende majumbani mwao wakapumzike. [MH 57.1; HU Aya ya 13

Katika maisha yaliyotolewa kikamilifu kwa ajili ya mema kwa wengine, Mwokozi aliona ni muhimu kujitenga kando kutoka kwenye shughuli zisizokoma, zinazokutana na mahitaji ya wanadamu, na kutafuta mahali pa utulivu, ili awe na mawasiliano yasiyokatika na Baba Yake. Umati uliomfuata ulipoondoka, alikwenda milimani, na huko, akiwa peke yake pamoja na Mungu, anamimina moyo Wake katika maombi kwa ajili watu hawa wanaoteseka, wenye dhambi na wahitaji. [MH 58.1; HU Aya ya 14]

Yesu alipowaambia wanafunzi Wake kwamba mavuno yalikuwa ni mengi ila watenda kazi ni wachache, hakuwahimiza juu ya ulazima wa kufanya kazi inayochosha bila kukoma, bali aliwaambia, “Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika Mavuno Yake.” Mathayo 9:38. Kwa watenda kazi Wake waliochoka sana leo, Yesu anazungumza nao kwa maneno haya ya huruma, kama vile Yupo nao uso kwa uso nao, kama ilivyokuwa kwa wale wanafunzi Wake wa kwanza, “Njoni ninyi peke yenu kwa faragha,…mkapumzike kidogo.” [MH 58.2; HU Aya ya 15]

Wote walio chini ya mafunzo ya Mungu wanahitaji saa ya utulivu kwa ajili ya mawasiliano na mioyo yao wenyewe, na asili/uumbaji, na pamoja na Mungu. Ndani yao hakuna budi kufunuliwa maisha ambayo hayapatani na ulimwengu, desturi zake, au matendo yake; nao wanahitaji kuwa na uzoefu binafsi katika kupata utambuzi wa mapenzi ya Mungu. Lazima kila mmoja wetu amsikie Yeye akinena moyoni. Pale kila sauti nyingine yo yote inapokuwa imenyamazishwa, na katika ukimya tukingojea mbele Zake, utulivu wa nafsi huifanya sauti ya Mungu kuwa dhahiri zaidi (inatofautishwa na mambo mengine ya kawaida). Yeye atuagiza, “Tulieni na kujua kuwa Mimi ni Mungu!.” Zaburi 46:10. Haya ndiyo maandalizi yenye matokeo yaliyo na ufanisi kwa kazi yo yote itendwayo

kwa ajili ya Mungu. Katikati ya msongamano wa watu usiotulia, na uchovu wa shughuli nyingi na nzito za maisha, mtu ambaye ameburudishwa hivyo (kwa kujipatia majira ya kupumzika) atazungukwa na angahewa la nuru na amani. Atapokea tunu mpya ya nguvu za kimwili na kiakili. Maisha yake yatatoa harufu nzuri ya manukato, nayo itadhihirisha uweza wa Bwana utakaoifikia mioyo ya watu. [MH 58.3; HU Aya ya 16]

SURA YA 4

MGUSO WA IMANI

"Alisema moyoni mwake, nikigusa vazi Lake tu, nitapona." Mathayo 9:21. Alkuwa ni mwanamke maskini aliyenena maneno haya—mwanamke ambaye kwa miaka kumi na miwili alikuwa ameteseka kwa ugonjwa ambao ulifanya maisha yake kuwa mzigo. Alikuwa ametumia mali yake yote kwa kuwaona madaktari mbalimbali na kutumia tiba tofauti-tofauti, lakini aliambiwa ugonjwa wake umeshindikana kutibika. Lakini aliposikia juu ya Yule Mponyaji Mkuu, matumaini yake yalifufuka. Naye akafikiria kuwa, "Laiti ningeweza kumsogelea karibu vya kutosha na kuzungumza Naye, hakika ningeponywa." [MH 59.1; HU Aya ya 1]

Kristo alikuwa njiani kuelekea nyumbani kwa Yairo, rabi wa Kiyahudi ambaye alikuwa amemsihi aje kumponya binti yake aliyekuwa akiumwa. Ombi la baba aliye na moyo uliokata tamaa, “Binti yangu mdogo yu karibu kufa; nakuomba, njoo uweke mikono yako juu yake, apate kuponywa” (Marko 5:23), lilikuwa limegusa moyo mpole na wenye huruma wa Kristo. Naye mara akaondoka pamoja na kiongozi huyu (wa sinagogi) kwenda nyumbani kwake. [MH 59.2; HU Aya ya 2]

Walizidi kusogea mbele lakini taratibu sana; kwa maana umati ulimsonga Kristo kila upande. Katika kutengeneza njia Yake katikati ya umati ili aweze kusogea mbele, Mwokozi alikuja karibu na mahali ambapo mwanamke mwenye kuteseka kwa taabu ya ugonjwa alikuwa amesimama. Tena na tena mwanamke huyu alikuwa amejaribu bila mafanikio kumkaribia Yesu. Sasa fursa yake ilikuwa imewadia. Mama huyu hakuona njia yo yote ambayo angeweza kuzungumza Naye. Na hakutaka kuzizuia hatua za Yesu kwenda mbele. Lakini alikuwa amesikia kwamba uponyaji ulitoka kwa kugusa mavazi Yake; na, akiogopa kupoteza nafasi yake adimu ya kujipatia uponyaji, alijitosa kwa kusonga mbele huku akijisemea moyoni mwake, “Nikigusa tu vazi Lake, nitapona.” [MH 59.3; HU Aya ya 3]

Kristo alijua kila wazo lililokuwa akilini mwake, Naye alikuwa akipiga hatua kuelekea mahali aliposimama huyu mwanamke. Alitambua haja yake kubwa, na alikuwa akimsaidia kuizoeza imani yake kwa vitendo. [MH 60.1; HU Aya ya 4]

Alipokuwa akipita, alinyoosha mkono na kufaulu kugusa kidogo tu lile pindo la vazi Lake. Papo hapo alijua kwamba alikuwa amepona. Katika mguso huo mmoja imani ya maisha yake iliongezeka, na papo hapo maumivu na udhaifu wake vikatoweka. Papo hapo alihisi msisimko, kama wa mkondo wa umeme ukipita kwenye kila chembe hai ya mwili wake. Kisha ukamwijia utambuzi wa afya kamili. “Alihisi mwilini mwake kwamba amepona ugonjwa huo.” Kifungu cha 29. [MH 60.2; HU Aya ya 5]

Mwanamke huyu mwenye moyo uliojawa shukrani alitamani kuielezea shukrani yake kwa Mponyaji Mkuu, ambaye alikuwa amemfanyia mengi zaidi kwake, kwa huo mguso mmoja tu, kuliko madaktari walivyofanya katika muda wa miaka kumi na miwili; lakini hakuthubutu. Kwa moyo wa shukrani alijaribu kujiondoa kutoka kwenye umati. Ghafla Yesu akasimama, akatazama huku na kule na kuuliza, “Ni nani aliyenigusa?” [MH 60.3; HU Aya ya 6]

Akimtazama kwa mshangao, Petro alijibu, “Bwana, umati umeshonana, na kukusonga, Nawe wasema, Ni nani aliyenigusa? Luka 8:45. [MH 60.4; HU Aya ya 7]

“Kuna mtu amenigusa,” Yesu alisema; “Kwa maana naona kwamba nguvu imenitoka.” Kifungu cha 46. Yesu aliweza kutofautisha mguso wa imani na mguso wa kawaida wa kusanyiko lisilo na uangalifu (lisilojali). Kuna mtu fulani

alikuwa amemgusa kwa kusudi lenye kina zaidi, hakika ulikuwa mguso usio wa kawaida, na kisha mtu huyu, alikuwa ameshapokea jibu. [MH 60.5; HU Aya ya 8]

Kristo hakuuliza swali ili ajipashe habari Yeye Mwenyewe. Yeye alikuwa na fundisho kwa watu, kwa wanafunzi Wake, na kwa mwanamke. Alitamani kuwatia moyo wote walioteseka kwa matumaini. Alitaka kuwaonyesha wanadamu kwamba imani ndiyo iliyoleta nguvu ya uponyaji kwa mwanamke huyu. Imani na matumaini ya mwanamke huyu hayakupaswa kurukwa au kupuuzwa bila ya Yeye kutoa maelezo au ufafanuzi. Mungu lazima atukuzwe kwa ushuhuda na ungamo lake la shukrani. Kristo alitamani mwanamke aelewe kwamba aliidhinisha na kuafikiana na tendo lake la imani. Yesu asingetaka mwanamke aondoke na baraka nusu tu. Hakupaswa kubakia bila utambuzi kwamba Yesu alikuwa na maarifa ya kina ya mateso yake, au upendo Wake wenye huruma na ukubali Wake kuhusiana na imani yake mwanamke, katika uweza Wake wa kuwaokoa kabisa wote wanaokuja Kwake. [MH 60.6; HU Aya ya 8]

Akitazama upande wa mwanamke, Kristo alisisitiza kujua ni nani aliyemgusa. Akiona kwamba kujificha itakuwa ni kazi bure, mama huyu alikuja mbele Yake akitetemeka, na kujitupa miguuni Pake. Kwa machozi ya shukrani alimwambia, mbele ya watu wote, kwa nini alikuwa ameligusa vazi Lake, na jinsi alivyoponywa mara moja. Aliogopa kwamba kitendo chake cha kugusa vazi Lake kilikuwa cha kimbelembele (au kudiriki kwa kupitiliza au kiburi); lakini hakuna Neno la karipio lililotoka katika midomo ya Kristo. Aliongea tu maneno ya ukubali kwa tendo lake la kugusa pindo la vazi Lake. Maneno hayo yalitoka katika moyo wa upendo, uliojaa huruma kwa taabu na majanga ya wanadamu. “Binti,” Alisema kwa upole, “jifariji; imani yako imekuponya; nenda kwa amani.” Kifungu cha 48. Maneno haya yalikuwa ya kuchangamsha moyo kwa kiasi kikubwa cha namna gani kwa huyu mama. Sasa hakukuwa na woga wo wote uliobakia moyoni ulioitia uchungu furaha yake kwamba amemwudhi Yesu. [MH 61.1; HU Aya ya 9]

Ule umati wenye udadisi uliokuwa ukimsonga Yesu haukubarikiwa na lo lote. Lakini mwanamke huyu atesekaye aliyemgusa Yeye kwa imani alipokea uponyaji. Ndivyo jinsi ilivyo katika mambo ya kiroho, mguso wa kawaida hutofautiana na mguso wa imani. Kumwamini Kristo tu kama Mwokozi wa ulimwengu hakuwezi kamwe kuleta uponyaji wa roho. Imani inayoleta wokovu si tu kuafikiana na ukweli wa injili. Imani ya kweli ni ile inayompokea Kristo moyoni, kama Mwokozi wa mtu mmoja mmoja. Mungu alimtoa Mwanawe pekee, ili mimi, kwa kumwamini Yeye, “nisipotee, bali niwe na uzima wa milele.” Yohana 3:16. Nijapo kwa Kristo, kufuatana na Neno Lake, ninapaswa kuamini kwamba ninaipokea neema Yake inayookoa. Maisha ninayoishi sasa, ni lazima “niishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, na kujitoa nafsi Yake kwa ajili yangu.” Wagalatia 2:20. [MH 62.1; HU Aya ya 10]

Wengi hushikilia imani kama kauli tu. Imani iokoayo ni mapatano, ambayo kwa hayo, wale wanaompokea Kristo hujiunga wenyewe katika agano la mahusiano na Mungu. Imani iliyo hai inamaanisha ongezeko la nguvu hai, tumaini lenye ujasiri, ambalo kwa hilo, kupitia neema ya Kristo, nafsi inakuwa nguvu ishindayo. [MH 62.2; HU Aya ya 11]

Imani ni mshindi mkuu kuliko mauti. Ikiwa wagonjwa wanaweza kuongozwa kutazama macho yao kwa imani juu ya Mponyaji Mkuu, tutaona matokeo ya kushangaza. Italeta uzima wa mwili na roho. [MH 62.3; HU Aya ya 12]

Unapofanya kazi kwa ajili ya waathirika wa matendo maovu, badala ya kuwaelekeza katika uharibifu wanaoukimbilia na katika kukata tamaa ambao, wewe elekeza macho yao kwa Yesu. Shughulika na kuyakaza macho yao kwa Yesu. Waelekeze kwenye mambo matukufu ya mbinguni. Hili litafanya makubwa kwao katika kuokoa mwili na roho kuliko vile vitisho vyote vya kaburi vinavyowekwa mbele ya wanyonge na watu wanaoonekana kukosa matumaini. [MH 62.4; HU Aya ya 13]

“Alituokoa Kufuatana na Rehema Zake”

Mtumishi wa akida mmoja alikuwa amelala, kwa kuwa alikuwa anaumwa ugonjwa wa kupooza (akida—ni afisa jeshi anayesimamia watu 100). Kwa Warumi watumishi wao walikuwa watumwa, walionunuliwa na kuuzwa sokoni, na mara nyingi walitendewa vibaya kwa kunyanyaswa na ukatili; lakini mahusiano ya yule akida na mtumishi wake yalikuwa mema na yenye huruma, naye alitamani sana kupona kwake. Aliamini kwamba Yesu angeweza kumponya. Hakuwa amemwona Mwokozi, lakini taarifa alizozisikia ziliitia moyo imani yake. Bila kujali dini ya Wayahudi, Mrumi huyu alisadikishwa kwamba dini yao ilikuwa bora kuliko yake. Tayari akida huyu alikuwa amevuka vizuizi vya ubaguzi wa kitaifa na chuki vilivyotenganisha mabwana na watumwa. Alikuwa ameonyesha heshima kwa utumishi wa Mungu na alikuwa ameonyesha wema na fadhili kwa Wayahudi kama wale wanaomwabudu Bwana. Katika mafundisho ya Kristo, kama ilivyoripotiwa kwake, alipata kile ambacho kilikidhi haja ya roho yake. Chembe-chembe zake zote za kiroho zilizokuwamo ndani yake ziliitikia maneno ya Mwokozi. Lakini hata hivyo alijiona kuwa hastahili kumkaribia Yesu, na akawasihi wazee wa Kiyahudi wamwombe Yesu uponyaji wa mtumishi wake akida. [MH 63.1; HU Aya ya 14]

Wazee waliwasilisha kesi hiyo kwa Yesu, wakisisitiza kwamba, mwanajeshi huyu “Amestahili umtendee neno hili; maana, analipenda taifa letu, naye alitujengea sinagogi.” Luka 7:4, 5. [MH 63.2; HU Aya ya 15]

Lakini walipokuwa njiani kuelekea nyumbani kwa yule akida, Yesu alipokea ujumbe kutoka kwa akida mwenyewe akimwomba kwa kusema, “Bwana,

usijisumbue, kwa maana mimi sistahili Wewe uingie chini ya dari yangu." Kifungu cha 6. [MH 63.3; HU Aya ya 16]

Mwokozi akiwa bado anaendelea kutembea katika njia Yake, yule akida akaja mwenyewe kukamilisha ujumbe akisema, "Wala sikujiona kuwa nastahili kuja Kwako," "lakini sema Neno moja tu, na mtumishi wangu atapona. Kwa maana mimi ni mtu niliye chini ya mamlaka, nina askari chini yangu; na mwingine, Njoo, naye huja; na mtumishi wangu, Fanya hivi, naye anafanya." Mstari wa 7; Mathayo 8:8, 9. [MH 63.4; HU Aya ya 17]

"Nawakilisha mamlaka ya Rumi, na askari wangu wanatambua mamlaka yangu kuwa kuu. Basi Wewe unawakilisha uweza wa Mwenyezi Mungu asiye na kikomo, na viumbe vyote vyalitii Neno Lako. Unaweza kuamuru ugonjwa uondoke, na utakutii. Sema Neno tu, na mtumishi wangu atapona." [MH 64.1; HU Aya ya 18]

"Kama ulivyoamini," Kristo akasema, "na iwe hivyo kwako. Na mtumishi wake akapona saa ile ile." Kifungu cha 13. [MH 64.2; HU Aya ya 19]

Wazee wa Kiyahudi walikuwa wamempongeza akida huyo kwa Kristo kwa sababu ya wema alioonyesha kwa "taifa letu." Walisema, anastahili, kwa maana ametujengea sinagogi. Lakini yule akida alisema juu yake mwenyewe, kwamba "Mimi sistahili." Hata hivyo hakuogopa kuomba msaada kutoka kwa Yesu. Hakuamini katika wema wake mwenyewe, bali katika rehema ya Mwokozi. Hoja pekee ya kuponywa kwa mtumishi wake, ilikuwa ni hitaji lake kuu. [MH 65.1; HU Aya ya 20]

Vivyo hivyo kila mwanadamu aweza kumjia Kristo kwa njia hii. "Si kwa matendo ya haki tuliyoyatenda sisi, bali kwa rehema Yake alituokoa." (kwa kuzaliwa kwa mara ya pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu) Tito 3:5. Je, unajisikia moyoni kwa vile wewe u mwenye dhambi mno, basi huwezi kuwa na tumaini la kupokea baraka kutoka kwa Mungu? Kumbuka kwamba Kristo alikuja ulimwenguni ili kuwaokoa wadhambi. Hatuna kitu kinachotufanya kustahili mbele za Mungu; ombi ambalo tunaweza kuweka msisitizo wetu sasa na siku zote ni hali yetu ilivyo ya kukatisha tamaa na isiyo na msaada kabisa, ifanyayo uweza Wake wa kuokoa kuwa wa lazima kwetu. Tukiacha kabisa kujitegemea wenyewe, twaweza kutazama msalaba wa Kalwari na kusema: [MH 65.2; HU Aya ya 21]

"Sina kitu chochote ninacholeta mikononi mwangu kama gharama ya ununuzi ninayopaswa kuitoa Kwako ili kujiokoa, na kwa hisani uliyonifanyia; cha kufanya tu ni mimi kuukumbatia na kuung'ang'ania msalaba Wako." Kutoka kwenye wimbo Mwamba Wenye Imara Kwako Nitajificha. [MH 65.3; HU Aya ya 22] *(Msisitizo umeongezwa)*

“Yesu akamwambia, Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye.” Marko 9:23. Ni imani pekee, ndiyo ambayo hutuunganisha na mbingu na kutupa ujasiri na nguvu za kukabiliana na nguvu za giza. Kupitia Kristo, Mungu ametupatia sisi njia za kutiisha kila tabia mbaya na kupinga kila jaribu, au uovu, hata vitu hivi viwe na nguvu kiasi gani. Lakini wengi huhisi kwamba hawana imani, na kwa hiyo wanabaki mbali na Kristo. Hebu roho hizi, katika hali yazo ya kutojiweza, zijidondoshe juu ya rehema ya Mwokozi wao Mwenye huruma. Usijiangalie mwenyewe, bali Kristo. Yeye aliyewaponya wagonjwa na kutoa pepo alipotembea miongoni mwa wanadamu bado leo pia ni Mkombozi Yule Yule Mwenye nguvu na uweza. Hivyo kwa uthabiti na ujasiri, wewe zing’ang’anie na kuzikumbatia zile ahadi Zake kama majani ya mti wa uzima: “Yeye ajaye Kwangu sitamtupa nje kamwe.” Yohana 6:37. Ujapokuja Kwake, amini kwamba Yeye anakukubali, kwa sababu Yeye ameahidi. Hakika huwezi kuangamia unapofanya hivi—kamwe huwezi. [MH 65.4; HU Aya ya 23]

“Mungu aonyesha pendo Lake Yeye Mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.” Warumi 5:8. [MH 66.1; HU Aya ya 24]

Na “Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja Naye?” Warumi 8:31, 32. [MH 66.2; HU Aya ya 25]

“Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, 8.39 wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.” Mstari wa 38, 39, ARV. [MH 66.3; HU Aya ya 26]

“Waweza Kunitakasa”

Kati ya magonjwa yote yaliyojulikana Mashariki ukoma ulikuwa wa kuogofya sana. Tabia yake ya kutotibika na kuambukiza, na athari yake ya kutisha kwenye miili na maisha ya waathirika wake, iliwajaza hofu mashujaa na watu hodari. Miongoni mwa Wayahudi iliaminika kuwa ugonjwa huu ni hukumu iliyofuatilia dhambi ya mtu, na kwa hiyo uliitwa “pigo,” “kidole cha Mungu.” Ukiwa na mizizi iliyokita chini isiyoweza kung’oka, ugonjwa wa kufisha, ulitazamwa na watu kama ishara ya dhambi. [MH 67.1; HU Aya ya 27

Kwa taratibu za sheria za kidini, mwenye ukoma alitangazwa kuwa najisi. Kila alichogusa kilikuwa najisi. Hewa yote karibu naye ilichafuliwa na pumzi yake. Kama mtu ambaye tayari ni mfu, alifungiwa nje ya makazi ya wanadamu. Mtu ye yote aliyeshukiwa kuwa na ugonjwa huo, ilikuwa ni lazima aende kujionyesha kwa makuhani, na hawa walipaswa kufanya uchunguzi na kufanya

maamuzi ya kesi yake. Ikiwa angetangazwa kuwa ana ukoma, alitengwa na familia yake, alitengwa mbali na jamii ya wanaisraeli, akiandikiwa kuwa pamoja na wale tu waliokuwa wameteseka kwa ugonjwa huo vivyo hivyo kama yeye. Hata wafalme na watawala hawakuachwa. Mfalme aliyeshambuliwa na ugonjwa huu mbaya ilimbidi aiache fimbo yake ya utawala na kukimbia kutoka kwa jamii. [MH 67.2; HU Aya ya 28]

Akiwa mbali na marafiki na jamaa zake, ilimlazimu mwenye ukoma huyo kubeba mzigo wa laana ya ugonjwa wake. Alilazimika kutangaza janga lake mwenyewe wakati alipokuwa akitembea barabarani mwenyewe, na kwa kurarua mavazi yake, na kupaza sauti ili kuwatahadharisha, na kuwaonya wote wakimbie kutoka kwenye uwepo wake wenye maambukizo anapotembea karibu nao, Kilio "Najisi! najisi!" kilipokuja kwa sauti ya huzuni kutoka uhamishoni penye upweke (karantini), kilikuwa ni ishara iliyosikika kwa watu na kuwafanya wawe na hofu na kukereka miongoni mwa watu walio wazima. [MH 67.3; HU Aya ya 29]

Mahali pa huduma ya Kristo walikuwapo wengi walioteseka kwa namna hii, na habari za kazi Yake ya uponyaji zilipowafikia, miongoni mwa wale waliovunjika moyo, kuna mmoja ambaye moyoni mwake imani yake ilianza kuchipuka. Ikiwa angeweza kwenda kwa Yesu, basi angeweza kuponywa. Lakini awezaje kumpata Yesu? Anawezaje kujiwasilisha kwa Mponyaji, katika hali hii ya kuhukumiwa na kutengwa daima? Na je, Kristo atamponya? Je, Yeye pia hatatamka laana kwake kama Mafarisayo, na hata matabibu waliomtupia laana, na kumwonya akimbie kutoka kwenye makazi ya watu? [MH 68.1; HU Aya ya 30]

Anafikiri juu ya yote ambayo ameambiwa kuhusu Yesu. Ya kwamba hakuna hata mmoja aliyeomba msaada Kwake na kuambiwa aondoke bila kusaidiwa. Mtu huyu mnyonge ananuia kumtafuta Mwokozi. Ingawa amefungiwa nje, huenda akakatisha kwenye njia Yake Yesu kando ya barabara za milimani, au hata anaweza kumpata Yesu mahali pale anapofundishia nje ya miji. Shida ni nyingi, lakini hili ndio tumaini lake la pekee. [MH 68.2; HU Aya ya 31]

Akiwa amesimama kwa mbali, mwenye ukoma huyu, akasikia maneno machache toka katika kinywa cha Mwokozi. Anamwona akiweka mikono Yake juu ya wagonjwa. Anawaona vilema, vipofu, waliopooza, na wale walio kifoni kwa magonjwa mbalimbali wakiinuka na wakiwa na afya kamili, wakimsifu Mungu kwa kukombolewa. Imani yake inaimarika. Anajongea karibu na karibu zaidi, anaukaribia umati unaosikiliza maneno Yake. Vizuizi vilivyowekwa juu yake, usalama wa watu, na hofu ambayo watu wote wanamchukulia nayo, yote anayasahau. Fikra zake zipo tu kwenye tumaini lenye baraka la uponyaji. [MH 68.3; HU Aya ya 32

Kuonekana kwake huwatia watu kinyaa. Ugonjwa huo umemvamia kwa namna ya kutisha, na mwili wake unaooza unatisha kutazamwa. Watu wanapomwona tu wanarudi nyuma kwa mshtuko. Hofu yao inafanya wabanane

wao kwa wao ili kuepuka kugusana naye. Wengine wanajaribu kumzuia asimkaribie Yesu, lakini hawakufanikiwa. Mwenye ukoma hawaoni wala hawasikii. Maneno yao ya chuki hayawekei umakini kabisa moyoni mwake. Anamwona tu Mwana wa Mungu, na kusikia sauti ile tu inenayo uzima kwa wale wanaokufa. [MH 69.1; HU Aya ya 33]

Akimsogelea Yesu, anajitupa miguuni Pake, na kwa sauti kuu analia, “Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa.” [MH 69.2; HU Aya ya 34]

Yesu anajibu, “Nitafanya hivyo; uwe safi,” na kisha anaweka mkono Wake juu yake. Mathayo 8:2, 3. [MH 69.3; HU Aya ya 35]

Papo hapo badiliko linapita juu ya mwenye ukoma (mujarabu wa kuwekewa mkono anapona). Damu yake inakuwa na afya, mishipa yake ya neva inakuwa na utambuzi, na misuli inaimarishwa. Sehemu nyeupe-nyeupe isiyo ya asili, na yenye magamba ambayo ni viashiria vya ugonjwa wa ukoma vinapotea; na nyama yake inakuwa kama nyama ya mtoto mdogo. [MH 69.4; HU Aya ya 36]

Endapo makuhani wangetambua kuhusu uponyaji kwa wenye ukoma, chuki yao kwa Kristo ingeweza kuwaongoza kutoa shitaka lisilo haki. Yesu alitaka uamuzi adili upatikane (uamuzi ulio na ubaguzi uzimwe, hivyo aende kwa makuhani kwa kuhakikishwa). Hivyo akamwambia mtu huyo asimwambie mtu ye yote juu ya uponyaji huu, ila bila kukawia aende moja kwa moja kujionyesha hekaluni akiwa na sadaka, kabla uvumi wo wote kuhusu muujiza huo haujaenezwa mbali. Kabla ya makuhani kukubali toleo la sadaka kama hilo, walitakiwa kumfanyia uchunguzi mwilini, mtoa sadaka na kuthibitisha kwamba amepona kabisa. [MH 69.5; HU Aya ya 37]

Uchunguzi huu ulifanyika. Makuhani waliomhukumu mwenye ukoma kumtenga mbali na watu, walishuhudia uponyaji wake. Mtu aliyeponywa alirudishwa kwenye jamii na nyumbani kwake. Alihisi kwamba baraka ya afya ilikuwa ni ya thamani sana. Alifurahia uhai, na nguvu za utu wake na kurejeshwa kwake kwenye familia yake. Ijapokuwa Yesu alikuwa amemwonya asiseme kwa watu, yeye hakuweza tena kuficha ile habari ya ukweli wa kuponywa kwake, mtu huyu kwa furaha alienda zake huku na huko akitangaza nguvu za Yule aliyemfanya kuwa mzima. [MH 69.6; HU Aya ya 38]

Mtu huyu alipomjia Yesu, alikuwa “amejaa ukoma,” sumu ya ugonjwa yenye kufisha ilienea mwilini mwake. Wanafunzi walitaka kumzuia Bwana wao asimguse; kwa maana yule aliyemgusa mwenye ukoma alikuwa najisi yeye mwenyewe. Lakini kwa kuweka mkono Wake juu ya mwenye ukoma, Yesu hakupata unajisi. Ukoma ulitakaswa. Ndivyo ilivyo kwa ukoma wa dhambi—ambao una mizizi mirefu ya kufisha, nao hauwezekani kusafishwa kwa nguvu za mwanadamu. “Kichwa chote ni kigonjwa, na moyo wote umezimia. Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake; bali jeraha, na michubuko, na vidonda vitokavyo usaha.” Isaya 1:5, 6. Lakini Yesu, alipokuja kukaa katika

ubinadamu, Yeye hakupokea unajisi au uchafu wo wote. Uwepo Wake ulikuwa na uponyaji kwa mwenye dhambi. Ye yote yule atakayeanguka miguuni Pake, akisema kwa imani, “Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa,” atasikia jibu, “Nitafanya hivyo; na utakasike.” [MH 70.1; HU Aya ya 39]

Katika visa fulani vya uponyaji, Yesu hakutoa mara moja baraka zilizokuwa zikitafutwa. Lakini katika kesi za ukoma, mara tu ombi la mkoma lilipotolewa, lilikubaliwa papo hapo. Tunapoomba baraka za kidunia, jibu la maombi yetu linaweza kuchelewa, au Mungu anaweza kutupa kitu kingine tofauti na kile tunachoomba; lakini haiwi hivyo tunapoomba ukombozi kutoka kwenye dhambi. Ni mapenzi Yake kutusafisha kutoka dhambini, kutufanya kuwa watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Kristo “alijitoa nafsi Yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu, iliyopo sasa, kama apendavyo Mungu, Baba yetu.” Wagalatia 1:4. “Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu chochote sawasawa na mapenzi Yake, Yeye atusikia; na kama tukijua ya kuwa atusikia, kwa lolote tunaloomba, basi tuna uhakika kwamba tumekwisha kupata haja zile tulizomwomba.” 1 Yohana 5:14, 15. [MH 70.2; HU Aya ya 40]

Yesu aliwatazama wenye dhiki na waliolemewa mioyo, wale ambao matumaini yao yalififishwa, na wale ambao kwa sababu tu ya furaha ya ulimwengu, walijaribu kuyatuliza matamanio ya mioyo yao, Naye akawaalika wote kupata pumziko katika Yeye. [MH 71.1; HU Aya ya 41]

“Mtapata Pumziko”

Kwa huruma na upole aliwaambia watu wanaotaabika, “Jitieni nira Yangu, jifunzeni Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu.” Mathayo 11:29. [MH 71.2; HU Aya ya 42]

Katika maneno haya, Kristo alikuwa akizungumza na kila mwanadamu. Iwe wanatambua hili au la, wote wamechoka na wamelemewa na mizigo. Wote wamezidiwa na mizigo ambayo ni Kristo pekee awezaye kuiondoa. Mzigo mzito kabisa tunaobeba ni ule mzigo wa dhambi. Tukiachiwa kubeba mzigo huu wenyewe, utatusaga-saga (ponda-ponda). Lakini Yule Asiye na Dhambi amechukua mahali petu. “Bwana ameweka juu Yake maovu yetu sisi sote.” Isaya 53:6. [MH 71.3; HU Aya ya 43]

Amebeba mzigo wa hatia yetu. Atauchukua mzigo kutoka kwa mabega yetu yaliyochoka. Atatupa raha. Mzigo wa masumbufu na huzuni pia ataubeba. Anatualika tumtwike Yeye mahangaiko yetu yote; kwa maana Yeye hutubeba moyoni Mwake. [MH 71.4; HU Aya ya 44]

Kaka mkubwa wa jamii yetu ya ubinadamu Yuko karibu na kiti cha enzi cha milele. Humtazama kila anayeelekeza uso wake Kwake kama Mwokozi. Kwa uzoefu ajua ni nini udhaifu wa ubinadamu, aajua ni nini mahitaji yetu, na ni wapi nguvu za majaribu yetu zilipo; kwa maana “alijaribiwa sawasawa na sisi

katika mambo yote, bila kufanya dhambi.” Waebrania 4:15. Anakuangalia wewe, mtoto wa Mungu unayetetemeka. Je, unajaribiwa? Yeye atakuokoa. Je, wewe ni dhaifu? Yeye atakuimarisha. Je, wewe ni mjinga? Yeye atakuangazia. Je, umejeruhiwa? Yeye atakuponya. Bwana “aihesabu idadi ya nyota;” na bado “Huwaponya waliovunjika moyo, na kuziganga jeraha zao.” Zaburi 147:4, 3. [MH 71.5; HU Aya ya 45]

Haijalishi mahangaiko na majaribu yako ni yapi, eleza mambo yako mbele za Bwana. Roho yako itaimarishwa ili iwe na uvumilivu. Njia itatolewa kwako ili kujinasua kutoka kwenye aibu na shida. Kadiri unavyojijua kuwa u dhaifu zaidi, nawe huna msaada, ndivyo utakavyozidi kuwa na nguvu katika nguvu Zake. Kadiri mizigo yako inavyozidi kuwa mizito, ndivyo ule mbaraka wa kupumzishwa utakavyokuwa mkubwa zaidi kwako, unapoitupa mizigo hiyo Kwake Yeye aliye Mbeba Mzigo wako. [MH 72.1; HU Aya ya 46]

Hali mbalimbali zinaweza kutenganisha marafiki; maji yasiyotulia ya bahari pana yanaweza kupita kati yetu na wao. Lakini hakuna hali, wala hakuna umbali, unaoweza kututenga na Mwokozi. Popote tulipo, Yeye Yuko kwenye mkono wetu wa kuume, ili kutegemeza, kudumisha, kutushikilia, na kutuchangamsha. Upendo wa Kristo kwa wale waliokombolewa, ni mkubwa kuliko upendo wa mama kwa mtoto wake. Ni fursa yetu kupumzika katika pendo Lake, na kusema, “Nitamwamini; kwa kuwa alitoa uhai Wake kwa ajili yangu.” [MH 72.2; HU Aya ya 47]

Upendo wa binadamu waweza kubadilika, lakini upendo wa Kristo haujui mabadiliko. Tunapomlilia Yeye kwa ajili ya msaada, mkono Wake hunyooshwa kwetu ili kutuokoa.

“Milima inaweza kuondoka,

Na vilima vitaondolewa;

Bali wema Wangu hautaondoka kwako,

Wala agano Langu la amani halitaondolewa,

asema BWANA akurehemuye.” Isaya 54:10, A.R.V. [MH 72.4; HU Aya ya 48]

SURA YA 5

UPONYAJI WA ROHO

Wengi kati ya wale waliokuja kwa Kristo kwa ajili ya msaada wa uponyaji, walikuwa wamejiletea wenyewe magonjwa hayo, hata hivyo hakukataa kuwaponya. Na ule utakatifu uliotoka Kwake ulipoingia ndani ya roho hizi, waliona hatia yao ya dhambi, kisha wengi waliponywa magonjwa yao ya kiroho na kimwili pia. [MH 73.1; HU Aya ya 1]

Miongoni mwao alikuwepo yule aliyepooza kule Kapernaumu. Kama yule mwenye ukoma, mtu huyu aliyepooza alikuwa amepoteza matumaini kabisa ya kupona. Ugonjwa wake ulikuwa ni matokeo ya maisha ya dhambi, na mateso yake yalimpa uchungu kwa majuto. Alikuwa ameomba msaada kwa Mafarisayo na madaktari bila kupata tiba; lakini walitangaza kwamba hawezi kupona, nao walimshutumu kuwa ni mwenye dhambi na kutangaza kwamba yeye angekufa chini ya ghadhabu ya Mungu. [MH 73.2; HU Aya ya 2]

Moyo wa mtu huyu aliyepooza ulikuwa umezama kaika kukata tamaa. Ndipo aliposikia kazi za Yesu. Wengine, wenye dhambi na wasio na msaada kama yeye, walikuwa wameponywa, naye alitiwa moyo kuamini kwamba yeye pia, angeweza kuponywa kama angeweza kubebwa na kupelekwa kwa Mwokozi. Lakini matumaini yalipungua alipokumbuka sababu ya ugonjwa wake, hata hivyo hakuweza kutupilia mbali wazo la uwezekano wake wa kupona. [MH 73.3; HU Aya ya 3]

Matamanio yake makubwa yalikuwa ni kupata tiba ya mzigo wa dhambi. Alitamani kumwona Yesu na kupokea hakikisho la msamaha na kuwa na amani pamoja na mbingu. Naye angeridhika kuishi au kufa, kufuatana na mapenzi ya Mungu. [MH 74.1; HU Aya ya 4]

Hakukuwa na wakati wa kupoteza; tayari nyama yake iliyoharibika ilikuwa na viashiria vya kifo. Aliwasihi marafiki zake wambebe kwenye kitanda chake hadi kwa Yesu, na jambo hilo walilikubali kwa furaha kulifanya. Lakini umati wa watu ambao walikuwa wamekusanyika ndani ya nyumba, ulishonana na kuizunguka nyumba ambamo Mwokozi alikuwemo, kiasi kwamba ilikuwa vigumu sana kwa mgonjwa na marafiki zake kumfikia Bwana, au hata kuwa mahali ambapo wangeisikia sauti Yake. Yesu alikuwa akifundisha katika nyumba ya Petro. Kulingana na desturi yao, wanafunzi Wake waliketi karibu Naye, na “palikuwa na Mafarisayo na waalimu wa torati, waliokuwa wameketi hapo, waliotoka katika kila kijiji cha Galilaya, na Uyahudi, na Yerusalemu.” Luka 5:17, Wengi wa hawa watu walikuja kama wapelelezi, wakitaka kumshtaki Yesu. Zaidi ya hayo umati huo ulikuwa na watu wenye tabia ovu, wenye shauku, wacha Mungu, wadadisi, na wasioamini. Mataifa tofauti na matabaka yote ya

jamii yaliwakilishwa. “Na uweza wa Bwana ulikuwapo kuponya.” Fungu la 17. Roho ya uzima ikajaa juu ya kusanyiko, lakini Mafarisayo na madaktari hawakutambua uwepo Wake. Hawakuhisi hitaji lao, na hivyo uponyaji haukuwa kwa ajili yao. “Amewashibisha wenye njaa vitu vyema; na matajiri amewaacha mikono mitupu.” Luka 1:53. [MH 74.2; HU Aya ya 5]

Tena na tena watu waliombeba yule aliyepooza walijaribu kuusukuma umati wa watu ili wapite, bila mafanikio. Yule mgonjwa alitazama hali ya mambo kwa uchungu usio na kifani. Je, angewezaje kulizima tumaini ilhali msaada aliokuwa akiutamani ulikuwa karibu hivyo? Kwa pendekezo lake, marafiki zake walimbeba hadi juu ya paa la nyumba na kisha, wakalibomoa hilo paa, nao wakamshusha mgonjwa miguuni pa Yesu. [MH 75.1; HU Aya ya 6]

Mazungumzo ya Yesu yaliyokuwa yakiendelea yalikatizwa. Naye Mwokozi aliutazama uso wa huzuni na kuona macho yenye kusihi yakiwa yameelekezwa Kwake. Alijua vyema matamanio ya nafsi hiyo iliyolemewa. Kristo Ndiye aliyeleta usadikisho kwenye dhamiri yake mwathirika alipokuwa angali nyumbani. Alipotubu dhambi zake na kuamini katika uweza wa Yesu wa kumponya, rehema ya Mwokozi ilikuwa imeubariki moyo wake. Yesu alikuwa ameona mwale wa kwanza wa imani ukikua na kuwa usadikisho kwamba Yeye pekee Ndiye msaidizi wa mwenye dhambi, na alikuwa ameiona ikiimarika zaidi kwa kila jitihada katika kuja katika uwepo Wake. Ni Kristo Ndiye aliyemvuta mwenye kuteseka. Sasa, kwa maneno yaliyoanguka kama muziki mtamu kwenye sikio la msikilizaji, Mwokozi alisema, “Mwanangu, jipe moyo; umesamehewa dhambi zako.” Mathayo 9:2. [MH 75.2; HU Aya ya 7]

Mzigo wa hatia unatoka katika nafsi ya mgonjwa. Sasa hawezi kutilia mashaka mambo haya. Maneno ya Kristo yanaonyesha uweza Wake wa kusoma moyo. Ni nani awezaye kukataa uweza Wake wa kusamehe dhambi? Matumaini yanachukua mahali pa kukata tamaa, na furaha inachukua nafasi ya ukungu wa huzuni unaogandamiza moyo. Maumivu ya kimwili ya mtu huyu sasa yamekwisha, na utu wake wote unabadilika. Bila kuomba zaidi, analala kimya kwa amani, akiwa na furaha kubwa isiyoweza kutamkika [MH 76.1; HU Aya ya 8]

Wengi walikuwa wakitazama kwa hamu kila harakati ihusuyo shughuli hii ya ajabu. Wengi walihisi kwamba Maneno ya Kristo yalikuwa ni mwaliko kwao. Je! hawakuwa wagonjwa wa roho kwa sababu ya dhambi? Je, hawakuwa na shauku ya kuachiliwa huru kutoka katika mzigo huu? [MH 76.2; HU Aya ya 9]

Lakini Mafarisayo, wakiogopa kupoteza ushawishi wao kwa umati wa watu, walisema mioyoni mwao, “Anakufuru; ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mmoja, Naye Ndiye Mungu?” Marko 2:7, RV MH 76.3; HU Aya ya 10]

Akiwakazia macho, wale waliokuwa chini kwa hofu na kutetemeka na kurudi nyuma, Yesu akasema, “Mbona mnawaza maovu mioyoni mwenu? Kwa maana ni lipi lililo rahisi zaidi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako; au ni kusema,

Inuka, uende? Lakini mpate kujua ya kuwa Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi," Naye akasema, akimgeukia yule mwenye kupooza, "Ondoka, ujitwike godoro lako, uende nyumbani kwako." Mathayo 9:4-6. [MH 76.4; HU Aya ya 11]

Kisha yule ambaye alikuwa amebebwa juu ya machela na kupelekwa kwa Yesu aliinuka kwa miguu yake, na misuli yake ikanyumbulika kwa nguvu za ujana. Na mara "akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, nao wakamtukuza Mungu, wakisema, namna hii hatujapata kuiona kamwe." Marko 2:12. [MH 77.1; HU Aya ya 12]

Hakukuhitaji chochote isipokuwa nguvu iumbayo kurejesha afya ya ule mwili uliokuwa unaooza. Sauti ile ile iliyonena uhai kwa mwanadamu aliyeumbwa kutokana na mavumbi ya ardhi, ilikuwa imetamka uzima kwa yule mwenye kupooza aliyekuwa anakaribia kufa. Na nguvu zile zile zilizoupa mwili uhai/uzima zilikuwa zimeufanya upya moyo. Yeye ambaye katika uumbaji "alinena, ikawa," ambaye "aliamuru, vikasimama" (Zaburi 33:9), alikuwa ametamka uzima kwa nafsi iliyokufa katika makosa na dhambi. Uponyaji wa mwili wake ulikuwa ushahidi wa nguvu ambayo ilikuwa imeufanya upya moyo wake. Kristo alimwambia yule aliyepooza ainuke na atembee, "ili mpate kujua," Alisema, "ya kuwa Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi." [MH 77.2; HU Aya ya 13]

Mwenye kupooza alipata kutoka kwa Kristo uponyaji wa roho na mwili. Alihitaji afya ya kiroho kabla ya kuiona thamani ya afya ya mwili. Kabla ya ugonjwa wa kimwili kuponywa, Kristo lazima alete uponyaji katika akili, na kuitakasa roho kutoka kwenye dhambi. Somo hili halipaswi kupuuzwa. Kuna maelfu ya watu leo wanaougua magonjwa ya kimwili ambao, kama yule aliyepooza, wanatamani sana ujumbe unaosema, "Umesamehewa dhambi zako." Mzigo wa dhambi, pamoja na misukosuko na matamanio yake yasiyoweza kuridhishwa, ndio msingi wa maradhi yao. Hawawezi kupata tulizo mpaka waje kwa Mponyaji wa roho. Amani ambayo Yeye peke yake, ndiye anaweza kuitoa ingerejesha nguvu za akili na afya ya mwili. [MH 77.3; HU Aya ya 14]

Matokeo yaliyoletwa juu ya watu baada ya huu uponyaji wa mtu aliyepooza ilikuwa kana kwamba mbingu ilikuwa imefunguka na kufunua utukufu wa ulimwengu ule ulio bora. Yule mtu aliyekuwa ameponywa alipokuwa akipita katikati ya ule umati, huku akimbariki Mungu katika kila hatua aliyopiga na kuubeba mzigo wake kirahisi kama vile furushi la manyoya ya ndege, watu walimpisha njia wakiwa wanarudi nyuma na wakiwa na nyuso zenye mshangao wanapomtazama, wakinong'onezana wenyewe kwa sauti ya chini, "Leo Tumeona mambo ya ajabu." Luka 5:26. [MH 78.1; HU Aya ya 15]

Kulikuwa na furaha kubwa kwenye nyumba ya mtu aliyepooza, aliporejea kwenye familia yake, akiwa amebeba kwa urahisi godoro ambalo alikuwa

amebebwa nalo polepole alipotoka kwao, muda mfupi tu uliopita. Sasa ndugu na jamaa walikusanyika na kumzunguka kwa machozi ya furaha, kwani ilikuwa vigumu kwao kuamini macho yao. Alisimama mbele yao katika nguvu kamili za mtu uzima. Mikono ile ambayo ilikuwa haina uhai sasa ilitii cho chote alichokiamuru. Nyama iliyokuwa imesinyaa na kuwa na rangi iliyofifia, sasa ilikuwa mpya na yenye afya kamili. Alitembea kwa hatua thabiti, akiwa huru kupiga hatua zinazomwongoza kwenda mbele. Furaha na tumaini viliandikwa katika kila kuonekana kwa uso wake, na mwonekano wa ukamilifu na amani vilikuwa vimechukua mahali pa alama za dhambi na mateso. Shukrani za furaha zilipanda na kwenda juu kutoka kwenye nyumba hiyo, na Mungu akatukuzwa kupitia Mwanawe, ambaye alikuwa amerejesha tumaini kwa yule asiye na tumaini na nguvu kwa yule aliyejeruhiwa. Mtu huyu na familia yake walikuwa tayari kuyatoa maisha yao kwa ajili ya Yesu. Hakuna mashaka yaliyohafifisha imani yao, hakuna kutokuamini kulikoharibu uaminifu wao kwa Yeye ambaye alileta nuru kwenye nyumba iliyokuwa yenye giza. [MH 79.1; HU Aya ya 16]

"Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana:
Na vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi Jina Lake takatifu.
Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana,
Wala usizisahau fadhili Zake zote,
Akusamehe maovu yako yote;
Akuponyaye magonjwa yako yote;
Aukomboa uhai wako na uharibifu;...
Hata ujana wako upate kufanywa upya kama tai.
Bwana hutenda haki
Na hukumu kwa wote walioonewa....
Hakututendea sawasawa na dhambi zetu;
Wala hakutulipa sawasawa na maovu yetu....
Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake,
Ndivyo Bwana awahurumiavyo wamchao.
Maana Yeye anatujua umbo letu;
Anakumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi." Zaburi 103:1-14.
[MH 79.2; HU Aya ya 17]

"Je, Uko Tayari Kufanywa Mzima?"

"Na huko Yerusalemu penye mlango wa kondoo pana birika, iitwayo kwa Kiebrania Bethzatha, nayo ina matao matano. Ndani ya hayo, umati mkubwa wa wagonjwa walikuwa wamelala, vipofu, viwete, waliopooza, wakingojea maji yatibuliwe." Yohana 5:2, 3. [MH 81.1; HU Aya ya 18]

Katika nyakati fulani maji ya birika hili yalikuwa yakitibuliwa, na ilikuwa inaamika kote kwamba hali hii ilikuwa ni matokeo ya nguvu zisizo za kawaida, na ya kwamba ye yote aliyekuwa wa kwanza kuingia baada ya kutibuliwa kwa maji birikani, basi angeponywa ugonjwa wo wote aliokuwa nao. Mamia ya wagonjwa walitembelea mahali pale; lakini umati ulikuwa mkubwa sana wakati maji yalipotibuliwa kiasi kwamba walipokimbia kwenda mbele, waliwakanyaga-kanyaga, wanaume, wanawake, na watoto waliokuwa dhaifu kuliko wao. Wengi walishindwa kufika karibu na birika. Wengi waliofanikiwa kulifikia, walifia kwenye ukingo wake. Vibanda vilikuwa vimejengwa karibu na mahali hapo, ili wagonjwa waweze kukingwa kutokana na joto la mchana na baridi ya usiku. Kulikuwa na wengine ambao walikaa usiku katika vibaraza vyake, huku wakitambaa hadi ukingoni mwa bwawa siku baada ya siku, kwa matumaini ya kupata uponyaji, lakini bila mafanikio. [MH 81.2; HU Aya ya 19]

Yesu alikuwa Yerusalemu. Naye alipokuwa akitembea peke yake, na huku akiwa katika kutafakari na maombi, alikuja birikani. Aliwaona watu wanyonge wenye huzuni na walioteseka wakitazama kile ambacho walidhani kuwa ndio nafasi yao ya pekee ya kuponywa. Alitamani kutumia nguvu Zake za uponyaji ili kumfanya kila mgonjwa kuwa mzima. Lakini ilikuwa ni siku ya Sabato. Umati wa watu ulikuwa ukienda hekaluni kwa ajili ya ibada, na alijua kwamba tendo hilo la uponyaji, lingechochea chuki ya Wayahudi kiasi cha kukatisha kazi Yake. [MH 81.3; HU Aya ya 20]

Lakini Mwokozi aliona mwathirika mmoja mwenye huzuni na mateso makubwa. Ilikuwa ni mtu aliyekuwa kiwete, naye hakuwa anajiweza kwa miaka thelathini na minane. Ugonjwa wake kwa kiwango kikubwa ulikuwa ni matokeo ya tabia zake mbaya na ulionekana kuwa hukumu kutoka kwa Mungu. Akiwa peke yake bila rafiki, akihisi kwamba ametengwa na rehema ya Mungu, mgonjwa huyo alikuwa amepitia taabu na mateso kwa miaka mingi. Wakati ule ilipotarajiwa kwamba maji yatatibuliwa, wale waliohurumia unyonge wake walimchukua hadi kwenye matao yake. Lakini wakati uliongojewa, yaani maji yalipotibuliwa maji, hakuwa na mtu wa kumsaidia kuingia ndani. Aliona maji yakitiririka na kurushwa juu, lakini hakuwahi kufika mbali zaidi ya ukingo wa bwawa. Wale waliokuwa wenye nguvu zaidi yake, waliweza kujitumbukiza kabla yake. Mgonjwa maskini asiyejiweza, hakuweza kushindana na umati wa watu wenye ubinafsi unaopambania kuyafikia maji. Juhudi zake za kudumu kuelekea kwenye lengo moja, wasiwasi wake na kukatishwa kwake tamaa mara kwa mara, vilikuwa vinamaliza kwa haraka nguvu zake zilizosalia. [MH 81.4; HU Aya ya 21]

Mgonjwa huyu alikuwa amelala juu ya mkeka wake na mara kwa mara alikiinua kichwa chake ili kutazama birikani, pale uso wa wema na wenye huruma ulipoinama juu yake, na kutamka maneno haya, “Je! Wataka kuwa mzima?” na kuvuta usikivu wake. Tumaini likaujia moyo wake. Naye akahisi kwamba kwa njia fulani angepata msaada. Lakini uso wake uliochangamka kwa

tabasamu la kutia moyo ulififia upesi. Alikumbuka jinsi alivyojaribu mara nyingi kulifikia lile birika, na sasa alikuwa na matarajio madogo ya kuliona lile birika likitibuliwa katika maisha yake, aligeuka kwa uchovu, akasema, “Bwana, mimi sina mtu wa kunitia birikani, maji yanapotibuliwa; ila wakati ninapokuja mimi, mtu mwingine hushuka mbele yangu.” [MH 83.1; HU Aya ya 22]

Yesu akamwamuru, “Simama, jitwike godoro lako, uende.” Mistari ya 6-8. Kwa tumaini hilo jipya, yule mgonjwa akamtazama Yesu. Udhihirisho wa uso Wake, ladha ya sauti Yake, havina mfanano na mtu mwingine ye yote. Upendo na nguvu vyaonekana kutoka kwenye uwepo Wake Yesu. Imani ya kiwete inalishikilia Neno la Kristo. Bila maswali anauamuru mwili wake wote kutii, na, anapofanya hivi, mwili mzima unaitikia. [MH 84.1; HU Aya ya 23]

Kila neva na misuli inashangilia maisha mapya, na uzima kamili unamijia miguu yake milemavu. Akisimama kwa miguu yake mwenyewe, anaendelea na safari yake kwa hatua thabiti, zinazojongea kwa uhuru, akimsifu Mungu na kufurahia nguvu Zake mpya alizozipata. [MH 84.2; HU Aya ya 24]

Yesu hakuwa amempa mtu huyo aliyepooza uhakikisho wo wote wa msaada wa mbingu. Huenda mtu huyo angeliweza kusema, “Bwana, ukiniponya, ndipo nitalitii Neno lako.” Angeweza kusimama hapo na kuanza kutilia tu mashaka maneno hayo, na hivyo kupoteza nafasi yake moja tu ya uponyaji. Lakini hapana, yeye hakufanya hivyo, kwani aliamini Neno la Kristo, aliamini kwamba alifanywa kuwa mzima; punde alifanya juhudi, Naye Mungu akampa uwezo; alinuia kutembea, naye akatembea. Kwa kutenda kwake kulingana na Neno la Kristo, yeye alifanywa mzima. [MH 84.3; HU Aya ya 25]

Kwa dhambi tumeugua na kukosa uzima wa Mungu. Nafsi zetu zimepooza. Sisi wenyewe hatuna uwezo wa kuishi maisha matakatifu kama yule kilema aliyekuwa hana uwezo wa kutembea. Wengi wanatambua unyonge wao; wanatamani uzima huo wa kiroho ambao utawaleta katika kupatana na Mungu, nao wanafanya juhudi ili kuupata. Lakini bila mafanikio. Wakiwa wamekata tamaa wanalia, “Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? “Warumi 7:24. Hebu hawa waliokata tamaa, na wanaohangaika watazame juu. Mwokozi anainama chini kwa ajili ya ununuzi wa damu Yake, akisema kwa upole na huruma isiyoelezeka, “Je, wataka kuwa mzima?” Anakualika uamke katika ukamilifu na amani. Usingoje kuhisi kuwa umefanywa mzima. Amini tu Neno la Mwokozi. Weka nia na mapenzi yako upande wa Kristo. Nia ya kumtumikia, na katika kulitenda Neno Lake, wewe utapokea nguvu. Haijalishi vile vitendo viovu ulivyovifanya, tamaa kuu ya matendo ya mwilini ambayo kwa kujifurahisha nayo kwa muda mrefu yameifunga roho na mwili, Kristo anaweza na anatamani kukuokoa. Yeye ataipa uhai nafsi ambayo “imekufa katika makosa na dhambi.” Waefeso 2:1. Atamweka huru mateka aliyeshikiliwa na udhaifu, maafa na minyororo ya dhambi. [MH 84.4; HU Aya ya 26]

Dhambi zimetia sumu chemchemi za uzima. Lakini Kristo asema, “Nitazichukua dhambi zenu; nitakupa amani. Nimekununua wewe kwa damu Yangu. Wewe ni Wangu. Neema Yangu itaimarisha nia yako iliyodhoofika; nitakuondolea majuto yako kwa ajili ya dhambi. Majaribu yajapokushambulia, masumbuko na fadhaa vijapokuzingira, pale, uwapo na majonzi na kukata tamaa, ukiwa karibu kufa moyo, mtazame Yesu, na giza linalokuzunguka, litaondolewa na mng’ao angavu wa uwepo Wake. Pale dhambi inapopigania kutawala nafsini mwako, na kuilemea dhamiri, mtazame Mwokozi. Neema Yake inakutosha kuitiisha dhambi. Ufanye moyo wako wa shukrani, unaotetemeka kwa kutokuwa na uhakika, umgeukie Yeye. Shikilia tumaini lililowekwa mbele yako. Kristo anasubiri kukupokea katika familia Yake. Nguvu Zake zitasaidia udhaifu wako; Yeye atakuongoza hatua kwa hatua. Weka mkono wako kwenye Mkono Wake, na umwache Yeye akuongoze. [MH 85.1; HU Aya ya 27]

Kamwe usijisikie kwamba Kristo Yuko mbali. Yeye Yu karibu daima. Uwepo Wake wa upendo wakuzingira. Mtafute Yeye kama Yeye anavyotamani kukutafuta wewe. Anakutamani sio tu uguse mavazi Yake, lakini utembee Naye katika ushirika wa maisha yote (daima). [MH 85.2; HU Aya ya 28]

“Nenda, Wala Usitende Dhambi Tena”

Sikukuu ya Vibanda ilikuwa ndiyo tu imeisha. Makuhani na marabi katika Yerusalemu walikuwa wamefeli katika njama zao dhidi ya Yesu, na, ilipofika jioni, “kila mtu alikwenda Nyumbani kwake. Yesu akaenda kwenye Mlima wa Mizeituni.” Yohana 7:53; 8:1. [MH 86.1; HU Aya ya 29]

Kutoka kwenye msisimko na mkanganyiko wa jiji hilo, kutoka kwenye umati wa watu wenye shauku na marabi waliokuwa wasaliti, Yesu aligeukia upande wa mashamba tulivu ya mizeituni, mahali ambapo Angeweza kuwa peke yake na Mungu. Lakini kulipopambazuka alirudi Hekaluni; na umati wa watu ulipomzunguka tena, Yeye aliketi na kuwafundisha. [MH 86.2; HU Aya ya 30]

Mara akakatishwa. Kundi la Mafarisayo na waandishi likamwendea, huku likimburuta mwanamke aliyeingiwa na hofu, ambaye kwa sauti za ukali na shauku, walimshtaki kwamba alikuwa amevunja amri ya saba. Wakimsukuma mwanamke huyu mbele Yake Yesu, walisema, kwa kuonyesha heshima ya kinafiki, “Bwana, mwanamke huyu amefumaniwa alipokuwa akizini. Basi katika torati Musa alituamuru kuwapiga mawe wanawake wa namna hii; Nawe wasemaje? Mstari wa 4, 5. [MH 87.1; HU Aya ya 31]

Heshima yao ya kujifanya, ilikuwa na njama iliyojificha, ya kumwangamiza Yesu. Ikiwa Yesu angemwachilia huru mwanamke huyo, angeshtakiwa kwa kuidharau sheria ya Musa. Iwapo angetangaza kuwa mwanamke huyu anastahili

kifo, angeweza kushtakiwa kwa Warumi kama mtu aliyejitwalia mamlaka ambayo ni ya kwao tu. [MH 88.1; HU Aya ya 32]

Yesu alitazama tukio hilo—mhanga aliyekuwa anatetemeka katika aibu yake, waheshimiwa wenye nyuso ngumu na kali, wasio na huruma hata ya ubinadamu. Moyo Wake safi ulisita mbele ya halaiki. Bila kutoa dalili ya kwamba amesikia swali hili, aliinama na, akikaza macho Yake ardhini, akaanza kuandika katika udongo. [MH 88.2; HU Aya ya 33]

Wakiwa wamekosa subira kwa kuchelewa Kwake na kutoonyesha kujali maneno waliyoweka dhahiri kabisa, washtaki walisogea karibu Naye zaidi, wakisitiza jambo hili lipate usikivu Wake. Lakini macho yao, yalifuatilia yale ya Yesu, na kisha yalipoanguka kwenye ardhi, mahali ambapo miguu Yake ilikuwepo, sauti zao zilinyamazishwa. Kile kilichokuwa kinaandikwa mbele yao, kilikuwa ni hatia za siri kwenye maisha yao wenyewe. [MH 88.3; HU Aya ya 34]

Akisimama, na kuwakazia macho wale wazee waliokuwa wakipanga njama, Yesu alisema, “Yeye asiye na dhambi miongoni *mwenu na* awe wa kwanza kumtupia jiwe.” Kifungu cha 7. Kisha, akainama chini tena, na kuendelea kuandika. [MH 88.4; HU Aya ya 35]

Hakuwa ameweka kando sheria ya Musa wala kuvunja sheria za mamlaka ya Rumi. Washtaki walishindwa. Sasa, mavazi yao ya utakatifu wa kujifanya yalikuwa yameraruliwa kutoka kwenye miili yao, nao walisimama, wakiwa na hatia na kuhukumiwa, mbele ya ukamilifu usio na kipimo. Wakitetemeka kwa kuogopa, isije uovu uliofichika wa maisha yao ukaanikwa wazi mbele ya kadamnasi ya watu, wakiwa wameinamisha vichwa chini na macho yao yakiangalia chini, walimwacha mhanga wao kwa Mwokozi Mwenye huruma. [MH 88.5; HU Aya ya 36]

Yesu alisimama, na akamtazama yule mwanamke, kisha akasema, “Wako wapi wale washitaki wako? hakuna aliyekuhukumu? Akasema, hapana, Bwana. Yesu akamwambia, Wala Mimi sikuhukumu; enenda zako, wala usitende dhambi tena. Mstari wa 10, 11. [MH 88.6; HU Aya ya 37]

Yule mwanamke alikuwa amesimama mbele ya Yesu, akiwa ameingiwa na hofu. Yale Maneno Yake, “Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza kumtupia jiwe,” yalikuwa yamemjia kama hukumu ya kifo. Naye hakuthubutu kuinua macho yake kuangalia uso wa Mwokozi, lakini alingojea kimyakimya adhabu au maafa yake. Kwa mshangao aliona washitaki wake wakiambaa wakiwa hawana la kusema na wakiwa wamefadhaika; ndipo maneno haya ya tumaini yalianguka sikioni mwake, “Wala Mimi sikuhukumu; enenda zako, wala usitende dhambi tena.” Moyo wake ukayeyuka, naye, akijitupa miguuni pa Yesu, alitoa shukrani zake na aliungama dhambi zake kwa machozi yenye uchungu. [MH 89.1; HU Aya ya 38]

Huu ukawa mwanzo wake wa maisha mapya, maisha yenye ukamilifu wa moyo na amani, yaliyowekwa wakfu kwa ajili ya Mungu. Katika kuiinua hii nafsi iliyoanguka, Yesu alifanya muujiza mkubwa zaidi kuliko kazi ya kuponya ugonjwa mbaya sana wa kimwili; Aliponya ugonjwa wa kiroho ambao hatima yake ni kifo cha milele. Mwanamke huyu aliyetubu akawa mmoja wa wafuasi Wake walio imara zaidi. Kwa kujitoa nafsi yake kwa upendo, mwanamke huyu alikuwa ameonyesha shukrani yake kwa rehema ya Bwana yenye kusamehe. Kwa mwanamke huyu mkosaji ulimwengu ulikuwa na dharau na mabezo tu, lakini Yule Asiye na Dhambi alihurumia udhaifu wake na kumnyoshea mkono wa msaada. Wakati Mafarisayo wanafiki walipokuwa wanashutumu, Yesu alimwambia, “Enenda zako, wala usitende dhambi tena.” [MH 89.2; HU Aya ya 39]

Yesu ajua hali/mazingira ya kila nafsi. Kadiri hatia ya mwenye dhambi inavyozidi kuwa kubwa, ndivyo anavyozidi kumhitaji zaidi Mwokozi. Moyo Wake wa upendo wa mbinguni na huruma, huvutwa zaidi kwa ajili ya aliyenaswa katika mitego ya adui. Kwa damu Yake Mwenyewe ametia sahihi hati ya kuachiwa huru jamii yote ya ubinadamu kutoka utumwani. [MH 89.3; HU Aya ya 40]

Yesu hataki wale ambao wamenunuliwa kwa gharama kubwa kiasi hicho, wafanyiwe mchezo wa majaribu ya adui. Yeye hataki sisi tushindwe na tuangamie. Yeye aliyewazuia simba katika tundu lao, na kutembea pamoja na mashahidi Wake waaminifu katikati ya moto mkali, leo Yu tayari kufanya kazi kwa niaba yetu ili kutiisha kila uovu ulio katika asili yetu. Leo anasimama kwenye madhabahu ya rehema, akiyawasilisha mbele za Mungu maombi ya wale wanaotaka msaada Wake. Yeye hamfukuzi yeye anayelia kwa moyo uliovunjika na kupondeka kwa majuto. Atawasamehe wote wanaomjia kwa ajili ya msamaha na kurejeshwa bila gharama. Yeye hamwambii mtu ye yote mwingine yale ambayo ni Yeye tu anaweza kuyafunua au kuyaanika wazi, kwa vile anayajua, bali anaiagiza kila nafsi inayotetemeka ijipe moyo. Hebu Ye yote yule atakaye, na ashikilie nguvu za Mwenyezi Mungu, na afanye amani Naye, Naye atafanya amani na mtu huyo. [MH 90.1; HU Aya ya 41]

Roho zinazomgeukia kwa ajili ya kimbilio, Yesu huziinua juu ya mashtaka na ugomvi wa ndimi za wanadamu. Hakuna mtu au malaika mwovu anayeweza kuzishtaki roho hizi. Kristo anawaunganisha wanadamu na asili Yake ya Kiungu na ya ubinadamu. Wanadamu wanasimama kando ya Mbeba Dhambi mkuu katika nuru itokayo kwenye kiti cha enzi cha Mungu. [MH 90.2; HU Aya ya 42]

Damu ya Yesu Kristo yatusafisha “kutoka dhambi yote.” 1 Yohana 1:7. [MH 90.3; HU Aya ya 43]

“Ni nani atakayewashtaki wateule wa Mungu? Mungu Ndiye Mwenye kuwahesabia haki. Ni nani atakayehukumu adhabu? Kristo Yesu Ndiye aliyekufa,

naam, na zaidi ya hayo amefufuka katika wafu, Naye Yuko mkono wa kuume wa Mungu, tena Ndiye anayetuombea." Warumi 8:33, 34. [MH 90.4; HU Aya ya 44]

Juu ya upepo na mawimbi, na juu ya watu waliokuwa na mapepo, Kristo alionyesha kwamba alikuwa na udhibiti kamili. Yeye aliyetuliza dhoruba na bahari iliyochafuka alizungumza amani kwenye akili zilizokengeushwa na kuzidiwa na Shetani. [MH 91.1; HU Aya ya 45]

Yesu alikuwa ananena kuhusu utume Wake Katika sinagogi la Kapernaumu kuwaweka huru watumwa wa dhambi. Mara alikatishwa na kelele za kuogofya. Mwendawazimu alikuwa akikimbia kutoka kundini mwa watu, na huku akipaza sauti na kusema, "tuna nini Nawe, Wewe Yesu wa Nazareti? Je, umekuja kutuangamiza? Nakujua Wewe U nani, Mtakatifu wa Mungu." Marko 1:24. [MH 91.2; HU Aya ya 46]

Yesu alimkemea yule pepo, akisema, "Fumba kinywa, umtoke; Na pepo akamtupa katikati, akamtoka, asimdhuru." Luka 4:35. [MH 91.3; HU Aya ya 47]

Mateso ya mtu huyu pia yalisababishwa na maisha yake mwenyewe. Alikuwa amevutiwa na anasa za dhambi na alikuwa akifikiri kufanya maisha kuwa karamu kuu. Kutokuwa na kiasi na upuuzi vilipotosha silika tukufu za asili yake, na Shetani akachukua udhibiti kamili juu yake. Majuto yakawa mjukuu (yakaja baadaye). Wakati angejinyima mali na raha ili kurudisha utu wake uliopotea alikuwa hajiwezi katika kumshinda yule mwovu. [MH 91.4; HU Aya ya 48]

Katika uwepo wa Mwokozi aliamshwa kutamani uhuru, lakini pepo alipinga nguvu za Kristo. Mtu huyo alipojaribu kumwomba Yesu msaada, yule pepo mchafu alimtia maneno kinywani, naye akalia kwa uchungu wa woga. Yule mwenye pepo alifahamu kwa sehemu fulani, kwamba alikuwa mbele ya Yule ambaye angeweza kumweka huru; lakini alipojaribu kuufikia mkono huo wenye nguvu, nia nyingine ilimzuilia, maneno ya mwingine yalitamkwa kupitia kinywani mwake. [MH 91.5; HU Aya ya 49]

Vita kati ya nguvu za Shetani na matamanio yake mwenyewe ya kuwekwa huru, ilikuwa ya kutisha. Ikaonekana kwamba mtu huyu aliyeteswa lazima apoteze maisha yake katika kupambana na adui ambaye alikuwa ameharibu utu wake. Lakini Mwokozi alinena kwa mamlaka na kumweka huru mateka huyo. Yule mtu aliyekuwa amepagawa alisimama mbele ya watu walio katika mshangao akiwa mtu huru. [MH 92.1; HU Aya ya 50]

Kwa sauti ya furaha alimsifu Mungu kwa ukombozi. Jicho ambalo siku za hivi karibuni lilikuwa likiangaza kwa moto wa wenda-wazimu sasa lilitazama kwa utambuzi na kububujikwa na machozi ya shukrani. Watu wakawa mabubu kwa mshangao. Mara tu waliporejea katika hali ya kuwa na usemi, waliulizana wao kwa wao, "Ni nini hiki? Mafundisho mapya! kwa uweza anawaamuru hata pepo wachafu, nao wanamtii." Marko 1:27, RV [MH 92.2; HU Aya ya 51]

Hakika kuna wengi hivi leo walio chini ya nguvu za pepo wabaya kama alivyokuwa yule mwenye pepo wa Kapernaumu. Wote wanaoacha amri za Mungu kwa makusudi wanajiweka chini ya udhibiti wa Shetani. Watu wengi hucheza na uovu, wakidhani kwamba wanaweza kujinasua wanapoona wanapenda kufanya hivyo; ila wanavutwa na kuendelea na uovu huo tu, mpaka wanajikuta wanatawaliwa na nia yenye nguvu kuliko yao. Hawawezi kuepuka nguvu zake mwovu zilizo za ajabu. Dhambi ya siri au tamaa kuu za mwilini zaweza kumshika na kumfunga mateka asiyejiweza kama alivyokuwa yule mwenye pepo wa Kapernaumu. [MH 92.3; HU Aya ya 52]

Hata hivyo hali yake mwadamu si ya kukatisha tamaa kabisa. Mungu hatawali akili zetu bila ridhaa yetu; lakini kila mtu ana uhuru wa kuchagua ni mamlaka gani anayotaka imtawale. Hakuna aliyeanguka chini sana, hakuna aliye mwovu sana, hata asiweze kupata ukombozi katika Kristo. Yule mtu mwenye pepo, badala ya kusali au kuomba, yeye alichoweza tu kutamka, ni maneno ya Shetani; lakini bado ombi alilokuwa nalo moyoni mwake, ambalo lilikuwa bado kutamkwa lilisikika kwa Yesu. Hakuna kilio cho chote kutoka kwa mtu mhitaji ambalo halitasikilizwa japo halikutamkwa kwa sauti. Wale wanaokubali kuingia katika agano na Mungu hawajaachwa kwenye nguvu za Shetani au udhaifu wa utu wao wa kale. [MH 93.1; HU Aya ya 53]

“Je! Aliye hodari aweza kunyang'anywa mateka yake, au jeshi lao waliofungwa halali waokoka? Naam, Bwana asema hivi, Hata jeshi la wafungwa wake aliye hodari watapokonywa mikononi mwake, na mateka yake aliye jabari waokoka; kwa maana nitateta na yeye atatetaye nawe, Nami nitawaletea wana wokovu wako.” Isaya 49:24, 25. [MH 93.2; HU Aya ya 54]

Kutakuwa na mabadiliko ya ajabu ndani yake ambaye kwa imani hufungua mlango wa moyo kwa Mwokozi. [MH 93.3; HU Aya ya 55]

“Nakupa Nguvu”

Kama ilivyokuwa kwa wale mitume kumi na wawili, wale wanafunzi sabini ambao Kristo aliwatuma baadaye, walipokea karama zisizo za kawaida kama muhuri wa utume wao. Kazi yao ilipokamilika, walirudi kwa furaha, wakisema, “Bwana, hata pepo wanatutii kwa Jina Lako.” Yesu akajibu, “Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme.” Luka 10:17, 18. [MH 94.1; HU Aya ya 56]

Tangu sasa wafuasi wa Kristo wanapaswa kumwona Shetani kuwa ni adui aliyeshindwa. Msalabani, Yesu alipata ushindi kwa ajili yao; ushindi huo alitamani waukubali kama wao binafsi. “Tazama,” alisema, “nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.” Mstari wa 19. [MH 94.2; HU Aya ya 57]

Uweza Mkuu wa Roho Mtakatifu ni silaha ya kila nafsi iliyotubu. Hakuna mtu ambaye kwa toba na imani amedai ulinzi Wake Kristo, Naye akamruhusu kupitia chini ya nguvu za adui. Ni kweli kwamba Shetani ni kiumbe mwenye nguvu; lakini, ashukuriwe Mungu, tunaye Mwokozi Mwenye nguvu, ambaye alimfukuza yule mwovu kutoka mbinguni. Shetani hufurahi tunapozikuza nguvu zake. Kwa nini wewe usizungumze juu ya Yesu? Kwa nini usizikuze na kuzitukuza nguvu Zake na pendo Lake? [MH 94.3; HU Aya ya 58]

Upinde wa mvua wa ahadi unaokizunguka kiti cha enzi kilicho juu ni ushuhuda wa milele kwamba “Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16. Huu unaushuhudia ulimwengu kwamba Mungu hatawaacha kamwe watoto Wake katika kukabiliana na uovu. Upinde ni uhakikisho kwetu wa nguvu na ulinzi maadamu kiti cha Enzi chenyewe kinaendelea kudumu. [MH 94.4; HU Aya ya 59]

SURA YA 6

KUOKOLEWA ILI KUTUMIKA

Ilikuwa ni asubuhi kwenye Bahari ya Galilaya. Yesu na wanafunzi Wake walikuwa wamefika ufukweni baada ya usiku wenye dhoruba kali juu ya maji, na nuru ya jua lililokuwa likichomoza, lilikuwa linagusa bahari na nchi kavu kama neema na baraka ya amani. Lakini wanapokanyaga ufuo huo wanakaribishwa na mwonekano wa kutisha zaidi kuliko bahari iliyojaa dhoruba. Kutoka sehemu fulani ya maficho katikati ya makaburi, wenda wazimu wawili wanawakimbilia kana kwamba wanataka wawararue vipande vipande. Vipande vya minyororo vinaning'inia kwenye miili ya watu hawa, minyororo ambayo wameivunja katika harakati ya kuondoka pale walipokuwa wamefungiwa. Nyama zao zimechanika na kuvuja damu, macho yao yanang'aa kutoka kwenye nywele zao ndefu zilizokuwa zinaning'inia nyusoni mwao, mwonekano wa ubinadamu unaonekana kama vile umetoweka. Wnaonekana kama wanyama wa mwituni kuliko walivyo wanadamu. [MH 95.1; HU Aya ya 1]

Wanafunzi na wale waliokuwa pamoja nao, walikimbia kwa hofu; lakini sasa wanagundua kwamba Yesu hayuko pamoja nao, hivyo wakageuka kumtafuta. Nao wakampata akiwa amesimama pale pale walipomwacha. Yeye ambaye alituliza tufani, na ambaye hapo awali alikutana na Shetani na kumshinda, hakimbii mbele za mapepo haya. Pale wenye mapepo, wakisaga-saga meno na kutokwa na povu kinywani, wanapomkaribia Bwana, anainua mkono Wake ule ambao uliyafanya mawimbi yatulie, na watu hawa hawathubutu kumkaribia. Wanasimama mbele Zake wakiwa wanaghadhabika, lakini hawana uwezo au nguvu ya kufanya lolote. [MH 95.2; HU Aya ya 2]

Kwa mamlaka, anaamuru pepo wachafu wawatoke watu hawa. Watu hawa. Watu hawa watesekao wanatambua kwamba Yuko Mmoja hapa karibu, ambaye anaweza kuwaokoa toka kwa mapepo yanayowatesa kwa ukatili mbaya. Wanaanguka miguuni pa Mwokozi ili kusihi rehema Yake; lakini midomo yao inapofunguliwa, mapepo yananena kupitia kwao, yakilia, “Tuna nini Nawe, Yesu, Mwana wa Mungu? Hata umekuja kututesa?” Mathayo 8:29. [MH 96.1; HU Aya ya 3]

Pepo wachafu wanalazimishwa kuwaachilia wahanga wao, na badiliko la kushangaza linakuja kwa watu hawa waliokuwa na mapepo. Nuru inaangaza kwenye akili zao. Macho yao yanaangaza kwa utambuzi. Nyuso zilizoharibika kwa muda mrefu sana kuwa sura ya Shetani, kwa ghafla zinakuwa na upole na kutulia kabisa, mikono iliyochafuliwa na damu inatulia, na watu hawa wanapaza sauti zao kwa kumsifu Mungu. [MH 97.1; HU Aya ya 4]

Wakati huo baada ya roho za hawa pepo waovu kufukuzwa kutoka katika makazi yao yaliyokuwa ndani ya wanadamu hawa wawili, waliingia ndani ya nguruwe na kuwaangamiza kabisa. Wachungaji wa nguruwe wanatimua mbio, kwenda kuwapasha watu habari hizo, na umati mkubwa unamiminika ili kuja kukutana na Yesu. Watu hawa wawili waliopagawa na pepo wachafu walikuwa kitu cha kuogopesha kwenye mji wao. Sasa watu hawa wamevikwa nguo na wakiwa na akili timamu, wameketi miguuni pa Yesu, wakisikiliza maneno Yake, na kulitukuza Jina Lake Yeye aliyewaponya na kuwafanya kuwa huru. Lakini wale wanaotazama maajabu haya, hawakuwa na furaha nyusoni mwao. Kupotea kwa nguruwe zao kwaonekana kuwa jambo kubwa zaidi mioyoni mwao kuliko ukombozi wa watu hawa waliochukuliwa mateka na nguvu za Shetani. Kwa kumtishia Yesu, wanamsonga mbele Zake na kumsihi aondoke kwenye mji wao, Naye anakubali, kwa kupanda kwenye mashua mara moja, kuelekea upande wa pili wa ufuo. [MH 97.2; HU Aya ya 5]

Hisia za wale wenye pepo walioponywa, zipo tofauti kabisa. Wao wanatamani kuambatana na Mwokozi wao. Wakiwa ndani ya uwepo Wake wanahisi wapo salama dhidi ya mapepo ambayo yamewatesa maishani mwao na kuharibu utu wao. Yesu anapokaribia kuingia kwenye mashua wanamsogelea kando Yake, nao wanapiga magoti miguuni Pake, wakimwomba waandamane Naye daima,

ambapo wanaweza kuyasikia maneno Yake. Lakini Yesu anawaamuru waende nyumbani kwao na kuwaambia wengine mambo makuu ambayo Bwana amewatendea. [MH 98.1; HU Aya ya 6]

Hapa kuna na kazi ambayo ilikusudiwa kwao kufanya—kwenda makwao na kuwaelezea watu kuhusu baraka walizozipokea toka kwa Yesu (walitoka sehemu yenye miji kumi yaani Dekapoli). Ilikuwa vigumu kwa watu hawa kutengana na Mwokozi. Matatizo makubwa yangewakumba katika kujumuika na watu wa nchi yao wasioamini (makafiri). Na kutengwa kwao kwa muda mrefu na jamii kunaonekana kuwanyima sifa za kutenda kazi hii (hawana stahiki ya kufanya kazi hii). Lakini mara tu Yesu anapowaonyesha wajibu wao, wanatii na kuwa tayari kwenda kwa moyo mmoja. [MH 98.2; HU Aya ya 7]

Si tu kwamba waliwaambia watu wa nyumbani mwao na majirani kuhusu Yesu, bali pia walizunguka Dekapoli yote (miji 10), wakitangaza kila mahali uweza Wake wa kuokoa na kueleza jinsi alivyowaweka huru dhidi ya nguvu za mapepo wachafu. [MH 98.3; HU Aya ya 8]

Ijapokuwa watu wa Gergesa hawakumpokea Yesu, Yeye hakuwaacha kwenye giza walilolichagua. Walipomwambia aondoke kwao, wao hawakuwa wameyasikia maneno Yake. Walikuwa ni wajinga kwa kile walichokuwa wanakikataa. Na hivyo Yeye alituma nuru kwao, na kwa njia ya wale (watu wawili) ambao (watu wa Dekapoli) wasingekataa kuwasikiliza. [MH 98.4; HU Aya ya 9]

Kwa kusababisha uharibifu wa nguruwe, lilikuwa kusudi la shetani kuwageuza watu kutoka kwa Mwokozi na kuzuia kuhubiriwa kwa injili katika eneo hilo. Lakini tukio hili liliamsha shauku za wakazi wa nchi kuliko ambavyo kitu kingine kingeweza kufanya, na kisha umakini wote ukaelekezwa kwa Kristo. Ingawa Mwokozi aliondoka, watu hawa aliowaponya walibaki kuwa mashahidi wa uweza Wake. Wale waliokuwa vyombo vya yule mkuu wa giza, waligeuka na kuwa wabeba nuru, wajumbe wa Mwana wa Mungu. Yesu aliporejea Dekapoli, watu walimiminika na kumzunguka, na kwa siku tatu maelfu kutoka katika vijiji vyote vinavyozunguka walisikia ujumbe Wake wa wokovu. [MH 98.5; HU Aya ya 10]

Wale watu wawili wenye pepo waliorejeshewa utu wao, wakawa wamishonari wa kwanza ambao Kristo aliwatuma ili kufundisha injili katika eneo la Dekapoli. Kwa muda mfupi tu watu hawa walikuwa wameyasikiliza maneno Yake. Hakuna hata hubiri moja kutoka kinywani Mwake Yesu, lililoangukia masikioni mwao. Hawakuweza kuwafundisha watu kama wanafunzi waliokuwa na Kristo kila siku na kufundishwa jinsi ambavyo wangeweza kufanya. Lakini wao walizungumza kile tu walichokielewa; kile ambacho wao wenyewe walikuwa wamekiona, na kusikia, na kuhisi uweza wa Mwokozi. Na Hivi ndivyo kila mtu ambaye moyo wake umeguswa na neema ya Mungu, anavyoweza kufanya. Huu ndio ushuhuda

ambao Bwana wetu hutuita tuufanye, na tukikosa kufanya hivi, ulimwengu unaangamia. [MH 99.1; HU Aya ya 11]

Injili inapaswa kuhibiriwa, si kama nadharia isiyo na uhai, bali kama msukumo ubadilishao maisha. Mungu angetaka watumishi Wake watoe ushuhuda wa uhalisia kwamba kwa njia ya neema Yake watu wanaweza kuwa na tabia inayofanana na Kristo, ili nao wafurahie uhakikisho wa upendo Wake mkuu. Yeye angetaka sisi tutoe ushuhuda wa uhalisia kwamba Yeye hawezi kuridhika mpaka wale wote ambao wataukubali wokovu wamerejeshwa katika hali zao tukufu, kama wana na binti Zake.[MH 99.2; HU Aya ya 12]

Hata wale ambao mwenendo wao umekuwa wa kuchukiza sana Kwake, Yeye Yuko huru kuwakubali. Wajapotubu, Yeye huwapa Roho Wake Mtakatifu, na kuwatuma kwenye kambi la wale wasio waaminifu ili kutangaza rehema Zake. Nafsi ambazo zimeshushiwa hadhi na kuwa vyombo vya Shetani, bado, kwa uweza wa Kristo, zinageuzwa kuwa wajumbe wa haki na wanatumwa kutangaza mambo makuu ambayo Bwana amewatendea na jinsi ambavyo amewahurumia. [MH 99.3; HU Aya ya 13]

"Sifa Zangu Zitakuwa Kwako Daima"

Baada ya mwanamke wa Kapernaumu kuponywa kwa mguso wa imani, Yesu alitamani mama huyu akiri na kushiriki zile baraka alizozipokea. Karama ambazo injili hutoa hazipaswi kufichwa, au kunyamaziwa kama jambo la mtu binafsi au kufurahiwa kwa siri. [MH 100.1; HU Aya ya 14]

"Ninyi ni mashahidi Wangu, asema Bwana, ya kuwa Mimi ni Mungu." Isaya 43:12. [MH 100.2; HU Aya ya 14]

Kukiri kwetu kuhusu uaminifu Wake, ni njia teule ya Mbingu kwa ajili ya kumdhihirisha Kristo ulimwenguni. Ni kweli kwamba twapaswa kukiri neema Yake kama ilivyodhihirishwa kupitia watakatifu wa kale; lakini kile ambacho kitakuwa na matokeo chanya zaidi, ni ushuhuda wa uzoefu wetu binafsi. Sisi ni mashahidi wa Mungu tunapofunua ndani yetu utendaji wa nguvu ambao ni wa Bwana. Kila mtu ana maisha tofauti na wengine wote, na uzoefu unaotofautiana kimsingi, kutoka kwa mtu na mtu. Mungu atamani kwamba sifa zetu zitapanda juu kuelekea Kwake, na zikiwa na uhalisi wa upekee wa mtu mmoja mmoja (tusizoee kuwa waigizaji katika kumsifu Yeye). Kukiri huku kwa thamani kupitia utoaji wa sifa na utukufu wa neema ya Mungu, kunapoungwa mkono na maisha kama ya Kristo, kuna nguvu isiyopingika, ambayo inatenda kazi kwa wokovu wa roho. [MH 100.3; HU Aya ya 15]

Ni kwa faida yetu kuifanya karama (ukarimu) ya Mungu iwe mpya daima kwenye kumbukumbu zetu. Kwa njia hii imani huimarishwa kudai na kupokea zaidi na zaidi. Twatiwa moyo zaidi katika baraka ndogo tunazopokea wenyewe

mmoja mmoja kutoka kwa Mungu kuliko katika masimulizi yote ya ajabu tunayoweza kuyasoma kuhusu imani na uzoefu wa wengine. Nafsi inayoitikia neema ya Mwenyezi Mungu itakuwa kama bustani iliyomwagiwa maji. Afya yake itachipuka mara moja; nuru yako itapambazuka kama asubuhi, na utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde (Isaya 58:8). [MH 100.4; HU Aya ya 16]

"Nimrudishie Bwana nini
Kwa ukarimu Wake wote alionitendea?
Nitakipokea kikombe cha wokovu,
Na kuliitia Jina la Bwana.
Nitaziondoa nadhiri zangu kwa Bwana,
Naam, mbele ya watu Wake wote." [MH 101.1; HU Aya ya 17]

"Nitamwimbia Bwana maadamu ninaishi,
Nitamshangilia Mungu wangu nikiwa hai.
Kutafakari kwangu na kuwe kutamu Kwake;
maana furaha yangu hutoka Kwake." [MH 101.2; HU Aya ya 18]

"Ni nani awezaye kuyanena matendo makuu ya BWANA?
Ni nani awezaye kutangaza sifa Zake zote?" [MH 101.3; HU Aya ya 19]

"Liitieni Jina Lake;
Yajulishe matendo Yake kati ya mataifa.
Mwimbieni, mwimbieni sifa: "
Zisimulieni kazi Zake zote za ajabu.
sifuni kwa Jina Lake takatifu;
na ufurahi moyo wao wamtafutao Bwana." [MH 101.4; HU Aya ya 20]

"Kwa kuwa fadhili Zako ni bora kuliko uhai,
Midomo yangu itakusifu....
Nafsi yangu itashiba kama mafuta na unono;
Na kinywa changu kitakusifu kwa midomo ya shangwe;
Ninapokukumbuka kitandani mwangu,
Na kukutafakari nyakati za usiku.
Kwa maana umekuwa msaada wangu,
Na katika uvuli wa mbawa Zako nitashangilia." [MH 101.5; HU Aya ya 21]

"Nimemtumaini Mungu, sitaogopa;
Mwanadamu atanifanya nini?
Ee Mungu, nadhiri Zako zi juu yangu,
Nitakutolea sadaka za shukrani.
Maana umeniokoa nafsi yangu na
mauti; [MH 101.6; HU Aya ya 22]

"Ewe Mtakatifu wa Israeli.
Midomo yangu itashangilia sana nitakapokuimbia;
Na nafsi yangu, uliyoikomboa.
Ulimi wangu nao utanena haki Yako mchana kutwa." [MH 101.7; HU Aya ya 23]

"Wewe Ndiwe tumaini langu tangu ujana wangu....
Sifa zangu zitakuwa Kwako Wewe daima."
"Nitalikumbusha Jina Lako;...
Kwa hiyo watu watakusifu. Zaburi 116:12-14, RV; 104:33, 34; 106:2; 105:1, 2 (ARV), 2, 3; 63:3-7, ARV; 56:11-13, ARV; 71:22-24, 5, 6; 45:17. [MH 102.1; HU Aya ya 24]

"Mmepokea Bure, Toeni Bure"

Mwaliko wa injili haupaswi kuwekewa mipaka na kuwasilishwa kwa watu wachache tu ambao mtu amewachagua, ambao, sisi twadhania kuwa watatuheshimu ikiwa wataukubali. Ujumbe unapaswa kutolewa kwa wote. Mungu anapobariki watoto Wake, sio kwa manufaa yao peke yao, bali kwa ajili ya ulimwengu wote. Yeye Anapotukabidhi karama Zake, hutaka tuziongeze kwa kuwagawia wengine. [MH 102.2; HU Aya ya 25]

Mwanamke Msamaria ambaye alikuwa amezungumza na Yesu kwenye kisima cha Yakobo, punde tu alipompata Mwokozi aliwaleta watu wengine Kwake. Alijidhihirisha kuwa mmishenari mwenye ufanisi zaidi kuliko wanafunzi Wake Kristo. Wanafunzi hawakuona cho chote katika Samaria chenye kuashiria kwamba shamba hilo la uinjilisti lilikuwa linatia moyo. Mawazo yao yalijikita katika kazi kubwa ambayo ingefanywa katika siku zijazo. Hawakuona kwamba karibu nao kulikuwa na mavuno ya kukusanywa. Lakini kupitia kwa huyu mwanamke ambaye walimdharau, mji mzima uliletwa kumsikiliza Yesu. Mwanamke huyu alibeba nuru mara moja kwa watu wa nchi yake. [MH 102.3; HU Aya ya 26]

Mwanamke huyu anadhihirisha utendaji wa imani kwa vitendo katika Kristo. Kila mfuasi wa kweli wa Bwana huzaliwa katika ufalme wa Mungu kama

mmishenari. Mara tu mtu anapokuja kumjua Mwokozi, anapata matamanio ya kuwafanya wengine wamfahamu Yeye pia. Ukweli unaookoa na utakasao hauwezi kufungwa moyoni mwake tu. Yule anywaye maji ya uzima, huwa chemchemi ya uzima. Mpokeaji anakuwa mtoaji. Neema ya Kristo ndani ya moyo ni kama chemchemi jangwani, inayobubujika ili kuwaburudisha wote, na kuwafanya wale walio karibu kuangamia kuwa na hamu ya kunywa maji ya uzima. Katika kufanya kazi hii twapokea baraka kubwa zaidi kuliko pale tunapofanya kazi ili kujinufaisha wenyewe tu. Ni katika kufanya kazi ya kueneza habari njema ya wokovu ndipo tunaletwa karibu na Mwokozi. [MH 102.4; HU Aya ya 27]

Kwa wale wote wanaopokea neema Yake Bwana asema hivi kwao: [MH 103.1; HU Aya ya 28]

“Nitawafanya wao na mahali palipouzunguka mlima Wangu kuwa baraka; nami nitafanya mvua inyeshe kwa wakati wake; kutakuwa na manyunyu ya baraka.” Ezekieli 34:26, ARV [MH 103.2; HU Aya ya 29]

“Siku ya mwisho, ambayo kwa kawaida ndiyo ilikuwa kilele cha sherehe, Yesu alisimama, akapaza sauti Yake, akisema, Mtu akiona kiu, na aje Kwangu anywe. Yeye aniaminiye Mimi, kama vile maandiko yalivyonena, vijito vya maji yaletayo uzima vitatiririka kutoka moyoni mwake.” Yohana 7:37, 38, ARV [MH 103.3; HU Aya ya 30]

Wale wanaopokea hawana budi kuwagawia wengine. Toka kila pande kuna miito inayosihi msaada. Mungu awaita watu kuwahudumia wanadamu wenzao kwa furaha. Twapaswa kujishindia taji za kutokufa; twapaswa kuutwaa ufalme wa mbinguni; ulimwengu, unaoangamia katika ujinga, unapaswa kuangaziwa nuru. [MH 103.4; HU Aya ya 31]

“Hamsemi, Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? tazama, nawaambia, Inueni macho yenu, mkatazame mashamba; kwa maana ni nyeupe tayari kuvunwa. Naye avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda kwa uzima wa milele.” Yohana 4:35, 36. [MH 103.5; HU Aya ya 32]

Kwa miaka mitatu mbele yao wanafunzi walikuwa na kielelezo cha ajabu cha Yesu. Siku baada ya siku walitembea na kuzungumza Naye, wakisikia maneno Yake ya furaha kwa waliochoka na kulemewa na mizigo, na kushuhudia udhihirisho wa nguvu Zake kwa niaba ya wagonjwa na watesekao. Pale muda ulipowadia wa Yeye kuwaacha, aliwapa neema na uwezo wa kuendeleza kazi Yake katika Jina Lake. Walipaswa kuangaza nchi zote nuru ya injili Yake ya upendo na uponyaji. Na Mwokozi aliahidi kwamba uwepo Wake ungekuwa nao daima. Kupitia Roho Mtakatifu, Yeye angekuwa karibu nao zaidi kuliko wakati alipotembea na kuonekana kwa macho kati ya wanadamu. [MH 104.1; HU Aya ya 33]

Kazi ambayo wanafunzi walifanya, sisi pia twapaswa kuifanya. Kila Mkristo anapaswa kuwa mmishenari. Kwa huruma na sikitiko inatupasa kuwahudumia wale wanaohitaji msaada, tukitafuta kwa bidii isiyokuwa na ubinafsi kupunguza taabu za wanadamu wanaoteseka. [MH 104.2; HU Aya ya 34]

Wote wanaweza kupata kitu cha kufanya. Hakuna haja ya kuhisi kana kwamba hakuna mahali ambapo wanaweza kufanya kazi kwa ajili ya Kristo. Mwokozi anajitambulisha Mwenyewe pamoja na kila mwanadamu. Ili tuweze kuwa washiriki wa familia ya mbinguni, Yeye alikuwa mshiriki wa familia ya duniani. Yeye ni Mwana wa Adamu, na hivyo ni ndugu kwa kila mwana na binti wa Adamu. Wafuasi wake wasijihisi kana kwamba wameng'atuka kutoka kwenye ulimwengu unaoangamia, uwazungukao. Wao ni sehemu ya wando mkubwa wa ubinadamu, na mbingu huwatazama kama ndugu za watu wenye dhambi na walio watakatifu pia. [MH 104.3; HU Aya ya 35]

Mamilioni kwa mamilioni ya wanadamu, katika magonjwa na ujinga na dhambi, hata hawajawahi kusikia kabisa kuhusu upendo wa Kristo kwao. Je, kama hali zetu zingebadilishwa na kuwa kama hali zao, tungetamani watu hawa watufanyie nini? Basi haya yote, kadiri ilivyo katika uwezo wetu, twapaswa kufanya kwa ajili yao. Kanuni ya maisha ya Kristo ambayo kwayo kila mmoja wetu lazima asimame au kuanguka kwa hiyo katika hukumu ni hii, "Lolote mtakalo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo. Mathayo 7:12. [MH 104.4; HU Aya ya 36]

Kwa yale yote ambayo tumenufaika kuyapata ukilinganisha na wengine,—iwe elimu na kutakaswa au kusafishwa ukilinganisha na wengine, ubora wa tabia, mafunzo ya Kikristo, uzoefu wa kidini,—tuna deni kwa watu wasio na upendeleo huu; na, kwa kadiri ilivyo katika uwezo wetu, hatuna budi kuwahudumia. Tunapokuwa na nguvu, twapaswa kuinua mikono ya wanyonge. [MH 105.1; HU Aya ya 37]

Malaika wa utukufu ambao daima hutazama uso wa Baba aliye mbinguni, hufurahia katika kuwahudumia viumbe wa Mungu walio wadogo. Daima malaika huwapo kila mahali wanapohitajika zaidi, pamoja na wale ambao wana vita ngumu zaidi ya kupigana na nafsi zao wenyewe, na wale ambao mazingira yao yanafanya mtu avunjike moyo zaidi. Watu dhaifu na wanaotetemeka na ambao wana tabia nyingi za kuchukiza ndiyo jukumu lao (malaika) mahsusi. Kile ambacho mioyo yenye ubinafsi ingekiona kuwa ni huduma ya kufedhehesha, yaani kuwahudumia wale walio wanyonge na kila hali duni ya tabia, ndiyo kazi ya viumbe wakamilifu, wasio na dhambi ambayo wameagizwa kutokea kwenye mahakama za juu mbinguni. [MH 105.2; HU Aya ya 38]

Yesu hakuona mbingu kuwa mahali pa kutamanika wakati ambapo tumepotea. Aliziacha mahakama za mbinguni kwa ajili ya maisha ya lawama, matusi, na kifo cha aibu. Yeye ambaye alikuwa tajiri katika hazina ya mbinguni isiyokuwa

na idadi, akawa maskini, ili kwa umaskini Wake sisi tuwe matajiri. Twapaswa kufuata katika njia aliyoikanyaga. [MH 105.3; HU Aya ya 39]

Yeye anayefanyika mtoto wa Mungu tangu sasa anapaswa kujitazama kama kiunganishi katika mnyororo uliotupwa chini ili kuuokoa ulimwengu, akiwa mmoja pamoja na Kristo katika mpango Wake wa rehema, akienda pamoja Naye kutafuta na kuokoa waliopotea. [MH 105.4; HU Aya ya 40]

Wengi hujisikia kwamba ingekuwa fursa kubwa kutembelea kwenye sehemu za matukio ya maisha ya Kristo, kutembea pale Alipokanyaga, kutazama ziwa ambalo alipenda kufundishia, na vilima na mabonde ambayo macho Yake mara nyingi yalitulia pale. Lakini hatuhitaji kwenda Nazareti, Kapernaumu, au Bethania, ili tutembee katika hatua za Yesu. Tutazipata nyayo Zake kando ya kitanda cha wagonjwa, katika mashimo ya umasikini, katika vichochoro vya miji mikubwa vilivyosongamana, na katika kila mahali ambapo kuna mioyo ya wanadamu inayohitaji kufarijiwa. [MH 105.5; HU Aya ya 41]

Twapaswa kuwalisha wenye njaa, kuwavisha walio uchi, na kuwafariji wanaoteseka na wale wenye shida. Twapaswa kuwahudumia watu wanaokata tamaa, na kuwatia moyo kwa matumaini wale wasio na tumaini. [MH 106.1; HU Aya ya 42]

Upendo wa Kristo, uliodhihirishwa katika huduma isiyo na ubinafsi, utakuwa na matokeo zaidi katika kumbadilisha mtenda mabaya kuliko ambavyo upanga au mahakama vinavyoweza kufanya. Hivyo huhitajika katika kumtia tu mvunja sheria hofu, lakini mmishenari mwenye upendo anaweza kufanya zaidi ya kutumia nyenzo hizo. Mara nyingi moyo ambao unakuwa mgumu chini ya karipio utayeyuka chini ya upendo wa Kristo. [MH 106.2; HU Aya ya 43]

Mmishonari hawezi tu kufanya uponyaji wa magonjwa ya kimwili, lakini pia anaweza kumwongoza mwenye dhambi kwa Tabibu Mkuu, ambaye aweza kusafisha roho kutokana na ukoma wa dhambi. Kupitia watumishi Wake, Mungu hukusudia kwamba wagonjwa, waathirika wa hali yo yote mbaya, na wale waliopagawa na pepo wachafu wasikie sauti Yake. Kupitia wakala wake wa kibinadamu Yeye anatamani kuwa mfariji ambaye ulimwengu haujamjua bado. [MH 106.3; HU Aya ya 44]

Mwokozi ametoa maisha Yake ya thamani ili kuanzisha kanisa lenye uwezo wa kuhudumia wanaoteseka, wenye huzuni, na wale wanaojaribiwa. Kundi la waumini laweza kuwa na ufukara, kukosa elimu, na kutojulikana; lakini katika Kristo wanaweza kufanya kazi nyumbani, katika jamii, na hata katika “nchi za ng’ambo,” ambapo matokeo yake yatakuwa makubwa sana, hata kufikia milele. [MH 106.4; HU Aya ya 45]

Kwa wafuasi wa leo wa Kristo, hawapo chini kuliko vile ambavyo wanafunzi wale wa kwanza walinenewa maneno haya: [MH 106.5; HU Aya ya 46]

“Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi.” “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Mathayo 28:18, 19; Marko 16:15. [MH 106.6; HU Aya ya 47]

Kwetu sisi pia, tunayo ahadi ya uwepo Wake, “Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Mathayo 28:20. [MH 107.1; HU Aya ya 48]

Leo hii hakuna umati wa watu wenye udadisi unaomiminika nyikani ili kumwona na kumsikia Kristo. Leo Sauti Yake haisikiki tena katika mitaa yenye shughuli nyingi. Hakuna kilio kinachosikika kando ya njia, “Yesu wa Nazareti anapita.” Luka 18:37. Hata hivyo neno hili ni la kweli kabisa leo. Kristo hutembea bila kuonekana katika mitaa yetu sasa. Yeye huja kwa jumbe za rehema majumbani mwetu. Yeye hungoja kushirikiana pamoja na wote wanaotafuta kuhudumu katika Jina Lake. Yeye Yuko katikati yetu, ili kutuponya na kutubariki, ikiwa tutampokea. [MH 107.2; HU Aya ya 49]

“BWANA asema hivi, Wakati uliokubalika nimekujibu, na siku ya wokovu nimekusaidia; Nami nitakulinda, na kukutoa uwe agano la watu, ili kuiinua nchi, na kuwarithisha urithi uliokuwa ukiwa; akiwaambia wafungwa, Nendeni nje; kwa hao walio gizani, jionyesheni.” [MH 107.3; HU Aya ya 50]

“Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima miguu Yake aletaye habari njema, yeye aitangazaye amani; Aletaye habari njema ya mambo mema, yeye autangazaye wokovu; auambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki. Isaya 49:8, 9, ARV; 52:7 . [MH 107.4; HU Aya ya 51]

“Pigeni kelele za furaha, imbeni pamoja, enyi mahali pa Yerusalemu palipokuwa ukiwa:...

Kwa kuwa Bwana amewafariji watu Wake....

Ameukomboa Yerusalemu. Bwana ameweka wazi mkono Wake mtakatifu Machoni pa mataifa yote; Na ncha zote za dunia Zitauona wokovu wa Mungu wetu.” Mstari wa 9, 10. [MH 107.5; HU Aya ya 52]

SEHEMU YA 2—KAZI YA TABIBU

“Nimewapa kielelezo, ili nanyi mfanye kama nilivyofanya.”

SURA YA 7

USHIRIKIANO WA UUNGU NA UBINADAMU

Katika huduma ya uponyaji tabibu anatakiwa kuwa mtendakazi mwenzi pamoja na Kristo. Mwokozi alihudumia mahitaji mawili, ya mwili na ya roho. Injili ambayo aliifundisha, ilikuwa ni ujumbe wenye kuleta uzima wa kiroho na urejeshaji wa kimwili. Ukombozi toka kwenye dhambi na uponyaji wa magonjwa viliunganishwa pamoja. Huduma hiyo hiyo imekabidhiwa kwa tabibu Mkristo. Tabibu anapaswa kuungana na Kristo katika kusaidia mahitaji ya kimwili na ya kiroho ya wanadamu wenzake. Yeye anapaswa kuwa mjumbe wa rehema kwa wagonjwa, akiwaletea tiba ya mwili uuguao, na pia roho iliyougua dhambi. [MH 111.1; HU Aya ya 1]

Kristo Ndiye mkuu katika taaluma ya tiba. Tabibu mkuu, Yu upande wa kila tabibu mcha Mungu, afanyaye kazi ya kuleta tiba kwa mwanadamu atesekaye. Wakati tabibu anatumia dawa za asili kwa ajili ya magonjwa ya kimwili, anapaswa pia kuwaelekeza wagonjwa wake Kwake Yule ambaye anaweza kuondoa maradhi ya roho na mwili. Kile ambacho matabibu wanaweza kuanza tu kusaidia katika utendaji kwenye mlolongo wa uponyaji, Kristo Ndiye ambaye hukitimiza. Waganga hujitahidi kusaidia utendaji wa maumbile ya asili katika kazi ya uponyaji; Kristo Mwenyewe Ndiye Mponyaji. Daktari hutafuta kuokoa maisha; Kristo hutoa uzima. [MH 111.2; HU Aya ya 2]

Chanzo Cha Uponyaji

Katika miujiza Yake, Mwokozi alifunua uweza utendao daima kwa niaba ya mwanadamu, katika kumtegemeza, kumdumisha na kumponya. Mungu anafanya kazi, kupitia mawakala wa asili, siku baada ya siku, saa baada ya saa, wasaa baada ya wasaa, ili kutuweka sisi hai, kutujenga, kututunza na kutuletea sisi urejeshwaji. Sehemu yo yote ya mwili inapopata jeraha, au changamoto fulani, mchakato wa uponyaji huanza mara moja; maumbile ya asili huwekwa katika utendaji ili kurejesha afya na uzima. Lakini nguvu inayofanya kazi kupitia vyombo hivi ni nguvu Yake Mungu. Nguvu zote za kuupatia mwili uzima zatoka Kwake Mungu. Mtu aponapo ugonjwa alio nao, Mungu Ndiye Mponyaji. [MH 112.1; HU Aya ya 3]

Ugonjwa, mateso, na kifo ni utendaji wa nguvu za upinzani. Shetani ndiye aliye mharibifu na mwangamizaji; Mungu Ndiye mrejeshaji. [MH 113.1; HU Aya ya 4]

Maneno yaliyonenwa kwa Israeli ni ya Kweli hata hivi leo kwa wale wanaopata afya ya mwili au afya ya roho. “Mimi Ndimi Bwana nikuponyaye.” Kutoka 15:26. [MH 113.2; HU Aya ya 5]

Matamanio ya Mungu kwa kila mwanadamu yanaonyeshwa katika maneno haya, “Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.” 3 Yohana 2. [MH 113.3; HU Aya ya 6]

Yeye Ndiye “akusameheaye maovu yako yote; Akuponyaye magonjwa yako yote; aukomboaye uhai wako na kaburi; akuvika taji ya fadhili na rehema.” Zaburi 103:3, 4. [MH 113.4; HU Aya ya 7]

Kristo alipoyaponya magonjwa, aliwapa wengi wa wale waliokuwa wakiteseka onyo hili, “Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi.” Yohana 5:14. Hivyo kwa jinsi hiyo, alifundisha kwamba walikuwa wamejiletea magonjwa wenyewe kwa kuzivunja sheria za Mungu, na kwamba afya ingetuzwa au kuhifadhiwa tu kwa utii. [MH 113.5; HU Aya ya 8]

Daktari anapaswa kuwafundisha wagonjwa wake kwamba wanatakiwa kushirikiana na Mungu katika kazi ya urejeshwaji. Daktari huendelea kupata uelewa endelevu, yaani unaoongezeka wa ule ukweli kwamba ugonjwa ni matokeo ya dhambi. Ajua kwamba sheria za asili ni za Bwana Mwenyewe, kama vile zilivyo Amri kumi Katika Maandiko Matakatifu, na kwamba ni katika kuzitii sheria tu ndipo afya inaweza kupatikana tena au kutunzwa. Aona watu wengi wakiteseka kama matokeo ya mazoea yenye kuumiza, ambapo wangeweza kurejeshewa afya zao ikiwa tu wangefanya yale wawezayo kuelekea kwenye urejeshwaji huo. Wanahitaji kufundishwa kwamba kila mazoea yanayoharibu nguvu za mwili, akili, au za roho ni dhambi, na kwamba afya inapaswa kulindwa kupitia utii wa sheria ambazo Mungu ameziweka kwa ajili ya manufaa ya wanadamu wote. [MH 113.6; HU Aya ya 9]

Pale tabibu ajapomwona mgonjwa anayeugua ugonjwa unaosababishwa na ulaji na unywaji usiofaa au mazoea mengine mabaya, lakini anapuuza kumwambia jambo hilo, yeye anamdhuru mwenzake. Walevi, wenda wazimu, na watu waliojiingiza katika anasa zenye tamaa mbaya, wote humsukuma tabibu atoe mwito wa waziwazi kwa wagonjwa kwamba mateso hutokana na dhambi. Wale wanaoelewa kanuni za afya wanapaswa kuwa wanyofu katika utendaji wa bidii ili kukabiliana na mambo yale yanayosababisha magonjwa kwa wanadamu. Matabibu waonapo hali ya maumivu yanayoendelea kwenye maisha ya mgonjwa, kwa vile daima wao wanahusika katika utendaji kazi wa kupunguza mateso, je hawa daktari awezaje basi kunyamaza kimya bila ya kusema jambo lolote kuhusu hali hii? Je, tabibu huyu atakuwa, mwema, mkarimu na mwenye rehema kweli kwa wagonjwa ikiwa atanyamaza kimya, na kutofundisha kuwa mtu anapaswa kuwa na mwenendo haswa wa kuwa kiasi kama tiba ya kuponya ugonjwa? [MH 114.1; HU Aya ya 10]

Na iwekwe wazi kwamba kufuata amri za Mungu ndio kuifuata njia ya uzima. Mungu ameziweka sheria za asili, lakini sheria Zake si amri kali zilizokaa kama hazina maana. Kila neno “Usifanye au usitende,” iwe katika sheria ya kimwili

au ya maadili, ina maana ya ahadi. Tukiitii, baraka zitaandama katika hatua zetu. Mungu kamwe hatulazimishi kutenda mema, lakini hutafuta kutuokoa na uovu na kutuongoza kwenye mema. [MH 114.2; HU Aya ya 11]

Umakini na uelekezwe kwenye sheria ambazo Israeli ilifundishwa. Mungu aliwapatia maelekezo hususani kuhusu mazoea na mitindo yao ya maisha. Aliwajulisha sheria zinazohusiana na hali bora ya kimwili na kiroho; na kwa sharti la utii wao, Yeye aliwahakikishia kwa kusema kwamba, “Bwana atakuondolea ugonjwa wote.” Kumbukumbu la Torati 7:15. “Yawekeni mioyoni mwenu Maneno yote ambayo nashuhudia kwenu hivi leo.” “Kwa maana ni uhai kwa wale wazipatao, na afya ya mwili wao wote.” Kumbukumbu la Torati 32:46; Mithali 4:22. [MH 114.3; HU Aya ya 12]

Mungu anatamani sisi tufikie kiwango cha ukamilifu ambacho alikifanya kuwezekana kwa ajili yetu kupitia zawadi ya Kristo. Atuita tufanye uchaguzi wetu kwenye upande sahihi, kwamba tuungane na mawakala wa mbinguni, tuchukue kanuni ambazo zitaturejeshea ndani yetu sura ya Mungu. Katika Neno Lake lililoandikwa na katika kitabu kikuu cha asili, Yeye amefunua kanuni za uzima. Ni kazi yetu kujipatia ujuzi wa kanuni hizi, na kwa utii kushirikiana Naye katika kurejesha afya ya mwili na roho. [MH 114.4; HU Aya ya 13

Wanadamu wanapaswa kujifunza kwamba baraka za utii, katika ukamilifu wake, zaweza kuwa zao tu wakiipokea neema ya Kristo. Ni neema Yake, ndiyo inayompatia mwanadamu uwezo wa kutii sheria za Mungu. Hii ndiyo imwezeshayo mtu kuvunja utumwa wa tabia mbaya. Hii ndiyo nguvu pekee inayoweza kumfanya na kuendelea kumdumisha katika kuwa imara kwenye njia iliyo sawa. [MH 115.1; HU Aya ya 14]

Injili inapopokelewa katika uhalisia wa usafi na nguvu zake, ni tiba ya magonjwa yanayotokana na dhambi. Jua la Haki huchomoza, “likiwa na uponyaji katika mbawa Zake.” Malaki 4:2. Sio kila ambacho ulimwengu huu unakitoa kinachoweza kuponya moyo uliovunjika, au kutoa amani ya moyo, au kuondoa masumbufu, au kufukuza magonjwa. Umaarufu, akili nyingi, talanta—yote haya hayana uwezo wa kufurahisha moyo wenye huzuni au kurejesha maisha yaliyotumiwa vibaya. Uzima wa Mungu nafsini ndio tumaini pekee la mwanadamu. [MH 115.2; HU Aya ya 15]

Upendo ambao Kristo huutawanya mwilini mwote ni nguvu imleteayo mtu uhai. Kila sehemu muhimu—ubongo, moyo, na mishipa ya fahamu—pendo hilo huviguswa kwa uponyaji. Kwa pendo Lake, viungo vyote vya mwili wa mtu huamshwa ili vitende kazi. Pendo hili huweka huru roho kutoka kwenye hatia na huzuni, wasiwasi na masumbufu, ambayo hukandamiza misukumo nguvu za uhai. Pamoja nao huu upendo, huja utulivu, kujitawala nafsi na amani. Unapandikiza ndani ya nafsi ya mtu furaha ambayo hakuna kitu duniani kinachoweza kuiharibu,—furaha katika Roho Mtakatifu,—iletayo afya- na kumpa mtu furaha ya uzima. [MH 115.3; HU Aya ya 16]

Maneno ya Mwokozi wetu, “Njooni Kwangu,... Nami nitawapumzisha” (Mathayo 11:28), ni maelekezo ya tiba na dawa kutoka kwa Tabibu kwa ajili ya uponyaji wa maradhi ya kimwili, kiakili, na kiroho. Ingawa wanadamu wamejiletea mateso au kuugua, kwa makosa yao wenyewe, Yeye huwatazama kwa huruma. Katika Yeye wanaweza kupata msaada. Atafanya mambo makubwa kwa wale wanaomtumainia. [MH 115.4; HU Aya ya 17]

Ingawa kwa muda mrefu dhambi imekuwa ikikomaa kwa jamii ya wanadamu, ingawa kwa njia ya uongo, ujanja na udanganyifu Shetani ameweka kivuli chake cheusi, cha tafsiri yake kuhusu Neno la Mungu, na kuwafanya watu watilie shaka wema Wake; lakini bado huruma na upendo wa Baba havijakoma kutiririka kuelekea duniani kwa wingi tele. Endapo wanadamu wangefungua madirisha ya roho kuelekea mbinguni, kwa kuthamini vipawa vya Bwana, basi mafuriko ya wema wa uponyaji yangemiminika kwao. [MH 116.1; HU Aya ya 18]

Tabibu anayetamani kuwa mfanyakazi mwenza anayekubalika pamoja na Kristo atajitahidi kuwa hodari katika kila kipengele cha kazi yake. Atajifunza kwa kusomea mambo yote husika kwa bidii, ili aweze kuwa na stahiki ihusuyo majukumu anayotarajiwa kuyafanya katika taaluma yake na daima atajibidisha kufikia viwango vya juu zaidi, akitafuta maarifa zaidi, mbinu na ubunifu wa juu zaidi, na uelewa wa kina zaidi. Kila daktari anapaswa atambue kuwa yule afanyaye kazi kwa dhaifu, na isiyo na ufanisi au kuridhisha, sio tu kwamba anawaumiza wagonjwa, bali pia anawakosea haki madaktari wenzake au wale wanaofanana naye katika sifa za kitaaluma. Tabibu ambaye anaridhika na viwango vya chini vya ujuzi na maarifa, sio tu anaidharau na kuipunguzia thamani taaluma ya utabibu, bali pia anamkosea heshima na kumwaibisha Kristo, ambaye ni Tabibu Mkuu. *(Msisitizo: Tabibu katika maelezo ya kitabu hiki inatumika kwa ye yote yule anayeagiza tiba au dawa – yaani Practioner mtu anayetoa agizo la tiba yaani Prescription, huyu anaweza kuwa mkunga, nesi, mtaalamu wa fiziotherapia, mwanasaikolojia, tabibu wa tiba asili –naturalpathic doctor, Medical Assistant au Physician Assistant– Msaidizi wa Daktari ambaye anatoa tiba kwa kuandika dawa, au mazoezi nk)*. [MH 116.2; HU Aya ya 19]

Wale ambao wanaona kwamba hawajakidhi vigezo vya kazi hii ya tiba, kwa ujuzi na maarifa, wanapaswa kuchagua kazi nyingine. Wale ambao wana uzoefu wa kutunza wagonjwa, lakini ambao elimu na sifa zao katika taaluma ya tiba ni ndogo, wangefanya vyema kuchukua sehemu za kazi zinazoonekana kama za chini, wakihudumu kwa uaminifu kama wauguzi. Kwa huduma yenye uvumilivu chini ya matabibu stadi wanaweza kuendelea wakijifunza daima, na kwa kuboresha kila fursa ya kupata ujuzi wanaweza baada ya muda kuwa na sifa za kustahili kazi ya udaktari. Matabibu walio na umri mdogo “kama wale watendao

kazi pamoja Naye [Tabibu Mkuu], ... wasiipokee neema ya Mungu bure, ... bila kuwa kikwazo kwa namna yo yote katika jambo lolote, ili huduma [ya wagonjwa] isilaumiwe; bali katika mambo yote tujipatie sifa njema kama watumishi wa Mungu." 2 Wakorintho 6:1-4. [MH 116.3; HU Aya ya 20]

Kusudi la Mungu kwetu sisi ni kwamba daima tuzidi kusogea kuelekea juu. Daktari aliye mmishonari wa kitabibu wa kweli atakuwa na utaalamu unaozidi kuongezeka. Madaktari Wakristo wenye vipawa, na uwezo wa kitaaluma wa hali ya juu, wanapaswa kutafutwa na kutiwa moyo kushiriki katika utumishi wa Mungu katika sehemu ambapo wanaweza kuelimisha na kuzoeza wengine wawe wamishonari wa kitabibu. [MH 117.1; HU Aya ya 21]

Tabibu anapaswa kukusanya nafsini mwake nuru ya Neno la Mungu. Anapaswa kukua daima katika neema. Dini au mambo ya kiroho kwake hayapaswi kuwa moja tu ya kipengele kidogo sana. Bali yapaswa itawale mambo yote. Tabibu anapaswa kutenda kutoka kwenye nia za juu, zilizo tukufu—nia ambazo zina nguvu kwa sababu zinatoka kwa Yule aliyeyatoa maisha Yake ili kutupa sisi uwezo wa kushinda uovu. [MH 117.2; HU Aya ya 22]

Ikiwa tabibu anajitahidi kwa uadilifu na bidii kujipatia ufanisi na kufuzu katika taaluma yake, naye akijiweka wakfu kwenye utumishi wa Kristo, na akichukua muda wa kuuchunguza moyo wake mwenyewe, basi, ataelewa jinsi ya kuzifahamu siri na mafumbo ya wito wake mtukufu. Anaweza kujitia nidhamu na kujielimisha kiasi kwamba wote walio ndani ya mazingira ya kuvutiwa naye watautambua ubora wa elimu na hekima anayoipata mtu yule aliyeunganishwa na Mungu Mwenye hekima na nguvu. [MH 117.3; HU Aya ya 23]

Hakuna mahali ambapo ushirika wa karibu na Kristo unahitajika kama katika kazi ya utabibu. Yeye ambaye ataweza kutimiza wajibu na jukumu la udaktari inavyopaswa, ni lazima kila siku na kila saa aishi maisha ya Kikristo. Uhai wa mgonjwa uko mikononi mwa daktari. Uchunguzi wa ugonjwa kizembe (mfano kusema mtu anaumwa ugonjwa ambao hana), kutoa tiba isiyo sahihi (dawa, upasuaji n.k), katika kumhudumia mgonjwa mahututi, au utendaji usio na ustadi wakati wa huduma ya upasuaji, hata kwa kosa dogo la kiwango cha wembamba wa unywele, yaweza kuondoa uhai wa mtu, na hatimaye roho kunyamazishwa milele. Wazo hili latisha kiasi kikubwa jinsi gani basi! Ni muhimu kiasi gani basi kwamba daktari daima awe chini ya usimamizi wa Tabibu wa mbinguni! [MH 117.4; HU Aya ya 24]

Mwokozi Yu radhi kuwasaidia wote wanaomwita ili kujipatia hekima na mawazo yaliyo shwari. Na ni nani anayehitaji hekima na uwazi wa fikra zaidi kuliko tabibu, ambaye maamuzi yake mengi hutegemea hekima na mawazo mema? Yule anayejaribu kuyarefusha maisha ya wanadamu na amtazame Kristo kwa imani ili aweze kupewa mwongozo katika kila hatua zake. Mwokozi atampa daktari mbinu na maarifa katika kushughulikia magonjwa yenye utata mkubwa. [MH 117.5; HU Aya ya 25]

Walinzi na walezi na watu wanaouguza wagonjwa wamepewa fursa za ajabu. Katika yote yanayofanywa kwa ajili ya urejeshwaji wa wagonjwa, wauguzi na waelewe kwamba tabibu anatafuta njia ya kuwasaidia washirikiane na Mungu katika kupambana na ugonjwa. Wagonjwa waongozwe kutambua kwamba katika kila hatua inayochukuliwa kwa kupatana na sheria za Mungu, wategemee kwa uhakika msaada wa nguvu za kiungu. [MH 118.1; HU Aya ya 26]

Wagonjwa na wanaoteseka watakuwa na ujasiri zaidi na tabibu ambaye wana uhakika kwamba anampenda na kumcha Mungu. Wanayaamini maneno yake. Wanajisikia kuwa wako salama wakiwa kwenye uwepo wake na usimamizi wa daktari huyo. [MH 118.2; HU Aya ya 27]

Kumjua Bwana Yesu, ni upendeleo alio nao tabibu Mkristo, kualika uwepo Wake Bwana katika chumba cha wagonjwa kwa maombi. Kabla ya kuanza kufanya huduma ya upasuaji nyeti, daktari na aombe msaada wa Tabibu Mkuu. Daktari na ampe mgonjwa anayeteseka matumaini kwamba Mungu anaweza kumvusha salama katika changamoto hiyo anayopitia, kwamba katika nyakati zote za taabu Yeye ni kimbilio la uhakika kwa wale wanaomtumaini. Daktari ambaye hawezi kufanya hivi hupelekea katika kuondoa uhai wa watu ambao wangeweza kuokolewa. Laiti tabibu angaliweza kuzungumza maneno ambayo yangehuisha imani ya mgonjwa katika Mwokozi Mwenye huruma, ambaye huhisi kila kilio cha uchungu, na kisha aweze kuwasilisha mahitaji ya nafsi Kwake Bwana katika maombi, naam, mara nyingi, changamoto hizo zingepita salama. [MH 118.3; HU Aya ya 28]

Yeye awezaye kusoma mioyo, Ndiye awezaye kujua wasiwasi na hofu ambavyo wagonjwa wengi hukabiliwa navyo wanaoafiki upasuaji chini ya mkono wa daktari wa upasuaji. Wagonjwa hutambua hatari yao. Ingawa wanaweza kuwa na matumaini katika umahiri wa daktari, bado wanatambua kwamba yeye kama mwanadamu, weledi wake hauna uhakikisho wa kutokukosea kabisa. Lakini wanapomwona daktari ameinama katika sala, akiomba msaada kutoka kwa Mungu, wanatiwa moyo na ujasiri. Shukrani, kutumaini na imani hufungua moyo kwa nguvu ya uponyaji ya Mungu, viungo vya mwili wote huhuishwa, na nguvu za uhai hushinda. [MH 118.4; HU Aya ya 29]

Uwepo wa Mwokozi ni ishara ya uwepo wa nguvu kwa daktari pia. Mara nyingi majukumu na mambo mengine yahusianayo na kazi yake humletea hofu moyoni mwake wakati anapoyafikiria. Pilikapilika zihusuzo kazi yake, wasiwasi wa kutokuwa na uhakika kuhusu ugonjwa wa mwathirika au tiba ya aina fulani, na hofu vyaweza kuufanya mkono wa tabibu kutokuwa na umahiri au weledi unaotakiwa. Lakini hakikisho kwamba Mshauri wa mbinguni Yuko karibu naye ili kumwongoza na kumtegemeza, huleta utulivu na ujasiri. Mguso wa Kristo kwenye mkono wa daktari huleta nguvu tendaji, uchangamfu, utulivu, ujasiri, na uwezo. [MH 119.1; HU Aya ya 30]

Pale changamoto ijapopita na kwisha kwa usalama, na kisha mafanikio yanaonekana wazi kwamba yapo njiani, daktari tumia dakika chache katika sala na mgonjwa. Onyesha shukrani zako kwa maisha ambayo yamehifadhiwa (mtu amepona). Jinsi maneno ya shukrani yanavyotiririka kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa daktari, sifa na shukrani hizo zielekezwe kwa Mungu. Mweleze mgonjwa kwamba maisha yake yameokolewa kwa sababu alikuwa chini ya ulinzi wa Tabibu wa mbinguni. [MH 119.2; HU Aya ya 31]

Tabibu anayefuata njia hiyo anamwongoza mgonjwa wake kwa Yule ambaye maisha yake tabibu yanategemea Kwake, Yule ambaye anaweza kuwaokoa kabisa wote wanaokuja Kwake. [MH 119.3; HU Aya ya 32]

Matamanio makubwa katika kazi ya umishenari wa kitabibu, yanapaswa yawekwe kwenye roho za watu. Kwa mganga kama ilivyo kwa mchungaji, yeye amepewa dhamana ya juu zaidi iliyowahi kukabidhiwa kwa mwanadamu. Haijalishi anatambu jambo hili au la, kila mganga amekabidhiwa kazi ya kutibu roho za watu. [MH 119.4; HU Aya ya 33]

Katika kazi yao ya kushughulika na magonjwa na kifo, mara nyingi sana madaktari hupoteza ufahamu wa mambo yaliyo mazito na halisi katika maisha yajayo. Katika juhudi zao za dhati za kuepusha hatari iliyomo kwenye miili ya wagonjwa, wanasahau hatari ya roho ya mtu. Yule wanayemhudumia huenda akapoteza uwezo wake wa kuishi-naye akafariki. Fursa zake za mwisho zinateleza kutoka mikononi mwake. Daktari aelewe kwamba atakutana na nafsi hii tena kwenye kiti cha hukumu cha Kristo. [MH 119.5; HU Aya ya 34]

Mara nyingi twakosa baraka za thamani zaidi kwa kupuuzia kusema neno la kufaa katika majira yanayofaa. Ikiwa fursa ya dhahabu haijalindwa kwa uaminifu, basi, hiyo itapotea. Kando ya kitanda cha mgonjwa pasiwe mahali pa mazungumzo yahusuyo Mafundisho makuu ya imani, mabishano, au mada zenye utata. Mtu aliye kitandani na anayeteseka, aelekezwe kwa Yule ambaye Yuko tayari kuwaokoa wote wamjiao kwa imani. Kwa dhati na huruma, jitahidi kwa upole kusaidia nafsi inayozunguka-zunguka kati ya uhai na kaburi. [MH 120.1; HU Aya ya 35]

Tabibu anayejua kwamba Kristo Ndiye Mwokozi wake binafsi, kwa sababu yeye mwenyewe ameongozwa kwenye Kimbilio, anajua jinsi ya kuchukuliana na roho zinazotetemeka, zenye hatia, zenye dhambi na zinazomgeukia yeye ili kupata msaada. Anaweza kujibu swali, “Nifanye nini ili nipate kuokolewa?” Anaweza kusimulia kisa cha upendo wa Mkombozi. Anaweza kuzungumza kutokana na uzoefu wa nguvu ya toba na imani. Kwa maneno rahisi na ya dhati, yeye anaweza kuwasilisha hitaji la nafsi kwa Mungu katika sala na anaweza kumtia moyo mgonjwa pia kuomba na kukubali rehema ya Mwokozi Mwenye huruma. Anapohudumu hivyo kando ya kitanda cha wagonjwa, na kujitahidi kusema maneno yatakayoleta msaada na faraja, Bwana hufanya kazi pamoja naye na kupitia yeye. Jinsi akili ya yule anayeteseka kwa ugonjwa

inapoelekezwa kwa Mwokozi, amani ya Kristo hujaa moyoni mwake, na afya ya kiroho inayomjia inatumiwa kama mkono wa msaada wa Mungu katika urejeshwaji wa afya ya mwili. [MH 120.2; HU Aya ya 36]

Katika kuhudumia wagonjwa, daktari mara nyingi atapata fursa ya kuwahudumia marafiki wa yule anayeumwa. Pale wanapomtazama mgonjwa kando ya kitanda chake cha mateso, wakihisi kutokuwa na uwezo hata tu kwenye umivu moja, mioyo yao italainika. Mara nyingi huzuni iliyofichwa ili watu wengine wasiione, hudhihirishwa kwa daktari. Kisha hiyo inakuwa fursa ya tabibu kuwaelekeza hawa wenye huzuni kwa Yeye ambaye amewaita wale waliochoka na kulemewa na mizigo waje Kwake. Mara nyingi sala inaweza kutolewa kwa ajili yao na pamoja nao, wakiwasilisha mahitaji yao kwa Mponyaji wa maafa na ole zote, Mponyaji wa huzuni zote. [MH 121.1; HU Aya ya 37]

Ahadi za Mungu

Tabibu ana nafasi zenye thamani za kuwaelekeza wagonjwa wake kwenye ahadi za Neno la Mungu. Yeye anapaswa kuleta kutoka katika nyumba ya hazina vitu vipya na vya kale, akizungumza hapa na pale maneno ya faraja na mafundisho ambayo yanatamaniwa. Daktari na afanye akili yake kuwa ghala la mawazo mapya. Hebu na ajifunze Neno la Mungu kwa bidii, ili apate kuzifahamu ahadi Zake. Hebu ajifunze kurudia Maneno ya kufariji ambayo Kristo aliongea wakati wa kipindi cha huduma Yake hapa duniani alipokuwa akitoa masomo Yake na kuponya wagonjwa. Anapaswa kuzungumza juu ya kazi za uponyaji zilizofanywa na Kristo, huruma, upole na upendo vyake. Kamwe asipuuze au kusahau kuzielekeza akili za wagonjwa wake kwa Kristo, Tabibu Mkuu. [MH 121.2; HU Aya ya 38]

Uweza ule ule ambao Kristo aliutumia alipotembea kwa kuonekana kati ya wanadamu umo hata leo katika Neno Lake. Ilikuwa kwa Neno lake ambapo Yesu aliponya magonjwa na kutoa pepo waovu; kwa Neno Lake aliituliza bahari na kuwafufua wafu, na watu walishuhudia kwamba Neno Lake lilikuwa na uweza. Alinena Neno la Mungu, kama alivyonena kwa manabii na waalimu wote wa Agano la Kale. Biblia nzima ni udhihirisho wa Kristo. [MH 122.1; HU Aya ya 39]

Maandiko yanapaswa kupokelewa kama Neno la Mungu kwetu, si kwa kuandikwa tu, bali kunenwa. Wale walioteseka walipomjia Kristo, hakuona tu wale walioomba msaada, bali wote ambao katika vizazi vyote wangelimjia kwa hitaji sawa na hilo na kwa imani ile ile. Alipomwambia yule aliyepooza, “Jipe moyo mwanangu; umesamehewa dhambi zako;” alipomwambia yule mwanamke wa Kapernaumu, “Binti, uwe na moyo mkuu, imani yako imekuponya; enenda zako kwa amani,” Kristo alikuwa amezungumza pia na wengine walioteseka, na wenye kulemewa na dhambi ambao watatafuta msaada Wake. Mathayo 9:2; Luka 8:48. [MH 122.2; HU Aya ya 40]

Ndivyo ilivyo kwa ahadi zote za Neno la Mungu. Ndani ya hizo Yeye hunena nasi mmoj mmoja, kama vile ambavyo tungekuwa tunaisikia sauti kama tungesimama naye mbashara. Ni kwa kupitia ahadi hizi ndiyo Kristo hutubarikia neema na uweza Wake. Ahadi hizi ni majani yatokayo katika ule mti ambao una "uponyaji wa mataifa." Ufunuo 22:2. Na ahadi hizi zikipokelewa, na kuingizwa rohoni, zitakuwa nguvu ya tabia, msukumo unaomtia moyo mtu na riziki za maisha (chakula, nguvu, kinywaji, na lishe ya maisha). Hakuna kingine cho chote kinachoweza kuwa na uponyaji kama huo. Hakuna kingine cho chote kinachoweza kutoa ujasiri na imani vitoavyo uhai wa viungo kwenye mwili wote (kiroho, kimwili, kijamii, kiuchumi na kiakili). [MH 122.3; HU Aya ya 41]

Kwa yule anayesimama akitetemeka kwa woga wa kuichungulia mauti, kwa mtu aliyechoka na mzigo wa maumivu, mateso na dhambi, basi daktari kila apatapo fursa na arudie-rudie maneno haya ya Mwokozi—kwa maana maneno yote ya Maandiko Matakatifu ni Yake: [MH 122.4; HU Aya ya 42]

"Usiogope, kwa maana nimekukomboa, nimekuita kwa jina lako; wewe ni Wangu. Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza. Kwa maana Mimi ni Bwana, Mungu wako, Mtakatifu wa Israeli, Mwokozi wako.... Kwa kuwa ulikuwa wa thamani machoni Pangu, umeheshimiwa, Nami nimekupenda." "Mimi, naam, Mimi, Ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili Yangu Mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako." "Usiogope, kwa maana Mimi ni pamoja nawe." Isaya 43:1-4, 25, 5. [MH 122.5; HU Aya ya 43]

"Kama vile baba awahurumiavyo watoto Wake, ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao. Maana Yeye anatujua umbo letu; Anakumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi." Zaburi 103:13, 14. [MH 123.1; HU Aya ya 44]

"Ungama uovu wako tu; ya kwamba umemwasi Bwana, Mungu wako." "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." Yeremia 3:13; 1 Yohana 1:9. [MH 123.2; HU Aya ya 45]

"Nimefuta makosa yako kama wingu zito, na dhambi zako kama wingu; kwa maana nimekukomboa." Isaya 44:22. [MH 123.3; HU Aya ya 46]

"Haya Njoni sasa tusemezane, asema Bwana; dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu. Mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi." Isaya 1:18, 19. [MH 123.4; HU Aya ya 47]

"Naam Nimekupenda kwa upendo wa milele; ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili Zangu." "kwa ghadabu ifurikayo nalikuficha uso Wangu nukta moja;

lakini kwa fadhili za milele nitakurehemu, asema Bwana Mkombozi wako." Yeremia 31:3; Isaya 54:8. [MH 123.5; HU Aya ya 48]

"Msifadhaike mioyoni mwenu." "Amani nawaachieni, amani Yangu nawapa; niwapavyo Mimi si kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga." Yohana 14:1, 27. [MH 123.6; HU Aya ya 49]

"Mtu atakuwa kama mahali pa kujificha na upepo, na mahali pa kujisitiri na tufani; kama mito ya maji mahali pakavu, kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu." Isaya 32:2. [MH 124.1; HU Aya ya 50]

"Maskini na wahitaji wakitafuta maji, wasipate, na ndimi zao zimekauka kwa kiu; Mimi, Bwana, nitawasikia; Mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha." Isaya 41:17. [MH 124.2; HU Aya ya 51]

"Bwana aliyekuumba asema hivi; nitamimina maji juu yake yeye aliye na kiu, na mito juu ya nchi kavu; nitamimina Roho Yangu juu ya uzao wako, na baraka Yangu juu ya uzao wako." Isaya 44:2, 3. [MH 124.3; HU Aya ya 52]

"Niangalieni Mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia." Isaya 45:22. MH 124.4; HU Aya ya 53]

"Yeye aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa yetu." "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu: Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa kKake sisi tumepona." Mathayo 8:17; Isaya 53:5. [MH 124.5; HU Aya ya 54]

SURA YA 8

DAKTARI, MWELIMISHAJI

Daktari wa kweli ni mwelimishaji. Atambua wajibu wake, si tu kwa wagonjwa walio chini ya uangalizi wake wa moja kwa moja, bali pia kwa jamii anayoishi. Anasimama kama mlinzi wa afya ya mwili na maadili. Jitihada yake si tu katika kufundisha njia sahihi za tiba kwa wagonjwa, bali kuhimiza kuwa na mitazamo, mielekeo, tabia na mitindo ya maisha iliyo sahihi, na kueneza maarifa ya kanuni sahihi. [MH 125.1; HU Aya ya 1]

Haja Ya Elimu Katika Kanuni Za Afya

Elimu katika kanuni za afya haijawahi kuhitajika kama ilivyo hivi sasa. Ijapokuwa maendeleo ya kushangaza katika nyanja nyingi zinazohusiana na maisha rahisi na ya kustareheka, na hata katika masuala ya usafi na matibabu ya magonjwa, hali ya kupungua kwa nguvu za kimwili na nguvu za kustahimili imekuwa ya kutisha. Jambo hili hakika linadai umakini kwa wote ambao moyoni mwao wanawiwa na ustawi wa wanadamu wenzao. [MH 125.2; HU Aya ya 2]

Mitindo yetu bandia yahimiza watu kutenda maovu ambayo yanaharibu kanuni njema. Desturi na mitindo ya wanadamu vyakabiliana na asili (mfano kula peremende badala ya kula matunda, kuvaa nguo za kubana n.k). Mazoea na matendo yanayopendelewa na watu, na mambo yote yaendekezwayo yanayohimizwa, vinazidi kupunguza nguvu za kimwili na kiakili kwa uhakika, na kuleta kwenye jamii ya ubinadamu mzigo usiovumilika. Kutokuwa na kiasi na uhalifu, magonjwa na unyonge, vipo kila mahali. [MH 125.3; HU Aya ya 3]

Wengi huvunja sheria za afya kwa kutokujua, na wanahitaji kuelimishwa. Lakini idadi kubwa zaidi wanajua kile kilicho bora kufanya kuliko utendaji wao ulivyo. Wanahitaji kuvutiwa juu ya umuhimu wa kuyafanya maarifa yao kuwa mwongozo wa maisha. Tabibu ana fursa nyingi za kuelimisha kanuni za afya na za kuonyesha umuhimu wa kufanyia kazi mambo haya kwa vitendo. Kwa maelekezo sahihi anapowafundisha wagonjwa, yeye anaweza kufanya mengi yatakayorekebisha maovu ambayo yanaleta madhara yasiyoweza kuelezeka. [MH 126.1; HU Aya ya 4]

Mazoea ambayo yanaweka msingi wa idadi kubwa ya magonjwa na hata maovu ya kutisha ni utumiaji huru wa madawa yenye sumu (dawa za maduka ya

dawa au zo zote zile zisizoendana na zile tiba nane sahili). Wengi wanaposhambuliwa na ugonjwa, hawataki kusumbuka kwa hali au mali kujua chanzo au mzizi wa ugonjwa wao. Wasiwasi wao mkuu upo katika kuyaondoa maumivu na usumbufu wanaopitia. Kwa hiyo hawa hukimbilia kwenye dawa za nostrum* ambazo sifa zake wanazijua kidogo tu, au humwomba daktari dawa fulani ya kukabiliana na matokeo ya makosa yake, lakini bila kufikiria kufanya mabadiliko katika mazoea yao yasiyofaa. Ikiwa kupona hakujaonekana mapema, dawa nyingine inajaribiwa, na kisha nyingine. Hivyo uovu huzidi kuendelea.

Dawa hizi ziliitwa nostrum, ambalo ni ua hapo mbele, na waliamini linatibu karibu kila kitu na kujipatia usemi wa dawa za nostrum. Hii inachukuliwa kama wazo la kusuluhisha shida, haswa kwa njia ambayo sio nzuri sana: Nostrum inarejelea dawa moja inasaidia tiba-yote, au dawa isiyofaa. Kabla ya dawa kudhibitiwa na serikali, kulikuwa na nostrums nyingi zilizouzwa kwa umma. "Mafuta ya nyoka" ni mojawapo ya maarufu zaidi. Ilisemekana kuponya ugonjwa wowote kutoka viungo vya mifupa kuuma hadi nywele kunyonyoka, michanganyiko ya mafuta ya nyoka yalikuwa na viungo kama mafuta ya karafuu, pilipili nyekundu na tapentaini.

Unaweza kurejelea mawazo au nadharia kuhusu nostrums, hasa unapofikiri kuwa ni ya kizamani au ina makosa kwa namna fulani au tiba feki. Ikiwa unarejelea dawa kama nostrum, unamaanisha kuwa haifai au haijajaribiwa kwa njia sahihi ya kisayansi, na pia haina hati miliki. Kwa kifupi Dawa ambayo ufanisi wake haujathibitishwa na viungo vyake kawaida ni siri; dawa ya kitapeli. [MH 126.2; HU Aya ya 5

Watu wanatakiwa kufundishwa kuwa dawa hazitibu au kuponya magonjwa. Ni kweli kwamba nyakati fulani zinaleta nafuu ya muda mfupi, na mgonjwa huonekana kupata nafuu kama matokeo ya dawa hizo; hii ni kwa sababu maumbile ya asili yana nguvu hai ya kutosha kupambana na kuondoa sumu na kisha kurekebisha hali zilizosababisha ugonjwa huo. *(Msisitizo: Mungu ameumba mwili kiasi kwamba 80% ya magonjwa yote hupona yenyewe, bila ya kufanya chochote, kwa vile aliumba mwili ukiwa na vinasaba vya uponyaji ndani yake)*. Afya inarejeshwa licha ya kutokuwa na dawa. Lakini katika matatizo mengi ya kuugua, dawa hubadilisha tu sura na eneo la ugonjwa huo. Mara nyingi athari ya sumu itokanayo na madawa kwa muda huonekana kama haipo, lakini matokeo hubakia kwenye mfumo na hufanya madhara makubwa katika kipindi fulani cha baadaye. [MH 126.3; HU Aya ya 6]

Kwa kutumia dawa zenye sumu, wengi hujiletea wenyewe magonjwa ya kudumu maishani mwao, na watu wengi wamepoteza maisha yao, ambao wangeweza kuokolewa kwa kutumia njia za asili za uponyaji. Sumu zilizomo katika dawa nyingi ziitwzo dawa huunda tabia na hamu ya kula ambayo inamaanisha uharibifu kwa roho na mwili. Nyingi ya dawa hizi maarufu za nostrum, zinazoitwa dawa za kaunta ambazo hazihitaji maagizo au maelekezo ya tiba toka kwa daktari unapotaka kununua (non-Prescription drugs-Rx) na hata baadhi ya dawa zinazotolewa na waganga (za famasia zinazoitwa dawa za magharibi au za wazungu), hushiriki katika kuweka msingi wa tabia ya uraibu wa vileo, wa bangi, uraibu wa mofini, ambazo ni laana mbaya sana kwa jamii (dawa nyingi za maumivu zitumiwapo baada ya muda hujenga uraibu maana ni vileo-narcotic). [MH 126.4; HU Aya ya 7]

Tumaini pekee la mambo yaliyo bora ni katika kuwaelimisha watu kanuni sahihi. Waganga wawafundishe watu kwamba nguvu za urejeshwaji hazipo katika madawa, bali katika asili. Ugonjwa ni juhudi ya maumbile ya asili ya

kuuweka mfumo huru kutoka kwenye hali iliyosababishwa na ukiukaji wa sheria za afya. Pale mtu anapopatwa na ugonjwa, sababu ya kuja kwa huo ugonjwa inapaswa kutambuliwa-kueleweka. Tabia mbaya yafaa zibadilishwe. Mazoea mabaya yarekebishwe. Kisha asili inapaswa kusaidiwa katika juhudi zake za kuondoa uchafu mwili na kuweka upya hali sahihi katika mfumo……

……Mfano wa tabia mbaya kwa afya ni kama vile kutokunywa maji, kutofanya mazoezi, kutolala masaa 8, kutopumzika mara moja kwa juma, kutopata jua na hewa safi, kutokuwa na kiasi, kula chakula kilichokobolewa au kusindikwa, kujiingiza katika mambo yanayokupa msongo kwa kupenda, kunywa pombe, kuvuta sigara, ngono haramu, kupenda ugomvi, kula baada ya saa moja usiku, kusengenya, kunywa kahawa, kunywa chai nyeusi ya mchina, kunywa vinywaji vya nishati (energy drinks), kutamani vitu vya wengine, kuwa na miungu mingine, kutoheshimu wazazi wako, kula katikakati ya milo, kunywa na maji, kutotawala mawazo yako, hizi ndiyo baadhi ya mizizi au shina la shida za afya- sasa tutachukua mfano mmoja, endapo mtu anakula pilipili manga au siki kwenye chakula chake au baking soda ambayo ina tabia ya kumomonyosha ukuta laini wa utumbo, naye akaanza kupata kiungulia na tumbo kumuuma, huyu asianze kwanza kuchukua vidonge vya magnesium bali anapaswa kusema hiki kiungulia kilichoanza kimekuja kwasababu gani? Je ,ni kula chakula kingi kupindukiwa na kuvembewa na hiyo hufanya kifungo cha kwanza na cha pili cha mfumo wa chakula –misuli ya sphincter kisifunge na hivyo chakula kinarudi nyuma au ni pilipili inayokera ukuta wa tumbo, au ni tabia ya kula na kwenda kulala papo hapo nk {1}, Basi afanye majaribio, aache pilipili, au aache kula chakula kingi, au asile baada ya saa 12 jioni, akijua kipi kimeleta hilo jambo mfano pilipili, tabia hiyo mbaya ya kutumia pilipili kwa chakula iondolewe {2} Kisha ausaidie mwili ambao Mungu ameuweka uweze kujirekebisha wenyewe kwa kupambana, kwani asili inasamehe makosa yetu

mengi, ndivyo Mungu alivyo Mwenye rehema, Naye ameuweka mfumo wa mwili wetu hivyo, basi, sasa kwasababu ya muda mrefu wa kiungulia, mambo mengi yamechafuka kwenye mfumo wa chakula, na sasa inabidi kuusaidia mfumo kupona kwa kunywa maji, kula vyakula vinavyokuwa rafiki kwa ukuta wa tumbo mfano, viazi, ndizi, ugali wa mtama n.k {3}. Mpaka hali inavyokuwa nzuri. Vinginevyo mtu atapatwa na magonjwa mengine mengi kwaajili ya tabia hii, kama vile vidonda au kansa ya tumbo n.k. [MH 127.1; HU Aya ya 8]

Tiba Nane asilia

Hewa safi, mwanga wa jua, kuwa na kiasi, pumziko, kufanya mazoezi, chakula kinachofaa, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu na uweza Wake—hizi ndizo tiba za kweli. Kila mtu apaswa kuwa na maarifa ya maumbile ya asili yaletayo uponyaji na jinsi ya kuyatumia (azifahamu tiba nane rahisi na kuzitumia, ikiwemo usafi, roho ya shukrani, mtazamo wa maisha, na kuhudumia watu). Ni muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba ya wagonjwa na kuwa na uzoefu wa vitendo utakaomwezesha mtu kutumia ujuzi huo kwa njia ifaayo. [MH 127.2; HU Aya ya 9]

Matumizi ya tiba za asili yanahitaji kiasi kikubwa cha uangalifu na jitihada, mambo ambayo wengi hawako tayari kuyafanyia kazi. Mchakato wa asili wa uponyaji na kuujenga mwili tena pale ulipoharibika ni wa taratibu ila una uhakika, na kwa wale wasio na subira, huona mambo yanaenda polepole sana kwao. Kusalimisha vile vitu vinavyoendekezwa au kujifurahisha navyo kunahitaji kujitoa kafara. Lakini mwishowe itagunduliwa kwamba asili, isipozuiwa, hufanya kazi yake kwa busara na kwa ubora. Wale wanaodumu katika kuzitii sheria zake watavuna thawabu katika afya zao za mwili na akili…

……Tiba sahili au mbadala zina usumbufu ukilinganisha na kumeza vidonge kwa nukta chache, mfano mtu akiumwa kichwa pengine ni kwa vile analala masaa machache au hanywi maji, mtu huyu anaona kazi kusahihisha tabia mbovu na hivyo anakunywa panadol, na kisha dawa inapokuwa nyingi, inaleta sumu au kansa kwenye ini). [MH 127.3; HU Aya ya 10]

Kwa ujumla, ni usikivu mdogo sana uliopo wa watu kuzingatia suala la afya. Ni bora kuzuia ugonjwa kuliko kujua jinsi ya kuutibu wakati umeupata (Kinga ni bora kuliko tiba au kuzuia ni bora kuliko kuponya). Ni jukumu la kila mtu, kwa

ajili yake mwenyewe, na kwa ajili ya jamii, kujielimisha mwenyewe kuhusu sheria za afya na kudhamiria kuzitii. Kila mtu anahitaji kuelewa kile kishangazacho kuliko vyote, yaani mwili wa binadamu *(Msisitizo: na viungo vyake vya mwili na utendaji ulio wa ajabu kuliko wa viumbe vyote, yaani mwili wa mwanadamu umeumbwa kwa jinsi ya ajabu na kutisha)*. Watu wanapaswa kuelewa kazi za viungo mbalimbali vya mwili na jinsi vinavyotegemeana, kiungo kimoja kinategemea kiungo kingine kwa ajili ya utendaji kazi mzuri wa viungo vyote. Wanapaswa kujifunza ushawishi wa akili juu ya mwili, na wa mwili juu ya akili, na sheria ambazo zinaendesha na kusimamia mwili na akili ya mwanadamu. [MH 128.1; HU Aya ya 11]

Mafunzo Kwa Ajili Ya Kukabiliana Na Maisha

Hatuwezi kukumbushwa mara nyingi kwamba afya haiji kwa bahati nasibu. Afya ni matokeo ya utii wa sheria. Jambo hili linatambuliwa na wanamichezo wanaoshindana katika riadha na mashindano mengine ya michezo ya nguvu (mieleka, masumbwi, kuogelea, kusketi kwenye theluji n.k). Watu hawa hufanya maandalizi makini. Hujisalimisha kwenye mafunzo ya kina na nidhamu ya hali ya juu. Kila mazoea ya mwili hudhibitiwa kwa uangalifu. Wanajua kwamba kupuuzia, kutokuwa na kiasi kwa kufanya vitu kupita kiasi, au uzembe na kutegea, hudhoofisha au kulemaza kiungo cha mwili au utendaji wa mwili, na hali hii ingeleta kushindwa katika shindano. [MH 128.2; HU Aya ya 12]

Je, ni muhimu jinsi gani basi kuwa na uangalifu kama huo ili kuhakikisha tunapata mafanikio katika makabiliano ya maisha. Sisi hatuko katika maigizo (hatuko kwenye drama au movie). Twapigana vita halisi kila siku ambayo ndiyo itakayoamua matokeo yetu kwa umilele. Twakutana na maadui wasioonekana. Malaika waovu wanajitahidi kumdhibiti kila mwanadamu. Cho chote kinachodhuru afya, sio tu hupunguza nguvu za kimwili, lakini pia huelekea kwenye kudhoofisha nguvu za akili na maadili. Kuendekeza mazoea yo yote yasiyo ya afya hufanya iwe vigumu kwa mtu kutofautisha kati ya mema na mabaya, na hivyo kufanya mambo yawe magumu zaidi katika kuupinga uovu. Hali hii huongeza hatari ya kushindwa. [MH 128.3; HU Aya ya 13]

“Wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja?” 1 Wakorintho 9:24. Katika vita ambayo twapigana, wote ambao watajitia nidhamu kwa kutii kanuni sahihi wanaweza kushinda. Matumizi kwa vitendo katika kanuni hizi, kwenye vipengele vya maisha, hutazamwa mara nyingi kana kwamba si jambo la muhimu—suala dogo sana lisilohitaji kuzingatiwa. Lakini tunapozingatia masuala yaliyo hatarini yaani mwili na roho, hakuna hata kimoja tusichopaswa kukichukulia kuwa ni kidogo. Kila tendo linashinikiza uzito wake katika mizani ambayo huamua kufaulu au kushindwa

katika maisha. Maandiko yanatuagiza, “Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate (tuzo).” Kifungu cha 24. [MH 129.1; HU Aya ya 14]

Kwa wazazi wetu wa kwanza, tamaa ya kutokuwa na kiasi ilileta hasara ya kupoteza bustani ya Edeni. Kuwa na kiasi katika mambo yote, yahusiana sana na urejeshwaji wa Edeni kwetu kuliko wanadamu wengi wanavyotambua. [MH 129.2; HU Aya ya 15]

Paulo akionyesha kuwa kujikana nafsi au kujinyima kulikofanywa na washindani katika michezo ya Kigiriki ya kale, aliandika hivi: “Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.” Mistari ya 25-27. [MH 129.3; HU Aya ya 16]

Mafanikio ya matengenezo hutegemea uelewa ulio dhahiri wa zile kweli za msingi alizoziweka Mungu. Wakati, kwa upande mmoja, hatari hujificha katika falsafa na imani za kishupavu, kwa upande mwingine, kuna hatari kubwa katika kuwa huru kiasi cha kutojali. Msingi wa matengenezo yote endelevu ni sheria ya Mungu. Twapaswa kuwasilisha kwa mistari iliyo wazi na bainishi, hitaji la kuitii sheria hii ya Mungu. Kanuni Zake hazina budi kuwekwa mbele ya watu. Na kanuni hizo ni za milele na zisizobadilika kama Mungu Mwenyewe……

> ……*Upande mmoja ni kuwa kama mtu wa dunia/mataifa, na kuwa huru kufanya unavyotaka kwa kulegeza sheria za Mungu–secular, liberal au sadukayo, na upande mwingine ni kugang’amaa kwa ukale na kutobadilika, kuwa mkali na baridi, mnafiki–conservative, farisayo. Sheria ya Mungu ina uwiano yaani balansi. Kwa kutunza sheria Yake, inazitunza sheria za Mungu kama zilivyo yaani conservative/ukale, na humpa mtu aamue yaani uchaguzi– liberal/uhuru, hivyo yote mawili yanafanikiwa). [MH 129.4; HU Aya ya 17]*

Mojawapo ya athari mbaya zaidi za uasi wa awali ilikuwa ni kupoteza uwezo wa mwanadamu wa kujidhibiti (kutawala nafsi, kujikana nafsi). Ni pale tu uwezo huu unapopatikana tena ndipo kunaweza kuwa na mafanikio ya kweli. [MH 129.5; HU Aya ya 18]

Mwili ndio chombo pekee ambacho akili na roho vinakuzwa kwa ajili ya kujenga tabia. Ndiyo maana adui wa roho huelekeza majaribu yake kwenye kudhoofisha na kudhalilisha nguvu za kimwili. Mafanikio yake hapa

yanamaanisha kujisalimisha mwili mzima kwenye uovu (mwili, akili, na roho). Mielekeo ya asili yetu ya kimwili, isipokuwa chini ya utawala wa mamlaka iliyo juu mbinguni, hakika italeta uharibifu na kifo. [MH 130.1; HU Aya ya 19]

Mwili unapaswa kutiishwa. Nguvu za juu za kiumbe ndizo zinapaswa kutawala. Tamaa za mwilini zinapaswa kutawaliwa na dhamiri ya mtu (nia), na dhamiri yenyewe inapaswa kuwa chini ya udhibiti wa Mungu. Nguvu ya kifalme ya kufikiri, iliyotakaswa na neema ya Mungu, inapaswa kubeba fimbo ya utawala ya maisha yetu (hatupaswi kutawaliwa na tamaa zetu za mwili). [MH 130.2; HU Aya ya 20]

Matakwa ya Mungu sharti yaletwe nyumbani kwenye dhamiri zetu. Wanaume na wanawake lazima waamshwe kwenye wajibu wa kuitawala nafsi yao, hitaji la usafi wa moyo, na kuwa huru kutoka kwenye kila tamaa ya mwili iliyo potovu na kila tabia inyochafua. Wanahitaji kuvutiwa na ukweli kwamba nguvu zao zote za akili na mwili ni zawadi kutoka kwa Mungu, na zinapaswa kutunzwa katika hali bora zaidi kwa ajili ya huduma Yake. [MH 130.3; HU Aya ya 21]

Katika kaida za dini za kale ambavyo vilikuwa injili katika ishara, hakuna sadaka yenye dosari ambayo ingeletwa kwenye madhabahu ya Mungu. Dhabihu ambayo ingemwakilisha Kristo lazima isiwe na dosari/waa. Neno la Mungu linaelekeza kwa hili kama kielelezo cha jinsi watoto Wake wanavyopaswa kuwa—“dhabihu iliyo hai,” “takatifu na isiyo na mawaa,” “yenye kumpendeza Mungu.” Warumi 12:1; Waefeso 5:27. [MH 130.4; HU Aya ya 22]

Bila uwezo na nguvu za Bwana, hakuna matengenezo ya kweli yanayoweza kufanyika. Vizuizi vya kibinadamu dhidi ya mielekeo ya asili na ile iliyokuzwa ni kama ukingo wa ukuta uliojengwa kwa mchanga dhidi ya kijito chenye mkondo wenye nguvu. Ni pale tu ambapo maisha ya Kristo yanapokuwa nguvu hai, na kutubidisha mioyo yetu ndipo twaweza kupinga vishawishi vinavyotushambulia ndani yetu na kutoka nje yetu. [MH 130.5; HU Aya ya 23]

Kristo alikuja katika ulimwengu huu na akaiishi sheria ya Mungu, ili mwanadamu awe na uwezo kamili wa kudhibiti na kupata ushindi dhidi ya mielekeo ya asili ambayo huharibu roho. Yeye aliye Tabibu wa nafsi na mwili, Anatupa ushindi dhidi ya tamaa zote za mwili zinazopigana vita mwilini mwetu. Ametoa kila nyenzo bora, ili kila mwanadamu amiliki ukamilifu wa tabia. [MH 130.6; HU Aya ya 24]

Pale mtu anapojisalimisha kwa Kristo, akili inaletwa chini ya udhibiti wa sheria; bali ni sheria ya kifalme, itangazayo uhuru kwa kila aliyetekwa. Kwa kuwa mmoja pamoja na Kristo, mwanadamu anawekwa huru. Kujitiisha na kuwa chini ya mapenzi ya Kristo kunamaanisha kurejeshwa kwa ule utu mkamilifu. [MH 131.1; HU Aya ya 25]

Utii kwa Mungu ni uhuru kutoka katika utumwa mzito wa dhambi na Shetani, ni ukombozi kutoka katika tamaa za mwili na misukumo ya mwanadamu. Mwanadamu anaweza kusimama akiwa mshindi wa nafsi yake mwenyewe, mshindi wa mielekeo yake mwenyewe, mshindi wa falme na mamlaka, na "watawala au wakuu wa giza wa ulimwengu huu," na "majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." Waefeso 6:12. [MH 131.2; HU Aya ya 26]

Hakuna mahali ambapo mafundisho kama haya yanahitajika zaidi, na hakuna po pote ambapo yataleta manufaa makubwa zaidi, kama nyumbani. Wazazi wanapaswa kujenga msingi katika mazoea na tabia. Harakati ya matengenezo lazima ianze katika kuwasilisha kanuni za sheria ya Mungu kama ndizo zinazobeba afya ya mwili na maadili. Onyesha kwamba kulitii Neno la Mungu ndiyo ulinzi wetu pekee dhidi ya maovu ambayo yanafagilia ulimwengu kwenye uangamivu. Weka wazi wajibu wa wazazi, si kwa ajili yao wenyewe tu, bali kwa watoto wao pia. Wazazi wanawapa watoto wao mfano wa kutii au kuasi (matengenezo ya afya au amri za Mungu). Kwa wao kuwa kielelezo pamoja na mafundisho yao, hatima ya kaya/familia zao huamuliwa *(Watoto watakuwa vile wazazi wao wanavyowafinyanga au kuwaumba; kama mfinyazi anavyotengeneza chungu au tunda halianguki mbali na mti, Mungu atuhurumie na kutusaidia kufinyanga jinsi Yeye anavyotupa maelekezo!)*. [MH 131.3; HU Aya ya 27]

Ikiwa wazazi wangeweza kuongozwa katika kufuatilia matokeo ya tendo lao, basi wangeweza kuona jinsi ambavyo kwa mfano wao na mafundisho, huendeleza na kuongeza ama nguvu za dhambi au nguvu za haki, na bila shaka badiliko lingefanywa. Wengi wangeacha mila na desturi, na kukubali kanuni za Bwana za uzima. [MH 131.4; HU Aya ya 28]

Nguvu Ya Kielelezo

Tabibu anayehudumu katika nyumba za watu, ambaye anawatembelea wagonjwa walio vitandani mwao, na kuondoa dhiki zao, akiwarudisha kutoka kwenye mipaka ya kaburi, akiwanenea tumaini wale walio mahututi, yeye ana nafasi ya kuaminiwa na kupendwa nao wagonjwa na hivyo kukubalika kirahisi, fursa ambayo ni wachache tu waliyo nayo. Hata wahudumu wa injili hawana nafasi kubwa ya ushawishi unaofika mbali sana kama ule alio nao tabibu. [MH 132.1; HU Aya ya 29]

Kielelezo cha matendo ya daktari, kama vile mafundisho yake yalivyo, kinapaswa kiwe nguvu nzuri iliyo upande sahihi. Kusudi la kufanya matengenezo lahitaji wanaume na wanawake ambao maisha yao ni kielelezo cha kuitawala nafsi (kwa kuwa na kiasi). Utendaji wetu kwa yale tunayosisitiza ndiyo hutoa uzito na mkazo kwa watu. Ulimwengu unahitaji onyesho la vitendo la kile

ambacho neema ya Mungu inaweza kufanya katika kuwarudishia wanadamu ufalme wao waliopoteza, na kuwapa uwezo wa kujitawala nafsi zao wenyewe. Hakuna kitu ambacho ulimwengu unahitaji sana kama elimu ya uwezo wa kuokoa wa injili unaofunuliwa katika maisha kama ya Kristo. [MH 132.2; HU Aya ya 30]

Daktari hukutana daima na wale wanaohitaji nguvu na kutiwa moyo kwa kielelezo halisi. Wengi ni dhaifu katika nguvu za maadili. Wanapungukiwa na uwezo wa kuitawala nafsi (wanashindwa kujinyima) na wanatekewa na majaribu kwa urahisi. Tabibu anaweza kuzisaidia roho hizi pale tu anapofunua katika maisha yake nguvu ya kanuni inayomwezesha yeye kushinda kila tabia mbaya inayojeruhi mwili na kila tamaa chafu. Katika maisha yake lazima uonekane utendaji kazi wa nguvu ile ambayo ni ya Bwana. Ikiwa atashindwa hapa, hata maneno yake yawe ya msukumo wa kiasi gani au yawe na mvuto wa namna gani, ushawishi wake utaonyesha na kuzungumza uovu tu. [MH 133.1; HU Aya ya 31]

Wengi ambao wameharibikiwa kimaadili kwa sababu ya mazoea yao mabaya hutafuta ushauri wa kitabibu. Hawa wamechubuka, wamedhoofika na wamejeruhiwa, wakihisi upumbavu wao wenyewe na kutokuwa na uwezo wa kushinda. Watu kama hao hawapaswi kuwa na cho chote katika mazingira yao kinachowatia moyo kuendeleza mawazo na hisia ambazo zimewafanya kuwa waathirika na wagonjwa kama walivyo. Wanahitaji kupumua angahewa yenye mazingira ya usafi, yenye mawazo yanayoelekea juu na bora zaidi. Inatisha kiasi gani pale ambapo wale wanaopaswa kuwapa kielelezo kinachofaa (matabibu au watu wa Mungu), wao wenyewe wawe ni wafungwa wa mazoea yenye kuumiza, na ushawishi wao ukawa wenye kuhamasisha majaribu yenye nguvu zaidi kwa wagonjwa! [MH 133.2; HU Aya ya 32]

Tabibu na Kazi ya Kiasi

Wengi ambao wanaharibu roho na mwili wao wenyewe kwa kutumia tumbaku au kileo hutafuta msaada wa madaktari na kuwa chini ya usimamizi wao. Daktari ambaye ni mkweli na mwaminifu kwa wajibu wake lazima awaonyeshe waathirika hawa sababu au chanzo cha tatizo au ugonjwa unaowatesa. Lakini ikiwa daktari mwenyewe ni mtumiaji wa tumbaku au vileo, maneno yake yatachukuliwaje? Akiwa anajitambua kuhusu kujiendekeza kwake mwenyewe na tabia mbovu, je hatasita kubainisha sababu halisi ya ugonjwa/tauni katika maisha ya mgonjwa wake? Wakati yeye mwenyewe anavitumia vitu hivi viovu, je, anawezaje kuwafanya vijana wasadiki kuhusu tabia zao zenye madhara mabaya? [MH 133.3; HU Aya ya 33]

Je! Tabibu anawezaje kusimama katika jumuiya kama kielelezo cha usafi na kujitawala nafsi, awezaje kuwa mfanyakazi mwenye matokeo yenye ufanisi katika mambo ya kiasi, hali yeye mwenyewe anaendekeza mazoea mabaya? Je,

awezaje kuhudumu kwa njia inavyokubalika kando ya kitanda cha hawa wagonjwa na watu walio kifoni, wakati pumzi ya mdomo wake mwenyewe inakera, na kujaa harufu ya vileo au tumbaku? (kama yeye hana kiasi, atakuwaje mfano kwa mwingine) [MH 134.1; HU Aya ya 34]

Wakati anaendelea kuvuruga mishipa yake ya fahamu na kufifisha ubongo wake kwa kutumia sumu za vileo (zikiwemo dawa za hospitalini za aina fulani), awezaje kuwa mwaminifu kwa dhamana iliyokabidhiwa kwake kama daktari bingwa? Ni jinsi gani isivyowezekana kwa tabibu huyu kutambua mambo upesi au kutekeleza wajibu wake kwa usahihi! [MH 134.2; HU Aya ya 35]

Ikiwa hafuati sheria zinazoongoza nafsi yake mwenyewe, akichagua kukidhi matamanio ya mwilini juu ya kuwa na utimamu wa akili na mwili, je, hajitangazi kuwa hafai kukabidhiwa dhamana ya maisha ya wanadamu? [MH 134.3; HU Aya ya 36]

Haijalishi kwamba daktari anaweza kuwa na umahiri wa stadi yake na uaminifu wa kiasi gani, kuna mengi ya kumvunja moyo na kumletea kushindwa katika uzoefu wake. Mara nyingi kazi yake inashindwa kutimiza kile anachotamani kuona kikitimizwa. Ingawa wagonjwa wake wanapona, huenda kusiwe na faida yo yote kwao au kwa ulimwengu. Wengi baada ya afya zao kurejea, hurudia tu kwenye yale waliyokuwa wakiyaendekeza hapo awali ambayo ndiyo yaliyosababisha ugonjwa. Wakiwa na shauku sawa na hapo awali, wanatumbukia tena katika mzunguko wa kujifurahisha na upumbavu. Kazi ya daktari kwao inaonekana kama juhudi iliyotupwa jalalani. [MH 134.4; HU Aya ya 37]

Kristo alipitia uzoefu kama huo, lakini Yeye hakukoma katika juhudi Zake kwa ajili ya nafsi moja inayoteseka. Kati ya wakoma kumi waliotakaswa, ni mmoja tu aliyethamini zawadi hiyo, tena alikuwa mtu baki na Msamaria. Ni kwa ajili tu ya huyo mmoja, Kristo aliwaponya wale wote kumi. Ikiwa daktari hatakutana na mafanikio bora katika kazi kuliko yale Mwokozi aliyoyapata, hebu ajifunze somo kutoka kwa Tabibu Mkuu. Kuhusu Kristo imeandikwa, “Hatazimia wala hatakata tamaa. “Ataona taabu ya Nafsi Yake, na kuridhika.” Isaya 42:4; 53:11. [MH 134.5; HU Aya ya 38]

Ikiwa hata mtu mmoja atakubali Injili ya neema Yake, Kristo atamwokoa huyo, na angeyachagua maisha Yake ya taabu na fedheha na kifo Chake cha aibu kwa ajili ya mtu huyo mmoja. Ikiwa jitihada zetu za kumwinua hata mwanadamu mmoja tu zitafanikiwa, naye akaadilishwa, na kisha akafaa kung’ara katika nyua za Bwana, je basi, sisi hatuna sababu ya kufurahi? [MH 135.1; HU Aya ya 39]

Majukumu ya daktari ni magumu na yenye mtihani mkubwa. Ili kuyatekeleza kwa mafanikio zaidi tabibu anahitaji kuwa mkamilifu wa mwili na afya njema. Mtu ambaye ni dhaifu au mgonjwa hawezi kuvumilia shughuli zenye kuchosha

zinazohusiana na wito wa tabibu. Mtu asiyejidhibiti nafsi kikamilifu hawezi kustahili kushughulika na aina zote za magonjwa. [MH 135.2; HU Aya ya 40]

Mara nyingi daktari hukosa usingizi, anaacha hata kula chakula, anakuwa ametengwa kwa kiwango kikubwa na starehe za kijamii (social enjoyment) na fursa za mambo ya kiroho/kidini (kutokwenda kwenye maombi mara zingine n.k), maisha ya tabibu huonekana yako hivyo daima. Mateso anayoyaona machoni pake, wanadamu tegemezi wanaosihi msaada, kukutana na wale waliokengeuka, huufanya moyo wake uugue, na karibu kupungua ujasiri wake kuwahudumia waathirika. [MH 135.3; HU Aya ya 41]

Katika kukabiliana na maradhi na kifo kila nguvu hushughulishwa na kuchoshwa hadi ustahimilivu unafikia kikomo chake. Mwitikio kutoka kwenye msongo wa aina hii huijaribu tabia haswa. Ndipo lile jaribu linakuwa na nguvu kubwa zaidi. Ukilinganisha na wito unaotolewa kwenye fani nyingine zote, madaktari wanahitaji kujitawala nafsi, kuwa na usafi wa moyo, na imani ile inayoshikilia mbingu. Kwa ajili ya watu wengine na kwa ajili yake mwenyewe, tabibu hawezi kumudu kupuuzia sheria ya mwili. Uzembe katika tabia za kimwili huondoa busara na kumwelekeza mtu kwenye uzembe na upotofu wa maadili. [MH 135.4; HU Aya ya 42]

Usalama pekee wa daktari chini ya hali zote, ni kutenda kutokana na kanuni, kuimarishwa na kuboreshwa na uthabiti wa kusudi lipatikanalo kwa Mungu pekee. Anapaswa kusimama katika ubora wa kimaadili wa tabia Yake. Daima anapaswa kuishi kama yupo machoni pa ulimwengu usioonekana. Kama Musa, ni lazima astahamili “kama anamwona Yeye asiyeonekana.” [MH 135.5; HU Aya ya 43]

Kuhesabiwa haki kuna mizizi yake katika kumcha Mungu. Hakuna mtu anayeweza kudumisha mbele ya wanadamu wenzake maisha safi, na yenye nguvu isipokuwa maisha yake yamesitirika pamoja na Kristo katika Mungu. Kadiri pilikapilika za huduma kwa wanadamu zinavyokuwa nyingi zaidi, ndivyo ushirika wa moyo wa tabibu unavyopaswa kukaribiana zaidi na mbingu. [MH 136.1; HU Aya ya 44]

Kadiri majukumu yake yanavyozidi kuwa ya dharura na makubwa zaidi, ndivyo anavyomhitaji zaidi uweza wa kiungu. Wakati lazima ukombolewe kutoka kwa vitu vya muda, na vya kidunia ili apate kutafakari juu ya mambo ya milele. Ni lazima apinge ulimwengu unaomvamia, ule ambao unambana sana hata kuweza kumtenga na Chanzo cha nguvu zake. Daktari, zaidi ya watu wengine wote, anapaswa kwa maombi na kujifunza Maandiko, kujiweka chini ya ngao ya ulinzi wa Mungu. Anapaswa kuishi daima katika ushirika ulio na utambuzi wa kanuni za kweli, haki, na rehema zifunuazo tabia na sifa za Mungu ndani ya nafsi. [MH 136.2; HU Aya ya 45]

Ni kwa kiwango tu ambacho Neno la Mungu linapokelewa na kutiiwa ndipo litavutia kwa uweza wake na mguso pamoja na maisha yake litavutia kila chemchemi ya utendaji, kila hatua ya tabia. Litatakasa kila wazo, na kuratibu kila tamanio. Wale ambao wanalifanya Neno la Mungu kuwa tumaini lao, watatenda na kuacha historia yao kama watu mashujaa kweli kweli, na kuwa hodari na wenye nguvu. Watainuka juu ya mambo yote duni hadi kwenye angahewa iliyo huru kutokana na unajisi. [MH 136.3; HU Aya ya 46]

Mwanadamu anapokuwa katika ushirika na Mungu, lile kusudi lisiloyumbayumba lililowahifadhi Yusufu na Danieli katikati ya upotovu wa mahakama za kipagani litafanya maisha ya tabibu kuwa ya usafi usiochafuliwa. Mavazi yake ya tabia yatakuwa bila mawaa au dosari. Katika maisha yake nuru ya Kristo haitafifia. Nyota angavu na ya asubuhi itaonekana iking'aa kwa uthabiti juu yake katika utukufu usiobadilika. [MH 136.4; HU Aya ya 47]

Maisha kama haya yatakuwa kipengele chenye nguvu katika jamii. Yatakuwa kizuizi dhidi ya uovu, ulinzi kwa wale wanaojaribiwa, nuru iongozayo wale ambao, katikati ya dunia ya matatizo na kuvunjika moyo, wanaitafuta njia iliyo sahihi. [MH 136.5; HU Aya ya 48]

SEHEMU YA 3—WAMISHONARI TIBA NA KAZI ZAO

"Watakuwa katikati ya watu wengi kama umande utokao kwa BWANA."

SURA YA 9

KUFUNDISHA NA KUPONYA

Kristo alipowatuma wanafunzi kumi na wawili katika safari yao ya kwanza ya umishenari, aliwausia akisema, "Mnapokwenda, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepokea bure, toeni bure." Mathayo 10:7, 8. [MH 139.1; HU Aya ya 1]

Kwa wale Sabini waliotumwa baadaye alisema: "Katika mji wo wote mtakaoingia,... wapozeni wagonjwa waliomo ndani yake, na waambieni, Ufalme wa Mungu umekaribia kwenu. Luka 10:8, 9. Uwepo na uweza wa Kristo vilikuwa pamoja nao, "na wale Sabini wakarudi tena kwa furaha, wakisema, Bwana, hata pepo wanatutii kwa Jina Lako. Kifungu cha 17. [MH 139.2; HU Aya ya 2]

Baada ya kupaa kwa Kristo kazi hiyo hiyo iliendelezwa. Matukio ya huduma Yake yalirudiwa. "Kutoka katika miji ya kandokando umati wa watu ulifika Yerusalemu, ukiwaleta wagonjwa, na wale waliosumbuliwa na pepo wachafu, nao wakaponywa, kila mtu. Matendo 5:16. [MH 139.3; HU Aya ya 3]

Nao wanafunzi “wakatoka, wakahubiri kila mahali, Bwana akitenda kazi pamoja nao.” “Filipo akashuka mpaka mji wa Samaria, akawahubiria Kristo. Na makutano kwa nia moja wakasikiliza yale aliyosema Filipo.... Kwa maana pepo wachafu ... waliwatoka wengi waliopagawa nao; na wengi waliopooza, na viwete, wakaponywa. Kukawa na furaha kubwa katika mji ule." Marko 16:20; Matendo 8:5-8. [MH 139.4; HU Aya ya 4]

Kazi ya Wanafunzi

Luka, mwandishi wa Injili inayobeba jina lake, alikuwa mmishenari wa kitabibu. Katika Maandiko anaitwa “tabibu mpendwa.” Wakolosai 4:14. Mtume Paulo alipata habari za taaluma yake kama tabibu, naye akamtafuta kama mtu ambaye Bwana alikuwa amemkabidhi kazi ya mahsusi. Alilinda ushirikiano na yeye, na kwa wakati fulani Luka aliandamana naye katika safari zake mahali mahali. Baada ya muda, Paulo alimwacha Luka katika mji wa Filipi, huko Makedonia. Hapa aliendelea kufanya kazi kwa miaka kadhaa, kama tabibu na pia mwalimu wa injili. Katika kazi yake kama tabibu, aliwahudumia wagonjwa, na kisha kuomba ili nguvu ya Mungu ya uponyaji ikae juu ya wale watesekao. Na hivyo njia ikafunguliwa kwa ajili ya ujumbe wa injili. Mafanikio ya Luka kama daktari yalimpatia fursa nyingi za kumhubiri Kristo kati ya wapagani. Ni mpango wa Mungu kwamba sisi tutende kazi kama wanafunzi walivyotenda. Uponyaji wa kimwili umefungamanishwa na agizo la injili. Katika kazi ya injili, mafundisho ya Mungu na uponyaji kamwe havipaswi kutenganishwa. [MH 140.1; HU Aya ya 5]

Kazi ya wanafunzi ilikuwa kueneza maarifa ya injili. Kwao ilikabidhiwa kazi ya kutangaza ulimwenguni kote habari njema ambayo Kristo alileta kwa wanadamu. Kazi hiyo waliitimiza kwa ajili ya watu wa wakati wao. Kwa kila taifa chini ya mbingu injili ilipelekwa katika kizazi kimoja hata kingine. [MH 141.1; HU Aya ya 6]

Utangazaji wa injili kwa ulimwengu ni kazi ambayo Mungu ameikabidhi kwa wale walibebao Jina Lake. Kwani tiba na dawa pekee ya dhambi na masaibu ya dunia hii ni injili. Kuwajulisha jamii yote ya wanadamu ujumbe wa neema ya Mungu ni kazi yetu ya kwanza ya wale wanaotambua nguvu yake (injili) ya uponyaji. [MH 141.2; HU Aya ya 7]

Pale Kristo alipowatuma wanafunzi wakiwa na ule ujumbe wa injili, imani katika Mungu na Neno Lake vilikuwa karibu kutoweka duniani. Miongoni mwa Wayahudi, waliodai kuwa na maarifa juu ya Yehova, Neno Lake lilikuwa limewekwa pembeni, na badala yake wakatwaa mapokeo na nadharia za wanadamu. Ubinafsi na kupenda makuu, kujionyesha, na uchu wa kujipatia faida, viliteka mawazo ya wanadamu. Jinsi uchaji wa Mungu ulivyotoweka, vivyo hivyo huruma kwa wanadamu iliondoka. Ubinafsi ulikuwa kanuni inayotawala, na Shetani alitenda mapenzi yake ili kuleta masaibu na udhalilishaji wa jamii ya wanadamu. [MH 142.1; HU Aya ya 8]

Mawakala wa kishetani walipagaa watu. Miili ya wanadamu, iliyoumbwa kwa ajili ya makao ya Mungu, ikawa makao ya pepo wachafu. Milango ya utambuzi, mishipa ya fahamu, na viungo vya wanadamu vilifanya kazi kwa nguvu za mawakala wasio wa kawaida katika kuendekeza tamaa mbaya za mwili. Chapa yenyewe ya mapepo ilipigwa kwenye nyuso za wanadamu. Nyuso za wanadamu ziliakisi mwonekano wa jeshi la uovu ambalo lilikuwa limewapagaa wanadamu. [MH 142.2; HU Aya ya 9]

Je, leo hali ikoje duniani? Je, imani katika Biblia haiharibiwi kikamilifu kwa ukosoaji, nadharia na uvumi wa siku hizi kama ilivyokuwa zama zile ilivyoharibiwa kwa mapokeo na mafundisho ya kidini katika siku za Kristo? Je, tamaa ya mali na makuu na kupenda anasa havijashikilia mioyo ya watu sasa kama ilivyokuwa wakati huo? Katika ulimwengu unaodai kuwa wa Kikristo, hata katika makanisa yanayodai kuwa ya Kristo, Je, ni wachache kiasi gani wanaoongozwa na kanuni za Kikristo. Katika biashara, mahusiano ya jamii, majumbani, na hata katika maisha ya kidini, ni wachache kiasi gani wanaofanya mafundisho ya Kristo kuwa kanuni ya maisha yao ya kila siku. Je, si kweli kwamba “haki imesimama mbali: ... haki haiwezi kuingia.... Na yeye ajiepushaye na uovu anajifanya kuwa mateka/mawindo”? Isaya 59:14, 15. [MH 142.3; HU Aya ya 10]

Twaishi katikati ya “mlipuko wa uhalifu,” ambapo watu wenye kufikiri, walio na busara, na wanaomcha Mungu kila mahali wanashtuka kwa tishio hilo. Upotovu unaoshamiri, kalamu ya kibinadamu haiwezi kuuelezea. Kila siku hufunua mambo mapya ya magomvi ya kisiasa, rushwa, na ulaghai. Kila siku hufunua rekodi inayohuzunisha moyo ya ukatili na uasi wa sheria, ripoti za kutojali mateso ya wanadamu, ukatili, udhalimu vinavyoleta uangamivu wa maisha ya mwanadamu. Kila siku inadhihirisha kuongezeka miongoni mwa watu wenda wazimu, mauaji, na kujiua. Ni nani anayeweza kutilia shaka kwamba mawakala wa kishetani wanafanya kazi miongoni mwa wanadamu pamoja na kushughulika zaidi katika kuvuruga, kupotosha akili, na kuunajisi na kuuharibu mwili? [MH 142.4; HU Aya ya 11]

Na wakati ulimwengu ukiwa umejaa maovu haya, injili mara nyingi huwasilishwa kwa namna ya kutojali sana kiasi cha kutambuliwa kidogo tu kwenye dhamiri au maisha ya wanadamu. Kila mahali kuna mioyo inayolilia kitu fulani ambacho haina. Wanatamani nguvu ambayo itawapa uwezo wa kushinda dhambi, nguvu ambayo itawakomboa toka katika utumwa wa uovu, nguvu ambayo itawapatia afya, uzima na amani. Wengi ambao hapo awali walijua nguvu ya Neno la Mungu wamekaa mahali ambapo hakuna Mungu hatambuliwi, na wanatamani uwepo wa kiungu. [MH 143.1; HU Aya ya 12]

Ulimwengu leo unahitaji kile ulichokihitaji miaka elfu mbili iliyopita—ufunuo wa Kristo. Kazi kubwa ya matengenezo inahitajika, na ni kwa neema ya Kristo

tu kwamba kazi ya urejeshwaji wa kimwili, kiakili na kiroho inaweza kukamilishwa. [MH 143.2; HU Aya ya 13]

Mbinu ya Kristo pekee ndiyo itatoa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alichangamana na wanadamu kama mtu aliyewatakia mema. Alionyesha huruma Yake kwao, akahudumia mahitaji yao, Naye akaaminika kwao. Kisha akawaambia, “Nifuateni.” [MH 143.3; HU Aya ya 14]

Kuna haja ya kuja karibu na watu kwa juhudi binafsi. Kama muda kidogo ungetengwa kwa ajili ya mahubiri, na muda mwingi zaidi ungetumiwa katika huduma binafsi kwa watu, matokeo makubwa zaidi yangeonekana. Maskini hawana budi kuponywa, wagonjwa wajaliwe, walio na huzuni na waliofiwa wafarijiwe, wasio na maarifa waelekezwe, wasio na uzoefu washauriwe. Hatuna budi kulia pamoja na wale wanaolia, na kufurahi pamoja na wale wanaofurahi. Ijapoambatana na nguvu ya ushawishi, nguvu ya maombi, na nguvu ya upendo wa Mungu, kazi hii haitaweza, na wala haiwezi kukosa matunda. [MH 143.4; HU Aya ya 15]

Twapaswa kukumbuka daima kwamba kusudi la kazi ya umishenari wa kitabibu ni kuwaelekeza wanaume na wanawake walio wagonjwa wa dhambi kwa Mtu wa Kalvari, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Kwa kumtazama Yeye, watabadilishwa ili kufanana na Yeye. Yatupasa kuwahimiza wagonjwa na wale watesekao kumtazama Yesu na kuishi. Watenda kazi na wamfunue Kristo, Tabibu Mkuu, mbele ya wale ambao ugonjwa wa mwili na roho umewaletea mvunjiko wa moyo. Waelekeze kwa Yule anayeweza kuponya magonjwa ya kimwili na ya kiroho. Waambie kuhusu Yule ambaye huguswa na hisia za magonjwa na udhaifu wao. Wahimize wajiweke chini ya uangalizi wa Yeye aliyetoa maisha Yake ili kuwawezesha wao kupata uzima wa milele. Zungumzia juu ya pendo Lake; simulia juu ya uweza Wake wa kuokoa. [MH 144.1; HU Aya ya 16]

Huu ni wajibu mkuu na fursa ya thamani ya mmishenari wa kitabibu. Na huduma binafsi mara nyingi hutayarisha njia kwa hili. Mara nyingi Mungu hufikia mioyo kupitia jitihada zetu za kupoza pale penye mateso ya mwili. [MH 144.2; HU Aya ya 17]

Kazi ya umishenari wa kitabibu ni kazi inayofungua milango ili kuanzisha kazi ya kupeleka injili. Katika huduma ya Neno na katika kazi ya umishonari wa kitabibu injili inapaswa kuhubiriwa na kutendwa (kuwekwa kwenye vitendo). [MH 144.3; HU Aya ya 18]

Karibu katika kila jumuiya kuna idadi kubwa ya watu wasiosikiliza mahubiri ya Neno la Mungu au kuhudhuria ibada yo yote ya kidini. Ikiwa watafikiwa na injili, basi ni lazima ipelekwe majumbani mwao. Mara nyingi msaada wa mahitaji yao ya kimwili ndiyo njia pekee ambayo wanaweza kufikiwa. Wauguzi wamishenari wanaowatunza wagonjwa na kupoza dhiki ya maskini watapata

fursa nyingi za kuomba pamoja nao, kuwasomea Neno la Mungu, na kuzungumza juu ya Mwokozi. Wanaweza kuomba pamoja na kwa ajili ya wale wasiojiweza ambao hawana nguvu ya dhamiri ya kudhibiti matamanio ambayo tamaa za mwili zimepelekea kuwavunjia heshima. Wanaweza kuleta mwale wa tumaini katika maisha ya wale walioshindwa na waliovunjika moyo. Upendo wao usio na ubinafsi, unaoonyeshwa katika matendo ya fadhili yasiyo na ubinafsi, utafanya iwe rahisi kwa watu wanaougua na kuteseka kuamini katika pendo la Kristo. [MH 144.4; HU Aya ya 19]

Wengi hawana imani katika Mungu na wameshindwa kumwamini mwanadamu. Lakini wanathamini matendo ya huruma na msaada. Wanapomwona mtu asiyechochewa na sifa za kidunia au kulipwa kwa kazi yake akija majumbani mwao kuwahudumia wagonjwa, akiwalisha wenye njaa, akiwavisha walio uchi, akiwafariji wale walio na huzuni, na kuwaelekeza wote kwa upole, kwa Yule ambaye upendo na huruma Vyake, ndiyo hutenda kazi kupitia mwanadamu ambaye ni mjumbe tu—wanapoona hili, mioyo yao huguswa. Shukrani hububujika. Imani yao huamshwa. Nao wanaona kwamba Mungu huwajali, kisha wanakuwa tayari kusikiliza Neno Lake linapofunguliwa. [MH 145.1; HU Aya ya 20]

Iwe ni katika utume kwenye nchi za kigeni au katika eneo la nyumbani, wamishonari wote, waume kwa wake, itazidi kuwa rahisi kwao kuwafikia watu, na wataona manufaa yao yakiongezeka zaidi, endapo wataweza kuwahudumia wagonjwa. Wanawake waendao kama wamishenari katika nchi za kipagani, wanaweza kupata fursa za kuifikisha injili kwa wanawake wa nchi hizi, pale ambapo kila mlango mwingine wa kufikia watu umefungwa. Watendakazi wote wa injili wanapaswa kujua jinsi ya kutoa tiba rahisi (tiba mbadala rahisi) ambayo hutenda kazi kwa ufanisi sana katika kupoza maumivu na kuondoa ugonjwa. [MH 145.2; HU Aya ya 21]

Kufundisha Kanuni Za Afya

Watendakazi wa Injili wanapaswa pia kutoa mafundisho katika kanuni za maisha yenye afya. Kuna magonjwa kila mahali, na mengi ya hayo yanaweza kuzuiwa kwa kuzingatia sheria za afya. Watu wanahitaji kuona umuhimu wa kanuni za afya katika ustawi wao kwenye maisha haya na maisha yajayo. Wanahitaji kuamshwa kwenye wajibu wao kwa ajili ya miili yao iliyoumbwa na Muumba wao kama makao Yake, ambayo Yeye huwataka wawe mawakili waaminifu kwa hayo makao (miili). Wanahitaji kuvutiwa na ile kweli itolewayo katika Maandiko Matakatifu: [MH 146.1; HU Aya ya 22]

“Ninyi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, Nitakaa ndani yao, na ndani yao nitatembea; Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu.” 2 Wakorintho 6:16. [MH 146.2; HU Aya ya 23]

Maelfu wanahitaji mafundisho, na hawa wangeyapokea kwa furaha maagizo yahusuyo njia rahisi za kuwatibu wagonjwa—njia mbadala zinazochukua nafasi ya matumizi ya dawa zenye sumu. Lipo hitaji kubwa la kufundisha kuhusu matengenezo ya lishe, na utayarishaji wa chakula bora. Mazoea mabovu ya ulaji na matumizi ya vyakula visivyokuwa na afya ndivyo vinahusika kwa kiwango kikubwa katika hali ya kukosa kiasi na uhalifu na unyonge ambavyo ni laana kwa ulimwengu. [MH 146.3; HU Aya ya 24]

Katika kufundisha kanuni za afya, weka kipaumbele akilini mwako cha lengo kuu la matengenezo—kwamba kusudi lake ni kudumisha maendeleo ya juu kabisa ya mwili, akili na roho. Onyesha kwamba sheria za asili, ambazo ni sheria za Mungu Mwenyewe, zimekusudiwa kwa ustawi wetu wenyewe; kwamba tujapozitii hizi, huhamasisha furaha katika maisha haya, na husaidia katika kujitayarisha kwa ajili ya maisha yajayo (ya mbinguni). [MH 146.4; HU Aya ya 25]

Waongoze watu wajifunze udhihirisho wa pendo na hekima vya Mungu katika kazi za maumbile ya asili. Waongoze watu kujifunza maumbile yaliyoumbwa kwa jinsi ya ajabu, mfumo wa mwanadamu, na sheria ambazo zinauongoza. Wale ambao wanatambua ushahidi wa upendo wa Mungu, wanaoelewa mambo fulani yahusuyo hekima na manufaa ya sheria Zake, na matokeo ya utii, watafikia hatua ya kuzingatia wajibu na majukumu yao kutoka kwenye mtazamo tofauti kabisa. BadSala ya wao kuona kwamba ushikaji wa sheria za afya ni kama kujitoa mhanga au kujikana nafsi, wataliona jambo hili kuwa ni baraka isiyo na kifani. [MH 147.1; HU Aya ya 26]

Kila mtendakazi wa injili anapaswa kuelewa kwamba uwasilishaji wa mafundisho ya kanuni za maisha bora yenye afya ni sehemu ya wito wa kazi yake aliyoteuliwa kuifanya. Kwenye kazi hii kuna hitaji kubwa, na ulimwengu uko tayari na wazi kwa ajili yake, yaani utaupokea ujumbe huu kwa moyo wote. [MH 147.2; HU Aya ya 27]

Kila mahali yapo mazoea kwa juhudi ya mtu binafsi kuiachia taasisi juhudi hii. Hekima ya kibinadamu ndiyo huongoza kwenye uimarishaji, ujumuishaji, ujenzi wa makanisa na taasisi kubwa. Wengi huziachia taasisi na mashirika kazi ya ukarimu; wanatoa visingizio ili wasichangamane na ulimwengu, na kisha mioyo yao huzizima. Wanakuwa watu waliosongwa na wasiotaka kuguswa mioyo yao. Upendo kwa Mungu na mwanadamu hufa nafsini zao. [MH 147.3; HU Aya ya 28]

Kristo huwakabidhi wafuasi Wake kazi binafsi (iliyo ya pekee kwao kuifanya)—kazi ambayo haiwezi kufanywa na wakala au mtu mwingine. Huduma kwa wagonjwa na watu walio maskini, uhubiri wa injili kwa wale waliopotea, haupaswi kuachwa kwa kamati au mashirika maalum yanayotoa misaada. Wajibu wa mtu binafsi, juhudi binafsi, kujitoa dhabihu binafsi, ndiyo matakwa ya injili. [MH 147.4; HU Aya ya 29]

“Tokeni katika njia kuu na vichochoroni, kisha mkawashurutishe waingie ndani,” ndiyo amri kutoka kwa Kristo, “ili nyumba Yangu ipate kujaa.” Anawaleta watu wakutane na kuwasiliana na wale ambao wanatafuta kuwanufaisha. “Walete maskini waliotupwa nyumbani kwako,” Anasema Bwana. “Unapomwona aliye uchi, umfunike.” “Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Luka 14:23; Isaya 58:7; Marko 16:18. Kupitia mchangamano wa moja kwa moja, kupitia huduma binafsi, baraka za injili zinapaswa kuwasilishwa. [MH 147.5; HU Aya ya 30]

Katika kuwapatia watu Wake nuru hapo zamani, Mungu hakufanya kazi kupitia tabaka moja peke yake. Danieli alikuwa mwana wa kifalme toka Yuda. Isaya pia alikuwa kutoka koo za kifalme. Daudi alikuwa mvulana aliyechunga mifugo, Amosi alikuwa mchungaji wa mifugo, Zekaria alikuwa mateka kutoka Babeli, Elisha alikuwa mkulima. Bwana aliwainua hawa manabii na wakuu wawakilishi wenye vyeo na watu wa hadhi ya chini, Naye akawafundisha zile kweli zinazopaswa kutolewa kwa ulimwengu. [MH 148.1; HU Aya ya 31]

Kwa ye yote ambaye anakuwa mshiriki wa neema Yake Bwana humteulia kazi kwa ajili ya wengine. Kila mmoja wetu anapaswa kusimama katika zamu na mahali pake, akisema, “Mimi hapa Bwana nitume mimi” Isaya 6:8. Wajibu upo juu ya wote, iwe ni mhudumu wa Neno, muuguzi mmishonari, tabibu Mkristo, Mkristo mmoja mmoja, awe ni mfanya-biashara au mkulima, mwana-taaluma au fundi mekanika—wajibu upo juu ya wote. Ni kazi yetu kuwafunulia wanadamu injili ya wokovu wao. Kila shughuli ambayo twajihusisha nayo, inapaswa kuwa daraja la kufanikisha lengo hili. [MH 148.2; HU Aya ya 32]

Wale wanaotwaa kazi waliyoteuliwa kuifanya, hawatakuwa tu mbaraka kwa watu wengine, bali wao wenyewe hakika watabarikiwa. Uelewa wa wajibu uliofanywa vizuri utakuwa na ushawishi usiopingika juu ya nafsi zao wenyewe. Wenye kufa moyo watasahau hali yao ya kukata tamaa, wanyonge watakuwa na nguvu, wasio na maarifa watakuwa na maarifa, na wote watapata msaidizi asiyechoka katika Yeye aliyewaita. [MH 148.3; HU Aya ya 33]

Kanisa la Kristo limeundwa kwa ajili ya huduma. Kauli-mbiu yake kuu ni huduma. Washiriki wake ni askari wanaofundishwa kukabiliana na mapambano chini ya Nahodha wa wokovu wao. Wachungaji na Wahudumu Wakristo, matabibu, walimu, wana kazi pana zaidi kuliko ambavyo wengi wanatambua. Sio tu katika kuwahudumia watu, bali pia katika kuwafundisha watu ili waweze kuhudumu. Hawapaswi tu kutoa mafundisho katika kanuni sahihi, bali pia kuwaelimisha wasikilizaji wao kuwagawia wengine kanuni hizi. Ukweli ambao mtu hauishi katika mtindo wake wa maisha, ule ambao hauenezwi kwa watu wengine, hupoteza nguvu zake za kuleta uzima, na sifa zake za uponyaji. Baraka yake inaweza kudumishwa tu pale mtu anapoigawa kwa wengine. [MH 148.4; HU Aya ya 34]

Ukinaifu wa huduma zetu kwa Mungu (mambo yanayokinaisha ujumbe) unahitaji kuvunjwa. Kila mshiriki kanisani apaswa kuhusishwa katika huduma fulani kwa ajili ya Bwana. Wengine hawawezi kufanya mengi kama wengine, lakini kila mtu anapaswa kufanya yote awezayo ili kurudisha nyuma wimbi la magonjwa na dhiki ambalo linafagia kila mahali katika ulimwengu wetu. Wapo wengi ambao wangekuwa tayari kufanya kazi ikiwa tu wangefundishwa jinsi ya kuanza. Kile wanachohitaji ni kufundishwa na kuhimizwa (kuhamasishwa). MH 149.1; HU Aya ya 35

Kila kanisa linapaswa kuwa shule ya mafunzo kwa watenda kazi Wakristo. Washiriki wake wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuwasilisha masomo ya Biblia, jinsi ya kuongoza na kufundisha madarasa ya shule ya Sabato, namna bora ya kuwasaidia watu maskini, na kuwahudumia wagonjwa, na jinsi ya kushughulika na wale ambao bado hawajaongoka. Hatuna budi kuwa na shule za afya, shule za mapishi, na madarasa katika safu mbalimbali za kazi saidizi ya Kikristo. Hatupaswi kuwa na ufundishaji tu, bali pia kazi halisi inapaswa ifanyike chini ya waalimu wenye uzoefu. Walimu na waongoze njia katika kufanya kazi miongoni mwa watu, na wengine, kwa kuungana nao, watajifunza kutokana na kielelezo chao. Kielelezo kimoja kina thamani zaidi kuliko maelekezo mengi. [MH 149.2; HU Aya ya 36]

Wote na wakuze nguvu zao za kimwili na kiakili, hadi wafikie kiwango cha juu kabisa cha uwezo wao, ili waweze kumfanyia Mungu kazi pale ambapo kudra Yake itawahitaji. Neema ile ile iliyotoka kwa Kristo na kwenda kwa Paulo na Apolo, iliyowatofautisha wote katika ubora wa kiroho, itakabidhiwa hata leo kwa wamishenari Wakristo waliojitoa wakfu. Mungu hutamani watoto Wake wawe na akili na maarifa, ili kwa nguvu na uwazi vyenyewe haswa, utukufu Wake uweze kudhihirishwa katika ulimwengu wetu. [MH 149.3; HU Aya ya 37]

Watendakazi wenye elimu na ambao wamejiweka wakfu kwa Mungu wanaweza kufanya huduma kwa njia anuwai zaidi na wanaweza kutimiza kazi kubwa zaidi kuliko wale ambao hawajaelimishwa. Nidhamu itokanayo na mafunzo ya kiakili, inawaweka katika eneo lenye nafasi itakayowanufaisha zaidi. Lakini wale ambao hawana karama/talanta kubwa wala elimu pana wanaweza kuwahudumia wengine kwa njia inayokubalika. Mungu atawatumia watu walio tayari kutumiwa. Sio watu walio werevu zaidi au wenye vipaji vikubwa zaidi ndio ambao kazi yao huleta matokeo makubwa na yenye kudumu zaidi. Waume na wake wote ambao wameusikia ujumbe kutoka mbinguni wanahitajika. Watendakazi wenye ufanisi zaidi ni wale wanaoitikia mwaliko, “Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu.” Mathayo 11:29. [MH 150.1; HU Aya ya 38]

Wamishenari walio na moyo, ndiyo wanaohitajika. Yeye ambaye moyo wake umeguswa na Mungu, huwa na hamu kubwa kuwafikia wale ambao hawajapata kuujua upendo Wake Bwana. Hali ya watu wasiomjua Mungu inamchoma moyo na shida zao zinakuwa na majonzi binafsi kwake. Huku akijitwalia maisha yake

mikononi mwake (kujihatarisha), anaondoka na kuwa mjumbe aliyetumwa na kuvuviwa na mbingu, ili aitende kazi ambayo malaika wanaweza kushirikiana naye. [MH 150.2; HU Aya ya 39]

Ikiwa wale ambao Mungu amewakabidhi vipaji vikubwa vya akili watazitumia karama hizi kwa ubinafsi au uchoyo, basi hawa wataachwa baada ya kipindi cha kujaribiwa, wazifuate njia zao wenyewe. Mungu atawachukua watu ambao hawaonekani kuwa wamekirimiwa kwa talanta nyingi sana, watu wasio na kujiamini wenyewe sana, Naye atawafanya watu hawa dhaifu kuwa na nguvu, kwa sababu wao wamemtumaini Yeye kuwafanyia yale ambayo hawawezi kuyafanya wenyewe. Mungu atakubali utumishi/huduma inayofanywa kwa moyo wote, na Yeye Mwenyewe atafidia mapungufu. [MH 150.3; HU Aya ya 40]

Mara nyingi Bwana amewachagua watu ambao wamepata fursa ndogo ya elimu ya darasani kuwa watenda kazi pamoja Naye. Watu hawa wametumia uwezo wao kwa uaminifu zaidi, na Bwana amewatunukia thawabu kwa uadilifu wao katika kazi Yake, bidii yao katika kazi, na kiu yao kutafuta maarifa. Yeye ameshuhudia machozi yao na kusikia maombi yao. Kama vile ambavyo baraka Zake ziliwajia mateka katika ikulu ya Babeli, hali kadhalika huwapatia watenda kazi Wake hekima na maarifa leo. [MH 150.4; HU Aya ya 41]

Watu wenye upungufu wa elimu ya darasani/shuleni, wale walio wa hadhi ya chini katika nafasi za kijamii, kupitia neema ya Kristo, nyakati zingine wamefanikiwa kwa namna ya kustaajabisha katika kuzileta roho kwa Bwana. Siri ya mafanikio yao ilikuwa imani yao kwa Mungu. Watu hawa walijifunza kila siku kutoka Kwake, Yeye ambaye Ndiye Mshauri wa ajabu na Mweza yote. [MH 151.1; HU Aya ya 42]

Watendakazi wa namna hii wanapaswa kutiwa moyo. Bwana huwaunganisha na wale walio na uwezo bora zaidi ili kujaza mapengo ambayo wengine huyaacha. Wepesi wao wa kuona kile kinachopaswa kufanywa, utayari wao wa kuwasaidia wale wenye uhitaji, maneno na matendo yao ya fadhila na ukarimu, hufungua milango ya manufaa ambayo vinginevyo ingeendelea kufungwa. Watu hawa huwakaribia wale walio shidani, na ushawishi wa maneno yao una nguvu ya kuzivuta nafsi nyingi zinazotetemeka kuja kwa Mungu. Kazi yao huonyesha kile ambacho maelfu wengine wangeweza kuzifanya, kama wangependa tu kufanya hivyo. [MH 151.2; HU Aya ya 43]

Maisha Yenye Mvuto Katika Wigo Mpana

Hakuna kitu kitakachoamsha ari ya kujitoa nafsi na kupanua na kuimarisha tabia kama vile kujihusisha katika kazi kwa ajili ya watu wengine. Wengi wanaojiita Wakristo, katika kutafuta uhusiano wa kanisa, hujifikiria wao wenyewe tu. Wanatamani kufurahia ushirika wa kanisa na malezi toka kwa mchungaji. Hupenda kuwa washiriki wa makanisa makubwa yenye ustawi, nao

wanaridhika kufanya kidogo kwa ajili ya wengine. Kwa njia hii wanajinyang'anya wenyewe baraka zenye thamani zaidi. Wengi wangenufaika kwa kiasi kikubwa kwa kusalimisha mahusiano yao mazuri na yenye kuleta urahisi wa mambo na faraja. Wanahitaji kwenda mahali ambapo nguvu zao zitaitwa ili zijishughulishe katika kazi ya Kikristo na kisha wajifunze kubeba majukumu. [MH 151.3; HU Aya ya 44]

Miti iliyosongamana karibu-karibu, haikui katika afya bora na uimara. Mtunza bustani huipandikiza tena ile miche ili iweze kupata nafasi ya kukua. Kazi kama hiyo ingewanufaisha washiriki wengi miongoni mwa makanisa makubwa. Wanahitaji kuwekwa mahali ambapo nguvu zao zitajipatia kazi ya kufanya katika jitihada ya utendaji ya Kikristo. Watu hawa wanapoteza uhai wao wa kiroho, nao wanadumazwa na kuwa wasiofaa kwa kukosa kazi ya kujitoa nafsi kwa ajili ya wengine. Wakipandikizwa kwa kutawanywa kwenye eneo fulani la umishenari, watachangamka/watachakarika na kuwa na nguvu na uwezo. [MH 152.1; HU Aya ya 45]

Lakini hakuna ye yote anayehitaji kungojea hadi aitwe kwenye eneo fulani la mbali kabla ya kuanza kuwasaidia wengine. Milango ya huduma ipo wazi kila mahali. Wote wanaotuzunguka ni wale wanaohitaji msaada wetu. Wajane, yatima, wagonjwa, walio kifoni (mahututi), wanaougua moyo, wanaosononeka moyoni, waliokata tamaa, wasio na maarifa, na wailokataliwa, na wanaobaguliwa wapo kila mahali. [MH 152.2; HU Aya ya 46]

Twapaswa kuelewa kuwa ni wajibu wetu maalum kuwahudumia wale waishio katika ujirani wetu. Jifunze jinsi unavyoweza kuwasaidia vyema wale wasiovutiwa na mambo ya kiroho. Unapotembelea marafiki na majirani zako, onyesha shauku kuhusu hali zao za kiroho na za kimwili pia. Zungumza nao juu ya Kristo kama Mwokozi anayesamehe dhambi. Waalike majirani zako nyumbani mwako, na kisha usome pamoja nao kutoka kwenye Biblia ya thamani na kutoka katika vitabu vinavyoelezea kweli Zake. Waalike kuungana nawe katika nyimbo na sala. Katika mikusanyiko hii midogo, Kristo Mwenyewe atakuwepo, kama alivyoahidi, na mioyo itaguswa na neema Yake. [MH 152.3; HU Aya ya 47]

Washiriki wa kanisa wanapaswa kujielimisha kufanya kazi hii. Jambo hili lina umuhimu sawa na ule wa kuziokoa roho katika nchi za ughaibuni. Ingawa wengine huhisi mzigo kwa ajili ya roho zilizo mbali, wengi walio nyumbani wahisi mzigo wa roho za thamani zilizowazunguka karibu nao, na kisha wafanye kazi kwa bidii, kwaajili ya wokovu wao. [MH 152.4; HU Aya ya 48]

Wengi hujutia kwamba wanaishi maisha finyu. Wao wenyewe wanaweza kufanya maisha yao kuwa na wigo mpana na yenye mvuto ikiwa watapenda kufanya hivyo. Wale wanaompenda Yesu kwa moyo na akili na roho, na jirani zao kama wao wenyewe, wana uwanja mpana wa kutumia uwezo na ushawishi wao. [MH 153.1; HU Aya ya 49]

Fursa Ndogondogo

Hebu mtu asiziachilie fursa ndogo-ndogo zimpite, eti kwa sababu anatafuta fursa kubwa zaidi. Unaweza kufanya kazi ndogo kwa ufanisi mkubwa, lakini ukashindwa kabisa hata kule kuifanya kazi iliyo kubwa, na kuanguka kwenye mvunjiko wa moyo. Ni kwa kufanya kwa uwezo wako wote kile ambacho mkono wako unapata kukifanya, ndipo unakuza umahiri wa kufanya kazi kubwa zaidi. Ni kwa kudharau fursa za kila siku, kwa kupuuzia mambo madogo yaliyopo karibu nawe, ndivyo watu wengi wanakosa kuzaa matunda na kunyauka. [MH 153.2; HU Aya ya 50]

Usitegemee msaada wa mwanadamu. Angalia ng'ambo ya wanadamu mpaka kwa Yule aliyeteuliwa na Mungu ili kubeba majonzi na huzuni zetu, na kututimizia mahitaji yetu. Huku ukimwamini Mungu kama alivyosema katika Neno Lake, kuwa na mwanzo mpya po pote pale unapopata kazi ya kufanya, na kisha songa mbele kwa imani isiyoyumba-yumba. Ni imani katika uwepo wa Kristo ndiyo inayotia nguvu na uthabiti. Tenda kazi bila maslahi ya kukunufaisha wewe tu, nawe ufanye kwa juhudi madhubuti, na kwa nguvu yenye ustahimilivu. [MH 153.3; HU Aya ya 51]

Katika maeneo ambayo hali ni zenye kuchukiza na zenye ukinzani, na kukatisha tamaa sana kiasi kwamba wengi wanayaepuka, yaani hawako radhi kwenda huko, mabadiliko makubwa yametokea kutokana na jitihada za watendakazi wenye kujidhabihu nafsi zao. Kwa subira na ustahimilivu wametenda kazi, bila kutegemea nguvu za kibinadamu, bali Mungu, na neema Yake iliwategemeza. Kiasi cha mafanikio mema yaliyotimizwa kwa namna hiyo kamwe hakitajulikana katika ulimwengu huu, lakini matokeo yenye baraka yataonekana baada ya maisha haya kule mbinguni. [MH 153.4; HU Aya ya 52]

Wamishonari Wanaojitegemeza Wenyewe

Katika sehemu nyingi wamishonari wanaojikimu wenyewe wanaweza kufanya kazi kwa mafanikio (walei wa kujitegemea). Jambo hili twaliona kwa mmishenari Paulo aliyejikimu maisha na kujitegemea, huku akijitahidi kueneza maarifa ya Kristo ulimwenguni pote. Alipokuwa akifundisha injili kila siku katika miji mikubwa ya Asia na Ulaya, alifanya kazi ya fundi-stadi ili kujitegemeza katika maisha yake na wenzake. Maneno yake alipokuwa akiwaaga wazee wa Efeso yanayoonyesha namna alivyotenda kazi, yana mafunzo adhimu kwa kila mtendakazi wa injili: [MH 154.1; HU Aya ya 53]

"Mnajua jinsi nilivyokaa kwenu sikuzote; na ya kuwa sikuwanyima kitu cho chote cha kuwafaa ninyi, bali nimewaonyesha, na kuwafundisha hadharani na nyumbani. Sikutamani fedha wala dhahabu wala mavazi ya mtu. Naam, ninyi

wenyewe mnajua kwamba mikono hii imetumikia mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami. Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi kwa namna hii, ninyi mnapaswa kuwasaidia wale walio dhaifu, na kuyakumbuka Maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema, Ni heri kutoa kuliko kupokea. Matendo 20:18-35. [MH 154.2; HU Aya ya 54]

Wengi leo, kama wangejazwa na roho hiyo ya kujitoa, wanaweza kufanya kazi nzuri kwa njia iyo hiyo. Hebu watu wawili au zaidi waanze pamoja kazi ya uinjilisti pamoja. Wawatembelee watu, na kisha waombe, waimbe, wafundishe, wafafanue Maandiko, na kuwahudumia wagonjwa. Wengine wanaweza kujikimu maisha kwa kuwa wainjilisti wa vitabu; wengine, kama mtume, wanaweza kufanya kazi ya mikono au juhudi katika nyanja zinginezo. Wasongapo mbele katika kazi yao, wakitambua kutokuwa na uwezo ndani yao wenyewe, bali kwa unyenyekevu wakimtegemea Mungu, wanapata uzoefu wenye baraka. Bwana Yesu huwatangulia, na miongoni mwa matajiri na maskini watumishi hawa hupata fadhila na msaada. [MH 154.3; HU Aya ya 55]

Wale ambao wamefunzwa kwa ajili ya kazi ya umishenari wa tiba katika nchi za ughaibuni wanapaswa kuhimizwa kwenda bila kuchelewa kule ambako wanatarajia kutenda kazi, na kuanza kazi miongoni mwa watu, wakijifunza lugha za kule wanapofanya kazi, na huku wakiendelea na kazi. Na haitachukua muda kwao kuweza kuzifundisha zile kweli rahisi za Neno la Mungu. [MH 155.1; HU Aya ya 56]

Ulimwenguni kote, wajumbe wa rehema wanahitajika. Kuna mwito kwa familia za Kikristo kwenda katika jamii mbalimbali zilizo gizani na kwenye mafundisho yenye makosa, kwenda katika maeneo ya ughaibuni, ili kufahamu mahitaji ya wanadamu wenzao, na kufanya kazi kwa ajili ya utume wa Bwana. Endapo familia kama hizo zingetulia katika maeneo yenye giza duniani, mahali ambapo watu wamefunikwa na utusitusi wa kiroho, na kuruhusu nuru ya maisha ya Kristo ing'ae kupitia kwao, ni kazi nzuri kama nini ingeweza kutekelezwa huko. [MH 155.2; HU Aya ya 57]

Kazi hii inahitaji kujitoa. Wakati wengi wakingoja kila kizuizi kiondolewe, kazi ambayo wangeweza kuifanya inaachwa bila kutimizwa, na umati mkubwa wa watu unakufa bila tumaini na bila Mungu. Wengine kwa ajili ya manufaa ya kibiashara, au kupata ujuzi wa kisayansi, hujitosa katika maeneo yenye kufadhaisha na kuvumilia kwa uchangamfu magumu na shida; lakini ni wachache kiasi gani kwa ajili ya wanadamu wenzao wako tayari kuhamisha familia zao katika maeneo ambayo yanahitaji kufikiwa na injili. [MH 156.1; HU Aya ya 58]

Kuwafikia watu po pote pale walipo, bila ya kujali nafasi au hali yao, na kuwasaidia kwa kila njia kwa kadiri inavyowezekana—hii ndiyo huduma ya kweli. Kwa juhudi kama hizo unaweza kuileta mioyo yao kwa Bwana na kufungua mlango wa kuzifikia hizo roho zinazoangamia. [MH 156.2; HU Aya ya 59]

Katika kazi yako yote hebu kumbuka kwamba wewe umefungamanishwa na Kristo, katika sehemu ya ule mpango mkuu wa ukombozi. Upendo wa Kristo, katika mkondo uhuishao na kuponya, unapaswa kutiririka katika maisha yako. Unapotafuta kuwavuta wengine ndani ya duara la upendo wa Bwana, hebu usafi wa lugha yako, kutokuwa na ubinafsi kwa huduma yako, furaha ya mwonekano wako, vishuhudie nguvu ya neema Yake. Upatie ulimwengu uwakilishi wa Mwokozi ulio safi na wa haki, ambao watu watamtazama Yeye katika uzuri Wake. [MH 156.3; HU Aya ya 60]

Ni jambo lenye manufaa kidogo kwa sisi kujaribu kuwafanyia matengenezo watu wengine kwa kushambulia yale ambayo twaweza kuyaona kama mazoea yao mabaya. Jitihada hizo mara nyingi husababisha madhara zaidi kuliko mema. Katika mazungumzo Yake na mwanamke Msamaria, Yeye badala ya kukidharau kile kisima cha Yakobo, Kristo aliwasilisha jambo bora zaidi. “Kama ungalijua karama ya Mungu,” alisema, “na ni nani akuambiaye, Nipe maji ninywe; ungemwomba, Naye angalikupa maji yaliyo hai.” Yohana 4:10. Aliyageuza mazungumzo kwenye ile hazina Aliyopaswa kuitoa, akimpa mwanamke yule kitu bora zaidi kuliko vile yule mama alivyokuwa navyo, yaani maji ya uzima, furaha na tumaini la injili. [MH 156.4; HU Aya ya 61]

Hiki ni kielelezo cha namna sisi tunavyopaswa kutenda kazi. Ni lazima tuwapatie wanadamu kitu kilicho bora zaidi kuliko kile walicho nacho, ambacho ni amani ya Kristo, ipitayo akili na ufahamu wote. Ni lazima tuwaambie watu kuhusu sheria takatifu ya Mungu, nakala ya tabia Yake, na udhihirisho wa kile Yeye anachotaka wawe. Waonyeshe jinsi utukufu wa mbinguni usioharibika ulivyo bora zaidi kuliko raha na anasa za kitambo kidogo za ulimwengu. Waambie juu ya uhuru na pumziko lipatikanalo kwa Mwokozi. “Ye yote atakayekunywa maji nitakayompa Mimi hataona kiu milele,” alisema. Kifungu cha 14. [MH 157.1; HU Aya ya 62]

Mwinue Yesu, ukipaza sauti “Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!” Yohana 1:29, ARV Yeye pekee Ndiye awezaye kutosheleza matamanio ya moyo na kuipa nafsi amani. [MH 157.2; HU Aya ya 63]

Kati ya wanadamu wote walio ulimwenguni, wanamatengenezo ndio wanapaswa kuwa watu wasio na ubinafsi kupita wote, watu wasio na uchoyo, wema zaidi, na wenye nidhamu na adabu zaidi. Katika maisha yao wema halisi wenye matendo yasiyo na ubinafsi unapaswa kuonekana kwa watu. Mtendakazi anayedhihirisha ukosefu wa adabu, yule ambaye anaonyesha kutokuwa na subira na wakaidi, ambaye huzungumza haraka-haraka au kutenda bila kufikiria, anaweza kufunga mlango wa mioyo ya watu naye hataweza kuwafikia kamwe. [MH 157.3; HU Aya ya 64]

Kama vile umande na mvua tulivu vinavyoanguka juu ya mimea inayonyauka, ndivyo maneno yetu yanavyopaswa kuanguka kwa upole pale tunapotafuta kuwavuta watu kutoka katika makosa yao. Mpango wa Mungu wa kwanza ni

kuufikia moyo. Twapaswa kusema ukweli kwa upendo, tukimtumaini Yeye kutoa uwezo wa kufanya matengenezo katika maisha. Roho Mtakatifu atalidondosha moyoni mwa mtu Neno linalozungumzwa kwa upendo. [MH 157.4; HU Aya ya 65]

Kwa kawaida sisi ni wabinafsi, twapenda kujifirikia wenyewe kung'ang'ania maoni yetu. Lakini tunapojifunza masomo ambayo Kristo anatamani kutufundisha, tunakuwa washiriki wa tabia Yake; na hivyo tangu wakati huo, tunakuwa tunaishi maisha Yake. Mfano wa ajabu wa Kristo, upole na huruma Yake isiyo na kifani, ambayo Yeye aliingia nayo katika hisia za wengine, akilia pamoja na wale waliolia, akifurahi pamoja na wale wanaofurahi, lazima iwe na mvuto wa kina katika tabia ya watu wote wanaomfuata Yeye kwa uaminifu. Kwa maneno na matendo ya fadhili watajaribu kurahisisha njia ya miguu iliyochoka. [MH 157.5; HU Aya ya 66]

"Bwana wa Milele amenipa lugha ya kufundisha." "Ili nipate kujua jinsi ya kusema neno kwa wakati, kwake yeye aliyechoka." Isaya 50:4, AV [MH 158.1; HU Aya ya 67]

Roho zinazoteseka zinatuzunguka kila upande. Twaweza kuwaona watu, hapa na pale, na kila mahali,. Hebu na tuwatafute watu hawa wanaoteseka na kusema neno kwa wakati, ili kufariji mioyo yao. Hebu na tuwe mikondo ambayo inatiririka maji yenye huruma na kuburudisha wakati wote. [MH 158.2; HU Aya ya 68]

Katika mahusiano yetu yote ikumbukwe kwamba katika uzoefu wa wengine kuna 'sura za kitabu' zilizofungwa kwenye macho ya mwanadamu. Kwenye kurasa za kumbukumbu kuna historia za kusikitisha ambazo zinalindwa kwa utakatifu kutoka kwenye macho ya udadisi. Ndani ya hizo sura yanasimama mapigano marefu, magumu na yenye kujaribu mtu, pengine shida katika maisha ya nyumbani, ambayo siku baada ya siku hudhoofisha ujasiri, kujiamini, na imani. Wale wanaopigana vita ya maisha katika hali ngumu wanaweza kuimarishwa na kutiwa moyo kwa kupewa umakini mdogo, unaogharimu tu jitihada ya upendo. Kwa watu kama hao, mkono wa shime wa rafiki wa kweli una thamani kubwa zaidi kuliko dhahabu au fedha. Maneno ya ukarimu hupokewa kama tabasamu la malaika. [MH 158.3; HU Aya ya 69

Kuna wengi wanaopambana na umaskini, wakilazimika kufanya kazi kwa bidii na kupewa ujira mdogo, na kukidhi ila sehemu ndogo sana ya mahitaji ya maisha. Kazi za suluba na umaskini wa hali ya juu, pasipo tumaini la mambo yaliyo bora, hufanya mzigo wao kuwa mzito sana. Wakati maumivu na ugonjwa vinaongezeka, wanaouona mzigo wao ni kana kwamba hauwezekani kubebeka. Wakiwa wamechoka kwa huzuni, wasiwasi na dhuluma za watu, hawajui waelekee wapi kupata unafuu. Wahurumie katika majaribu na maumivu yao ya moyo, na kuvunjwa moyo. Hii itakufungulia njia ya kuwasaidia. Zungumza nao juu ya ahadi za Mungu, omba pamoja nao na kwa ajili yao, watie moyo kwa matumaini. [MH 158.4; HU Aya ya 70

Maneno ya kuchangamsha na kutia moyo yanayosemwa pale roho zao zinapougua na mapigo ya moyo ya ujasiri yanapungua—maneno haya yanachukuliwa na Mwokozi kana kwamba yamesemwa Kwake Mwenyewe. Mioyo inapochangamshwa, malaika wa mbinguni hutazama wakipendezwa na ukarimu huo. [MH 159.1; HU Aya ya 71

Tangu enzi hata enzi Bwana amekuwa akitafuta kuamsha katika roho za wanadamu utambuzi wa udugu wao wa Kimungu. Iweni watenda kazi pamoja Naye. Ingawa kutoaminiana na kutengwa kunaenea ulimwenguni pote, wanafunzi wa Kristo wanapaswa kuifunua roho itawalayo mbinguni. [MH 159.2; HU Aya ya 72]

Zungumza kama ambavyo Kristo angezungumza, tenda kama ambavyo Yeye angetenda. Daima onyesha utamu/uzuri wa tabia Yake. Funua utajiri wa upendo ambao ndio msingi wa mafundisho Yake yote na kushughulika Kwake kote na wanadamu. Watendakazi wanyenyekevu zaidi, kwa kushirikiana na Kristo, wanaweza kugusa nyuzi ambazo mitetemo ya mwangwi wake itasikika hadi miisho ya dunia na kutoa muziki katika zama za zisizo na ukomo. [MH 159.3; HU Aya ya 73]

Mbingu inangoja kushirikiana na vyombo vya kibinadamu, ili ziweze kuufunulia ulimwengu kile ambacho wanadamu wanaweza kuwa, na kile ambacho, kupitia muungano na Mungu kinaweza kutimizwa kwa ajili ya kuokoa roho zilizo karibu kuangamia. Hakuna kikomo kwa manufaa ya mtu yule ambaye, ameuweka kando ubinafsi, wanatengeneza nafasi kwa ajili ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu moyoni mwake na akiishi maisha yaliyowekwa wakfu kikamilifu kwa Mungu. Wote wanaoweka wakfu mwili, nafsi na roho kwa ajili ya kumtumikia, daima watakuwa wakipokea karama mpya ya nguvu za kimwili, kiakili, na kiroho. Ukarimu usiokoma wa mbinguni uko mikononi mwao. Kristo huwapa pumzi ya Roho Wake Mwenyewe, uzima wa maisha Yake Mwenyewe. Roho Mtakatifu huweka nguvu Zake za juu zaidi kufanya kazi katika akili na moyo. Kupitia neema tuliyopewa twaweza kupata ushindi ambao, kwa sababu ya mawazo yetu yenye hitilafu na mitazamo yetu ya zamani, kasoro zetu za tabia, udogo wetu wa imani, ushindi huo umeonekana kuwa ni jambo lisilowezekana. [MH 159.4; HU Aya ya 74]

Kwa kila mtu anayejitoa kwa Bwana kumtumikia, bila kujibakiza cho chote, amepewa uwezo kwa ajili ya kupata matokeo yasiyo na kipimo. Kwa ajili ya hawa Mungu atafanya mambo makuu. Atafanya kazi katika akili za wanadamu ili, hata katika ulimwengu huu, kutaonekana katika maisha yao utimilifu wa ahadi ya maisha ya baadaye yatakavyokuwa. [MH 160.1; HU Aya ya 75]

“Nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi; jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi. Litachanua maua mengi, na kufurahi, naam, kwa shangwe na kuimba; litapewa uzuri wa Lebanoni, utukufu wa Karmeli na Sharoni; watauona utukufu wa Bwana, ukuu wa Mungu wetu.” [MH 160.2; HU Aya ya 76

“Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu, yafanyeni imara magoti yaliyolegea.

Waambieni walio na moyo wa hofu, Jipeni moyo, msiogope; tazama, Mungu wenu.” [MH 160.3

“atakuja na kuwaokoa ninyi.

Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa.

Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba; maana katika nyika maji yatabubujika; na vijito jangwani.” [MH 160.4; HU Aya ya 77]

“Na mchanga ung'aao mfano wa maji utakuwa ziwa la maji, na nchi yenye kiu itakuwa chemchemi za maji; katika makao ya mbweha, walipokuwa wamelala, patakuwa na majani, pamoja na mianzi na manyasi.

Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa, Njia ya utakatifu; wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao; wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo.” [MH 160.5; HU Aya ya 78]

“Hapo hapatakuwa na simba, wala mnyama mkali hatapanda juu yake; hawataonekana hapo; bali waliokombolewa watakwenda katika njia hiyo.

10 Na hao waliokombolewa na Bwana watarudi, watafika Sayuni wakiimba; na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; nao watapata kicheko na furaha, huzuni na kuugua zitakimbia.” Isaya 35:1-10. [MH 160. ; HU Aya ya 79]

SURA YA 10

KUSAIDIA WALIOJARIBIWA

Sio kwa sababu sisi tulimpenda Yeye kwanza; ndiyo sababu Kristo anatupenda sisi, bali “Kristo alitupenda sisi tulipokuwa tungali wadhambi” Yeye alikufa kwa ajili yetu. Yeye hatutendei kulingana na kukengeuka kwetu.

Ingawa dhambi zetu zimestahili hukumu, Yeye hatuhukumu. Mwaka baada ya mwaka ameubeba udhaifu na ujinga wetu, pamoja na ukosefu wetu wa shukrani na upotovu wetu. Ijapokuwa kutangatanga kwetu, ugumu wetu wa mioyo,na kupuuzia kwetu Neno Lake Takatifu, mkono Wake bado umenyooshwa kutuelekea sisi. [MH 161.1; HU Aya ya 1]

Neema ni sifa ya Mungu wanayotunukiwa wanadamu wasiostahili. Hatukuitafuta, bali yenyewe ndiyo ilitumwa kuja kututafuta. Mungu anafurahia kutoa neema Yake juu yetu, si kwa sababu sisi twastahili, la! Bali kwa sababu hatustahili kabisa. Dai letu pekee la rehema Yake, ni hitaji letu kuu *(Msisitizo: Uhitaji wetu wa msaada peke yake ndiyo unatufanya tupewe rehema Yake na si kwamba twastahili)*. [MH 161.2; HU Aya ya 2]

Bwana Mungu kupitia Yesu Kristo ananyosha mkono Wake mchana kutwa ili kuwaalika wenye dhambi na walioanguka. Yeye anawapokea wote. Yeye anawakaribisha wote. Ni utukufu Wake kuwasamehe wenye dhambi. Atamchukua mateka kutoka kwa wale walio hodari, atamkomboa mateka, Naye atakitoa kijinga kutoka kwenye moto. Yeye aushusha mnyororo wa thamani wa rehema Zake hadi kwenye kina cha chini kabisa cha unyonge/udhaifu wa mwanadamu, na kuiinua nafsi iliyoshushwa chini kabisa katika uchafu wa dhambi. [MH 161.3; HU Aya ya 3]

Kila mwanadamu ni chombo kinachompendeza Yeye ambaye alitoa maisha Yake ili Aweze kuwapatanisha na kuwarejesha wanadamu kwa Mungu. Nafsi zenye hatia na zisizokuwa na msaada, ambazo zipo hatarini kushawishwa na mbinu na mitego ya Shetani, hutunzwa kwa kujaliwa sana, kama vile mchungaji anavyowachunga na kuwatunza kondoo wa kundi lake. [MH 162.1; HU Aya ya 4]

Mfano wa Mwokozi ndio unapaswa kuwa kiwango chetu cha huduma kwa wale wanaojaribiwa na kufanya makosa na dhambi. Nia ile ile, upole na uvumilivu ambao ameonyesha kwetu, vivyo hivyo sisi pia twapaswa kuonyesha kwa wengine. “Kama vile nilivyowapenda ninyi,” Anasema, “nanyi pia mpendane ninyi kwa ninyi.” Yohana 13:34. Ikiwa Kristo anakaa ndani yetu, tutaonyesha upendo Wake usio na ubinafsi hata chembe, kwa watu wote tunaopaswa kufanya hivyo kwao. Tunapowaona wanaume na wanawake wanaohitaji huruma na msaada wetu, hatutauliza, “Je, hawa wanastahili kweli?” bali “Je, Ninaweza kuwanufaisha watu hawa kwa namna gani?” [MH 162.2; HU Aya ya 5]

Tajiri na maskini, wa juu na wa chini, walio huru na watumwa, **ni urithi wa Mungu**. Yeye aliyetoa maisha Yake ili kumkomboa mwanadamu aona ndani ya

kila mwanadamu thamani isiyoweza kukadiriwa kabisa. Kwa fumbo na utukufu wa msalaba, sisi hatuna budi kuelewa kipimo Chake kuhusiana na thamani ya roho ya mwanadamu. Tunapofanya hivi, tutahisi kwamba haijalishi wanadamu wamedhalilishwa kwa kiasi gani, wao wamegharimu sana mbingu kutendewa ukatili au dharau. Tutatambua umuhimu wa kufanya kazi kwa ajili ya wanadamu wenzetu, ili wapate kuinuliwa kwenye kiti cha enzi cha Mungu. [MH 162.3; HU Aya ya 6]

Sarafu iliyopotea kwenye mfano wa Mwokozi katika Luka 15:8-10, ingawa ilikuwa katika udongo na takataka, bado ilikuwa na thamani ya kipande cha fedha. Mmiliki wake aliitafuta kwa sababu ilikuwa ya thamani. Ndivyo ilivyo kwa kila mwanadamu, yeye ajapokuwa amedhalilishwa kwa dhambi, bado anahesabiwa kuwa wa thamani machoni pa Mungu. Kama vile sarafu ya fedha ilivyokuwa na sura na maandishi juu yake ya ile mamlaka inayotawala, ndivyo ilivyokuwa katika kuumbwa kwake mwanadamu, alikuwa na sura na maandishi ya muhuri wa Mungu. Ingawa sasa maandishi hayo yameharibiwa na kufifia kwa sababu ya kushawishika kutenda dhambi, alama za maandishi haya zinabaki juu ya kila nafsi *(Msisitizo: Sura ya Mungu imebaki ndani ya kila nafsi)*. Mungu anatamani kuirejesha nafsi hiyo na kuirudisha sura Yake Mwenyewe katika haki na utakatifu. [MH 163.1; HU Aya ya 7]

Je, ni kwa udogo kiasi gani sisi tunakuwa katika huruma pamoja na Kristo kwa kile kinachopaswa kuwa ushirika imara zaidi—yaani kuzihurumia nafsi zilizopotoka, zenye hatia, zinazoteseka, na zinazokufa dhambini na katika makosa! Ukatili wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake ndio dhambi yetu kuu. Wengi hufikiri kwamba wanawakilisha haki ya Mungu na huku wakishindwa kabisa kuuonyesha upole Wake na upendo Wake mkuu. Mara nyingi wale wanaokumbana na ukali na ushupavu huwa katika taabu ya majaribu. Shetani anakuwa akishindana na roho hizi na maneno makali yasiyo na huruma, huwavunja moyo na huwafanya mawindo ya nguvu zake ibilisi. [MH 163.2; HU Aya ya 8]

Ni suala nyeti na la kuvutia kushughulika na akili za mwanadamu. Yeye peke Yake asomaye mioyo ajua jinsi ya kuleta mtu kwenye toba. Hekima Yake pekee ndiyo inayoweza kutufanikisha katika kuwafikia watu waliopotea. Unaweza kusimama kwa ukakamavu, na kuhisi kuwa “Mimi ni mtakatifu kuliko wewe,” na hakika haijalishi uko sahihi kwa kiasi gani katika mawazo au maneno yako; wewe hautaweza kuigusa mioyo ya watu kamwe kwa maneno hayo. Pendo la Kristo, linalodhihirika kwa maneno na matendo ndilo ambalo litaifikia njia yake kuielekea roho, wakati ambapo kurudia-rudia kanuni za

Mungu au mabishano kunaweza kusifanikishe kitu chochote. [MH 163.3; HU Aya ya 9]

Twahitajika tuwe watu wa huruma zaidi kama Kristo alivyo; huruma zetu hazipaswi tu kudhihirishwa kwa wale wanaoonekana kwetu kuwa hawana dosari, bali hata watu maskini, wanaoteseka, na kutaabika, ambao mara nyingi hujikwaa katika makosa, na kutenda dhambi na kutubu, wanaojaribiwa na kukatishwa tamaa. Hatuna budi kwenda kwa wanadamu wenzetu, tukiwa tumeguswa na hisia za udhaifu wao kama anavyoguswa Kuhani wetu Mkuu Mwenye rehema. [MH 164.1; HU Aya ya 10]

Ilikuwa ni watu waliotengwa na jamii, mtoza ushuru na mwenye dhambi, aliyetwezwa na mataifa, ambao Kristo aliwaita na kwa wema Wake aliwavuta Kwake. Tabaka moja ambalo Yeye hakuweza kuwaonyesha upendeleo Wake kamwe lilikuwa ni la watu waliojitenga katika kujiamini kwao na hata kuwadharau wengine. [MH 164.2; HU Aya ya 11]

“Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani,” Kristo anatuagiza, “ili nyumba Yangu ipate kujaa.” Kwa kutii Neno hili inatupasa kwenda kwa wapagani walio karibu nasi, na kwa wale walio mbali. “Watoza ushuru na makahaba” lazima wasikie mwaliko wa Mwokozi. Kwa huruma na uvumilivu wa wajumbe Wake, mwaliko huwa na nguvu inayoshurutisha kuwainua wale waliozama katika vilindi vya chini kabisa vya dhambi. [MH 164.3; HU Aya ya 12]

Misukumo ya Kikristo yadai kwamba tufanye kazi kwa kusudi thabiti, shauku isiyokoma, na maombi yasiyokoma yanayoongezeka daima, kwa ajili ya roho ambazo Shetani anazitafuta ili kuziangamiza. Hakuna kitu kinachopaswa kupooza moto wa nguvu yenye bidii, ya kuonea shauku wokovu wa watu waliopotea. [MH 164.4; HU Aya ya 13]

Angalia jinsi roho ya kusisitiza inavyodhihirishwa kote katika Neno la Mungu, roho ya kuwasihi wanaume na wanawake waje kwa Kristo. Ni lazima tuchukue kila fursa, faraghani na hadharani, kuwasilisha kila hoja, tukihimiza kila msukumo usiopimika wa kuwavuta watu kwa Mwokozi. Kwa uwezo wetu wote, ni lazima tuwasihi watu kumtazama Yesu na kukubali maisha Yake ya kujinyima na kujitoa nafsi. Ni lazima tuonyeshe kwamba tunatazamia watu hawa, waupe furaha moyo wa Kristo kwa kutumia kila moja ya karama Zake katika kuliheshimu Jina Lake. [MH 164.5; HU Aya ya 14]

Tumeokolewa Kwa Tumaini

"Tuliokolewa kwa taraja." Warumi 8:24. Walioanguka lazima waongozwe kuhisi kuwa bado hawajachelewa kuwa watu mashujaa. Kristo alimheshimu mwanadamu kwa kumpa ujasiri Wake na hivyo kumweka juu, na kumfanya mtu huyu aiishi ile heshima aliyompa. *(Msisitizo: aliwaonyesha ana matumaini nao na anajua kuwa watafanya vyema)*. Hata wale ambao walikuwa wameanguka chini kabisa aliwatendea kwa heshima. Yalikuwa maumivu ya kudumu ya Kristo kuletwa karibu na uadui, upotovu, na unajisi; lakini kamwe hakutamka hata usemi mmoja wa kuonyesha kwamba hisia Zake zilishtushwa au ladha Yake iliyosafishwa iliudhika. Haikujalisha jinsi ambavyo tabia ya mtu ilikuwa mbaya kiasi gani, chuki yao ilivyokuwa kali, au tamaa za mwili zilivyopitiliza, yeye alikabiliana na haya yote kwa wema. Tunaposhiriki Roho Wake, tutawachukulia watu wote kama ndugu, wanaojaribiwa sawasawa na sisi, ambao mara nyingi huanguka na kuhangaika kuinuka tena, wanaopambana na kuvunjwa moyo na matatizo, wakitamani huruma na msaada. Ndipo tutakutana nao kwa namna si ya kuwakatisha tamaa au kuwafukuza, bali kuamsha tumaini katika mioyo yao. Wanapotiwa moyo hivi, wanaweza kusema kwa ujasiri, “Usifurahi juu yangu, Ee adui yangu; niangukapo, nitasimama tena; nikaapo gizani, Bwana atakuwa nuru kwangu. Nitaivumilia ghadhabu ya Bwana, kwa kuwa nimemwasi; hata atakaponitetea teto langu, na kunifanyia hukumu; atanileta nje kwenye nuru, nami nitaiona haki yake.” Mika 7:8, 9. [MH 165.1; HU Aya ya 15]

Mungu “Toka mahali pake aketipo Huwaangalia wote wakaao duniani; yeye aiumbaye mioyo yao wote Huzifikiri kazi zao zote.” Zaburi 33:14, 15. [MH 166.1; HU Aya ya 16]

Anatuagiza, katika kushughulika na waliojaribiwa na wanaokosea, jifikirie nafsi yako “usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.” Wagalatia 6:1. Kwa utambuzi wa udhaifu wetu wenyewe, sisi tutakuwa na huruma kwa ajili ya udhaifu wa wengine. [MH 166.2; HU Aya ya 17]

“Ni nani anayekupambanua na mwingine? Nawe una nini usichokipokea? “Mwalimu wenu ni mmoja; ... nanyi nyote ni ndugu.” “Lakini wewe je! Mbona wamhukumu ndugu yako? Au wewe je! Mbona wamdharau ndugu yako? “Basi tusizidi kuhukumiana, bali afadhali toeni hukumu hii, mtu asitie kitu cha kumkwaza ndugu au cha kumwangusha.” 1 Wakorintho 4:7; Mathayo 23:8; Warumi 14:10, 13. [MH 166.3; HU Aya ya 18]

Siku zote mtu hufedheheshwa makosa yake yanapobainishwa. Hakuna mwanadamu anayepaswa kufanya uzoefu wa mtu fulani kuwa mchungu zaidi kwa kumkosoa bila sababu. Hakuna aliyewahi kurudishwa na kuwa kwenye mstari sahihi kwa masuto; lakini wengi wamefukuziwa mbali, na mioyo yao imeongozwa kuwa migumu kama chuma, na matokeo yake ni kuwa dhamiri

zao haziwezi kusadikishwa na injili. Roho ya upole, uungwana, staha ivutiayo, inaweza kuokoa wakosefu na kusitiri wingi wa dhambi. [MH 166.4; HU Aya ya 19]

Mtume Paulo aliona kuna ulazima wa kukemea kosa, lakini alijitahidi kwa mwangalifu kama nini, kuonyesha kwamba yeye alikuwa ni rafiki wa waliokosea! Jinsi gani alivyowaeleza kwa shauku sababu ya tendo lake hili la kumkaripia mtu! Aliwafanya waelewe kwamba ilimgharimu yeye maumivu, kuwapa wao maumivu. Alionyesha imani yake na huruma kwa wale ambao walikuwa wakijitahidi kushinda dhambi. [MH 166.5; HU Aya ya 20]

Alisema, “katika dhiki nyingi na taabu ya moyo niliwaandikia na machozi mengi; si kwamba mhuzunishwe, bali mpate kujua upendo wangu nilio nao kwenu jinsi ulivyo mwingi.” 2 Wakorintho 2:4 . “ijapokuwa naliwahuzunisha kwa waraka ule, sijuti; hata ikiwa nalijuta...Sasa nafurahi, si kwa sababu ya ninyi kuhuzunishwa, bali kwa sababu mlihuzunishwa, hata mkatubu... Maana, angalieni, kuhuzunishwa kuko huko kwa jinsi ya Mungu kulitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo... Kwa hiyo tulifarijiwa.” 2 Wakorintho 7:8-13. [MH 166.6; HU Aya ya 21]

“Nafurahi, kwa sababu katika kila neno nina moyo mkuu kwa ajili yenu…” “Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, sikuzote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza Injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi.; vile vile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu na katika kazi ya kutetea Injili na kuithibitisha, ninyi nyote mmeshirikiana nami neema hii.Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu; vile vile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu na katika kazi ya kutetea Injili na kuithibitisha, ninyi nyote mmeshirikiana nami neema hii.” “Basi, ndugu zangu, wapendwa wangu, ninaowaonea shauku, furaha yangu, na taji yangu, hivyo simameni imara katika Bwana, wapenzi wangu..Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;

“Kwa kuwa sasa twaishi, ikiwa ninyi mnasimama imara katika Bwana..” Mstari wa 16; Wafilipi 1:3-5; 1:6, 7 ; 4:1; 1 Wathesalonike 3:8. [MH 167.1; HU Aya ya 22]

Paulo aliwaandikia ndugu hawa kama “watakatifu katika Kristo Yesu;” lakini hakuwa akiwaandikia wale ambao walikuwa wakamilifu wa tabia. Aliwaandikia kama wanaume na wanawake waliokuwa wakishindana na majaribu na waliokuwa katika hatari ya kuanguka. Aliwaelekeza kwa “Mungu wa amani, aliyemleta tena kutoka kwa wafu Bwana wetu Yesu, yule Mchungaji Mkuu wa kondoo.” Aliwahakikishia kwamba “kwa damu ya agano la milele” ‘atawakamilisha katika kila tendo jema, wapate kufanya mapenzi Yake, akitenda ndani yenu lile lipendezalo machoni Pake, kwa njia ya Yesu Kristo. Waebrania 13:20, 21. [MH 167.2; HU Aya ya 23]

Wakati mtu mwenye makosa anatambua wazi kosa lake, hebu uwe mwangalifu katika kutoharibu heshima, ujasiri au hadhi yake. Usimkatishe tamaa kwa kutojali, kutoonyesha huruma au kutomwamini. Usiseme, "Kabla ya mimi kukupa ujasiri wangu, nitasubiri kuona kama kweli utasimama imara na kuyapinga majaribu." Mara nyingi hali hii ya kutoaminiana humfanya mtu aliyejaribiwa kujikwaa. [MH 167.3; HU Aya ya 24]

Twapaswa kujitahidi kuelewa udhaifu wa wengine. Tunajua kidogo kuhusu majaribu yaliyo ndani ya mioyo ya watu ambao wamefungwa katika minyororo ya giza na ambao hawana msimamo imara katika kufanya maazimio na nguvu ya maadili. Mtu wa kuhurumiwa zaidi ni yule ambaye anateseka kwa kujutia yale aliyoyafanya; huyu ni kama mtu aliyepigwa na butwaa, akiyumba-yumba, na kuzama mavumbini. Hawezi kuona chochote kwa uwazi. Akili yake ina ukungu, naye hajui achukue hatua gani. Nafsi nyingi maskini hazieleweki, wala kuthaminiwa, hizi zimesheheni dhiki na uchungu moyoni- Ni kondoo aliyepotea, anayemangamanga huku na kule. Hawezi kumpata Mungu, wakati anatamani sana apate msamaha na amani. [MH 168.1; HU Aya ya 25]

Lo, neno lolote lisisemwe ili kuongezea maumivu makali zaidi! Kwa nafsi zilizochoka kwa maisha ya dhambi, lakini bila kujua ni wapi pa kupata kitulizo, mwasilishe Mwokozi Mwenye huruma. Mshike mkono mtu wa namna hiyo na kumwinua, zungumza naye maneno ya kumtia moyo, yanayoimarisha ujasiri na imani yake na kumpa matumaini. Msaidie mtu huyu kuushika mkono wa Mwokozi. [MH 168.2; HU Aya ya 26]

Inakuwa rahisi sana kwetu kukata tamaa juu ya nafsi ambazo hazijibu mara moja jitihada zetu. Kamwe tusiache kufanya kazi kwa ajili ya roho za watu wakati kukiwa hata na mwale mmoja wa tumaini. Nafsi za thamani zilimgharimu sana Mkombozi wetu, aliyejidhabihu kwa bei isiyokadirika, nawe pia usizikatie tamaa haraka roho hizi na kuziachilia ziende kwa mjaribu. [MH 168.3; HU Aya ya 27]

Twahitaji kujiweka katika nafasi ya wale waliojaribiwa. Fikiria nguvu ya urithi, yaani kile walichopata toka kwa wazazi wao, na kisha ushawishi katika mahusiano mabaya na mazingira wanayoishi, nguvu ya mazoea mabaya. Je, sisi tunaweza kweli kujiuliza kwamba kwanini wameshushwa na kuwa na maadili ya chini kiasi hicho? Je, twaweza kujiuliza kwamba kwanini hawana wepesi katika kuitikia jitihada za kuwainua? [MH 168.4; HU Aya ya 28]

Mara nyingi, watu wanapoamua kuja upande wa injili, huoonekana kuwa rafu-rafu kwa tabia mbaya na wasio na matumaini, ila mbeleni watakuwa miongoni mwa wafuasi waaminifu na watetezi wa injili bora zaidi. Hawa sio watu waovu moja kwa moja kabisa. Ndani ya ule mwonekano wao wa nje, tunaouona kwa macho yetu, ambao unachukiza na kukimbiza watu, ipo misukumo mizuri ambayo inaweza kufikiwa. Bila ya mkono wa kuwasaidia kunyanyuka, watu hawa hawatakuwa na nguvu za kurudi katika hali bora kimwili, na kiroho, lakini kwa subira, na juhudi endelevu wanaweza kuinuliwa. Watu hawa wanahitaji maneno ya upole, upendo, kujaliwa kwa kutendewa fadhila, na msaada unaoonekana kwa macho. Wanahitaji aina ya ushauri ambao hautauzima mwanga hafifu wa ujasiri ulio katika nafsi zao. Hebu watendakazi wanaowasiliana na watu hawa walizingatie jambo hili. [MH 168.5; HU Aya ya 29]

Watu wengine wataonekana kuwa na akili ambazo zimedhalilishwa kwa muda mrefu kwa ufisadi na tukaona kwamba kamwe katika maisha haya hawataweza kuwa katika hali bora zaidi ambayo ilikuwa ni upendeleo wa Muumbaji wetu wawe nayo. Lakini bado miale angavu ya Jua la Haki inaweza kuangaza ndani ya nafsi zao. Ni fursa yao kuwa na maisha yanayopimwa na maisha ya Mungu (kuishi milele zote). Panda akilini mwa watu hawa mawazo yenye kuinua, yale yanayoboresha zaidi. Hebu mtindo wa maisha yako ukawawekee wazi watu hawa tofauti kati ya uovu na usafi wa moyo, giza na nuru. Kwa mfano wako, waache wasome maana ya kuwa Mkristo. Kristo ana uwezo wa kuwainua wadhambi-kupindukia na kuwaweka mahali ambapo watakubaliwa kama watoto wa Mungu, warithi pamoja na Kristo katika ule urithi wa kutokufa. [MH 169.1; HU Aya ya 30]

Kwa muujiza wa neema ya Mungu, wengi wanapata stahiki ya kuishi maisha ya manufaa. Wamedharauliwa na kuachwa, wamekata tamaa kabisa; wanaweza kuonekana kana kwamba hawajali, na kuonyesha hisia za kuvutiwa au kuchangamkia jambo, huonyesha utulivu, japokuwa wanapitia maumivu makali, wanakataa kabisa kuonyesha hisia zao. Lakini chini ya huduma ya Roho Mtakatifu, upumbavu unaofanya kuinuliwa kwao kuonekane hakuna uwezekano au tumaini kutapita. Akili mbaya, iliyojaa mawingu itaamshwa. Mtumwa wa dhambi atawekwa huru. Maadili mabaya na uovu utatoweka

mwishowe, na watu hawa wataushinda ujinga. Kupitia imani itendayo kazi kwa upendo, moyo utatakaswa na akili kuangaziwa. [MH 169.2; HU Aya ya 31]

SURA YA 11

KUFANYA KAZI NA WATU WASIO NA KIASI

Kila matengenezo ya kweli yana nafasi yake katika kazi ya injili na huelekea katika safari ya kuinua roho kufikia maisha mapya na matukufu. Matengenezo, haswa ya kiasi, yanahitaji kuungwa mkono na watendakazi Wakristo. Hawa wanapaswa kutilia maanani kazi hii na kuifanya kuwa suala hai. Wanapaswa wawasilishe kwa watu kila mahali kanuni za uhalisi wa kuwa na kiasi na kuwaita watu waliotia sahihi kwenye kiapo cha kuwa na kiasi. Jitihada za dhati zinapaswa kufanywa kwa ajili ya wale walio katika utumwa wa mazoea maovu....

....Msisitizo: Harakati ya kiasi ya kijamii inayokuza kiasi na kujiepusha kabisa na unywaji wa vileo au sigara ilianzishwa kwenye nchi nyingi. Washiriki katika vuguvugu hili kwa kawaida hukosoa ulevi wa pombe au kukuza utiifu wa kutotumia vileo vya aina yoyote, viongozi wake wanasisitiza athari mbaya za pombe kwa afya ya watu, haiba na maisha ya familia. Kwa kawaida harakati hiyo inafundisha elimu ya ubaya wa pombe na pia inadai kupitishwa kwa sheria mpya dhidi ya uuzaji wa pombe, au kukataza kabisa. Wakati wa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20, vuguvugu la kiasi lilipata umaarufu, hasa kwenye zile zinazozongumza Kiingereza, na nchi Skandinavia zilizo na Waprotestanti walio wengi, na hatimaye lilisababisha kutangazwa marufuku ya kitaifa katika nchi ya Canada (1918 hadi 1920), Norway (1919 hadi 1926), Finland (1919 hadi 1932), na Marekani (1920 hadi 1933), na India (1948 hadi sasa). Kuna mashirika kadhaa ya kiasi ambayo yanakuza kiasi na utii kama wema.). [MH *171.1*; HU Aya ya 1]

Kila mahali kuna kazi ya kufanywa kwa wale ambao kwa kukosa kiasi wameanguka. Maeneo yaliyosheheni makanisa, taasisi za kidini, na nyumba zinazodai kuwa za Kikristo, vijana wengi wanachagua njia ya uharibifu. Kupitia mazoea ya kutokuwa na kiasi wanajiletea magonjwa, na kupitia tamaa na pupa ya kujipatia pesa kwa ajili ya kujifurahisha katika anasa za dhambi wanaangukia kwenye mazoea ya kukosa uaminifu. Afya na tabia vinaharibiwa. Wanakuwa wageni kwa Mungu, na watu waliotengwa na jamii, roho hizi maskini huhisi kwamba hazina tumaini ama kwa maisha haya au kwa maisha yajayo. Mioyo ya wazazi imevunjika. Watu huwazungumzia watu hawa wakosefu kuwa hawana tumaini; lakini Mungu hawangalii kwa msimamo huo. Yeye anaelewa hali zote ambazo zimewafanya kuwa walivyo, Naye anawatazama huruma na kusikitika. Hili ni kundi la watu linalohitaji msaada. Usiwape watu hawa nafasi ya kusema, “Hakuna mtu anayeijali nafsi yangu.” [MH 171.2; HU Aya ya 2]

Miongoni mwa wahanga wa kutokuwa na kiasi, wapo wanaume wa tabaka zote na taaluma zote. Watu wenye vyeo vya juu, wenye vipaji vya hali ya juu, na walio na mafanikio makubwa, hawa wamejianika kwenye tamaa ya kuridhisha hamu mpaka wanapungua katika uwezo wa kukabiliana na majaribu. Baadhi yao ambao wakati fulani walikuwa na mali, sasa hawana hata makazi, hawana marafiki, na wanapitia katika mateso, taabu, huzuni, magonjwa, na fedheha. Wamepoteza uwezo wa kutawala nafsi zao (wanashindwa kujizuia). Pasipo mkono wa msaada, watazama chini na chini zaidi. Pamoja na haya, mazoea ya kuendekeza au kujifurahisha na anasa sio tu kwamba yanaleta ukosefu wa maadili mema na dhambi, bali pia huleta ugonjwa kwenye mwili wa mwanadamu. [MH 172.1; HU Aya ya 3]

Mara nyingi katika kuwasaidia watu wasio na kiasi ni lazima tutende kama ilivyokuwa kawaida ya Kristo, hebu tuzingatie kwanza afya ya miili yao. Watu hawa wanahitaji chakula na vinywaji vyenye afya, visivyochochea tamaa za mwili au kuwa na kileo, mavazi safi, mahali pa kujipatia usafi wa mwili. Wanahitaji kuzungukwa na mazingira yanayowasaidia katika kuinua ushawishi wa Kikristo. Inabidi kuwepo na eneo katika kila mji ambapo watumwa wa mazoea mabaya wanaweza kupokea msaada wa kuvunja minyororo inayowafunga. Kinywaji kikali, yaani kileo, kimechukuliwa na wengi kwamba ndio kitulizo pekee cha shida; lakini jambo hili halihitaji kuwa hivi ikiwa watu wa Mungu wataepuka kutenda sehemu ya kuhani na Mlawi katika Luka 10, na badala yake kama Wakristo, wafuate kielelezo cha Msamaria mwema. [MH 172.2; HU Aya ya 4]

Katika kushughulika na wahanga wa kutokuwa na kiasi lazima tukumbuke kwamba hatushughuliki na watu wenye utimamu wa akili, bali na wale ambao

kwa wakati huu wako chini ya nguvu za pepo wachafu. Hebu uwe mvumilivu na mwenye subira. Usifikirie juu ya sura ya hali ya kuchukiza, au mwonekano usio rafiki na wenye kuleta tishio, bali maisha ya thamani ambayo Kristo alikufa ili ayakomboe. Mlevi anapoamshwa na hisia ya kujidhalilisha kwake, wewe fanya yote unayoweza ili kumwonyesha kwamba wewe ni rafiki yake. Usiseme maneno yenye kukosoa kwa ukali. Usiruhusu tendo au mwonekano wako umdhihirishie kwamba wewe unamsimanga, umemkatia tamaa, unamchukia, au humpendi. Kuna uwezekano mkubwa kwamba mtu huyu masikini tayari anajilaani mwenyewe hata bila ya watu wengine kumsaidia kufanya hivyo. Hebu wewe msaidie ainuke. Zungumza naye maneno yatakayoimarisha imani yake. Tafuta jinsi ya kuimarisha kila sifa njema aliyo nayo katika tabia yake. Mfundishe jinsi ya kufika juu. Mwonyeshe kwamba inawezekana kwake kuishi na kujipatia heshima ya wanadamu wenzake. Msaidie aone thamani ya talanta ambazo Mungu amempa, lakini ambazo amepuuzia kuziboresha. [MH 172.3; HU Aya ya 5]

Ingawa dhamira yake imekengeuka na kudhoofishwa, bado kuna tumaini kwake katika Kristo. Bwana ataamsha moyoni mwake misukumo na matamanio matakatifu zaidi. Mhimize kushikilia tumaini lililowekwa mbele yake katika injili. Fungua Biblia mbele ya yule aliyejaribiwa, na anayejitahidi kushinda, kisha msomee tena na tena ahadi za Mungu. Ahadi hizi kwake zitakuwa kama majani ya mti wa uzima. Endelea kwa subira katika juhudi zako, mpaka kwa furaha na shukrani mkono wake unaotetemeka ushikamane na tumaini la ukombozi kupitia Kristo. [MH 173.1; HU Aya ya 6]

Lazima uwashikilie kwa nguvu wale unaojaribu kuwasaidia, vinginevyo hautashinda kamwe kwa ajili yao. Watakuwa wanajaribiwa kutenda uovu daima. Tena na tena wataonekana wako karibu kushindwa na uchu wa kileo; tena na tena wanaweza kuanguka; lakini kwa sababu ya hili, usisitishe juhudi zako. [MH 173.2; HU Aya ya 7]

Watu wameamua kuweka jitihada katika kuishi kwa ajili ya Kristo; lakini uwezo wao wa dhamiri umedhoofika, na hivyo, hawa ni lazima walindwe kwa uangalifu na wale wanaolinda roho kama wale ambao wanapaswa kutoa hesabu. Wamepoteza utu wao, na lazima waurudishe utu huu tena. Wengi inabidi wakabiliane na mielekeo mikali ya uovu waliyoirithi kutoka kwa wazazi wao. Tamaa kali zisizo za asili, misukumo ya kimwili, vilikuwa ndiyo urithi wao tangu kuzaliwa. Hawa ni lazima walindwe kwa uangalifu. Ndani na nje ya watu hawa, wema na uovu vinapigania ukuu. Wale ambao hawajawahi kupitia uzoefu kama huo hawawezi kujua hata kidogo jinsi nguvu kubwa za kuendekeza hamu au ukali wa mzozo kati ya mazoea ya kujifurahisha na

azimio la kuwa na kiasi katika mambo yote. Tena na tena vita lazima ipiganwe. [MH 173.3; HU Aya ya 8]

Wengi wanaovutwa kwa Kristo hawatakuwa na ujasiri wa kimaadili ili kuendeleza vita dhidi ya hamu na tamaa zingine za mwili. Lakini mtendakazi hapaswi kukatishwa tamaa na hili. Hivi ni wale tu waliookolewa kutoka kwenye vilindi vya chini kabisa ndio wanaorudi nyuma? [MH 173.4; HU Aya ya 9]

Kumbuka kwamba wewe hufanyi kazi peke yako. Malaika wahudumu huungana nawe katika huduma pamoja na kila mwana na binti wa Mungu aliye na moyo mkunjufu. Na Kristo Ndiye mrejeshaji. Tabibu Mkuu Mwenyewe husimama kando ya watenda-kazi Wake waaminifu, akiiambia nafsi iliyotubu, “Mwanangu, umesamehewa dhambi zako.” Marko 2:5, [MH 174.1; HU Aya ya 10]

Wengi ni miongoni mwa watu waliotengwa watakaolishikilia tumaini lililowekwa mbele yao katika injili na wataingia katika ufalme wa mbinguni, huku wale ambao walibarikiwa kuwa na fursa kubwa na nuru kuu ambayo hawakuitumia vizuri maishani mwao, wataachwa nje gizani. [MH 174.2; HU Aya ya 11]

Wahanga wa mazoea mabaya lazima waamshwe na kuona umuhimu wa kufanya jitihada kwa ajili yao wenyewe. Wengine waweza kujitahidi sana kuwainua, neema ya Mungu yaweza kutolewa kwao bure, Kristo aweza kuwasihi, malaika Zake waweza kutumika; lakini bado yote haya yakawa bure, isipokuwa wao binafsi kuamka na kupigana vita kwa niaba yao wenyewe. [MH 174.3; HU Aya ya 12]

Maneno ya mwisho ya Daudi kwa Sulemani, angali yu kijana mdogo, na ambaye karibuni ilikuwa anaenda kupokea kiti cha ufalme Israeli, yalikuwa, “uwe hodari, ujionyeshe kuwa mwanamume.” 1 Wafalme 2:2. Kwa kila mtoto wa mwanadamu, nafasi imetolewa kwake kuwa mteule wa taji ya milele, ananenewa maneno haya yaliyovuviwa, “uwe hodari, ujionyeshe kuwa mwanamume.” [MH 174.4; HU Aya ya 13]

Wale wapendao kujifurahisha wenyewe kwa mazoea maovu lazima waongozwe kuona na kutambua kwamba matengenezo makubwa ya maadili ni muhimu ikiwa wangetaka kuwa watu bora. Mungu awaita hawa waamke na kwa nguvu za Kristo warudishe utu bora walioumbiwa na Mungu ambao wanakuwa wumeudhabihu kwa kuendekeza dhambi. [MH 174.5; HU Aya ya 14]

Utambuzi wa nguvu ya kutisha ya kujaribiwa, tamanio chochezi liongozalo katika kuendekeza dhambi, wengi huomboleza kwa kukata tamaa, “Siwezi

kuupinga uovu.” Hebu mwambie mtu huyu kwamba aweza, kwamba ni lazima aupinge. Huko nyuma anaweza kuwa alishindwa tena na tena, lakini historia hiyo, sio lazima iwe hivyo kila mara. Mtu huyu ni kweli kwamba ni dhaifu katika nguvu za maadili, akitawaliwa na mazoea ya maisha ya dhambi. Ahadi na maazimio yake ni kama kamba za mchanga. Utambuzi wake kuhusiana na ahadi zake zilizovunjwa na viapo ambavyo hakuvishikilia hudhoofisha imani yake katika unyofu wake mwenyewe na kumfanya ahisi kwamba Mungu hawezi kumkubali au kutendea kazi juhudi zake. Lakini mtu hana haja ya kukata tamaa. [MH 174.6; HU Aya ya 15]

Wale wanaoweka tumaini lao katika Kristo hawapaswi kufanywa watumwa wa tabia au mwelekeo wowote waliorithi au kuupalilia wenyewe. Badala ya kufungiwa katika utumwa wa kuipenda dunia na anasa zake, wanapaswa kutawala kila hamu na tamaa ya mwili. Mungu hajatuacha tupigane na uovu kwa nguvu zetu wenyewe zenye ukomo. Haijalishi kwamba tuna mielekeo tuliyoirithi au tuliyoipalilia wenyewe kwa kufanya mabaya, twaweza kuwa washindi kupitia nguvu ambayo Yeye Yuko tayari kutupatia. [MH 175.1; HU Aya ya 16]

Nguvu ya Dhamiri (Kusudi)

Mtu ajaribiwaye anahitaji kuelewa nguvu halisi ya dhamiri. Hii ndiyo nguvu yenye mamlaka katika asili ya mwanadamu—nguvu ya uamuzi, uwezo wa kuchagua (uchaguzi wa mtu). Kila kitu hutegemea hatua ya utendaji sahihi wa dhamiri ya mtu. Matamanio ya wema na usafi wa moyo ni jambo jema na sahihi, kwa kadiri yanavyokwenda; lakini tukiishia hapa, hayafai kitu. Wengi wataangukia kwenye uharibifu na huku wakiendelea kupoteza muda kwa kutarajia na kutamani kushinda tabia zao mbaya. Watu hawa hawayasalimishi mapenzi yao kwa Mungu. Hawachagui kumtumikia Yeye. [MH 176.1; HU Aya ya 17]

Mungu ametupatia uwezo wa kuchagua kwa hiari; ni fursa na kazi yetu kuufanyia mazoezi. Sisi hatuwezi kubadilisha mioyo yetu, hatuwezi kudhibiti mawazo yetu, misukumo yetu, nia zetu. Wanadamu hatuwezi kujisafisha wenyewe ili tufae kwa ajili ya utumishi wa Mungu. Lakini twaweza kuchagua kumtumikia Mungu, twaweza kumpa Yeye mapenzi yetu; ndipo Yeye atafanya kazi ndani yetu kunia na kutenda kufuatana na mapenzi Yake mema. Hivyo asili yetu yote italetwa chini ya utawala wa Kristo. [MH 176.2; HU Aya ya 18]

Kwa kuizoeza dhamiri kunavyotakiwa (nia zetu), mabadiliko yote yanaweza kufanywa katika maisha yetu. Kwa kusalimisha mapenzi yetu kwa Kristo, twaungana wenyewe pamoja na uweza wa Mungu. Twapokea nguvu kutoka juu ili kutufanya tuwe imara. Maisha safi na bora, maisha ya ushindi dhidi ya

kuridhisha hamu na tamaa zote za mwili, yanawezekana kabisa kwa kila mtu ambaye atayaunganisha mapenzi yake ya kibinadamu yaliyo dhaifu na yanayoyumbayumba kwenye mapenzi ya Mungu yasiyoyumbayumba ya aliye Mweza wa yote. [MH 176.3; HU Aya ya 19]

Wale wanaopambana dhidi ya nguvu ya hamu (ulafi) wanapaswa kufundishwa kanuni za maisha yenye afya. Wanapaswa kuonyeshwa kuwa ukiukwaji wa sheria za afya, kwa kuunda mazingira ya ugonjwa mwilini na tamaa zisizo za kawaida, huweka msingi wa tabia ya uraibu. Ni kwa kuishi tu kwa utii wa kanuni za afya ndipo waweza kuwa na tumaini la kukombolewa kutoka kwenye tamaa ya vichocheo na vikolezo visivyo vya asili *(Msisitizo: vichocheo kama pombe, madawa ya kulevya, tumbaku kama sigara na ugoro, kahawa, chai ya Uchina ile nyeusi n.k)*. Ingawa watu wanategemea nguvu za Bwana ili kuvunja vifungo vya hamu (tamaa za mwili), hawana budi kushirikiana na Mungu kwa kutii sheria Zake, za maadili na mwili. [MH 176.4; HU Aya ya 20]

Wapeni ajira watu walio na bidii katika kufanya matengenezo. Hakuna mtu yeyote anayeweza kufanya kazi ambaye anapaswa kufundishwa kutarajia kupewa chakula na mavazi na malazi bila gharama yoyote (atoke jasho kwa kazi au anunue). Kwa ajili yao wenyewe hawa wahitaji, na kwa ajili ya wengine, mikakati fulani inapaswa kuwekwa ili waweze kurudisha sawasawa na yale wanayopokea. Himiza kila juhudi ili wajitegemeze. *(Msisitizo: watu watiwe moyo katika kila juhudi inayofanywa ili kuwasaidia watu kujikimu kimaisha)*. Hii itaiwamarisha katika kujiheshimu wenyewe na kuwa na uhuru adili. Na akili inapotumiwa kwenye kazi inayonufaisha na inayoshughulisha akili na mwili ni muhimu sana katika ulinzi dhidi ya vishawishi. [MH 177.1; HU Aya ya 21]

Kukatishwa Tamaa; Hatari

Wale wanaofanya kazi kwa ajili ya watu walioanguka watakatishwa tamaa na wengi wanaotoa ahadi za kufanya matengenezo. Wengi watafanya badiliko la juu juu tu katika tabia na mazoea yao. wanachochewa na msisimko, na kwa muda wanaweza kuonekana kana kwamba wamebadilika; lakini hakuna badiliko la kweli la moyoni. Wanathamini upendo uleule wenye ubinafsi, wana kiu ileile ya anasa za kipumbavu, tamaa ile ile ya kujifurahisha wenyewe. Hawana maarifa yahusuyo kazi ya kujenga tabia, na hawawezi kutegemewa kama watu wa kanuni. Wamedhoofisha nguvu zao za akili na roho kwa kuendekeza hamu na tamaa za kimwili, na hii inawafanya kuwa dhaifu. Wao ni vigeugeu na wanaobadilika-badilika. Misukumo yao inaelekea kwenye

matamanio machafu. Watu hawa mara nyingi ni chanzo cha hatari kwa wengine. Wanapoangaliwa kama wanaume na wanawake waliofanya matengenezo, wanaaminiwa na kupewa majukumu na kisha kuwekwa mahali ambapo ushawishi wao huwaharibu watu wasio na hatia. [MH 177.2; HU Aya ya 22]

Hata wale ambao kwa dhati wanatafuta kufanya matengenezo, hawako nje ya mpaka wa hatari ya kuanguka (kiroho na kimwili). Wanahitaji kuhudumiwa kwa hekima kubwa pamoja na huruma na upole. Tabia ya kuwasifia kwa kutia chumvi na kuwainua watu hawa ambao wameokolewa kutoka kwenye vilindi vya chini kabisa, wakati mwingine huthibitisha uharibifu wao. Kitendo cha kuwaalika wanaume na wanawake kuelezea hadharani uzoefu wa maisha yao ya dhambi ni cha hatari kwa msemaji na wasikilizaji. Kukita kwenye matukio ya uovu huharibu akili na roho. Na umaarufu wanaopewa watu waliookolewa una madhara kwao. Wengi huongozwa kuhisi kwamba maisha yao ya dhambi yamewapa umaarufu fulani. Kupenda kuvumisha ubaya walioutenda na roho ya kujitumainia wenyewe huhimizwa ambayo huthibitisha kifo cha roho. Ni kwa kutojitumainia tu na kutegemea huruma ya Kristo ndipo watu hawa wanaweza kusimama *(Msisitizo: Wengi hupata nafasi ya kutoa ushuhuda wenye mambo mengi ya kina ambayo walifanya wakiwa waraibu au wafuasi wa Shetani, haya yangechujwa kwanza hasa kwa waamini wachanga, maana mengine hayana sababu kuanikwa hadharani)*. [MH 178.1; HU Aya ya 23]

Wote wanaotoa uthibitisho wa wongofu wa kweli wanapaswa kutiwa moyo kuwasaidia wengine kushinda uraibu. Mtu awaye yote asimfukuze mtu aliyeacha utumishi kwa Shetani kwa ajili ya utumishi kwa Kristo. Mtu anapotoa uthibitisho kwamba Roho wa Mungu anapigana mieleka naye, mhimize uwezavyo ili ajiunge katika utumishi wa Bwana. “Wahurumieni wengine walio na shaka.” Yuda 22. Wale walio na busara katika hekima itokayo kwa Mungu wataona roho zinazohitaji msaada, watu ambao wametubu kwa dhati, lakini ambao bila kutiwa moyo itakuwa vigumu kwao kuthubutu kushikilia tumaini. Bwana ataweka ndani ya mioyo ya watumishi Wake, hekima ya kuwakaribisha watu hawa wanaotetemeka na kutubu kwenye ushirika wao wa upendo. Haijalishi ni dhambi gani zinazowazongazonga, au hata wameanguka chini kiasi gani, watu hawa wanapomjia Kristo kwa majuto, Yeye huwapokea. Kisha wape kitu cha kumfanyia Yeye. Ikiwa wanatamani kufanya kazi katika kuwainua na kuwaimarisha wengine kutoka kwenye shimo la uharibifu ambalo wao wenyewe waliokolewa, basi wapewe nafasi hiyo. Wape fursa ya kushirikiana na Wakristo wenye uzoefu, ili wapate nguvu za

kiroho. Jaza mioyo na mikono yao kazi kwa ajili ya Bwana. [MH 178.2; HU Aya ya 24]

Nuru inapomulika ndani ya nafsi, wengine ambao walionekana kuwa wamezama kabisa dhambini watakuwa wafanyakazi wenye mafanikio makubwa kwa ajili ya wadhambi wengine kama wao wenyewe walivyokuwa hapo awali. Kwa imani katika Kristo wengine watakuwa katika viwango vya juu katika utumishi na kukabidhiwa majukumu katika kazi ya kuokoa roho. Watu hawa wanaona udhaifu wao wenyewe ulipo, wanatambua upotovu wa asili yao. Wanajua nguvu ya dhambi, na nguvu ya mazoea ya uovu. Wanatambua kutoweza kwao kufaulu bila msaada wa Kristo, na kilio chao cha mara kwa mara ni, “Naitupa nafsi yangu isiyo na uwezo juu Yako.” “(I cast my helpless soul on Thee)” [MH 179.1; HU Aya ya 25]

Hawa wanaweza kusaidia wengine. Yule ambaye amejaribiwa, ambaye tumaini lake lilikuwa karibu kutoweka, lakini ambaye aliokolewa kwa kusikia ujumbe wa upendo, anaweza kuelewa maarifa ya namna ya kuokoa roho. Yeye ambaye moyo wake umejaa pendo la Kristo kwa sababu yeye mwenyewe ametafutwa na Mwokozi na kurudishwa kundini, ajua jinsi ya kuwatafuta wale waliopotea. Anaweza kuwaelekeza wadhambi kwa Mwana-Kondoo wa Mungu. Amejitoa kikamilifu kwa Mungu na amekubaliwa katika huyo Mpendwa (Efeso 1:6). Mkono ambao katika udhaifu ulinyooshwa kutoa msaada umefumbatiwa hasa. Kwa huduma ya watu kama hao, wapotevu wengi wataletwa kwa Baba. [MH 179.2; HU Aya ya 26]

Kwa kila nafsi inayohangaika kuinuka toka katika maisha ya dhambi na kuingia katika maisha ya usafi, sehemu kuu ya uwezo inakaa katika jina lile ambapo hakuna “jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.” Matendo 4:12. “Mtu akiona kiu” ya tumaini lenye utulivu, kwa ajili ya kukombolewa kutoka katika mazoea ya dhambi, Kristo asema, “na aje Kwangu, anywe.” Yohana 7:37. Dawa pekee ya uovu ni neema na uweza wa Kristo. [MH 179.3; HU Aya ya 27]

Maazimio mazuri yanayofanywa kwa nguvu za mtu mwenyewe hayana msaada wowote. Si viapo vyote duniani vitavunja nguvu ya mazoea mabaya. Kamwe watu hawawezi kuwa na kiasi katika mambo yote, mpaka mioyo yao ifanywe upya kwa neema ya Mungu. Kwa uwezo wetu wenyewe hatuwezi kukaa mbali na dhambi hata wasaa mmoja. Kila wasaa sisi tu utegemezi katika Mungu. [MH 179.4; HU Aya ya 28]

Matengenezo ya kweli huanza na utakaso wa roho. Kazi yetu kwa walioanguka itapata mafanikio ya kweli pale tu neema ya Kristo

inapotengeneza upya tabia, na nafsi inaletwa katika uhusiano hai na Mungu. [MH 180.1; HU Aya ya 29]

Kristo aliishi maisha ya utii kamili kwa sheria ya Mungu, na katika hili aliweka kielelezo kwa kila mwanadamu. Maisha aliyoyaishi katika ulimwengu huu hatuna budi kuyaishi kwa nguvu Zake na chini ya maagizo Yake. [MH 180.2; HU Aya ya 30]

Tunapofanya kazi yetu kwa ajili ya watu walioanguka, matakwa ya sheria ya Mungu na hitaji la uaminifu Kwake Mungu vinapaswa kusisitizwa kwenye akili na moyo. Usikose kamwe kuonyesha kwamba kuna tofauti kubwa kati ya yule anayemtumikia Mungu na yule asiyemtumikia. Mungu ni upendo, lakini Yeye hawezi kutoa udhuru wa watu kupuuzia amri Zake kwa makusudi. Maagizo ya serikali Yake (katiba) ni ya namna kwamba watu hawawezi kusalimika na athari ya kukosa uaminifu. Ni wale tu wanaomheshimu Yeye, ndio Naye aweza kuwaheshimu. Mwenendo wa mwanadamu katika ulimwengu huu huamua hatima yake ya milele. Vile alivyopanda, ndivyo apaswavyo kuvuna. Chanzo kitafuatiwa na matokeo. [MH 180.3; HU Aya ya 31]

Hakuna upungufu wa utii kamili uwezao kupatana na kiwango cha matakwa ya Mungu. Mungu hajaacha matakwa Yake yasijulikane kwa wanadamu. Yeye hajaamuru cho chote ambacho siyo cha lazima ili kusudi amlete mwanadamu katika kupatana Naye. Yatupasa kuwaelekeza watu wenye dhambi kwenye ubora Wake wa tabia na kuwaongoza kwa Kristo, ambaye ni kwa neema Yake pekee ubora huu wa tabia waweza kufikiwa. [MH 180.4; HU Aya ya 32]

Mwokozi alichukua juu Yake udhaifu wa wanadamu na kuishi maisha yasiyo na dhambi, ili wanadamu wasiwe na hofu kuwa kwa sababu ya udhaifu wa asili wa mwanadamu, basi wao hawawezi kushinda dhambi. Kristo alikuja kutufanya sisi “washiriki wa tabia ya Uungu,” (partakers of the divine nature) na maisha Yake yatangaza kwamba ubinadamu, ukiwa umeungana na Uungu, hautendi dhambi. [MH 180.5; HU Aya ya 33]

Mwokozi alishinda ili amwonyeshe mwanadamu jinsi anavyoweza kushinda. Kristo alikutana na majaribu yote ya Shetani kwa Neno la Mungu. Kwa kutumainia ahadi za Mungu, Alipokea nguvu za kutii amri za Mungu, na mjaribu hangeweza kunufaika kwa lolote kutoka Kwake. Kwa kila jaribu, jibu Lake lilikuwa, “Imeandikwa.” Ndiyo sababu Mungu ametupa Neno Lake ambalo kwa hilo sisi tuweze kupinga uovu. Ahadi kubwa mno na za thamani ni zetu, ili kwamba kwa hizo tupate “kuwa washirika wa tabia ya Uungu, tukiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.” 2 Petro 1:4. [MH 181.1; HU Aya ya 34]

Msihi yule ajaribiwaye asiangalie hali ilivyo, udhaifu wa nafsi yake, au nguvu ya majaribu, bali aangalie nguvu ya Neno la Mungu. Nguvu zote za Neno la Mungu ni zetu sisi wanadamu. Asema mtunga zaburi, “moyoni mwangu nimeliweka Neno Lako, nisije nikakutenda dhambi. "Kwa Neno la midomo Yako nimejiepusha na njia za mharibifu." Zaburi 119:11; 17:4. [MH 181.2; HU Aya ya 35]

Zungumzia ujasiri kwa watu; wainue watu kwa Mungu kwa sala. Wengi walioshindwa na majaribu wamefedheheshwa na kushindwa kwao, na wanaona kwamba ni bure kwao kumkaribia Mungu; lakini wazo hili ni pendekezo la adui. Wanapokuwa wametenda dhambi, na kuhisi kwamba hawawezi kuomba, waambie kwamba huu ndio wakati haswa wa kuomba. Kwa vyo vyote wanavyoweza kuona haya, na kujisikia wanyonge sana; lakini wakiziungama dhambi zao, Yeye aliye mwaminifu na Mwenye haki atawasamehe dhambi zao, na kuwasafisha na udhalimu wote. [MH 181.3; HU Aya ya 36]

Hakuna kinachoonekana kwamba hakina msaada, lakini kisichoweza kushindwa kabisa, kama ile roho ambayo inahisi kutokufaa kabisa na kutegemea kikamilifu neema za Mwokozi. Kwa sala, kwa kujifunza Neno Lake, kwa imani katika uwepo Wake wa kudumu, wanadamu walio dhaifu zaidi waweza kuishi katika kwa ukaribu na Kristo aliye hai, Naye atawashika mkono ambao hautawaacha kamwe. [MH 182.1; HU Aya ya 37]

Maneno haya ya thamani kila nafsi inayokaa ndani ya Kristo inaweza kuyafanya kuwa yake. Inaweza kusema: [MH 182.2; HU Aya ya 38]

“Lakini mimi, nitamtazamia Bwana; nitamngojea Mungu wa wokovu wangu; Mungu wangu atanisikia. 8 Usifurahi juu yangu, Ee adui yangu; niangukapo, nitasimama tena; nikaapo gizani, Bwana atakuwa nuru kwangu.” Mika 7:7, 8. [MH 182.3; HU Aya ya 39]

“Atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari.” Mika 7:19, Noyes. [MH 182.4; HU Aya ya 40]

Mungu ameahidi: [MH 182.5; HU Aya ya 41]

“Nitafanya wanadamu kuadimika kuliko dhahabu safi, na watu kuliko dhahabu ya Ofiri.” Isaya 13:12. [MH 182.6; HU Aya ya 42]

“Kwa nini kulala mazizini arukapo hua, Mbawa zake ziking'aa kama fedha Na manyoya yake kama dhahabu?.” Zaburi 68:13. [MH 182.7; HU Aya ya 43]

Wale ambao Kristo amewasamehe zaidi watampenda zaidi. Hawa ndio ambao katika siku ya mwisho watasimama karibu na kiti Chake cha enzi. [MH 182.8; HU Aya ya 44]

“Nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao.” Ufunuo 22:4. [MH 182.9; HU Aya ya 45]

SURA YA 12

KUSAIDIA WATU WASIO NA AJIRA/KAZI NA WASIO NA MAKAZI

Wako wanaume na wanawake wenye mioyo mikunjufu ambao kwa shauku wanajali hali duni ya watu maskini, na ni njia gani zaweza kupatikana kwa ajili ya faraja yao. Namna watu wasio na ajira na wasio na makazi wanavyoweza kusaidiwa kujipatia baraka za majaliwa ya Mungu na kuishi maisha Aliyokusudia mwanadamu aishi, ni swali ambalo wengi wanafanya bidii sana kulipatia jibu. Lakini si wengi, hata miongoni mwa waelimishaji na

viongozi wa serikali ambao wanaelewa sababu za hali hii ya sasa ya jamii. Wale wanaoshikilia hatamu za serikali wanashindwa kutatua tatizo la umaskini, ufukara uliokithiri, na uhalifu unaozidi kuongezeka. Wanahangaika bure kuweka misingi mizuri ya shughuli (na biashara) katika hali salama zaidi. [MH 183.1; HU Aya ya 1]

Laiti watu wangezingatia kwa makini zaidi mafundisho ya Neno la Mungu, basi wangepata suluhu la matatizo haya yanayowatatanisha. Katika suala hili, kuna mengi ya kujifunza kutoka katika Agano la Kale kuhusiana na suala la ajira na faraja kwa maskini. [MH 183.2; HU Aya ya 2]

Mpango wa Mungu kwa Ajili ya Israeli

Katika mkakati wa Mungu kwa ajili ya Israeli kila familia ilikuwa na nyumba/makazi kwenye kipande cha ardhi, na eneo la kutosha kwa ajili ya kilimo. Hivyo ndivyo ilivyowezekana kuwa na njia, uwezo na motisha kwa ajili ya maisha yenye kunufaisha wanadamu na yenye bidii katika stadi za kazi mbalimbali, zenye kusaidia watu kujikimu/kujitegemea wenyewe kimaisha. Na hakuna ubunifu wa mwanadamu ye yote ambao umewahi kuboresha mpango huu wa Mungu. Kwa dunia kuuacha mpango huu wa Mungu, kumesababisha kwa kiwango kikubwa umaskini na unyonge uliopo leo (Viwanda, miji mikubwa na watu wasio na ardhi). [MH 183.3; HU Aya ya 3]

Katika makazi ya Israeli Kanaani, ardhi iligawanywa kati ya watu wote, na ni Walawi peke yao, kama wahudumu wa Patakatifu ndio hawakuwa kwenye mpango wa mgawanyo sawa wa ardhi. Makabila yalihesabiwa kulingana na familia, na kila familia, kulingana na hesabu yake, iligawanyiwa urithi. [MH 184.1; HU Aya ya 4]

Na ingawa mtu angeweza kwa muda fulani kuuza au kumpa mwingine urithi au mali yake hii, hangeweza kubadilishana na mwingine urithi huu kwa kudumu, ambao ulipaswa kurithiwa na watoto wake. Mtu huyu alipokuwa na uwezo wa kuikomboa ardhi yake, alikuwa huru wakati wo wote kufanya hivyo, na akarudishiwa ardhi yake. Madeni yote yaliondolewa katika kila mwaka wa saba, na katika mwaka wa hamsini, au mwaka wa yubile, mali yote ihusianayo na ardhi ilirudishwa kwa familia iliyopewa ardhi hiyo tangu awali (mwanzoni mwa ugawaji). [MH 184.2; HU Aya ya 5]

“Nchi haitauzwa kabisa kabisa,” ulikuwa ni mwongozo wa Bwana; “Kwani nchi ni yangu mimi; maana ninyi ni wageni na wasafiri wangu. Nanyi mtatoa ukombozi kwa ajili ya nchi, katika nchi yote ya milki yenu. Kwamba nduguyo amekuwa maskini, na kuuza sehemu ya milki yake, ndipo jamaa yake aliye karibu naye atakuja, naye ataikomboa ile aliyoiuza nduguye. Na kama mtu hana atakayeikomboa, naye mwenyewe amepata mali na kujiona kuwa anayo

ya kutosha kuikomboa; ndipo na aihesabu hiyo miaka ya kuuzwa kwake, na kilichozidi kumrudishia huyo mtu aliyeinunua; naye atairejea milki yake. Lakini asipoweza kujipatia mwenyewe, ndipo hiyo iliyouzwa itakaa mkononi mwake huyo aliyeinunua, hata mwaka wa yubile; na katika yubile itatoka, naye atairejea milki yake. Mambo ya Walawi 25:23-28. [MH 184.3; HU Aya ya 6]

"Na mwaka wa hamsini mtautakasa, na kupiga mbiu ya kuachwa mahuru katika nchi yote kwa watu wote wanayokaa; itakuwa ni yubile kwenu, nanyi kila mtu atairudia milki yake mwenyewe, nanyi mtarejea kila mtu kwa jamaa yake." Kifungu cha 10. [MH 185.1; HU Aya ya 7]

Kwa hivyo kila familia ilikuwa na uhuru katika milki yake, na ulinzi ulitolewa dhidi ya kuwa na mali na utajiri, au ufukara na uhitaji uliokithiri. [MH 185.2; HU Aya ya 8]

Mafunzo Ya Tasnia Au Stadi Za Kazi Ikiwemo Juhudi Katika Kazi

Katika Israeli, mafunzo ya tasnia au stadi za kazi mbalimbali za mikono na zinginezo, pamoja na bidii katika kuzifanya kazi hizi, vilizingatiwa kama wajibu. Kila baba aliwajibika kuwafundisha wanawe shughuli fulani yenye manufaa, yaani uzalishaji wa aina fulani. Wanaume wakuu katika Israeli walizoezwa shughuli za tasnia/ujuzi fulani. Ujuzi wa majukumu yahusianayo na mama wa nyumbani ulizingatiwa kuwa muhimu kwa kila mwanamke. Na ujuzi katika majukumu haya ulizingatiwa kama ndiyo nyadhifa ya juu kabisa katika jamii kwa mwanamke. [MH 185.3; HU Aya ya 9]

Tasnia mbalimbali zilifundishwa katika shule za manabii, na wanafunzi wengi walijitegemeza kimaisha kwa kazi ya mikono. [MH 186.1; HU Aya ya 10]

Kuwajali Maskini

(Kutilia maanani maskini mioyoni mwetu)

Mipango hii, hata hivyo, haikuondoa umaskini kabisa. Halikuwa kusudi la Mungu kwamba umaskini ukome kabisa. Umaskini ni mojawapo ya njia Zake Mungu katika ujengaji wa tabia bora. "Kwa maana maskini hawatakoma katika nchi milele; ndipo ninakuamuru na kukuambia, Mfumbulie kwa kweli mkono wako nduguyo, mhitaji wako, maskini wako, katika nchi yako." Kumbukumbu la Torati 15:11. [MH 186.2; HU Aya ya 11]

"Kama akiwapo mtu maskini pamoja nawe, nduguzo mmojawapo, ndani ya malango yako mojawapo, katika nchi yako akupayo Bwana, Mungu wako, usifanye moyo wako kuwa mgumu, wala usimfumbie mkono wako nduguyo maskini; lakini mfumbulie mkono wako kwa kweli, umkopeshe kwa kweli

yatoshayo haja yake katika ahitajiayo.” Mstari wa 7, 8. [MH 186.3; HU Aya ya 12]

“Na ikiwa ndugu yako amekuwa maskini, na mkono wake umelegea kwako, ndipo utamsaidia, atakaa nawe kama mgeni, na msafiri.” Mambo ya Walawi 25:35. [MH 186.4; HU Aya ya 13]

“Na mtakapovuna mavuno ya nchi yenu, usivune kabisa kabisa pembe za shamba lako, wala usiyakusanye masazo ya mavuno yako;. “1Uvunapo mavuno yako katika shamba lako, ukasahau mganda shambani, usirudi kuuchukua; na uwe wa mgeni, au yatima, au mjane; ili Bwana, Mungu wako, akubariki katika kazi yote ya mikono yako. Utakapochuma matunda ya mizeituni yako, usirudi kuchuma mara ya pili; yaliyobaki apewe mgeni, na yatima, na mjane. Uchumapo zabibu katika shamba lako la mizabibu, usichume mara ya pili; zilizobaki apewe mgeni, na yatima, na mjane.” Mambo ya Walawi 19:9; Kumbukumbu la Torati 24:19-21. [MH 186.5; HU Aya ya 14]

Hakuna aliye na haja ya kuogopa kwamba ukarimu wake ungeletea uhitaji au ufukara. Kuzitii amri za Mungu bila shaka kungeleta mafanikio na ushindi. “Kwa ajili ya jambo hili,” Mungu alisema, “Mpe kwa kweli, wala moyo wako usisikitike utakapompa; kwa kuwa atakubarikia Bwana, Mungu wako, kwa neno hili katika kazi yako yote, na katika kila utakalotia mkono wako.” “Kwani Bwana, Mungu wako, atakubarikia, kama alivyokuahidi; nawe utakopesha mataifa mengi, lakini hutakopa; tena utayatawala mataifa mengi, usitawaliwe na wao.” Kumbukumbu la Torati 15:10, 6. [MH 187.1; HU Aya ya 15]

Kanuni za Biashara

Neno la Mungu halitoi idhini yo yote ambayo italitajirisha tabaka moja kwa kulidhulumu na kulipatia mateso tabaka lingine. Katika shughuli zetu zote za kibiashara Mungu atufundisha kujiweka mahali pa wale tunaowashughulikia, kujali si tu mambo yetu, bali pia ya wengine. Yule ambaye anatafuta kujinufaisha mwenyewe kwa maafa ya mwingine, au anayetafuta kujinufaisha mwenyewe kupitia kutojiweza au udhaifu wa wengine kwa kuwakandamiza kwa namna fulani, ni mvunjaji wa kanuni na maagizo ya Neno la Mungu. [MH 187.2; HU Aya ya 16]

“Usipotoshe hukumu ya mgeni, wala ya yatima; wala usitwae mavazi ya mjane, yawe rehani. “Umkopeshapo jirani yako cho chote kikopeshwacho usiingie katika nyumba yake kwenda kutwaa rehani kwake. Simama nje, yule umkopeshaye akuletee nje ile rehani.Naye akiwa ni mtu maskini, usilale na rehani yake.” “Kama ukitwaa vazi la jirani yako kuwa rehani, utampa kabla ya jua kuchwa; maana hilo ndilo vazi lake tu: ... na itakuwa, atakaponililia,

nitasikia; kwa maana mimi ni mwenye neema." "Kama ukiuzia jirani yako kitu, au ukinunua kitu chochote mkononi mwa jirani yako, msidhulumiane" Kumbukumbu la Torati 24:17, 10-12; Kutoka 22:26, 27; Mambo ya Walawi 25:14. [MH 187.3; HU Aya ya 17]

"Msifanye udhalimu katika hukumu, au katika vipimo vya urefu, wala uzani, wala wingi." "Usiwe na vipimo mbalimbali katika mfuko wako, kubwa na dogo. Usiwe na vipimo mbalimbali katika nyumba yako, kikubwa na kidogo." "Mizani ya haki, na mizani ya haki, na efa ya haki, na hini ya haki, mtakuwa nayo. Mambo ya Walawi 19:35, ARV; Kumbukumbu la Torati 25:13, 14, ARV; Mambo ya Walawi 19:36, ARV [MH 188.1; HU Aya ya 18]

"Akuombaye mpe, na anayetaka kukopa kwako usimgeuze." "Mtu mbaya hukopa wala halipi; bali mwenye haki hurehemu, na kutoa." Mathayo 5:42; Zaburi 37:21. [MH 188.2; HU Aya ya 19]

"Toeni shauri, fanyeni haki; fanya kivuli chako kuwa kama usiku katikati ya adhuhuri; kuficha waliofukuzwa; usimsaliti mkimbizi." "Waliofukuzwa wangu na wakae nawe; ... uwe siri kwao mbele ya mtekaji nyara." Isaya 16:3 4. [MH 188.3; HU Aya ya 20]

Mpango wa maisha ambao Mungu aliwapa Waisraeli ulikusudiwa kuwa somo lenye kielelezo muhimu kwa wanadamu wote. Ikiwa kanuni hizi zingetekelezwa leo, ulimwengu huu ungekuwa mahali tofauti jinsi gani! [MH 188.4; HU Aya ya 21]

Ndani ya mipaka mikubwa ya asili bado kuna nafasi kwa watu wanaoteseka na wahitaji kupata makazi. Ndani ya kifua cha ardhi kuna rasilimali za kutosha kukidhi chakula na haja zote za wanadamu. Utajiri huu uliofichwa katika vilindi vya dunia ni baraka kwa wote walio na ujasiri na nia na ustahimilivu wa kukusanya hazina zake. [MH 188.5; HU Aya ya 22]

Kuilima ardhi, kazi ambayo Mungu alimpa mwanadamu pale Edeni, hufungua uwanja wa fursa kwa wengi kupata riziki zao zote (Kilimo na Ufugaji). [MH 189.1; HU Aya ya 23]

"Mtumaini Bwana, ukatende mema;

Ukae katika nchi, upendezwe na uaminifu" Zaburi 37:3. [MH 189.2; HU Aya ya 24]

Maelfu na makumi ya maelfu wangeweza kuwa wanafanya kazi ya kulima ardhi, ambao sasa wameshonana mijini, wakitafuta nafasi ya kujipatia kipato kidogo tu. Mara nyingi kipato hiki kidogo hakitumiki kwa ajili ya chakula, bali

hupelekwa kwa muuzaji pombe, ili kukipata kile kinachoharibu roho na mwili. [MH 189.3; HU Aya ya 25]

Wengi huona shida kufanya kazi na kujichosha, nao hujaribu kutafuta riziki kwa hila badala ya kufanya kazi kwa bidii. Tamaa hii ya kujipatia riziki bila ya kufanya kazi hufungua mlango wa unyonge na uovu na uhalifu usio na kikomo. [MH 189.4; HU Aya ya 26]

Mitaa Duni Ya Jiji

Katika miji mikubwa kuna makundi makubwa ya watu waliosahaulika, ambao hupata matunzo na umakini mdogo zaidi ya wanavyotunzwa wanyama wasioweza hata kusema. Fikiria familia zinazoishi pamoja katika nyumba zenye hali duni, nyingi zikiwa na vyumba vya chini ya ardhi vyenye giza, vinavyovuja na kuwa na unyevunyevu na uchafu. Katika maeneo haya duni watoto huzaliwa na kukua na kufa. Hawajawahi kuona uzuri wa maumbile ya asili ya Mungu yaliyoumwa kuburudishaili miili yao na kuinua mioyo yao. Wakiwa na mavazi yaliyotatuka na bila kushiba vizuri, wanaishi katikati ya uovu na upotovu, wakifinyangwa tabia za unyonge na dhambi inayowazunguka. Watoto hulisikia jina la Mungu likitajwa katika lugha chafu tu. Maneno machafu ya makufuru, matusi, kukosolewa, kugombezwa na kusimangwa hujaa masikioni mwao. Moshi wa vileo na tumbaku, uvundo mbaya, upotovu wa maadili, huharibu fahamu zao. Hivyo wengi hufunzwa kuwa wahalifu, maadui kwa jamii ambayo imewaacha kwenye taabu na udhalilishaji. [MH 189.5; HU Aya ya 27]

Sio maskini au walala hoi wote waliosongamana kwenye makazi duni ndio wapo kwenye hili tabaka. Waume na wake wanaomcha Mungu wameangushwa kwenye dimbwi la kina kirefu cha umaskini kwa sababu ya ugonjwa au maafa, mara nyingi kupitia hila za watu wasiotenda haki, wale wanaoishi kwa kuwasumbua wenzao. Wengi walio wanyofu na wenye nia njema wanakuwa maskini kwa kukosa mafunzo stadi fulani ili kujikimu kimaisha. Kwa ujinga wao wanafikia hatua ya kutoweza kushindana na ugumu wa maisha. Watu hawa wakikimbilia mijini, mara nyingi hawawezi kupata kazi. Wakiwa wamezungukwa na matukio yenye vituko na sauti za uovu, wanakabiliwa na majaribu mabaya sana. Wakiwa wameshonana karibu na watu wengine, mara nyingi hujumuishwa pamoja na kundi la watu wabaya na waliodhalilishwa, ni kwa mapambano tu ya nguvu zisizokuwa za mwanadamu, nguvu zisizo za kawaida, ndipo wanaweza kusitiriwa ili wasizame hadi kwenye vilindi vile vile. Wengi hushikilia uadilifu wao, wakichagua kuteseka kuliko kutenda dhambi. Tabaka hili hasa linahitaji msaada, huruma, na kutiwa moyo. [MH 190.1; HU Aya ya 28]

Endapo maskini waliojazana sasa katika miji wangeweza kupata makazi yaliyo na ardhi, sio tu wangejiwezea kujipatia riziki, bali pia wangepata afya na furaha ambayo sasa haijulikani kwao (60% ya watu duniani wapo mijini). Kama wakiendelea kukaa mijini watakuwa watu ambao daima wana kazi ngumu, bila makazi na wakikaa kwenye vichochoro, na kupata chakula chenye lishe ndogo kisichokidhi mahitaji ya mwili, uchumi usio mzuri, na wakizalisha cho chote kile wanatumia chote, hivyo hawawezi kuuza nje ya makazi yao, mara nyingi shida na ufukara vinakuwa ndiyo fungu lao). Lakini ni baraka iliyoje kwao kuuacha mji, pamoja na mivuto yake ya uovu, misukosuko yake na uhalifu, taabu na uchafu, kwa ajili ya utulivu na amani na usafi wa mashambani. [MH 190.2; HU Aya ya 29]

Kwa wengi waishio mijini ambao hawana hata kipande cha nyasi za kijani ambazo miguu yao inaweza ikakanyaga, ambao mwaka baada ya mwaka wamekuwa tu wakitazama nje mazingira machafu na vichochoro vyembamba, kuta za matofali na lami, na anga lililojaa mavumbi na moshi—ikiwa watu hawa wangeweza kupelekwa kwenye maeneo ya mashambani, yaliyozungukwa na maeneo yenye kijani kibichi, misitu na vilima na vijito, angahewa wazi na hewa safi na iburudishayo huko mashambani, ingeonekana kwa hawa watu kana kwamba wapo mbinguni. [MH 191.1; HU Aya ya 30]

Wakiwa wamejitenga kwa kiasi kikubwa na kutokuwa karibu wala kutegemeana na wanadamu wengine, na wakiwa wamejitenga na kanuni na mazoea potovu na misisimko mibaya ya dunia, watakuwa karibu zaidi na mahali maumbile ya asili yalipo. Uwepo wa Mungu utakuwa halisi zaidi kwa watu hawa. Wengi wangejifunza somo la kumtegemea Mungu kwa njia hii. Kupitia asili wataisikia sauti Yake, ikinena na mioyo yao juu ya amani na upendo Wake mioyoni mwao, na akili na roho na mwili vitaitikia nguvu za uponyaji, zitoazo uzima. [MH 192.1; HU Aya ya 31]

Endapo watu hawa watakuwa na bidii ya kazi kwa ajili ya kujikimu kimaisha, basi ni lazima wengi wao wapate msaada, kutiwa moyo na mafunzo yanayotoa mwongozo vizuri. Kuna wingi wa familia maskini ambazo hakuna kazi bora zaidi itakayowasaidia ila umishenari unaofanywa kwao kwa kuwasaidia kupata ardhi na kufanya makazi hapa na kisha wajifunze jinsi ya kuiboresha ardhi hii ili iweze kuwa na uzalishaji mzuri na kisha iweze kuwapatia riziki. [MH 192.2; HU Aya ya 32]

Hitaji la msaada kama huu wa mafunzo yaliyopangiliwa vyema hauko tu mijini. Hata mashambani lipo hitaji hilo, pamoja na uwezekano wake wote wa maisha bora, watu wengi maskini walio huko mashambani wana uhitaji mkubwa *(Msisitizo: jinsi ya kushughulika na ardhi, tasnia/stadi, ujuzi na mambo mengine yahusuyo*

maisha bora ikiwemo na kufanya kazi kwa bidii). Jumuiya nyingi hazina elimu katika masuala ya tasnia, stadi, bidii ya kazi, elimu, afya na usafi. Familia nyingi huishi katika vibanda vibovu, zikiwa haina vitu vya samani/fanicha na mavazi *(ya kujistiri kulingana na umri na majira)*, bila zana *(majembe, nyundo, koleo, misumari, mkokoteni, ndoo, spana, fagio, n.k)*, bila vitabu (vya kujifunza zaidi), bila starehe au faraja na vitu vya muhimu vinavyofanya maisha kuwa rahisi *(upatikanaji rahisi wa maji, vyanzo vya nishati, choo kizuri na vyombo vingine vya nyumbani)*. Watu hawa wanaoishi maisha ya ufukara, na viwango vilivyoshushwa chini kama wanyama, wana miili dhaifu na yenye ulemavu wa namna fulani, hudhihirisha matokeo ya urithi mbaya kutoka kwa wazazi na mazoea mabaya. Watu kama hawa ni lazima waelimishwe kuanzia kwenye msingi haswa *(Mfano jinsi ya kuoga, jinsi ya kushika jembe, kusafisha mikono, kutunza maji ya mvua, kupika mboga bila ya kuzipotezea lishe n.k)*. Wameishi maisha yasiyobadilika, ya kivivuvivu, ya kipotovu, na sasa wanahitaji kusaidiwa kwa kufundishwa matengenezo ya tabia. [MH 192.3; HU Aya ya 33]

Je, wanawezaje kuamshwa kutoka usingizini ili waone hitaji lao la kuwa na maisha bora au maendeleo? Wanawezaje kuelekezwa kwenye maisha ya juu zaidi ambayo Mungu anataka waishi? Watasaidiwa vipi ili waweze kuinuka? Je, ni nini kifanyike mahali ambapo umaskini umekithiri na wanashindana na huu umaskini katika kila hatua? Hakika kazi hii ni ngumu. Matengenezo ya lazima hayawezekani isipokuwa waume na wake hawa kusaidiwa na nguvu iliyo nje ya uwezo wao wenyewe. Ni kusudi la Mungu kwamba matajiri na maskini wafungamanishwe pamoja kwa ukaribu kwa mahusiano ya huruma na kusaidiana. Wale ambao wana mali, vipaji, na uwezo hawana budi kuzitumia karama hizi kuwabariki wenzao. [MH 193.1; HU Aya ya 34]

Wakulima Wakristo wanaweza kufanya kazi halisi ya umishenari katika kuwasaidia maskini kupata makazi kwenye maeneo ya mashambani na kuwafundisha jinsi ya kutumia zana za kilimo na kuufanya udongo uwe wenye kutoa matunda. Wafundishe jinsi ya kutumia zana za kilimo, jinsi ya kulima mazao tofauti-tofauti, jinsi ya kupanda kwa ubora na kutunza bustani za miti ya matunda. [MH 193.2; HU Aya ya 35]

Wengi wanaolima ardhi hushindwa kupata mrejesho wa mavuno wanayostahili au mapato ya kutosha kwa sababu ya uzembe wao. Bustani zao hazitunzwi vizuri, mbegu au miche ya mazao havipandwi kwenye shamba katika wakati ufaao, na kazi ya juu tu ndiyo ambayo inafanywa katika kulima

udongo (hawatengenezi mboji n.k). Kisha baada ya mavuno au matokeo haya mabaya watu husingizia kuwa yanasababishwa na ardhi kutokuwa na rutuba. Ushahidi huu wa uongo mara nyingi hutolewa katika kuilaani ardhi ambayo, kama ingefanyiwa kazi ipasavyo, hakika ingeleta faida kubwa. Mipango dhaifu, nguvu kidogo zinazowekezwa, utafiti mdogo tu wa mbinu bora za kilimo (je, udongo umepimwa na kujua rutuba yake, na mazao gani yalimwe kwenye aina hii ya udongo n.k), yote haya hutoa kengele yenye sauti kubwa ya hitaji la matengenezo (matengenezo ya kilimo na mbinu bora itakayosaidia kujikimu kimaisha). [MH 193.3; HU Aya ya 36]

Hebu bora zifundishwe kwa watu wote walio tayari kujifunza. Ikiwa kuna ye yote ambaye hataki uzungumze nao juu ya mawazo haya ambayo ni ya hali ya juu, toa masomo yako kimyakimya. Boresha ardhi ya shamba lako mwenyewe. Zungumza na majirani zako pale unapoweza na yaache mavuno ya shamba lako yawe msemaji fasaha wa mbinu sahihi na bora za ukulima na lishe ya ardhi kuliko jambo lo lote ambalo ungeweza kulifanya. Onyesha kile kinachoweza kufanyika kwenye ardhi wakati inashughulikiwa na kufanyiwa kazi ipasavyo. [MH 193.4; HU Aya ya 37]

Umakini utolewe kuhusiana na kuanzisha tasnia/stadi mbalimbali ili familia maskini zijipatie kazi ya kufanya. Mafundi seremala, wahunzi, na kwa kweli kila mtu anayeelewa stadi fulani iliyo muhimu, anapaswa kuhisi kwamba ni jukumu lake kuwafundisha na kuwasaidia wale wasiojua na wasio na kazi. [MH 194.1; HU Aya ya 38]

Katika kutoa huduma kwa maskini, upo wigo mpana wa huduma kwa wanawake na wanaume pia. Mpishi stadi, mtunza-nyumba, mshona nguo, muuguzi—hakika msaada wa watu hawa wote unahitajika hapa. Familia maskini zifundishwe jinsi ya kupika, kutengeneza na kukarabati nguo zao wenyewe, jinsi ya kuuguza wale walio wagonjwa, jinsi ya kuitunza nyumba ipasavyo. Wavulana na wasichana wafundishwe kikamilifu baadhi ya shughuli na biashara muhimu au kazi. [MH 194.2; HU Aya ya 39]

Familia za Wamishonari

Familia za wamishenari (walei yaani familia zenye utume mioyoni mwao, ambazo zimebobea stadi mbalimbali) zinahitajika kwenda kukaa mahali pasipokuwa na watu nje ya mji. Wakulima, wawezeshaji wa uchumi, wajenzi, na wale walio na ujuzi wa sanaa za ufundi mbalimbali, waende kwenye mashamba yaliyotelekezwa na kuboresha ardhi, kuanzisha vituo vya kujifunza stadi mbalimbali, wakiandaa nyumba zisizo na gharama kubwa kwa ajili yao wenyewe, na kuanza kuwasaidia majirani zao. [MH 194.3; HU Aya ya 40]

Maeneo ya asili yaliyparuza, maeneo ya porini, Mungu ameyafanya yavutie kwa kuweka mambo mazuri katika maumbilie haya yasiyopendeza machoni. Hii ndiyo kazi tuliyoitiwa kuifanya. Hata maeneo ya dunia yaliyo na majangwa, mahali ambapo kuonekana kwake machoni ni pabaya, yanaweza kuwa kama bustani ya Mungu. “Na katika siku hiyo viziwi watasikia Maneno ya hicho chuo, na macho ya vipofu yataona katika upofu na katika giza. Wanyenyekevu nao wataongeza furaha yao katika Bwana, na maskini katika wanadamu watafurahi katika Mtakatifu wa Israeli.” Isaya 29:18, 19. [MH 194.4; HU Aya ya 41]

Kwa maelekezo katika nyanja ya vitendo, mara nyingi twaweza kuwasaidia maskini kwa ufanisi zaidi. Kama ilivyo kawaida, wale ambao bado hawajafundishwa kufanya kazi, hawana ujuzi, uvumilivu, utunzaji wa fedha, kujikana nafsi na kujinyima. Hawajui jinsi ya kusimamia shughuli (shamba, kazi n.k). Mara nyingi kwa kukosa uangalifu na maamuzi sahihi wanapoteza yale yote yahusuyo uzalishaji bora ambayo yangezikimu familia zao katika kukidhi mahitaji muhimu na kuwapatia faraja ikiwa vitu hivi vingetumika kwa uangalifu na kujali/kusimamia matumizi. “Chakula kingi chapatikana kwa ukulima wa masikini; lakini viko viharibiwavyo kwasababu ya dhuluma.” Mithali 13:23. [MH 194.5; HU Aya ya 42]

Twaweza kuwapa maskini kwa njia ambayo itawadhuru, pale tunapowafundisha kuwa tegemezi. Elimu kama hiyo huhimiza ubinafsi na kutokuwa msaada ama kwa mtoaji au mpokeaji. Mara nyingi hupelekea uvivu, ubadhirifu, na kutokuwa na kiasi. Hakuna mtu anayeweza kupata riziki yake mwenyewe ambaye ana haki ya kuwategemea watu wengine. Msemo “Ninaudai ulimwengu riziki yangu” ndani yake una maana ya uongo, ulaghai, na wizi. Ulimwengu hauna deni lo lote la mtu ambaye anaweza kufanya kazi na kujipatia riziki. [MH 195.1; HU Aya ya 43]

Upendo wa kweli huwasaidia watu ili waweze kujisaidia wenyewe. Mtu akija kwenye malango yetu na kutuomba chakula, tusimrudishe nyumbani kwake akiwa na njaa; umaskini wake waweza kuwa ni matokeo mabaya yaliyowahi kumkumba. Lakini wema wa kweli humaanisha zaidi ya kumpa vizawadi-zawadi tu. Inamaanisha nia ya kweli katika ustawi wa wengine. Twapaswa kutafuta namna ya kuelewa mahitaji ya maskini na wenye dhiki, na kisha kuwapa msaada ambao utawanufaisha kwa namna bora zaidi. Kutoa mawazo kama vile njozi, mashauri, wakati, na juhudi binafsi kunagharimu zaidi ya kutoa pesa tu. Lakini hii ndiyo sadaka ya kweli (ukiwapa viazi wafundishe pia kulima viazi). [MH 195.2; HU Aya ya 44]

Wale wanaofundishwa kujipatia kile wapokeacho watajifunza kwa dhati kufanya mengi kutokana na hicho. Katika kujifunza kujitegemea, wanapata kile ambacho si tu kitawafanya wajitegemee, bali kitawawezesha kuwasaidia

wengine pia. Fundisha umuhimu wa majukumu ya maisha kwa wale wanaochezea fursa zao. Waonyeshe kwamba dini ya Biblia kamwe haiwafanyi wanadamu kuwa wakaaji tu. Daima Yesu aliwahimiza watu kufanya kazi kwa bidii. “Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi?” Na alimwambia mtu mvivu. “Ni lazima nifanye kazi ... maadamu ni mchana: usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi.” Mathayo 20:6; Yohana 9:4. [MH 195.3; HU Aya ya 45]

Ni fursa ya watu wote kwenye maisha yao ya nyumbani, mila na desturi zao na utaratibu, kutoa ushuhuda kwa ulimwengu wa kile ambacho injili inaweza kukifanya kwa wale wanaoitii. Kristo alikuja katika ulimwengu wetu ili kutupa kielelezo cha vile tunavyoweza kuwa. Yeye hutarajia wafuasi Wake wawe vielelezo sahihi katika mahusiano yote ya maisha. Atamani mguso wa mbingu uonekane kwenye mambo yale yanayoonekana nje. [MH 196.1; HU Aya ya 46]

Nyumba na mazingira yetu wenyewe vinapaswa kuwa vielelezo vya msingi, zikifundisha mbinu za uboreshaji ili bidii ya kazi, usafi, ladha nzuri, na utakaswaji viweze kuchukua mahali pa uvivu, uchafu, uduni na machafuko. Kwa maisha na kilelelezo vyetu twaweza kuwasaidia wengine kutambua kile ambacho kinachukiza katika tabia zao au mazingira yao, na kwa adabu na uungwana wa Kikristo twaweza kuhimiza uboreshaji. Tunapoonyesha kuwajali au kuwapenda watu hawa, tutapata fursa ya kuwafundisha jinsi ya kutumia nguvu zao kwa njia bora zaidi. [MH 196.2; HU Aya ya 47]

Tumaini Na Moyo Mkuu

Hatuwezi kufanya cho chote bila kuwa na moyo mkuu na uvumilivu. Zungumza maneno ya tumaini na moyo wa ushujaa kwa maskini na watu waliokata tamaa. Ikihitajika, toa uthibitisho unaoonekana kwa macho wa kuwajali na kuwapenda kwa kuwasaidia wanapofika katika maeneo magumu au changamoto zinazowashinda kutatua. Wale ambao wamekuwa na hali nzuri kimaisha, au mafaniko mengi, hata na wao wakumbuke kwamba bado hukosea katika mambo mengi, na kwamba hata wao inawauma pale makosa yao yanapobainishwa na kuwekewa mbele yao mfano mzuri wa yale wanayopaswa kuwa. Kumbuka kwamba wema unatatimiza mambo makuu zaidi kuliko kuwakemea au kuwakosoa watu. Unapojaribu kuwafundisha watu, waache waone kwamba wewe unatamani wafikie viwango vya juu zaidi, na kwamba wewe upo tayari kuwapa msaada ili wafikie hapo. Ikiwa katika baadhi ya mambo watu hawa wanashindwa, usiwe mwepesi kuwalaumu. [MH 196.3; HU Aya ya 48]

Unyenyekevu, kujinyima, kujikana nafsi, jinsi ya kutunza pesa vyema na kuepukana na ubaradhifu, ni masomo muhimu sana ambayo watu maskini

wanapaswa kujifunza, japokuwa mara nyingi huyaona kuwa ni magumu na hawapendi kuyakaribisha kwa moyo mkunjufu. Jinsi ulimwengu ulivyo, na roho yake husisimua watu kila mara na kukuza kiburi, kupenda kujionyesha, kujifurahisha nafsi, upotovu, na uvivu. Maovu haya huleta maelfu kwenye umaskini na kuzuia maelfu zaidi kutoka kwenye unyonge, shida na udhaifu. Wakristo wanapaswa kuwatia moyo maskini kupinga ushawishi wa namna hii. [MH 196.4; HU Aya ya 49]

Yesu alikuja katika ulimwengu huu kwa unyenyekevu. Alizaliwa katika mazingira ya ufukara. Mkuu wa enzi ya mbinguni, Mfalme wa utukufu, Amiri jeshi wa malaika wote, Alijinyenyekeza na kuukubali ubinadamu, na kisha akachagua maisha ya ufukara, kudhalilishwa na unyonge. Hakuwa na fursa ambazo maskini walizikosa. Taabu, shida, na ufukara vilikuwa sehemu ya uzoefu Wake wa kila siku. “Mbweha wana mapango,” Alisema, “na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa Chake.” Luka 9:58. [MH 197.1; HU Aya ya 50]

Yesu hakutafuta kusifiwa, kuthaminiwa, kushabikiwa au kupigiwa makofi na wanadamu. Hakuamrisha jeshi lo lote duniani. Hakutawala ufalme wo wote hapa duniani. Hakujipendekeza kwa matajiri na waheshimiwa wa ulimwengu huu. Hakudai cheo miongoni mwa viongozi wa taifa. Alikaa miongoni mwa watu wa hali ya chini. Alipuuza tofauti za bandia/feki zilizokuwepo katika jamii. Yeye hakutoa umakini wo wote maalumu, au kujipendekeza kwa watu waliotoka katika koo za watu wenye nyadhifa za juu, watu wenye mali, talanta, elimu, na vyeo vya juu. [MH 197.2; HU Aya ya 51]

Alikuwa Mfalme wa mbinguni, lakini hakuwachagua wanafunzi Wake kutoka miongoni mwa wanasheria wasomi, watawala, waandishi, au Mafarisayo. Watu kama hawa aliwaacha, kwa sababu walijivunia elimu na vyeo vyao. Walikuwa wametekwa na mila zao na ushirikina. Yeye aliyeweza kusoma mioyo yote, alichagua wavuvi wanyenyekevu waliokuwa tayari kufundishwa na kujifunza. Alikula pamoja na watoza ushuru na watu wenye dhambi, na kuchangamana na watu wa kawaida, sio ili kuwa kama wao kiulimwengu, bali kwa kanuni na kuwa kielelezo sahihi kwao Yeye aweze kuwainua kutoka katika udunia na unyonge wao. [MH 197.3; HU Aya ya 52]

Yesu alitaka kurekebisha viwango vya ulimwengu visivyofaa kuipima thamani ya wanadamu. Alichukua nafasi Yake pamoja na maskini, ili aweze kuondoa unyanyapaa ambao ulimwengu ulikuwa umeuhusianisha na umaskini. Ndani ya umaskini, Yeye ameondoa milele aibu na dharau, kwa kuwabariki maskini, warithi wa ufalme wa Mungu. Naye atuelekeza hata leo, kwenye njia aliyoikanyaga, akisema, “Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe,

ajitwike msalaba wake kila siku, na anifuate Mimi.” Kifungu cha 23. [MH 197.4; HU Aya ya 53]

Watendakazi Wakristo wanapaswa kukutana na watu pale walipo, na kuwaelimisha, sio kwa majivuno, bali kwa kujenga tabia. Wafundishe jinsi Kristo alivyofanya kazi na alivyojikana nafsi Yake Mwenyewe. Wasaidie kujifunza kutoka Kwake masomo ya kujikana nafsi, kujinyima na kujitoa kikamilifu. Wafundishe wajihadhari na kuendekeza masuala ya kufuata mitindo. Maisha ni ya thamani sana, nayo yamesheheni majukumu mazito, na matakatifu, na hivyo hayawezi kupotezwa katika kujifurahisha nafsi au kupenda ubinafsi na uchoyo. [MH 198.1; HU Aya ya 54]

Mambo Bora Zaidi Maishani

Waume kwa wake wengi hawajaanza kikamilifu kuelewa lengo kuu la maisha haya. Wanavutiwa kirahisi na vitu vinavyong’aa machoni na wanapenda maonyesho. Wana matamanio ya ukuu wa dunia hii. Malengo makuu na ya kweli ya maisha yamehatarishwa kwa matamanio yao ya ukuu. Mambo bora na muhimu zaidi maishani—unyenyekevu, uaminifu, ukweli, ukamilifu/usafi wa moyo, uadilifu—hayawezi kununuliwa au kuuzwa kwa fedha. Mambo haya hutolewa bure kwa mwenye elimu kama kwa yule asiye na elimu, kwa mtendakazi wa hali ya chini kama kwa mtawala anayeheshimiwa. Kwa maana Mungu ametoa kwa kila mtu raha inayoweza kufurahiwa na tajiri na maskini vilevile—furaha ipatikanayo katika kupalilia na kukuza usafi wa mawazo na kutokuwa na ubinafsi katika matendo yetu, furaha itokanayo na kunena maneno ya huruma na kutenda matendo ya ukarimu. Toka kwa wale wanaotumika hivyo, nuru ya Kristo hung'aa ili kuangazia maisha yaliyotiwa giza na kiza. [MH 198.2; HU Aya ya 55]

Tuwasaidiapo maskini katika mahitaji yao ya kimwili, daima tuzingatie mahitaji yao ya kiroho. Tufanye maisha yetu wenyewe yashuhudie juu ya uwezo wa uangalizi wa Mwokozi. Tufanye tabia zetu zidhihirishe kiwango cha juu ambacho watu wote wanaweza kukifikia. Fundisha injili katika vielelezo rahisi. Fanya kila kitu unachotakiwa kufanya kiwe somo katika kujenga tabia. [MH 198.3; HU Aya ya 56]

Katika mzunguko duni wa kazi ngumu za maisha, watu walio dhaifu sana, na wasiojulikana kabisa, wanaweza kuwa watendakazi pamoja na Mungu na kujipatia faraja kwa uwepo Wake na neema Yake idumishayo. Hawapaswi kujichosha wenyewe kwa mahangaiko mengi, wasiwasi na fadhaa zisizo za lazima. Wafanye kazi siku baada ya siku, wakitimiza kwa uaminifu kazi ambayo majaliwa ya Mungu huwakabidhi, na Yeye anaahidi kwamba atawatunza. Asema: [MH 199.1; HU Aya ya 57]

“Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu.” "Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.” Wafilipi 4:6; 4:7. [MH 199.2; HU Aya ya 58]

Uangalizi wa Bwana u juu ya viumbe Vyake vyote. Yeye awapenda wote pasipo ubaguzi, isipokuwa ana huruma zaidi kwa wale ambao wameitwa kubeba majukumu yenye mizigo mizito zaidi maishaini kuliko wengine. Watoto wa Mungu sharti wakutane na majaribu na mambo magumu. Lakini wanapaswa kupokea fungu lao hili kwa moyo mkunjufu, wakikumbuka kwamba kwa yale yote ambayo ulimwengu huu umepuuza kuwapa, Mungu Mwenyewe atalijaza hilo pengo kwa upendeleo Wake ulio bora zaidi. [MH 199.3; HU Aya ya 59]

Ni pale tunapopitia katika maeneo magumu ndipo Yeye hudhihirisha nguvu na hekima Yake katika kujibu maombi yetu ya kinyenyekevu. Tuaminini na kuwa na moyo mkuu kabisa ndani Yake kwamba Yeye ni Mungu asikiaye na kujibu maombi. Atajidhihirisha kwako kama Yule ambaye ni msaada hakika katika kila hitaji. Yeye aliyemwumba mtu, aliyempa uwezo wake wa ajabu kimwili, kiakili, na kiroho, hakika hatamnyima mwanadamu kile ambacho ni cha lazima kudumisha uhai ambao ametupatia Yeye Mwenyewe. Yeye aliyetupatia Neno Lake—majani ya mti wa uzima—hatazuia maarifa ya namna ya kuwahudumia watoto Wake wahitaji. [MH 199.4; HU Aya ya 60]

Hekima yawezaje kupatikana kwa yeye ashikaye jembe la plau na kuwaongoza ng'ombe ili walime shamba? Kwa kuitafuta kama fedha, na kuisaka kama hazina iliyositirika. “Kwa maana Mungu wake anamwagiza vizuri, na kumfundisha." Isaya 28:26. “Hayo nayo yatoka kwa BWANA wa majeshi, mwenye shauri la ajabu, apitaye wote kwa hekima Yake.” Mstari wa 29, [MH 199.5; HU Aya ya 61]

Yeye aliyewafundisha Adamu na Hawa namna ya kuitunza bustani ya Edeni, leo atamani kuwafundisha wanadamu. Kuna hekima kwake yeye aliendeshaye jembe la plau na kupanda mbegu. Watu wanaomwamini na kumtii, Yeye atafungua njia mbele yao ili waweze kusonga mbele. Na wasonge mbele kwa ujasiri na moyo mkuu, wakimtumaini Yeye kuwapatia mahitaji yao kwa kadiri ya utajiri na wema Wake. [MH 200.1; HU Aya ya 62]

Yeye aliyeulisha umati wa watu kwa mikate mitano na samaki wawili wadogo, leo pia anaweza kutupatia matunda ya jasho la kujishughulisha kwetu. Yeye aliyewaambia wavuvi wa Galilaya, “Tupeni nyavu zenu na kuvua samaki,” na ambaye walipotii, alizijaza nyavu zao mpaka zikachanika, atamani watu Wake waone katika hili uthibitisho wa yale ambayo atawafanyia

hivi leo. Mungu Yule Yule ambaye kule jangwani aliwapa wana wa Israeli Mana kutoka mbinguni bado Yu hai na anatawala. Atawaongoza watu Wake na kuwapa stadi, ujuzi na maarifa katika kazi walizoitiwa kufanya. Atawapa hekima wale wanaojitahidi kufanya wajibu wao kwa umakini na kwa akili. Yeye amilikiye dunia ni tajiri wa rasilimali, na atabariki kila mtu anayetafuta kuwabariki watu wengine. [MH 200.2; HU Aya ya 63]

Twahitaji kutazama juu mbinguni kwa imani. Hatupaswi kukatishwa tamaa pale tunaposhindwa, wala hatupaswi kuvunjika moyo kwa kwa sababu ya kucheleweshwa. Twapaswa kufanya kazi kwa uchangamfu, tumaini, na moyo wa shukrani, tukiamini kwamba dunia hii ina hazina nyingi ndani mwake kwa ajili ya mtendakazi mwaminifu kuzikusanya, akiba hii yenye utajiri kuliko dhahabu au fedha. Milima na miinuko huwa inabadilika-badilika; dunia huchakaa kama vazi; lakini baraka za Mungu, ambazo Yeye huwaandalia watu Wake na kuzitandaza kwenye meza jangwani, hazitakoma kamwe. [MH 200.3; HU Aya ya 64]

SURA YA 13

MASKINI WASIOJIWEZA

Yote yajapofanywa yawezayo kufanywa katika kuwasaidia maskini ili waweze kujisaidia wenyewe, bado kuna wajane na yatima, wazee, wasiojiweza, na wagonjwa, wanaohitaji huruma na uangalizi wetu. Hawa hawapaswi kupuuziwa kamwe. Wamekabidhiwa kwetu na Mungu Mwenyewe, ambaye ametufanya tuwe wasimamizi na mawakili Wake ili tuwaonyeshe huruma, upendo, na ukarimu. [MH 201.1; HU Aya ya 1]

Kaya/Jamaa Ya Watu Wa Imani

"Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema, na hasa jamaa ya waaminio." Wagalatia 6:10. [MH 201.2; HU Aya ya 2]

Kwa namna ya pekee, Kristo ameweka juu ya kanisa Lake wajibu wa kuwatunza wahitaji walio miongoni mwa washiriki wa kanisa. Amewaruhusu maskini Wake kuwa ndani ya kila kanisa. Daima wanapaswa kuwa kati yetu, Naye huwapa washiriki wa kanisa jukumu binafsi la kuwatunza. [MH 201.3; HU Aya ya 3]

Kwa jinsi ndugu wa familia za kawaida tunavyojaliana sisi kwa sisi, tukiwahudumia wagonjwa, kuwategemeza walio dhaifu, kufundisha wasio na elimu, kuwafundisha stadi kwa vitendo watu wasio na uzoefu, ndivyo "nyumba ya imani" inavyopasa kuwatunza wahitaji na wale wasiojiweza. Majukumu haya hayapaswi kuwekewa visingizio vya namna yo yote. [MH 201.4; HU Aya ya 4]

Wajane na Yatima

Mjane na yatima ndiyo lengo kuu la utunzaji maalum wa Bwana. [MH 202.1; HU Aya ya 5]

"Baba wa yatima na mwamuzi wa wajane, Mungu katika kao Lake takatifu." [MH 202.2; HU Aya ya 6]

"Kwa sababu Muumba wako ni mume wako; Bwana wa majeshi ndilo Jina Lake; na Mtakatifu wa Israeli Ndiye Mkombozi wako; Yeye ataitwa Mungu wa dunia yote." [MH 202.3; HU Aya ya 7]

"Waache watoto wako wasio na baba, Mimi nitawahifadhi hai, na wajane wako na wanitumaini Mimi." Zaburi 68:5; Isaya 54:5; Yeremia 49:11. [MH 202.4; HU Aya ya 8]

Akina baba wengi, wanapofariki, na kutengana na wapendwa wao, wanapumzika kwa imani juu ya ahadi ya Mungu ya kuitunza familia yao. Bwana huwapa wajane na yatima mahitaji yao, sio kwa kufanya muujiza wa kudondosha mana kutoka mbinguni, si kwa kuwatumia kunguru kuwaletea chakula; bali kwa muujiza wa kufukuza ubinafsi kwenye mioyo ya wanadamu, na kufungua chemchemi za upendo kama wa Kristo mioyoni mwao. Wenye dhiki na waombolezao, Yeye huwakabidhi kwa wafuasi Wake kama amana yenye thamani. Wana mengi wanayoyahitaji toka kwetu. [MH 202.5; HU Aya ya 9]

Katika nyumba zilizojawa mahitaji muhimu ya maisha, katika magunia na maghala yaliyosheheni mavuno tele ya mashambani, katika mabohari yaliyojaa bidhaa za nguo, na vyumba vilivyohifadhi dhahabu na fedha, Mungu amejalia mali hizo kuwa riziki ya wahitaji hawa. Atuita tuwe njia ya ukarimu Wake. [MH 202.6; HU Aya ya 10]

Akina mama wengi wajane walio na watoto wasio na baba wanajitahidi kwa ujasiri kubeba mzigo wao kama baba na kama mama, wakijitaabisha kupitavyo uwezo wao, ili kusudi waweze kuishi pamoja na watoto wao na kuweza kuwapatia mahitaji yao. Wanao wakati mchache kwa ajili ya kuwafundisha watoto wao nadharia na elimu ya vitendo, wanayo fursa ndogo

ya kuwafunika kwa mivuto ambayo ingeangazia maisha yao. Wanahitaji kutiwa moyo, kuhurumiwa, na kusaidiwa hakika. [MH 203.1; HU Aya ya 11]

Mungu atuita tuwakimu watoto hawa kwa kadiri tuwezavyo, matunzo yanayochukua nafasi ya malezi ya baba. Badala ya kukaa kando, huku ukilalamika juu ya makosa yao, na matatizo ambayo yanaweza kuonekana machoni petu, wasaidie watoto hawa kwa kila njia iwezekanayo. Tafuta jinsi ya kumsaidia mama huyu aliyechoka kwa masumbufu ya ujane. Mpunguzie mama huyu mizigo yake. [MH 203.2; HU Aya ya 12]

Aidha kuna watoto wengi ambao wamekosa kabisa malezi ya wazazi na mvuto wa nyumba ya Kikristo unaosaidia katika utii wa watoto. Hebu Wakristo wafungue mioyo na nyumba zao kwa watoto hawa wasio na msaada. Kazi ambayo Mungu amewakabidhi watu kama wajibu binafsi haipaswi kukabidhiwa kwenye taasisi fulani inayosaidia watu au kuachwa iangukie kwenye hisani za ulimwengu. Ikiwa watoto hawa hawana ndugu au jamaa wanaoweza kuwaangalia, washiriki wa kanisa wawapatie watoto hawa makazi. Yeye aliyetuumba alituamuru tufungamane kindugu, na kwa hivyo maumbile ya mtoto *(kimwili, kiakili na kiroho)* hukuzwa vyema katika mazingira ya upendo kwenye nyumba ya Kikristo. [MH 203.3; HU Aya ya 13]

Wengi ambao hawana watoto wao wenyewe wangeweza kufanya kazi njema katika kutunza watoto wa wengine. Badala ya kutoa umakini wao kwa wanyama wapendwao (paka na mbwa), kuwapenda sana hawa wanyama wasio na uwezo wa kunena (utashi), hebu waelekeze umakini wao kwa hawa watoto wadogo, ambao tabia zao zaweza kufuatana natabia ya Mungu. Wapende washiriki wasio na makazi miongoni mwetu. Angalia ni watoto wangapi kati ya hawa unaoweza kuwalea katika malezi na maonyo ya Bwana. Wengi wamenufaishwa sana kwa kufanya hivi. [MH 203.4; HU Aya ya 14]

Wazee

Wazee pia wanahitaji uangalizi unaonufaisha wa kifamilia. Watu hawa wakiwa katika nyumba za wapendwa katika Kristo wanaweza kufidia hasara ya kupoteza nyumba zao wenyewe kwa ajili ya uzee. Wanapotiwa moyo kushiriki katika masuala na shughuli za familia hiyo, itawasaidia kuhisi kwamba umaana wao haujakoma. Wafanye wazee wahisi kuwa msaada wao unathaminiwa, kwamba bado wana mambo ya kufanya katika kuhudumia wengine, na hili litawachangamsha mioyo yao nao watayapenda tena maisha yao. [MH 204.1; HU Aya ya 15]

Kwa kadiri inavyowezekana wale ambao vichwa vyao vimekuwa vyeupe kwa mvi na hatua za miguu yao kuzidi kupungua waonyesheni kuwa wanaelekea kupumzika usingizi wa mauti, hivyo wabaki miongoni mwa marafiki na watu

wanaowafahamu. Waabudu miongoni mwa wale ambao wamewajua na kuwapenda katika maisha yao. Watunzeni kwa mikono mikarimu na yenye upendo. [MH 204.2; HU Aya ya 16]

Ni fursa ya washiriki wa kila familia kuhudumia jamaa zao wenyewe, pindi inapowezekana kufanya hivyo. Jambo hili lisipowezekana, kazi hii ni ya kanisa, na inapaswa kupokelewa kama fursa na kama jukumu la kanisa. Wote wenye roho ya Kristo watakuwa na huruma kwa wale walio dhaifu na wazee. [MH 204.3; HU Aya ya 17]

Uwepo wa mmoja wa wazee hawa wasiojiweza majumbani mwetu, ni fursa ya thamani ya kushirikiana na Kristo katika huduma Yake ya rehema na kukuza sifa za tabia kama Yake. Upo mbaraka mkubwa kwenye mahusiano kati ya wazee na vijana. Vijana wanaweza kuchangamsha mioyo na maisha ya wazee. Wale ambao maisha yao yanadhoofika wanahitaji kunufaika kwa kuwa karibu na roho ya matumaini na uchangamfu wa vijana. Na vijana kwa upande wao wanaweza kunufaika na hekima na uzoefu wa wazee. Na zaidi ya yote, vijana wanahitaji kujifunza somo la huduma isiyo na ubinafsi. Uwepo wa mtu anayehitaji huruma na uvumilivu na upendo wa kujitoa watakuwa mbaraka wa thamani isiyo na kifani kwenye nyumba nyingi. Kutaburudisha na kustaarabisha maisha ya nyumbani, na kisha kuvuta tabia hizo kama za Kristo za wazee na vijana ambazo zingewafanya wawe na uzuri kama wa Bwana na kuwa matajiri katika hazina ya mbinguni isiyoharibika. [MH 204.4; HU Aya ya 18]

Kipimo Cha Tabia

“Maana sikuzote mnao maskini pamoja nanyi, na kila mpendapo mwaweza kuwatendea mema; lakini Mimi hamnami sikuzote..” "Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa." Marko 14:7; Yakobo 1:27. [MH 205.1; HU Aya ya 19]

Kwa kuwaweka watu wanyonge na masikini miongoni mwetu ili wategemee matunzo kutoka kwetu, Kristo awapima wale wanaodai kuwa wafuasi Wake. Kwa upendo wetu na kuwahudumia watoto Wake wenye mahitaji, twathibitisha ukweli wa upendo wetu Kwake. Kuwapuuza watu hawa ni kujitangaza kwamba sisi tu wanafunzi waongo (bandia), wasiopatana na Kristo na pendo Lake. [MH 205.2; HU Aya ya 20]

Ikiwa yote ambayo yangeweza kufanyika yangeweza kufanywa katika kuwapatia watoto yatima makazi kwenye familia fulani, bado kungekuwa na watoto waliobakia ambao wanahitaji malezi na matunzo. Wengi wa watoto hawa wamerithi uovu kutoka kwa wazazi wao. Wanaonekana wasiofaa,

wasiovutia, waliopotoka, lakini wamenunuliwa kwa damu ya Kristo, na machoni Pake Yeye, watoto hawa ni wa thamani sawa na watoto wetu tuliowazaa wenyewe. Ikiwa mkono wa msaada hautawafikia, basi watakulia katika ujinga na kutumbukia katika uovu na uhalifu. Wengi wa watoto hawa wangeweza kuokolewa kupitia kazi ya nyumba za umma za watoto yatima zinazoendeshwa na serikali au mashirika binafsi.....

Mfano:

Reach Internationaal ya Jasmine na Jacob wa Michigan, ina watoto yatima 26,000 duniani, katika nchi 38, kituo chao cha kwanza kilikuwa kule Rwanda mwaka 1975. Hawa walikuwa wakipenda watoto na kuwiwa kufanya kitu. Tulipoenda nao kule Bunere Majita Tanzania, katika mkakati wa kuanzisha kituo huko Mara Konferensi, waliuliza maswali kadhaa kwa Mchungaji Machage, Makoye, Fue na Kajula. Walipewa ekari 54 kwa ajili ya kilimo na mengineyo. Wakasema kituo kitaitwa Lake Victoria children Village, na watafute baba na mama walezi watakaolea watoto 10 kwenye kila nyumba ili wakae katika mkao wa familia, ndipo wakajenga nyumba hiyo, na shule ya msingi na sekondari yenye masomo ya kawaida na mafunzo ya Biblia). [MH *205.3*; HU Aya ya 21]

Taasisi kama hizo, ili ziwe na ufanisi zaidi katika huduma hii, zinapaswa ziige mpangilio ulivyo wa nyumba ya Kikristo. Badala ya kuwa na miundombinu mikubwa au majumba makubw, na kuongeza idadi kubwa ya watoto pamoja, kuwe na taasisi ndogo-ndogo katika maeneo tofautitofauti. Badala ya kuwa ndani au karibu na mjini, nyumba hizi za kutunza watoto, ziwe mahambani penye ardhi kubwa ambayo itasaidia katika kilimo na kisha watoto hawa wanaweza kukutana kwa ukaribu na uumbaji/asili na kujipatia manufaa ya mafunzo stadi na kuwa hodari katika bidii ya kazi. [MH 205.4; HU Aya ya 22]

Wale wanaosimamia nyumba hizi wanapaswa kuwa wanaume na wanawake wenye mioyo yenye ukarimu, walioelimika na wenye kujitoa kikamilifu; wanaume na wanawake wanaofanya kazi kwa ajili ya upendo wao kwa Kristo na wawafundishao watoto hawa kwa ajili ya Mungu. Chini ya uangalizi huu watoto wengi wasio na makazi na waliotelekezwa wazururao wanaweza

kutayarishwa kuwa washiriki wenye kuinufaisha jamii, na wao wenyewe kumletea Kristo heshima, na hata kwa upande wao kuwasaidia watu wengine wenye mahitaji. [MH 206.1; HU Aya ya 23]

Wengi hudharau mambo yahusuyo uchumi, wakichanganya jambo hili na ubahili na kuishi maisha ya kujibana/kujiminya sana. Lakini kuwa mchumi au mtu anayejali uchumi, kunahusiana sana na ukarimu kwa namna iliyo pana sana. Hakika, usipojali uchumi, yaani ukiwa mtu mfujaji, huwezi kuwa na ukarimu wa kweli. Twapaswa kutunza vitu au mali, ili tuwe na kitu cha kutoa kwa watu. [MH 206.2; HU Aya ya 24]

Hakuna mtu anayeweza kuwa mkarimu kwelikweli, bila kujinyima. Ni kwa kuishi maisha ya unyenyekevu, kujinyima, na kuangalia mambo ya uchumi kwa karibu ndipo tunaweza kutimiza kazi tuliyopewa, kama wawakilishi wa Kristo. Kiburi na tamaa za dunia lazima viondolewe mioyoni mwetu. Kanuni ya kutokuwa na ubinafsi iliyofunuliwa katika maisha ya Kristo inapaswa kudhihirishwa katika kazi zetu zote. Kwenye kuta za nyumba zetu, picha, fanicha na vyombo, hatuna budi kusoma maneno haya, “Walete maskini waliotupwa nje, nyumbani kwako.” Kwenye kabati zetu za nguo twapaswa kuona maneno haya yakiwa yameandikwa, kama kwa kidole cha Mungu, “Wavikeni walio uchi.” Katika chumba cha kulia chakula, juu ya meza iliyosheheni chakula kingi, twapaswa kuona maandishi haya, “Je, siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako?” Isaya 58:7. [MH 206.3; HU Aya ya 25]

Milango elfu moja ya kunufaisha iko wazi mbele yetu. Mara nyingi huwa tunasikitika juu ya rasilimali chache tulizo nazo, lakini kama Wakristo wangelikuwa na bidii, basi wangeweza kuongeza rasilimali zao mara elfu. Ni ubinafsi, kujifurahisha wenyewe, na kujiendekeza ndio hufunga njia ya kuwa watu wa faida au kuwa watu wa kunufaisha wengine. [MH 206.4; HU Aya ya 26]

Ni kiasi kikubwa kiasi gani cha pesa ambacho kinatumiwa kwa ajili ya vitu ambavyo ni sanamu au miungu tu, vitu ambavyo hushughulisha sana akili na muda na nguvu, ambavyo vinapaswa kutumiwa kwa matumizi makuu zaidi! Ni pesa kiasi gani hupotezwa kwa nyumba na samani za bei ghali, kwa ajili ya anasa binafsi, vyakula vya anasa na visivyofaa, na anasa ziumizazo! Ni kiasi gani cha fedha kinachotapanywa kwa ajili ya kununua zawadi ambazo hazimnufaishi mtu yeyote! Kwa mambo ambayo hayana ulazima, na ambayo mara nyingi hudhuru, wale wanaodai kuwa ni Wakristo leo hutumia vingi, na mara nyingi, zaidi kwa ajili yao wenyewe, kuliko ambavyo wanatumia katika kutafuta kuokoa roho kutoka kwa yule mjaribu. [MH 207.1; HU Aya ya 27]

Wengi wanaodai kuwa Wakristo hutumia pesa nyingi sana katika mavazi kiasi kwamba hawabakizi cho chote kwa ajili ya mahitaji ya wengine.

Wanafikiria kuwa ni lazima wawe na mapambo na mavazi ya gharama, bila kujali mahitaji ya wale ambao wanahangaika kujipatia hata mavazi ya kawaida, yenye gharama ndogo, na ambayo ni ya lazima kwa kila mwanadamu. [MH 207.2; HU Aya ya 28]

Dada zangu, kama mngefanya mtindo wenu wa kuvaa upatane na sheria zilizotolewa katika Biblia, mtakuwa na fedha nyingi za kuwasaidia dada zenu maskini zaidi. Siyo tu mtakuwa na fedha, lakini pia muda. Mara nyingi muda ndiyo unahitajika zaidi. Kuna wengi ambao unaweza kuwasaidia kwa mashauri, busara na ujuzi wako. Waonyeshe wengine jinsi ya kuvaa kawaida na bado mavazi yao yawe na mwonekano mzuri. Wanawake wengi hukaa mbali na nyumba ya Mungu kwa sababu mavazi yao ni machakavu, yasiyositiri vizuri yanatofautiana sana na mavazi ya wengine. Watu wengi wenye roho ndogo huweka mioyoni mwao hisia za uchungu kwa ajili ya utofauti huo. Na kwa sababu hiyo wengi huongozwa kutilia shaka uhalisi wa dini na kuifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi ya injili. [MH 207.3; HU Aya ya 29]

Kristo atuagiza, “Kusanyeni vipande vilivyosalia, kisipotee chochote.” Ingawa maelfu wanaangamia kila siku kutokana na njaa, umwagaji damu, moto, na tauni/magonjwa, ni jukumu la kila ajipendaye nafsini mwake kuona kwamba hakuna kitu kinachosazwa na kutupwa, kwamba hakuna kitu kinachotumiwa bila sababu, ambacho kinaweza kumnufaisha mwanadamu mwingine. [MH 207.4; HU Aya ya 30]

Ni makosa kupoteza muda wetu, ni makosa kupoteza mawazo yetu. Twapoteza kila wasaa tunaoutumia ikiwa twajifurahisha wenyewe. Ikiwa kila wakati ungethaminiwa na kutumiwa ipasavyo, lazima kungekuwa na wakati wa kila kitu tunachohitaji kufanya kwa ajili yetu wenyewe au kwaajili ya ulimwengu. Kwenye matumizi ya fedha, katika matumizi ya muda, nguvu, na fursa, kila Mkristo amwangalie Mungu kwa ajili ya mwongozo. “Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; Naye atapewa.” Yakobo 1:5. [MH 208.1; HU Aya ya 31]

“Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa”

“Tendeni mema, na kukopesha msitumaini kupata malipo, na thawabu yenu itakuwa nyingi; nanyi mtakuwa wana wa Aliye juu, kwa kuwa Yeye ni mwema kwa wasiomshukuru, na waovu.” Luka 6:35. [MH 208.2; HU Aya ya 32]

“Afichaye macho yake atakuwa na laana nyingi; bali “Mwenye kuwagawia maskini hatahitaji kitu;.” Mithali 28:27. [MH 208.3; HU Aya ya 33]

“Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.” Luka 6:38. [MH 208.4; HU Aya ya 34]

SURA YA 14

HUDUMA KWA WALIO MATAJIRI

Kornelio, akida wa Kirumi, alikuwa mtu tajiri na mzaliwa kutoka koo iliyoheshimika, yaani familia ya kifahari. Nafasi ya cheo chake ilikuwa ya

kuaminiwa na ya heshima. Mpagani kwa kuzaliwa, akijifunza, na kupata elimu juu ya Mungu kwa njia ya kuwa karibu na Wayahudi akawa amepata kumjua Mungu wa kweli, na kumwabudu, akionyesha uaminifu kwa imani yake kwa kuwaonea huruma maskini. Alitoa “sadaka nyingi (kwa wahitaji), na kumwomba Mungu daima.” Matendo 10:2. [MH 209.1; HU Aya ya 1]

Kornelio hakuwa na maarifa ya injili kama yalivyofunuliwa katika maisha na kifo cha Kristo, na Mungu alituma ujumbe moja kwa moja kwake kutoka mbinguni, na kisha akatuma ujumbe mwingine kwa kumwelekeza mtume Petro kumtembelea Kornelio na kumfundisha. Kornelio hakuwa na ushirika na kanisa la Kiyahudi, na angelitazamwa na marabi kama mpagani na mtu najisi; lakini Mungu alisoma unyenyekevu wa moyo wa Kornelio, na kutuma wajumbe kutoka kwenye kiti Chake cha enzi ili kukutana na mtumishi Wake aliyeko duniani katika mkakati wa kumfundisha injili ofisa huyu wa Rumi. [MH 209.2; HU Aya ya 2]

Ndivyo ilivyo hivi leo Mungu anatafuta roho miongoni mwa tabaka za watu walio juu na walio chini. Wapo wengi kama Kornelio, ambao Bwana atamani kuwaleta katika na kanisa Lake. Huruma na matamanio yao viko kwa watu wa Bwana. Lakini mahusiano ambayo yanawafunga pamoja na ulimwengu huu huwashikilia kwa kuwabana sana. Unahitajika moyo wa uthubutu kwa watu kama hawa kuchukua msimamo wa kushirikiana pamoja na watu wa hali ya chini. Juhudi za pekee zinapaswa kufanywa kwa ajili ya roho hizi ambazo ziko katika hatari kubwa sana kwa sababu ya wajibu na mahusiano waliyo nayo na wenzao kwenye jamii. [MH 209.3; HU Aya ya 3]

Mengi husemwa kuhusu wajibu wetu kwa maskini waliopuuzwa; je, uangalifu fulani hautakiwi pia utolewe kwa kushughulikia matajiri waliopuuzwa? Wengi hulitazama kundi hili kana kwamba halina matumaini, na hufanya sehemu ndogo sana katika kufungua macho ya wale ambao, wakiwa wamepofushwa na kupumbazwa na mvuto wa ufahari wa kilimwengu, wamepoteza hatima tukufu ya milele ambayo hata hawaijali. Maelfu ya matajiri wamekwenda wamelala mauti bila kupata maonyo. Ingawa matajiri hawa waonekana kana kwamba hawajali au kuguswa na kitu, wengi miongoni mwao nafsi zao zimelemewa na mzigo. “Apendaye fedha hatashiba fedha; wala yeye apendaye wingi haongezeki.” Yeye aiambiaye dhahabu safi, “Wewe ndiwe tegemeo langu” ame—“mkana Mungu aliye juu.” “Hakuna hata mmoja wao awezaye kumkomboa ndugu yake, wala kumpa Mungu fidia kwa ajili yake; (Kwa maana ukombozi wa nafsi zao ni wa thamani, nao umekoma milele)” Mhubiri 5:10; Ayubu 31:24, 28; Zaburi 49:7, 8. [MH 210.1; HU Aya ya 4]

Utajiri na heshima vya kidunia haviwezi kukidhi hitaji la roho. Wengi kati ya matajiri watamani uhakikisho fulani kutoka kwa Mungu, tumaini fulani la

kiroho. Wengi watamani kitu kitakachokomesha maisha yao yasiyokuwa na maana (mambo yanayojirudia tena na tena na kukinaisha nafsi). Wengi katika maisha yao maofisini kwenye nyadhifa zao, hujisikia hitaji la kitu ambacho hawana. Ni wachache tu kati yao, ndio huenda kanisani; kwani huhisi kwamba wananufaika kidogo sana wanapokuwa katika nyadhifa zao hizo. Wanaona yote wanayoyasiki huko hayagusi mioyo yao. Je, hatupaswi mmoja mmoja kuwaendea watu hawa na kuwasihi? (waje kwa Mungu) [MH 210.2; HU Aya ya 5]

Miongoni mwa wahanga wa dhambi na mahitaji muhimu ya maisha wapo wale ambao hapo awali walikuwa na mali. Watu wa taaluma na nyadhifa mbalimbali katika maisha wametekwa na machafuko ya ulimwengu, mathalani matumizi ya vileo vikali, kuendekeza tamaa mbaya za mwili, na wakajikuta wameangukia majaribuni. Ingawa watu hawa walioanguka tayari wanahitaji kujaliwa na msaada, je, umakini fulani haupaswi kutolewa kwa wale ambao bado hawajashuka kiasi hiki, kwenye kina cha chini kabisa, lakini ambao miguu yao ipo safarini kuelekea katika njia ile ile? [MH 210.3; HU Aya ya 66]

Maelfu ya walio kwenye nafasi za kuaminiwa nakuheshimiwa wanaendekeza mazoea yanayowaletea uharibifu wa roho na mwili. Watendakazi wa injili, wakuu wa serikali, waandishi, watu wenye mali na talanta, watu wenye uwezo mkubwa wa kibiashara na wenye uwezo unaonufaisha, wako katika hatari ya kufisha kwa sababu hawaoni umuhimu wa kujidhibiti nafsi zao katika mambo yote. Wanapaswa kuelekeza umakini wao kwenye kanuni za kuwa na kiasi (kutawala nafsi), si kiholela, bila ya kutumia utashi, bali katika nuru ya kusudi kuu la Mungu kwa wanadamu. Laiti kanuni halisi za kuwa na kiasi zingeweza kuletwa mbele ya tabaka hili, kuna wengi sana miongoni mwa kundi hili la watu wa hadhi za juu katika jamii, ambao wangetambua thamani yao na kukubaliana na kanuni hizi za kuwa na kiasi mioyoni mwao kwa furaha. [MH 211.1; HU Aya ya 7]

Twapaswa kuwaonyesha watu hawa matokeo ya kuendekeza tamaa za mwili na kujifurahisha na anasa kwamba zinaongoza katika kudhoofisha nguvu za kimwili, kiakili na kimaadili. Wasaidie kutambua wajibu wao kama mawakili wa karama za Mungu. Waonyeshe mema ambayo wangeweza kutenda kupitia pesa ambazo sasa wanazitumia kwa yale ambayo huwadhuru tu. Wasilisha mbele yao kiapo kamili cha kuachana na yote wayendekezayo, ukiwasihi kwamba zile pesa ambazo wangezitumia katika matumizi ya vileo, tumbaku, au yanayohusiana na hayo, vitolewe kwa ajili ya kuwasaidia maskini wagonjwa, kuwaelimisha watoto na vijana kwa manufaa ya ulimwengu. Mwito kama huu ni wachache sana ambao watakataa kuusikiliza na kuutenda. [MH 211.2; HU Aya ya 8]

Kuna hatari nyingine ambayo ndiyo inawakabili zaidi watu matajiri, na hapa pia kuna eneo la kazi kwa ajili ya mmishenari wa kitabibu. Kundi kubwa la watu waliofanikiwa katika ulimwengu, na ambao kamwe hawajihusishi na uhalifu na maovu ya namna yo yote, bado huelekea kwenye uharibifu kwa njia ya kupenda utajiri kuliko Mungu. Kikombe kigumu zaidi kukibeba si kikombe kilicho tupu, bali kikombe kilichojaa hadi pomoni. Ni kikombe hiki ambacho kinahitaji kusawazishwa kwa uangalifu (kubebwa kwa uangalifu ili vilivyomo visimwagike). Taabu na shida hutuhuzunisha mioyo na kutukatisha tamaa; ila ni mafanikio ya mtu (utajiri/umaarufu) ndivyo ambavyo vina hatari zaidi kwa maisha ya kiroho ya mtu. [MH 211.3; HU Aya ya 9]

Wale wanaopitia taabu (kinyume cha hao wenye hadhi ya juu katika jamii) wanawakilishwa na kijiti ambacho Musa alikiona jangwani, ambacho, ingawa kilikuwa kinawaka, hakikuteketea. Malaika wa Bwana alikuwa katikati ya kile kichaka. Kwa hivyo katika kukosa mali au ufukara na dhiki, mng'ao wa uwepo wa Yeye asiyeonekana Uko pamoja nasi kutufariji na kututegemeza. Aghalabu (mara nyingi/kwa kawaida) maombi hutolewa kwa wale watesekao kwa magonjwa au shida; lakini maombi yetu yanahitajika zaidi kwa wale wenye ukwasi wa mali na walio mashuhuri. [MH 212.1; HU Aya ya 10]

Katika bonde la fedheha, mahali ambapo wanadamu huhisi hitaji lao na kumtegemea Mungu kuongoza hatua zao, pana usalama usio kifani (ukilinganisha na ule wakati ambapo mtu anapofanikiwa na mambo yote yanakwenda vizuri). Lakini watu wasimamao, vile ilivyo, kwenye kilele cha ufahari, na ambao, kwa sababu ya nyadhifa zao, watu wanawategemea wawe na hekima nyingi—watu wa namna hii wako katika hatari kubwa zaidi. Wasipomfanya Mungu kuwa mhimili/tegemeo lao, hakika wataanguka. [MH 212.2; HU Aya ya 11]

Biblia haimlaumu mtu ye yote kwa kuwa tajiri, ikiwa amepata utajiri wake kwa njia halali. Sio fedha, bali kupenda fedha, ndio mzizi/chanzo cha uovu wote. Mungu Ndiye awapaye wanadamu uwezo wa kupata mali; na mikononi mwa yule atendaye kama msimamizi na wakili wa Mungu, akitumia mali yake bila ubinafsi, utajiri wake ni mbaraka, kwa yule aliye nao na kwa ulimwengu wote pia. Lakini wengi, wakiwa wamezama kwa kuwekeza katika matamanio ya hazina za ulimwengu huu, wanakuwa na hali ya kutojali matakwa ya Mungu na mahitaji ya wanadamu wenzao. Wanachukulia utajiri wao kama njia ya kujitukuza. Wanaongeza nyumba baada ya nyumba, na mashamba baada ya mashamba; wanazijaza nyumba zao anasa, na huku wawazungukao ni wanadamu walio katika shida, huzuni, uhalifu, magonjwa na kifo. Wale wanaotoa maisha yao kwa kujitumikia na kujifurahisha wenyewe, hawakuzi na

kupalilia ndani yao sifa za Mungu, bali sifa za yule mwovu. [MH 212.3; HU Aya ya 12]

Watu hawa wanahitaji injili. Macho yao yanahitaji kugeuzwa kutoka kwenye ubatili wa vitu vya kimwili ili watazame thamani ya ule utajiri udumuo milele. Wanahitaji kujifunza furaha ya kutoa, ambao ni mbaraka wa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. [MH 213.1; HU Aya ya 13]

Bwana atuagiza, “Waagize matajiri wa dunia hii” wasiutumainie “utajiri wa usio yakini, bali wamtumaini Mungu, atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha; watende mema, wawe matajiri katika matendo mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima wa milele ulio kwelikweli.” 1 Timotheo 6:17-19. [MH 213.2; HU Aya ya 14]

Watu matajiri, wapendao ulimwengu, na kuuabudu wanaweza kuvutwa kwa Kristo, sio kwa mguso wa kawaida, ule wa kumgusa mtu kwa bahati nasibu. Watu hawa aghalabu ndio wagumu zaidi kuwafikia. Juhudi binafsi lazima zitolewe kwa ajili yao na wanaume na wanawake waliojaa moyo wa umishenari, wale ambao hawatashindwa au kuvunjika moyo. [MH 213.3; HU Aya ya 15]

Wapo watu wenye sifa stahiki za kufanya kazi kwa makundi ya watu wenye hadhi za juu. Wanapaswa kutafuta hekima kutoka kwa Mungu ili wajue jinsi ya kuwafikia watu hawa, sio kwa kuwakaribia kwa mazoea dhaifu, bali kupitia juhudi binafsi na imani iliyo hai ili kuwaamsha na kuwafanya watambue mahitaji ya mioyo yao, kuwaongoza kwenye ujuzi wa ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu. [MH 213.4; HU Aya ya 16]

Wengi wanadhani kwamba ili kufikia madaraja ya watu walio juu kimaisha, njia na mbinu fulani ambayo itawafaa lazima ifuatwe. Wanafikiri ni muhimu kwao kwamba ili kuwafikia watu wa tabaka hili, inawabidi wawe na mwonekano wa kitajiri, majumba na mavazi ya gharama, vifaa vya aina ya pekee katika kuwafikia, mazingira ya kitajiri, waendane sambamba na mazoea yao, usasa, mtindo wao wa maisha, ufasaha na utanashati. Hili ni kosa. Njia ya kidunia sio njia ya Mungu ya kufikia matabaka ya juu. Kile kitakachowafikia kwa ufanisi ni uwasilishaji thabiti, usio na ubinafsi wa injili ya Kristo. [MH 213.5; HU Aya ya 17]

Uzoefu wa mtume Paulo alipokutana na wanafalsafa wa Athene una fundisho kwetu. Katika kuitangaza injili mbele ya mahakama ya Areopago, Paulo alikutana na mantiki kwa mantiki, sayansi kwa sayansi, falsafa kwa falsafa. Hadhira (wale waliokuwa wakimsikiliza) ya wale wenye hekima ilitekewa kwa mshangao na kunyamazishwa. Maneno yake yasingeweza

kukabiliwa. Lakini juhudi hizo zilizaa matunda kidogo tu. Ni wachache tu walioongozwa kuikubali injili. Tangu hapo Paulo alitumia mbinu tofauti ya kazi. Aliepuka mabishano ya kina na majadiliano ya nadharia (midahalo), na kwa unyenyekevu aliwaelekeza waume na wake kwa Kristo kama Mwokozi wa wenye dhambi. Akiwaandikia Wakorintho kazi yake kati yao, alisema: [MH 214.1; HU Aya ya 18]

"Ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala wa hekima. Kwa maana naliazimu nisijue neno lolote kwenu, ila Yesu Kristo, Naye alimesulibiwa.... Maneno yangu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu, ili imani yenu isipate kuwa katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu." 1 Wakorintho 2:1-5. [MH 214.2; HU Aya ya 19]

Na tena, katika barua yake kwa Warumi, anasema: [MH 215.1; HU Aya ya 20]

"Kwa maana Siionei haya Injili; kwa maana ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye; kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia." Warumi 1:16. [MH 215.2; HU Aya ya 21]

Wale wanaofanya kazi kwa watu walio katika tabaka la juu wabebe hadhi halisi, wakikumbuka kuwa malaika huambatana nao. Na waitunze hazina ya akili na moyo na ijazwe na, "Imeandikwa." Hifadhi maneno adhimu ya Kristo kwenye akili yawe kumbukumbu. Hayana budi kuthaminiwa kuliko dhahabu au fedha. [MH 215.3; HU Aya ya 22]

Kristo amesema ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. Katika kufanya kazi kwenye kundi hili kuna mambo mengi ambayo yatamvunja moyo mhubiri, mafunuo mengi ya kuhuzunisha moyo yatatolewa. Lakini yote yawezekana kwa Mungu. Yeye aweza, na atatenda kazi kupitia wakala wa kibinadamu juu ya mawazo ya watu ambao maisha yao yamejitoa kikamilifu kwenye kusumbukia pesa. [MH 215.4; HU Aya ya 23]

Kuna miujiza ya kutendwa katika wongofu wa kweli, miujiza ambayo kwa sasa haitambuliki. Watu wakuu zaidi duniani hawako nje ya uwezo wa ajabu wa utendaji wa Mungu wetu. Ikiwa wale ambao ni watenda kazi pamoja Naye watafanya wajibu wao kwa ushujaa na uaminifu, Mungu atawaongoa watu wenye nafasi za uwajibikaji, watu wenye umahiri wa akili na mashuhuri. Kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, wengi wataongozwa kuzikubali kanuni za Mungu. [MH 216.1; HU Aya ya 24]

Inapowekwa wazi kwa watu hawa kwamba Bwana anatazamia kutoka kwao kama wawakilishi Wake kuwapoza watesekao, wengi wataitikia wito huo, na watatoa mali zao na huruma kwa ajili ya kuwanufaisha wale walio maskini. Vile mawazo yao yanapovutwa mbali na maslahi yao yenye ubinafsi, wengi watajisalimisha wenyewe kwa Kristo. Wakiwa na talanta zao za umashuhuri na mali, watajiunga kwa furaha katika kazi ya rehema pamoja na mmishenari mnyenyekevu ambaye alikuwa wakala wa Mungu katika wongofu wao. Kwa kutumia vyema hazina zao za duniani watakuwa wamejiwekea “hazina isiyopungua mbinguni, mahali ambapo mwivi hakaribii, wala nondo haharibu.” [MH 216.2; HU Aya ya 25]

Wajapoongoka na kuwa upande wa Kristo, wengi wa watu hawa watakuwa mawakala katika mkono wa Mungu kufanya kazi kwa ajili ya wengine wa tabaka lao. Watajisikia kwamba kipindi hiki cha injili kimetolewa kwao kwa ajili ya wale ambao wamefanya ulimewngu huu kuwa tumaini na kila kitu kwao. Wakati na pesa vitawekwa wakfu kwa Mungu, talanta na umashuhuri vitatolewa kwa kazi ya kuzileta roho kwa Kristo. [MH 216.3; HU Aya ya 26]

Ni maisha ya milele tu ndiyo pekee yatakayofunua kile ambacho kimekamilishwa kwa huduma ya namna hii—ni roho ngapi, zinazougua mashaka na ambazo zimechoshwa na mambo ya dunia na machafuko, zimeletwa kwa Mrejeshaji mkuu, ambaye hutamani kuwaokoa kabisa wote wanaomjia. Kristo ni Mwokozi aliyefufuka, na kuna uponyaji katika mbawa Zake. [MH 216.4; HU Aya ya 27]

SEHEMU YA 4—UANGALIZI WA WAGONJWA

“Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.”

SURA YA 15

KATIKA CHUMBA CHA WAGONJWA

Wale wanaohudumia wagonjwa ni sharti waelewe umuhimu wa kuzingatia kwa umakini sheria za afya. Hakuna mahali ambapo utii wa sheria hizi ni wa muhimu zaidi kama kwenye chumba cha mgonjwa. Hakuna mahali po pote kama hapa ambapo mambo mengi sana hutegemea uaminifu wa wahudumu katika mambo madogo-madogo. Ugonjwa ujapofikia katika hali mbaya (mithili ya kuwa mahututi), uzembe mdogo, kupuuzia kidogo tu mahitaji maalum au hatari ya mgonjwa, kumwonyesha hofu mgonjwa, msisimko au maudhi, au hata kukosa huruma, vyaweza kugeuza mizani ambayo inaamua uhai na kifo cha mtu anayeugua, na kusababisha mauti ambapo vinginevyo angepona. [MH 219.1; HU Aya ya 1]

Ufanisi wa muuguzi kwa kiwango kikubwa hutegemea nguvu zake za kimwili. Kadiri afya yake ilivyo bora, ndivyo atakavyoweza kuvumilia usumbufu wa kuwahudumia wagonjwa, na ndivyo anavyoweza kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio zaidi. Wale wanaofanya uangalizi wa wagonjwa wanapaswa kuzingatia mlo, usafi, hewa safi, na mazoezi. Mambo hayo hayo wakiyazingatia wanafamilia wa mgonjwa kutawawezesha kustahimili mizigo ya ziada inayoletwa juu yao, na itasaidia kuwaepusha na magonjwa. [MH 219.2; HU Aya ya 2]

Pale ambapo ugonjwa umefikia hatua mbaya sana, ukihitaji huduma ya muuguzi usiku na mchana, kazi hii igawanwe na angalau wauguzi wawili mahiri, ili kwamba kila mmoja apate fursa ya kupumzika na kufanya mazoezi katika mahali pa wazi. Jambo hili ni muhimu hasa katika mazingira ambayo ni vigumu kupata hewa safi katika chumba cha wagonjwa. Kwa kutotambua umuhimu wa hewa safi, sehemu ipitishayo hewa wakati mwingine huzuiwa kwa kutokuwa na madirisha au matundu ya kuingiza hewa toka nje, na maisha ya mgonjwa na mhudumu aghalabu huwa hatarini. [MH 220.1; HU Aya ya 3]

Tahadhari zinazofaa zikizingatiwa, magonjwa yasiyoambukiza hayatoathiri wengine. Mazoea yawe sahihi, na kwa usafi na kuruhusu sehemu za jengo kupitisha hewa, chumba cha wagonjwa kiwekwe mbali na vitu vinavyoweza kuwa na athari kiafya. Kwa mazingira na hali kama hivyo, kuna uwezekano mkubwa zaidi wa mgonjwa kupona, na mara nyingi si wahudumu wa mgonjwa

wala wanafamilia watakaoambukizwa na ugonjwa huo. [MH 220.2; HU Aya ya 4]

Mwanga Wa Jua, Kuruhusu Hewa, Na Jotoridi

Ili kumweka mgonjwa katika mazingira mazuri zaidi ya kupona, chumba anachoishi kinapaswa kuwa kikubwa, chenye mwanga wa jua, kinachochangamsha, pamoja na uwepo wa sehemu zinazoruhusu hewa ya kutosha. Kile chumba ndani ya nyumba ambacho kinakidhi vigezo hivi vyema ndio kinapaswa kutengwa kama chumba cha wagonjwa. Nyumba nyingi hazina sehemu zenye kupitisha hewa ya kutosha, na kukifanya kifae inakuwa vigumu; lakini kila jitihada iwezekanayo na ifanywe katika kukipanga chumba cha wagonjwa kwa namna ambayo hewa safi itaweza kuingia, usiku na mchana. [MH 220.3; HU Aya ya 5]

Kwa kadiri inavyowezekana urari wa joto katika chumba cha mgonjwa usibadilike-badilike. Kipima joto kitumiwe kuhakikisha joto ni lile lifaalo. Wale wanaomtunza wagonjwa, ambao aghalabu hunyimwa usingizi au kuamshwa usiku ili kumhudumia mgonjwa, wana uwezekano wa kuhisi baridi kali mwilini na wasiweze kuwa waamuzi wazuri wa hali ya jotoridi ifaayo. [MH 221.1; HU Aya ya 6]

Lishe

Sehemu muhimu ya jukumu la muuguzi ni umakini wa lishe ya mgonjwa. Mgonjwa asiruhusiwe kuteseka au kudhoofika kwa kukosa lishe, wala uwezo wa mfumo wake wa mmeng'enyo haupaswi kulemewa kwa ajili ya chakula kingi au kile ambacho ni vigumu kumeng’enywa kwa urahisi. Uangalifu unapaswa kuchukuliwa ili kutayarisha na kumtengea mgonjwa chakula ambacho kitakuwa kitamu, lakini uamuzi wa busara zaidi utumike katika kukitumia kulingana na mahitaji ya mgonjwa, kwa wingi na ubora wake. Katika nyakati za mgonjwa kupona, wakati hamu ya kula inaanza kurudi kwa nguvu, kabla viungo vya umeng’enyaji chakula havijaimarika, kuna hatari kubwa ya kujeruhi mwili kutokana na makosa katika lishe. [MH 221.2; HU Aya ya 7]

Wajibu wa Wauguzi

Wauguzi, na wote wanaohusika na chumba cha mgonjwa, wanapaswa kuwa wachangamfu, watulivu, na wenye uwezo wa kudhibiti hisia zao. Mambo ya kuwa na haraka-haraka, msisimko, au machafuko yo yote, viepukwe. Milango inapaswa kufunguliwa na kufungwa kwa uangalifu, na nyumba nzima iwe katika ukimya na utulivu. Katika hali ya homa (yaani joto linapopanda juu), uangalizi maalum wahitajika wakati shida inapotokea na kisha homa kuondoka.

Hivyo ni muhimu kuwa na uangalizi daima. Ukosefu wa elimu, usahaulifu, na uzembe vimesababisha vifo vya wengi ambao wangeishi kama wangeangaliwa ifaavyo kutoka kwa wauguzi wenye hekima na wenye mawazo bora. [MH 221.3; HU Aya ya 8]

Kuwatembelea Wagonjwa

Ni wema usioratibiwa vyema, wazo baya la uungwana, kwa watu kumtembelea mgonjwa mara kwa mara isivyokuwa na kiasi. Wale ambao ni wagonjwa sana hawapaswi kutembelewa sana. Taharuki huja pale mgonjwa anapokuwa akisemeshwa mara nyingi na humchosha hali ya kuwa yu katika uhitaji mkubwa wa utulivu, pumziko tulivu. [MH 222.1; HU Aya ya 9]

Kwa mgonjwa aliyepata ahueni au anayeugua ugonjwa wa muda mrefu, na ambaye anaendelea kupata matibabu, mara nyingi hufurahi na kunufaika wakati mtu anapokuja kumtembelea na kuona kwamba anakumbukwa; lakini uhakikisho huu ukitolewa kwa jumbe zenye kumhurumia au kwa zawadi ndogo aghalabu hufanya kusudi bora, lisilosababisha badiliko baya kwa afya ya mgonjwa kuliko ziara tu za watu binafsi. [MH 222.2; HU Aya ya 10]

Uuguzi katika Taasisi

Katika hospitali na vituo vya afya vinavyowapa wagonjwa tiba, chakula maalum na mazoezi, mahali ambapo aghalabu wauguzi huhudumia idadi kubwa ya wagonjwa, yahitajika jitihada yenye kudhamiria kuwepo daima, ikiambatana na moyo wa kirafiki, uchangamfu, na kuonyesha unajali watu kikamilifu katika kila neno na tendo (ili usiwachukize, uwe mwangalifu kuhusiana na kile mgonjwa anataka, anahisi au kuhitaji). Katika taasisi hizi ni muhimu sana kwamba wauguzi wajitahidi kufanya kazi zao kwa busara na vyema. Daima wanahitaji kukumbuka kwamba katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku, wanamtumikia Kristo, ambaye ni Bwana. [MH 222.3; HU Aya ya 11]

Maneno yenye hekima yanahitaji kuzungumzwa kwa wagonjwa. Wauguzi wanapaswa kujifunza Biblia kila siku, ili waweze kuzungumza maneno yatakayowaangazia na kuwasaidia wagonjwa. Malaika wa Mungu huwa katika vyumba ambamo watesekao hawa wanahudumiwa, na mazingira yanayomzunguka yule mtu anayetoa matibabu inapaswa kuwa safi na yenye kupendeza. Matabibu na wauguzi hawana budi kuzithamini na kuzitenda kanuni za Kristo. Katika maisha yao wema Wake wapaswa uonekane kwa macho. Ndipo, kwa kile wanachotenda na kusema, watawavuta wagonjwa kwa Mwokozi. [MH 223.1; HU Aya ya 12]

Muuguzi wa Kikristo anapokuwa akitoa tiba kwa ajili ya uponyaji, atafanikiwa kuivuta akili ya mgonjwa kwa Kristo, ambaye Ndiye Mponyaji wa roho na mwili. Nasaha za hapa na pale zitakuwa na matokeo mema. Wauguzi wenye umri mkubwa hawapaswi kupoteza fursa yo yote ifaayo ya kuwaelekeza wagonjwa kwa Kristo. Wanapaswa kuwa tayari kila wakati kuhusianisha uponyaji wa kiroho na uponyaji wa kimwili. [MH 223.2; HU Aya ya 13]

Kwa namna ya ukarimu na upole wauguzi hawana budi kufundisha kwamba yeye ambaye ataponywa kikamilifu ni sharti aache kuivunja sheria ya Mungu. Ni sharti aache maisha ya dhambi. Mungu hawezi kumbariki yule anayeendelea kujiletea magonjwa na mateso kwa kuvunja kwa makusudi sheria za mbinguni. Lakini Kristo, kwa njia ya Roho Mtakatifu, huja kama nguvu ya uponyaji kwa wale wanaoacha kufanya maovu na kujifunza kutenda mema. [MH 224.1; HU Aya ya 14]

Wale ambao hawampendi Mungu, daima watakuwa wanafanya kazi dhidi ya mahitaji ya roho na mwili. Lakini wale walio chonjo kuhusiana na umuhimu wa kuishi kwa kumtii Mungu katika ulimwengu huu wa sasa ulio mwovu watakuwa tayari kujitenga na kila tabia mbaya. Shukrani na upendo vitajaza mioyo yao. Wanajua kwamba Kristo ni rafiki yao. Katika hali mbalimbali watakuwa wakitambua kwamba kuwa na Rafiki kama huyo kunamaanisha mengi zaidi katika safari ya kupona kwa wale wanaoteseka na ugonjwa kuliko tiba iliyo bora zaidi inayoweza kutolewa kwenye hospitali hizo walizoajiriwa. Lakini mistari yote miwili ya utumishi ni muhimu. Inapaswa kwenda sambamba, ikishikana mkono. [MH 224.2; HU Aya ya 15]

SURA YA 16

MAOMBI KWA AJILI YA WAGONJWA

Maandiko yasema kwamba “imewapasa wanadamu kumwomba Mungu siku zote, na wala wasikate tamaa” (Luka 18:1); na kama kuna wakati ambapo wanahisi hitaji lao la kuomba, ni pale nguvu zinaposhindwa, na maisha yenyewe yanaonekana kushindwa. Mara nyingi watu walio na afya kamili husahau rehema za ajabu zilizodumu maishani mwao siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, na hawampi Mungu shukrani zo zote kwa mema yote ambayo Yeye huwatunukia. Lakini magonjwa yanapokuja, hapo ndipo Mungu anakumbukwa. Nguvu za kibinadamu zinapopungua, watu huhisi hitaji lao la msaada wa Mungu. Na Mungu wetu Mwenye rehema kamwe haipuuzi nafsi inayomtafuta Yeye kwa dhati kwa ajili ya msaada Wake. Ndiye kimbilio letu katika magonjwa kama ilivyo katika kuwa wazima. [MH 225.1; HU Aya ya 1]

“Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao. Maana Yeye anatujua umbo letu; Anakumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi.” Zaburi 103:13, 14. [MH 225.2; HU Aya ya 2]

“Kwa sababu ya makosa yao,

Na kwa sababu ya maovu yao, [wanadamu] wanateswa.

Nafsi zao huchukia kila aina ya chakula;

Nao wanaikaribia malango ya mauti.” Zaburi 107:17, 18, [MH 225.3; HU Aya ya 3]

“Ndipo wakamlilia Bwana katika dhiki zao,

Naye huwaponya na shida zao.

Hulituma Neno Lake, na kuwaponya,

na kuwatoa katika maangamizo yao.” Mistari ya 19, 20, RV [MH 225.4; HU Aya ya 4]

Mungu Yu tayari sasa kuwarudisha tena wagonjwa katika hali ya afya kama wakati Roho Mtakatifu aliposema Maneno haya kupitia mwandishi wa Zaburi. Na Kristo Ndiye tabibu Yule Yule Mwenye huruma sasa kama alivyokuwa wakati wa huduma Yake hapa duniani. Ndani Yake mna tiba/zeri ya uponyaji kwa kila ugonjwa, na akirejesha nguvu kwa kila udhaifu. Wanafunzi Wake katika wakati huu hawana budi kuwaombea wagonjwa kwa hakika kama vile wanafunzi wa kale walivyoomba. Na kupona kutafuata; kwa maana "kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa." Tuna nguvu za Roho Mtakatifu, uhakikisho mtulivu wa imani, uwezao kudai ahadi za Mungu. Ahadi ya Bwana isemayo, "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya" (Marko 16:18), ni yenye kutegemewa sasa kama ilivyokuwa katika siku za mitume. Ahadi hii huonyesha vizuri fursa ya watoto wa Mungu, na imani yetu inapaswa kushikilia yale yote ambayo ahadi hii inayakumbatia. Watumishi wa Kristo ni njia ya kazi Yake, na kupitia kwao atamani kutumia uweza Wake wa uponyaji. Ni kazi yetu kuwaelekeza wagonjwa na wale watesekao kwa Mungu katika mikono ya imani yetu. Twapaswa kuwafundisha kumwamini Yule Mponyaji Mkuu. [MH 226.1; HU Aya ya 5]

Mwokozi angetaka tuwatie moyo wagonjwa, wasio na tumaini, watesekao, kushikilia nguvu Zake. Kupitia imani na maombi chumba cha wagonjwa kinaweza kugeuzwa kuwa Betheli, yaani nyumba ya Mungu. Kwa maneno na matendo, matabibu na wauguzi wanaweza kusema, kwa uwazi sana kiasi kwamba haiwezi kabisa kueleweka vibaya, "Mungu Yuko mahali hapa" kuokoa, na sio kuharibu. Kristo atamani kuonyesha uwepo Wake katika chumba hiki cha wagonjwa, akijaza mioyo ya madaktari na wauguzi uzuri wa pendo Lake. Ikiwa maisha ya wauguzi kwa wagonjwa ni ya namna ambayo Kristo anaweza kwenda pamoja nao mpaka kando ya kitanda cha mgonjwa, kutamjia usadikisho kwamba kwamba Mwokozi Mwenye huruma Yuko pale, na usadikisho huu wenyewe utafanya mengi kwa ajili ya uponyaji wa yote mawili, roho na mwili. [MH 226.2; HU Aya ya 6]

Na Mungu husikia maombi. Kristo alisema, "Mkiniomba neno lo lote kwa Jina Langu, nitalifanya. Tena asema, "Mtu akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu." Yohana 14:14; 12:26. Ikiwa tunaishi kulingana na Neno Lake, kila ahadi ya thamani ambayo Yeye ameitoa, itatimizwa kwetu. Sisi hatustahili rehema Zake, lakini pale tunapojitoa Kwake, Yeye hutupokea. Atafanya kazi kwa ajili na kupitia kwa wale wote wanaomfuata. [MH 226.3; HU Aya ya 7]

Lakini ni pale tu tunapoishi kwa kulitii Neno Lake ndipo twaweza kudai utimilifu wa ahadi Zake. Mwandishi wa Zaburi asema, "Kama nafikiri maovu moyoni mwangu, Bwana hatanisikia." Zaburi 66:18. Ikiwa twamtii Mungu kwa

sehemu tu, na kwa moyo nusu-nusu, basi ahadi Zake hazitatimizwa kwetu. [MH 227.1; HU Aya ya 8]

Katika Neno la Mungu tunayo maagizo kuhusiana na maombi maalum kwa ajili ya kuponywa kwa wagonjwa. Lakini kuomba ombi kama hilo ni tendo tukufu mno, na halipaswi kutekelezwa bila ya kuzingatia kwa umakini. Katika matukio mengi ya maombi kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa, kile ambacho kinaitwa imani na wanadamu si kitu zaidi ya ufidhuli

(Msisitizo: ni kudhania au kuomba jambo fulani ambalo Mungu bado hajatupa kibali, na bado tukafiriki kwamba Mungu anawajibika tu kutuunga mkono katika safari yetu ya ombi hilo, ni ombi lenye kiburi cha namna fulani, huitwa imani bandia, imani ya kudhania. Hii inatenganishwa na mstari ambao hauonekani vizuri na imani ya Kweli, zote mbili zinaanza na ahadi za Mungu, kama jaribu la pili la Yesu, "Jitupe," kwa ahadi hii Yesu alirudisha amri ya Shetani kwa kusema, "imeandikwa usimjaribu Mungu Wako, maana imeandikwa." Imani ya kweli inatupa hekima ya kutii mapenzi ya Mungu, imani bandia au feki inatoa visingizio vya kutotii amri ya Mungu, dhambi ya kudhania umetenda wema, kama Sauli kwa kutoangamiza Waamaleki, au Uza kushika sanduku alipoona viongozi hawajatelekeza yale yaliyotakiwa, naye akahalalisha ubaya wa wengine kwa kufanya uovu wake—ni maombi mtu anaomba bila kufanya sehemu yake kama mwanadamu kwa kutumia maji, kuacha kileo katika uponyaji, na bado akafikiri lazima tu Mungu aidhinishe kile mtu anataka). [MH *227.2*; HU Aya ya 9]

Watu wengi hujiletea magonjwa kwa kujiendekeza na kujifurahisha kwao wenyewe. Hawaishi kwa mujibu wa sheria ya asili au kanuni za ukamilifu wa afya. Wengine wamepuuza sheria za afya katika mitindo yao ya ulaji na unywaji, uvaaji, au kujishughulisha. Aghalabu aina fulani ya uovu ndiyo sababu ya kudhoofika kwa akili au mwili. Ikiwa watu hao wangepata baraka ya uzima, wengi wao wangeendelea na mwenendo wao wa kutojali na uvunjaji wa sheria za asili na za kiroho za Mungu, wakifikiri kwamba ikiwa Mungu huwaponya kwa kujibu sala, basi wako huru kuendelea na mazoea yao

yasiyofaa na kuendekeza tamaa za mwili bila kuwa na mipaka. Endapo ikatokea kwamba Mungu anamfanyia mtu huyu muujiza wa kumrejeshea afya yake, Angekuwa anaihamasisha dhambi iendelee. [MH 227.3; HU Aya ya 10]

Ni kazi bure kuwafundisha watu kumtazama Mungu kama mponyaji wa udhaifu wao, mpaka wafundishwe kuacha mazoea yasiyofaa. Ili kupokea baraka Zake katika jibu la maombi, ni sharti waache kutenda maovu na kujifunza kutenda mema. Mazingira yao lazima yawe masafi, mienendo yao maishani iwe sahihi. Ni sharti waishi kwa kupatana na sheria ya Mungu, ya asili na ya kiroho. [MH 227.4; HU Aya ya 11]

Kuungama Dhambi

Kwa wale wanaotamani maombi kwa ajili ya kurejeshewa afya, inapaswa wafahamishwe wazi kwamba uvunjaji wa sheria ya Mungu, iwe ya asili au ya kiroho, ni dhambi, na kwamba ili wao wapate baraka Zake, dhambi lazima iungamwe na kuachwa. [MH 228.1; HU Aya ya 12]

Maandiko yatuagiza hivi: “Ungamianeni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Yakobo 5:16. Kwa yule aombaye, mawazo kama haya yatolewe kwake: “Hatuwezi kuusoma moyo, wala kujua siri za maisha yako. Haya yanajulikana kwako tu na kwa Mungu. Ukitubu dhambi zako, ni wajibu wako kuziungama.” Dhambi ya mtu ya siri inapaswa kuungamwa kwa Kristo, mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu. Kwa maana “mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki.” 1 Yohana 2:1. Kila dhambi ni kosa dhidi ya Mungu na inapaswa kuungamwa Kwake kupitia Kristo. Kila dhambi ambayo imetendwa wazi inapaswa kuungamwa waziwazi. Kosa alilotenda kwa mwenzake linapaswa kungamwa kwa yule aliyekosewa. Ikiwa wapo watafutao kuwa wazima wamekuwa na hatia ya kunena maovu, ikiwa wamepanda mafarakano nyumbani, kwenye ujirani, au kanisani, na kuchochea watu kutengana na mafarakano, ikiwa kwa kitendo cho chote kibaya wamewaingiza wengine katika dhambi, mambo hayo yanapaswa kuungamwa mbele za Mungu na mbele ya wale ambao wametendwa makosa. “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki na atatusamehe dhambi zetu, na kututakasa na uovu wote.” 1 Yohana 1:9. [MH 228.2; HU Aya ya 13]

Pale makosa yanaposahihishwa, twaweza kupeleka mahitaji ya wagonjwa kwa Bwana kwa imani tulivu, kama vile Roho Wake anavyoweza kuonyesha. Amjua kila mtu kwa jina, na amjali kila mmoja kana kwamba hapana mtu mwingine duniani ambaye kwa ajili yake Baba alimtoa Mwanawe mpendwa. Kwa kuwa upendo wa Mungu ni mkuu sana na haushindwi, wagonjwa wanapaswa kuhimizwa kumtumaini Yeye na kuwa wachangamfu. Kuwa na

tashwishwi juu yao wenyewe huelekea kusababisha udhaifu na magonjwa. Ikiwa watainuka juu ya sonona na huzuni, matarajio yao ya kupona yatakuwa bora; kwa maana “Jicho la Bwana li juu yao” “wanaotumainia fadhili Zake.” Zaburi 33:18. [MH 229.1; HU Aya ya 14]

Katika kuwaombea wagonjwa ikumbukwe kwamba “Kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo.” Warumi 8:26. Hatujui ikiwa mbaraka tunaotamani utafaa au la. Hivyo maombi yetu yanapaswa kujumuisha wazo hili: “Bwana, Wewe wajua kila siri ya nafsi. Unawafahamu watu hawa. Yesu, Wewe uliye Mtetezi wao, ulitoa maisha Yako kwa ajili yao. Upendo Wako kwao ni mkuu kuliko wetu unavyoweza kuwa. Kwa hivyo, ikiwa ni kwa ajili ya utukufu wako na nia njema ya watesekao, twaomba, katika Jina la Yesu, ili waweze kurejeshwa kwenye afya njema. Ikiwa si mapenzi Yako warejeshwe, twaomba neema Yako iwafariji na uwepo Wako uwe nao katika kuteseka kwao.” [MH 229.2; HU Aya ya 15]

Mungu ajua mwisho tangu mwanzo. Aijua mioyo ya watu wote. Husoma kila siri ya roho. Ajua ikiwa wale wanaoombewa wanaweza au hawawezi kustahimili majaribu ambayo yangeliwapata ikiwa wangelidumu kuishi. Ajua kama maisha yao yatakuwa baraka au laana kwao wenyewe na kwa ulimwengu. Hii ndiyo sababu moja kwa nini, tunapowasilisha maombi yetu kwa dhati, twapaswa kusema, “Walakini si mapenzi yangu, bali Yako yafanyike.” Luka 22:42. Yesu aliongeza maneno haya ya kujisalimisha kwenye hekima na mapenzi ya Mungu alipokuwa katika bustani ya Gethsemane aliposihi, “Ee Baba Yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke.” Mathayo 26:39. Na kama haya maneno yalikuwa ya kufaa Kwake Yeye, ambaye ni Mwana wa Mungu, ni zaidi kiasi gani yatakuwa ya kufaa kwenye midomo yetu sisi wanadamu wakosefu na wenye ukomo! [MH 230.1; HU Aya ya 16]

Njia ya kudumu ni kuweka matamanio yetu kwa Baba yetu wa mbinguni Mwenye hekima yote, na kisha, kwa ujasiri na imani kamili, kuweka Yote Kwake na kumtumaini Yeye. Twajua kwamba Mungu hutusikia tukiomba sawasawa na mapenzi Yake. Lakini kushinikiza maombi yetu bila roho ya kujisalimisha si sahihi; maombi yetu lazima yawe yenye roho ya maombezi na siyo kumwamrisha Mungu. [MH 230.2; HU Aya ya 17]

Yapo mambo ambayo Mungu huyatenda bila kipingamizi kwa uweza Wake mkuu katika kuponya. Lakini si wagonjwa wote huponywa. Wengi huwaruhusu kulala usingizi wa mauti katika Yesu. Yohana kwenye Kisiwa cha Patmo aliagizwa kuandika: “Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa; naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao, kwa kuwa matendo yao yafuatana nao.” Ufunuo 14:13. Kutokana na fungu hili twaona kwamba ikiwa watu hawaponywi na kurejea tena kwenye hali ya afya njema, wale

waliokuwa wakimwombea mgonjwa hawapaswi kuchukuliwa kuwa wamepungukiwa na imani. [MH 230.3; HU Aya ya 18]

Sote twatamani majibu mujarabu (ya haraka) na ya moja kwa moja kwa maombi yetu, na twajaribiwa kukata tamaa pale jibu linapochelewa au kuja kwa namna ambayo hatukutazamia. Lakini Mungu ni Mwenye hekima sana, na ni mwema sana kujibu maombi yetu daima kwa wakati tunaotaka na kwa jinsi tunavyotamani yajibiwe. Yeye Atafanya mengi na bora zaidi kwa ajili yetu kuliko tu kutimiza matakwa yetu yote. Na kwa sababu twaweza kutumaini hekima na upendo Wake, hatupaswi kumwomba akubali mapenzi yetu, bali twapaswa kutafuta kuingia katika kusudi Lake na kulitimiza hilo. Matamanio na maslahi yetu yapaswa kupotelea ndani ya mapenzi Yake. Uzoefu mbalimbali namna hii ujaribuo imani yetu, ni kwa manufaa yetu. Kwa udhoefu huo hudhihirika ikiwa imani yetu ni ya kweli na ya dhati, iegemeayo kwenye neno la Mungu pekee, au itegemeayo hali, haina uhakika na yenye uwezekano wa kubadilika. Imani huimarishwa na mazoezi. Sharti turuhusu subira iwe na kazi yake kamilifu, tukikumbuka kwamba kuna ahadi za thamani katika Maandiko kwa wale wamngojeao Bwana. [MH 230.4; HU Aya ya 19]

Si wote wanaoelewa kanuni hizi. Wengi watafutao rehema ya Bwana ya uponyaji hufikiri kwamba lazima wapate jibu la moja kwa moja na la haraka kwa maombi yao au imani yao ina kasoro fulani. Kwa sababu hii, wale waliodhoofishwa na magonjwa wanahitaji kushauriwa kwa hekima, ili watende kwa busara. Hawapaswi kupuuza wajibu wao kwa marafiki ambao wanaweza kuwaacha wanapokufa, au kupuuza kutumia tiba za asili kwa ajili ya kurejesha afya. [MH 231.1; HU Aya ya 20]

Mara nyingi kuna hatari ya kukosea hapa. Wakiamini kwamba wataponywa kama jibu la sala yao, wengine huogopa kufanya jambo lo lote ambalo huenda likaonekana kana kwamba wana ukosefu wa imani. Lakini wasipuuze kuweka mambo yao sawa kama vile ambavyo wangetamani kufanya wakati ambapo wangetarajia kulala usingizi wa mauti. Wala hawapaswi kuogopa kusema maneno ya kutia moyo au nasaha ambayo wakati wa kuagana wangetaka kunena kwa wapendwa wao. [MH 231.2; HU Aya ya 21]

Wale watafutao uponyaji kwa maombi wasipuuze kutumia tiba ambazo zimo katika uwezo wao kuzifikia. Kutumia tiba zifaazo sio kuikana imani kwa maana Mungu amezitoa ili kupunguza maumivu na kuishuhudia asili katika utendaji wake wa uponyaji. Kushirikiana na Mungu kwa kujiweka katika mkao mwafaka zaidi katika safari ya kupona siyo kuikana imani (pamoja na maombi, lakini pia utumiaji wa dawa si kukosa imani). Mungu ameweka karibu yetu maarifa ya kanuni za uzima. Ujuzi huu umewekwa ndani ya uwezo wetu ili tuweze kuutumia. Twapaswa kutumia kila njia kwa ajili ya urejeshaji,

tukichukua kila kinachonufaisha kwa kadiri iwezekanavyo, tukitenda kazi kwa kupatana na sheria za asili. Tujapoomba uponyaji wa mgonjwa, twaweza kufanya kazi kwa nguvu zetu zote, tukimshukuru Mungu kwamba tunao upendeleo wa kushirikiana Naye, na kuomba baraka Zake kwa njia ambazo Yeye Mwenyewe ametupatia (yaani tiba za miti shamba) (Inasemekana kuwa 80% ya magonjwa yote yanapona yenyewe, hii ni neema ambayo Mungu ameiweka kwenye asili—homeostasis). [MH 231.3; HU Aya ya 22]

Tuna idhini ya neno la Mungu kutumia tiba rahisi kuleta uponyaji. Hezekia, mfalme wa Israeli, alikuwa mgonjwa, na nabii wa Mungu alimletea ujumbe kwamba lazima afe. Alimlilia Bwana, na Bwana akamsikia mtumishi Wake na kumpelekea ujumbe kwamba miaka kumi na mitano ingeongezwa kwenye maisha yake. Sasa, neno moja tu toka kwa Mungu lingemponya Hezekia mara moja; lakini maelekezo maalum yalitolewa kwa huyu mfalme, "Na watwae bonge la tini, wakaliweke juu ya jipu, naye atapona." Isaya 38:21 *(watu wengi siku hizi huchukua kitunguu, au viazi ulaya na kukatakata na kuweka kwenye jipu, na keshoye hulikuta limenywea, limetoa usaha, na hakuna maumivu tena)*. [MH 232.1; HU Aya ya 23]

Wakati mmoja Kristo aliyapaka macho ya kipofu kwa udongo na kumwambia, "Nenda ukanawe katika bwawa la Siloamu.... Basi akaenda, akanawa, akaja akiona." Yohana 9:7. Tiba hiyo ingeweza kufanywa tu kwa uweza wa Mponyaji Mkuu, lakini Kristo alitumia njia rahisi ya asili. Ingawa hakupendezwa na dawa zile tunazozijua za hospitalini, Aliidhinisha matumizi ya tiba rahisi na za asilia (soma zaidi jinsi watu wanavyotumia leo udongo kama wa bentonite kama dawa). [MH 233.1; HU Aya ya 24]

Tujapoomba uponyaji kwa mgonjwa, haijalishi hatima ya hali ya mgonjwa itakuwaje, tusipoteze imani kwa Mungu. Ikiwa tunaitwa kukutana na msiba, tupokee kikombe hiki kichungu, tukikumbuka kwamba mkono wa Baba yetu ndiyo hukishikilia midomoni mwetu. Lakini tujapopona, isisahaulike kwamba mpokeaji wa rehema ya uponyaji anawekwa chini ya wajibu uliofanywa upya kwa Muumba (yaani afuate kanuni za afya). Wakoma kumi walipotakaswa, ni mmoja tu ndiye ambaye alirudi kumtafuta Yesu na kumpa utukufu. Ye yote kati yetu asiwe kama wale tisa wasiofikiria vyema, ambao mioyo yao haikuguswa na rehema ya Mungu. "Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; Kwake hakuna kubadilika-badilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka. Yakobo 1:17. [MH 233.2; HU Aya ya 25]

SURA YA 17

MATUMIZI YA TIBA RAHISI

Ugonjwa hauji bila sababu. Njia huandaliwa, na ugonjwa hukaribishwa mwilini, kwa kupuuza sheria za afya *(Msisitizo: kama siyo ajali au bahati mbaya basi 100% huja kwa kupuuza sheria za afya)*. Wengi huteseka kwa sababu ya uasi wa wazazi kwa sheria za afya. Wakiwa hawawajibiki kwa yale ambayo wazazi wao wametenda, hata hivyo ni wajibu wao kuhakikisha kipi ambacho ni ukiukwaji au ni kipi ambacho si ukiukwaji wa sheria za uzima. Wanapaswa kuepuka mazoea mabaya ya wazazi wao na, kwa kuishi inavyotakiwa, wanajiweka katika mkao wa kiafya ulio bora zaidi. [MH 234.1; HU Aya ya 1]

Hata hivyo, idadi kubwa ya watu huteseka kwa sababu ya mwenendo wao mbaya wa maisha *(Msisitizo: Hii inajumuisha mtazamo wa ulimwengu au kiakili ulivyo kutokana na tamaduni za jamii na jamii au dunia kwa ujumla, mathalani makabila fulani yana mazoea fulani ya kula au kunywa kwa rika au jinsia tofauti, au hata mambo*

kama kutahiri wana wa kike n.k). Wengi hupuuza kanuni za afya katika mazoea yao ya ulaji, unywaji, uvaaji, na katika kujishughulisha. Uasi wao kwa sheria za asili huzaa matokeo hakika kuhusiana na afya; na magonjwa yanapowajia, wengi hawaamini sababu halisi ya mateso yao (kwamba hiyo ndiyo sababu ya kuugua kwao), bali humlalamikia Mungu kwa sababu ya mateso wanayoyapata. Lakini Mungu hakuwajibika katika mateso ambayo huja kama matokeo ya kukiuka sheria ya asili. [MH 234.2; HU Aya ya 2]

Mungu ametukirimia kiasi fulani cha nguvu muhimu za uzima. Pia ametuumba na viungo mahsusi kudumisha utendaji mbalimbali wa uhai, Naye hupanga kwamba viungo hivi viweze kufanya kazi pamoja kwa kupatana (yaani bila ya kuhitilafiana na kingine). Ikiwa tunatunza kwa uangalifu nguvu ya uhai, na kuuweka mfumo nyeti wa mwili katika mpangilio unaofaa, matokeo yake ni kuwa na afya njema; lakini ikiwa nguvu hiyo muhimu itachoshwa haraka, basi mfumo wa fahamu wa mwili, huazima nguvu kwa ajili ya matumizi yake ya wakati uliopo kutoka kwenye vyanzo vyake vya nguvu, na pale kiungo kimoja kinapojeruhiwa, vyote huathirika. Mwili huvumilia utumizi mwingi mbaya bila pasipo kuleta ukinzani unaoonekana wazi; kisha mwili huzinduka na kufanya jitihada za dhati kuondoa athari zilizosababishwa na utendwaji mbaya wake mwili. Jitihada yake katika kurekebisha hali hizi za uharibifu uliofanywa, mara nyingi hudhihirika katika kupanda juu kwa joto la mwili (homa) na aina zingine mbalimbali za kuugua. [MH 234.3; HU Aya ya 3]

Tiba Sahihi (Tiba Mujarabu)

Pale utumiaji vibaya wa afya unapopitiliza kiasi cha mwili kuugua, mara nyingi mwathirika anaweza kujifanyia mambo ambayo hakuna mtu mwingine anaweza kumfanyia. Jambo la kwanza kufanya ni kudadisi chanzo halisi cha huo ugonjwa na kisha kwenda kuufanyia kazi kwa akili (yaani kuutibu) ili kuondoa sababu zilizouleta. Ikiwa utendaji kazi linganifu wa mfumo wa mwili umekuwa haupatani kwa sababu ya kufanya kazi kupita kiasi, kula kupita kiasi, au makosa mengine, usijaribu kutibu shida hizo kwa kuongeza mzigo wa dawa zenye sumu mwilini mwako *(Msisitizo: Mfano mzuri ni kama unakula chakula kingi kupita unavyopaswa kula, au chenye tindikali nyingi, au pilipili, au baking soda na kisha ukawa na mazoea ya kutumia dawa za kupunguza tindikali au antacids/magnesium bila ya kutumia njia za asili, na kuacha kula kwa ulafi au kuacha pilipili n.k basi unakuwa haujasahihisha*

tatizo la urari au balansi ya mwili, hivyo dawa za famasia zitaleta shida kubwa zaidi ya uliyonayo kwenye mfumo, kama vile kuharibu figo, ini, kuharisha, na kuharibu mmeng'enyo wa chakula). [MH 235.1; HU Aya ya 4]

Ulaji usio na kiasi mara nyingi ndio chanzo cha kuugua, na kile ambacho asili (mwili) huhitaji ni kupumzishwa na mzigo usiofaa ambao umewekwa juu yake. Katika masuala mengi ya kuugua, tiba bora kabisa ifaayo ni mgonjwa afunge asile mlo mmoja au miwili, ili viungo vinavyofanya kazi nyingi kupita kiasi kwa umeng'enyaji wa chakula zipate fursa ya kupumzika. Mlo wa matunda kwa siku chache mara nyingi umeleta nafuu kubwa kwa wale wanaofanya kazi kwa kushughulisha zaidi ubongo *(Msisitizo: hawafanyi kazi za mikono zinazotumia nguvu au zinazoyeyusha chakula kwa urahisi)*. Mara nyingi kipindi kifupi cha kuacha kula kitu chochote, kikifuatiwa na ulaji rahisi, wa wastani, kimefanya watu wengi wapone kupitia jitihada za mwili/asili kujiponya wenyewe. Lishe inayohusisha kiasi kwa mwezi mmoja au miwili huweza kuwashawishi wengi wauguao ya kwamba njia ya kujinyima ni njia ielekeayo kwenye afya njema. [MH 235.2; HU Aya ya 5]

Pumziko Kama Dawa

Wengine hujisababishia wenyewe kuugua kwa kufanya kazi kupita kiasi. Kwa watu kama hawa, mapumziko, kuwa huru na masumbufu ya maisha haya kwa kutulia, na kula chakula cha kiasi, ndiyo tiba muhimu katika kurejesha afya yao tena. Kwa wale waliochoka kiakili na wameharibika kwa sababu ya kutingwa na kazi daima na wamefungiwa kwenye sehemu moja tu, kutembelea mashambani, ambapo waweza kuishi maisha rahisi, yasiyokuwa ya masumbufu, wakija kukutana kwa ukaribu zaidi na kazi za uumbaji wa Mungu (mashamba, miti, mabonde n.k), itakuwa msaada kwao. Kuzunguka-zunguka katika mashamba na misitu, kuchuma maua, kusikiliza nyimbo za ndege, kutafanya mengi zaidi katika safari kuelekea uponyaji, zaidi ya njia nyingine yo yote. [MH 236.1; HU Aya ya 6]

Katika afya njema na katika kuugua, maji safi ni mojawapo ya baraka bora na za pekee kabisa za mbingu. Matumizi yake sahihi huimarisha afya. Ni kinywaji ambacho Mungu alitupatia ili kutuliza kiu kwa wanyama na mwanadamu. Yakinywewa kwa uhuru kwa jinsi ipasavyo, husaidia kusafirisha mahitaji ya mfumo wa mwili, na kusaidia mwili kukabiliana na magonjwa *(Msisitizo: lita mbili mpaka tatu kwa siku kama*

huna magonjwa yanayotunza maji mwilini). Matumizi ya maji kwa nje ya mwili ni mojawapo ya njia rahisi na toshelevu katika kurekebisha mzunguko wa damu (haidrotherapia; maji huosha mwili ndani na nje). Kuoga na maji baridi yaliyotulia kunasaidia mwili uwe mchangamfu. Kuogea maji ya moto husaidia kufungua matundu ya vinyweleo vya ngozi na hivyo husaidia uondoaji wa uchafu mwilini (takamwili). Kuogea maji ya moto, na maji vuguvugu huzipoza neva na husawazisha mzunguko wa damu. [MH 237.1; HU Aya ya 7]

Lakini wengi hawajawahi kujifunza kupitia uzoefu binafsi kuhusu matokeo yenye manufaa ya matumizi sahihi ya maji, na huogopa jambo hili. Tiba ya maji haithaminiwi jinsi inavyopaswa, na ili kuyatumia maji kwa ustadi kuna hitaji la kufanya kazi yenye juhudi, ambayo wengi hawataki kuifanya *(Msisitizo: wengi husema tiba rahisi zina mlolomgo mrefu kuziandaa)*. Lakini hakuna anayepaswa kuhisi kuwa na kisingizio kwa sababu tu ya ujinga wake au uzembe kuhusiana na jambo hili. Zipo njia nyingi ambazo maji yaweza kutumika kutuliza maumivu na kuzuia ugonjwa. Watu wote wapaswa kuwa na utambuzi katika maarifa ya matumizi ya tiba rahisi majumbani mwao. Hasa akina mama, wanapaswa kujua jinsi ya kutunza familia zao katika suala la afya na maradhi. [MH 237.2; HU Aya ya 8]

Utendaji (kujishughulisha na kushughulika kwa kila kiungo) ni sheria ya uhai wetu wanadamu. Kila kiungo cha mwili kina kazi yake mahsusi, ambapo kujishughulisha kwa kiungo cha mwili ndio msingi wa maendeleo yake mazuri na nguvu. Utendaji sahihi wa viungo vyote huleta nguvu na uimara, bali mwelekeo wa kutokitumia kabisa hicho kiungo huelekea uharibifu na kufa. Jaribu tu kuufunga mkono wako, hata kwa majuma machache, na kisha ondoa vifungo vyake, nawe utaona kwamba mkono huo utakuwa dhaifu kuliko ule ambao umekuwa ukiutumia kwa matumizi ya wastani tu wakati huo huo. Kutovishughulisha viungo kwa kazi/mazoezi huleta athari ya namna ile ile kwenye mfumo mzima wa misuli. [MH 237.3; HU Aya ya 9]

Ugonjwa ni matokeo ya viungo vya mwili kutojishughulisha. Mazoezi huvichangamsha viungo vya mwili na kusawazisha mzunguko wa damu, lakini pasipo kujishughulisha na lo lote, damu haizunguki kwa uhuru, na mabadiliko ndani yake ambayo ni muhimu sana kwa uhai na afya, hayafanyiki. Vivyo hivyo ngozi hulala. Taka-mwili hazitolewi jinsi inavyopaswa wakati ambapo mzunguko wa damu ungeharakishwa kwa kufanya mazoezi ya nguvu, na ngozi ikawekwa katika hali nzuri ya afya, na mapafu yakaingiza hewa safi. Hali hii ya mfumo hushinikiza mzigo maradufu kwenye viungo vinavyohusika na utoaji taka-mwili (figo, mapafu, utumbo mkubwa, ini, ngozi, n.k) na kisha ugonjwa unakuwa ndiyo matokeo ya hali hii. [MH 238.1; HU Aya ya 10]

Wagonjwa hawapaswi kutiwa moyo kwa kukaa bila shughuli yo yote. Pale viungo vinaposhughulishwa kupita kiasi, pumziko kabisa kwa muda fulani wakati mwingine hukinga ugonjwa wenye hali mbaya; lakini kwa wale ambao wamethibithiswa kuwa wagonjwa, iwe nadra sana au afadhali kusimamisha shughuli zote *(Msisitizo: si lazima kuacha shughuli zote, wanaweza hata kukunja nguo, kumenya maharage n.k).* [MH 238.2; HU Aya ya 11]

Wale ambao wameathirika kiafya kwa kazi zinazotumia sana akili, wanapaswa kupumzisha akili zao kutoka kwenye kufikiri vya kuchosha; lakini wasiaminishwe kuwa ni hatari kwao kutumia kabisa nguvu zao za kiakili. Wengi wana mwelekeo wa kudhani kuwa hali yao ni mbaya zaidi kuliko uhalisia wenyewe ulivyo. Fikra za namna hii huchelewesha uponyaji, na hazipaswi kuhimizwa *(Msisitizo: zina mwelekeo mbaya—wrong mindset)*. [MH 238.3; HU Aya ya 12]

Wachungaji, walimu, wanafunzi, na wafanyakazi wengine wenye kazi zinazotumia sana ubongo, mara nyingi hupatwa na magonjwa kwa sababu ya kushughulisha akili kupita kiasi, na hawajishughulishi na kufanya mazoezi ya mwili. Watu hawa wanahitaji maisha yenye kuushughulisha mwili. Kujizoeza kujitiisha kuwa na kiasi, pamoja na kufanya mazoezi inavyofaa, kutaleta matokeo mazuri ya uimara wa akili na mwili, na kutaleta uwezo wa ustahamilivu kwa wafanyakazi wote watumiao zaidi ubongo. [MH 238.4; HU Aya ya 13]

Wale ambao wamezishughulisha nguvu zao za mwili kupita kiasi hawapaswi kuhimizwa kuacha kabisa kazi za mikono. Lakini ili kazi iwanufaishe zaidi, inapaswa kuwa na mpangilio na yenye kupendeza. Mazoezi yanayofanywa nje ya nyumba ndiyo yaliyo bora zaidi kwa mwili; mazoezi haya yanapaswa yawe na mikakati ya kuimarisha kwa kuvitumia viungo ambavyo vimekuwa dhaifu; na moyo ni lazima uwe ndani ya mazoezi haya; kazi ya mikono haitakiwi kugeuka na kuwa yenye kuchosha sana *(Msisitizo: kazi ile ambayo mtu anaona kwamba 'ni lazima nifanye hii kazi ila moyo wangu haumo ndani ya hii kazi).'* [MH 238.5; HU Aya ya 14]

Pale Wagonjwa wanapokosa lo lote la kufanya lenye kuchukua muda na usikivu wao, mawazo yao hujikita kwao wenyewe, (yaani wanajifikiria wao wenyewe tu—umimi), na wanakuwa watu wenye chuki na wepesi wa kuudhika. Mara nyingi hujikita kwenye mawazo yao yasiyofaa mpaka wanajidhania wenyewe kuwa wabaya kuliko walivyo kwa uhalisia na ya kwamba hawawezi kabisa kufanya lo lote ili kujisaidia. [MH 239.1; HU Aya ya 15]

Katika visa hivi vyote mazoezi ya mwili yaliyoratibiwa vizuri, yatathibitika kuwa njia nzuri ya tiba na uponyaji. Wakati mwingine itaonekana kwamba mazoezi ni muhimu kwa kiasi kikubwa katika kurejesha afya. Dhamiri huendana na kazi za mikono; na kile ambacho wagonjwa wanahitaji ni dhamiri zao kuamshwa. Pale dhamiri ya mtu inapokuwa mfu, (yaani imekaa tu bila kushughulishwa kabisa), uwezo wa kufikiri huwa usio wa kawaida, na inakuwa haiwezekani kwa mtu huyo kuukabili ugonjwa. [MH 239.2; HU Aya ya 16]

Kutokuwa na shughuli ya kufanya au mazoezi ndio laana kuu ambayo inaweza kuwapata wagonjwa wengi. Shughuli nyepesi inayofaa, ikiwa haishughulishi mwili na akili kwa kupita kiasi, ina mvuto unaoleta matokeo yenye furaha kwa mwili na akili. Huimarisha misuli, huboresha mzunguko wa damu, na humridhisha mgonjwa kwa kutambua kwamba yeye si mtu asiye na thamani kabisa katika ulimwengu huu wenye shughuli nyingi. Aweza kujishughulisha na kufanya mazoezi ingwa mwanzoni itakuwa kidogo, baada ya muda atagundua kwamba nguvu zake zinaongezeka, na kiwango cha kazi zinazofanywa huzidi kuongezeka kwa kadiri nguvu zake zinavyoendelea kuongezeka. [MH 240.1; HU Aya ya 17]

Mazoezi humsaidia aliyevimbewa kwa kuvichangamsha viungo vya umeng'enyaji wa chakula. Kujishughulisha na kusoma sana au mazoezi makali mara tu baada ya kula, huzuia kazi ya mmeng'enyo wa chakula; lakini kutembea umbali mfupi baada ya kupata mlo, huku kichwa kikiwa kimesimamishwa wima na mabega yakiwa nyuma, ni jambo linalonufaisha zaidi. [MH 240.2; HU Aya ya 18

Licha ya mengi kusemwa na kuandikwa kuhusu umuhimu wa mazoezi, bado kuna wengi ambao hupuuza mazoezi ya mwili. Wengine hunenepa kupita kiasi kwa sababu mfumo wa mwili umeziba; wengine huwa wembamba sana na kudhoofika kwa sababu nguvu zao muhimu zimechoshwa katika kutupa chakula cha ziada. Ini hulemewa katika jitihada yake ya kusafisha damu chafu, na matokeo yake ni ugonjwa. [MH 240.3; HU Aya ya 19]

Wale ambao wana mazoea ya kukaa sana bila kazi yo yote ya mikono, kila wakati hali ya hewa inaporuhusu wanapaswa kufanya mazoezi katika eneo la wazi nje ya nyumba, iwe ni msimu wa joto au baridi. Kutembea ni zoezi bora kuliko kupanda farasi au kuendesha gari, kwa kuwa misuli yote ya mwili hushughulishwa katika mazoezi. Mapafu hulazimishwa kuchukua hatua za kuyasaidia kiafya, kwani haiwezekani mtu kutembea kwa haraka bila ya kuyafanya mapafu yaingize hewa vizuri na kutanuka. [MH 240.4; HU Aya ya 20]

Mazoezi kama haya mara nyingi huwa msaada kwa kujipatia afya bora kuliko kutumia vidonge. Madaktari mara nyingi huwashauri wagonjwa wao kufanya

safari kwa meli baharini, kama burudani, au kwenda kwenye chemchemi zenye madini, au kutembelea sehemu mbalimbali kwa ajili ya kubadilisha hali ya hewa, na mazingira, wakati ambapo watu kama hawa wangekuwa tu na mtindo wa maisha ya kuwa na kiasi, na kufanya mazoezi yanayosaidia afya na kuchangamsha, wangeweza kurejeshwa tena kwenye hali ya afya, na pia wangeweza kuokoa pesa na muda. [MH 240.5; HU Aya ya 21]

SURA YA 18

KUIPONYA AKILI

Uhusiano uliopo kati ya akili na mwili ni wa karibu mno. Kimoja kinapoathiriwa, kingine hukihurumia chenzake. Hali ya akili huathiri afya kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko wengi wanavyofikiri. Magonjwa mengi ambayo watu hukabiliwa nayo ni matokeo ya msongo wa mawazo (imagination). Huzuni, tashwishwi, kutoridhika, majuto, hatia, kutoaminiana, yote huelekea kuvunja nguvu za uhai na kukaribisha uharibifu na kifo. [MH 241.1; HU Aya ya 1]

Ugonjwa wakati mwingine huja, na aghalabu huchochewa na mawazo ya mtu ya kudhania-dhania (imagination). Wengi wamekuwa wagonjwa wa maisha yote, ambao wangeweza kuwa na afya nzuri tu, endapo wangefikiria hivyo (yaani wasingeishi wakiwaza magonjwa). Wengi hufikiri kwamba kila kujianika kidogo tu kwa namna fulani kwenye ugonjwa kutasababisha ugonjwa, na matokeo mabaya huja kwa sababu tu ya kutazamia kwamba ataugua. Wengi hufa kutokana na ugonjwa ambao sababu yake ni ya kufikirika kabisa. [MH 241.2; HU Aya ya 2]

Ujasiri, tumaini, imani, huruma, upendo, vinafanya afya iwe na ubora na kurefusha/kuongeza maisha ya mtu. Akili iliyoridhika, roho changamfu, ni afya ya mwili na nguvu kwa roho. “Moyo uliochangamka ni mzuri kama dawa.” Mithali 17:22. [MH 241.3; HU Aya ya 3]

Katika tiba ya wagonjwa, athari ya ushawishi wa kiakili haipaswi kupuuzwa. Ukitumiwa kwa usahihi, ushawishi huu utatoa mojawapo ya mawakala wenye ufanisi zaidi katika kupambana na ugonjwa. [MH 241.4; HU Aya ya 4]

Akili Inavyopaswa Kuisimamia Akili

Hata hivyo kumekuwa na aina ya tiba ambayo imetumiwa katika kuponya akili, nayo ni mojawapo ya mawakala wenye ufanisi zaidi kwa uovu. Kupitia kile watu wanachokiita sayansi, akili ya mtu mmoja inawekwa chini ya utawala wa mtu mwingine ili kwamba upekee wa yule aliye dhaifu uunganishwe na ule wa mtu mwenye akili yenye nguvu zaidi. Mtu mmoja anakuwa akitenda mapenzi ya mwingine (au pia kufanya maamuzi ya mtu mwingine). Hivyo watu husema kwamba mwelekeo wa mawazo wa mtu yule aliye dhaifu, anayetawaliwa na mawazo ya mwingine, unaweza kubadilishwa, kwamba misukumo ya kutoa afya bora inaweza kupandikizwa kwa mgonjwa huyu, na jambo hili litamwezeshwa kuyapinga na kuyashinda magonjwa, na kuwa na hali nzuri kiafya. [MH 242.1; HU Aya ya 5]

Njia hii ya tiba imetumiwa na watu ambao hawana ufahamu kuhusiana na asili ya ugonjwa, na mwelekeo wake halisi, wakiamini kuwa ni njia yenye kumnufaisha mgonjwa. Lakini kile kinachoitwa sayansi kimejengwa kwenye

msingi wa kanuni za uongo. Jambo hili ni geni kabisa kwenye asili na Roho ya Kristo. Nadharia hii haimwelekezi mtu kwa Yeye ambaye Ndiye uzima na wokovu. Yule anayevutia akili za wengine kwake, huwaongoza wanadamu kujitenga na Chanzo cha Kweli cha nguvu zao. [MH 242.2; HU Aya ya 6]

Si kusudi la Mungu kwamba mwanadamu ye yote asalimishe akili na utashi wake chini ya udhibiti wa mtu mwingine, na kuwa chombo cha kuburuzwa na mwingine bila hiari, yaani chombo kisicho na sauti, na kufanya kazi mikononi kwa kumtegemea yule anayemtawala kiakili. Hakuna mtu anayepaswa kuunganisha utu wake katika ule wa mtu mwingine. Mtu ye yote hatakiwi kabisa kumwangalia mwanadamu mwingine kuwa ndiye chanzo chake cha uponyaji. Mategemeo yake, lazima yawe kwa Mungu na si kwa mwanadamu. Katika hadhi ya utu wake aliopewa na Mungu, mwanadamu anapaswa kuongozwa na kusimamiwa na Mungu Mwenyewe tu, na siyo kwa akili nyingine yo yote 'mahiri' ya mwanadamu (mtu si roboti, anapaswa kuwa na utambulisho na uchaguzi wake binafsi na kumtegemea Mungu tu). [MH 242.3; HU Aya ya 7]

Mungu atamani kuwaleta wanadamu katika mahusiano ya moja kwa moja na Yeye Mwenyewe. Katika kushughulika Kwake kote na wanadamu, atambua kanuni ya uwajibikaji binafsi wa mtu. Anatafuta kumhimiza mwanadamu awe na utambuzi wa wajibu binafsi na kuhimiza hitaji la kuwa na mwongozo wake mwenyewe kama mwanadamu. Anatamani kumleta mwanadamu ashirikiane na Mungu, ili wanadamu wageuzwe na kufanana na Mungu. Shetani hutenda kazi ya kuzuia kusudi hili la Mungu. Atafuta kuhimiza watu wawe tegemezi kwa wanadamu wenzao. Pale akili za watu zinapogeuzwa kutoka kwa Mungu, mjaribu aweza kuziweka hizi akili chini ya utawala wake. Na kwa jinsi hiyo aweza kuudhibiti kikamilifu ubinadamu. [MH 242.4; HU Aya ya 8]

Wazo la kuidhibiti akili nyingine imetokana na Shetani, kujitambulisha mwenyewe kama mtendaji mkuu, kuweka falsafa ya kibinadamu mahali ambapo falsafa ya Mwenyezi Mungu inapaswa kuwepo. Kati ya makosa yote ambayo yanakubaliwa kirahisi miongoni mwa watu wanaodai kuwa Wakristo, hakuna lenye udanganyifu na la hatari zaidi, na hakuna lenye uhakika wa kumtenganisha mwanadamu na Mungu, zaidi ya hili. Ingawa laweza kuonekana kuwa ni njia isiyokuwa na hatia, lakini endapo itatumiwa kwa wagonjwa itaelekea kwenye njia ya kuwaangamiza, na si kwenye njia ya kurejeshwa kwao. Hufungua mlango ambao Shetani ataingia ili kuzitawala akili zote mbili zilizojitoa kutawaliwa na mtu mwingine, pamoja na ile akili inayotawala mwenzake. [MH 243.1; HU Aya ya 9]

Ni nguvu itishayo jinsi gani, inapotolewa kwa wanaume na wanawake wenye nia mbaya. Nadharia hii inawapa fursa kubwa kiasi gani wale wanaoishi kwa

kutumia udhaifu au upumbavu wa wengine! Ni wangapi, kwa njia ya kudhibiti akili za wanadamu wengine zilizo dhaifu au zenye maradhi, watapata njia ya kuridhisha tamaa zao mbaya za mwili au kujipatia faida kwa ajili ya tamaa ya maslahi! [MH 243.2; HU Aya ya 10]

Kuna jambo bora zaidi kwetu kujihusisha nalo, kuliko ubinadamu kuudhibiti ubinadamu (mwanadamu mmoja kumtawala mwanadamu mwenziwe kwa kuichukua akili ya mwenzake). Daktari apaswa kuwaelimisha watu kutoa mawazo yao kwa mwanadamu na kuyaelekeza kwa Mungu. Badala ya kuwaelekeza wagonjwa kuwategemea wanadamu kwa ajili ya uponyaji wa nafsi na mwili wao, apaswa kuwaelekeza kwa Yule ambaye aweza kuwaokoa kabisa wote wamjiao Kwake. Yeye aliyeiumba akili ya mwanadamu ajua akili inahitaji nini. Mungu peke Yake Ndiye awezaye kuponya. Wale ambao akili na miili yao vinaugua wanapaswa kumtazama Kristo ambaye Ndiye Mrejeshaji. “Kwa sababu Mimi ni hai, Yeye asema, “nanyi mtaishi.” Yohana 14:19. Huu ndio uzima na afya tunaopaswa kuunena kwa wagonjwa, tukiwaambia kwamba ikiwa wana imani katika Kristo kama mrejeshaji, ikiwa watashirikiana Naye kwa kutii sheria za afya, na kujitahidi kufikia utakatifu kamili katika hofu ya Mungu, atawapa uzima/uhai Wake. Tunapomleta Kristo kwao kwa njia hii, twawapa watu hawa uwezeshaji, na nguvu, ambayo ni ya thamani; kwa maana hii hutoka tu Kwake juu. Hii ndiyo sayansi ya Kweli ya uponyaji kwa mwili na roho. [MH 243.3; HU Aya ya 11]

Huruma Ya Wataalamu Wa Afya

Hekima kubwa inahitajika katika kukabiliana na magonjwa ambayo yanasababishwa kupitia akili. Moyo wenye kidonda kinachouma sana, moyo uliojeruhiwa, unaougua, na akili iliyokata tamaa, vinahitaji matibabu yasiyo na ukali, matibabu ya upole. Mara nyingi baadhi ya shida za nyumbani ni, kama kidonda kinachouma, kikichimba mwilini, na kudhoofisha nguvu ya uhai. Na wakati mwingine ndivyo hali hii inavyokuwa, kwamba majuto mtu aliyo nayo kwa ajili ya dhambi hudhoofisha maumbile ya mwili na kuondoa utimamu wa akili kwa kufanya akili isiwe na msawaziko mzuri. Ni kwa huruma tu ndiyo tabaka hili la wagonjwa laweza kunufaishwa. Tabibu apaswa kwanza kujipatia kuaminika na kisha kuwaelekeza kwa Mponyaji Mkuu. Ikiwa imani ya wagonjwa inaweza kuelekezwa kwa Tabibu wa Kweli, na hawa wakaweza kuwa na imani kwamba Yeye amejitolea kwa kuchukua jukumu la kubeba udhaifu wao, hii itawaletea utulivu wa akili na mara nyingi itawaletea afya ya mwili. [MH 244.1; HU Aya ya 12]

Huruma na hekima aghalabu vitathibitisha kuwa faida kubwa kwa wagonjwa kuliko tiba zitolewazo kwa ustadi na ujuzi mwingi kwa moyo usiojali au usio na upendo. Pale tabibu anawasili kwenye kitanda cha mgonjwa bila

uchangamfu au ari, bila kujali, bila umakini, na kufanya mambo kizembezembe tu, akimtazama mgonjwa kwa kuonyesha kujali kidogo, kwa neno au tendo akitoa wazo la kwamba ugonjwa huo si ule unaohitaji uangalifu mwingi, na kisha kumwacha mgonjwa aanze kudadavua mambo mwenyewe, anakuwa amemtendea mgonjwa huyo madhara ya uhakika. Mashaka na kuvunjwa moyo ambavyo huja kwa mgonjwa kutokana na kutojali kwa tabibu, aghalabu huzuia matokeo mazuri ya tiba ambazo anaweza kuagiza mgonjwa apewe. [MH 244.2; HU Aya ya 13]

Ikiwa tabibu angeweza kujiweka mahali pa yule ambaye roho yake imenyenyekezwa na ambaye dhamiri yake imedhoofishwa na kuteseka, na ambaye sasa anatamani maneno ya huruma na uhakikisho kutoka kwake, basi angekuwa tayari kuzithamini hisia za mgonjwa. Upendo na huruma ambavyo Kristo alidhihirisha kwa wagonjwa vinapounganishwa na ujuzi wa daktari, itafanya uwepo wa daktari kuwa mbaraka. [MH 245.1; HU Aya ya 14]

Uwazi katika kushughulika na mgonjwa humtia moyo na ujasiri, na hivyo kuthibitisha msaada muhimu katika safari ya kupona. Kuna waganga wanaoona kuwa ni jambo la busara kumficha mgonjwa asili na sababu ya maradhi yake. Wengi miongoni mwa madaktari hawa, wakihofu kumsisimua au kumkatisha tamaa mgonjwa kwa kusema ukweli, wanaweka matumaini ya uongo ya kupona kwa huyu mgonjwa, na hata kumruhusu mgonjwa kushuka kaburini bila kumwonya juu ya hatari yake. Yote haya si mambo ya busara kufanya. Inaweza isiwe jambo bora au salama daima kwa mgonjwa kumwelezea habari kamili ya hatima au hatari yake. Kwani jambo hili laweza kumshtua kwa hofu na kuchelewesha au hata kuzuia uponyaji wa maradhi yake. Na kwa wale wagonjwa ambao maradhi yao kwa kiasi kikubwa ni ya kufikirika, hawapaswi kuambiwa ukweli wote kila mara. Wengi wa watu hawa huwa hawana hekima ya kuchambua mambo vizuri, na hawajajizoeza kuzidhibiti nafsi zao. Wana mawazo ya kipekee, nao hufikiria mambo mengi ambayo ni ya uongo kuhusu wao wenyewe na watu wengine pia. Kwa watu kama hawa, mambo haya ni halisi, na wale wanaowatunza katika ugonjwa wao, wanahitaji kudhihirisha fadhili, subira na busara daima. Ikiwa wagonjwa hawa wangeambiwa ukweli kuhusu wao wenyewe, wengine wangeudhika, na hata kukata tamaa. Kristo aliwaambia wanafunzi Wake, “Ningali na mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili sasa hivi.” Yohana 16:12. Ingawa ukweli wote hauwezi kusemwa katika nyakati zote, kamwe hatupaswi au hatuna haki ya kusema uongo. Kamwe tabibu au muuguzi hapaswi kukwepa kusema ukweli. Mganga afanyaye hivi hujiweka mahali ambapo Mungu hawezi kushirikiana naye, na pale anapopoteza imani ya wagonjwa wake kumwamini anakuwa ametupilia mbali mojawapo ya misaada ya kibinadamu yenye ufanisi zaidi katika urejeshwaji wa afya. [MH 245.2; HU Aya ya 15]

Nguvu ya dhamiri ya mtu haithaminiwi kama vile inavyopaswa (nia, kunuia, kuazimia). Hebu nia ya mtu iwekwe kwenye utendaji na kuelekezwa kwa usahihi, nayo itaimarisha mwili mzima na kuwa msaada wa ajabu katika kudumisha afya. Dhamiri ya mtu ni nguvu pia katika kukabiliana na magonjwa. Dhamiri au nia ya mtu, vikishughulishwa katika mwelekeo sahihi, vitadhibiti mawazo na kuwa njia yenye nguvu kwenye kuzuia na kushinda ugonjwa wa kiakili na kimwili. Kwa kushughulisha uwezo wa dhamiri (nia/kunuia) katika kujiweka katika kuhusiana na maisha kunakofaa, wagonjwa wanaweza kufanya mengi ili kushirikiana na jitihada za daktari kwa ajili ya kupona kwao. Kuna maelfu ya watu ambao watapona na hivyo kurudisha afya zao kwenye ubora, ikiwa tu watania kufanya hivyo. Bwana hataki wanadamu waugue. Yeye Atamani wawe na afya njema na furaha, na wanapaswa kunuia kwenye akili zao kuwa wazima. Mara nyingi wagonjwa waweza kupinga magonjwa kwa kukataa kujisalimisha chini ya magonjwa na kupinga maisha ya kukaa bila kuushughulisha mwili kwa namna yoyote (yaani wasitulie katika hali ya kutofanya kazi). Wakiinuka juu ya maumivu na uchungu wao, na wakazane kujihusisha na kazi muhimu inayoendana na uwezo wao. Kwa kazi kama hiyo na utumiaji wa hewa, na mwanga wa jua, watu wengi waliodhoofika wanaweza kupata afya na nguvu. [MH 246.1; HU Aya ya 16]

Kanuni za Biblia za Matibabu

Kwa wale ambao wangependa kuirudisha na kuitunza tena afya yao, kuna somo katika Maneno ya Maandiko Matakatifu, “Msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho.” Waefeso 5:18. Sio kwa msisimko, au kutojali kunakosababishwa na vichochezi visivyo vya asili au visivyofaa *(vitu ambavyo mwanadamu anajitengenezea kama vile kahawa, pombe, vileo, baadhi ya dawa za famasia [narcotics], bangi, redbull au energy drinks, tumbaku, nyama na madawa yote ya kulevya, chai nyeusi, pilipili kali angalia zaidi kwenye 3T 487 na kabrasha la The use of Stimulants by EGW)*; si kwa kuendekeza hamu na tamaa mbaya za mwili, kwamba kunaweza kuonekana kuwa uponyaji wa kweli au burudisho la mwili au roho. Miongoni mwa wauguao kuna wengi ambao hawana Mungu na hawana tumaini. Wanateseka kutokana na tamaa ambazo hawawezi kuziridhisha, tamaa zinazoleta mkanganyiko, na kuhukumu dhamiri zao wenyewe; wanapoteza uwezo wao wa kushikilia uhai wao katika maisha haya, na hawana matarajio ya maisha yajayo ya mbinguni. Wale wanaohudumia watu wenye maradhi, wasifikiri kwamba wanaweza kuwanufaisha wagonjwa hawa kwa kuwapatia mambo ya kianasa, na kusisimua tamaa ambazo huziendekeza. Hizi zimekuwa laana katika maisha yao. Nafsi yenye njaa na kiu

itaendelea kuona njaa na kiu alimradi tu inatafuta kuridhishwa na mambo ya hapa duniani. Wale wanaokunywa kwenye chemchemi ya raha za ubinafsi na uchoyo, hakika wamedanganyika. Wanachanganya msisimko na kudai hivyo ndiyo nguvu, na kisha msisimko unapokoma, msukumo wao huisha, na wanaachwa katika hali ya kutoridhika na kukata tamaa (kulewa na kisha kudondoka chini wakati kafeini au kileo kimekwisha). [MH 246.2; HU Aya ya 17]

Amani ya kudumu, pumziko la kweli la roho, lina Chanzo kimoja tu. Ilikuwa ni jambo hili ambalo Kristo alizungumza aliposema, “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha.” Mathayo 11:28. “Amani nawaachieni; amani Yangu nawapa; niwapavyo Mimi si kama ulimwengu utoavyo.” Yohana 14:27. Amani hii si kitu ambacho Mungu hukitoa mbali na Yeye Mwenyewe. Hii iko ndani ya Kristo, na twaweza kuipokea tu kwa kumpokea Yeye. [MH 247.1; HU Aya ya 18]

Kristo Ndiye chemchemi ya kisima cha uzima. Kile ambacho wengi wanahitaji ni kuwa na ujuzi dhahiri zaidi juu Yake; wanahitaji kuwa na subira na upole, hata hivyo wanahitaji wawe dhati na wenye bidii katika kufundishwa jinsi mwili mzima wa mwanadamu unavyoweza kuelekezwa kwenye uponyaji kwa njia za Mungu (njia za tiba asili). Pale nuru ya jua la upendo wa Mungu inapoangaza rohoni, uchovu usioleta utulivu na kutoridhika vitakoma, na furaha ya kuridhisha itaimarisha kwenye akili na afya na ukakamavu wa mwili. [MH 247.2; HU Aya ya 19]

Tu katika ulimwengu wa mateso. Ugumu, kujaribiwa, na huzuni hutungoja sote njiani katika safari ya kuelekea nyumbani mbinguni. Lakini kuna wengi ambao hufanya mizigo ya maisha kuwa mizito maradufu kwa kudumu kutazamia shida. Endapo wakakutana na shida au kuvunjwa moyo, hufikiri kwamba kila kitu kinaenda kuharibika, kwamba fungu lao ndio kipande kilicho kigumu zaidi ya vyote, na daima wanakuwa na uhakika kuwa wanakaribia kuwa wahitaji. Hivyo hujiletea wenyewe unyonge (majanga) na kuwatia uvuli wale walio karibu nao. Maisha yenyewe huwa mzigo kwao. Lakini si lazima jambo hili liwe hivyo. Itawagharimu watu kama hawa juhudi iliyodhamiriwa, ili kubadili mkondo wa mawazo waliyo nayo. Lakini mabadiliko yanaweza kufanywa. Furaha yao, kwa maisha haya na yale yajayo, hutegemea kukaza mawazo yao juu ya mambo yenye kuchangamsha. Hebu na wasishughulike na mamvo ya kufikirika tu, bali watazame manufaa ambayo Mungu ameyatawanya katika njia yao, na mbele zaidi ya hizi, kwa imani, wazione faida zisizoonekana, za milele. [MH 247.3; HU Aya ya 20]

Kwa kila jaribu, Mungu ametoa msaada. Israeli walipofika jangwani kwenye maji machungu ya Mara, Musa alimlilia Bwana. Bwana hakutoa tiba mpya; Aliita umakini wao kwa kile kilichokuwa mkononi mwao. Kichaka ambacho

Yeye alikuwa amekiumba kilipaswa kutupwa kwenye chemchemi ili kuyafanya maji kuwa safi na matamu. Jambo hili lilipofanyika, watu walikunywa maji na kuburudishwa. Tukimtafuta Kristo katika kila jaribu, Yeye atatupa msaada. Macho yetu yatafunguliwa ili kutambua ahadi za uponyaji zilizoandikwa katika Neno Lake. Roho Mtakatifu atatufundisha jinsi ya kutumia ifaavyo kila baraka ambayo itakuwa kwetu dawa ya huzuni. Kwa kila rasimu ya uchungu ambayo imewekwa kwenye midomo yetu, tutapata tawi la uponyaji. [MH 248.1; HU Aya ya 21]

Hatupaswi kuruhusu wakati ujao, pamoja na matatizo yake magumu, matazamio yake yasiyoridhisha, kuifanya mioyo yetu kuzimia, magoti yetu kutetemeka, na mikono yetu kulegea. “Na azishike nguvu Zangu,” asema Mungu Mwenye Nguvu, “ili afanye amani Nami; naye atafanya amani Nami.” Isaya 27:5. Wale wanaosalimisha maisha yao kuongozwa Naye Mungu na kwenye utumishi Wake, kamwe hawatawekwa katika nafasi ambayo Yeye hajatoa msaada au ugavi. Haijalishi hali yetu ilivyo, ikiwa sisi tu watendaji wa Neno Lake, tunaye Kiongozi wa kutuelekeza njiani mwetu; haijalishi ni mifadhaiko gani tuliyo nayo, sisi tunaye Mshauri wa hakika; haijalishi kama huzuni, kufiwa, au upweke wetu ni mzito kiasi gani, tunaye Rafiki anayetuhurumia. [MH 248.2; HU Aya ya 22]

Ikiwa katika ujinga wetu twafanya makosa, Mwokozi hatutupi. Kamwe hatuhitaji kujisikia kwamba tuko peke yetu. Malaika ni wenzi wetu. Msaidizi ambaye Kristo aliahidi kumtuma katika Jina Lake, Naye anakaa pamoja nasi (Roho Mtakatifu). Katika njia iendayo kwenye Jiji la Mungu hakuna magumu ambayo wale wanaomtumaini Yeye, hawawezi kuyashinda. Hakuna hatari ambazo hawawezi kuziepuka. Hakuna huzuni, hakuna kukosewa haki, hakuna udhaifu wa kibinadamu, ambao Yeye hajatoa suluhisho au tiba. [MH 249.1; HU Aya ya 23]

Hakuna haja ya kujiachia kwenye shimo la ukataji tamaa na kukosa matumaini. Shetani anaweza kuja kwako na pendekezo lenye ukatili akisema, “Kesi yako ni ya kukatisha tamaa. Wewe huwezi kukombolewa.” Lakini kuna tumaini kwako katika Kristo. Mungu hatuambii tushinde kwa nguvu zetu wenyewe. Yeye Anatuomba tuje karibu na upande Wake. Shida zozote tunazojitaabisha nazo, na zinazolemea nafsi na mwili, Yeye hungojea ili atuweke huru kutoka kwa hizo. [MH 249.2; HU Aya ya 24]

Yeye aliyeuchukua ubinadamu juu Yake Mwenyewe anajua jinsi ya kuhurumia mateso ya wanadamu. Sio tu kwamba Kristo anajua kila nafsi, na mahitaji yake ya kipekee na majaribu yake, lakini pia anajua hali zote zinazoikera na kuisumbua roho. Mkono Wake umenyooshwa kwa huruma kwa kila mtoto anayeteseka. Wale wanaoteseka zaidi, hupata huruma na sikitiko

Lake zaidi. Yeye Anaguswa na hisia za udhaifu wetu, na anatamani sisi tuweke fadhaa, kuchanganyikiwa na shida zetu miguuni Pake na kisha tuviache hivyo vyote hapo. [MH 249.3; HU Aya ya 25]

Si jambo la hekima kujitazama wenyewe na kujifunza kuhusiana na hisia zetu. Tukifanya hivyo, adui atawasilisha mambo magumu na majaribu ambayo yanadhoofisha imani na kuharibu ujasiri wetu. Kusoma kwa karibu hisia zetu na kuzipa kipaumbele ni kutumbuiza mashaka na kujifungafunga kwenye uzi wa fadhaa na mkanganyiko. Twapaswa kutazama mbali kutoka kwenye nafsi zetu na kuelekeza macho yetu kwa Yesu. [MH 249.4; HU Aya ya 26]

Wakati majaribu yanapokushambulia, wakati wasiwasi, masumbufu ya maisha, fadhaa, na giza vinaonekana kuzunguka nafsi yako, angalia nyuma na ili kuona mahali ulipoona nuru mara ya mwisho. Tulia katika upendo wa Kristo na chini ya ulinzi Wake. Dhambi inaposhindana ili kutawala moyoni mwako, wakati hatia inapogandamiza roho na kulemea dhamiri yako, kutokuamini kunapoifunika akili, kumbuka kwamba neema ya Kristo inatosha kuitiisha dhambi na kufukuza giza. Kuingia katika ushirika na Mwokozi, ni kuingia katika eneo la amani. [MH 250.1; HU Aya ya 27]

Ahadi za Uponyaji

"Bwana huzikomboa nafsi za watumishi Wake, Wala hawatahukumiwa wote wamkimbiliao." Zaburi 34:22. [MH 250.2; HU Aya ya 28]

"Kumcha Bwana ni tumaini imara,

Na watoto Wake watakuwa na kimbilio." Mithali 14:26. [MH 250.3; HU Aya ya 29]

“ Bali Sayuni alisema, Yehova ameniacha,

Bwana amenisahau.

Je! mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye,

Hata asimhurumie mwana wa

tumbo lake?

Naam, hawa wanaweza kukusahau, lakini Mimi sitakusahau wewe.

Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono Yangu; kuta zako ziko mbele Zangu daima.” Isaya 49:14-16, [MH 250.4; HU Aya ya 30]

“Usiogope; kwa maana Mimi ni pamoja nawe:

usifadhaike; kwa maana Mimi ni Mungu wako; naam, nitakusaidia;

Naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki Yangu." Isaya 41:10. [MH 251.1; HU Aya ya 31]

"Nisikilizeni, enyi nyumba ya Yakobo, ninyi mliochukuliwa na Mimi tangu tumboni,

Mlioinuliwa tangu mimbani, Na hata uzee wenu, Mimi Ndiye Yule Yule;

Na hata wakati wenu wa mvi nitawabeba;

nimefanya, Nami nitawabeba, Naam

Nitakuchukua, na kukuokoa wewe." Isaya 46:3, 4, [MH 251.2; HU Aya ya 32]

Hakuna kitu chochote kinachoelekea kuimarisha na kukuza afya ya mwili na roho kuliko roho ya shukrani na sifa. Ni wajibu chanya wa mwanadamu kuipinga hali ya huzuni, na mawazo na hisia za kutoridhika—kama vile ulivyo wajibu wetu kusali. Ikiwa tunaenda mbinguni, twawezaje kwenda kama kundi la waombolezaji, tukiugua na kutoa sauti ya kuonyesha kwamba tuna maumivu na kulalamika katika safari yetu, njiani mwote, kuelekea nyumbani mwa Baba yetu? [MH 251.3; HU Aya ya 33]

Wale wanaojiita kuwa ni Wakristo, na ambao daima wanalalamika, na kuonekana kufikiria uchangamfu na furaha ni dhambi, hakika hawana dini ya kweli. Wale wanaofanya maombolezo kana kwamba ndiyo starehe yao kwa kila kitu chenye masikitiko kwenye ulimwengu wa asili/uumbaji, na kuchagua kutazama majani yaliyokufa badala ya kukusanya maua mazuri yaliyo hai, watu wasioona uzuri katika vilele vya milima mikubwa na katika mabonde yaliyovikwa kijani kibichi, ambao huzifunga hisia zao ili wasisikie sauti ya furaha zinazongumza nao kwenye asili/uumbaji, naam, sauti ambazo ni tamu na za muziki kwa sikio linalosikiliza—watu hawa, hawamo ndani ya Kristo. Wanajikusanyia ukungu na giza, wakati ambapo wangeweza kuwa na mwangaza, naam, hata Jua la Haki linalochomoza mioyoni mwao likiwa na uponyaji katika miale Yake. [MH 251.4; HU Aya ya 34]

Mara nyingi akili yako inaweza kuwa na mawingu kwa sababu ya maumivu. Basi usijilazimishe kufikiria. Wewe unajua kwamba Yesu anakupenda. Naye Anaelewa udhaifu wako. Unaweza kufanya mapenzi Yake tu kwa kujidondosha na kupumzika mikononi Yake. [MH 251.5; HU Aya ya 35]

Ni sheria ya asili kwamba mawazo na hisia zetu zinahamashishwa na kuimarishwa pale tunapoziweka katika maneno, yaani tunapozitamka. Ingawa maneno huelezea mawazo yetu, ila ni kweli pia kwamba mawazo yetu huendana na maneno yetu. Kama tungeielezea kwa maneno imani yetu zaidi,

na kufurahia zaidi baraka ambazo tunajua tunazo,—rehema kuu na upendo wa Mungu—Lazima tungekuwa na imani zaidi na furaha kubwa zaidi. Hakuna ulimi unaoweza kuelezea, hakuna akili yenye ukomo inayoweza kufikiria baraka inayotokana na kuthamini wema na upendo wa Mungu. Hata humu-humu duniani, twaweza kuwa na furaha kama chemchemi yenye utajiri, isiyopungua kamwe, kwa sababu inalishwa maji na vijito vinavyotiririka kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu. [MH 251.6; HU Aya ya 36]

Basi na tuelimishe mioyo na midomo yetu kunena sifa za Mungu kwa upendo Wake usio na kifani. Hebu na tuelimishe roho zetu kuwa na matumaini na kukaa katika nuru inayoangaza kutoka kwenye msalaba wa Kalvari. Kamwe tusisahau kwamba sisi ni watoto wa Mfalme wa mbinguni, wana na binti za Bwana wa majeshi. Ni fursa yetu kuwa na utulivu endelevu katika Mungu. [MH 253.1; HU Aya ya 37]

“Na Amani ya Kristo itawale mioyoni mwenu; ... Iweni watu wa shukrani.” Wakolosai 3:15.

Tukisahau magumu na shida zetu zote, hebu tumsifu Mungu kwa fursa ya kuishi kwa utukufu wa Jina Lake. Hebu baraka mpya za kila siku mpya, ziamshe sifa za Mungu kwenye mioyo yetu, kwa viashiria/alama za utunzaji Wake tunazoiona, pamoja na upendo Wake. Unapofungua macho yako asubuhi, mshukuru Mungu kwamba amekulinda usiku kucha. Mshukuru kwa amani Yake moyoni mwako. Asubuhi, adhuhuri, na usiku, hebu shukrani zipande mbinguni kama manukato. [MH 253.2; HU Aya ya 38]

Wakati mtu anapokuuliza Je, unajisikiaje, usijaribu kuchekecha ubongo wako kwa kufikiria ni jambo gani unaweza kumwambia, ambalo ni la kuhuzunisha ili upate huruma yake. Usizungumze juu ya ukosefu wako wa imani, na huzuni na mateso yako. Mjaribu hufurahia kusikia maneno kama hayo. Unapopenda kuzungumzia juu ya mada za kusikitisha, wewe unamtukuza adui. Hatupaswi kupiga kambi kwenye kuelezea nguvu kubwa za Shetani ambazo zitatushinda. Mara nyingi tunajiangusha wenyewe mikononi mwake kwa kuzungumza juu ya uwezo wake. Hebu badala yake sisi tuzungumzie kuhusu uweza mkuu wa Mungu kuyafunga maslahi yetu yote pamoja na maslahi Yake Mwenyewe. Elezea juu ya uwezo wa Kristo usio na kikomo, na kisha uongee juu ya utukufu Wake. Mbingu zote zina shauku na wokovu wetu. Malaika wa Mungu, maelfu kwa maelfu, na elfu kumi mara elfu kumi, wametumwa kuwahudumia wale ambao watakuwa warithi wa wokovu. Hawa wanatulinda dhidi ya uovu na kurudisha nyuma nguvu za giza ambazo zinatafuta maangamizi yetu. Je, sisi hatuna sababu ya kuwa na shukrani kila wakati, watu wenye moyo wa shukrani hata wakati inapoonekana wazi kwamba kuna matatizo katika njia yetu? [MH 253.3; HU Aya ya 39]

Imba Sifa

Hebu sifa na shukrani zionyeshwe kwa nyimbo. Tunapojaribiwa, badala ya kutoa matamko ya kuelezea hisia zetu, hebu kwa imani tuinue wimbo wa shukrani kwa Mungu. [MH 254.1; HU Aya ya 40]

1. Twamsifu Mungu Mwana wa upendo, aliyetufia na kupaa juu.

Aleluya! Usifiwe, aleluya! Amin; aleluya usiwe, utubariki.

2. Twamsifu Mungu, Roho mtukufu,

Akatufunulia Mwokozi wetu.

3. Twamsifu Mwana, aliyetufia,

Akatukomboa na kutuongoza.

4. Twamsifu Mungu, wa neema yote,

Aliyetwaa dhambi, akazifuta.

5. Tuamshe tena, tujaze na pendo.

Moyoni uwashe moto wa roho.. [MH 254.2; HU Aya ya 41]

Tunakusifu, Ee Mungu, kwa Roho Wako wa nuru,

Ambaye ametuonyesha Mwokozi wetu, na kuutawanya usiku wetu. [MH 254.3; HU Aya ya 42]

Utukufu na sifa zote kwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa,

Ambaye amezichukua dhambi zetu zote, na kutakasa kila waa. [MH 254.4; HU Aya ya 43]

Utukufu na sifa zote kwa Mungu wa neema yote,

ambaye ametununua, na kututafuta, na kuziongoza njia zetu. [MH 254.5; HU Aya ya 44]

Utuhuishe tena; jaza kila moyo na upendo Wako;

Kila nafsi iwashwe moto kutoka juu. [MH 254.6; HU Aya ya 45]

Chorus: Haleluya! Utukufu wako, Haleluya! amina; Haleluya! Utukufu Wako, Utuhuishe tena. [MH 254.7; HU Aya ya 46]

Wimbo ni silaha ambayo tunaweza kutumia kila wakati dhidi ya kukata tamaa. Tunapofungua hivyo moyo kwa nuru ya jua ya uwepo wa Mwokozi, tutakuwa na afya na baraka Zake. [MH 254.8; HU Aya ya 47]

“Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema;

Kwa maana fadhili Zake ni za milele.

Na waseme hivi waliokombolewa na Bwana, wale ambao amewakomboa katika mkono wa mtesi/adui.” [MH 255.1; HU Aya ya 48]

“Mwimbieni, mwimbieni Kwa Zaburi,

Zitafakarini ajabu Zake zote.

Jisifuni kwa Jina Lake takatifu;

na ufurahi moyo wao wamtafutao Bwana.” [MH 255.2; HU Aya ya 49]

“Maana hushibisha nafsi yenye shauku,

Na nafsi yenye njaa huijaza mema.

Waliokaa katika giza na uvuli wa mauti,

Wamefungwa katika taabu na chuma; ...

Wakamlilia Bwana katika dhiki zao,

Akawaponya na shida zao.

Akawatoa katika giza na uvuli wa mauti,

Akayavunja mafungo yao.

Na watu wamshukuru/wamhimidi Bwana kwa fadhili Zake,

Na maajabu Yake kwa wanadamu! [MH 255.3; HU Aya ya 50]

“Ee nafsi yangu, kwa nini kuinama?

Na kwa nini unafadhaika ndani yangu?

Umtumaini Mungu;

Kwa maana nitakuja kumsifu,

Aliye afya ya uso wangu,

Na Mungu wangu.” Zaburi 107:1, 2; 105:2, 3; Zaburi 107:9-15; 42:11. [MH 255.4; HU Aya ya 51]

“Shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.” 1 Wathesalonike 5:18. Agizo hili ni uhakikisho kwamba hata yale yanayoonekana kuwa yanakwenda kinyume na sisi yatafanya kazi kwa faida yetu. Mungu asingetuambia tushukuru kwa yale yatakayotudhuru. [MH 255.5; HU Aya ya 52]

“Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu;

Nimwogope nani?

Bwana ni ngome ya uzima wangu;

Nimhofu nani?”

“ Mradi atanisitiri bandani Mwake siku ya mabaya, atanisitiri katika sitara ya hema Yake, na kuniinua juu ya mwamba; ...

Nami nitatoa dhabihu za shangwe katika hema Yake;

Nitaimba, naam, nitamhimidi Bwana. [MH 255.6; HU Aya ya 53]

“Nalimngoja Bwana kwa saburi;

Naye akaniinamia, akakisikia kilio changu.

Tena alinipandisha kutoka shimo la uharibifu, kutoka

udongo wa utelezi,

Akaisimamisha miguu yangu mwambani, akaziimarisha hatua zangu.

Naye akatia wimbo mpya kinywani mwangu, ndio sifa Zake za Mungu wetu

kwa Mungu wetu.”

“Bwana ni nguvu zangu na ngao yangu;

Moyo wangu ulimtumaini, nami nikasaidiwa.

Kwa hiyo moyo wangu unashangilia sana;

Na kwa wimbo wangu nitamsifu.” Zaburi 27:1; 27:5, 6; 40:1-3; 28:7. [MH 256.1; HU Aya ya 54]

Mojawapo ya vizuizi vya uhakika vya kupona kwa wagonjwa ni kuweka umakini juu yao wenyewe (kujifikiria wenyewe tu). Walemavu wengi huwa wanaona kwamba kila mtu anapaswa kuwahurumia na kuwasaidia, wakati kile ambacho wanachokihitaji ni kuondoa umakini kwao wenyewe, na kisha wawafikirie na kuwajali watu wengine. [MH 256.2; HU Aya ya 55]

Mara nyingi watu huulizia maombi yatolewe kwa watu wenye shida, watu wenye huzuni, na watu waliokata tamaa; na jambo hili ni sahihi. Tunapaswa kuomba kwamba Mungu aangazie nuru katika akili zile zilizotiwa giza na kuufariji moyo wenye huzuni. Lakini Mungu hujibu maombi kwa ajili ya wale wanaojiweka kwenye mfereji wa baraka Zake. Wakati tunasali kwa ajili ya watu hawa wenye huzuni, tunapaswa kuwatia moyo/shime wajaribu kuwasaidia wale wenye uhitaji zaidi kuliko wao wenyewe. Ndipo giza

litaondolewa katika mioyo yao wenyewe pale wanapojaribu kuwasaidia wengine. Tunapojaribu kutafuta jinsi ya kuwafariji watu wengine kwa faraja ambayo kwayo tunafarijiwa nayo, baraka huturudia sisi wenyewe. [MH 256.3; HU Aya ya 56]

Sura ya hamsini na nane ya Isaya ni maagizo ya tiba kwa magonjwa ya mwili na roho (Rx:Doctors prescriptions). Ikiwa tunatamani afya na furaha ya kweli ya maisha, ni lazima tuweke katika vitendo sheria zilizotolewa katika Andiko hili. Hapa Mungu anatuagiza juu ya utumishi unaokubalika Kwake, na baraka Zake ambazo huambatana nazo, Bwana asema: [MH 256.4; HU Aya ya 57]

“7 Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?

8 Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde.

9 Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu;

10 na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri.

11 Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.” 256.5; HU Aya ya 58]

Matendo mema yana baraka mara mbili, yanamnufaisha mtoaji na mpokeaji wema. Ufahamu wa kutenda haki ni mojawapo ya dawa bora kwa miili na akili zilizo na magonjwa. Wakati akili inapokuwa huru na yenye furaha kutokana na hisia ya wajibu uliyofanywa vyema na moyo ulioridhika unaotokana na kuwapa watu wengine furaha, ushawishi ushangiliao na wenye kuinua huleta maisha mapya kwenye nafsi nzima. [MH 257.1; HU Aya ya 59]

Badala ya kuhitaji huruma kila wakati kutoka kwa watu wengine, hebu watu wenye ulemavu na wasiojiweza, watafute kuitoa na kuionyesha hiyo huruma kwa watu wengine. Hebu mzigo wa udhaifu wako mwenyewe na huzuni na uchungu vitupwe juu ya Mwokozi Mwenye huruma. Fungua mlango wa moyo wako kwa upendo Wake, na uruhusu utiririke kwa wengine. Kumbuka kwamba wanadamu wote wana mitihani ambayo ni migumu kuistahimili, yaani majaribu ambayo ni magumu kuyapinga, na wewe unaweza kufanya jambo

fulani ili kupunguza mizigo hii. Onyesha shukrani kwa baraka ulizo nazo; onyesha kuthamini umakini unaopokea kutoka kwa watu. Sheheni moyo wako kwa ahadi za thamani za Mungu, ili uweze kutoa kutoka kwenye hazina hii maneno ambayo yatakuwa faraja na nguvu kwa wengine. Hii itakufanya uzungukwe kwa hali ambayo itakuwa ya msaada na ya kuinua kwako. Hebu lengo lako liwe kuwabariki watu walio karibu nawe, ndipo utakapopata njia za kuwa msaada, kwa washiriki wa familia yako mwenyewe na kwa wanadamu wengine. [MH 257.2; HU Aya ya 60]

Ikiwa wale wanaougua magonjwa wangejisahau wenyewe na kujali maslahi ya wengine; kama wangetekeleza agizo la Bwana la kuwahudumia wale wenye mahitaji makubwa kuliko wao wenyewe, basi wangetambua Ukweli wa ahadi ya kinabii, “Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea upesi.” [MH 258.1; HU Aya ya 61]

Mara na Elim

Leo Elim na mitende na visima vyake,

Na kivuli chake chenye furaha kwa uchovu wa jangwa;

Ilikuwa Mara jana, na mwamba na mchanga wake

Upweke usio na kivuli na huzuni.

Ila bado ni jangwa moja hilo hilo lililo na yote mawili,

Upepo ule ule wa Moto ambao hutangatanga kwenye ardhi tupu;

Sehemu ile ile yenye bonde la kwenda chini linafunika sehemu hizo mbili,

Na milima iyo hiyo huizunguka pande zote. [MH 258.2; HU Aya ya 62]

Ndivyo ilivyo hapa kwetu duniani,

kwa kadri navyokumbuka, huwa imekuwa hivyo daima

Uchungu na utamu, huzuni na furaha,

Huegemeana kwa ukaribu sana, na kuna siku moja tu kati yao. [MH 258.3; HU Aya ya 63]

Wakati mwingine Mungu hugeuza uchungu wetu kuwa utamu,

Wakati mwingine Yeye hutupatia chemchemi zenye maji ya kupendeza;

Wakati fulani hutuwekea kivuli kwa Nguzo ya wingu Lake,

Na wakati mwingine kivuli cha mitende iliyobarikiwa huletwa. [MH 258.4; HU Aya ya 64]

Ni nini kinachojalisha basi? Muda hautakuwa mrefu;

Mara na Elim vyote vitapita kwa pamoja;

Visima na mitende yetu itakoma jangwani hivi karibuni,

Hatimaye tutafika "Mji wa Mungu wetu"

Ewe nchi yenye furaha! Ng'ambo ya milima hii ya upweke,

Mahali ambapo mbubujiko wa chemchemi za furaha za milele ulipo;

Ewe Paradiso takatifu! Juu ya mbingu hizi tunazoziona hapa duniani,

Mahali ambapo tutakomesha kutangatanga kwetu kwa jangwani. - Horatius Bonar. [MH 259.1; HU Aya ya 65]

Uhakikisho Uliobarikiwa

YESU MWOKOZI KWA HAKIKA

1. Yesu Mwokozi (wangu) kwa hakika, Hunipa furaha na amani (na utukufu Wako!)

Mrithi wa wokovu wangu, natakaswa kwa damu Yako

(urithi ulionunuliwa Nawe, Nazaliwa katika Roho Wako, na kutakaswa kwa damu Yako) [MH 259.2; HU Aya ya 66]

Kibagwizo:

Habari hii wimbo wangu,

daima nitamsifu Yesu;

habari hii wimbo wangu,

daima nitamsifu Yesu. [MH 259.3; HU Aya ya 67]

2. Nijitoapo nina raha, Na kwa imani namwona Bwana;

Aniletea malaika, Wananilinda, niokoke. [MH 259.4; HU Aya ya 68]

3. Hali na mali anaitwaa, Katika Yesu nabarikiwa;

Nikimngoja kwa subira, Wema Wake unanitosha

-Fanny J. Crosby. [MH 259.5; HU Aya ya 69]

SURA YA 19

KUWASILIANA NA ASILI

Muumba aliwachagulia wazazi wetu wa kwanza mazingira mazuri ambayo yangewafaa, yangekubaliana na kuendana na afya na furaha yao. Hakuwaweka katika jumba la kifalme au kuwazungushia mapambo ya bandia na anasa (luxury) ambazo watu wengi wanahangaikia kuzipata leo. Aliwaweka katika mahusiano ya karibu na asili na ushirika wa karibu na watakatifu wa mbinguni. [MH 261.1; HU Aya ya 1]

Katika bustani ambayo Mungu aliiandaa kama makazi ya watoto Wake, vichaka vya kupendeza na maua maridadi na laini yalivutia macho kila upande. Kulikuwa na miti mingi ya kila namna, ambayo kati yake yalisheheni matunda yenye harufu nzuri na matamu. Juu ya matawi ya hii miti, ndege waliimba nyimbo zao za sifa. Chini ya kivuli chake, viumbe vya dunia vilicheza pamoja kwa kufurahiana bila hofu. [MH 261.2; HU Aya ya 2]

Adamu na Hawa, katika usafi usio na dosari au kuchafuliwa na dhambi, walifurahishwa na yote waliyoyaona na sauti za Edeni. Mungu aliweka kazi yao katika bustani, “ili wailime na kuitunza.” Mwanzo 2:15 . Kazi ya kila siku iliwaletea afya na furaha, na wenzi hawa wawili wenye furaha walimkaribisha kwa shangwe Muumba wao alipowatembelea bustanini jioni, wakati wa kupunga upepo, akitembea na kuzungumza nao. Mungu aliwafundisha masomo Yake kila siku. [MH 261.3; HU Aya ya 3]

Mpango wa maisha ambao Mungu aliweka kwa wazazi wetu wa kwanza una masomo kwa ajili yetu sote. Ingawa dhambi imeweka kivuli chake juu ya dunia, Mungu anatamani watoto Wake wapate furaha katika kazi za mikono Yake. Kadiri mpango Wake wa maisha unavyofuatwa kwa ukaribu zaidi, ndivyo Atakavyofanya kazi ya ajabu zaidi kuurejesha ubinadamu unaoteseka kwa uponyaji. Wagonjwa wanahitaji kuletwa kwa karibu mguso wa asili. Maisha ya nje kati ya mazingira asilia, yanaweza kufanya maajabu kwa watu wengine wasio na uwezo na wanaokaribia kukosa tumaini. [MH 261.4; HU Aya ya 4]

Kelele, fujo, msisimko na mkanganyiko wa miji, maisha yaliyo na mbinyo, na ya bandia, huwa ni yenye kuchosha sana, ni yenye kupunguza nguvu za mwili na kuboesha wagonjwa. Hewa, iliyojaa moshi na vumbi, na gesi zenye sumu, na viini vya magonjwa, ni hatari kwa maisha. Wagonjwa, waliofungwa ndani ya kuta nne, wanafikia wakati ambao wanahisi kuwa kwa sehemu kubwa, ni kana kwamba wamekuwa wafungwa katika vyumba vyao. Wanatazama nje na kuona nyumba na barabara za lami na umati wa watu wanaoharakisha kutembea, labda hata hawaoni anga la buluu au mwanga wa jua, nyasi au maua au miti. Wakiwa wamefungiwa ndani kwa njia hii, wanatafakari juu ya

mateso na huzuni zao, na kuwa mawindo ya mawazo ya huzuni ambayo yanatoka kwao wenyewe. [MH 262.1; HU Aya ya 5]

Na kwa wale walio dhaifu katika nguvu za maadili, miji ina hatari nyingi. Ndani yake, wagonjwa ambao wana hamu zisizo za asili ambazo wanapaswa kuzishinda, wanaanikwa kwenye majaribu kila wakati. Wanahitaji kuwekwa kwenye mazingira mapya, mahali ambapo mkondo wa mawazo yao utabadilishwa; wanahitaji kuwa chini ya ushawishi tofauti kabisa na ule ambao umeharibu maisha yao. Hebu watu hawa waondolewe kwa kipindi fulani kutoka kwenye mivuto hiyo inayowapeleka mbali na Mungu, hadi katika mazingira safi na bora zaidi. [MH 263.1; HU Aya ya 6]

Taasisi za kutunza wagonjwa zingekuwa na mafanikio makubwa zaidi ikiwa zingeanzishwa mbali na miji. Na kwa kadri iwezekanavyo, wote wanaotafuta kurejesha afya yao, wajiweke katikati ya mazingira yaliyo nje ya mji, yaani mashambani, huko wanaweza kunufaika na maisha ya nje ya nyumba kwenye hewa iliyo wazi. Asili ni daktari wa Mungu. Hewa safi, mwanga wa jua wenye furaha, maua na miti, bustani za miti ya matunda na mashamba ya mizabibu, na mazoezi nje ya nyumba kwenye mazingira haya, ni mambo yenye kutoa afya, na kutoa uhai-afya bora. [MH 263.2; HU Aya ya 7]

Madaktari na wauguzi wanapaswa kuwatia moyo wagonjwa kukaa nje kwenye hewa iliyo wazi. Maisha ya nje ndio tiba pekee ambayo walemavu wengi wanaihitaji. Hii ina nguvu ya ajabu katika uponyaji wa magonjwa yanayosababishwa na msisimko na maisha ya mitindo/fasheni ambayo hudhoofisha na kuangamiza nguvu za mwili, akili, na roho. [MH 264.1; HU Aya ya 8]

Ni shukrani iliyoje kwa walemavu waliochoshwa na maisha ya jiji, yaliyo na mwanga wa taa nyingi, na makelele ya mtaani, kujipatia ukimya na uhuru wa mashambani, nje ya mji! Wanageuka kwa hamu kubwa kiasi gani kuangalia maonyesho ya asili! Wanafurahi kwa kiasi kikubwa kukaa nje kwenye hewa wazi, na kushangilia mwanga wa jua, na kuvuta harufu nzuri ya miti na maua! Kuna sifa zinazotoa maisha kwenye miti ya utomvu wa mipaini (pine balsam), katika harufu ya mwerezi na mti wa fir, na miti mingine pia, kuna visifa ambavyo hurejesha afya. [MH 264.2; HU Aya ya 9]

Kwa walemavu wa kudumu, hakuna kitu kinachoelekea kwenye afya na furaha kama kuishi katikati ya mazingira mashambani -nje ya miji. Hapa watu walio dhaifu na wanyonge zaidi wanaweza kukaa au kulala kwenye jua au kwenye vivuli vya miti. Hawa wanapaswa tu kuinua macho yao ili kuona majani mazuri ya miti. Hisia tamu na halisi za utulivu, kupokea na kuburudishwa huja juu yao wanaposikiliza upepo ukinong'ona. Nafsi

zilizoshuka chini kwa huzuni hufufuka. Nguvu ya ajira. Bila kujua akili inakuwa na amani, mapigo ya moyo yenye homa huwa shwari na ya kawaida. Wagonjwa wanapokuwa na nguvu zaidi, watakuwa na uthubutu wa kuchukua hatua chache ili kukusanya baadhi ya maua ya kupendeza, wajumbe wa thamani wa upendo wa Mungu kwa familia Yake kuteseka hapa chini. [MH 264.3; HU Aya ya 10]

Mikakati inabidi iwekwe kwaajili ya kuwaweka wagonjwa nje ya milango ya majumba. Kwa wale wanaoweza kufanya kazi, acha kazi ya kupendeza na rahisi itolewe kwa hawa. Waonyeshe jinsi kazi hii ya nje inavyopendeza na kusaidia watu na wao wenyewe. Watie moyo kuvuta hewa safi. Wafundishe maana kuvuta pumzi kwa kina (deep breathing) na wakati wanapumua na kufanya mazoezi waishughulishe misuli ya tumbo kwa mazoezi. Hii ni elimu ambayo itakuwa ya thamani kwao (* -4-7-8- Vuta pumzi kwa undani kupitia pua yako kwa sekunde 4 na ufungue macho yako kwa upana, kisha ishikilie pumzi uliyoivuta kwa sekunde 7. Wakati huo huo, fungua mdomo wako kwa upana na utoe ulimi wako, ukileta ncha chini kuelekea kidevu chako. Punguza misuli iliyo mbele ya koo lako unapotoa nje kupitia mdomo wako sauti ndefu ya "haaa" kwa sekunde 8. Utaratibu huu wa kupumua unalenga kupunguza wasiwasi, kuongeza afya au kuwasaidia watu kupata usingizi. Angalia zaidi video za deep breathing, na ufanye kila siku dakika 10, kwa wale wazungumzaji wa hadhara wanabidi kujifunza haya ili wasidhuru afya zao. https://youtu.be/aNXKjGFUlMs). [MH 264.4; HU Aya ya 11]

Mazoezi katika hewa-wazi ni lazima yaagizwe kama tiba kwani ni hitaji linaloboresha afya na uhai (Rx). Na kwa mazoezi kama hayo hakuna kitu kilicho bora zaidi ya kulima ardhi. Hebu wagonjwa washirikishwe katika kuweka vitalu vya maua na kuvitunza, wasaidiwe kulima miti ya matunda na bustani za mboga-mboga, wanapohamashishwa kunyanyuka kutoka katika vitanda vyao na kutumia muda kwenye hewa iliyo wazi, kulima maua au kufanya kazi nyingine nyepesi au ndogo-ndogo za kupendeza, mawazo yao yataelekezwa kutoka kwao wenyewe na mateso au kuugua kwo. [MH 265.1; HU Aya ya 12]

Kwa kadiri mtu anavyoweza kukaa nje kwenye hewa bora, ndivyo atakavyohitaji matunzo kidogo zaidi kutoka kwa watu. Kadiri mazingira yake yanavyokuwa ya uchangamfu, ndivyo atakavyokuwa mtu wa msaada zaidi kwa wengine na kwake mwenyewe. Akifungiwa ndani ya nyumba, hata kama imepambwa kwa umaridadi, mtu atakuwa mwenye wasiwasi, huzuni, kuboeka na kuudhika kirahisi. Mzunguke na mambo mazuri ya asili; mweke mahali ambapo anaweza kuona maua yakikua na kusikia ndege wakiimba, na moyo wake utajisikia kuimba ghafla, ili kuendana na nyimbo za ndege. Afueni

itakuja kwenye mwili na akili. Akili itaamshwa, mawazo yatahuishwa, na akili itaandaliwa kukubali na kuthamini uzuri wa Neno la Mungu. [MH 265.2; HU Aya ya 13]

Katika asili daima kunakuwa na kitu cha kugeuza mawazo ya wagonjwa kutoka kwa wenyewe na kuelekeza mawazo yao kwa Mungu. Wakiwa wamezungukwa na kazi Zake za maajabu, akili zao huinuliwa kutoka kwenye vitu vinavyoonekana hadi kwenye visivyoonekana (Je, ni vitu gani vizuri ambavyo havionekani?). Uzuri wa asili/uumbaji huwaongoza watu kutafakari kuhusu makao ya mbinguni, mahali ambako hakutakuwa na chochote cha kuharibika au kuharibu uzuri au wema, hakuna chenye kutia madoa au mawaa, mahali ambapo hakuna magonjwa au kifo. [MH 265.3; HU Aya ya 14]

Hebu matabibu na wauguzi wachukue kutoka kwenye vitu vya asili, mafundisho ya Mungu. Hebu wawaelekeze wagonjwa Kwake Yeye ambaye mkono Wake umeiumba miti mirefu, nyasi, na maua, wakiwatia moyo kuona katika kila chipukizi na Ua, udhihirisho wa upendo wa Mungu kwa watoto Wake. Yeye anawayetunza ndege na maua awatunza na kuwajali viumbe vilivyoumbwa kwa mfano Wake Mwenyewe. [MH 266.1; HU Aya ya 15]

Nje ya malango yetu, katikati ya vitu ambavyo Mungu ameviumba, akipumua hewa safi, yenye afya, mgonjwa anaweza kusimuliwa kwa ubora zaidi kuhusu maisha mapya katika Kristo. Neno la Mungu lisomwe hapa nje. Hapa nje ya nyumba, nuru ya haki ya Kristo inaweza kuangaza ndani ya mioyo iliyotiwa giza na kuchafuliwa na dhambi. [MH 266.2; HU Aya ya 16]

Laiti ningepata kuwa karibu siku baada ya siku,

na Mungu wangu,

Ndipo saa zangu zingekuwa zinapita kwa utamu,

Na huku nikiegemea Neno Lake. [MH 267.1; HU Aya ya 17]

Bwana, natamani kuishi Nawe

Kwa Upya siku hadi siku,

Katika furaha ambazo kamwe dunia haiwezi kuzitoa,

Au kuzitwaa. [MH 267.2; HU Aya ya 18]

Yesu ubarikiwe, njoo, naomba utawale moyo wangu,

Na unifanye kuwa wako kabisa,

Ili nisiondoke tena toka mikononi Mwako,

Wala kuhuzunisha upendo Wako Eh Mungu wangu. - Benjamin Cleveland. [MH 267.3; HU Aya ya 19]

Wanaume na wanawake wanaohitaji msaada wa kuponywa kimwili na kiroho wanaunganishwa na wale ambao maneno na matendo yao yatawavuta kwa Kristo. Wanapaswa kuletwa chini ya ushawishi wa Mmishenari mkuu wa Tiba, Bwana Mwenyewe, Ndiye anayeweza kuponya nafsi na mwili pia. Watasikia kisa cha Upendo wa Mwokozi, na msamaha hutolewa bure kwa wote wanaokuja Kwake, wakiziungama dhambi zao. [MH 267.4; HU Aya ya 20]

Chini ya mvuto kama huo, watu wengi wanaoteseka wataongozwa kwenye njia ya uzima. Malaika wa mbinguni hushirikiana na vyombo vya kibinadamu katika kuleta faraja, matumaini, furaha na amani kwenye mioyo ya wagonjwa na wale wanaoteseka. Chini ya hali kama hizo wagonjwa hubarikiwa maradufu, na wengi hutunukiwa afya. Hatua za miguu dhaifu hurudishiwa unyumbulifu wa misuli. Jicho huweza kuona mwangaza wake tena. Wasio na tumaini hupata matumaini. Uso ambao wakati fulani ulikata kabisa tamaa huvikwa furaha inayonekana na watu. Sauti za minong'ono ya kulalamika hubadilika na kuwa sauti zenye uchangamfu na moyo ulioridhika. [MH 267.5; HU Aya ya 21]

Wakati afya ya mwili inaporudishwa, wanaume na wanawake wanaweza kuizoesha imani hiyo katika Kristo ambayo inalinda afya ya roho. Katika ufahamu wa dhambi zilizosamehewa kuna amani isiyoelezeka, kuna furaha na pumziko. Tumaini lililofifia la Mkristo linang'aa tema. Maneno haya ya imani, "Mungu ni kimbilio letu na nguvu zetu, Msaada unaoonekana tele wakati wa mateso." "Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; Gongo lako na fimbo yako vyanifariji." "Huwapa nguvu wazimiao; na huwaongezea nguvu wale wasio na uwezo." Zaburi 46:1; 23:4; Isaya 40:29 . [MH 267.6; HU Aya ya 22]

Yesu kwa Imani

Imani yangu inakutazama Wewe,

Mwana-Kondoo wa Kalvari,

Mwokozi uliye Mungu;

Sasa nisikie ninapoomba,

Niondolee hatia yangu yote,

Ee nijalie kutoka siku hii ya leo

Niwe Wako kabisa. [MH 268.1; HU Aya ya 23]

Hebu neema Yako tele na initie

Nguvu ndani ya moyo wangu uliozimia,
Bidii yangu itie moyo;
Kama vile ulivyokufa kwa ajili yangu,
Ee pendo langu Kwako na liwe
Safi, lenye joto na lisilobadilika,
Moto wa Roho Mtakatifu ulio hai. [MH 268.2; HU Aya ya 24]

Ninapokanyaga vichochoro vyenye giza vya maisha,
Na majonzi yanaponizunguka kwa karibu,
Bwana naomba Uwe Kiongozi wangu;
Liagize giza ligeuke kuwa mchana,
Futa machozi ya huzuni,
Wala usiniruhusu kamwe nipotee
Kutoka kando Yako.- Ray Palmer. [MH 268.3; HU Aya ya 25]

Imetoka kwenye wimbo huu (YESU KWA IMANI)
1. Yesu kwa imani, nakutumaini, peke Yako
Nishike sasa, na kunitakasa, ni Wako kabisa
Tangu leo.

2. Nipe nguvu pia za kusaidia moyo wangu;
Ulikufa Wewe, wokovu nipewe, nakupenda Wewe,
Bwana wangu.

3. Hapa nazunguka katika mashaka, na matata;
Palipo na giza utaniongoza, hivi nitaweza,
Kufuata.

SEHEMU YA 5—KANUNI ZA AFYA

Bila ya Maarifa ya Kanuni za Afya, hakuna aliye na stahiki ya Kuchukua Majukumu ya Maisha

SURA YA 20

USAFI WA JUMLA

Kujua kwamba mwili wa mwanadamu unapaswa kuwa hekalu la Mungu, makao ya kufunua utukufu Wake, ni elimu inayopaswa kuwa kichocheo cha juu zaidi kuhusiana na kutunza na kukuza nguvu zetu za mwili. Muumba wetu ameuumba mwili wa mwanadamu kwa jinsi ya ajabu na kutisha, na anatuagiza tulifanye somo letu, yaani tujifunze viungo vya mwili wetu, na jinsi vinavyofanya kazi, ili tuelewe mahitaji yake, na tutekeleze sehemu yetu katika kuutunza mwili, ili usipate madhara na unajisi. [MH 271.1; HU Aya ya 1]

Mzunguko wa Damu

Ili kuwa na afya njema, ni lazima tuwe na damu safi; maana damu ndiyo mkondo wa maisha. Hurekebisha taka za mwili na kurutubisha mwili. Inapopata vipengele vyenye virutubisho au lishe sahihi kutoka kwenye chakula na inaposafishwa na kuhuishwa kwa kuwasiliana na hewa safi, naam, hubeba uhai na nguvu kwenye kila sehemu ya mfumo. Kadiri mzunguko unavyokuwa mzuri zaidi, ndivyo kazi hii inatekelezwa na kukamilishwa ipasavyo. [MH 271.2; HU Aya ya 2]

Katika kila mpigo wa moyo, damu inapaswa kutembea katika njia yake kwa haraka na urahisi kwenye sehemu zote za mwili. Mzunguko wake haupaswi kuzuiwa na nguo zinazobana au kifungo chochote (Kama mikanda, nywele zilizosukwa kwa kukaza, viatu vinavyobana, au kuweka mguu wako juu ya mguu mwingine kwa kuandika namba 4, au sehemu ya kiungo cha mwili kuegemea kitu kwa mbinyo mkali n.k), au kutokuwa na nguo za kutosha kwenye viungo vilivyo mbali na moyo kama vile miguu, mikono na kichwa wakati wa baridi. Chochote kinachozuia mzunguko wa damu hulazimisha damu kurudi kwenye viungo muhimu, na jambo hili husababisha msongamano wa damu kwa kuwa sehemu moja. Maumivu ya kichwa, kikohozi, moyo kupiga kwa jinsi isiyo ya kawaida,* au kuvembewa kwa kutokuwa na mmeng'enyo mzuri wa chakula, mara nyingi ni matokeo *(Palpitation ya moyo ni mapigo ya moyo yanayoruka mpigo, au yanakuwa ya ziada au yasiyo ya kawaida - ni aina ya mdundo wa moyo usio wa kawaida , au kwenda kasi sana, au polepole sana -arrhythimia. Hutokea wakati mawimbi ya umeme yanapowaka kutoka mahali

pasipofaa, na kwa wakati usiofaa, na kusababisha moyo kupiga nje ya mdundo wake wa kawaida). [MH 271.3; HU Aya ya 3]

Kupumua

Ili kuwa na damu nzuri au nzuri, ni lazima tupumue vizuri. Kuvuta pumzi yenye hewa safi kwa kina na kikamilifu, huyajaza mapafu kwa oksijeni, na kusafisha damu. Na kuipa damu rangi iliyo angavu na kuipa mkondo wa uzima kwenye kila sehemu ya mwili. Kupumua vizuri kunapunguza msongo wa mishipa, kwa kuituliza au kuibembeleza kwa namna fulani; hufanya mtu awe na hamu nzuri ya kula (bon appetite) na hufanya usagaji-chakula kuwa mkamilifu zaidi; na huleta usingizi wenye afya nzuri na wenye kuburudisha mwili. [MH 272.1; HU Aya ya 4]

Mapafu yanapaswa kuruhusiwa kutanuka na kuwa na uhuru mkubwa kwa kadiri iwezekanavyo. Uwezo wa utendaji kazi wa mapafu, unakuzwa kutokana na uhuru kwenye utendaji wake-na hivyo mapafu hayabanwi, na hivyo yanatanuka ipaswavyo; ikiwa mapafu yamebanwa au kufinywa kwa namna fulani, ufanisi wa kazi yake unakuwa mdogo sana. Kwa hivyo athari ya mazoea mabaya ambayo ni ya kawaida sana kwa watu wengi, haswa katika kukaa-kaa kwenye kiti kwa muda, au kuinamisha kichwa chini au kuelekea mbele au kuinama wakati mtu anafanya kazi huathiri sana mapafu. Katika mkao wa namna hii, haiwezekani kabisa kwa mtu kuvuta pumzi kwa undani. Kupumua juujuu kumekuwa mazoea ya watu wengi na kisha mapafu hupoteza uwezo wake wa kutanuka vizuri. Athari ile ile husababishwa na nguo zinazobana (*ambazo watu wa zamani hasa, walipenda kuzivaa ili kubana tumbo au kifua ili kionekane kidogo (corset au tight lacing), soma haya zaidi kwenye kitabu cha matengenezo katika mavazi, kama hauna tuandikie katika email: UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com).* Nafasi ya kutosha haitolewi kwenye sehemu ya chini ya kifua (diaphgram); misuli ya tumbo, ambayo iliumbwa kusaidia zoezi la kupumua, haichezichezi kikamilifu, kwa kwenda juu na chini, na kutanuka, na mapafu yanazuiwa katika utendaji wake. [MH 272.2; HU Aya ya 5]

Matokeo yake ni viungo kupokea ugavi usiotosha wa oksijeni. Damu hutembea kivivuvivu. Taka-mwili ambazo ni sumu sasa mwilini mwa mtu, ambazo kwa kawaida zingepaswa kutupwa nje wakati wa kutoa pumzi, au hewa kwenda nje kutoka kwenye mapafu, zinahifadhiwa, na damu inakuwa chafu. Sio tu mapafu, lakini pia tumbo, maini, na ubongo vinadhurika. Ngozi

inakuwa na rangi ya manjano au kahawia kuonyesha kwamba kuna shida ya afya, mmeng'enyo wa chakula unazorota; moyo unakuwa na huzuni; ubongo unajaa mawingu; mawazo yanapata mkanganyiko; giza au huzuni hutanda juu ya roho; mfumo mzima unakuwa na mfadhaiko kwa kukosa furaha na kutofanya kazi, na kushambuliwa kirahisi na magonjwa. [MH 273.1; HU Aya ya 6]

Muda wote, mapafu yanatoa nje uchafu kupitia kupumua hewa kwenda nje, na hivyo yanahitaji ugavi wa hewa safi wakati wote. Hewa chafu haitoi ugavi unaohitajika wa oksijeni, na damu hupita kwenye ubongo na viungo vingine bila kuwa na uhai au nguvu. Kwa hivyo hitaji la uingizaji hewa kikamilifu ni muhimu sana. Kuishi katika vyumba ambavyo vimefungwa madirisha, visivyo na hewa ya kutosha, mahali ambapo hewa ni mfu na imeharibiwa, hudhaifisha mfumo mzima. Katika hali ya baridi mfumo unakabiliana na mambo kwa unyeti sana, hivyo mfiduo/kuanikwa kudogo kwenye maambukizi fulani au hali ya hewa mbaya husababisha ugonjwa kirahisi sana. Kujifungia ndani ya nyumba siku nzima, ndiko ambako kunawafanya wanawake wengi wawe na rangi ya ngozi isiyonawiri vizuri, ngozi inakuwa imepauka na kupitia ngozi inaonekana kwamba hawana afya (ngozi ya mtu huonyesha afya yake, mfano kwa wazungu wao rangi ikiwa imekuwa haina pink yaani pale, inaonyesha damu haitembei inavyopaswa). Wanavuta hewa ileile wanayoitoa nje mle chumbani tena na tena mpaka inajazwa na sumu iliyotolewa nje kupitia kwenye mapafu na matundu ya vinyweleo, na hivyo uchafu hurejeshwa tena na tena kwenye damu. [MH 274.1; HU Aya ya 7]

Uvutaji hewa na mwanga wa jua

Katika ujenzi wa majengo ya nyumba za kuishi wanadamu, iwe kwa madhumuni ya umma au kama makazi ya watu, uangalifu mkubwa unapaswa kuchukuliwa ili kutoa uingizaji wa hewa mzuri na mwangaza wa jua mwingi. Makanisa na vyumba vya shule mara nyingi hufanya makosa katika suala hili. Kupuuza uingizaji hewa mzuri husababisha mtu kuchokachoka na kujisikia ana usingizi siku nzima na hata kuwa butu kiakili jambo ambalo lina athari ya kutosikia au kuelewa jumbe na mahubiri mengi yanayoendelea kutolewa makanisani na kufanya kazi ya mwalimu kuwa ngumu, isiyo na ufanisi au isiyoleta matunda yoyote. [MH 274.2; HU Aya ya 8]

Kwa kadiri inavyowezekana, majengo yote yanayokusudiwa kuwa makazi ya mwanadamu yanapaswa kuwekwa kwenye uwanda wa ardhi ulio juu, inayofanya maji yasisimame mahali pamoja, bali yatembee na kutiririka, na kutoka karibu na nyumba. Hii itahakikisha mazingira ya nyumba ni makavu na jambo hilo litazuia hatari ya vimelea au magonjwa yanayotokana na unyevunyevu na harufu mbaya ya uvundo wa maji yaliyosimama (miasma).

Jambo hili mara nyingi huchukuliwa kwa urahisi sana au kupuuzwa kabisa. Magonjwa yanayoendelea, magonjwa yenye hatari, na vifo vingi, hutokana na unyevunyevu kando ya makazi ya watu, na hewa mbaya ya nyumba zilizo bondeni ambazo, haziwezi kuondoa maji yaliyosimama inavyopaswa na hivyo madimbwi ya maji au unyevunyevu vinakuwa kwenye mazingira ya nyumba muda wote. [MH 274.3; HU Aya ya 9]

Katika ujenzi wa nyumba ni muhimu sana mjenzi aweke mfumo wa uingizaji mkamilifu wa hewa na jua jingi (ventilation). Hebu kuwe na mkondo wa hewa unaotembea muda wote na mwanga mwingi wa jua katika kila chumba ndani ya nyumba. Vyumba vya kulala vinapaswa kujengwa kwa namna ambayo mzunguko huru wa hewa utakuwepo mchana na usiku. Hakuna chumba kinachofaa kutumiwa kama chumba cha kulala isipokuwa kimeweza kuwa wazi kila siku ili kupitisha mwanga wa jua na hewa safi inayozunguka siku nzima. Katika nchi nyingi zenye majira ya baridi kali, vyumba vya kulala vinahitaji kupewa faraja ya joto kwa urahisi kwa ajili ya watu, ili vyumba vyote vipate joto na kuweza kukaushwa wakati wa misimu ya mvua nyingi zinazoleta unyevunyevu au ubaridi. [MH 274.4; HU Aya ya 10]

Chumba cha wageni nacho kiwekewe umakini sawa na vyumba vilivyokusudiwa kuwa vya matumizi ya kila wakati. Kama vyumba vingine vya kulala, chumba hiki kinapaswa kuwa na hewa na mwanga wa jua, na kinapaswa kuwa na njia fulani za kupokea joto ili kisivunde, na hivyo kusaidia kukausha unyevunyevu ambao hujilimbikiza kila wakati kwenye chumba ambacho huwa hakitumiki kila wakati. Yeyote anayelala katika chumba kisicho na jua, au analalia kitanda ambacho hakijakaushwa vizuri na chenye uwezo wa kuingiza hewa vizuri, hufanya hivyo kwa hatari ya afya yake mwenyewe, na mara nyingi hatari ya maisha yake (matandiko, magodoro, yatolewe nje yapate hewa mara kwa mara). [MH 275.1; HU Aya ya 11]

Katika ujenzi wa nyumba, wengi hufanya mikakati makini kwa mimea na maua yao (vitalu na sehemu ya kuvipanda). Greenhouse au dirisha linalotolewa kwa ajili ya kuweka mimea hii ili hupitisha vizuri joto, hewa na jua; kwani bila joto, hewa, na mwanga wa jua, mimea isingeishi na kunawiri au kusitawi. Ikiwa hali hizo ni muhimu kwa maisha ya mimea, je, si muhimu kwa ukubwa zaidi kwenye afya zetu wenyewe na familia zetu, pamoja na wageni wetu wanaotutembelea! [MH 275.2; HU Aya ya 12]

Ikiwa tungetaka nyumba zetu ziwe mahali ambapo afya na furaha inatamalaki, ni lazima tuziweke nyumba zetu juu ya maji yanayosimama kwa uvundo na ukungu wa nyanda za chini au mabonde, na kuwezesha uingiaji huru wa mawakala wanaotoa uzima wa mbinguni. Yaondoe mapazia mazito kwenye madirisha yako na kisha, fungua madirisha na yale mapazia ya plastiki

yanayofunguliwa na kufungwa kwa kamba (blinds) nayo yafungue pia, usiruhusu mimea yoyote inayotambaa juu ya ukuta izinge madirisha yako mwanga na hewa, haijalishi kwamba inapendeza macho kwa kiasi gani, wewe usiweke kivuli kwenye madirisha yako, na wala usiruhusu miti isimame karibu na nyumba yako kiasi cha kuzuia mwanga wa jua kwenye vyumba vyako. Mwangaza wa jua unaweza kufifisha rangi za mapazia na mazulia, na kufanya picha zako ulizotundika zipauke; lakini utaleta mng'ao wenye afya kwenye mashavu ya watoto wako (watanawiri ngozi yao). [MH 275.3; HU Aya ya 13]

Wale ambao wanatunza wazee na kuwasaidia katika shughuli mbalimbali, wanapaswa kukumbuka kwamba hawa wanahitaji vyumba vizuri na vyenye joto. Nguvu hupungua kadiri miaka inavyosonga kwa kwenda mbele, na hivyo kuacha nishati ndogo ya kustahimili ushawishi mbaya wa kiafya; Hivyo kunakuwa na ulazima mkubwa kwa wazee kuwa na mwanga mwingi wa jua, na hewa safi, na freshi. [MH 275.4; HU Aya ya 14]

Umakini mkubwa katika usafi wa kiakili ni muhimu kwa afya ya mwili na akili. Uchafu hutupwa nje kila mara kutoka mwilini kupitia kwenye ngozi. Mamilioni ya vinyweleo vya ngozi huziba haraka ikiwa haviwekwi safi kwa kuoga mara kwa mara, na uchafu ambao unapaswa kupita kwenye ngozi na kutoka, sasa unaziba ngozi, na kisha huwa mzigo wa ziada kwenye viungo vingine vya kuondoa taka-mwilini (kama vile figo, maini, mapafu n.k). [MH 276.1; HU Aya ya 15]

Watu wengi wangepata faida kutokana na kuoga maji ya baridi au ya vuguvugu kila siku asubuhi au jioni. Badala ya kuongeza riski ya kupata mafua na kikohozi, kuoga, kukifanywa kwa jinsi inavyofaa, huimarisha mwili dhidi ya magonjwa ya baridi kama vile mafua, kikohozi, pnemonia au fundo-fundo (tonsils), kwa sababu huboresha mzunguko wa damu na virutubisho vyake; damu huletwa juu ya uso wa ngozi, na mtiririko unaofanyika kwa urahisi na ulio wa kawaida huendelea kufanyika. Akili na mwili navyo pia vinachangamshwa kwa usawa. Misuli inakuwa inanyumbulika kwa urahisi zaidi, na akili inafanywa kuwa mahiri zaidi. Kuoga ni msaada unaoleta utulivu wa mishipa ya fahamu (Kuoga hubembeleza mishipa ya fahamu). Kuoga husaidia utumbo mkubwa, tumbo, na ini, na hutoa afya na nishati kwa kila kimoja cha viungo, na kukuza usagaji wa chakula. [MH 276.2; HU Aya ya 16]

Ni muhimu mavazi yawe safi. Nguo zilizovaliwa, hufyonza uchafu ambao hupita kwenye vitundu vya vinyweleo; na ikiwa nguo hizi hazibadilishwa mara kwa mara na kuoshwa, uchafu utafyonzwa kurudi tena kwenye mfumo wa mwili wa mvaaji nguo. [MH 276.3; HU Aya ya 17]

Kila aina ya uchafu huelekea kwenye magonjwa. Viini vya wadudu vinavyozalisha kifo lazima vipo katika giza, tena vimejaa katika kona za nyumba zilizopuuzwa, katika takataka zinazoozeana, katika unyevunyevu na ukungu na fangasi/kuvu. Usitupe mboga za aina yoyote au lundo la majani lisibaki karibu na nyumba yako na kuoza na hivyo kusumisha hewa. Hakuna kitu kichafu au kinachooza kinachopaswa kuvumiliwa ndani ya nyumba. Katika miji au majiji yanayoonwa kuwa yana afya kamilifu au tele, magonjwa mengi ya homa yamefuatiliwa na kuhusishwa na vitu vinavyooza, kwenye makao ya mwenye nyumba fulani asiyejali. [MH 276.4; HU Aya ya 18]

Usafi mkamilifu, mwanga mwingi wa jua, uangalifu na umakini katika usafi wa mazingira katika kila jambo la maisha ya nyumbani, ni muhimu katika kuwa huru kutokana na magonjwa na uchangamfu na nguvu za watu waliofungiwa ndani ya nyumba na hata wasiweze kutoka nje. [MH 276.5; HU Aya ya 19]

SURA YA 21

USAFI MIONGONI MWA WAISRAELI

Katika mafundisho ambayo Mungu aliwapa Wana Israeli, utunzaji wa afya ulizingatiwa kwa makini. Watu hawa ambao walikuwa wametoka utumwani wakiwa na tabia chafu na zisizosaidia afya au zile hatarishi kwa afya walipewa mafunzo makali zaidi nyikani kabla ya kuingia Kanaani. Walifundishwa kanuni za afya na sheria za usafi zilisisitizwa na kutekelezwa. [MH 277.1; HU Aya ya 1]

Je ni ukoma unaosumbua; ni unajisi. Basi ataliteketeza vazi hilo, kwamba ni lililofumwa au lililosokotwa, ikiwa ni la sufu, au la kitani, au kitu cho chote cha ngozi, ambacho ndani yake hilo pigo; kwa kuwa ni ukoma mbaya; itateketezwa kwa moto." Mambo ya Walawi 13:46-52. [MH 278.2; HU Aya ya 2]

4 Kitanda cho chote akilaliacho mwenye kisonono kitakuwa najisi; na kitu cho chote ambacho akiketia kitakuwa najisi.

5 Mtu ye yote atakayekigusa kitanda chake huyo, atazifua nguo zake, na kuoga mwili wake majini, naye atakuwa najisi hata jioni.

6 Na mtu atakayeketi katika kitu cho chote alichokiketia mwenye kisonono, atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni.

7 Na mtu atakayegusa mwili wake mwenye kisonono atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni.

8 Tena kama mwenye kisonono akimtemea mate mtu aliye safi; ndipo atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa yu najisi hata jioni.

9 Na tandiko lo lote atakalolipanda mwenye kisonono litakuwa najisi.

10 Mtu awaye yote atakayegusa kitu cho chote kilichokuwa chini yake huyo atakuwa najisi hata jioni; na mtu atakayevichukua vitu vile atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni.

11 Na mtu ye yote atakayeguswa na mwenye kisonono, asipokuwa amenawa mikono yake majini, atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni.

12 Na chombo cha udongo ambacho amekigusa mwenye kisonono, kitavunjwa-vunjwa; na kila chombo cha mti kitaoshwa majini.

46 Siku zote ambazo pigo li ndani yake, yeye atakuwa mwenye unajisi; yeye yu najisi; atakaa peke yake; makazi yake yatakuwa nje ya marago.

47 Tena, vazi nalo ambalo pigo la ukoma li ndani yake, kwamba ni vazi la sufu, au kwamba ni la kitani;

48 likiwa limefumwa, au kusokotwa; likiwa ni la kitani au la sufu; kwamba ni katika ngozi, au kitu cho chote kilichofanywa cha ngozi;

49 hilo pigo likiwa la rangi ya majani au jekundu, katika vazi, au katika ngozi, au katika lililofumwa, au katika lililosokotwa, au katika kitu cho chote cha ngozi; ni pigo la ukoma, nalo ataonyeshwa kuhani;

50 na kuhani ataliangalia hilo pigo, naye atakiweka mahali kile kilicho na pigo muda wa siku saba;

51 kisha siku ya saba ataliangalia hilo pigo; kama pigo limeenea katika hilo lililofumwa, au katika hilo lililosokotwa, au katika ngozi, ijapokuwa hiyo ngozi ina matumizi yo yote; hilo pigo ni ukoma unaokula; vazi hilo ni najisi.

52 Naye atalichoma moto vazi hilo, kwamba ni lililofumwa au kwamba ni lililosokotwa, kama ni la sufu, au la kitani, au kitu cho chote cha ngozi, ambacho kina hilo pigo ndani yake; kwa maana, ni ukoma unaokula; vazi hilo litachomwa moto;

Kwa hivyo pia, ikiwa nyumba ilitoa uthibitisho wa hali zinazoifanya kuwa isiyo salama kwa makazi, ilibomolewa. Kuhani alipaswa “kuibomoa nyumba, mawe yake, na miti yake, na chokaa yote ya hiyo nyumba; naye atavichukua nje ya mji mpaka mahali palipokuwa na uchafu. Tena yeye aingiaye ndani ya nyumba wakati huo iliofungwa, atakuwa najisi hata jioni. Na mtu alalaye ndani ya nyumba hiyo atazifua nguo zake; naye alaye chakula ndani ya nyumba hiyo atazifua nguo zake.” Mambo ya Walawi 14:45-47. [MH 278.3; HU Aya ya 3]

Usafi

Umuhimu wa usafi binafsi ulifundishwa kwa njia ya kuvutia zaidi. Kabla ya kukusanyika katika Mlima Sinai ili kusikiliza tangazo la sheria kwa sauti ya Mungu, watu walitakiwa kuosha nafsi zao na mavazi yao. Mwelekeo huu ulitekelezwa kwa penalti ya kifo. Hakuna uchafu uliopaswa kuvumiliwa mbele za Mungu. [MH 279.1; HU Aya ya 4]

Wakati wa kukaa nyikani, karibu kila mara Waisraeli walikuwa kwenye eneo la wazi, mahali ambapo uchafu ungekuwa na athari ndogo kuliko kwa wakazi walio ndani ya nyumba zilizofungwa milango na madirisha. Lakini umakini mkali katika usafi ulihitajika ndani na nje ya mahema yao. Hakuna takataka iliyoruhusiwa kubaki ndani au karibu na kambi. Bwana akasema: [MH 279.2; HU Aya ya 5]

“Kwa kua BWANA, Mungu wako, Yuatembea katika kituo akuokoe, na kuwatoa adui zako mbele yako; kwa hiyo na kiwe kitakatifu kituo chako; asije akaona kitu kwako kisichokuwa safi akageuka na kukuacha.” Kumbukumbu la Torati 23:14. [MH 280.1; HU Aya ya 6]

Mlo

Tofauti kati ya safi na najisi iliwekwa katika masuala yote ya chakula: [MH 280.2; HU Aya ya 7]

“Mimi ni Bwana, Mungu wenu, niliyewatenga ninyi na mataifa. Kwaajili ya hayo mtapambanua kati ya mnyama aliye safi na najisi, na ndege walio najisi na walio safi; wala msifanye nafsi zenu kuwa chukizo kwa njia ya mnyama, au kwa njia ya ndege, au kwa njia ya kitu, ambacho nchi imejaa nacho chochote nilichowatenga nanyi kuwa najisi.” Mambo ya Walawi 20:24, 25. [MH 280.3; HU Aya ya 8]

Vyakula vingi vilivyoliwa kwa uhuru mkubwa na wapagani waliowazunguka vilikatazwa kwa Waisraeli. Hatua hii haikufanyika kwa ubaguzi wa kiholela. Mambo yote yaliyokatazwa yalikuwa ni yale yasiyofaa. Na ile hali ya kutajwa kuwa najisi ilifundisha somo kwamba matumizi ya vyakula hivi vya kudhuru ni kujinajisi wenyewe. Kile kinachoharibu mwili wako, kinaelekea kuharibu roho pia. Kinamfanya yule anayetumia asiwe na uwezo unaofaa katika mawasiliano na Mungu, hafai kuwa katika huduma ya juu, na takatifu. [MH 280.4; HU Aya ya 9]

Katika Nchi ya Ahadi nidhamu iliyoanza nyikani iliendelezwa chini ya hali zinazofaa kwa kulea mazoea mazuri. Watu hawakusongamana pamoja katika majiji, lakini kila familia ilimiliki kipande cha ardhi ambayo ilitoa uhakikisho wa baraka zote zinazotoa afya za maisha ya asili yasiyopotoshwa. [MH 280.5; HU Aya ya 10]

Kuhusu matendo ya ukatili na uasherati wa Wakanaani, ambao waliondolewa kwenye makazi ya Israeli, Bwana alisema: [MH 280:6; HU Aya ya 11]

“Msiende katika desturi za taifa hili, niwafukuzao mbele yenu; kwa kuwa walifanya mambo haya yote, na kwa hiyo naliwachukia. Kifungu cha 23 . "Na machukizo usilete machukizo ndani ya nyumba yako, usitie ndani ya nyumba yako, usije wewe kuwa kitu cha haramu/ kilicholaaniwa mfano wake; ukichukie kabisa, na kukikataa kabisa; kwa kuwa ni kitu kilichoharimishwa." Kumbukumbu la Torati 7:26. [MH 280.7; HU Aya ya 12]

Katika shughuli zao zote kwenye maisha ya kila siku, Waisraeli walifundishwa somo lililowekwa wazi na Roho Mtakatifu: [MH 281.1; HU Aya ya 13]

“Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo; kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.” 1 Wakorintho 3:16, 17. [MH 281.2; HU Aya ya 14]

Kufurahi

"Moyo uliochangamka ni mzuri kama dawa." Mithali 17:22 . Moyo wa shukrani, furaha, ukarimu, tumaini katika upendo na utunzaji wa Mungu—hivi ndivyo ulinzi mkubwa wa afya. Kwa Waisraeli hivi vilipaswa kuwa ufunguo na kaulimbiu ya maisha. [MH 281.3; HU Aya ya 15]

Safari iliyofanywa mara tatu kwa mwaka kwenye sherehe za kila mwaka huko Yerusalemu, na kuishi kama wageni kwa juma moja kwenye vibanda wakati wa Sikukuu ya Vibanda, zilikuwa fursa za burudani nje nyumba na maisha ya kijamii. Sherehe hizi zilikuwa nyakati za furaha, zilizofanywa kuwa za kupendeza, na kufanywa kuwanyororo kwa ukaribishaji wa mgeni, Mlawi, na maskini kwa ukarimu. [MH 281.4; HU Aya ya 16]

“Ukayafurahie mema yote ambayo Bwana, Mungu wako, amekupa, na nyumba yako, wewe, na Mlawi, na mgeni aliye kati yenu.” Kumbukumbu la Torati 26:11. [MH 281.5; HU Aya ya 17]

Kwa hiyo, katika miaka ya baadaye, wakati sheria ya Mungu iliposomwa huko Yerusalemu kwa mateka waliorudi kutoka Babeli, kisha watu wakalia kwa sababu ya makosa yao, Maneno haya ya neema yalitamkwa: [MH 281:6; HU Aya ya 18]

“Msiomboleze.... Enendeni zenu, mle kilichonona, na kunywa kilicho kitamu, tena mpelekeeni sehemu yeye asiyewekewa kitu; kwa maana siku hii ni

takatifu kwa Bwana wetu; kwa kuwa furaha ya Bwana ni nguvu zenu." Nehemia 8:9, 10. [MH 281.7; HU Aya ya 19]

Na maneno haya yalitamkwa na wahubiri na kutangazwa kwenye mhadhara wa watu "katika miji yao yote, na katika Yerusalemu, kusema, enendeni mlimani, mkalete matawi ya mizeituni, na matawi ya mzeituni mwitu na mihadasi, na mitende, na matawi ya miti minene, ili kufanya vibanda, kama ilivyoandikwa. Basi watu wakatoka, wakavileta, wakajifanyia vibanda, kila mtu juu ya dari ya nyumba yake, na katika nyua zao, na katika nyua za nyumba ya Mungu, na katika mtaa wa Lango la Maji, na katika mtaa wa lango la Efraimu. Na mkutano wote wa watu waliorudi kutoka katika uhamisho vilifanyizwa vibanda, na watu wakakaa katika vibanda hivyo.... Pakawa na furaha kubwa sana." Mistari ya 15-17. [MH 282.1; HU Aya ya 20]

Mungu aliwapa Waisraeli maagizo katika kanuni zote muhimu kwa afya ya kimwili na kimaadili, na kanuni hizi za afya hazikuwa pungufu au chini ya sheria ya maadili ambazo Yeye pia aliwaagiza kuzitenda: [MH 283.1; HU Aya ya 21]

"Na Maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na utembeapo njiani, na ulalapo na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena uyaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako." Kumbukumbu la Torati 6:6-9. [MH 283.2; HU Aya ya 22]

"Na mwanao atakapokuuliza katika siku zijazo, akisema ni nini mashuhudizo, na amri na hukumu, ... Bwana alituamuru kuzifanya amri hizi zote, tumche Bwana, Mungu wetu, tuone mema siku zote, ili atuhifadhi hai kama hivi leo." Mistari ya 20-24. [MH 283.3; HU Aya ya 23]

Kama Waisraeli wangetii maagizo waliyopokea, na kunufaika na faida zake, hili lingekuwa somo kwa dunia kuhusu afya na ustawi. Ikiwa kama watu wangeishi kulingana na mpango wa Mungu, basi wangehifadhiwa kutokana na magonjwa ambayo yaliwatesa mataifa mengine. Wangekuwa na nguvu za kimwili na nguvu za akili kuliko watu wengine wowote duniani. Wangekuwa taifa lenye nguvu zaidi duniani. Mungu alisema: [MH 283.4; HU Aya ya 24]

"Utabarikiwa kuliko watu wote." Kumbukumbu la Torati 7:14. [MH 283.5; HU Aya ya 25]

"Naye Bwana amekuungama hivi leo kuwa taifa iliyotengwa iwe Yake Yeye, kama alivyokuahidi, na kuwa yakupasa kushika maagizo Yake yote;

na kuwa atakutukuza juu ya mataifa yote aliyoyafanya, kwa sifa, na jina, na heshima, nawe upate kuwa taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako, kama alivyosema." Kumbukumbu la Torati 26:18, 19. [MH 284.1; HU Aya ya 26]

"Na baraka hizi zote zitakujilia na kukupata usikiapo sauti ya Bwana, Mungu wako. Utabarikiwa mjini, utabarikiwa na mashambani. Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, maongeo ya ng'ombe wako, na wadogo wa kondoo zako. Litabarikiwa kapu lako na chombo chako cha kukandia chakula. Utabarikiwa uingiapo, na utabarikiwa utokapo." Kumbukumbu la Torati 28:2-6. [MH 284.2; HU Aya ya 27]

"Bwana ataiamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na katika yote utakayotia mkono wako; Naye atakubarikia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako. Bwana atakufanya kuwa taifa takatifu Kwake, kama alivyokuapia, utakaposhika maagizo ya Bwana, Mungu wako, na kutembea katika njia Zake. Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa Jina la Bwana; nao watakuwa na hofu kwako. Naye Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri, katika uzao wa tumbo lako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako, katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako kwamba atakupa. Bwana atakufunulia hazina yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati wake, na kubarikia kazi yote ya mkono wako..... Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini; utakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kufanya." Mistari ya 8-13. [MH 284.3; HU Aya ya 28]

Kwa Haruni kuhani mkuu na wanawe maagizo haya yalitolewa: [MH 285.1; HU Aya ya 29]

"Kwa njia hii mtawabariki wana wa Israeli, mkiwaambia, [MH 285:2; HU Aya ya 30]

"BWANA akubarikie, na kukulinda;

BWANA akuangazie nuru za uso Wake,

na kukufadhili;

BWANA akuinulie uso Wake,

na kukupa amani.

Ndivyo watakavyoweka Jina Langu juu ya wana wa Israeli;

Nami nitawabarikia." [MH 285.3; HU Aya ya 31]

"Kadri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako.

Hapana aliyefanana na Mungu, Ee Yeshuruni,

Ajaye amepanda juu ya mbingu ili akusaidie,

Na juu ya mawingu juu ya utukufu Wake.

Mungu wa milele ndiye makazi Yako,

Na mikono ya milele I chini yako…..

Israeli anakaa salama,

Chemchemi ya Yakobo peke yake, [MH 285:4; HU Aya ya 32]

“Katika nchi ya ngano na divai;

Naam, mbingu zake zadondoza umande.

U heri wewe, Ee Israeli,

ni nani aliye kama wewe, taifa lililookolewa na Bwana

Ndio ngao ya msaada Wako,

Na upanga wa utukufu Wako! Hesabu 6:23; 6:24-27, ARV; Kumbukumbu la Torati 33:25-29, RV [MH 285.5; HU Aya ya 33]

Waisraeli walishindwa kutimiza kusudi la Mungu, na hivyo kushindwa kupokea baraka ambazo zingeweza kuwa zao. Lakini katika Yusufu na Danieli, katika Musa na Elisha, na wengine wengi, tuna mifano bora ya matokeo ya mpango halisi na wa Kweli wa kuishi. Uaminifu wa leo utaleta matokeo kama hayo. Kwetu imeandikwa: [MH 285.6; HU Aya ya 34]

“Ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu; mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu.” 1 Petro 2:9. [MH 286.1; HU Aya ya 35]

"Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana,

Ambaye Bwana ni tumaini lake."

“Mwenye haki atasitawi kama mtende;

Atakuwa kama mwerezi wa Lebanoni.

Waliopandwa katika nyumba ya Bwana

Waliopandwa katika nyumba ya Bwana Watastawi katika Nyua za Mungu wetu.

Watazaa matunda hadi wakati wa uzee, watajaa utomvu, watakuwa na ubichi.”

"Watakuwa na nguvu na kufunikwa na majani." [MH 286.2; HU Aya ya 36]

"Moyo wako uzishike amri zangu; Maana

zitakuongezea wingi wa siku, na maisha marefu, Na amani."

“Ndipo utakapokwenda katika njia yako salama,

Wala mguu wako hautajikwaa.

Ulalapo, hutaona hofu;

Naam, utalala, na usingizi wako utakuwa mtamu.

Usiogope hofu ya ghafula,

Wala uharibifu wa waovu utakapofika.

Kwa kuwa Bwana atakuwa tumaini lako,

Naye atakulinda mguu wako usinaswe." Yeremia 17:7; Zaburi 92:12-14; 92:14; Mithali 3:1, 2, 23-26. [MH 286.3; HU Aya ya 37]

SURA YA 22

MAVAZI

Biblia inafundisha kuwa na kiasi katika mavazi. “Vivyo hivyo wanawake wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri.” 1 Timotheo 2:9. Hii inakataza maonyesho katika mavazi, rangi zinazongaa ambazo zinapoteza ladha nzuri, au kufanya utazamwe sana endapo unaweka mapambo mengi. Mbinu yoyote inayowekewa mkakati ili kuvuta macho kwa mvaaji au kusisimua, haijumuishwi katika vazi la kiasi ambalo Neno la Mungu linaamuru (kila tunapovaa tujiulize, je navaa kwa utukufu wa Mungu vazi langu hili leo). [MH 287.1; HU Aya ya 1]

Mavazi yetu yanapaswa kuwa yale yasiyo na gharama kubwa—hayatakiwi yawe na “dhahabu, au lulu, au mavazi ya gharama kubwa.” Kifungu cha 9. [MH 287.2; HU Aya ya 2]

Fedha ni amana kutoka kwa Mungu. Sio zetu kuzitumia kwa ajili ya kutosheleza kiburi au tamaa za kimwili. Mikononi mwa watoto wa Mungu,

fedha ni chakula kwa wenye njaa, na nguo kuwavika wahitaji walio uchi. Ni ulinzi kwa walioonewa, njia ya afya kwa wagonjwa, njia ya kuhubiri injili kwa maskini. Unaweza kuleta furaha kwenye mioyo ya watu wengi kwa kutumia kwa hekima fedha au njia ambazo sasa zinatumika kwa ajili ya maonyesho. Fikiria maisha ya Kristo. Jifunzeni tabia Yake, na mshiriki Naye katika kujikana nafsi Kwake. [MH 287.3; HU Aya ya 3]

Katika ulimwengu unaodai kuwa wa Kikristo vito na mavazi ya bei ghali hunuliwa na fedha ambazo zingeweza kuwalisha watu wote wenye njaa na kuwavisha wale walio uchi. Mitindo na kujionyesha huchukua nafasi na fedha zinazoweza kuwafariji maskini na watu wanaoteseka. Wanaiibia dunia injili ya upendo wa Mwokozi. Misheni inadhoofika. Umati wa watu wanaangamia kwa kukosa mafundisho ya Kristo. Kando ya milango yetu wenyewe na katika nchi za kigeni wapagani hawajafunzwa na hawajaokoka. Ijapokuwa Mungu ameikirimia dunia kwa fadhila Zake na kuzijaza ghala Zake kwa starehe za maisha, huku akiwa ametupatia bure maarifa ya kuokoa ya Ukweli Wake, ni udhuru gani sisi tunaweza kutoa kwa kuruhusu vilio vya wajane na yatima? wagonjwa na wanaoteseka, watu wasiofundishwa na wasiookoka, ili wawe tayari kupaa na kwenda mbinguni? Katika siku ya Mwenyezi Mungu, wanapokutana uso kwa uso na Yeye ambaye alitoa maisha Yake kwa ajili ya wahitaji hawa, Je, ni udhuru gani watatoa wale ambao wanatumia muda na fedha zao kwa ajili ya kuendekeza na kujifurahisha na vitu ambavyo Mungu amekataza? Kwa watu kama hao Kristo hatasema, “Nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha;… hukunitembelea Mimi”? Mathayo 25:42, 43. [MH 287.4; HU Aya ya 4]

Lakini mavazi yetu, ingawa ni ya kiasi na sahili, yanapaswa kuwa na ubora mzuri, yenye rangi nyingi, na yafae kwa utumishi. Yanapaswa kuchaguliwa kwa uimara badala ya kujionyesha kwa watu. Yanapaswa kutoa joto na kumlinda mtu kwausahihi. Mwanamke mwenye hekima anayetajwa katika Mithali “hawahofii theluji watu wa nyumbani mwake; Methali 31:21 , pambizo. [MH 288.1; HU Aya ya 5]

Mavazi yetu yanapaswa kuwa safi. Uchafu katika mavazi hauna afya, na unapelekea unajisi mwili na roho. "Ninyi ni hekalu la Mungu .... Mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu." 1 Wakorintho 3:16, 17. [MH 288.2; HU Aya ya 6]

Katika mambo yote, mavazi yanapaswa kuwa yenye afya. “Zaidi ya mambo yote,” Mungu anatamani tuwe “katika afya”—afya ya mwili na nafsi. Nasi tunapaswa kuwa watenda kazi pamoja Naye kwa afya ya roho na mwili pia. Yote mawili yanakuzwa kwa mavazi yenye afya. [MH 288.3; HU Aya ya 7]

Inapaswa kuwa yenye staili nzuri ya kupendeza, uzuri wa kufaa wa usahili wa asili. Kristo ametuonya dhidi ya kiburi cha uzima, lakini sio dhidi ya neema Yake na uzuri wa asili. Alielekeza kwenye maua ya shambani, kwenye yungiyungi linalokunjuka katika usafi wake, na kusema, “Hata Sulemani katika fahari yake yote hakupambwa kama mojawapo la hayo. Mathayo 6:29 . Hivyo kwa mambo ya asili Kristo ameonyesha uzuri ambao mbingu inathamini, neema ya kiasi, usahili, usafi, kufaa, ambavyo vingefanya vazi letu kumpendeza. [MH 289.1; HU Aya ya 8]

Yeye anatuamuru Nguo nzuri zaidi tuzivae juu ya roho zetu. Hakuna kujipamba kokote kwa nje ambako kunaweza kulinganishwa kwa thamani au kunakopendeza zaidi ya ile “roho ya upole na utulivu” ambayo ni ya “thamani kuu” machoni Pake. 1 Petro 3:4. [MH 289.2; HU Aya ya 9]

Kwa wale wanaozifanya kanuni za Mwokozi kuwa mwongozo wao, Maneno haya ya thamani kutoka kwenye Yake ahadi Zake, yatakuwa na thamani kwa kiasi kikubwa: [MH 289.3; HU Aya ya 10]

“Na mavazi, ya nini kuyasumbukia?Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti vizuri kama mojawapo la hayo. Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yalivyo. Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?...Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini? Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa. Mathayo 6:28-33, [MH 289.4; HU Aya ya 11]

"Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Wewe katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini Wewe." Isaya 26:3. [MH 289.5; HU Aya ya 12]

Ni tofauti iliyoje ukilinganisha na uchovu, machafuko, ugonjwa, unyonge na uangamivu, unaotokana na utawala wa mitindo au fasheni! Mitindo ya leo iko kinyume kabisa kwa kiasi gani na kanuni zinazotolewa katika Maandiko, au zile ambazo Maandiko yanatuagiza! Fikiria mitindo ambayo imeshamiri kwa mamia ya miaka iliyopita au hata kwa miongo michache iliyopita. Ni mitindao mingapi kati yao, wakati haiko katika kilele cha mtindo au fasheni, bado ingetangazwa kuwa ni yenye kustahi, yenye kusitiri au yenye adabu; ni mingapi kati ya mitindo hii, ambayo ingetamkwa kuwa haifai kabisa kwa mwanamke ambaye amesafishwa (au mwenye usafi wa moyo), mwanamke mcha Mungu, na mwenye kujiheshimu mwenyewe. [MH 289.6; HU Aya ya 13]

Kufanya mabadiliko kwenye mavazi yako eti kwaaajili ya kuendana na mtindo tu hakukubaliwi na Neno la Mungu. Kubadilisha mitindo mbalimbali ya

nguo na mapambo yenye kinagaubaga au kina (details), yenye gharama kubwa hupoteza wakati na fedha za matajiri, na kupoteza nguvu za akili na nafsi. Mitindo hushinikiza mzigo mzito kwa watu wa tabaka la kati na maskini. Wengi ambao hawawezi kupata riziki, na ambao kwa njia sahili wanaweza kujitengenezea mavazi yao wenyewe, sasa wamelazimika kuwageukia washonaji ili tu waendane na mtindo. Wasichana wengi maskini, kwa ajili ya kujipatia gauni maridadi lililo katika fasheni, wamejinyima nguo za ndani ambazo zingewapa joto, na kulipa kwa adhabu, maisha yao yote. Wengine wengi, wakitamani maonyesho na umaridadi wa matajiri, wamevutwa kwenye njia za kukosa uaminifu na aibu. Nyumba nyingi hukosa faraja au mahitaji muhimu, wanaume wengi wanasukumwa na ubadhirifu au kufilisika, ili kukidhi matakwa ya ubadhirifu wa mke au watoto. [MH 290.1; HU Aya ya 14]

Wanawake wengi, wakiwa wamelazimishwa kujitayarisha wenyewe au watoto wao kwa mavazi ya umaridadi yaendanayo na mitindo, wameadhibiwa kwa uchungu usio na mwisho (wanachukua muda mwingi sana kushona hizi nguo zenye marembo na mambo mengi ya kina). Akina mama wengi walio na mishipa ya fahamu yenye maumivu (neuralgia) na vidole vinavyotetemeka hufanya kazi ngumu hadi usiku wa manane ili tu kuongeza urembo kwenye mavazi ya watoto wao ambayo hayasaidii chochote katika kuwa na afya njema, faraja, au urembo halisi. Kwa ajili ya mitindo au fasheni, yeye hudhabihu afya na utulivu wa roho, vitu ambavyo ni muhimu sana katika kuwapa mwongozo sahihi watoto wake. Ukuzaji wa akili na moyo hupuuzwa. Roho zao huwa mbilikimo (mambo ya kiroho ni dhaifu). [MH 290.2; HU Aya ya 15]

Mama hana wakati wa kusoma kanuni za ukuaji wa mwili, ili ajue jinsi ya kutunza afya za watoto wake. Anakuwa hana wakati wa kuhudumia mahitaji ya watoto ya kiakili au ya kiroho, hana wakati wa kuonyesha huruma katika hali zao za kukatishwa tamaa kudogo na majaribu yao kama watoto, au kushiriki katika mambo wanayoyapenda na kuonyesha shauku katika shughuli zao. [MH 291.1; HU Aya ya 16]

Mara tu watoto wanapokuja ulimwenguni, wanawekwa chini ya ushawishi wa mitindo (blanketi la watoto, soksi zao, kusukwa nywele, kitanda, kofia, viatu vifanane na visiwe vya zilipendwa.) Wanasikia zaidi mambo ya mavazi kuliko kuhusu Mwokozi wao. Wanawaona mama zao wakizungumzia na kuangalia masahani yanayoongoza kwenye mitindo au hata picha za mitindo mbali mbali ya mishono, kwa bidii zaidi kuliko Biblia (fashion plates na dress catalogues designs). Maonyesho ya mavazi yanachukuliwa kuwa ya umuhimu zaidi kuliko maendeleo ya tabia. Wazazi na watoto wameibiwa kile ambacho ni bora, chema na cha kweli maishani. Kwaajili ya mambo ya mitindo

wanatapeliwa wasifanye maandalizi ya maisha yajayo, maisha ya umilele. [MH 291.2; HU Aya ya 17]

Adui wa mema yote ndiye aliyechochea uvumbuzi wa mitindo inayobadilika kila kukicha. Yeye hupenda chochote kile ambacho kinaleta huzuni na fedheha kwa Mungu kwa kuleta taabu na uharibifu kwa wanadamu. Moja ya njia ambayo yeye hufanikisha lengo lake hili kwa ufanisi zaidi ni mada ya mitindo ambayo inadhoofisha mwili na kudhoofisha akili na kuidhalilisha roho pia. [MH 291.3; HU Aya ya 18]

Wanawake wanakabiliwa na magonjwa mazito, na mateso yao huongezeka zaidi kwaajili ya aina ya mavazi yao. Badala ya kuhifadhi afya zao kwa ajili ya dharura ambazo huwa changamoto kubwa kukabiliana nazo na ambazo hakika zitakuja, wao kwa mazoea yao mabaya mara nyingi hudhabihu si afya tu bali uhai, na kuwaachia watoto wao urithi wa misiba/ole katika mwili/katiba ulioharibika, mazoea potovu, na mawazo bandia kuhusu maisha (maisha feki). [MH 291.4; HU Aya ya 19]

Mojawapo ya vitu vyenye upotevu na ubaya katika mitindo ni sketi inayofagia barabara (refu sana walivaa wanawake wa enzi hizo, na ilikuwa na kiuno cha kubana sana, iliitwa hoop skirts, na gagulo la chuma, soma kitabu cha Kingereza au Kiswahili kuhusu matengenezo ya mavazi, kama huna tuandikie tutakutumia). Hii sketi refu yenye shepu ya mwavuli, inazoa uchafu wa njiani, haileti faraja kuivaa (haina comfort), inabughudi, inaumiza afya— yote haya na mengine zaidi ni ya kweli kuhusu hizi sketi zinazoburuza chini. Imepitiliza kwa namna mbili, kwanza kitambaa kikubwa kinatumika kuishona na kisha kuchanika na kuharibika kwa sababu ya urefu wake. Na mtu yeyote ambaye amemwona mwanamke katika sketi sketi hii inayoburuza au kufagia barabara, akiwa na vifurushi vingi mikononi mwake na akijaribu kupanda au kushuka ngazi, au kuingia kwenye gari la abiria kwenye usafiri wa umma kama daladala au matatu, na jinsi anavyopita katikati ya umati wa watu, au hata kutembea wakati mvua inanyesha au kwenye barabara ya matope, hahitaji kuvaa hii sketi au ahitaji ushahidi mwingine kuona jinsi usumbufu, bughuda na kukosa raha kwa huyu mama kulivyo. [MH 291.5; HU Aya ya 20]

Uovu mwingine mkubwa ni uvaaji wa sketi ya mwamvuli ambayo ni kubwa na uzito wake wote unahimiliwa na kiuno na makalio. Gauni hili ni zito, nalo hukandamiza viungo vya ndani, na kuviburuta chini, na hivyo kusababisha udhaifu wa tumbo na kuleta hisia ya udhaifu na kumfanya mvaaji kuinama, jambo ambalo hukandamiza zaidi mapafu, na kufanya upumuaji sahihi kuwa mgumu zaidi. [MH 292.1; HU Aya ya 21]

Katika miaka ya hivi majuzi, hatari zinazotokana na mgandamizo wa kiuno zimejadiliwa kikamilifu kiasi kwamba ni wachache sana wanaweza kuzivaa, naam, wanaweza kuwa wajinga kuhusu hizi sketi; lakini nguvu ya mtindo ni kubwa sana hivi kwamba uovu huu unazidi kuendelea. Kwa kitendo hiki, wanawake na wasichana wadogo wengi hujiletea madhara yasiyoelezeka. Ni muhimu kwa afya kwamba kifua kiwe na nafasi ya kutanuka hadi kufikia kiwango chake kamili cha utanukaji, ili mapafu yawezeshwe kuchukua kwa ukamilifu hewa inayovutwa ili kuingia ndani ya mapafu kupitia mdomo na pua. Wakati mapafu yamezuiwa kutanuka inavyopaswa, kiasi cha oksijeni kinachopokelewa ndani ya mwili hupunguzwa na kuwa kidogo (ujazo mdogo). Damu hailishwi kwa jinsi ipasavyo, na taka-mwili na dutu zenye sumu ambazo zinapaswa kutupwa nje kwa kupitia mapafu au ngozi, huhifadhiwa ndani ya mwili. Mbali na hayo mzunguko wa damu unazorota na kuwa na changamoto, na viungo vya ndani vinakuwa vimebanwa sana na kusongamana mahali ambapo kwa kawaida si nafasi yake, na hivyo haviwezi kufanya kazi yake ipasavyo. [MH 292.2; HU Aya ya 22]

Corset au nguo ya ndani iliyo kama vest inayobinya kifua na tumbo, haisaidii kufanya umbo au shepu ya mtu iwe nzuri (google corset). Moja ya vipengele vikuu katika uzuri wa kimwili ni ulinganifu, uwiano au usawa wa sehemu za mwili, yaani kushoto na kulia kwenye umbo la mtu vifanane (symmetry), upande mmoja usiwe mkubwa kuliko mwingine. Na kielelezo sahihi cha ukuaji wa kimwili kinaweza kupatikana, sio katika takwimu zinazoonyeshwa na madisaina wa nguo za fasheni huko Ufaransa, bali katika umbo la mwanadamu linalokuzwa kulingana na sheria za Mungu katika asili. Mungu Ndiye Mwasisi wa uzuri wote halisi, yaani ulio wa kweli, na tunapopatana na ukamilifu Wake ndipo tunapokuwa tumekaribia kiwango cha uzuri wa Kweli. [MH 292.3; HU Aya ya 23]

Uovu mwingine ambao desturi inakuza ni ugawaji usio sawa wa mavazi, yaani, wakati baadhi ya viungo vya mwili vimevunikwa kwa nguo zaidi ya inavyotakiwa, viungo vingine havijavikwa kabisa, au vimevikwa kwa udogo. Miguu na mikono iko mbali na viungo muhimu kama vile moyo, na mapafu, na inapaswa kulindwa hasa kutokana na baridi kwa kuwekewa nguo za kutosha (mbali na moyo ikimaanisha vigumu zaidi kufikiwa na damu, virutubisho, oxygen nk ukilinganisha na viungo karibu na moyo). Haiwezekani kuwa na afya wakati viungo vilivyo mbali na moyo vinakuwa na baridi; kwa maana ikiwa kuna damu kidogo ndani ya hivi viungo, kutakuwa na damu nyingi katika sehemu nyingine za mwili. Afya kamili inahitaji mzunguko wa damu mkamilifu; lakini hii haiwezekani wakati kuna nguo mara tatu au nne zaidi juu ya viungo muhimu, na hakuna nguo yoyote inayofunika miguu na mikono. [MH 293.1; HU Aya ya 24]

Wanawake wengi wana wasiwasi, uchovu na masumbufu kwa sababu wanajinyima hewa safi ambayo ingetengeneza damu safi, na kufanya utembeaji wa damu kwenye mishipa uwe huru na hivyo kuingia kwenye hatari ya kutoa uhai, afya, na nguvu zao. Wanawake wengi wamethibitishwa kuwa walemavu wakati ambapo wangeweza kufurahia afya, na wengi wamekufa kwaajili ya magonjwa ya mishipa ya fahamu na kifua kikuu (consumption) na magonjwa mengine wakati wangeweza kuishi maisha marefu ambayo walipangiwa kuwa nayo kama tu wangevaa kulingana na kanuni za afya na kufanya mazoezi kwa uhuru katika hewa ya wazi. [MH 293.2; HU Aya ya 25]

Ili kupata mavazi yenye afya zaidi, mahitaji ya kila sehemu ya mwili lazima yatanyiwe utafiti kwa uangalifu. Hali ya hewa mahali ulipo, mazingira, hali ya afya, umri, na kazi, vyote hivi lazima vizingatiwe kwani vinachangia sehemu kubwa. Kila kipande cha vazi kinapaswa kutosha sehemu kinapovaliwa kwa urahisi, ili kisizuie mzunguko wa damu kuwa kamili, au mtu asishindwe kupumua kwa uhuru kama mwanadamu alivyoumbwa kupumua kwa asili. Kila kipande cha vazi kinachovaliwa kinapaswa kisibane hivi kwamba wakati mikono imeinuliwa mavazi yatainuliwa pia, bila ya kuzuiwa au kupasuka. [MH 293.3; HU Aya ya 26]

Wanawake walio katika hali duni ya afya wanaweza kujifanyia mengi ili kujisaidia wenyewe, kwa kuvaa kwa busara na kufanya mazoezi. Wakiwa wamevalia kwa jinsi inavyofaa kwa ajili ya kufurahia mazingira ya nje, hebu wafanye mazoezi kwenye hewa wazi, wakichukua tahadhari mwanzoni, lakini wakiendelea kuongeza kiasi cha mazoezi kadri wanavyoweza kustahimili. Kwa kufuata mwenendo huu, wengi wanaweza kurejesha afya yao tena na kuishi kwa afya, na kuendelea kushiriki katika kazi za ulimwengu huu. [MH 293.4; HU Aya ya 27]

Kujitegemea kwa Mitindo

Badala ya kujitahidi kukidhi mahitaji ya mitindo, hebu wanawake wenyewe wawe na ujasiri wa kuvaa kwa afya na kwa usahili. Badala ya kutindikiwa na kuhenyeka tu na kazi za nyumbani, hebu mke na mama achukue wakati wake kusoma pia, kujitunza vizuri, kuwa mwandamani wa mume wake, na kuwasiliana na akili zinazokua za watoto wake. Hebu atumie fursa alizo nazo kwa busara sasa ili aweze kuwashawishi wapendwa wake kwaajili ya maisha ya juu zaidi. Hebu achukue muda kumfanya Mwokozi mpendwa kuwa mwandani wake wa kila siku, na rafiki wa karibu, ambaye anamfahamu vizuri. Hebu achukue muda kwa ajili ya kujifunza Neno Lake, na kuchukua muda wa kwenda na watoto wake mashambani, na nje ya mji na kujifunza kutoka kwa Mungu kupitia uzuri wa kazi Zake. [MH 294.1; HU Aya ya 28]

Hebu aendelee kuwa mcheshi, mwenye furaha, na asiye na wasiwasi kila mara. Badala ya kutumia kila wakati kushona nguo bila kufikia mwisho wa kazi yake, aifanye kila jioni kuwa msimu wa kupendeza wa kijamii (social), aweke mkakati wa familia kukutana pamoja baada ya majukumu ya siku. Kwa njia hii, wanaume wengi wataongozwa kuchagua jamii ya nyumbani kwao kabla ya ile ya klabu au baa ya pombe. Wavulana wengi wangenyanguliwa kutoka kwenye kukaa katika kona za mitaani na karibu na maduka (kijiweni). Wasichana wengi wangeokolewa kutoka kwenye magenge ya marafiki wenye kuwapotosha na mambo ya kipuuzi yasiyokuwa na 'kichwa wala miguu', au yasiyokuwa na ajenda za maana zinazomjenga mwanadamu. Mvuto wa nyumbani ungekuwa kwa wazazi na watoto jinsi ambavyo Mungu amepanga iwe, baraka ya maisha yote kwa wanachama wote wa familia. [MH 294.2; HU Aya ya 29]

Soma zaidi Isaya 3:18-23, 1 Timotheo 2:9 na 1 Petro 3:3

SURA YA 23

LISHE NA AFYA

Miili yetu inajengwa kutokana na chakula tunachokula. Kuna kuzeeka au hata kufa kwa tisho za mwili mara kwa mara (seli hufa kila baada ya wiki kadhaa na nyingine hutengenezwa); kila mjongeo wa kila kiungo/ogani unajenga taka-mwili, na taka hizi hutoka kwenye chakula chetu baada ya mmeng'enyo. Kila kiungo cha mwili kinahitaji sehemu yake ya lishe. Ubongo lazima upewe sehemu yake ya virutubisho; mifupa, misuli, na mishipa hudai

lishe yao pia. Hakika huu ni mchakato wa ajabu, unaogeuza chakula kuwa damu na kutumia damu hii kama matofali ya kujenga, na kukarabati sehemu mbalimbali za mwili; na mchakato huu unaendelea daima kwenye miili yetu 24/7, ukitoa uhai na nguvu kwenye kila neva, msuli, na tishu. [MH 295.1; HU Aya ya 1]

Jinsi ya Kuchagua Chakula Cha Kula

Vyakula mtu anavyopaswa kutumia ni vile ambavyo vinasambaza kwa ubora vipengele/virutubisho vile vinavyohitajika kwa ajili ya kuujenga mwili. Katika uchaguzi huu, hamu au tamaa tu ya chakula sio mwongozo salama. Kupitia mazoea mabaya ya kula, hamu ya kula inapotoka. Mara nyingi hudai chakula ambacho huharibu afya ya mwili na kusababisha udhaifu badala ya nguvu. Hatuwezi kuongozwa salama na desturi za jamii. Ugonjwa na mateso ambayo kila mahali yameshamiri vimetokana na makosa maarufu na yanayopendwa na wengi kuhusu lishe-chakula au milo tunayokula. [MH 295.2; HU Aya ya 2]

Ili kujua ni vyakula gani vilivyo bora zaidi, ni lazima tujifunze mpango wa asili wa Mungu wa lishe kwa mwanadamu Mwanzo 1:29. Yeye aliyemuumba mwanadamu na anayeelewa mahitaji Yake alimteulia Adamu chakula chake. “Tazama,” akasema, “nimewapa kila mche utoao mbegu, ….. na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; itakuwa chakula chenu. Mwanzo 1:29, Baada ya kuondoka Edeni ili kujitafutia riziki yake kwa kulima ardhi chini ya laana ya dhambi, mwanadamu alipewa ruhusa ya kula pia “mboga za kondeni.” Mwanzo 3:18. [MH 295.3; HU Aya ya 3]

Nafaka, matunda, njugu, na mboga-mboga hutengeza lishe tuliochaguliwa na Muumba wetu. Vyakula hivi, vikitayarishwa kwa njia sahili na ya asili kwa kadri iwezekanavyo, ndivyo vyenye afya na lishe zaidi kuliko vingine (sio kwa kukaanga nk). Vinatoa nguvu, uwezo wa kustahimili, na nguvu ya akili ambayo haipatikani katika chakula kilichokobolewa na kusindikwa na kile ambacho kinasisimua mwili. [MH 296.1; HU Aya ya 4]

Lakini sio vyakula vyote ambavyo havijakobolewa au kusindikwa ndivyo vyenye afya na kwa vyenyewe ndiyo vinafaa kwa mahitaji yetu katika hali zote. Uangalifu unapaswa kuchukuliwa katika uteuzi wa chakula. Lishe yetu inapaswa kuendana na msimu, hali ya hewa tunapoishi, na kazi tunayofanya. Baadhi ya vyakula ambavyo vinaendana na msimu mmoja kwa matumizi au katika hali ya hewa moja havifai kwa matumizi kwenye msimu mwingine au hali hewa nyingine. Kwa hivyo kuna vyakula tofauti vinavyofaa zaidi kwa watu wanaofanya kazi tofauti. Mara nyingi chakula ambacho kinaweza kutumika kwa kunufaisha wale wanaofanya kazi nzito za mikono, huwa hakifai kwa watu wenye shughuli za kukaa muda wote ofisini au kutumia sana akili kuliko

kazi za mikono. Mungu ametupatia aina mbalimbali za vyakula vyenye afya, na kila mtu anapaswa kuchagua kutoka humo kile ambacho uzoefu na maamuzi yenye busara huthibitisha kuwa kinafaa zaidi kwa mahitaji yake binafsi. [MH 296.2; HU Aya ya 5]

Ugavi mwingi wa mazao ambayo asili hutoa, pamoja na karanga, na nafaka za kutosha, na mwaka baada ya mwaka mazao ya nchi zote husambazwa kwa ujumla kwa wote, kwaajili ya ongezeko la njia za usafirishaji. Matokeo yake ni kuwa, vyakula vingi ambavyo miaka michache iliyopita vilizingatiwa kama anasa/lakshari kwa vile ni vya bei ghali, sasa vinaweza kupatikana kwa wote kama vyakula vya matumizi ya kila siku. Hii ni kweli hasa kuhusiana na matunda yaliyokaushwa na ya makoponi (wakati wao ilikuwa vigumu kuona ndizi au machungwa na vile ambavyo vilitoka kwenye nchi za tropiki). [MH 297.1; HU Aya ya 6]

Njugu na vyakula vya jamii ya karanga na zinakuja na kutumika kwa kiasi kikubwa sasa, vikichukua nafasi ya nyama, samaki, mayai na maziwa. Karanga zinaweza kutengenezwa kwenye mlo mmoja pamoja na nafaka, matunda, na baadhi ya vyakula vya mizizi, ili kufanya chakula kuwa na afya na lishe bora zaidi. Umakini unapaswa kuchukuliwa, hata hivyo, kwa kutotumia kiasi kikubwa cha jamii ya karanga (kiganja kimoja cha mkono!). Wale wanaotambua madhara yatokanayo na matumizi yanayopitiliza ya vyakula vya jamii ya karanga, wanaweza kuona kwamba ugumu huu huondolewa kwa kuzingatia tahadhari hii, (yaani usile karanga au jamii ya karanga kwa kiasi kikubwa zaidi ya kiganja chako cha mkono kwa siku maana unafanya kazi ya tumbo iwe ngumu na itakupa shida). Ikumbukwe pia kwamba jamii ya karanga zingine zina lishe bora zaidi ukilinganisha na jamii zingine za karanga. Lozi zina lishe bora kuliko njugu, lakini ukitumia njugu kwa kiasi kidogo, kwa kuzichanganywa na nafaka, zina lishe nzuri na pia huhamasisha mmeng'enyo (Baadhi ya jamii za karanga na mbegu ambazo zinalimwa Afrika Mashariki ni nazi, korosho, njugu, mbegu za maboga, ufuta, kweme, alzeti, makadamia nk). [MH 298.1; HU Aya ya 7]

Wakati matunda ya mizeituni yanatumiwa vizuri kama karanga, basi huchukua sehemu ya siagi na vyakula vya nyama. Mafuta yanapoliwa kwenye tunda la mzeituni, yana ubora zaidi kuliko mafuta ya wanyama au mafuta ya mimea. Yanasaidia kulainisha tumbo na hivyo kufanya mtu asifunge choo, yaani haja kubwa kutoka kwa urahisi. Matumizi yake yatajulikana kuwa yenye manufaa kwa wagonjwa wa kifua kikuu, na uponyaji kwa tumbo ambalo ukuta wake umevimba, na linasumbua au linakasirishwa kirahisi (inflamation). [MH 298.2; HU Aya ya 8]

Watu ambao wamezoea lishe ya mafuta, siagi, nyama, krimu, mayai, na vyakula vilivyokobolewa na kusindikwa (rich foods), vyenye kuchochea mwili sana, wana ladha isiyo ya asili, na hawawezi kufurahia mara moja chakula ambacho ni sahili na rahisi. Itachukua muda kwa ladha yao kuwa ya asili na kwa tumbo kupona kutokana na unyanyasaji ambao umekuja. Lakini wale wanaostahimili matumizi ya chakula bora, kisichokobolewa wala kusindikwa, basi baada ya muda, watakiona kuwa chakula hiki ni kitamu. Ladha zake maridadi na ya kupendeza zitathaminiwa baada ya muda, na kisha chakula hicho kitaliwa kwa furaha zaidi kuliko chakula kilichosindikwa na kukobolewa (junk food). Na tumbo, katika hali yake ya afya, halitaleta homa au kufanya kazi kupita kiasi, na litakuwa tayari kufanya kazi yake kwa jinsi linavyotakiwa (chakula tajiri kama alivyoelezea hapa ni junk foods au rich food, au unwholesome foods ni vile vilivyokobolewa na kusindikwa, vyenye sukari nyingi na mafuta mengi kama vile keki, maandazi, vitumbua, kuku wa kukaanga nk). [MH 298.3; HU Aya ya 9]

Ili kudumisha afya, ugavi wa kutosha wa chakula bora, chenye lishe unahitajika (Vyakula bora zaidi ni vile visivyosindikwa na kukobolewa, visivyo na sukari, mafuta, vinakuwa kama vilivyo mashambani kwa asili. Vyakula hivi ni vya jamii tano-jamii ya mboga-mboga, jamii ya matunda, jamii ya karanga, jamii ya nafaka na jamii ya karanga-Orodhesha mazao matano kwenye kila kundi la mazao haya). [MH 299.1; HU Aya ya 10]

Ikiwa tunapanga mambo kwa hekima, yale ambayo yanafaa kwa afya yanaweza kupatikana karibu kila nchi. Maandalizi mbalimbali ya mazao ya mchele, ngano, mahindi, na shayiri hupelekwa nje ya nchi, na kwenda kila mahali, pia maharagwe, njegere, na dengu. Hivyo, pamoja na matunda ya asili au yale yanayoagizwa toka nje, na aina mbalimbali za mboga-mboga zinazokua katika maeneo mahalia, yote haya hutoa fursa ya uchaguzi wa chakula ambacho ni kamili, bila ya kuwa na hitaji la kutumia vyakula vya nyama. [MH 299.2; HU Aya ya 11]

Mahali popote ambapo matunda yanaweza kupandwa kwa wingi, ugavi mwingi unapaswa kutayarishwa kwaajili majira ya baridi, kwa kuwekwa kwenye makopo au kukaushwa. Matunda madogo, kama vile aina za beri, au miforosadi, mifano ni groundcherries, raspberries, blackberries, black currants zinaweza kukaushwa raspberries, matunda yanaweza kupandwa ili kunufaisha maeneo mengi ambayo yana matunda machache au pale kilimo kinapuuzwa (Matunda haya nimeyaona yakikua mwituni zaidi --angalia kwenye google matunda haya na utakuwa umeyaona mahali na kuyafamu kwa majina ya nyumbani nchi zingine wanayalima, matunda ya tropiki, ambayo yanaweza kukaushwa ni kama maembe, mananasi, mafenesi, songwa, mapea, ndizi nk,

mboga nyingi pia zinaweza kukaushwa kama vile majani ya maboga, mnafu, mgagani, majani ya kunde nk). [MH 299.3; HU Aya ya 12]

Kwa matunda yanayochemshwa ili kuhifadhiwa kwenye vyombo, chupa ni bora kwa kuyahifadhi (caning) kuliko makopo ya bati, hivyo tumia chupa kwa kadri inavyowezekana. Ni muhimu kwamba matunda yanayohifadhiwa kwenye chombo, yawe katika hali nzuri, yaani yasiwe yameoza au yenye afya mbaya. Tumia sukari kidogo kuongeza ladha na kuyatunza vyema, na uyapike matunda kwa muda tu unaofaa utunzaji wake, usiyapike muda mrefu. Matunda yakindaliwa kwa njia hii, ni mbadala mzuri kwa matunda freshi (inasaidia kuyahifadhi wakati wa msimu wa matunda, na hasa kwenye nchi za baridi ambacho hakuna mazao yoyote wakati wa msimu wa theluji, soma zaidi kuhusu caning fruits and vegetables na chupa zake za kuhifadhi na yote hayusuyo ili kisioze au kisiwe sumu). [MH 299.4; HU Aya ya 13]

Popote pale ambapo matunda yaliyokaushwa, kama vile zabibu, plum, tufaha, pea, pichi, na apricot yanapatikana kwa bei ya wastani, itagundulika kwamba yanaweza kutumika kama chakula kikuu kwa uhuru zaidi kuliko ilivyokuwa zamani, na matokeo yake ni bora zaidi kwa afya na nguvu kwa tabaka zote za watendakazi (Matunda bora ni yale yanayopatikana pale unapoishi, kitabu kiliandikwa kwenye nchi ambayo watu hawakuwa na hali ya hewa ya kulima matunda tuliyo nayo, orodhesha matunda 20 ambayo yanapatikana ulipo, na uanze kuchunguza yale yenye lishe bora zaidi kutokana na utafiti wa kisayansi, kisha ulime na kuyatumia haya kwa kadri unavyoweza, kwetu sisi haya yatakuwa mapapai, maembe, machungwa, machenza, topetope, mananasi, ndizi, tikiti, parachichi, komamanga,mafenesi, songwa, mapera nk). [MH 299.5; HU Aya ya 14]

Hatupaswi kula aina nyingi za vyakula katika mlo mmoja, kwa sababu jambo hili uhamasisha ulaji wa kupita kiasi, yaani ulafi na husababisha kuvembewa (visizidi vitatu, sasa wakati wa potluck watu huzidisha namba!). [MH 299.6; HU Aya ya 15]

Sio vizuri kula matunda na mboga kwenye mlo mmoja. Ikiwa mmeng'enyo ni dhaifu, kutumia matunda na mboga kwa wakati mmoja kutasababisha shida ya tumbo na kushindwa kwa akili kufanya kazi ifaavyo. Ni bora kula matunda kwenye mlo mmoja na mboga kwenye mlo mwingine. [MH 299.7; HU Aya ya 16]

Milo inapaswa kuwa tofauti. Chakula cha aina ile ile, kilichoandaliwa kwa njia ile ile, hakipaswi kuonekana kwenye meza siku baada ya siku. Mlo huliwa kwa furaha zaidi, na mfumo hulishwa vizuri zaidi, wakati chakula kinakuwa cha aina tofauti tofauti (usile chakula kile kile, usiku na mchana bila

kubadilisha aina ya chakula au mapishi, yaani ugali na maharage asubuhi, mchana maharage na ugali, kesho yake hivyo hivyo). [MH 300.1; HU Aya ya 17]

Maandalizi ya Chakula

Ni makosa kula ili tu kutosheleza uchu wa chakula, ila unapaswa kujali unachokula, ubora wake na namna ya kukitayarisha. Ikiwa chakula kinacholiwa hakifurahishi, mwili hautapokea lishe kwa ubora. Chakula kinapaswa kuchaguliwa kwa uangalifu na kutayarishwa kwa akili, ujuzi na stadi. [MH 300.2; HU Aya ya 18]

Kwa kuoka mkate, unga laini na mweupe, yaani uliokobolewa si mzuri. Matumizi yake hayaleti afya wala kusaidia kiuchumi. Mkate wa unga laini uliokobolewa unakosa virutubisho vinavyopatikana katika mkate uliotengenezwa kwa ngano isiyokobolewa (punje ya ngano nzima). Kutumia unga uliokobolewa, ni sababu ya mara kwa mara ya watu kuvembiwa na hali zingine zisizokuwa na afya. [MH 300.3; HU Aya ya 19]

Matumizi ya soda au baking powder katika kuoka mikate ni hatari na sio ya lazima. Baking soda husababisha kuvimba kwa tumbo na mara nyingi ni sumu kwa mfumo mzima. Wakina mama wengi wa nyumbani wanafikiri kwamba hawawezi kufanya mkate kuwa mzuri bila baking soda, lakini hili ni kosa. Ikiwa wangechukua muda kujifunza mbinu bora, mkate wao ungekuwa wenye lishe bora zaidi, na ladha yake ingekuwa ya asili, na ungekuwa mtamu zaidi. [MH 300.4; HU Aya ya 20]

Katika kutengeneza mkate unaoumuka au mkate unaowekea hamira, maziwa hayapaswi kutumiwa badala ya maji. Matumizi ya maziwa huleta gharama ya ziada, na hufanya mkate usiwe na afya. Mkate wa maziwa hauendelei kuwa mtamu kwa muda mrefu baada ya kuokwa kama ule unaotengenezwa kwa maji, na huchacha kwa urahisi zaidi tumboni. [MH 301.1; HU Aya ya 21]

Mkate unapaswa kuwa mwepesi na mtamu (usiwe mkubwa na mzito). Uchachu hata mdogo haupaswi kuvumiliwa kwenye mkate. Mikate inapaswa kuwa midogo na kuokwa vizuri kabisa kwa kadri iwezekanavyo, ili seli za hamira zife kabisa (hamira ni zao hai). Wakati mkate ni wa moto au ndiyo tu umeokwa, mkate ulioumuka wa aina yoyote ile, ni mgumu kwa mmeng'enyo. Haupaswi kuonekana kwenye meza kamwe. Sheria hii, hata hivyo, haitumiki kwa mkate usiotiwa chachu. Skonis safi zilizotengenezwa kwa unga wa ngano bila chachu au hamira, na kuokwa katika tanuru la moto vizuri, ni nzuri na zenye kupendeza. [MH 301.2; HU Aya ya 22]

Nafaka zinazotumiwa kwa uji, zinapaswa kupikwa kwa masaa kadhaa. Lakini vyakula laini au vya majimaji kama uji, havina afya kuliko vyakula vikavu (kama ugali), ambavyo vinahitaji utafunaji kamili vizuri. Zwieback, au mkate uliookwa mara mbili wa kijerumani unaofanana sana ukoko unaobakia baada ya kupika ugali, ni mojawapo ya vyakula vinavyoyeyushwa kwa urahisi tumboni na ni vitamu zaidi. Hebu mkate wa kawaida ulioumuliwa ukatwe vipande vipande na ukaushwe kwenye oveni yenye joto hadi athari ya mwisho ya unyevunyevu itoweke kabisa. Kisha endelea kuuweka mpaka uwe na rangi ya kahawia kidogo kote. Weka mkate huu katika sehemu kavu, na mkate huu unaweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu zaidi kuliko mkate wa kawaida, na, utakapoupasha moto tena kabla ya kuutumia, utakuwa freshi kama vile ni mpya. [MH 301.3; HU Aya ya 23]

Sukari nyingi sana hutumiwa katika chakula. Keki, puddings tamu, jamii ya keki na maandazi, jam, ndizo sababu za kuvembewa au mmeng'enyo mbaya. Hasa, custards na puddings ambazo maziwa, mayai, na sukari ndivyo viungo vikuu (ice cream ina viamba upishi hivi pia). Matumizi huru ya maziwa na sukari katika mlo mmoja, au utengenezaji wa chakula kimoja yanapaswa kuepukwa. [MH 301.4; HU Aya ya 24]

Ikiwa maziwa hutumiwa, yanapaswa kuchemshwa vizuri ili vijidudu vife kabisa (sterilized); kwa tahadhari hii, kuna hatari ndogo ya kuambukizwa magonjwa yanayotokana na matumizi ya maziwa haya yasiyochemshwa vizuri. Siagi ina madhara kidogo inapoliwa kwenye mkate baridi kuliko inapotumika katika kupika; lakini, kama kanuni, ni bora uachane nayo kabisa. Jibini bado ni kitu cha kupigwa vita kabisa; haifai kabisa kwa chakula.[Kulinda chakula ili kiwe safi kwa kuondokana na vyakula vyote vyenye asili ya maziwa ni jambo la muhimu sana. Ingawa upimaji wa mara kwa mara wa mifugo ya ng'ombe wa maziwa unafanyika, pamoja na uchemshaji maziwa kwa muda mrefu (sterilization) na kuyaweka kwenye friji, ni njia ambayo hutumika ili yatufikie sisi, vyakula kama hivyo, ikiwa vimetoka kwenye vyanzo visivyo na uhakika, au vinavyoshughulikiwa bila uangalifu, ni tishio kubwa kwa afya zetu; kama ilivyoelezwa katika USA Department of Agriculture Famers Bulletin No. 1705 na mtaalamu wa Serikali, Rowena Schmidt Carpenter: "Kemikali zilezile na sifa zinazopendekeza maziwa kuwa chakula bora cha binadamu hukifanya pia kuwa chakula bora kwa bakteria." Msomaji ataelewa kwamba marejeo ya jibini hayajumuishi jibini la Cottage au vyakula vya aina kama hiyo tu, ambavyo mwandishi aliwahi kuvitambua kuwa ni vyenye afya.—Wachapishaji.] [MH 302.1; HU Aya ya 25]

Chakula kidogo kilichopikwa kwa kulipua-kulipua huharibu damu kwa kudhoofisha viungo vya kutengeneza damu. Vinaharibu mfumo na kuleta

magonjwa, pamoja na kuambatana na mishipa ya fahamu inayosumbua-sumbua na kuleta mtu kukasirika kwa urahisi au kuwa mudi-mudi. Waathiriwa wa upishi duni wanahesabiwa kwa maelfu na makumi ya maelfu. Juu ya makaburi mengi ingeweza kuandikwa: “Walikufa kwa sababu ya upishi mbaya;” "Alikufa kwa tumbo lililonyanyaswa.” *(pengine mfano mzuri ni takwimu ya tabia za makabila mbali mbali na vitu wanavyokula na hata pengine kesi zinazohusisha hasira zilizo kwenye mahakama ya nchi yako)* [MH 302.2; HU Aya ya 26]

Ni wajibu mtakatifu kwa wale wanaopika kujifunza jinsi ya kuandaa chakula chenye afya. Roho nyingi zimepotea kwa sababu ya upishi mbaya. Akili, umakini na ubunifu vinapaswa kutumika ili kutengeneza mkate mzuri; lakini kuna dini kubwa zaidi katika mkate mzuri kuliko ambavyo wengi wanafikiri. Kuna wapishi wachache wazuri. Mabinti wengi hufikiri kwamba kupika, pamoja na kazi zote nyingine za nyumbani ni shughuli za kuchosha na zizokuwa na hadhi, yaani ni kazi ya watu wa chini, na kwa sababu hii wasichana wengi wanaoolewa, wana fununu kidogo sana ya majukumu ya kazi ya mke na mama. [MH 302.3; HU Aya ya 27]

Kupika sio sayansi yenye kuchukiza, na ni moja ya elimu muhimu zaidi katika maisha ya kivitendo. Ni sayansi ambayo wanawake wote wanapaswa kujifunza, na inapaswa kufundishwa kwa njia ya kunufaisha tabaka lililo maskini zaidi. Ili kufanya mtu awe na hamu ya chakula na wakati huo huo chakula kiwe sahili na chenye lishe bora, kunahitajika ujuzi; lakini jambo hili linaweza kufanyika. Wapishi wanapaswa kujua jinsi ya kuandaa chakula kwa usahili na kwa njia rahisi na kwa afya, na ili kiwe kitamu zaidi, na pia kizuri zaidi, kwa sababu ya usahili wake. [MH 302.4; HU Aya ya 28]

Kila mwanamke ambaye ni kichwa cha familia na bado haelewi stadi ya upishi wenye afya, anapaswa kuamua kujifunza kile ambacho ni muhimu sana kwa ustawi wa familia yake. Katika maeneo mengi shule za afya na usafi, zinatoa fursa ya kufundisha upishi. Yeye ambaye hana msaada wa shule kama hizo, anapaswa kujiweka chini ya mafundisho ya mpishi mzuri na kuwa mvumilivu katika juhudi zake za kuboresha stadi yake ya mapishi, hadi awe bibi aliyebobea sanaa ya upishi. [MH 303.1; HU Aya ya 29]

Kula kwa wakati uliopangwa ni muhimu sana. Kila mlo unapaswa kuwa na wakati maalum. Wakati huu ndio ule ambao kila mtu anapaswa kula kile ambacho mfumo wake unakihitaji na kisha asiingize chochote mdomoni hadi mlo unaofuata. Kuna wengi ambao hula wakati mfumo wao hauhitaji chakula, katika masaa tofauti tofauti kila siku, na katikati ya milo, kwa sababu hawana nguvu za kutosha za kupinga mwelekeo wa ulafi. Wakati wa kusafiri, wengine huguguna kama kuchakulo kila wakati tu wanapoweza kufikia chochote kile

kinacholiwa, basi watu hawa wataendelea kuguguna siku nzima. Jambo hili linadhuru mwili kwa hakika. Ikiwa wasafiri wangekula kwa masaa yaleyale, chakula ambacho ni sahili na chenye lishe, hawangelihisi uchovu mwingi sana au kuteseka kutokana na ugonjwa safarini. [MH 303.2; HU Aya ya 30]

Tabia nyingine mbaya ni ile ya kula kabla tu ya kulala. Mtu anaweza kuwa alikula mlo wa kawaida; lakini kwa sababu kuna hisia ya kuzimia, basi anaendelea tu kula chakula. Kwa kuendekeza tendo hili baya la kula-kula ovyo, mazoea mabaya hujengeka kwa uthabiti sana hivi kwamba hufikiriwa kuwa haiwezekani kulala bila kula chakula. Matokeo ya kula chakula cha jioni kwa kuchelewa, ni mchakato wa umeng'enyaji wa chakula kuendelea hata masaa ya kulala. Lakini ingawa tumbo linaendelea kufanya kazi mara kwa mara, kazi yake haikamilishwi ipasavyo. Usingizi mara nyingi huhangaishwa kwa ndoto zisizofurahisha, na asubuhi mtu huamka na uchovu, na bila burudisho na furaha ya kupata kifungua kinywa. Tunapolala ili kupumzika, tumbo linapaswa kuwa limemaliza kufanya kazi yake yote, ili, lifurahie kupumzika, pamoja na viungo vingine vya mwili. Kwa watu wenye tabia ya kukaa kwenye kiti, mlo wa usiku ni hatari sana. Kwa watu wenye mtindo wa maisha wa kukaa kaa kwenye kitu tu, mlo wa usiku unaleta madhara kwenye miili yao. Usumbufu unaotengenezwa kwenye mwili kama mwitikio wa tabia hii mbaya ya kula usiku, ndiyo mwanzo wa ugonjwa ambao huisha kwenye kifo (maandishi mengine ya Roho ya unabii anasema ikifika saa tatu na nusu usiku uwe kitandani, na acha kula angalau masaa mane kabla ya kwenda kitandani, Peleleza zaidi). [MH 303.3; HU Aya ya 31]

Katika visa vingi hali ya kuzirai ambavyo husababisha mtu atamani kula chakula kingine zaidi, huonekana kwa sababu viungo vya usagaji chakula vimehenyeshwa sana wakati wa mchana kwa ulafi. Baada ya kuuondoa mlo mmoja tu kwenye ratiba yako ya kula, viungo vya umeng'enyaji vinahitaji kupumzika. Angalau saa tano au sita zinapaswa kupita kati ya milo, usile mlo unaofuata kama hazijapita saa tano, na hakika watu wengi wanaojaribu mpango huo wanagundua kwamba milo miwili kwa siku ni bora kuliko mitatu. [MH 304.1; HU Aya ya 32]

Hali Mbaya za Kula

Chakula hakipaswi kuliwa kikiwa cha moto sana au baridi sana. Ikiwa chakula chako ni baridi, nguvu muhimu za tumbo hutolewa ili kukipasha moto kabla ya kukimeng'enya. Vinywaji baridi vinadhuru kwa sababu hiyo hiyo; Matumizi huru ya vinywaji vya moto sana humdhoofisha mtu. Jambo halisi ni kwamba, kadri unavyokula na kunywa maji kwa pamoja, yaani unakula na hapo hapo unakunywa kimiminika fulani, inakuwa vigumu zaidi kwa chakula kusagwa inavyotakiwa kwenye tumbo lako; kwani vile vimiminika ni lazima

vifyonzwe kwanza kabla ya mmeng'enyo wa chakula kuanza na pia unapunguza nguvu ya vimiminika (dilute). Usile chumvi nyingi, yaani epuka kabisa kutumia chumvi kwa kiasi kikubwa, epuka matumizi ya vyakula vyenye pilipili na viungo vyenye kukasirisha au kukera tumbo, epuka achari zilizo na siki na chumvi nyingi* (angalia zaidi kuhusu spices za kuepuka ambazo zinakera tumbo), kula matunda mengi, na usumbufu unaolikasirisha tumbo lako na kukusukuma kutaka kunywa sana maji wakati unakula chakula, utatoweka kwa kiasi kikubwa *(pickles inayotajwa haya ni matango yaliyotengenezwa kama achari, kwa kuweka siki nyingi, chumvi nyingi, na hata pilipili, ugwadu wake unakuwa mkali sana na jambo hili linakera, linadhuru na kumomonyosha ukuta wa tumboL—stomach lining inflamation and injury. Vyakula vingine vya kutilia maanani vinavyokera tumbo ni kama baking soda na pilipili manga, hivi viachwe kabisa, na kuna vitu kama karafuu, tangawizi, na pilipili ya cayenne au mbuzi vitumiwe kwa kiasi kidogo sana maana navyo vina pilipili ya aina fulani). [MH 305.1; HU Aya ya 33]

Chakula kinapaswa kuliwa polepole na kutafunwa vizuri kabisa. Jambo hili ni muhimu ili mate yaweze kuchanganywa vizuri na chakula na vimiminika vinavyoshughulika na usagaji chakula viitwe ili kuanza kazi yake uyeyushaji bila ya kuvihafifisha kwa kuvipunguzia nguvu yake kwa maji unayokunywa (Majina ya vichocheo au enzymes zinazotumika katika kuyeyusha au kusaga chakula ni kama pepsin, amylase, protease, lipase, lactase, maltase- Usivihafifishe nguvu yake hivi kwa kunywa maji Do not dilute them). [MH 305.2; HU Aya ya 34]

Uovu mwingine mbaya ni kula wakati usiofaa, kama baada ya mazoezi makali au mazoezi yaliyopitiliza, wakati mtu amechoka sana au mwili umepata joto jingi. Mara baada ya kula kuna rasimu kali juu ya nishati ya neva yaani nguvu za mishipa ya fahamu; na wakati akili au mwili inatozwa ushuru mwingi kabla au baada tu ya kula, na hivyo mmeng'enyo wa chakula huzuiwa. Wakati mtu ana msisimko, wasiwasi, au haraka, ni bora aache kula mpaka upumzike vizuri au upate nafuu. [MH 305.3; HU Aya ya 35]

Tumbo linahusiana kwa karibu sana na ubongo; hivyo wakati tumbo limepata maradhi, nguvu ya mishipa ya fahamu (neva) huitwa kutoka kwenye ubongo kuja kusaidia viungo dhaifu vya usagaji chakula. Wakati hitaji la namna hili linakuwa la mara kwa mara, ubongo unakuwa na msongamano. Wakati ubongo unapotozwa ushuru, yaani unahenyeshwa kila wakati katika kuhusika kufanya kazi hii ya usagaji wa chakula, na mtu akose kufanya mazoezi ya mwili, hapo ndipo hata chakula cha kawaida kinapaswa kuliwa kwa udogo sana ili kusaidia urekebishaji wa hali hii mbaya na tete. Wakati wa chakula ni lazima uyatupilie mbali masumbufu ya maisha haya na wasiwasi;

yaondoe haraka kichwani, usifikirie ni lazima uharakishe, sasa wewe ni lazima ule polepole na kwa uchangamfu, na huku moyo wako ukiwa umejaa shukrani kwa Mungu kwa baraka Zake zote. [MH 306.1; HU Aya ya 36]

Wengi wanaoacha kabisa kula nyama na vitu vingine vibaya na vyenye kuchukiza*, vinavyoleta madhara hufikiri kwamba basi kwa sababu sasa wao chakula chao ni sahili na chenye afya na kwa vile hakijakobolewa wala kusindikwa (whole food), wako huru kujiingiza kwenye uchu wa chakula (foodie), yaani wanaweza kujaza tumbo nde, bila ya kujizuia, na hivyo hula kupita kiasi, nyakati hizo ndiyo watu huendelea kula bila kuweka breki, mtu akifikia hatua hii, tendo hili huitwa uroho, umelo au ulafi wa chakula. Hili ni kosa. Viungo vya usagaji wa chakula havipaswi kulemewa kwa kiasi au ubora wa chakula ambacho kitautinga mfumo wa umeng'enyaji kukidhi hitaji ya kusaga kila kipande cha chakula. [MH 306.2; HU Aya ya 37]

Desturi ambazo watu wamerithi huamuru kwamba chakula kitawekwa mezani kwa awamu kadhaa* (meal course-watu huanza na supu, kisha vitafunio, kisha chakula chenyewe, kicha vinywaji na keki au dessert). Bila kujua nini kitakachofuata, mtu anaweza kula chakula cha kutosha ambacho labda hakimfai zaidi katika raundi ya kwanza. Wakati raundi ya mwisho inaletwa, mara nyingi hujaribu kuvuka mipaka, na kuchukua vitu vyenye sukari (dessert) kwa kujaribiwa, ambavyo, hata hivyo, vinathibitisha kwamba sivyo kitu kizuri kabisa kwake. Ikiwa chakula chote kilichopangwa kuliwa katika mlo mmoja kinawekwa mezani mwanzoni, mtu ana fursa ya kufanya uchaguzi ulio bora zaidi *(awamu au raundi tatu za mlo–kishtua hamu ya kula, entrée au chakula chenyewe kisha, dessert yaani vitu vitamu kama keki, maandazi, chocolate nk. Awamu nne za mlo supu, saladi, entrée yaani mlo wenyewe, na dessert. Awamu tano za mlo kishtua hamu ya kula, supu, mlo wenyewe, dessert, na jibini. Mlo wenye awamu sita–vitafunwa, supu, samaki, mlo wenyewe, saladi, kahawa na kisha dessert).* [MH 306.3; HU Aya ya 38

Wakati mwingine matokeo ya kula kupita kiasi huhisiwa kwenye mwili mara moja. Katika hali nyingine hakuna hisia za maumivu au uchungu; lakini viungo vya usagaji hupoteza nguvu zake muhimu, na msingi wa nguvu za mwili hupunguzwa. [MH 306.4; HU Aya ya 39]

Chakula cha ziada, ambacho wanadamu hula japo hakihitajiki kabisa katika mwili wa mtu, hulemea mfumo na kutoa hali ya ugonjwa, homa na hata kuanza safari ya kuelekea kifoni. Hali hii inafanya damu iitwe kwa kwenye tumbo kwa kiasi kikubwa kuliko vile inavyostahili ili kusaidia kuyeyusha chakula, na kusababisha viungo vilivyo mbali na moyo kama miguu na mikono

kuanza kupata ubaridi kwa haraka. Inavihenyesha kwa ukali viungo vya usagaji na wakati viungo hivi vimeshakamilisha kabisa kazi yake ya kusaga chakula, kuna hisia ya uchovu mkali au kuzimia. Baadhi ya wanaoendelea kula kupita kiasi huita hii hisia ni njaa ambayo imeisha ila huwa inarudia (all-gone feeling hunger); lakini shida hii husababishwa na hali ya viungo vya usagaji chakula tumboni, kufanya kazi kupita kiasi. Wakati fulani kunakuwa na ganzi kwenye ubongo, na mtu anakuwa na hali ya kutopenda kushughulisha akili au mwili wake. [MH 307.1; HU Aya ya 40]

Dalili hizi zisizofurahisha humjia mtu, na kuhisiwa kwa sababu tu maumbile yamekamilisha kazi yake kwa nguvu isiyo ya lazima kutolewa na sasa yako hoi au tabani kwa uchovu. Tumbo linasema, " mpendwa Nipe pumziko." Lakini kwa watu wengi zile hisia za kuzirai zinatafsiriwa kama tumbo linahitaji chakula zaidi; kwa hivyo badala ya kulipumzisha tumbo, mtu anaamua kuleta mzigo mwingine wa chakula juu ya tumbo tena. Matokeo yake ni viungo vya usagaji chakula hupata uchakavu wakati vingepaswa kuwa na uwezo mzuri tu wa kufanya kazi yake kama ambavyo inatakiwa. [MH 307.2; HU Aya ya 41]

Katika siku ya Sabato tunapaswa kupunguza ugavi mkubwa wa chakula ulio huria kuliko siku zingine za wiki. Badala yake tunapaswa tule chakula sahihi kwa kiasi kidogo tu, ili akili iwe safi na wazi na yenye nguvu kuelewa mambo ya kiroho. Tumbo lililoziba maana yake ni ubongo uliozibа. Maneno ya thamani zaidi katika siku ya Sabato yanaweza kuanguka kwenye sikio na wala yasithaminiwe, kwa sababu tu akili imekanganyikiwa na mlo usiofaa, kwa aina ya chakula na kiasi kilicholiwa. Kwa kula kupita kiasi siku ya Sabato, watu wengi hufanya zaidi ya wanavyofikiri katika kutojistahilisha wenyewe kupokea manufaa ya fursa za Sabato takatifu. [MH 307.3; HU Aya ya 42]

Tunapaswa kuepuka upikaji wa Sabato kabisa; lakini hii haimaanishi kuwa tule chakula baridi. Katika hali ya hewa ya baridi chakula kilichoandaliwa siku moja kabla kinapaswa kupashwa moto. Hebu milo iwe sahili, yenye kupendeza na ya kuvutia. Hasa kwenye familia ambazo zina watoto, ni vizuri, siku ya Sabato, wale chakula ambacho kitaonekana zawadi maalumu, kitu ambacho familia hawali kila siku. [MH 307.4; HU Aya ya 43]

Mahali mbapo tabia mbaya za lishe zimeendekezwa na kufurahiwa, hebu kusiwe na ucheleweshaji kwa matengenezo. Wakati kuvembea na maumivu ya tumbo yametokana na unyanyasaji wa tumbo, jitihada zinapaswa kufanywa kwa uangalifu ili kutunza nguvu muhimu zilizobaki kwa kuondoa kila mzigo unaofanya mfumo utingwe au kulemewa. Tumbo haliwezi kupona kabisa na kurudi kwenye afya yake baada ya unyanyasaji wa muda mrefu; lakini lishe sahihi itaokoa unyogovu unaoendelea kukithiri, na kisha wengi watapona kabisa, au kwa kiasi kikubwa. Si rahisi kutoa maagizo au kuweka sheria za

ulaji ambao utakidhi kesi ya kila mtu; lakini, kwa kuzingatia kanuni zinazofaa katika ulaji, matengenezo makubwa yanaweza kufanywa, na mpishi hahitaji kuhenyeka sikuzote ili tu awatie watu kwenye majaribu ya ulafi. [MH 308.1; HU Aya ya 44]

Kuacha chakula kwa muda kutatoa zawadi kwenye nguvu ya akili na maadili; Jambo hili husaidia pia kudhibiti tamaa za mwili. Kula kupita kiasi ni hatari sana kwa wale ambao wana hulka ya uvivu; watu kama hawa wanapaswa kula kidogo tu na kufanya mazoezi mengi ya mwili. Kuna wanaume na wanawake wenye uwezo bora wa asili ambao hawatimizi hata nusu ya kile ambacho wangeweza ikiwa tu wangejidhibiti katika kuikana hamu ya kula. [MH 308.2; HU Aya ya 45]

Waandishi na wanenaji wengi hufeli kwenye kipengele hiki. Baada ya kula na kujaza matumbo tele kwa ulafi,, wanajishughulisha na kazi za kukaa-kaa tu, kusoma, kujifunza, kutafiti, au kuandika, bila kuruhusu wakati wa kufanya mazoezi ya mwili kwenye ratiba zao. Kama matokeo, mtiririko huru wa mawazo na maneno unawekewa alama. Hawawezi kuandika au kuzungumza kwa nguvu ya msukumo unaohitajika ili kufikia mioyo yao au mioyo ya watu wengine; juhudi zao zimezorota na zenye matunda sifuri. [MH 309.1; HU Aya ya 46]

Wale waliopewa majukumu muhimu, wale, ambao ukilinganisha na wengine, ndio walinzi wa mambo ya kiroho, wanapaswa kuwa watu wenye hisia kali na utambuzi wa haraka. Hawa zaidi ya watu wengine, wanahitaji kuwa na kiasi katika kula. Vyakula tajiri, yaani vilivyokobolewa na kusindikwa na vya anasa havipaswi kabisa kupewa nafasi kwenye meza zao. [MH 309.2; HU Aya ya 47]

Kila siku watu walio katika nafasi za amana, wana maamuzi ya kufanya yale ambayo matokeo yenye umuhimu mkubwa hutegemea. Mara nyingi wanapaswa kuchangamka na kuwa wepesi katika kufikiri kwa haraka, na hii inaweza kufanywa kwa mafanikio na wale tu ambao mazoea yao ya afya na kiasi yana ukali. Akili huimarika chini ya tiba sahihi ya nguvu za kimwili na kiakili. Ikiwa shida sio kubwa sana, nguvu mpya huja na kila shughuli nzito. Lakini mara nyingi kazi ya wale ambao wana mipango muhimu ya kuzingatia na maamuzi muhimu ya kufanya huathiriwa kwa uovu na matokeo ya lishe isiyofaa. Tumbo lisilo na utaratibu hutoa hali ya akili iliyochanganyikiwa, na isiyo na uhakika. Mara nyingi husababisha hasira, ukali, au ukosefu wa haki. Mipango mingi ambayo ingekuwa baraka kwa ulimwengu imewekwa pembeni, hatua nyingi zenye udhalimu, uonevu, na hata ukatili zimechukuliwa, kama matokeo ya hali ya ugonjwa iliyokuja kutokana na tabia mbaya za ulaji chakula. [MH 309.3; HU Aya ya 48]

Hapa kuna pendekezo kwa wote ambao kazi yao ni ya kukaa kwenye kiti au wanafanya kazi inayotumia akili, yaani kazi za ofisini; Hebu yule aliye na ujasiri wa kutosha wa kimaadili na ambaye anaweza kujizuia nafsi ajaribu hili: Katika kila mlo achukue tu aina mbili au tatu za vyakula rahisi, na asile chakula zaidi ya kile kinachotakiwa kukidhi njaa. Kisha afanye mazoezi ya nguvu kila siku, na kisha aone ikiwa hatapata (kuna) faida. [MH 310.1; HU Aya ya 49]

Watu wenye nguvu ambao wanajishughulisha na kazi za mikono/kimwili, hawabanwi sana na kuwa waangalifu kuhusu wingi au ubora wa chakula chao kama ilivyo kwa watu wenye tabia ya kukaa-kaa tu kwenye vitu siku nzima; lakini hata hawa, wangekuwa na afya bora zaidi ikiwa wangejizoeza kujizuia katika kula na kunywa. [MH 310.2; HU Aya ya 50]

Wengine wanatamani maagizo fulani, kwamba sheria mahsusi, iliyobainishwa kinagaubaga, iweze kuagizwa au kuwekwa chini kuhusiana na lishe yao. Wanakula kupita kiasi, na kisha wanajuta, na kwa hivyo wanaendelea kufikiria juu ya kile wanachokula na kunywa daima. Maagizo ya namna hii hayapaswi kuwepo. Mtu mmoja hawezi kuweka chini sheria mahususi kwa mtu mwingine kuhusu ulaji wake. Kila mtu anapaswa kutumia busara na kujitawala, na anapaswa kutenda kutokana na kanuni *(Mfano ale lita mbili za chakula, saa nne, na saa kumi lita, asile baada ya saa 12 jioni, na asile nyama wala samaki n.k).* [MH 310.3; HU Aya ya 51]

Miili yetu ni mali iliyonunuliwa na Kristo Mwenyewe, na hatuna uhuru wa kuifanyia au kuitumia tupendavyo. Wote wanaoelewa sheria za afya wanapaswa kutambua wajibu wao wa kuzitii sheria hizi ambazo Mungu ameziweka katika nafsi zao. Utii wa sheria za afya unapaswa kufanywa kuwa suala la wajibu binafsi. Sisi wenyewe, ni lazima tupate matokeo ya kukiukwa kwa sheria. Ni lazima kila mmoja wetu ajibu kwa Mungu kwa tabia na mazoea yake-atoe hesabu ya uwakili wake wa ulaji. Kwa hivyo swali linalokuja kwetu sio, "Mazoea ya ulimwengu ni nini?" bali, “Mimi kama mtu binafsi nitayatendeaje makao ambayo Mungu amenipa?” [MH 310.4; HU Aya ya 52]

SURA YA 24

NYAMA KAMA CHAKULA

Chakula alichopewa mwanadamu tangu hapo mwanzo hakikujumuisha chakula cha wanyama (yaani nyama, samaki, senene au kitu chochote chenye uso/face). Ilikuwa baada ya Gharika, wakati ambapo kila kitu chenye kijani kibichi kilipoharibiwa, ndipo mwanadamu alipopata kibali cha kula nyama. [MH 311.1; HU Aya ya 1]

Katika kuchagua chakula cha mwanadamu katika Edeni, Bwana alionyesha kile ambacho kilifaa kuwa lishe bora kabisa; hata katika uchaguzi uliofanywa kwa ajili ya Israeli, Yeye alifundisha somo lile lile (mana). Alipowatoa Waisraeli kutoka Misri, alianza mazoezi na mafunzo yao kuhusu lishe, ili wawe watu wa milki Yake Mwenyewe. Kupitia jukwaa hili la Waisraeli, Yeye alitamani kuubariki na kuufundisha ulimwengu wote kupitia kwao. Aliwaandalia chakula kilichofaa zaidi kwa kusudi hilo, si nyama, bali mana, “mkate wa mbinguni.” Ni kwasababu ya kutoridhika na manung’uniko ya vyungu vya nyama za Misri, ndiyo kwamba walipewa chakula cha nyama, na jambo hilo lilikuwa liwe kwa muda mfupi tu. Matumizi yake yalileta magonjwa na vifo kwa maelfu ya watu. Bado katazo la lishe ya nyama halikukubaliwa kamwe kwa moyo wote na Waisraeli (hawakukubali). Hii ikaendelea kuwa sababu ya kutoridhika na manung'uniko yao ya wazi au ya siri, na hivyo jambo hili halikufanywa kuwa la kudumu. [MH 311.2; HU Aya ya 2]

Walipofika Kanani na kuichukua nchi kama wamiliki na kuishi, Waisraeli waliruhusiwa kutumia chakula cha nyama, lakini ilikuwa chini ya vizuizi vyenye maelekezo maalumu ambayo yalielekea kupunguza matokeo mabaya ya nyama. Matumizi ya nyama ya nguruwe yalikatazwa, kama vile ya wanyama wengine na ndege na samaki ambao nyama zao zilitangazwa kuwa najisi. Kwa

wanyama walioruhusiwa, ulaji wa mafuta na damu ya mnyama ulikatazwa kabisa (Walawi 11 na 3 inaelezea vizuri mpango wa Mungu wa nyama za kula). [MH 311.3; HU Aya ya 3]

Wanyama kama hao tu ndio wangeweza kutumika kwa chakula kama walikuwa katika hali nzuri ya afya. Hakuna kiumbe chochote kilichoraruliwa, kilichokufa chenyewe - kibudu, au ambacho damu yote haikutolewa vizuri ambacho kilipaswa kutumika kama chakula. [MH 312.1; HU Aya ya 4]

Kwa kukiuka mpango uliowekwa na Mungu kwaajili ya chakula chao, Waisraeli walijipatia hasara kubwa. Walitamani chakula cha nyama, na wakavuna matokeo yake. Hawakufikia ubora wa tabia ya Mungu au kutimiza kusudi Lake. Bwana “aliwapa haja ya moyo wao; bali aliwapelekea ukonda nafsini mwao.” Zaburi 106:15. Walivithamini vitu vya duniani kuliko vitu vya rohoni, na kile kielelezo cha ubora na ukuu mtakatifu kwa dunia nzima ambalo ndilo lilikuwa kusudi la Mungu kwaajili yao, kwao hawakulifikia. [MH 312.2; HU Aya ya 5]

Sababu za Kuacha Vyakula vya Nyama

Wale wanaokula nyama, hula tu mitumba ya nafaka na mboga-mboga ambazo tayari zilikuwa zimeshaliwa na wale wanyama ambao wanawala (second hand food); kwani mnyama hupokea kutoka kwenye vyakula hivi vya mimea lishe ambayo hutoa ukuaji na ustawi. Uhai uliokuwa kwenye nafaka na mboga hupita ndani ya mnyama mlaji- mfano ng’ombe au kuku. Na kisha sisi wanadamu tunaipokea lishe hiyo kwa kula nyama, samaki, mayai au maziwa. Ni afadhali kama chakula hiki mimi tungekipata moja kwa moja toka kwenye mimea, kwa kula chakula ambacho Mungu alikiandaa kwaajili ya matumizi yetu! [MH 313.1; HU Aya ya 6]

Vyakula hivi vya nyama, havikuwa chakula bora kabisa kwa wakati ule wa zamani; na hata leo matumizi yake kwenye ulimwengu, hayafai maradufu kwa matumizi yanayomfaa mwanadamu, kwa kuwa magonjwa katika wanyama yanaongezeka kwa kasi sana (haya yaliandikwa mwaka 1905 au miaka 115 iliyopita). Wale wanaotumia vyakula vya nyama hakika hawajui wanakula nini. Mara nyingi kama wangeweza kuwaona wanyama wakati wa kuishi kwao na kujua ubora wa nyama wanayokula, wangeiacha kuila, na kuichukia nyama. Watu wanaendelea kula nyama iliyojaa viini vya kifua kikuu (Tuberculosis) na saratani/kansa. Hivi ndivyo kifua kikuu, saratani na magonjwa mengine mabaya hupitishwa kwa maambukizo kutoka kwa kiumbe kimoja na kwenda kwa kiumbe kingine. [MH 313.2; HU Aya ya 7]

Tishu za nguruwe zimejaa vimelea (minyoo, bakteria na virusi). Mungu alisema hivi kuhusu nguruwe, “Ni najisi kwenu, msile nyama yake, wala

msiguse mizoga yao." Kumbukumbu la Torati 14:8 . Amri hii ilitolewa kwa sababu nyama ya nguruwe haifai kutumiwa kama chakula. Nguruwe ni wanyama wasafishao maiti au mizoga ya wanyama waliokufa duniani, na takataka na hivi ndivyo wanavyotumika kusaidia ulimwengu wetu wanapokula mizoga, yaani ndiyo matumizi pekee waliyokusudiwa kutumikia. Kamwe, kwa hali yoyote ile, nyama yao haikufaa kuliwa na wanadamu. Haiwezekani kwa nyama ya kiumbe chochote kilicho hai kuwa na afya njema wakati uchafu ni sehemu yake ya asili na wakati kiumbe hiki kinakula kila kitu cha kuchukiza. [MH 313.3; HU Aya ya 8]

Mara nyingi wanyama hupelekwa sokoni na kuuzwa kwa ajili ya chakula wakiwa wamesheheni magonjwa kiasi kwamba wamiliki wao huogopa kuwatunza kwenye mazizi yao kwa muda mrefu kwani watapata hasara wanayama hawa wakimfia nyumbani kwake. Na baadhi ya michakato ya kuwanenepesha ili wawe na soko zuri huleta magonjwa kwa wanyama na hatimaye kwa wanadamu wanaomla (watu huwapa kuku damu ya ng'ombe, antibiotics, homoni, na mengine ya kunenepesha ili uzito uwe mkubwa, ila ambayo mwishowe huingia na kudhuru mwili wa mwanadamu). Wanyama wengi wamefungiwa mbali na mwanga na hewa safi, hupumua angahewa ya mazizi machafu, pengine kuwanenepesha na chakula kilichooza, na hivyo mwili mzima punde huambukizwa au kuchafuliwa na vitu hivi vichafu. [MH 314.1; HU Aya ya 9]

Wanyama mara nyingi husafirishwa umbali mrefu kuelekea sokoni na kupata mateso makubwa katika mchakato wa kulifikia soko. Wanaacha malisho ya malisho ya kijani kibichi, na kusafiri kwa maili nyingi na hata kupata uchovu kwenye barabara zenye joto, na vumbi, na msongamano kwenye magari machafu, yenye homa na uchovu, mara nyingi hukaa masaa mengi bila kupewa chakula na maji, viumbe hawa maskini huburuzwa kwa ukali hadi kuelekea kwenye kifo chao cha kuchinjwa, ili tu wanadamu wakasherekee katika kuila mizoga yao. [MH 314.2; HU Aya ya 10]

Katika sehemu nyingi samaki hupokea uchafuzi mkubwa kutokana na uchafu wanaokula na kuwaletea magonjwa mengi. Hali hii inashamiri zaidi kwenye kesi ambazo samaki hukutana na maji-taka ya miji mikubwa, yaani mahali palipo na maji ya chooni nk. Samaki wanaolishwa kwenye mifereji ya maji machafu wanaweza wakasafiri kwenye maji kwa umbali mkubwa na kuvuliwa mahali ambapo maji ni masafi na freshi. Hivyo hawa samaki watakapotumika kama chakula, watawaletea watu ambao hawakushuku hatari hiyo magonjwa na kifo. [MH 314.3; HU Aya ya 11]

Madhara ya lishe ya nyama hayaonekani mara moja; lakini huu sio ushahidi kwamba nyama hizi hazina madhara. Ni watu wachache tu ambao wanaweza

kuaminishwa kuwa nyama waliyokula ndiyo ambayo imesumisha damu yao na kusababisha ugonjwa au mateso yao. Wengi hufa kwa magonjwa yaliyotokana na ulaji wa nyama peke yake na wala si kitu kingine zaidi, ila ukweli halisi haushukiwi na wao wenyewe au na wanadamu wengine. [MH 315.1; HU Aya ya 12]

Maovu ya kimaadili yanayotokana na lishe ya nyama hayaachi alama alama chache tunapolinganisha na magonjwa ya kimwili (ulaji wa nyama huleta madhara kwa maadili na mwili). Vyakula vya nyama hudhuru mwili na kuhatarisha afya, na chochote kinachoathiri mwili kina athari sawa kwenye akili na roho. Hebu fikiria jinsi ukatili kwa wanyama unavyohusishwa na ulaji wa nyama, na matokeo yake kwa wale wanaowadhuru hawa viumbe na watazamaji wa ubaya huu. Jinsi jambo hili linavyotuharibia huruma yetu wanadamu kwa kiasi kubwa, huruma ambayo tulipaswa kuwachukulia na kuwatendea hawa viumbe wa Mungu! [MH 315.2; HU Aya ya 13]

Akili inayoonyeshwa na wanyama wengi mabubu, yaani wasiojua kitu, hukaribia sana na akili ya mwanadamu hivi kwamba ni siri na fumbo kwetu wanadamu. Wanyama wanaona, wanasikia, wanapenda, na wana hofu na pia wanateseka. Wanyama wananatumia viungo vyao kwa uaminifu zaidi kuliko wanadamu wengi wanavyotumia vyao (hata kwenye mambo ya ushoga wanyama hawashiriki nk). Wanadhihirisha huruma na kusikitikia wenzao katika mateso. Wanyama wengi huonyesha upendo kwa wale wanaowashughulikia au kuwasimamia, kuliko mapenzi yanayoonyeshwa na baadhi ya jamii ya wanadamu. Wanajenga mahusiano yenye mapenzi kwa mwanadamu ambayo hayavunjiki bila wao kujipatia mateso makubwa. [MH 315.3; HU Aya ya 14]

Ni mtu gani mwenye moyo wenye ubinadamu, ambaye amewahi kufuga wanyama wa nyumbani ambaye angeweza kuwatazama machoni mwao akiwa amejaa ujasiri na upendo, na kwa hiari akawakabidhi kwenye kisu cha mfanya biashara mwenye bucha ili amchinje mnyama wake? Je, angewezaje kuichovya nyama hiyo na kuilia ugali kama kitoweo cha tonge tamu la chakula? [MH 316.1; HU Aya ya 15]

Ni kosa kudhania kwamba nguvu za misuli zinategemea matumizi ya lishe ya nyama. Mahitaji ya mfumo wa miili yetu yanaweza kupatikana vyema tu kwenye mimea, na kisha tukawa watu wenye afya na kufurahia nguvu nyingi bila matumizi ya nyama, nafaka pamoja na matunda, karanga, na mboga, zina virutubishi vyote na tosha, vinavyohitajika ili kutengeneza damu nzuri. Virutubisho hivi muhimu havipatikana kwa ubora au ukamilifu kwenye lishe ya nyama. Ikiwa matumizi ya nyama yangekuwa muhimu kwa afya na nguvu, lishe ya Mungu ingejumuishwa katika chakula cha wanadamu katika kile

ambacho Yeye alikiteua kwa mwanadamu hapo mwanzo. [MH 316.2; HU Aya ya 16]

Wakati matumizi ya lishe ya nyama yamesitishwa/yameachwa, mara nyingi mtu anajisikia kama vile ana hisia ya udhaifu, na uchovu au ukosefu wa nguvu. Wengi husisitiza kuwa jambo hili ndiyo ushahidi kwamba chakula cha nyama ni muhimu; ila jambo hili hutokea kwa sababu vyakula vya tabaka hili la nyama vinasisimua damu, na kwa sababu vinaifanya damu kuwa na joto kwa homa kwa kuisisimua mishipa ya fahamu, ndiyo maana watu wanaona kama wamepungukiwa wasipokuwa navyo (wameimiss). Watu wengine watajionea kwamba ni vigumu kwao kuacha kula nyama kama ilivyo kwa mlevi kuacha pombe yake; lakini watakuwa katika hali bora kwa kufanya mabadiliko. [MH 316.3; HU Aya ya 17]

Mtu anapoacha kutumia lishe ya nyama, mbadala wake unapasa uwe aina mbalimbali za nafaka, njugu, mboga-mboga, na matunda ambayo yatakuwa yenye lishe ya kuvutia na kupendeza na hivyo kumfanya mtu awe na hamu ya kula. Hii ni muhimu sana, hasa kwa wale ambao ni dhaifu au ambao wanapata uchovu kwa kujishughulisha na kazi daima. Kwenye baadhi ya nchi ambako umaskini umesheheni, nyama ndicho chakula chenye bei nafuu zaidi. Chini ya hali kama hizi, mabadiliko yatafanywa kwa shida zaidi; lakini mabadiliko yanaweza kutekelezwa. Tunapaswa, hata hivyo, kuzingatia mazingira ya watu na nguvu ya mazoea ya maisha na katika kuleta mabadiliko, na tunapaswa kuwa waangalifu na wenye busara ili tusisitize yale mawazo ambayo siyo sahihi kwa njia isiyofaa. Hakuna anayepaswa kulazimishwa kufanya mabadiliko ya ghafla. Ulaji wa nyama unapaswa kuachwa kwa kuingiza mbadala wa vyakula vizuri ambavyo ni vya bei nafuu. Katika suala hili, mengi yanategemea mpishi. Kwa kuwa na uangalifu na stadi, chakula ambacho kitakuwa na lishe ya kupendeza, na ambacho kwa kiwango kikubwa, kinaweza kutayarishwa chakula na kitakuwa mbadala wa chakula cha nyama. [MH 316.4; HU Aya ya 18]

Katika hali zote elimisha dhamiri, wekeza nia yako, weka chakula kizuri chenye afya, kisichokobolewa au kusindikwa, na badiliko la kutoka ulaji wa nyama na kwenda kwenye ulaji wa mimea (vegetarian) litafanywa kwa urahisi, na taratibu kule kutaka kula nyama kutakoma hivi karibuni (wataelewa na kubadilika). [MH 317.1; HU Aya ya 19]

Je, huu sio wakati wa watu wote kuachana na vyakula vya nyama? Je, wale wanaotafuta kuwa safi, waliosafishwa, na watakatifu, wanawezaje kuwa na ushirika na malaika wa mbinguni, wanawezaje kuendelea kutumia chochote kile wanachokiita chakula, kitu chenye madhara makubwa kwa nafsi na mwili? Je, wanawezaje kuutoa uhai wa viumbe vya Mungu ili tu wapate kula nyama

kama burudani au starehe/luxury yao? Hebu watu hawa badala yake, warudi kwenye chakula chenye afya na kitamu alichopewa mwanadamu hapo mwanzo, na wao wenyewe wawe watendaji halisi wa jambo hili na kisha wawafundishe watoto wao kuacha kutumia vyakula vya nyama, na kuwa na huruma kwa viumbe mabubu ambavyo Mungu amevifanya na kuviweka chini ya utawala wetu. [MH 317.2; HU Aya ya 20]

SURA YA 25

LISHE ILIYOPITILIZA

Sio wote wanaodai kuamini katika matengenezo ya lishe ni wanamatengenezo wa kweli. Kwa watu wengi matengenezo yanajumuisha kukataa tu baadhi ya vyakula visivyofaa. Hawazielewi kwa uwazi kanuni za afya, na meza zao, ambazo bado zimejaa vitafunwa vyenye kudhuru, ziko mbali na kuwa kielelezo cha kiasi cha Kikristo na kiasi. [MH 318.1; HU Aya ya 1]

Kundi jingine, kwaajili ya shauku yao ya kuweka mfano sahihi, huenenda kwa kupitiliza kinyume cha yale waliyopasa kuyafanikisha. Wengine hawawezi kupata vyakula vinavyofaa kwa ubora zaidi, watu hawa badala ya kutumia vitu ambavyo vinaweza kutosheleza mahitaji ya mwili, wanajitwalia lishe duni. Chakula chao hakitoi virutubisho vinavyohitajika kutengeneza damu nzuri. Afya yao inadhurika, manufaa yao yanaharibiwa, na mfano wao badala ya kuunga matengenezo ya lishe, unayapinga. [MH 318.2; HU Aya ya 2]

Wengine wanafikiri kwamba kwa kuwa afya inahitaji mlo sahili, basi hakuna haja ya wao kuwa na uangalifu hata mdogo katika uteuzi au utayarishaji wa chakula. Wengine hujibinya kwa lishe duni sana, bila kuwa na aina tofauti za virutubisho vya kutosha kwenye chakula chao ili kujipatia mahitaji

yanayotakiwa na mfumo wa mwili na hivyo, huteseka kama matokeo ya huku kupitiliza. [MH 318.3; HU Aya ya 3]

Wale ambao wana uelewa nusu-nusu tu kuhusu kanuni za matengenezo, mara nyingi ndio wanang'ang'ania tabia ya kutokata kubadilika, sio tu katika kutekeleza maoni yao wenyewe, lakini katika kuwasisitizia maoni yao wanafamilia na majirani zao. Na kisha Matokeo ya matengenezo yao potofu, kama yanavyoonekana katika afya zao mbaya, na juhudi zao za kuyalazimisha maoni yao kwa wengine, huwapa wengi wazo potofu la matengenezo ya kweli ya lishe, na kuwaongoza kuyakataa kabisa hata yale maoni mazuri ya matengenezo ya chakula. [MH 318.4; HU Aya ya 4]

Wale wanaoelewa sheria za afya na ambao wanatawaliwa na kanuni, wataepuka kuwa watu wenye kupitiliza katika ujumbe wa kiasi, kwa pande zote mbili, yaani, kwa kuendekeza ulafi wa chakula au kula kupita kiasi na pia kwa kujiwekea vizuizi vikali ambavyo vinaharibu afya. Lishe yao huchaguliwa, si tu kwa ajili ya kutosheleza hamu ya kula, bali kwa ajili ya kuujenga mwili. Wanatafuta kuhifadhi kila nguvu ya mwili katika ya ubora zaidi kwa ajili ya huduma ya juu zaidi kwa Mungu na wanadamu. Hamu ya chakula iko chini ya udhibiti wa akili na dhamiri, na huzawadiwa kwa afya ya mwili na akili. Ingawa watu hawa hawasisitizi maoni yao kwa njia ya kuudhi wengine, kielelezo chao ni ushuhuda bora wa kuungwa mkono na kanuni zinazofaa. Watu hawa wana ushawishi mkubwa kwa wema. [MH 319.1; HU Aya ya 5]

Kuna akili ya kuzaliwa inayohitaji kutumika katika katika matengenezo ya lishe, hii sisi tunaiita hekima. Somo hili linapaswa kuchunguzwa kwa upana na kwa kina, na hakuna mtu anayepaswa kuwakosoa watu wengine eti kwa sababu mazoea yao ya lishe hayapatani na yake mwenyewe, katika mambo yote. Hatuwezi kuweka sheria isiyobadilika ili tu kudhibiti tabia za kila mtu, na hakuna mtu anayepaswa kujifikiria kuwa yeye ndiye kigezo cha wote. Watu wote hawawezi kula vitu vinavyofanana kabisa, yaani vitu vilivyo sawa (kila mtu ale ndizi moja, mboga kijiko kimoja, na karanga 19!). Vyakula vinavyopendeza na vizuri kwa mtu mmoja vinaweza kumchukiza, na hata kumdhuru mtu mwingine. Wengine hawawezi kutumia maziwa, wakati wengine hunawiri wanapoyatumia. Baadhi ya watu hawawezi kumeng'enya njegere, mbaazi, dengu na maharagwe; wakati wengine wengine wanaziona zinafaa. Kwa baadhi ya maandalizi ya nafaka, iliyopasuliwa kwenye vipande vikubwa vikubwa kidogo- ni chakula bora (Mf. bulga), wakati wengine hawawezi kutumia hii. [MH 319.2; HU Aya ya 6]

Wale wanaoishi katika nchi mpya kama Australia na Marekani, kwenye wilaya zenye umaskini, mahali ambapo matunda na karanga ni adimu, hawapaswi kulazimishwa kuacha maziwa na mayai kwenye lishe yao. Ni kweli

kwamba watu ambao wamezoea sana kula nyama na ambao tamaa za kinyama ziko ndani yao wanahitaji kuepuka matumizi ya vyakula vyenye kusisimua mwili (animal passion). Hasa katika familia zenye watoto ambao wanajikita kwenye tabia za matendo ya kimwili, anasa na starehe, mayai hayapaswi kutumiwa. Lakini katika kesi za watu ambao viungo vyao vya kutengeneza damu ni dhaifu, - haswa ikiwa vyakula vingine vya kutoa lishe inayohitajika haviwezi kupatikana, - maziwa na mayai hayapaswi kuachwa kabisa. Uangalifu mkubwa unapaswa kuchukuliwa, hata hivyo, ili kupata maziwa kutoka kwenye ng'ombe wenye afya nzuri, na mayai kutoka kwa ndege/kuku wenye afya, wanaolishwa vizuri na kutunzwa vizuri; na mayai yanapaswa kupikwa vizuri ili yaweze kumeng'enywa kwa urahisi zaidi. [MH 320.1; HU Aya ya 7]

Matengenezo ya lishe yanapaswa kuwa endelevu. Kadiri magonjwa yanavyoongezeka kwa wanyama, matumizi ya maziwa na mayai yatazidi kuwa yasiyo na usalama. Jitihada yapaswa kufanywa ili kuandaa mbadala wake na vitu vingine vyenye afya na vya bei nafuu. Watu kila mahali wanapaswa kufundishwa jinsi ya kupika bila ya kutumia maziwa na mayai kwa kadiri inavyowezekana, na bado wawe na chakula kizuri na kitamu. [MH 320.2; HU Aya ya 8]

Mazoea ya kula milo miwili kwa siku, kwa ujumla huonyesha yana faida kwa afya; lakini katika hali fulani watu wanaweza kuhitaji mlo wa tatu. Hata hivyo, endapo mlo wa tatu utakuwa unahitajika, basi, uwe mwepesi sana, kwa kujumuisha chakula kinachosagwa kwa urahisi zaidi. “Crackers”—biskuti ya Kiingereza—au zwieback, ambayo haina sukari na matunda, au kinywaji cha nafaka, yaani mtama uonasagwa na kuwa kuwekwa kwenye maji ya moto na kunyewa kama chai (coffee cereal), ndivyo vyakula vinavyofaa zaidi kwa mlo wa jioni (mkate wa zwieback una ladha kama ya ukoko wa ugali). [MH 321.1; HU Aya ya 9]

Wengine huwa na wasiwasi kwamba chakula chao, hata kama ni sahili na chenye afya, bado kinaweza kuwadhuru au kuwaumiza. Napenda kuwaambia watu hawa kuwa, Msidhani ya kuwa chakula chenu kitawadhuru; tafadhali msifikirie hivyo kabisa. Kuleni kwa kadiri ya maamuzi yenu bora; na pale unapomwomba Bwana akibariki chakula chako kwa ajili ya kuimarisha mwili wako, amini kwamba Yeye anasikia maombi yako, na uwe na pumziko moyoni (tulia kwa Bwana). [MH 321.2; HU Aya ya 10]

Kwa sababu kanuni inatutaka tutupilie mbali vile vitu vinavyokera tumbo na kuharibu afya, tunapaswa kukumbuka kuwa lishe duni huleta upungufu wa virutubisho vinavyotakiwa kwenye damu, na kufanya damu iwe duni. Kesi nyingi za magonjwa ambayo yamekuwa magumu sana kutibiwa, huletwa na sababu hii. Mfumo haulishwi vya kutosha, na mtu huvembewa kwaajili ya

mmeng'enyo mbaya na udhaifu wa jumla ndiyo matokeo (dyspepctic). Wale wanaojikuta wakitumia lishe ya namna hii, umasikini siyo sababu inayowapelekea kufikia hatua hii mara zote, bali wanachagua lishe hii kwa ujinga au uzembe wao, au kutekeleza mawazo yao potofu ya matengenezo ya chakula na afya. [MH 321.3; HU Aya ya 11]

Mungu haheshimiwi mwili unapopuuzwa au kutumiwa vibaya na hatimaye unakuwa haufai kwenye utumishi Wake. Kutunza mwili kwa kuuandalia chakula chenye ladha nzuri na chenye kutia nguvu ni mojawapo ya wajibu wa kwanza wa mwenye nyumba. Ni afadhali uwe na nguo na samani za bei ya chini kuliko kufanya ubahili wa ugavi wa chakula chako kinachokusaidia afya ya mwili. [MH 322.1; HU Aya ya 12]

Baadhi ya wenye nyumba huipunja familia na lishe muhimu, ili tu kuwatumbuiza wageni, kwa kuwaandalia chakula kilicho ghali. Kufanya hivi, sio busara kabisa. Katika burudani ya wageni kunapaswa kuwa na usahili mkubwa zaidi. Hebu mahitaji ya familia yawe na kipaumbele kwenye umakini wetu. [MH 322.2; HU Aya ya 13]

Uchumi usio na hekima na desturi za bandia mara nyingi huzuia ukaribishaji-wageni mahali inapohitajika kufanya hivi na kuwa mbaraka. Ugavi wa kawaida wa chakula kwenye meza zetu unapaswa kuwa hivi kwamba mgeni asiyetarajiwa anaweza kukaribishwa wakati wowote bila ya kumlemea mama wa nyumbani kufanya maandalizi ya ziada. [MH 322.3; HU Aya ya 14]

Wote wanapaswa kujifunza nini cha kula na jinsi ya kukipika. Wanaume, pamoja na wanawake, wanahitaji kuelewa maandalizi sahili ya chakula ambayo yatakuwa na ubora kiafya. Shughuli au biashara zao mara nyingi huwaita mahali ambapo hawawezi kupata chakula kizuri, ambacho hakikubolewa wala kusindikwa; na watu hawa wakiwa wana ujuzi wa upishi, wanaweza kuutumia ujuzi huu kwa malengo mazuri. [MH 323.1; HU Aya ya 15]

Fikiria kwa uangalifu lishe yako. Jifunze kutoka sababu hadi athari (nini unakula? Na matokeo yake ni nini). Sitawisha tabia ya kuikana nafsi, yaani kutawala nafsi, kujinyima. Weka hamu ya kula chini ya udhibiti wa busara. Kamwe usilinyanyase tumbo kwa kula kupita kiasi, lakini pia usijinyime chakula chenye afya, kile kilicho kitamu na ambacho afya inadai. [MH 323.2; HU Aya ya 16]

Mawazo finyu ya baadhi ya watu wanaotaka kuwa wana matengenezo wa afya yamekuwa jeraha kubwa kwa misheni ya afya na usafi (hygeine). Wataalamu wa afya na usafi wanapaswa kukumbuka kwamba matengenezo ya lishe yatahukumiwa au kutathminiwa kwa kiwango kikubwa, na kile ambacho watu wanaweka katika meza zao; badala ya kuchukua njia ambayo

itaifedhehesha misheni hiyo, watu wanapaswa kuwa mfano wa kanuni zake kiasi cha kuwa pendekezo zuri kwa watu wenye akili safi na zenye hekima*. Kuna tabaka kubwa ambalo litapinga vuguvugu lolote la matengenezo hata kama ni la kufaa watu, ikiwa kunawekwa kizuizi kwenye kipengele cha hamu ya kula. Wanashauriana na ladha ya chakula badala ya sababu au sheria za kiafya. Kwa kikundi hiki, wote wanaoacha mkondo wa mabadiliko ya desturi zilizoewa na watu na kuwa watetezi wa matengenezo, watahesabiwa kuwa ni watu wenye msimamo mkali bila ya kujali jinsi mwenendo wao ulivyo thabiti. Ili watu wasipate mpenyo wa kukosolewa, wapenda afya na usafi wasijaribu kuona jinsi wanavyoweza kuwa tofauti na wengine, lakini wanapaswa kuja karibu na watu kwa kadri iwezekanavyo bila ya kudhabihu kanuni* (Watu wenye elimu, uzoefu na hali nzuri wavutiwe, na wasiseme hawa watu hakika ni wajinga, hawajui wanachokifanya, afya zao ni mbaya wanaumwa kila mara, wala hawapendezi na sasa wanataka kutuuzia ujinga wao sisi). [MH 323.3; HU Aya ya 17]

Wale wanaotetea matengenezo ya afya na usafi wanapopitiliza mipaka, hatushangai kwamba watu wengi wanaowaona watu hawa ndiyo nembo inayowawakilisha kanuni za afya na kisha wanakataa kabisa matengenezo hayo. Hali hizi za ushupavu katika matengenezo yanayopitiliza kiasi, mara nyingi huleta madhara kwenye muda mfupi kuliko ambavyo inaweza kutenguliwa/kufutwa kwa kuishi maisha bora kipindi chote cha maisha ya mtu. [MH 324.1; HU Aya ya 18]

Matengenezo ya afya na usafi yanategemea kanuni ambazo ni pana na zinazofika mbali, na hatupaswi kuyadharau kwa kutenda maoni na mazoea finyu. Lakini hakuna mtu yeyote anayepaswa kuruhusu upinzani, dhihaka, shauku ya kuwapendeza au kuwavuta watu wengine, imgeuze kutoka kwenye kanuni za Kweli, au kumfanya ayapuuzie haya maagizo, kwa kuyachukulia kwa wepesi. Wale wanaotawaliwa na kanuni watakuwa imara na kudhamiria katika maamuzi yao, kusimama kwa ajili ya haki; hata hivyo katika mahusiano yao yote watadhihirisha roho ya wema na ukarimu kama ya Kristo, katika kujikana nafsi au kuwa na kiasi cha kweli. [MH 324.2; HU Aya ya 19]

SURA YA 26

VICHOCHEO NA MADAWA YA KULEVYA

Chini ya mwavuli wa vichocheo na dawa za kulevya za hospitali, au hata zile ambazo watu hununua kwa magendo na mwishowe zinaleta uraibu (narcotics) huainishwa aina mbalimbali za vitu ambavyo, kwa ujumla hutumika kama chakula au kinywaji, na ambavyo hukera tumbo, huisumisha damu, na kusisimua mishipa ya fahamu, yaani neva. Hakika matumizi yake ni uovu mkubwa. Watu hutafuta msisimko wa vichocheo, kwa sababu kwa muda fulani, matokeo yake yanakubalika na wanakuwa wanapendezwa nayo. Lakini daima kuna mwitikio wa hivi vitu. Matumizi ya vichocheo visivyo vya asili daima huwa yana kupitiliza kiasi, na ni wakala hai anayefanya kazi katika ukuzaji unaozorotesha mwili na kufanya uoze. [MH 325.1; HU Aya ya 1]

Viungo au vikolezo vya chakula (Mf. Ketchup au tomato sauce, siki, achari, soya sauce nk)

Katika enzi hizi za kasi au haraka (dotcom), ni vyema kula vyakula visivyosisimua, kwani kwa kadri ambavyo vyakula vinakuwa siyo vya kusisimua ndivyo linakuwa jambo bora zaidi kwa afya. Viungo (vikolezo) vinadhuru

katika asili yake. Haradali, pilipili, viungo vyenye tabia ya pilipili (spices), matango yaliyolowekwa kwenye siki (pickles au achari za aina fulani), na vitu vingine vinavyofanana na hivyo, hukasirisha tumbo na kufanya damu kuwa na homa na uchafu. Hali ya kuvimba kwa ukuta wa tumbo la mlevi, mara nyingi huonyeshwa picha ya athari za vileo. Hali sawa ya kuvimba huzalishwa na matumizi ya viungo vinavyokera huu ukuta wa tumbo. Mtu anapoendelea kuvitumia vitu hivi, haitapita muda kwa chakula chake kukosa ladha, yaani hakikidhi hamu ya kukila, kwa vile ulimi umezoea vikolezo vikali-vikali na vitu vya kusisimua (kama vile pilipili manga, kahawa na etc. Chakula kinakuwa flat au baridiii, mtu anaona ni kama anakula godoro). Mfumo unahisi unahitaji kitu chenye ladha kali zaidi kwenye ulimi na chenye kufanya mwili usisimke, na unakitamani hicho na kukimezea mate, yaani kitu cha kusisimua zaidi (mtu anapoweka vitu kama pilipili kwenye chakula huwa anafika hatua ya kuona chakula chote hakina ladha, na anaweza tu kuongeza kiasi cha chakula akili yake ikifikiria wingi ule unafidia ladha. Viungo kama kitunguu saumu, kitunguu maji, manjano na vingine ni sawa kuvitumia, ila usitumie kwa wingi mpaka vikere tumbo). [MH 325.2; HU Aya ya 2]

Chai na Kahawa

Chai hufanya kazi kama kichocheo (stimulant) na, kwa kiwango fulani, huleta ulevi na uraibu*. Matokeo ya kahawa na vinywaji vingine vingi maarufu kwa mwili, huwa na athari sawa. Athari ya kwanza ni ya kusisimua mwili. Mishipa ya fahamu ya tumbo inapata msisimko; hii hupeleka muwasho kwenye ubongo, na ubongo huamshwa ili kutoa utendaji ulioongezeka kwenye moyo na nishati ya muda mfupi kwenye mfumo mzima. Uchovu unasahaulika; nguvu inaonekana kama vile inaongezeka. Akili inasisimka, na mawazo yanakuwa wazi zaidi. (yaani mtu anajiona ana akili au hekima nyingi sana yaani genius. Kafein imo kwenye chai nyeusi ya China, kahawa, energy drinks, coca-cola, 7 up na vinywaji vingi vingine). [MH 326.1; HU Aya ya 3]

Kwa sababu ya matokeo haya, watu wengi hufikiri kwamba chai au kahawa yao waliyokunywa huwa inawasaidia sana (kuwa na nguvu, kusisimka au kukesha). Lakini hili ni kosa. Chai na kahawa haisaidii kuulisha mfumo- haina lishe. Athari yake hutolewa kabla ya kuwa na wakati wa kuyeyusha chakula na kukitumia, na kile kinachoonekana kuwa ni nguvu ni msisimko wa neva tu. Wakati ushawishi wa kichocheo umepita au umekwisha kwenye damu, nguvu hiyo ‘iliyodhaniwa,’ ambayo ilikuja ghafla, na isiyo ya asili hupungua, na matokeo yake ni kiwango kinacholingana cha uchovu na unyonge. [MH 326.2; HU Aya ya 4]

Kuendelea kwa matumizi ya vichochezi vinavyokera neva, yaani mishipa ya fahamu, hufuatiliwa na maumivu ya kichwa, kutopata usingizi, kwa kuwa

mwili wote unakuwa umeamka kabisa, na mapigo ya moyo yanaanza kwenda mbio au kutokuwa katika mpigo wake, kutomeng'enywa vizuri kwa chakula, kutetemeka, na uovu mwingine mwingi; maana vinachakaza na kuchosha nguvu za maisha. Mishipa iliyochoka inahitaji kupumzika na kupata utulivu badala ya kusisimuliwa na kufanya kazi kupita kiasi. Asili inahitaji muda ili kurejesha nguvu zake zilizonyanganywa. Nguvu zake zinapochochewa na matumizi ya vichocheo, mengi zaidi yatatimizwa kwa muda; lakini, kadiri mfumo unavyodhoofika kwa matumizi ya vichocheo hivyo mara kwa mara, basi taratibu, hatua kwa hatua inakuwa vigumu zaidi kuziamsha nguvu kwenye ile hatua ambayo mtu alitaka. Na hitaji la vichocheo linakuwa gumu zaidi kudhibiti, hadi mapenzi au nia ya mtu inafeli/inashindwa na sasa inaonekana kwamba hakuna nguvu ya nia ya kuweka katazo kwa hamu hii isiyo ya asili (kichocheo). Vichocheo vikali na bado vyenye nguvu zaidi hutumiwa ili kukidhi hamu hii ya uraibu, hadi asili iliyochoka haiwezi kuitikia/kujibu tena. [MH 326.3; HU Aya ya 5

Tabia ya Tumbaku

Tumbaku ni sumu inayofanya kazi polepole, na kwa siri, lakini ni mbaya zaidi. Inapotumika kwa namna yoyote ile iwe ni ugoro, sigara, vape, kiko nk, ina matokeo kwenye mwili ambayo mtu anayetumia pamoja na watu wengine huyaona ; tumbaku ina hatari zaidi kwa sababu athari zake ni za polepole na mwanzoni huwa hazionekani kabisa. Inasisimua mwili na kisha kuipooza mishipa. Hudhoofisha na kuutia mawingu ubongo. Mara nyingi huathiri mishipa kwa njia yenye nguvu zaidi kuliko vileo. Tumbaku ina hila zaidi, na madhara yake yana ugumu zaidi kuyaondoa kwenye mfumo. Matumizi yake yanasisimua kiu ya vinywaji vikali na mara nyingi hujenga msingi wa tabia ya ulevi. [MH 327.1; HU Aya ya 6]

Utumiaji wa tumbaku haufai, haumsaidii mtu, ni ghali, unamfanya mtu awe mchafu, huleta uchafuzi wa mazingira, unamnajisi mtumiaji, na unawakera watu wengine. Wale waliojitoa kwenye hii tabia wako kila mahali duniani. Si rahisi upite kwenye umati bila ya kumwona mvuta sigara akitoa moshi wake wenye sumu usoni mwako (sheria zimesaidia kidogo jambo hili katika kipindi cha miaka 20 iliyopita). Uvutaji sigara haupendezi kwa mvutaji na wala haufai kwa afya ya abiria anayepakia kwenye gari la moshi au gari la abiria lenye watu ambao wanavuta sigara na anga linakuwa limejaa moshi wa pombe na tumbaku. Ingawa wanadamu wengi huendelea kutumia sumu hizi wao binafsi, lakini je, wana haki gani ya kuchafua hewa ambayo lazima wengine wapumue? (hata ikiwa ni familia yao) [MH 328.1; HU Aya ya 7]

Miongoni mwa watoto waliozaliwa na walio tumboni, na vijana matumizi ya tumbaku yanaleta madhara makubwa kuliko kwa watu wazima. Mazoea

yasiyofaa ya vizazi vilivyopita huathiri watoto na vijana wa leo. Kutokuwa na uwezo wa kiakili, udhaifu wa kimwili, mishipa ya fahamu iliyoharibika, na tamaa za mwili zisizo za asili hupitishwa kama urithi kutoka kwa wazazi na kwenda kwa watoto. Na mazoea yale yale, yanayoendelezwa na watoto, yanaongezeka na kuendeleza matokeo mabaya kwenye kizazi kinachofuata au kwa watu wengine. Tumbaku ndiyo sababu ya mwili, akili, na maadili kuzorota kwa kiwango kikubwa, jambo ambalo linatoa kengele ya kutisha. [MH 328.2; HU Aya ya 8]

Wavulana huanza kutumia tumbaku katika umri mdogo sana. Kwa hiyo, tabia hizi mbaya na uraibu, hutokea wakati mwili na akili uko katika hatua tete na hivyo huathiri zaidi, na nguvu za mwili hudhoofishwa zaidi, na mwili hufanywa udumae, akili haiwezi kufikiri vizuri, na maadili uharibiwa kabisa. [MH 329.1; HU Aya ya 9]

Lakini ni nini chaweza kufanywa ili kuwafundisha watoto na vijana maovu ya mazoea ambayo wazazi, walimu, na wachungaji wamewawekea watoto kielelezo? Wavulana wadogo, ambao ndiyo kwanza wanaacha utoto na kuelekea kipindi cha balehe, wanaweza kuonekana wakivuta sigara zao. Ikiwa mtu atazungumza nao juu ya jambo hili, wao hujibu, "Hata baba yangu anatumia tumbaku." Wanamsonda kidole mchungaji au msimamizi wa shule ya Jumapili (Sunday School) na kusema, “Kama mtu wa cheo cha namna hii anavuta sigara; kuna ubaya gani mimi nikimfuatilisha yeye?" Wafanyakazi wengi katika katika shirika la kuwa na kiasi au kutawala nafsi, wameyazoea matumizi ya tumbaku. Je, watu kama hawa wanaweza kuwa na uwezo gani wa kuzuia mwelekeo wa kutokuwa na kiasi? [MH 329.2; HU Aya ya 10]

Ninatoa wito kwa wale wanaodai kuamini na kulitii Neno la Mungu: Je, wewe kama Mkristo unaweza kuendekeza tabia ambayo inalemaza akili zako na kukunyang'anya uwezo wako wa kukadiria kwa uhalisi mambo ya umilele? Je, unaweza kukubali kila siku kumnyang'anya Mungu huduma ambayo ni haki Yake kuipata, na kuwaibia wanadamu wenzako, huduma unayoweza kutoa na nguvu za kielelezo chako? [MH 329.3; HU Aya ya 11]

Je, umezingatia wajibu wako kama msimamizi na wakili wa Mungu, kwa mali iliyo mikononi mwako? Je, unatumia kiasi gani cha fedha za Bwana kwa tumbaku? Hesabu pesa zote ulizotumia kwa kununua tumbaku katika maisha yako. Je, hichi kiasi kinachotumiwa na tamaa inayouchafua mwili wako kinalinganaje na kile ambacho wewe umetoa kwa ajili ya kuwasaidia maskini na kueneza injili? [MH 329.4; HU Aya ya 12]

Hakuna mwanadamu anayehitaji tumbaku, kwamba bila tumbaku hawezi kuishi, lakini watu wengi wanaangamia kwa kukosa pesa ambayo watu

wengine wanaitumia vibaya kuliko hata kuitupa pipani. Je, wewe haujatumia vibaya mali za Bwana kwa kuvuta kwako sigara? Je, wewe huna hatia kweli ya kumpora Mungu na wanadamu wenzako? “Hamjui ya kuwa... ninyi si mali yenu wenyewe? Maana mlinunuliwa kwa thamani; basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na katika roho zenu ambazo ni za Mungu. 1 Wakorintho 6:19, 20. [MH 330.1; HU Aya ya 13]

Vinywaji vya Vinavyolevya au Vileo

“Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi;

na adanganyikaye kwa hayo hana hekima.”

“29 Ni nani apigaye, Yowe? Ni nani aliaye, Ole? Ni nani mwenye ugomvi? Ni nani mwenye mguno? Ni nani aliye na jeraha zisizo na sababu? Ni nani aliye na macho mekundu?

30 Ni wale wakaao sana kwenye mvinyo; Waendao kutafuta divai iliyochanganyika.

31 Usiitazame mvinyo iwapo ni nyekundu; Iitiapo bilauri rangi yake, ishukapo taratibu;

32 Mwisho wake huuma kama nyoka; Huchoma kama fira.”

Mithali 20:1; 23:29-32. [MH 330.2; HU Aya ya 14]

Kamwe hakuna kalamu iliyoshikwa na mkono wa mwanadamu ambayo iliwahi kuchora picha iliyo wazi zaidi ya udhalilishaji na utumwa wa mhasiriwa wa kileo. Akiwa amesisimka, akiwa ameshushwa hadhi, au hata anapoamshwa na hisia ya taabu yake, yeye hana uwezo wa kutoka kwenye mtego; “Utasema, Wamenichapa wala sikuumia; Wamenipiga wala sina habari; Nitaamka lini, nitazidi kuitafuta tena..” Kifungu cha 35. [MH 330.3; HU Aya ya 15]

Hakuna hoja inayohitajika kuonyesha athari mbaya za kileo kwa mlevi. Majeruhi na mabaki ya wanadamu waliyohafifishwa, na kudanganywa—nafsi ambazo Kristo Mwenyewe alizifia, na ambazo malaika wa mbinguni hulia kwa huzuni juu yao—ziko kila mahali. Wao ni dosari katika ustaarabu wetu tunaojivunia. Watu hawa wenye uraibu, wakuwa aibu na laana na hatari kubwa na iliyo karibu na watu wa kila nchi. [MH 331.1; HU Aya ya 16]

Na ni nani awezaye kuwa na picha ya uangamivu huu mawazoni mwake, uchungu mzito, na moyo uliovunjika, ambavyo vimefichwa katika nyumba ya mlevi? Hebu mfikirie mke wake, ambaye mara nyingi alilelewa kwa njia nyeti kama mayai, mdada mwenye kujali, na sasa ameunganishwa na yule ambaye kinywaji kimembadilisha, na sasa amekuwa mlevi wa kutupwa,

anayeyumbayumba au pepo mchafu. Wafikirie watoto wake walioporwa faraja za nyumbani, elimu, na mafunzo, wakiishi kwa hofu juu ya yule ambaye wanapaswa kujivunia kama baba na mlinzi wao, na sasa wametupwa ulimwenguni, wakiwa na chapa ya aibu wanapotembea mbele za watu, na mara nyingi wakiwa na laana ya kiu cha kileo waliyoirithi kutoka kwa baba yao. [MH 331.2; HU Aya ya 17]

Fikiria ajali za kutisha ambazo hutokea kupitia ushawishi wa kunywa pombe. Afisa fulani anayeendesha treni anapuuzia kutii ishara au ilani za barabarani au anatafsiri vibaya magizo ya uendeshaji. Treni inaendelea kwenda mbele kwasababu ya hilo kosa; treni zinagongana, na maisha ya watu wengi yanapotea. Au meli inazama chini ya maji kwa vile rubani wake alikuwa amelewa, na wafanyakazi pamoja na abiria wanazama chini, na maji yanakuwa kaburi lao. Wakati suala hilo linafanyiwa utafiti kwa undani, inagunduliwa kwamba mtu aliyekuwa katika nafasi muhimu ya kushughulikia hicho chombo (meli) chini ya ushawishi wa pombe, ndiye ambaye ameyaleta majanga haya yote. Ni kwa kiwango gani mtu anaweza kuendekeza tabia ya ulevi na bado akaaminiwa na maisha ya watu, kwamba atatenda kwa usalama na maisha ya wanadamu? Hakika, mtu anaweza kuaminiwa pale tu anapojiepusha kabisa na kileo. [MH 331.3; HU Aya ya 18]

Vileo Visivyo na Ukali kama wa Pombe

Watu ambao wamerithi hamu ya vichochezi au vileo visivyo vya asili, kwa vyovyote vile hawapaswi kuweka mbele ya macho yao divai, bia, au sharubati/juisi ya apo iitwayo apple cider, au karibu na wao (hii apple cider juice inabalikia kuwa pombe haraka sana, nafikiri mfano wake utakuwa kama togwa, mtu akichelewa kidogo tu, atakuwa anakunywa pombe); kwa maana kufanya hivi, ni kuwawekea daima majaribu mbele yao. Kuhusu apple cider (apo saida), ambayo huanzwa kutengenezwa kama juisi ya matunda ya apo au tufaha ambayo inakuwa haijachacha mwanzoni, ila baadaye inaanza kuwa na kileo, na asilimia ya kileo inazidi kuongezeka, na watu wengi huiona kwamba ni tamu au isiyo na madhara, na wengi hawaoni shida katika kuinunua, na hivyo wanajisikia wako huru kwa vile siyo bia. Lakini hichi kinywaji huwa kinabaki kuwa kitamu kwa muda mfupi tu (kama juisi ya zabibu ilivyo); kisha uchachushaji wake huanza. Ladha yake kali ambayo inakuja baada ya siku kadhaa, huifanya ikubalike zaidi kwenye ndimi za watu wengi, na mtumiaji anakasirika kukiri kwamba sasa hii siyo juisi tena bali pombe, au kinywaji ambacho kimechacha. [MH 331.4; HU Aya ya 19]

Kuna hatari kwa afya, hata katika matumizi ya juisi tamu ya apo kutokana na utengenezaji wake ulivyo kwa asili*. Endapo watu wangejionea wenyewe kile ambacho darubini inafunua kuhusu apple cider au (juisi ya apo) wanayonunua, ni wachache wangekuwa tayari kuinywa. Mara nyingi wale wanaotengeneza hii juisi kwenye soko, huwa si watu makini kuhusu hali ya matunda yanayotumika, na hivyo maapo yaliyo na minyoo na yaliyooza hukamuliwa humo, na darubini inaonyesha haya yote. Wale ambao hawakuwa na fununu ya jambo hili hata kidogo wanaweza kutumia maapo yaliyo na sumu, au yaliyooza kwa namna nyingine yoyote, wanabugia hii apo saida waliyotengenezewa, na kusema ni starehe kubwa (luxury); lakini darubini inaonyesha kuwa hata kama kinywaji hiki kikiwa safi yaani fresh, na vyombo vilivyotumiwa katika kukamuliwa ni vizuri kabisa, hakifai kabisa kutumiwa na wanadamu (*mfano uchafu mwingi, matunda hayaoshwi bali hukamuliwa, kemikali zinazotumika kwenye ulimaji wa haya matunda ni nyingi, matunda ya apo na strawberry yanaongoza, mfano kabla ya kuchuma strawberry zinapuliziwa mara 19 hivi ndani ya miezi miwili). [Tamko hili lilipotolewa mwaka wa 1905, ilikuwa ni jambo la kawaida kutengeneza juisi ya apo cider kama ilivyoelezwa hapa na mwandishi. Leo, mahali ambapo usafi wa vyakula haudhibitiwi, juisi ya apo cider bado inaweza kuwa inatengenezwa kwa njia ile ile. Lakini pale ambapo juisi ya Apo cider hutengenezwa katika hali ya usafi, kwa kutumia matunda mazuri na yenye afya, ni wazi kwamba pingamizi hizo hazipo.—Wachapishaji]. [MH 332.1; HU Aya ya 20]

Ulevi huja hata kwa divai, bia, na apo cider kama unavyokuja kutoka kwenye vinywaji vikali zaidi. Matumizi ya vinywaji hivi huamsha ladha ya wale walio na nguvu zaidi, na hivyo tabia ya unywaji wa pombe au ulevi huanzishwa. Kunywa pombe kwa kiasi ni shule ambayo watu hufundishwa kazi ya kuwa waraibu au walevi. Bado kazi ya vichochezi hivi ni vya hila sana, hivi kwamba njia kuu ya kuelekea kwenye ulevi inaanzwa kukanyagwa hata kabla ya mwathiriwa kushuku hatari yake. [MH 332.2; HU Aya ya 21]

Kuna watu wengine ambao hawafikiriwi kuwa wamelewa, ila kila wakati huwa chini ya ushawishi wa kileo kidogo. Miili yao huwa na homa, hawana utimamu wa akili, na akili yao haina msawaziko mzuri (hamna balansi). Hawa huwa wanajiwazia kuwa wako salama tu, na kisha wanaendelea na safari ya kunywa, mpaka kila kizuizi kitakapovunjwa, na kila kanuni itolewe mhanga. Maazimio yenye nguvu zaidi yanadhoofishwa, mambo ya juu zaidi hayatoshi kuuzima uchu huu mbaya, yaani tamaa iliyoshuka kuelekea chini kwenye uovu, kudhibitiwa na busara. [MH 332.3; HU Aya ya 22]

Hakuna mahali popote katika Biblia panaporuhusu au kuafikiana na matumizi ya juisi ya matunda au mizabibu yenye kuchacha. Divai ambayo

Kristo alitengeneza kwa maji kwenye karamu ya arusi ya Kana ilikuwa ni maji safi ya zabibu. Hii ndiyo “divai mpya.... ipatikanayo katika kishada,” ambayo Maandiko yanasema, “Usiiharibu; kwa maana kuna baraka ndani yake.” Isaya 65:8. [MH 333.1; HU Aya ya 23]

Ni Kristo ambaye, katika Agano la Kale, alitoa onyo kwa Israeli, “Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Mithali 20:1. Yeye Mwenyewe hakuwapa watu kinywaji kama hicho. Shetani huwajaribu watu kuendekeza mambo ya kuwafurahisha ambayo yatafunika hekima na kuweka ganzi akilini kuhusiana na mitazamo ya kiroho, lakini Kristo anatufundisha kuitiisha asili ya chini. Yeye kamwe haweki mbele ya watu kile ambacho kingekuwa ni majaribu kwao. Maisha yake yote yalikuwa kielelezo cha kujinyima. Ilikuwa ni katika kuvunja nguvu ya hamu ya kula ndiyo alifanya mfungo wa siku arobaini jangwani, na kuteseka kwa niaba yetu mtihani mzito zaidi ambao wanadamu wangeweza kustahimili. Kristo Ndiye aliyetoa maagizo kwamba Yohana Mbatizaji asinywe divai wala kileo. Yeye Ndiye aliyemuusia mke wa Manoa kujiepusha na mambo yote yahusianayo na kileo. Kristo hakuyapinga mafundisho Yake Mwenyewe. Divai isiyotiwa chachu ambayo Yeye aliwaandalia wageni kwenye arusi, ilikuwa kinywaji chenye afya na kuburudisha (Yohana 2-juisi freshi). Hii ndiyo divai ambayo ilitumiwa na Mwokozi wetu na wanafunzi Wake katika Komunio au meza ya Bwana ya kwanza. Hii ndiyo divai inayopaswa kutumika kila mara kwenye meza ya Bwana kwenye makanisa yetu kama ishara ya damu ya Mwokozi. Ibada ya sakramenti ya Meza ya Bwana imeundwa ili kuiburudisha nafsi na kutoa uzima. Hakuna chochote chenye kuhudumia uovu kinachopaswa kuunganishwa na huduma hii (hata mkate wenyewe unapaswa usichache, nao unawakilisha mwili wa Yesu, basi hata zabibu nazo hazipaswi kuchacha, maana zinawakilisha damu ya Yesu, kitu cha thamani kupita vyote, hakipaswi kuwakilishwa na matunda yaliyooza). [MH 333.2; HU Aya ya 24]

Kwa kuzingatia kile ambacho tumefundishwa na Maandiko, na asili, na busara ihusuyo matumizi ya vileo, Je, Wakristo wanawezaje kushiriki katika ulimaji wa maua ya mpaini yaitwayo hops kwa ajili ya kutengeneza bia, au katika utengenezaji wa divai au apo cider sokoni? Ikiwa wanampenda jirani yao kama wanavyojipenda wao wenyewe, wanawezaje basi, kujihusisha katika kuweka mtego kwa wanadamu wenzao? (maua ya mpaini yaitwayo hops, pamoja na maji, na nafaka, yalitumika kutengenezea pombe, maua haya yaliongeza kwa namna fulani harufu na asilimia ya kileo kwenye pombe wakati wa utengenezaji. Pombe hutengenezwa kwa njia kadhaa mfano: kuozesha matunda huitwa mvinyo, kuozesha viazi huitwa rum, kuozesha nafaka huitwa bia n.k) [MH 333.3; HU Aya ya 25]

Mara nyingi kutokuwa na kiasi huanza nyumbani. Kwa matumizi ya chakula tajiri chenye kalori nyingi, kilichosindikiwa na kukobolewa, yaani chenye mafuta mengi, chumvi nyingi, na sukari nyingi, kisicho na afya kwa viungo vya umeng'enyaji chakula na kinachodhaifisha tumbo, na kisha ulafi huundwa kwa chakula ambacho bado kinachochea zaidi mwili au ulimi. Kwa hivyo hamu ya kula kitu fulani, kwa kawaida watu ndiyo huifundisha kutamani kila wakati kitu chenye nguvu zaidi na kujenga mazoea kwa kile kilichokolezwa viungo au kuchochea mwili zaidi. Hamu kali ya vichocheo huja mara kwa mara na inakuwa vigumu zaidi kuipinga. Mfumo unajazwa na sumu, kwa ukubwa au kwa udogo, na unaendelea kuwa dhaifu, na ndivyo hamu ya vitu hivi inavyoongezeka. Hatua moja katika mwelekeo mbaya hutayarisha njia nyingine mbovu. Wengi ambao kwa kawaida wasingekuwa na hatia ya kuweka juu ya meza zao divai au kileo cha aina yoyote, meza zao zimechafuliwa au kujazwa na chakula ambacho huleta kiu ya vileo vikali, kiasi kwamba kupinga ushawishi wa pombe, kwao linakuwa jambo lisilowezekana kabisa. Tabia mbaya za ulaji na unywaji huharibu afya na kuandaa njia ya ulevi na uraibu. [MH 334.1; HU Aya ya 26]

Hivi karibuni kutakuwa na ulazima mdogo wa kufanya vita vya kiasi ikiwa vijana katika jamii ambazo ndiyo matofali ya kujenga fasheni za jamii, na kanuni sahihi kuhusiana na kiasi zingeweza kupandikizwa. Hebu wazazi waanze mapambano wenyewe dhidi ya kutokuwa na kiasi wakiwa wanaota moto kwenye sebule zao na kuzungumza na watoto wao, nao wawafundishe watoto kanuni njema toka utoto wao, ambazo watazifuata toka wakiwa wachanga, na hakika watakuwa na matumaini ya kufaulu. [MH 334.2; HU Aya ya 27]

Kuna kazi kwa akina mama katika kuwasaidia watoto wao kujenga tabia sahihi na kuwa na ladha safi. Elimisha hamu ya kula (appetite); wafundishe watoto kuchukia vichocheo (pombe zote, mfano -mbege, chai nyeusi ya china, kahawa, pilipili, na vyakula vilivyokolezwa viungo sana). Wakuze watoto wako ili wawe na uimara wa kimaadili kwamba waweze kupinga uovu unaowazunguka. Wafundishe kutoshawishiwa au kupindishwa na watu wengine, kwamba wasikubali kuathiriwa na mvuto wenye nguvu, bali wawashawishi watu wengine kwa wema. [MH 334.3; HU Aya ya 28]

Juhudi kubwa zinafanywa ili kuweka chini mikakati ya kufagilia mblai kutokuwa na kiasi; lakini kuna juhudi nyingi ambazo hazielekezwi kwenye pointi sahihi. Watetezi wa matengenezo ya afya na kiasi wanapaswa kuwa macho na maovu yanayotokana na matumizi ya vyakula visivyofaa, vikolezo vikali au viungo vinavyokasirisha tumbo*, chai nyeusi ya china, na kahawa. Tunawaombea watendakazi wote wa kiasi kuanza safari hii ya kiasi vizuri;

lakini tunawaalika pia waangalie kwa undani zaidi sababu ya uovu wanaopigana nao na kuwa na thabiti na uendelevu katika kazi yao ya matengenezo. [MH 334.4; HU Aya ya 29]

Tunapaswa kuweka wazi mbele za watu kwamba uwiano sahihi wa nguvu za akili na maadili hutegemea kwa kiwango kikubwa na hali sahihi ya mfumo wa mwili wa mwanadamu. Dawa zote za kulevya, ziwe za famasia au za magendo (narcotics) na vichocheo visivyo vya asili vinavyodhoofisha na kuharibu asili ya mwili huwa na uwezo wa kupunguza utimamu wa akili na maadili mema. Ukosefu wa kiasi umejengwa kwenye msingi wa upotovu wa maadili wa ulimwengu. Kwa kuendekeza na kuzifurahia tamaa potovu, mwanadamu hupoteza uwezo wake wa kuyapinga majaribu. [MH 335.1; HU Aya ya 30]

Wanamatengenezo wa kiasi wana kazi ya kufanya katika kuwaelimisha watu katika mambo haya. Wafundishe kwamba afya, tabia, na hata maisha, yanahatarishwa na utumiaji wa vichocheo, vitu ambavyo husisimua nguvu za mtu zilizochoka-choka tayari kwa hatua isiyo ya asili, ambayo inakuja na kuondoka. [MH 335.2; HU Aya ya 31]

Kuhusiana na chai nyeusi ya China, kahawa, tumbaku, na vinywaji vya pombe, njia pekee iliyo salama ni usiviguse, usivionje, usishughulike navyo (Wakolosai 2:21-23 touch not, taste not, handle not). Mwelekeo wa chai, kahawa, na vinywaji vingine vinavyofanana kwa kuchochea mwili ni mmoja na ule wa kileo na tumbaku, na katika baadhi ya matukio ni vigumu kuacha tabia ya uraibu wa vitu hivyo kama ilivyo kwa mlevi kuacha vileo. Wale wanaojaribu kuacha vichocheo hivi kwa muda watahisi kwamba wamepata hasara na kwamba watateseka wasipokuwa navyo. Lakini kwa kuendelea kuvipinga kwa kutovitumia, watashinda uchu au tamaa yake, na kuacha kuhisi kupungukiwa (upungufu). Asili inaweza kuhitaji muda kidogo ili kupona kutokana na unyanyasaji ambao imeupata; lakini ipe asili nafasi, na itajikusanya tena, na kusimama dede, ikijifunga mkanda, tayari kufanya kazi yake kwa ubora na vizuri kabisa. [MH 335.3; HU Aya ya 32]

Madawa ya kulevya na athari zake katika jamii zetu

Vilevi ambavyo mtumiaji akitumia huleta athari kwenye mwili na akili. Vilevi viko katika mfumo wa kuvuta kama sigara, au baghi, kumung'unya kama pipi, tembe au vidonge, ungaunga wa kunusa, majimaji au vimiminika ambavyo hunywewa, kutafauta na kutema kama miraa, nyingine hupikwa kama mboga, zingine zinaungwa na kufanywa vinywaji, na pia kuna kudunga

sindano mtumiaji anaweza kudhoofika na kuathiri mwili hata kupelekea kifo

Aina nne ya dawa za kulevya

1. Vipumbaza-hupunguza kasi ya mfumo wa fahamu kufanya kazi, mfano ni pombe, heroin na madrake- mfumo wa fahamu huongeza kasi kisha mtu anaweza kuwa na shida ya presha, huleta furaha kidogo, ila mtu akiweka kiwango kikubwa kizunguzungu huweza kuja, kuvuta ulimi na kukosa busara, na kuchanganyikiwa ubongo kiasi cha kushindwa kuratibu shughuli

2. Vichangamshi- Hufanya mfumo wa fahamu kwenda kasi, mifano ni heroin, kahawa, mirungi. Mapigo ya moyo yanapata changamoto na mfumo wa fahamu unaingia na mtu anaanza kuwa na wasiwasi na kukosa usingizi

3. Vileta njozi au hallucinogen- Mfano ni kama banghi, uyoga wa aina fulani. Mtu anajiona anapaa, kuongezeka kwa mboni ya jicho, au macho kutoka kuliko kawaida kuona vitu visivyokuwepo, anajiona katika mazingira tofauti, anaweza kujiona anapaa na kuna kubadilika kwa utambuzi

4. Viyeyushi- Hivi viko katika mvuke au hewa kama vile gundi rangi ya kucha etc petroli nk. Utumiaji wa viyeyushi hufanya kichwa kuuma na kuona mwanga unakuwa mkali

Kwanini watu hutumia vitu hivi?

1. Kufuata mkumbo -mfano marafiki, mtu anaona bora niwe miongoni mwa wezangu

2. Kukimbia matatizo, umasikini, ugomvi kwa vile inamtoa katika uhalisia

Baadhi ya Athari Zake

1. Saratani ya damu au mapafu

2. Kupunguka kwa hewa safi ya oksijeni kwenye damu

3. Kuwakosesha familia matunzo na kuwarithisha watoto wake uovu huu

4. Ajali, talaka na shida zingine

5. mtu anakuwa hana tija kwenye jamii

Watu hawa ni vyema wasaidiwe kuacha hii tabia

Lazima watu wote wasimame ili kupata muafaka, elimu katika mashule na taasisi, na visababishi vichunguzwe. Watu wapewe mahitaji ya msingi kwa kukaa na kuzungumza nao ili uweze kubaini ni nini wanapitiaKwa jumla uraibu unamgharimu kila mwanadamu]

SURA YA 27

USAFIRISHAJI WA VILEO NA MAKATAZO AU MARUFUKU YALIYOWEKWA KWENYE UTUMIAJI

"Ole wake yeye aijengaye nyumba yake kwa uovu! Na vyumba vyake kwa udhalimu; ... asemaye, nitajijengea nyumba pana, na vyumba vipana, na kujikatia

Madirisha yake; na kuta zake zimeezekwa kwa mierezi, na kupakwa rangi nyekundu. Je! utatawala, kwa sababu unashindana na watu kwa mierezi? ... Bali macho yako na moyo wako hauna utakalo ila kutamani, na kumwaga damu isiyo na hatia, na kudhulumu, na kutenda jeuri." Yeremia 22:13-17. [MH 337.1; HU Aya ya 1]

Kazi ya Muuza Pombe

Andiko hili linaonyesha kazi ya wale wanaotengeneza na kuuza vileo. Biashara yao maana yake ni kupora watu. Kwa katika kupokea pesa za watu wanaonunua pombe, hawarudishi bidhaa yenye thamani sawa (bidhaa zao ni sumu, wanapokea pesa ambayo hawastahili, wanawaibia watu, hawawapi mali ambayo ina thamani ya fedha). Kila dola wanayoongeza kwenye mfuko wa0 inaleta laana kwa mtumiaji. [MH 337.2; HU Aya ya 2]

Mungu amewapa wanadamu baraka Zake kwa mkono uliojaa ukarimu. Kama karama Zake zingetumiwa kwa hekima, ni kwa udogo kiasi gani, ulimwengu ungekuwa na umaskini au dhiki! Uovu wa wanadamu ndio unaogeuza baraka Zake Mungu, kuwa laana. Ni kwa uroho wa faida, na uchu wa pombe, ndiyo watu hutumia nafaka na matunda yaliyotolewa na Bwana kwa ajili ya riziki zetu na kuyabadilisha kuwa sumu zinazoleta taabu na uharibifu duniani. [MH 337.3; HU Aya ya 3]

Kila mwaka mamilioni kwa mamilioni ya galoni za vileo hunywewa. Mamilioni kwa mamilioni ya dola hutumiwa kununua unyonge, umaskini, magonjwa, uharibifu, tamaa mbaya, uhalifu, na kifo. Kwa ajili ya kupata faida, muuzaji pombe anashughulika na wahasiriwa wake, kwa kile kinachoharibu na kuangamiza akili na mwili. Analeta umaskini na unyonge kwenyefamilia ya mlevi. [MH 338.1; HU Aya ya 4]

Wakati mhasiriwa wake amekufa, yaani yule baba mlevi, uovu wa muuza pombe haukomei hapo. Anamwibia mjane na kuwafanya watoto wawe

masikini na ombaomba. Hasiti kuchukua mahitaji muhimu ya maisha kutoka kwenye familia maskini, kulipa bili ya kinywaji cha mume na baba aliyekufa na kuacha deni kwenye klabu cha pombe. Vilio vya watoto wanaoteseka, machozi ya mama mwenye uchungu, humuongezea jazba tu. Yeye inamhusu nini ikiwa watoto hawa na mama yao wanateseka kwa njaa? Je, kuna maumivu gani kwake ikiwa watoto hawa pia, watasukumwa kwenye maadili yaendayo chini na uangamivu kama baba yao? Muuza pombe anakuwa tajiri kwa hasara za wale ambao anaowaongoza upotevuni. [MH 338.2; HU Aya ya 5]

Nyumba za ukahaba, mapango ya uovu, mahakama za uhalifu, magereza, nyumba za misaada, nyumba za watu wenye maradhi ya akili, na hospitali, sehemu zote hizi zimejaa kwa kiwango kikubwa kutokana na kazi ya muuzaji wa pombe. Kama vile Babeli ya kimafumbo ilivyo katika unabii wa kutisha wa siku za mwisho, muuza pombe anashughulika na “watumwa, na roho za wanadamu.” Katika kila nyumba ya kila muuzaji pombe amesimama mharibifu mkuu wa roho, yaani Shetani mwenyewe, na kila sanaa ambayo dunia au kuzimu inaweza kubuni, inatumiwa kuwavuta wanadamu chini ya nguvu na utawala wake. Katika majiji na mashambani, kwenye treni, kwenye meli kubwa, mahali pa biashara, katika kumbi za starehe, katika zahanati za tiba, na hata makanisani, kwenye meza ya Bwana takatifu au komunio, mitego yake imechomekwa. Hakuna kinachoachwa bila kuwekewa mtego unaounda na kukuza hamu ya vileo. Karibu kila kona linasimama jumba la umma, likiwa na taa zake zenye kung'aa na giza la namna fulani, makaribisho yake na uchangamfu, unawaalika mwanamume na mwanamke aliyetoka kazini, tajiri mvivu, vijana wasioshuku uovu. [MH 338.3; HU Aya ya 6]

Kwenye vyumba vya vya siri vya chakula cha mchana na majumba ya mtindo, wanawake hupewa vinywaji maarufu, vilivyo na jina fulani la kupendeza, ila ni vileo halisi. Kwa wagonjwa na waliochoka, matangazo ya biashara yanatolewa kwao, ambayo yanajumuisha pombe kwa kiasi kikubwa. [MH 338.4; HU Aya ya 7]

Ili kuunda hamu ya pombe kwa watoto wadogo, pombe huletwa kwenye maduka ya peremende, chokoleti na aisikrimu (ice cream). Maduka hayo ya vitu vitamu kama hivyo huuza pombe. Na kwa zawadi za pipi hizi muuzaji wa pombe huwashawishi watoto kwenye vituo vyake kuhusiana na burudani ya pombe (siku hizi baghi au CBD imeingia kwenye maduka mengi ambayo yanaiuza kama peremende, au kwa mtu yeyote kirahisi, angalia zaidi mtandaoni. [MH 339.1; HU Aya ya 8]

Siku kwa siku, mwezi hadi mwezi, mwaka hadi mwaka, kazi hii inaendelea. Akina baba na waume na kaka, nguzo na tumaini na fahari ya taifa, wanapita

kwa kasi kuelekea kwenye makazi ya wauzaji vileo, ili warudishwe kwao wakiwa wameharibikiwa na kumalizwa. [MH 339.2; HU Aya ya 9]

Kilicho kibaya zaidi, ni laana hii inagonga moyo wa kila nyumba. Wanawake wanaendelea pia kuongezeka kwa idadi, kwenye hizi tabia za ulevi. Katika nyumba nyingi, watoto wadogo, hata katika hali ya kutokuwa na hatia na unyonge wa utoto, wako katika hatari ya kila siku kwa sababu ya kutelekezwa, kunyanyaswa, na unyonge wa wakina mama walevi. Wana na mabinti wanakua chini ya kivuli cha uovu huu mbaya. Je! Hawa watakuwa na mtazamo gani kuhusiana na maisha yao ya baadaye kama siyo kuzama chini zaidi, hata kuliko wazazi wao? [MH 339.3; HU Aya ya 10]

Kutoka kwenye zile zinazoitwa nchi za Kikristo, laana hupelekwa kwenye maeneo ya nchi za kipagani, ambazo zina ibada ya sanamu (Wakristo huwapelekea Wapagani pombe). Masikini, watu hawa wasiostaarabika (washenzi), na wajinga, wote wanafundishwa matumizi ya vileo na Wakristo. Hata miongoni mwa makafiri, ambao wana akili zao timamu, wanatambua na kupinga jambo hilo kuwa ni sumu mbaya; lakini wametafuta na wameshindwa kabisa kulinda nchi zao kutokana na uharibifu wake kutoka kwenye hizi zinazoitwa za magharibi ambazo zamani zilijulikana kama nchi za Kikristo. Watu wanaosemekana ni waungwana, yaani wamestarabika, na kisha wanapeleka tumbaku, vileo na bangi na kuyalazimsiha mataifa ya kipagani wavitumie. Tamaa zisizotawaliwa za yule mtu asiyestaarabika (mshenzi), zikichochewa na unywaji pombe, humshusha hadi kwenye udhalilishaji wa chini kabisa, ambao yeye hakuwa ameujua kabla ya hapo, na inakaribia kuwa kazi isiyo na matumaini kuwatuma tena wamishonari kwenye nchi hizi ili kuwapelekea watu hawa injili (*Mf. Uingereza ilikuwa ikiipa HongKong bhangi ili kuwateka mawazo yao zaidi na kuchukua vitu vyao au kusaidia kazi ya ukoloni vizuri, soma zaidi mtandaoni. Wakati wa uandishi Nchi za Kikristo zilikuwa Ulaya na Marekani, pengine sasa nchi za Kikristo zimegeuka kuwa Afrika na Amerika ya Kusini). [MH 339.4; HU Aya ya 11]

Kupitia mawasiliano na watu ambao walipaswa kuwapa ujuzi wa Mungu, wapagani hawa wanaongozwa katika maovu ambayo yanathibitisha uharibifu wa kabila lote na jamii yote ya ubinadamu. Na katika maeneo ya giza duniani watu wa mataifa yaliyostaarabika ya magharibi, wanachukiwa kwa sababu ya hiana hii. [MH 339.5; HU Aya ya 12]

Wajibu wa Kanisa

Maslahi yahusianayo na vileo au pombe yana nguvu katika ulimwengu wetu tunaoishi. Kwenye upande wake kuna nguvu iliyowekezwa pamoja na pesa, tabia, na hamu ya kula. Nguvu yake inasikika hata ndani ya kanisa. Watu

ambao pesa zao zimepatikana moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja katika biashara ya vileo, ni washiriki wa makanisa, “Washiriki wazuri tu na wa kawaida.” Wengi wao hutoa kwa ukarimu kwenye mashirika ya misaada yanayopendwa na maarufu (NGOs). Michango yao inasaidia biashara za kanisa na kuwategemeza wachungaji au wahudumu wake. Wanaamuru watu wazingatie na kuonyesha nguvu ya pesa. Makanisa yanayokubali washiriki kama hao kwa hakika yanaendeleza biashara ya vileo. Mara nyingi wachungaji hawana ujasiri wa kutetea haki. Hawatangazi kwa walei wao kile ambacho Mungu amesema kuhusu kazi ya muuza vileo. Kusema waziwazi kutamaanisha kuliudhi kanisa lake, kutoa mhanga umaarufu wake au kupendwa kwake na washiriki, na kisha kupoteza mshahara wake. [MH 340.1; HU Aya ya 13]

Lakini juu ya mahakama ya kanisa tunayoiona kwa macho, ipo mahakama ya Mungu Mwenyewe. Yeye ambaye alimtangazia muuaji wa kwanza, “Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi” (Mwanzo 4:10), hatakubali zawadi, au sadaka inayoletwa juu ya madhabahu Yake na muuza vileo. Hasira Yake inawaka dhidi ya wale wanaojaribu kufunika hatia yao kwa joho la ukarimu. Pesa zao zimetapakaa damu. Laana iko juu ya hizo pesa. [MH 340.2; HU Aya ya 14]

11 Huu wingi wa sadaka zenu mnazonitolea una faida gani? Asema Bwana. Nimejaa mafuta ya kafara za kondoo waume, na mafuta ya wanyama walionona; nami siifurahii damu ya ng'ombe wala ya wana-kondoo wala ya mbuzi waume.

12 Mjapo ili kuonekana mbele zangu, ni nani aliyetaka neno hili mikononi mwenu, kuzikanyaga nyua zangu?

13 Msilete tena matoleo ya ubatili; uvumba ni chukizo kwangu; mwezi mpya na sabato, kuita makutano; siyawezi maovu hayo na makutano ya ibada.

14 Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zenu zilizoamriwa, nafsi yangu yazichukia; mambo hayo yanilemea; nimechoka kuyachukua.

15 Nanyi mkunjuapo mikono yenu, nitaficha macho yangu nisiwaone; naam, mwombapo maombi mengi, sitasikia; mikono yenu imejaa damu. Isaya 1:11-15. [MH 341.1; HU Aya ya 15]

Mlevi ana uwezo wa mambo yaliyo bora kabisa. Mungu amemkabidhi amana ya talanta za kumheshimu Yeye na kuubariki ulimwengu; lakini wanadamu wenzake wameibana nafsi yake kwenye mtego na kujijenga wenyewe kimaisha kwa uharibifu wake. Wameishi maisha ya anasa na starehe na huku wahanga maskini wa pombe, ambao wamewaibia, wanaishi katika umaskini na unyonge. Lakini Mungu atahitaji hesabu itolewe kwa hili siku ya hukumu,

kutoka yule ambaye wamemsaidia mlevi kwenda kwenye uharibifu kwa kasi. Yeye Mwenye kutawala mbinguni hajasahau bado sababu ya kwanza ya ulevi au matokeo ya mwisho ya ulevi. Yeye ambaye anamtunza shomoro na kuyavika majani yaliyo makondeni, hatapita karibu na wale ambao wameumbwa kwa mfano Wake, wanadamu walionunuliwa kwa damu Yake Mwenyewe, bila ya Yeye kujali kilio chao. Mungu anatia alama uovu huu wote unaoendeleza uhalifu na taabu hapa duniani. [MH 341.2; HU Aya ya 16]

Ulimwengu na kanisa vinaweza kumpa kibali mtu ambaye amepata mali kwa kuidhalilisha nafsi ya mwanadamu. Wanaweza kumkenulia meno kwa tabasamu yule ambaye anawaongoza watu kwenda chini, hatua kwa hatua katika safari ya aibu na udhalilishaji. Lakini Mungu anaona yote haya, Naye daima hutoa hukumu ya haki. Ulimwengu unaweza kumsifia muuzaji pombe kuwa ni mfanya biashara mzuri; lakini Bwana asema, Ole wake mtu huyo. Atashtakiwa kwa kuwafanya watu wakose matumaini, waingine kwenye taabu na mateso, yanayoletwa ulimwenguni kwasababu tu ya biashara hii ya vileo au pombe. Mtu huyu atalazimika kujibu uhitaji/umasikini, huzuni na ole za wakina mama na watoto ambao wameteseka kwa ajili ya chakula na mavazi na malazi, na ambao wamezika matumaini na furaha yote. Mfanya biashara huyu atalazimika kujibu kwa ajili ya roho alizozituma jehanamu bila ya kutayarishwa katika umilele. Na wale wanaomtegemeza muuza vileo katika kazi yake, wanashiriki katika hatia yake. Mungu anawaambia, "Mikono yenu imejaa damu." (Matangazo ya biashara ya vichocheo vyovyote, viwanda vya bidhaa mbaya kwa mwili) [MH 341.3; HU Aya ya 17]

Sheria za Leseni

Utoaji wa leseni za biashara mbaya ya vileo unatetewa na wengi kwamba umekita katika kulenga uzuiaji uovu wa unywaji pombe. Lakini leseni ya biashara hii inawekewa ulinzi wa kisheria na Serikali. Serikali inaidhinisha uwepo wake, na hivyo kuendeleza maovu ambayo inadai kuwa inayazuia. Chini ya ulinzi wa sheria za leseni za pombe, viwanda vya kutengeneza pombe, wataalamu wa kemia ambao ndiyo wanaitengeneza na kujua kilichomo ndani na ni asilimia ngapi ya kileo iwepo (distillers), na viwanda vya mvinyo vinajengwa kila mahali ndani ya nchi, na muuzaji pombe hutekeleza kazi yake kwa juhudi kwenye milango ya ujirani wetu kabisa. [MH 342.1; HU Aya ya 18]

Mara zingine anakuwa kama amekatazwa kumuuzia kileo mtu aliyelewa au aliyethibithishwa kama mraibu (au hata mtu aliye chini ya miaka 21); lakini kazi ya kuwafanya vijana wawe waraibu na kileo inaendelea kwa kasi. Biashara ya pombe hutegemea sana vijana, kwani watu wa viwanda vya pombe hupenda kuunda hamu ya pombe kwa vijana, na hata uraibu ili maisha ya biashara zao yawe endelevu na wapate faida. Vijana wanaongozwa, hatua

kwa hatua, hadi kufikia tabia ya ulevi, kiu hii inasimikwa, ambayo ndiyo lengo yao wauzaji kuifikia, inaundwa kwa gharama yoyote ili tu waridhishwe kwamba sasa wamempata kijana huyu kuwa mteja wao. Yangekuwa madhara kidogo kama watu hawa wangempa mtu mzima ambaye amethibithishwa kuwa ni mlevi tayari pombe yao, mtu ambaye uharibifu wake mara nyingi, tayari umedhamiriwa kufanywa, kuliko kuruhusu Maua yetu ya taifa, yaani vijana wetu wenye nguvu na uwezekano wa kufanya mengi mazuri wavutwe kwenye uharibifu kupitia tabia hii mbaya. [MH 342.2; HU Aya ya 19]

Kwa kutoa leseni kwa biashara ya vileo, majaribu yanawekwa kila mara mbele ya wale wanaojaribu kujirekebisha kwa kufanya mikakati ya kuachana na pombe. Taasisi zimeanzishwa ambapo waathiriwa wa kutokuwa na kiasi wanaweza kusaidiwa kwenye urejeshwaji wa hali nzuri na hivyo kuondokana na hamu ya kula. Hii ni kazi adhimu/bora; lakini mradi wa uuzaji wa vileo umeidhinishwa na sheria, watu wasio na kiasi wananufaika kwa udogo sana kutoka kwenye makazi yanayojengwa kwaajili ya urejeshwaji wa walevi*. Hawawezi kubaki hapo kila wakati. Lazima wachukue nafasi zao katika jamii tena na kuendelea na maisha. Hamu ya kileo, ingawa imewekwa chini kwa kiasi fulani, haimalizwi kabisa; na majaribu yanapowavamia, kama yanavyotokea kila upande, mara nyingi wao huwa mawindo rahisi ya kurudi tena kwenye ulevi (*rehabilitation homes-nyumba za urejeshwaji, ila vituo hivi ni nadra kuviona Afrika maana vina gharama kubwa kuvijenga, na wengi wanapambana na umasikini, na hivyo haya yapo juu kwenye ufikiaji wao). [MH 342.3; HU Aya ya 20]

Mtu aliyefunga mnyama mkali, na ambaye,akijua tabia ya huyo mnyama, bado akamruhusu awe huru, basi kwa sheria za nchi anawajibika kwa uovu ambao mnyama huyo anaweza kufanya. Katika sheria walizopewa Israeli Bwana alielekeza kwamba wakati mnyama anayejulikana kuwa mkatili aliposababisha kifo cha mwanadamu, uhai wa mwenye mali utafidia gharama ya uzembe au uovu wake. Kwa kanuni hiyo hiyo serikali inayompa muuzaji leseni inapaswa kuwajibika kwa matokeo ya biashara yake. Na ikiwa ni uhalifu unaostahili kifo, Je, kumwachia uhuru mnyama mkali, ni kosa la kuidhinisha kazi ya muuza vileo ? Basi hakika ni kosa la kutisha kwa ukubwa wa kiasi gani! [MH 343.1; HU Aya ya 21]

Leseni za kuuza pombe hutolewa kwa ombi la maalumu kwamba mapato ya kodi za kuuzia vileweshi, yatasaidia hazina ya serikali. Lakini ni mapato gani haya kweli, ukilinganisha na gharama kubwa zinazotumiwa ili kuwashughulikia wahalifu , wendawazimu, na masikini, ambao ni matunda ya biashara ya vileo! (polisi, magereza, msaada kwa ombaomba, hospitali, fedha kwa masikini nk) Mwanamume aliyelewa na pombe anafanya uhalifu halisi; yeye anapofikishwa

mahakamani; wale waliohalalisha biashara hii mbaya wanalazimika kukabiliana na matokeo ya kazi zao wenyewe. Waliidhinisha uuzaji wa rasimu ambayo imemfanya mtu mwenye akili timamu awe mwendawazimu; na sasa ni lazima wampeleke mtu huyo gerezani au kwenye mti wa kumnyongea, na huku mara nyingi mkewe na watoto wake wanaendelea na maisha wakiwa wanyonge na wakiitegemea jamii wanayoishi iwasimamie katika mahitaji waliyo nayo. [MH 343.2; HU Aya ya 22]

Kuzingatia tu kipengele cha kifedha au kipato kwenye swali hili la vileweshi, hakika tunaweza kusema “ni upumbavu mkubwa kiasi gani basi kuvumilia biashara kama hiyo!”. Lakini kweli ni mapato makubwa kiasi gani yawezayo kufidia upotevu wa akili ya mwanadamu, kwa kudhoofisha na kuharibu sura ya Mungu ndani ya mwanadamu, kwa kuharibu watoto, na kuwafanya waishie kwenye ufukara na hata kuwa ombaomba na udhalilishaji, ili tu kuendeleza ndani ya watoto wao mwelekeo mbaya wa baba zao walevi? [MH 344.1; HU Aya ya 23]

Marufuku/Makatazo

Mwanaume aliyejijengea tabia ya kutumia vileweshi yuko katika hali ya kukata tamaa. Ubongo wake ni mgonjwa, nguvu zake za nia au mapenzi zimedhoofika. Kwa kadiri uwezo wowote ndani yake unavyohusika, hamu au uchu wake kwa vileweshi haiwezi kudhibitiwa. Hawezi kusaidiwa kwa busara au hata kushawishiwa kujinyima mwenyewe pombe au kuitawala nafsi yake mwenyewe. Akivutwa ameburutwa kwenye shimo la uovu, mtu ambaye ameamua kabisa moyoni kuacha kunywa kileo huongozwa tena kukamata glasi pombe (au dawa za kulevya), na kwa ladha ya kwanza ya kileo kwenye ulimi wake, kila azimio jema linafeli kabisa, kila salio la nia ya maamuzi au mapenzi inaharibiwa kabisa. Ladha moja ya rasimu ya wazimu wa pombe, hufanya mawazo yote ya matokeo yake kutoweka kabisa. Mke aliyevunjika moyo amesahaulika kabisa. Baba mwenye maadili machafu hajali tena kwamba watoto wake wana njaa au wako uchi. Kwa kuhalalisha biashara hii mbaya, sheria za serikali zinatoa idhini yake kwa anguko hili la roho za watu na linakataa kabisa kusimamisha biashara inayojaza ulimwengu maovu. [MH 344.2; HU Aya ya 24]

Je, jambo hili lazima liendelee kwa namna hii kila wakati? Je! Mwanadamu alazimike kung’ang’ana na kupambana katika kujipatia ushindi wa pombe daima, huku mlango wa majaribu ukiwa wazi mbele yao? Je, laana ya kutokuwa na kiasi inapaswa kutua milele kama doa juu ya ulimwengu uliostaarabika? Je, ni lazima jambo hili liendelee kufagilia mbali maelfu ya nyumba zenye furaha, kila mwaka, kama moto unaoteketeza? Je, meli inapovunjika mbele ya ufuo, huwa watu wanaiangalia tu hivyo bila ya kufanya

kitu? La! Wanahatarisha maisha yao katika juhudi za kuwaokoa wanaume na wanawake kutoka kwenye kaburi la maji. Je, basi, juhudi kubwa kiasi gani zinahitajika katika kuwaokoa wanadamu kutoka kwenye hatima ya uraibu! [MH 344.3; HU Aya ya 25]

Sio mlevi na familia yake peke yao ndio ambao wako hatarini kwa kazi hii ya muuza pombe, na mzigo mzito wa uovu huu mkuu wa biashara ya vileo hauitindikii jamii anayoishi tu. Sisi sote tumeunganishwa pamoja katika mtandao wa ubinadamu. Uovu unaoipata sehemu yoyote ya udugu mkubwa wa kibinadamu huleta hatari na maafa kwa wote. [MH 345.1; HU Aya ya 26]

Wanaume wengi ambao kwa kupenda faida au urahisi wa maisha hawapendi kujihusisha kwa namna yoyote na uzuiaji wa biashara ya vileo, na hawa wamegundua wakiwa wamechelewa sana kwamba biashara hiyo inahusiana nao kwa karibu. Wamewaona watoto wao wenyewe wakidanganywa na kuangamia. Uasi huleta ghasia. Mali iko hatarini. Maisha si salama. Ajali za baharini na nchi kavu zinaendelea kuongezeka. Magonjwa yanayohamasishwa katika maeneo yenye uchafu na unyonge yanaelekea hata kwenye nyumba za fahari za matajiri na zenye starehe (luxury). Uovu unaokuzwa na watoto wa ufisadi na uhalifu huwaambukiza wana na mabinti wa koo zilizosafishwa, zenye elimu nzuri, ujuzi wa sanaa na nidhamu nzuri. [MH 345.2; HU Aya ya 27]

Hakuna mtu ambaye biashara ya pombe haihatarishi maslahi yake. Kila mwanadamu, kwaajili ya ulinzi wake mwenyewe anapaswa kujiweka mwenyewe katika mkao wa kuiharibu biashara hii. [MH 345.3; HU Aya ya 28]

Kumbi za kutunga sheria na mahakama za haki zinapaswa kuwa huru kutokana na laana ya kutokuwa na kiasi kuliko nyanja nyingine yoyote inayohusiana na maslahi ya ulimwengu. Magavana, maseneta, wabunge, majaji, watu wanaotunga na kusimamia sheria za taifa, watu wanaoshikilia maisha ya watu mikononi mwao, watu maarufu wanaoshughulikia haki za watu na mali za wenzao, wanapaswa kuwa watu wenye kiasi kwa ukali sana. Ni kwa njia hii tu ndipo akili zao zinaweza kuwa wazi, na hivyo kutofautisha kati ya mema na mabaya. Ni kwa njia hii tu wanaweza kuwa na uthabiti wa kanuni, na hekima ya kusimamia haki na kuonyesha rehema/huruma. Lakini rekodi inaonyeshaji? Ni wangapi kati ya watu hawa ambao akili zao zimetingwa na ukungu, fahamu zao za mema na mabaya zimekanganyikiwa kwa vileo vikali! Je, ni sheria ngapi zenye kukandamiza zinazotungwa, Je, ni watu wangapi wasio na hatia ambao wamehukumiwa kifo, kupitia ukosefu wa haki wa watunga sheria wanaokunywa pombe, mashahidi, wasimamizi, wanasheria, na hata mahakimu! Kuna wengi, ambao “ni mashujaa wa unywaji wa mvinyo,” na “watu walio hodari katika kuchanganya kileo,” “wasemao uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; wampao haki mwenye uovu ili wapewe ijara, na

kumwondolea mwenye haki, haki yake! Kwa watu kama hawa, Mungu anasema: [MH 345.4; HU Aya ya 29]

“22 Ole wao walio hodari kunywa kileo chenye nguvu, watu waume wenye nguvu kuchanganya vileo;

24 Kwa hiyo kama vile mwali wa moto uteketezavyo mabua makavu, na kama manyasi makavu yaangukavyo katika mwali wa moto; kadhalika shina lao litakuwa kama ubovu, na ua lao litapeperushwa juu kama mavumbi; kwa sababu wameikataa sheria ya Bwana wa majeshi, na kulidharau Neno Lake aliye Mtakatifu wa Israeli.” Isaya 5:22-24. [MH 346.1; HU Aya ya 30]

Heshima ya Mungu, uthabiti wa taifa, ustawi wa jamii, ustawi wa nyumbani, na ustawi wa mtu binafsi, vinadai kwamba kila juhudi iwezekanayo ifanywe katika kuwaamsha watu kutoka kwenye uovu wa kutokuwa na kiasi. Hivi karibuni tutaona matokeo mabaya ya uovu huu kama hatuuoni sasa. Ni nani atakayeweka jitihada iliyoazimiwa kusimamisha kazi ya uharibifu? Bado mashindano hayajaanza. Hebu liundwe jeshi la kukomesha uuzwaji wa pombe kali zinazowatia wanaume wazimu. Acha hatari kutoka kwa usafirishaji wa pombe iwe wazi na hisia ya umma iundwe ambayo itadai marufuku yake. Wacha wanaume walio na ulevi wapewe fursa ya kutoroka kutoka kwa ujinga wao. hebu sauti ya taifa iwadai wabunge wake kukomeshwa kwa msongomano huu mbaya. [MH 346.2; HU Aya ya 31]

“11 Uwaokoe wanaochukuliwa ili wauawe; Nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe.

12 Ukisema, Sisi hatukujua hayo; Je! Yeye aipimaye mioyo siye afahamuye? Naye ailindaye nafsi yako siye ajuaye? Je! Hatamlipa kila mtu sawasawa na kazi yake? “Nawe utasemaje atakapokuadhibu? Kwa kuwa ni wewe mwenyewe umewafundisha kuwa marafiki zako……Mithali 24:11, 12; Yeremia 13:21. [MH 346.3; HU Aya ya 32]

SEHEMU YA 6—NYUMBANI

"Maisha haya, ni shule ya mafunzo ambayo wazazi na watoto watahitimu kwaajili ya kwenda shule ya juu zaidi katika makao makuu ya Mungu."
(mbinguni)

SURA YA 28

HUDUMA YA NYUMBANI

Urejeshwaji na kuinuliwa kwa ubinadamu huanzia nyumbani. Kazi ya wazazi ndiyo kazi yenye kipaumbele cha kila kazi duniani, yaani ndiyo msingi wa kazi zote za mwanadamu. Jamii inaundwa na familia, na kile ambacho wakuu wa familia wataifanya iwe. Linda moyo wako kuliko vyote ulindavyo; Maana ndiko zitokazo "chemchemi za uzima" (Mithali 4:23); moyo wa jumuiya, moyo wa kanisa, na moyo wa taifa ni kaya. Ustawi wa jamii, mafanikio ya kanisa, na ustawi wa taifa, hutegemea mvuto wa nyumbani. [MH 349.1; HU Aya ya 1]

Umuhimu na fursa za maisha ya nyumbani zimeonyeshwa katika maisha ya Yesu. Yeye aliyekuja kutoka mbinguni kuwa Kielelezo na Mwalimu wetu, Alitumia miaka thelathini kama memba/mshiriki wa nyumba huko Nazareti. Kuhusiana na miaka yake aliyoishi kwenye familia, rekodi Yake katika Biblia ni fupi sana kwenye msimu huu wa maisha Yake. Hakuna miujiza mikubwa aliyoifanya, ambayo ilivutia umati wa watu. Hakuna umati wenye shauku ulioziofuata hatua Zake wakati anatembea au hata kusikiliza Maneno Yake. Hata hivyo katika miaka hii yote ya awali, Yeye Alikuwa akitimiza utume Wake wa Kiungu. Aliishi kama mmoja wetu, akishiriki maisha ya nyumbani, akitii nidhamu ya maisha hayo ya nyumbani na akifanya kazi Zake siku kwa siku na kubeba mizigo Yake. Chini ya hifadhi ya nyumba masikini, alishiriki katika uzoefu wa hali yetu ya pamoja kama wanadamu, Yeye "alikua katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu." Luka 2:52. [MH 349.2; HU Aya ya 2]

Katika miaka hii yote ambayo haikuwa na huduma ya umma, maisha Yake yalitiririka katika mikondo ya huruma na kusaidia watu. Kutokuwa na ubinafsi na uvumilivu, subira, ujasiri, uaminifu, kupinga Kwake majaribu, amani Yake isiyo na kikomo na furaha yenye utulivu, vilikuwa na msukumo endelevu kwenye maisha Yake. Alileta angahewa tamu, na iliyovutia ndani ya nyumba, na maisha Yake yalikuwa kama chachu ifanyayo kazi katika masuala ya jamii. Hakuna mtu aliyesema kwamba alimwona akifanya muujiza; walakini wema—uponyaji, na uzima wenye upendo—ulitoka Kwake na kwenda kwa watu

waliojaribiwa, kwa wagonjwa, na wale waliokata tamaa. Kwa njia isiyozuilika, kutokea utoto Wake, Yeye Alihudumia watu wengine, na kwa sababu hii, Alipoanza huduma Yake ya hadhara, wengi walimsikiliza kwa furaha. [MH 350.1; HU Aya ya 3]

Miaka ya mwanzo ya Mwokozi ni zaidi ya mfano kwa vijana. Haya ni somo kwao, na yanapaswa kuwa faraja kwa kila mzazi. Mzunguko wa majukumu ya familia na ujirani ni eneo la kwanza kabisa la kuwekeza juhudi kwa wale wote ambao watafanya kazi kwa ajili ya kuwainua wanadamu wenzao. Hakuna eneo lililo na umuhimu zaidi ambalo tunapaswa kushinikiza juhudi kuliko lile lilokabidhiwa kwa waanzilishi, walinzi na walezi wa nyumba/familia. Hakuna kazi waliyotunukiwa wanadamu ambayo inahusisha matokeo makubwa zaidi au yanayoenda kwa umbali mkubwa zaidi kuliko kazi ya baba na mama. [MH 350.2; HU Aya ya 4]

Ni kwa vijana na watoto wa leo ndiyo mustakabali wa jamii utaamuliwa, jinsi vijana na watoto hawa watakavyokuwa, hakika inategemea nyumba waliyotoka. Kukosekana kwa mafunzo sahihi nyumbani, kukifuatiliwa, kutaonekana kwa wazi kumechangia sehemu kubwa ya ugonjwa huo na huzuni na uhalifu unaowalaani wanadamu. Ikiwa maisha ya nyumbani yangekuwa safi na ya kweli, ikiwa watoto wangelitoka chini ya uangalizi wa majumbani mwao, wakiwa wametayarishwa kwa uangalifu mkubwa kukabiliana na majukumu na hatari za maisha, ni mabadiliko makubwa kiasi gani yangeonekana duniani! [MH 351.1; HU Aya ya 5]

Juhudi kubwa zinawekwa, kisha, pesa na kazi inawekezwa bila kikomo, katika mashirika na taasisi za kurekebisha wahasiriwa wa tabia mbaya. Ila hata hizi juhudi hazitoshi kukidhi hitaji kubwa lililopo. Kwani bado matokeo bado ni madogo sana! Ni wachache kiasi gani wanaorerejeshwa kabisa kwenye hali ya kuwa watu wenye tabia njema! [MH 351.2; HU Aya ya 6]

Watu wengi wanatamani maisha bora, lakini wanakosa ujasiri na azimio la kuachana na nguvu ya mazoea. Wanasinyaa katika kuwekeza jitihada, mapambano na dhabihu inayohitajiwa, na hivyo maisha yao yanaharibika na kuangamizwa. Hivyo hata watu wenye akili mahiri zaidi, watu wenye matarajio ya hali ya juu kuhusu maisha na uwezo ulio bora, waliowekwa kwenye hali nzuri kielimu ili waweze kujaza nafasi za amana na uwajibikaji, wanashushwa hadhi na kupotea kwa maisha haya na maisha yajayo ya milele. [MH 351.3; HU Aya ya 7]

Wale wanaofanya matengenezo, hupitia uchungu mkubwa ulioje, katika kupambana ili kurudisha utu wao! Na maisha yao yote kwa muda mrefu, yanakuwa na katika miili iliyovunjika, nia inayoyumba-yumba, akili

iliyoharibika, na nguvu za nafsi zilizodhoofika, wengi huvuna mavuno ya ule uovu walioupanda. Ni mambo makubwa kiasi gani, yangeweza kutimizwa kama uovu wao ungeshughulikiwa hapo mwanzo majumbani mwao! [MH 351.4; HU Aya ya 8]

Kazi hii imekita kwa kiwango kikubwa kwa wazazi. Katika juhudi zilizowekwa ili kuzuia uendelevu wa kutokuwa na kiasi na maovu mengine ambayo yanakula tabia kama saratani katika mwili wa jamii, ikiwa umakini zaidi ungetolewa katika kuwafundisha wazazi jinsi ya kuunda mazoea na tabia ya watoto wao, matokeo yangekuwa mara mia kwa ubora. Mazoea ambayo ni nguvu ya kutisha sana kwa uovu, yako ndani ya uwezo wa wazazi kuyafanya yawe nguvu kwaa wema. Mazoea yanahusiana sana na mkondo katika chanzo chake, na hili liko upande wa wazazi kuuelekeza huu mkondo ipasavyo. [MH 352.1; HU Aya ya 9]

Wazazi wanaweza kuwawekea watoto wao msingi wa maisha yenye afya na furaha. Wanaweza kabisa kuwatuma kwenda ulimwenguni, kutoka kwenye nyumba zao wakiwa na nguvu ya kiadili ili kupinga vishawishi (stamina), ujasiri na nguvu za kupigana mieleka kwa mafanikio na matatizo ya maisha. Wanaweza kuhuisha ndani yao lengo kuu la maisha na kukuza uwezo wa kuyafanya maisha yawe yenye heshima kwa Mungu na baraka kwa ulimwengu. Wanaweza kutengeneza njia zilizonyooka ili waweze kuzikanyaga kwa miguu yao, wakati wa mwanga wa jua na kivuli, hadi kwenye vilele vya utukufu vilivyo juu mbinguni. [MH 352.2; HU Aya ya 10]

Utume wa nyumbani unaenda mbali zaidi ya wanachama wake wenyewe. Nyumba ya Kikristo inapaswa kuwa somo kuu la kuonyesha ubora wa kanuni za Kweli za maisha. Kielelezo kama hicho kitakuwa na nguvu ulimwenguni. Nguvu kubwa zaidi, kuliko mahubiri yoyote yanayoweza kuhubiriwa ni mvuto wa nyumba ya kweli juu ya mioyo na maisha ya wanadamu (true home). Vijana wanapotoka kutoka katika nyumba kama hiyo, mambo ambayo waliyojifunza yanaambukizwa kwa wengine. Kanuni bora za maisha huletwa katika kaya zingine, na ushawishi wa kuinua hufanya kazi katika jamii. [MH 352.3; HU Aya ya 11]

Kuna wengi wetu ambao tunaweza kuzifanya nyumba zetu kuwa baraka. Burudani zetu za kijamii zisitawaliwe na misukumo ya desturi za ulimwengu, bali na Roho wa Kristo na mafundisho ya Neno Lake. Waisraeli, katika sherehe zao zote, walimjumuisha maskini, mgeni, na Mlawi, ambaye alikuwa msaidizi wa kuhani katika Patakatifu, na mwalimu wa dini na mmishenari. Hawa walichukuliwa kama wageni wao, walipaswa wakaribishwe kwa ukarimu katika hafla zote za shangwe za kijamii na kidini, na kupewa matunzo kwa upole katika magonjwa au mahitaji. Ni watu kama hawa ndio ambao tunapaswa

kuwakaribisha majumbani mwetu. Je, mwaliko kama huu unaweza kuwasaidia kwa ukubwa wa kiasi gani, katika kuchangamka, kushangilia na kutiwa moyo-muuguzi mmishenari au mwalimu, mama aliyelemewa na mzigo, na ambaye anafanya kazi kwa bidii, au watu wanyonge na wazee, ambao mara nyingi wanaishi bila makazi, na kuhangaika kwa umaskini na kukatishwa tamaa mara nyingi. [MH 352.4; HU Aya ya 12]

Yesu alisema “Ufanyapo chakula cha mchana au cha jioni,” “usiwaite rafiki zako, wala ndugu zako, wala jamaa zako, wala jirani zako wenye mali; wao wasije wakakualika wewe tena, ukapata malipo. Bali ufanyapo karamu, waite maskini, vilema, viwete, vipofu, nawe utakuwa heri; kwa maana wao hawana cha kukulipa; kwa maana utalipwa katika ufufuo wa wenye haki.” Luka 14:12-14. [MH 353.1; HU Aya ya 13]

Wageni wa namna hii, ni wale ambao hautapata mzigo mkubwa juu yako kuwakaribisha nyumbani mwako. Huna haja ya kuwatumbuuza kwa mambo mengi au gharama kubwa. Hutahitaji kuwekeza juhudi yoyote katika kufanya maonyesho ili watu wakuone. Joto-joto la ukaribishaji wenye ukarimu, kando ya mahali pa kuotea moto nyumbani mwako, kiti karibu na meza yako nyumbani, fursa ya kushiriki baraka za saa ya maombi, kwa wengi wa watu hawa itakuwa kama wamepata mtazamo wa mbinguni. [MH 354.1; HU Aya ya 14]

Huruma zetu zinapaswa kufurika na kutoka nje kabisa ya mipaka ya ubinafsi na uzio wa kuta za familia. Kuna fursa za thamani kwa wale ambao watafanya nyumba zao kuwa baraka kwa watu wengine. Ushawishi wa kijamii una nguvu ya ajabu. Tunaweza kuutumia ikiwa tutaufanya kuwa daraja la kuwasaidia wale wanaotuhusu na kutuzunguka. [MH 354.2; HU Aya ya 15]

Nyumba zetu zinapaswa kuwa mahali pa kimbilio kwa vijana wanaojaribiwa. Kuna wengi wanaosimama katika njia panda. Kila mvuto, kila mwonekano, unachangia kwenye uchaguzi unaounda hatima yao ya hapa na baadaye. Uovu unawaalika. Vituo vyake vinafanywa ving’ae na kuvutia. Wanapewa ukaribisho kwenye kila kona. Kila mahali tunazungukwa na vijana ambao hawana makazi, na wengi ambao nyumba zao hazina uwezo wa kuwasaidia, uwezo wa kuwainua, na kisha vijana hawa wanaingia kwenye uovu. Wanaelekea chini kwenye uharibifu, wakiwa kwenye kivuli cha milango yetu wenyewe. [MH 354.3; HU Aya ya 16]

Vijana hawa wanahitaji mkono ulionyooshwa kwao kwa huruma. Maneno ya fadhili yanayonenwa kwao kwa urahisi, umakini mdogo tu unaotolewa, utafagilia mbali mawingu ya majaribu yanayokusanyika juu ya nafsi zao. Kuwaonyesha watu huruma za kweli za mbinguni, huwa na uwezo wa

kufungua mlango wa mioyo inayohitaji manukato ya Maneno kama ya Kristo, na mguso sahili na wa upole wa roho ya upendo wa Kristo. Ikiwa tungeonyesha kwamba tunapendezwa na vijana, na kisha tuwaalike kwenye majumba yetu, na kuwazunguka kwa kuwashangilia kama njia ya kuwatia moyo, na kutoa mvuto ulio wa msaada, kuna wengi ambao wangegeuza hatua zao kuelekea njia ya kuelekea juu kwa furaha. [MH 354.4; HU Aya ya 17]

Fursa za Maisha

Muda wetu hapa duniani ni mfupi. Tupo safarini, na tunapita katika ulimwengu huu mara moja tu; hebu tunapopita humo njiani, tufanye mambo mengi yenye kunufaisha kwa kadri iwezekanavyo. Kazi ambayo tumeitiwa kuifanya haihitaji mali au cheo katika jamii, au hata uwezo mkubwa. Inahitaji roho ya fadhili, roho ya kujitoa na kusudi thabiti. Taa, japo ni ndogo sana, ikiwa mwali wake unaendelea kuachwa uangaze, ile taa itaendelee kuwaka, na taa hiyo inaweza kuwa njia na msaada wa kuziwasha taa nyingine nyingi. Nyanja yetu ya ushawishi inaweza kuonekana kuwa ni finyu, na uwezo wetu mdogo, fursa zetu chache, na upatikanaji wake ukawa mdogo; lakini bado uwezekano usio na kikomo ni wetu kupitia utumiaji wa fursa zetu kwa uaminifu majumbani mwetu wenyewe. Ikiwa tutafungua mioyo na nyumba zetu kwa kanuni takatifu za maisha, tutakuwa njia za mikondo yenye nguvu ya uzima. Kutoka kwenye nyumba zetu kutatiririka mikondo ya uponyaji, na kuleta uhai, uzuri na uzaaji wa matunda mahali ambapo sasa kuna jangwa na uhaba. [MH 355; HU Aya ya 18]

SURA YA 29

WAJENZI WA NYUMBA

Yeye aliyempa Hawa Adamu kama msaidizi (helpmeet), alifanya muujiza Wake wa kwanza kwenye sherehe ya arusi. Katika ukumbi wa sherehe, mahali ambapo marafiki na jamaa walifurahi pamoja, ndipo Kristo alianza huduma Yake ya hadhara. Hivyo aliidhinisha ndoa, akiitambua kuwa ni taasisi ambayo Yeye Mwenyewe alikuwa ameianzisha (Ndiye Mwasisi). Aliagiza kwamba wanaume na wanawake wanapaswa kuunganishwa katika ndoa takatifu, ili kulea familia ambazo washiriki wake, waliovikwa taji la heshima, wanapaswa kutambuliwa kuwa washiriki wa familia iliyo juu mbinguni. [MH 356.1; HU Aya ya 1]

Kristo aliheshimu uhusiano wa ndoa kwa kuufanya pia ishara ya muungano kati yake na wale waliokombolewa. Yeye mwenyewe ndiye Bwana-arusi; bibi-arusi ni kanisa, ambalo, kama mteule Wake, anasema, “Wewe ni mzuri, mpenzi wangu; hamna doa ndani yako.” Wimbo Ulio Bora 4:7. [MH 356.2; HU Aya ya 2]

Kristo “alilipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha;...ili liwe takatifu lisilo na mawaa au kunyanzi.” "Vivyo hivyo wanaume wanapaswa kuwapenda wake zao." Waefeso 5:25-28. [MH 356.3; HU Aya ya 3]

Uhusiano wa familia ndio wa karibu zaidi, mwororo zaidi na mtakatifu kuliko mahusiano yoyote duniani. Uhusiana huu ulikusudiwa kuwa baraka kwa wanadamu. Ndoa ni baraka popote pale ambapo agano hili la ndoa linaingiwa/linafanywa kwa kutumia akili na busara, kwa kumcha Mungu, na kwa kuzingatia wajibu wa ndoa. [MH 356.4; HU Aya ya 4]

Wale wanaofikiria kuingia katika mahusiano ya ndoa, yaani kuoa au kuolewa, wanapaswa kuzingatia nini itakuwa tabia na ushawishi wa nyumba wanayoianzisha. Watapokuwa wazazi, amana takatifu inakabidhiwa kwao. Juu yao inategemea kwa kiasi kikubwa mustakabali wa watoto wao katika ulimwengu huu, na furaha katika ulimwengu unaokuja. Kwa kiasi kikubwa wazazi ndio huamua muhuri wa kimwili na wa kimaadili ambao watoto wadogo hupokea. Na hali ya jamii hutegemeana na tabia ya nyumbani; uzito wa ushawishi wa kila familia utaonyeshwa katika mizani ukielekea juu au chini. [MH 357.1; HU Aya ya 5]

Uchaguzi wa mwenzi wa maisha unapaswa kuwa bora zaidi ili kuweza kujipatia hali njema ya kimwili, kiakili, na kiroho kwa wazazi na kwa watoto wao pia— hali ambayo itasaidia kuwawezesha wazazi na watoto pia kuwabariki wanadamu wenzao na kumheshimu Muumba wao. [MH 357.2; HU Aya ya 6]

Kabla ya kuchukua majukumu yanayohusika katika maisha ya ndoa, vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kuwa na uzoefu katika maisha ya vitendo yanayowatayarisha kwa ajili ya majukumu yake na mizigo yake. Ndoa za mapema zisihamasishwe. Uhusiano ulio muhimu sana kama wa ndoa, una matokeo yanayofika mbali, hivyo haupaswi kuchukuliwa kwa haraka, bila ya maandalizi ya kutosha, na kabla ya nguvu za akili na kimwili hazijakuzwa vizuri. [MH 358.1; HU Aya ya 7]

Wahusika, yaani mwanamume na mwanamke wanaweza wasiwe na utajiri wa kidunia, lakini wanapaswa kuwa na baraka kubwa zaidi ya afya. Na katika hali nyingi hawapaswi kutofautiana umri kwa kiasi kikubwa. Kupuuzwa kwa sheria hii kunaweza kusababisha kudhoofika sana kwa afya ya yule aliye na umri mdogo. Na mara nyingi watoto wanaozaliwa wanaporwa nguvu za kimwili na kiakili kwasababu ya umri tofauti wa wazazi wao. Hawawezi kupokea kutoka kwa mzazi aliyezeeka matunzo na mahusiano ambayo maisha yao ya utotoni hudai, na wanaweza kupokonywa mzazi kwa kifo cha baba au mama wakati uleule ambapo upendo na mwongozo wa maisha kwao, unahitajika sana. [MH 358.2; HU Aya ya 8]

Ni katika Kristo pekee, ndiyo ambapo muungano wa ndoa unaweza kufanywa kwa usalama. Upendo wa kibinadamu unapaswa kuchota vifungo vyake vya ukaribu wa mahusiano kutoka kwenye upendo wa Mungu. Ni pale tu Kristo anapotawala, ndipo panapoweza kuwa na mapenzi ya kina, ya kweli, na yasiyo na ubinafsi. [MH 358.3; HU Aya ya 9]

Upendo ni zawadi ya thamani, ambayo tunapokea kutoka Kwake Yesu. Upendo safi na mtakatifu sio hisia, lakini ni kanuni. Wale wanaochochewa na

upendo wa kweli sio watu wanaokosa busara na akili, wala kuwa vipofu. Wakifundishwa na Roho Mtakatifu, hawa wanampenda Mungu kuliko watu wote, na kuwapenda jirani zao kama wao wenyewe. [MH 358.4; HU Aya ya 10]

Hebu wale wanaofikiria kuoa wapime kila hisia na waangalie kila ukuaji wa tabia katika yule ambaye wanamfikiria kuunganisha hatima yao ya maisha naye. Hebu kila hatua kuelekea mapatano ya ndoa ivikwe kiasi, usahili, unyoofu, na kusudi la dhati la kumpendeza na kumheshimu Mungu. Ndoa huathiri maisha ya baada ya kifo katika ulimwengu huu na katika ulimwengu ujao. Mkristo aliye dhati, hatapanga mipango yoyote ambayo Mungu hawezi kuidhinisha. [MH 359.1; HU Aya ya 11]

Ikiwa umebarikiwa na wazazi wanaomcha Mungu, tafuta ushauri kutoka kwao. Waelezee matumaini na mipango yako, jifunze masomo ambayo uzoefu wao wa maisha umewafundisha, na utaokolewa kutoka kwenye maumivu mengi ya moyo. Zaidi ya yote, mfanye Kristo kuwa mshauri wako mkubwa. Jifunze Neno Lake kwa maombi (Mshauri wa ajabu Isaya 9:6). [MH 359.2; HU Aya ya 12]

Chini ya mwongozo huu, hebu kila binti amkubali yule tu aliye na tabia safi, kuwa mwandamani wa maisha yake, mti aliye na tabia za kiume, mtu mwenye utu, mtu mwenye bidii, mtu mwenye mipango mizuri ya maisha, mwaminifu, na yule anayempenda na kumcha Mungu. Hebu kijana wa kiume amtafute binti aliye tayari kusimama kando yake, ambaye anafaa kubeba sehemu yake ya mizigo ya maisha, binti ambaye mvuto wake utamboresha na kumsafisha, na ambaye atamfurahisha katika upendo wake. [MH 359.3; HU Aya ya 13]

"Mke mwenye busara mtu hupewa na Bwana." "Moyo wa mumewe humwamini ..... humtendea mema wala si mabaya siku zote za maisha yake." “Hufumbua kinywa chake kwa hekima; na sheria ya wema, i katika ulimi wake. Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake, Wala hali chakula cha uvivu. Wanawe huondoka na kumwita heri; mumewe naye humsifu, na kusema, Binti za watu wengi wamefanya mema, lakini wewe umewapita wote. Yeye apataye mke wa namna hiyo “Apata kitu chema; naye ajipatia kibali kwa Bwana.” Mithali 19:14; 31:11, 12, 26-29; 18:22. [MH 359.4; HU Aya ya 14]

Ijapokuwa watu wameingia kwenye ndoa kwa uangalifu na busara kubwa, lakini ni wanandoa wachache tu, ndiyo ambao huunganishwa kabisa, wakati sherehe ya ndoa inapofanywa. Muunganiko halisi wa wenzi hawa wawili katika ndoa ni kazi ya miaka mingi ya badaye. [MH 359.5; HU Aya ya 15]

Wakati maisha na mizigo yake, na masumbufu, na changamoto zake ziletazo tashwishwi, zinapokutana na wenzi hawa ambao ndio tu wameoana, mahaba ambayo mara nyingi wenzi huwekeza kwenye fikra zao kabla ya ndoa,

hutoweka. Mume na mke hujifunza tabia ya kila mmoja wao kwani haikuwezekana kujifunza katika mahusiano yao ya awali ya uchumba. Hiki ni kipindi nyeti na muhimu zaidi katika uzoefu wao. Furaha na manufaa ya maisha yao yote ya baadaye hutegemea kuchukua hatua sahihi zinachokuliwa na wenzi hawa sasa. Mara nyingi huu ndiyo wakati ambao kila mmoja anatambua udhaifu na kasoro za mwenzake zisizotarajiwa; lakini mioyo iliyounganishwa na upendo itatambua ubora wa mwenzake, ambao ulikuwa haujajulikana hapo awali. Hebu wote watafute kugundua ubora wa mwingine, badala ya kasoro. Mara nyingi ni mtazamo wetu wenyewe, mazingira ambayo yanatuzunguka sisi wenyewe, ndiyo ambayo ndiyo huamua ni nini kitafunuliwa kwetu kutoka kwa mwingine. Kuna watu wengi wanaoona kuwa kuonyesha mapenzi ni silika ya udhaifu, nao hudumisha hali ya kujizuia kuonyesha upendo kwa kuwa wakavu kwa mwenzi jambo ambalo humfukuza mwenzi au kumfanya awe na ubaridi pia. Roho ya mtu ina tabia ya kuanaglia mkondo wa huruma wa mwingine. Wakati misukumo ya urafiki, ushirikiano na ukarimu inapokandamizwa, huwa inanyauka, na moyo unakuwa ukiwa na baridi. Tunapaswa kujihadhari na kosa hili. Upendo hauwezi kuwepo kwa muda mrefu bila kujieleza na kujionyesha. Usiruhusu moyo wa mtu aliyeunganishwa nawe ufe kwa njaa ya kukosa joto la mapenzi, wema na huruma. [MH 360.1; HU Aya ya 16]

Ingawa matatizo, mashaka, na mambo yanayovunja moyo yanaweza kutokea, mume au mke wasiwe na wazo kwamba ndoa yao ni kosa au ni jambo la kuwakatisha tamaa. Amua kwamba wewe utakuwa yote yanayopaswa kuwa kwa mwenzi wako. Endeleeni kupeana umakini mliokuwa mnapeana wakati wa awali, wakati wa kuposana. Katika kila jambo tianeni moyo katika kupigana katika mapambano ya maisha. Jifunzeni namna ya kuendeleza furaha ya kila mmoja wenu. Hebu kuwe upendo katika pande zote, na uvumilivu wa pande zote. Kisha ndoa, badala ya kuwa mwisho wa upendo, itakuwa kama inavyopaswa kuwa, yaani, mwanzo tu wa upendo wenu. Joto la urafiki wa kweli, upendo unaofunga moyo kwa moyo mwingine, ni muonjo wa urojorojo wa furaha ya mbinguni. [MH 360.2; HU Aya ya 17]

Kila familia, ina mduara mtakatifu ambao unapaswa kulindwa ili usivunjike. Ndani ya mduara huu hakuna mtu mwingine aliye na haki ya kuja ndani isipokuwa mume na mke. Mume au mke asiruhusu mtu mwingine kushiriki siri ambazo ni za kwao wenyewe. [MH 361.1; HU Aya ya 18]

Hebu kila mmoja atoe upendo wake kwa mwingine kwa hiari, kuliko kulazimishwa. Sitawisheni yaliyo na ubora ndani yenu, na muwe wepesi kutambua sifa njema za kila mmoja wenu. Fahamuni ya kuwa kuthaminiwa na mwingine ni kichocheo cha ajabu kinachofanya moyo uridhike kwa furaha na

kufanya mabadiliko ambayo vinginevyo yasingefanyika. Huruma na kumheshimu mwenzi huchochea mwenzi kujitahidi kufanya vitu kwa ubora zaidi, na upendo wenyewe huongezeka kwa kadri unavyochochewa kufikia malengo bora zaidi. [MH 361.2; HU Aya ya 19]

Mume wala mke hapaswi kuunganisha utu wake katika ule wa mwingine-Kila mtu ana upekee wake. Kila mmoja ana uhusiano wake binafsi na Mungu. Kila mmoja wenu anapaswa kujiuliza swali hili, “Je, ni nini sahihi na haki kutenda?” "Je, ni kipi kilicho makosa kufanya?" “Je, ninaweza kutimizaje kusudi la maisha kwa njia bora zaidi?” Hebu utajiri wa mapenzi yako utiririke kwa Yeye ambaye alitoa maisha Yake kwa ajili yako (Mwenyezi Mungu). Mfanye Kristo kuwa wa kwanza na wa mwisho na bora katika kila jambo. Upendo wako Kwake unapozidi kuwa wa kina na wenye nguvu zaidi, ndivyo upendo wenu kwa kila mmoja utatakaswa na kuimarishwa zaidi. [MH 361.3; HU Aya ya 20]

Roho ambayo Kristo anadhihirisha kwetu ni roho ambayo mume na mke wanapaswa kudhihirisha kila mmoja kwa mwenzake. “Kama Kristo Naye alivyotupenda sisi,” “enendeni katika upendo.” “Kama vile kanisa linavyomtii Kristo, vivyo hivyo wake na wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo Naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili Yake.” Waefeso 5:2, 24, 25. [MH 361.4; HU Aya ya 21]

Mume wala mke hapaswi kujaribu kumtawala mwenzake kiholela. Usijaribu kumlazimisha kwa nguvu mwenzako ili akubali matakwa yako. Hamuwezi mkafanya hivi na bado mkatunza upendo wenu kwa kila mmoja wenu. Uwe mwenye fadhili, mvumilivu, na mwenye subira, mwenye kujali, mwungwana na mwenye adabu. Kwa neema ya Mungu mnaweza kufanikiwa kumfurahisha kila mmoja wenu, kama mlivyoahidi kufanya katika kiapo chenu cha ndoa. [MH 361.5; HU Aya ya 22]

Furaha katika Huduma Isiyo na Ubinafsi

Lakini kumbuka kwamba furaha haipatikani kwa kujifungia nyingi wawili wenyewe, na kujiridhisha kwa kumwagiana upendo wenu wote juu ya kila mmoja wenu tu. Tumieni kila fursa pia kwa ajili ya kuchangia furaha ya watu wanaowazunguka, iwe ni ujirani wenu au watu ambao mnajikuta mko nao kwenye maisha yenu ya kila siku. Kumbuka kwamba furaha ya kweli inaweza kupatikana tu katika utumishi usio na ubinafsi. [MH 362.1; HU Aya ya 23]

Uvumilivu na kutokuwa na ubinafsi ni alama ya maneno na matendo ya wote wanaoishi maisha mapya katika Kristo. Mnapotafuta kuishi maisha Yake, mkijitahidi kushinda ubinafsi na uchoyo na kuhudumia mahitaji ya watu

wengine, mtajipatia ushindi baada ya ushindi. Na kwa jambo hilo, ushawishi wenu utaubariki ulimwengu. [MH 362.2; HU Aya ya 24]

Wanaume na wanawake wanaweza kufikia lengo na ubora ambao Mungu ameweka kwao, ikiwa watamchukua Kristo kama msaidizi wao. Kile ambacho hekima ya mwanadamu haiwezi kukifanya, neema Yake itatimiza kwa wale wote wanaojitoa Kwake kwa upendo na wakimtumaini Yeye. Majaliwa Yake yanaweza kuunganisha mioyo katika vifungo ambavyo vina asili ya mbinguni. Upendo hautakuwa kubadilishana maneno laini na ya kudanganyana tu kwa kutia chumvi au kumpaka mwenzako mafuta kwa chupa ya mgongo. Ufumaji wa jora la mbinguni unaweka nyuzi zilizosokotwa kwa mapana na marefu vyema zaidi, kuliko mashine za kushonea majora ya dunia yanavyofumwa. Matokeo yake hakitakuwa kitambaa cha kawaida tu, bali jora linalostahimili uchakavu, mitihani na majaribio. Moyo utafungwa kwa moyo wa mwingine kwa vifungo vya dhahabu, na vya upendo unaodumu (golden bonds). [MH 362.3; HU Aya ya 25]

Nyumba yenye amani ni bora kuliko dhahabu,

Mahali ambapo ukarimu wote wa kando ya moto huja;

Hekalu la upendo na mbingu ya uzima,

Imetakaswa na mama, au dada, au mke.

Haijalishi vile ambavyo nyumba inaweza kuwa duni au nyenyekevu,

Au kujaribiwa kwa huzuni kwa maagizo ya mbinguni,

Baraka ambazo hazikununuliwa au kuuzwa,

Zitakazokuwa zinatamalaki hapo, ni bora kuliko dhahabu. Anon. [MH 362.4; HU Aya ya 26]

SURA YA 30

CHAGUO NA MAANDALIZI YA NYUMBA

Injili ni ‘kirahisisha matatizo’ ya maisha kwa jinsi ya ajabu (injili ni nyenzo ya kufanya maisha yawe rahisi kuishi). Ikiwa maagizo yake, yatazingatiwa, naam, yangeweka wazi matata na changamoto zetu nyingi na kutuokoa kutokana na makosa mengi. Injili inatufundisha kukadiria mambo kwa thamani yake halisi na itatufanya tujitolea mhanga zaidi kwa mambo yenye thamani zaidi, mambo yenye thamani ya kweli—mambo yatakayodumu. Somo hili linahitajika na wale ambao juu yao wamepewa wajibu wa kuchagua makazi ya kuishi. Hawapaswi kujiruhusu kupotoshwa kutoka kwenye lengo lililo la juu zaidi. Watu hawa kumbuke kwamba makao ya duniani yanapaswa kuwa ishara na matayarisho ya makao yetu ya mbinguni. Maisha ni shule ya mafunzo, ambayo wazazi na watoto wanapaswa kuhitimu hadi kuingia kwenye ile shule ya juu katika makao ya Mungu. Wakati eneo la nyumba linatafutwa, hebu kusudi hili kuu, iwe ndiyo kauli mbiu ya chaguo lenu, kusudi kuu la kuongoza uchaguzi wenu. Usitawaliwe na tamaa ya mali, kuamrishwa na mtindo, au desturi za jamii. Fikiria kile kitakachoelekea zaidi kwenye usahili, ukamilifu, afya, na thamani halisi. [MH 363.1; HU Aya ya 1]

Ulimwenguni kote, majiji yanazidi kuwa vitovu vya maovu. Kwenye kila upande kuna matukio, vituko na sauti za uovu. Vishawishi vya ufisadi au tamaa za mwili kama vile uchafu wa ngono, ulevi, ubaradhifu wa pesa, nguvu, mamlaka na rasilimali mbalimbali. Wimbi la rushwa, wizi, kukosa uaminifu, kutumia madaraka vibaya, manyanyaso, kujiunganisha na watu wengine ili kutenda uovu na uhalifu vinazidi kuongezeka na kushamiri kila mahali. Kila siku huleta rekodi ya ukatili, na ujeuri—wizi, mauaji, watu kujiua, na uhalifu usioweza kutamkwa kwa vile unatisha kama nini. [MH 363.2; HU Aya ya 2]

Maisha ya mijini ni ya bandia na ya juu-juu tu (feki). Shauku kubwa ya kujipatia fedha, kimbunga cha msisimko na kutafuta raha, kiu kali ya kujionyesha kwa watu, anasa/luxury, matumbuizo na ubadhirifu kwa kutokuwa na kiasi katika kutumia fedha na rasilimali, yote haya ni nguvu ambazo, zikijumuishwa na umati mkubwa wa wanadamu, zinageuza akili za mwanadamu kutoka kwenye kusudi la Kweli la maisha. Zinafungua mlango wa maovu elfu moja kwa wanadamu. Kwa vijana mambo haya yana nguvu inayokaribia kutozuilika au kupingika kwao. [MH 364.1; HU Aya ya 3]

Mojawapo ya vishawishi vyenye hila na hatari ambavyo huwavamia watoto na vijana katika miji ni kupenda raha. Sikukuu ni nyingi; matukio ya michezo na mbio za farasi huwavuta maelfu, na kimbunga cha msisimko na raha huwavuta mbali na majukumu ya maisha ya kiasi na kutumia akili zao kwa utulivu na utimamu. Pesa ambazo zilipaswa kuhifadhiwa kwa matumizi bora zaidi zinatiririka kwa ajili ya matumbuizo (amusements). [MH 364.2; HU Aya ya 4]

Kupitia kufanya kazi kwa mashirika yenye nguvu ambayo ndiyo yana sauti ya soko (monopolies), na matokeo ya vyama vya wafanyikazi na migomo, hali ya maisha katika jiji inazidi kuwa ngumu zaidi na zaidi. Shida nzito ziko mbele yetu; na kwa familia nyingi, kuondoka mijini kunakuwa jambo la lazima. [MH 364.3; HU Aya ya 5]

Mazingira halisi ya miji mara nyingi ni hatarishi kwa afya. Uwezekano wa kugusana na magonjwa mara kwa mara, kuenea kwa hewa chafu, maji machafu, chakula kisicho kisafi (mbolea, GMO, angahewa lenye uchafuzi kwa viwanda na mioshi ya magari hufanya mimea iwe michafu nk), makao yenye msongamano, giza, yasiyo na afya, ni baadhi ya maovu mengi ambayo watu wanagusana nayo. [MH 365.1; HU Aya ya 6]

Halikuwa kusudi la Mungu kwamba watu wasongamane katika majiji, kwamba wakusanyike pamoja katika nyumba zilisoshonana kama matuta na hata nyumba za kupanga. Hapo mwanzo Yeye aliwaweka wazazi wetu wa kwanza katikati ya mandhari iliyoosheheni uzuri kwa macho na masikio, naye

anatutaka sisi tufurahie mambo hayo hata leo pia. Kadiri tunavyokaribia kupatana na mpango wa asili wa Mungu, ndivyo nafasi yetu inakavyokuwa nzuri zaidi kupata afya ya kimwili, na kiakili, na kiroho. [MH 365.2; HU Aya ya 7]

Makazi yenye nyumba ya bei ghali, madoido yenye kinagaubaga kwenye samani za bei ya juu, maonyesho, anasa/luxury, na kukaa kivivuvivu bila ya kujishughulisha, havitoi mazingira muhimu kwa maisha yenye furaha na yenye kunufaisha wanadamu na kazi ya Mungu. Yesu alikuja duniani ili kutimiza kazi kubwa zaidi ambayo mwanadamu amewahi kuifanya. Alikuja akiwa balozi wa Mungu, ili kutuonyesha jinsi ya kuishi na kupata matokeo bora zaidi maishani. Je, ni vigezo gani muhimu, vilivyobainishwa katika uchaguzi na Baba asiye na mwisho kwa ajili ya Mwanawe kama makazi Yake hapa duniani, kabla hajashuka duniani na kufanyika mwili? Nyumba iliyojitenga katika vilima vya Galilaya; kaya inayodumishwa na kazi zenye uadilifu, kazi inayomheshimsha mtu kwa mapato halali kwa kutoa jasho; maisha sahili na ya unyenyekevu; migogoro ya kila siku, changamoto na ugumu wa maisha; kujidhabihu, maisha yenye kuweka umakini katika kushughulika na uchumi kwa jinsi ipasavyo, na utumishi wenye subira, na kufurahisha; saa ya kusoma kando ya mama Yake, wakiwa na gombo la Maandiko lililofunguliwa; utulivu wa alfajiri au jioni katika bonde la kijani; huduma takatifu itokanayo na kitabu cha asili (book of nature); ujifunzaji wa uumbaji na majaliwa ya Mungu; na ushirika wa nafsi na Mungu—hizi ndizo hali na fursa za maisha ya awali ya Yesu zilivyokuwa. [MH 365.3; HU Aya ya 8]

Hali hii ndivyo ilivyo pia, kwa idadi kubwa ya watu bora na watukufu wa kila kizazi-wamepitia kwenye mazingira kama haya. Soma historia ya Abrahamu, Yakobo, Yosefu, Musa, Daudi, na Elisha. Jifunze maisha ya watu wa nyakati za baadaye ambao walikuwa na sifa au stahiki ya kujaza nafasi za amana kwa jinsi ipasavyo, nafasi zinazotumainiwa, na zenye uwajibikaji, watu ambao ushawishi wao umekuwa wa ufanisi zaidi katika kuuinua ulimwengu. [MH 366.1; HU Aya ya 9]

Wengi wa watu hawa walilelewa katika nyumba zilizokuwa nje ya miji, huko mashambani. Walijua anasa kidogo (luxury chache). Hawakutumia ujana wao katika kujifurahisha na matumbuizo. Wengi walilazimika kuhangaika na umaskini na shida. Walijifunza namna ya kufanya kazi mapema maishani mwao, yaani utotoni, na maisha yao ya kazi katika hewa ya wazi nje ya nyumba, yalitoa nguvu na unyumbulifu kwenye vitivo vyao vyote vya mwili. Wakiwa wamelazimishwa kutegemea rasilimali zao wenyewe, walijifunza kupambana na matatizo na kushinda vikwazo, na wakapata ujasiri na uvumilivu. Walijifunza masomo ya kujitegemea na kutawala nafsi zao. Wakiwa

wamejikinga kwa kiwango kikubwa kutokana na mahusiano ya marafiki waovu, walitosheka na starehe za asili na mahusiano bora yatakayowasaidia kuboreshana, urafiki wa dhati (wholesome companionships). Walikuwa na ladha sahili na kiasi katika tabia zao. Walitawaliwa na kanuni, na walikuwa safi, watu wenye nguvu na Kweli. Walipoitwa kwenye kazi yao ya maisha, waliitika na kuja kwenye kazi hiyo wakiwa na nguvu za kimwili na kiakili, nishati na uchangamfu wa roho, uwezo wa kupanga na kutekeleza, na uthabiti katika kupinga maovu, ni mambo ambayo yaliwafanya kuwa watu wenye uwezo chanya kwa ajili ya wema duniani. [MH 366.2; HU Aya ya 10]

Urithi ulio bora kuliko mwingine unaoweza kuwapa watoto wako, ule ambao unazidi mali, ni zawadi ya afya ya mwili utimamu wa akili, na tabia nzuri. Elewa vizuri kile kinachojumuisha mafanikio ya kweli maishani. Wazazi watazingatia mambo bora zaidi maishani katika uchaguzi wao wa nyumba ambayo ndiyo itakuwa makazi yao. [MH 366.3; HU Aya ya 11]

Badala ya kuishi mahali ambapo kazi za mikono ya wanadamu tu ndiyo zinaweza kuonekana, mahali ambapo macho yanaona na masikio kusikia vurugu, mahangaiko, na misukosuko, na kuleta uchovu na mfadhaiko. Nenda mahali unapoweza kutazama kazi za Mungu. Pata pumziko la roho katika uzuri, utulivu na amani ya asili/nature. Hebu jicho lako litulie kwenye mashamba ya kijani kibichi, vichaka vya miti na vilima. Tazama juu anga la buluu, ambalo halijafunikwa na vumbi na moshi wa jiji, nawe upumue hewa ya mbinguni yenye kuchangamsha. Nenda mahali ambapo, ni mbali na vikengeusha-fikira (distractions) na akili haitatenganishwa na Mwenyezi Mungu kirahisi kwa maisha ya mjini ya anasa na uovu, hapo unaweza kuwapa watoto wako muda wako wa kuhusiana nao, hapo ndiyo mahali ambapo unaweza kuwafundisha jinsi ya kujifunza juu ya Mungu wa mbinguni, kupitia kazi Zake, na kuwazoeza kwa ajili ya maisha ya uadilifu na manufaa. [MH 367.1; HU Aya ya 12]

Urahisi katika Samani/Fenicha

Tabia zetu za bandia hutunyima baraka nyingi, raha na starehe nyingi (hatuenjoy), na hazitufai katika kuishi maisha yenye kutunufaisha sisi wenyewe au kuwanufaisha watu wengine. Samani za nyumba za fahari na gharama kubwa sio tu ni upotevu wa pesa, lakini pia ni kupoteza kile ambacho ni cha thamani zaidi mara elfu (muda na akili timamu). Fenicha au vyombo hivi vya ndani ya nyumba, ni mzigo mzito katika kuvitunza, na kazi na mahangaiko na pilikapilika zingine. [MH 367.2; HU Aya ya 13]

Je, hali ikoje katika nyumba nyingi, hata pale ambapo rasilimali ni chache na kazi ya familia inamtegemea mama zaidi? (watu ni masikini). Upambaji wa vyumba vilivyo bora zaidi unatolewa kwenye mtindo kuliko fedha walizo nazo

wakazi, na vyumba hivi havisaidii kurahisisha maisha kwa kuwafanya watu hawa wastarehe vizuri au kufurahia maisha (hakuna kuenjoy nyumba hizi kwaajili ya staili za mitindo ya kupamba nyumba au fanicha). Kuna mazulia ya bei ghali, samani zilizochongwa kwa ustadi, maridadi na nyeti, zikiwa na vitambaa laini kama hariri au velvet nzuri, au kutariziwa kwa kazi ya ustadi na kuvifanya kuwa mzigo kuvitunza. Meza, fremu za mbao zenye mapambo kwenye mahali pa kuotea moto zilizo ghali nk, kisha kila nafasi nyingine inayopatikana ndani ya nyumba imejazwa kwa mapambo, na kuta zimefunikwa na picha, mpaka macho yanapata uchovu kuangalia haya yote kwa jinsi yalivyosheheni. Na ni kazi kubwa kiasi gani inayohitajika ili kuweka vitu hivi vyote katika utaratibu na pasipo vumbi! Kazi hii, na tabia zingine feki au za bandia za familia zinazohenyeka ili kuendana na mtindo, humlazimisha mama mwenye nyumba afanye kazi ngumu isiyo na mwisho ili tu aweze kuvidumisha. [MH 367.3; HU Aya ya 14]

Katika nyumba nyingi mke na mama hawana muda wa kusoma, na hata kujiweka katika hali ya kupata maarifa kwa kujijulisha mambo yanayoendelea duniani au katika ulimwengu wa kiroho, hana wakati wa kuwa mwandamani wa mume wake, hana wakati wa kuwasiliana na akili za watoto wake zinazoendelea kukua kila kukicha. Hana muda au mahali pa Mwokozi mpendwa wa thamani kuwa mwandamani wake wa karibu. Pole pole anazama katika dhiki ya kazi za nyumbani zinazochosha nguvu zake, zinazoboesha, na zisizofurahisha na kisha wakati wake na shauku zake (kiroho na hobby) humezwa katika vitu hivi vinavyoharibika kadri vinavyoendelea kutumika. Wakati akiwa amechelewa sana anaamka na kujikuta amekuwa kama mgeni katika nyumba yake mwenyewe. Fursa za thamani alizo nazo za kuwashawishi wapendwa wake kwaajili ya maisha ya juu mbinguni, hazijaboreshwa, na hivyo zimepita milele. [MH 368.1; HU Aya ya 15]

Hebu wale wanaotengeneza makazi ya kuishi, waamue kuishi kwa mpango wa busara zaidi. Hebu lengo lako la kwanza liwe kutengeneza nyumba ya kupendeza. Hakikisha unatoa nafasi ya vifaa ambavyo vitapunguza nguvu-kazi na kukuza afya na faraja (comfort). Panga kwa ajili ya burudani ya wageni ambao Kristo ametuagiza tuwakaribishe, na ambao anasema kuhusu watu hawa, “Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi. Mathayo 25:40. [MH 369.1; HU Aya ya 16]

Pamba nyumba yako kwa vitu vilivyo rahisi na sahili kutumika na kutunzwa, (plain and simple), vitu ambavyo vitahimili hali ya kusogezwa, na kushikwa, vile ambavyo havivunjiki au kuharibika kirahisi, vitu ambavyo vinaweza kuwekwa safi kwa urahisi, na ambavyo vinaweza kubadilishwa pale vinapochakaa bila ya gharama kubwa. Kwa kutumia ladha yenye busara nzuri,

wewe unaweza kuifanya nyumba iliyo sahili sana, yenye kuvutia na yenye kukaribisha macho ya watu, ikiwa upendo na kuridhika vimo humo ndani ya nyumba. [MH 370.1; HU Aya ya 17]

Mazingira Mazuri

Mungu anapenda uzuri, na urembo. Yeye Ameivika dunia na mbingu uzuri, na kwa furaha ya Baba anatazama furaha ya watoto Wake wanaposhiriki katika vitu ambavyo ameviumba. Anatamani tuzingire nyumba zetu kwa uzuri wa vitu vya asili. [MH 370.2; HU Aya ya 18]

Takribani wakaaji wote nchini, haijalishi wawe maskini kwa kiasi gani, wangeweza kuwa na maeneo yenye nyasi za kijani kibichi, miti michache inayotoa vivuli, vichaka vya maua, au maua yenye harufu nzuri. Na vitu hivi vitahudumia furaha ya familia au kaya kuliko mapambo yoyote ya bandia yanavyoweza kuhudumu. Vitaleta katika maisha ya nyumbani ushawishi wenye kulainisha, kuboresha, kusafisha, na kuimarisha kuipenda asili, na kuwavuta washiriki wa kaya karibu zaidi na wao kwa wao na karibu zaidi na Mungu. [MH 370.3; HU Aya ya 19]

SURA YA 31

MAMA

Namna vile wazazi walivyo, kwa kiwango kikubwa ndivyo watoto watakuwa. Hali ya wazazi ya kimwili, mambo yao yalivyojipanga na hamu zao ya kula, mielekeo yao ya kiakili na kimaadili, kwa kiwango kikubwa au kidogo, hutozalishwa kwa watoto wao, nayo huathiri, tabia, mienendo na mitazamo kwa watoto wao. [MH 371.1; HU Aya ya 1]

Kadiri malengo yanavyokuwa mazuri au bora zaidi, ndivyo karama za kiakili na kiroho zinavyokuwa za juu zaidi, na kadiri nguvu za kimwili za wazazi zinavyokuzwa, ndivyo miili ambayo wanawapa watoto wao itavyokuwa bora zaidi. Katika kukuza na kupalilia vile vilivyo bora zaidi kwao wenyewe, wazazi huwa wanashinikiza mvuto katika kuiejenga jamii na kuviinua vizazi vijavyo

(mwili hapa unaitwa chombo cha maisha au life equipment). [MH 371.2; HU Aya ya 2]

Baba na mama wanapaswa kuelewa wajibu wao. Ulimwengu umejaa mitego inayonasa miguu ya vijana. Umati wa watu unavutiwa na maisha ya ubinafsi na starehe zinazohusisha tamaa za mwili kama vile ngono chafu na ulevi. Watu hawawezi kutambua hatari zilizofichika au mwisho wa kutisha wa njia ambayo inaonekana kwao kama ni njia ya furaha tu. Kupitia kuendekeza na kujifurahisha na uchu wa chakula na tamaa za mwili, nguvu zao zinapotea, na mamilioni wanaharibikiwa kwa ajili ya ulimwengu huu na kwa ulimwengu ujao. Wazazi wanapaswa kukumbuka kwamba watoto wao lazima wakutane na majaribu haya. Hata kabla ya mtoto kuzaliwa, maandalizi ambayo yatamwezesha mtoto kupigana vita na kupata mafanikio kwenye dhidi ya uovu, yanapaswa kuanza mara moja. [MH 371.3; HU Aya ya 3]

Wajibu huu upo zaidi juu ya mama. Yeye, ndiye ambaye damu yake inampa lishe, mtoto hulishwa na umbo la mwili wake hujengwa kwa hivyo virutubisho vyake, na mama ndiye humpa mtoto mvuto wa kiakili na wa kiroho ambao huelekea katika kujenga akili na tabia. Alikuwa Yokebedi, mama wa Kiebrania, ambaye, kwaajili ya nguvu yake ya imani, “hakuogopa amri ya mfalme” (Waebrania 11:23), mama huyu ndiye alimzaa, yule ambaye alikuwa mkombozi wa Israeli. Ilikuwa ni Hana, mwanamke wa maombi na mwenye kujidhabihu nafsi yake na aliyehuishwa na mbingu, ambaye alimzaa Samweli, mtoto aliyefundishwa na mbingu, mwamuzi asiye na ufisadi, mwanzilishi wa shule takatifu za Israeli (schools of prophets) Alikuwa Elizabeti jamaa wa ukoo na marafiki walioshibana na kufanana kwa ukaribu na Mariamu wa Nazareti, ambaye alikuwa mama wa mtangazaji wa kuzaliwa kwa Mwokozi. [MH 372.1; HU Aya ya 4]

Kiasi na Kujitawala nafsi-Kujidhibiti

Uangalifu ambao mama anapaswa kuulinda katika mazoea yake ya maisha unafundishwa katika Maandiko. Wakati Bwana anamwinua Samsoni kuwa mkombozi wa Israeli, “malaika wa Yehova” alimtokea mama huyo, akiwa na maagizo ya pekee kuhusu tabia zake zinavyopaswa kuwa, na pia kile cha kumtendea mtoto wake atakayezaliwa. “Jihadharini,” akasema, “na sasa msinywe divai wala kileo, wala msile kitu chochote kilicho najisi. Waamuzi 13:13, 7. [MH 372.2; HU Aya ya 5]

Athari za mivuto kabla ya mtoto kuzaliwa zinaangaliwa na wazazi wengi kama suala la muda mfupi; lakini mbingu hazichukulii suala hilo hivyo. Ujumbe uliotumwa na malaika wa Mungu, na kutolewa mara mbili kwa njia

iliyoshinikiza kwa uzito mkubwa, unatuonyesha sisi kuwa unastahili kuwekewa umakini wetu mkubwa zaidi. [MH 372.3; HU Aya ya 6]

Katika haya Maneno aliyoambiwa mama wa Kiebrania, Mungu anazungumza na mama wote katika kila kizazi. “Mkeo anapaswa kushika yote niliyomwambia-Hebu na ajihadhari,” malaika akasema; “yote niliyomwamuru na ayafuate.” Ustawi wa mtoto unaathiriwa na tabia za mama. Hamu yake ya kuridhisha mwili hasa ya chakula na shauku zake zinapaswa kudhibitiwa na kanuni. Kuna jambo analopaswa kuliepuka, jambo ambalo anapaswa kulipinga kabisa, ikiwa huyu mama atatimiza kusudi la Mungu kwa ajili yake la kumpa mtoto wake kile kilicho bora. Ikiwa kabla ya kuzaliwa kwa mtoto wake yeye anaiendekeza nafsi yake mwenyewe na kujifurahisha, ikiwa ana ubinafsi, uchoyo, asiye na uvumilivu, na mkali, sifa hizi zitaonekana katika tabia ya mtoto. Hivyo watoto wengi wamepokea kama haki ya urithi wa kuzaliwa, mielekeo ya uovu ambayo yaonekana ni kana kama inakaribia kabisa kushindwa kupingana na uovu. [MH 372.4; HU Aya ya 7]

Lakini ikiwa mama atashikamana na kanuni zifaazo bila ya kuyumbayumba, ikiwa ni mwenye kiasi na mwenye kujinyima au kuikana nafsi yake, ikiwa ni mwenye fadhili, mpole, na asiye na ubinafsi, yeye anaweza kumpa mtoto wake sifa hizo-hizo zenye thamani. Amri yenye katazo la matumizi ya divai kwa mama huyu lilikuwa wazi kabisa. Kila tone moja la kinywaji kikali anachokunywa mama ili kutosheleza hamu yake, huhatarisha afya ya mwili, akili, na maadili ya mtoto wake, na ni dhambi ya moja kwa moja dhidi ya Muumba wake. [MH 373.1; HU Aya ya 8]

Washauri nasaa wengi husisitiza kwamba kila takwa ya mama mjamzito ni lazima litoshelezwe; kwamba ikiwa anataka hamu ya chakula chochote, basi, hata kama kitakuwa na madhara au hatari kwake, basi yeye ajiendekeze tu kwenye mwelekeo huo wa kufurahisha hamu yake ya chakula. Ushauri kama huo ni mbaya na wa uwongo. Mahitaji ya kimwili ya mama hayapaswi kupuuzwa. Maisha ya watu wawili yanamtegemea, na matakwa yake yanapaswa kuzingatiwa kwa ulaini/wororo, ni kweli anapaswa kutimiziwa mahitaji yake kwa ukarimu. Lakini katika wakati huu zaidi kuliko wakati mwingine wowote, katika nyanja ya chakula, huyu mama anapaswa kuepuka chochote kitakachopunguza nguvu za kimwili au za kiakili. Kwa amri ya Mungu Mwenyewe, mama mjamzito amewekwa chini ya wajibu mzito sana wa kujitawala nafsi. [MH 373.2; HU Aya ya 9]

Kufanya kazi kupita kiasi

Nguvu ya mama inapaswa kuthaminiwa kwa upole. Badala ya kutumia nguvu zake za thamani katika kazi inayochosha, masumbufu na mizigo yake

inapaswa kupunguzwa. Mara nyingi mume na baba anakuwa hafahamu sheria za kimwili ambazo ustawi wa familia yake unahitaji azielewe. Akiwa amejikita katika mapambano ya kutafuta riziki, au amejikita katika kutafuta mali na kubinywa na mahangaiko na fadhaa, huwa anaruhusu mke na mama abebeshwe mizigo ambayo hulemea nguvu zake katika kipindi hiki kigumu zaidi na kusababisha unyonge na maradhi. [MH 373.3; HU Aya ya 10]

Waume na baba wengi wanaweza kujifunza somo lenye msaada kutoka kwenye utunzaji wa mchungaji mwaminifu. Yakobo, alipohimizwa afunge safari ya haraka na ngumu, alijibu hivi: [MH 374.1; HU Aya ya 11]

“Watoto ni wachanga, tena kondoo na ng’ombe nilio nao wanyonyesha. Hao wanyama wakiharakishwa siku moja, watakufa wote wako ……nitawaongoza polepole kwa kadri ya mwendo wa wanyama walio mbele yangu, kwa kwa kadiri ya mwendo wa watoto….” Mwanzo 33:13, 14. [MH 374.2; HU Aya ya 12]

Katika maisha yenye kazi ngumu hebu mume na baba ‘asonge mbele kwa upole,’ kwa kuwa kama mwandamani wa safari yake, yeye aweza kuvumilia mengi kuliko huyu mama. Katikati ya shauku ya dunia ya pilikapilika za kukimbilia mali na utawala, hebu na ajifunze kupunguza hatua zake, kwa kumfariji na kumuunga mkono yule aliyeitwa kutembea kando yake. [MH 374.3; HU Aya ya 13]

Uchangamfu

Mama anapaswa kusitawisha tabia ya uchangamfu, kuridhika na furaha. Kila juhudi katika mwelekeo huu italipwa kwa wingi katika ustawi wa mwili na tabia ya maadili ya watoto wake. Roho ya uchangamfu itakuza furaha ya familia yake na kwa kiwango kikubwa sana kuboresha afya yake mwenyewe. [MH 374.4; HU Aya ya 14]

Hebu mume amsaidie mke wake kwa huruma yake na upendo usiofeli. Ikiwa anataka kumfanya mkewe aburudike na kuwa mwenye furaha, ili ang’ae kama mwanga wa jua hapo nyumbani mwao, basi na amsaidie kubeba mizigo yake. Fadhili, uungwana na adabu iliyoandamana na upendo, itakuwa kwa mkewe kama kitia-moyo chenye thamani, na furaha anayoitoa baba mwenye nyumba, itamrudia kwa kuleta furaha na amani moyoni mwake. [MH 374.5; HU Aya ya 15]

Mume na baba ambaye si mcheshi, mbinafsi, na mwenye jeuri, sio tu kwamba mwenyewe hana furaha, bali pia anatupa kivuli cha huzuni kwa wakazi wote wa nyumbani mwake. Mwanamume huyu atavuna matokeo kwa kumwona mkewe akiwa amekata tamaa na mgonjwa, na watoto wake

wakiharibikiwa kwaajili ya hulka yake mwenyewe isiyopendeza. [MH 374.6; HU Aya ya 16]

Ikiwa mama atanyimwa matunzo, faraja na starehe za maisha anazopaswa kuwa nazo (comfort), ikiwa ataruhusiwa kutumia nguvu zake kwa kufanya kazi kupita kiasi au kwa wasiwasi na utusitusi, watoto wake watanyang'anywa nguvu muhimu na unyumbulifu wa akili na nishati ya uchangamfu wanaopaswa kuurithi. Ni bora zaidi kuyafanya maisha ya mama kuwa angavu na ya uchangamfu, ili kumkinga na uhitaji, na kazi ngumu inayochakaza mtu, na masumbufu yenye kuhuzunisha, na kuwaacha watoto warithi katiba nzuri ya mwili, ili waweze kupambana na maisha kwa nguvu zao wenyewe. [MH 375.1; HU Aya ya 17]

Heshima na wajibu uliotunukiwa juu ya baba na mama ni mkuu, kwa kuwa wanapaswa kusimama mahali pa Mungu kwa watoto wao. Tabia zao, maisha yao ya kila siku, mbinu zao za mafunzo, zinafasiri Maneno Yake Yehova kwa hawa walio wadogo. Ushawishi wao utashinda au kurudisha nyuma ujasiri na imani ya mtoto katika Uhakikisho wa Bwana. [MH 375.2; HU Aya ya 18]

Upendeleo wa Wazazi katika Mafunzo ya Mtoto

Wana furaha wazazi ambao maisha yao yanaakisi tabia halisi ya Mwenyezi Mungu, ili ahadi na amri za Mungu ziamshe katika mtoto shukrani na kicho; wazazi ambao huruma, ulaini, haki na uadilifu na ustahimilivu hutafsiri kwa mtoto upendo na haki na uvumilivu wa Mungu, basi, hakika wazazi hawa humfundisha mtoto kumpenda na kumwamini na kumtii Baba yake wa mbinguni. Wazazi wanaompa mtoto zawadi kama hiyo wanakuwa wamemkrimia hazina yenye thamani zaidi kuliko utajiri wa zama zote—hazina inayodumu milele zote. [MH 375.3; HU Aya ya 19]

Kila mama ana jukumu takatifu kutoka kwa Mungu, kwa kila mtoto ambaye Bwana amempa kumtunza,. “Mchukue mwana huyu, au binti huyu,” Yeye Anasema; “Mfunze kwa ajili Yangu; mpe umbo linalong'aa kwa mfano wa jumba la kifalme la mbinguni, ili apate kung'aa katika nyua za Bwana milele." (Zaburi 144:12) [MH 376.1; HU Aya ya 20]

Kazi ya mama mara nyingi kwake inaonekana kama vile ni huduma isiyo na umuhimu. Ni kazi ambayo haithaminiwi sana. Watu wengine wanajua kwa udogo sana kuhusu masumbufu na mizigo yake mingi. Siku zake zimejawa na pilikapilika na majukumu madogo-madogo, yote yakihitaji jitihada yenye subira, kujikana nafsi, busara, hekima, na upendo wenye kujidhabihu; lakini yeye hawezi kujivunia kile alichokifanya kwa siku hiyo kwamba amepata mafanikio yoyote makubwa. Alichokifanya ni kuweka tu sawa mambo yote ili yaende vizuri; mara nyingi akiwa amechoka na kuchanganyikiwa, anakuwa

amejaribu kuzungumza kwa fadhili na watoto wake, kuwashughulisha na hivyo kufanya muda wao upendeze na kuwa wa furaha, na pia ameongoza miguu hiyo midogo katika njia sahihi. Mama hapa huwa anajisikia kana kwamba hajatimiza lolote siku hiyo. Lakini jambo hili sio hivyo. Malaika wa mbinguni humtazama mama aliyechoka kwa masumbufu, na kuona kila mizigo anayobeba siku baada ya siku. Huenda jina lake lisisikike ulimwenguni, lakini hakika limeandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo *(hakuwa kwenye taarifa ya habari kama shujaa ila ana rekodi bora zaidi)* [MH 376.2; HU Aya ya 21]

Fursa aliyopewa Mama

Kuna Mungu aliye juu, na nuru na utukufu kutoka kwenye kiti Chake cha enzi hukaa juu ya mama huyo mwaminifu anapojaribu kuwaelimisha watoto wake kupinga mvuto wenye uovu. Hakuna kazi nyingine duniani inayoweza kufanana na yake kwa umuhimu. Yeye, ukimlinganisha na fundi wa sanaa, hajachora umbo lenye urembo kwenye picha (fine art), wala, kama fundi wa sanaa ya uchongaji (sculptor), hajachonga kutoka katika mawe ya marumaru na kutengeneza umbo. Yeye, hajajumuisha wazo lolote zuri na kuliweka katika maneno yenye nguvu kwa uandishi wa vitabu, wala, kama mwanamuziki, hajazielezea hisia nzuri kwa kuziweka katika wimbo. Kazi yake mama kwa msaada wa Mungu, ni kukuza ndani ya nafsi ya mwanadamu Mfano wa Mungu. [MH 377.1; HU Aya ya 22]

Mama anayethamini jambo hili, ataziona fursa zake kuwa ni za thamani sana. Kwa bidii na dhati, atatafuta katika tabia yake mwenyewe, na kwa mbinu zake za kufundisha, kuwasilisha mbele ya watoto wake kile kilicho bora zaidi. Kwa bidii, subira, ujasiri, atajitahidi kuboresha uwezo wake binafsi, ili autumie ipasavyo, uwezo ulio wa juu zaidi wa akili katika kuwafundisha na kuwazoeza watoto wake. Atauliza kwa bidii katika kila hatua, “Je, Mungu amesema au anasemea nini katika jambo hili?” Kwa bidii atalisoma Neno Lake Mungu. Atakaza macho yake kumtazama Kristo vizuri, ili kwamba uzoefu wake mwenyewe wa kila siku, katika mzunguko wake duni wa masumbufu na wajibu, uweze kuwa kielelezo cha kweli cha maisha yale ya Kweli (na wala si maisha bandia au feki). [MH 378.1; HU Aya ya 23]

SURA YA 32

MTOTO

Sio tabia za mama tu, bali pia malezi ya mtoto yalijumuishwa katika maagizo ya malaika kwa wazazi wa Kiebrania. Haikutosha kwamba Samsoni, mtoto ambaye angewakomboa Israeli, awe na urithi mzuri wakati wa kuzaliwa

kwake. Haya yote yalipaswa kufuatiwa na mafunzo makini baada ya kuzaliwa. Tangu utotoni alipaswa kuzoezwa tabia za kuwa na kiasi kwa ukali kabisa. [MH 379.1; HU Aya ya 1]

Maagizo kama hayo yalitolewa kwa mama wa Yohana Mbatizaji. Kabla ya kuzaliwa kwa mtoto huyu, ujumbe uliotumwa kutoka mbinguni kwa baba ulikuwa: [MH 379.2; HU Aya ya 2]

“Nawe utakuwa na furaha na shangwe; na wengi watakufurahia kuzaliwa kwake. Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana, hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu tangu tumboni mwa mamaye.” Luka 1:14, 15, [MH 379.3; HU Aya ya 3]

Kwenye rekodi ya mbinguni ya watu wakuu, bora kabisa na waungwana, Mwokozi alitangaza kwamba hakuna aliyesimama kwa ukuu kuliko Yohana Mbatizaji. Kazi aliyokabidhiwa ilikuwa si ile iliyohitaji nguvu za kimwili na uvumilivu tu, bali pia sifa za juu zaidi kwenye umahiri wa akili, nia na nafsi. Mazoezi sahihi ya kimwili yalikuwa maandalizi muhimu sana kama maandalizi ya kazi hii hivi kwamba malaika mkuu zaidi mbinguni alitumwa na ujumbe wa maagizo kwa wazazi wa mtoto (Gabrieli). [MH 379.4; HU Aya ya 4]

Maelekezo yanayotolewa kuhusu watoto wa Kiebrania yanatufundisha kwamba hakuna chochote kinachoathiri ustawi wa kimwili wa mtoto kinachopaswa kupuuzwa au kufanyiwa uzembe. Hakuna lile lisilokuwa na muhimu. Kila kile ambacho kinathiri afya ya mwili huwa kinabeba matokeo yenye kugusa akili na tabia. [MH 380.1; HU Aya ya 5]

Umuhimu mkubwa unapaswa kuwekwa kwenye mafunzo ya awali ya watoto. Masomo wanayojifunza, na mazoea wanayojenga, wakati wa miaka ya utoto uchanga na utoto, yana sauti kubwa zaidi kwenye tabia ya mwanadamu katika kujenga maisha kuliko maagizo na mafunzo yote ya miaka ya baadaye ukubwani. [MH 380.2; HU Aya ya 6]

Wazazi zingatieni hili kwa umakini. Ninyi mnapaswa kuzielewa kanuni zinazosimamia malezi na mafunzo ya watoto. Mnapaswa kuwa na uwezo wa kuwalea katika afya ya kimwili, kiakili na kimaadili. Wazazi wanapaswa kujifunza sheria za asili. Wanapaswa kuufahamu mwili wa mwanadamu. Wanahitaji kuelewa kazi za viungo mbalimbali, na namna vinavyohusiana na kutegemeana. Wanapaswa kusoma uhusiano wa akili na nguvu za mwili, na hali zinazohitajika ili kuwe na utendaji mzuri wa kila kimoja. Kujipa majukumu ya uzazi bila maandalizi haya ni dhambi. [MH 380.3; HU Aya ya 7]

Watu hufikiria machache sana kuhusu chanzo kichosababisha vifo, ugonjwa na kuzorota kwa mwili, ambayo vipo leo hata katika nchi zilizostaarabika na

zinazopendwa na watu wengi kwasababu ya maendeleo ya kiafya. Jamii ya wanadamu inazidi kuzorota. Zaidi ya theluthi moja ya watoto hufa wakiwa wachanga; [Taarifa hii kuhusu vifo vya watoto wachanga Marekani, ilikuwa sahihi wakati kitabu hiki kilipoandikwa mwaka wa 1905. Hata hivyo, tiba za kisasa na matunzo ya afya yaliyo mazuri yamepunguza makali ya takwimu hizi kwenye viwango vya vifo vya watoto wachanga kabisa (kuzaliwa mpaka mwaka mmoja) na watoto wa umri inaofuata hawa wachanga.—Wachapishaji (mwaka mmoja mpaka miaka mitano)] Na kwa wale wanaofikia umri wa utu uzima, wake kwa waume, idadi kubwa zaidi huugua magonjwa kwa namna fulani, na ni wachache tu ambao wanaufikia umri ule aliopewa mwanadamu baada ya dhambi (Zaburi 90:10-12). [MH 380.4; HU Aya ya 8]

Mengi ya maovu ambayo yanaleta taabu na uharibifu kwenye jamii ya binadamu, yanaweza kuzuiwa, na uwezo wa kukabiliana nayo upo kwa kiwango kikubwa kwa wazazi. Sio “majaliwa ya Mungu ya ajabu" kama watu wasemavyo, ndiyo ambayo huwaondoa watoto wadogo duniani-(Watu husema ni mapenzi ya Mungu kwamba mtoto au mtu huyu amekufa na wakati si Mungu ila ni uzembe tu wa watu). Mungu hapendezwi na vifo vya watoto. Yeye anawapa watoto kwa wazazi ili wafundishwe ili wanufaishwe kwa mambo ya hapa duniani, na kwa ajili ya mbingu, baada ya maisha haya. Je, wakina baba na wakina mama walifanya kila wawezalo ili kuwapa watoto wao urithi mzuri kabisa, na kisha kwa usimamizi ufaao wakajitahidi kurekebisha hali zozote mbaya walizozaliwa nazo, Ikiwa watafanya haya, ni mabadiliko makubwa na bora kwa kiasi gani, ulimwengu huu utayaona! [MH 380.5; HU Aya ya 9]

Utunzaji wa Watoto wachanga (mwezi 0 hadi 12)

Kadri maisha ya mtoto yanavyokuwa ya utulivu na sahili, ndivyo yatakavyokuwa mazuri na kufaa zaidi kwa ukuaji wa mwili na kiakili. Wakati wote mama anapaswa kujitahidi kuwa mtulivu, asiye na kelele, na mwenye kujimiliki mwenyewe, yaani kuitawala nafsi yake kwa kujizuia kufanya vile ambavyo hapaswi kufanya. Watoto wengi wachanga huathirika sana na msisimko wa neva, na tabia ya mama nyororo, isiyo ya harara (haraka-haraka) itakuwa na ushawishi wa kupooza na kubembeleza, ambayo itakuwa manufaa makubwa, yasiyoweza kuneneka. [MH 381.1; HU Aya ya 10]

Watoto wanahitaji joto, lakini kosa kubwa mara nyingi hufanyika katika kuwaweka ndani ya vyumba vyenye joto la juu, nao hunyimwa hewa safi kiwango kikubwa. Mazoea ya kufunika uso wa mtoto mchanga wakati amelala ni hatari, kwani humzuia mtoto kupumua kwa uhuru. [MH 381.2; HU Aya ya 11]

Mtoto anapaswa kuwekwa huru kutokana na kila ushawishi ambao unaweza kudhoofisha au kudhuru mfumo. Matunzo makini yanapaswa kuchukuliwa ili kila kitu kuhusu mtoto kiwe ni kile ambacho kinapendeza na safi. Ingawa inaweza kuwa muhimu kumlinda mtoto kutokana na mabadiliko makubwa yajayo ghafla ya hali ya hewa au joto, uangalifu unapaswa kuchukuliwa, kwamba anapolala au kuamka, mchana au usiku, anapumua hewa safi, na yenye angahewa linalosaidia afya na nguvu za mtoto. [MH 381.3; HU Aya ya 12]

Katika maandalizi ya kabati la nguo za mtoto, yaani mavazi yake, usahili, faraja/comfort, na afya vinapaswa kushughulikiwa kwa kipaumbele kabla ya fasheni au matamanio ya mzazi kusisimua watu wampongeze au wamthamini zaidi kwaajili ya uvaaji wa mtoto wake. Mama hatakiwi kutumia muda katika kutarizi au kufuma urembo kwenye mavazi ya mtoto mdogo, ili yawe mazuri, na hivyo kujichosha kwa kazi isiyo ya lazima kwa gharama ya afya yake na afya ya mtoto wake. Mama hapaswi kuinamisha kichwa kwa muda mrefu akiwa anashona, jambo ambalo hutoza ushuru sana macho na mishipa, wakati ambapo anahitaji mapumziko na kujipatia mazoezi yenye kupendeza. Mama anapaswa kutambua wajibu wake wa kuthamini nguvu zake, ili aweze kukidhi mahitaji ambayo yatahitajika kutoka kwake. [MH 381.4; HU Aya ya 13]

Ikiwa mavazi ya mtoto yanaleta joto, ulinzi, na faraja, moja ya sababu kuu za kukerwa kwa mtoto na tashwishwi zitakuwa zimeondolewa. Mtoto huyu mdogo atakuwa na afya bora, na mama atagundua kwamba kazi ya kumhudumia mtoto haimtindikii nguvu na wakati wake. [MH 382.1; HU Aya ya 14]

Mikanda iliyofungwa kiunoni au kamba za aina yoyote huzuia utendaji wa moyo na mapafu, na inapaswa kuepukwa. Hakuna sehemu yoyote ya mwili inayopaswa kusumbuliwa na kukosa faraja wakati wowote kwa mavazi ambayo yanabana kiungo chochote au kuzuia uhuru wake wa kujongea au kusogea. Nguo za watoto wote zinapaswa kuwa na uhuru kutosha kukubali kupumua kwa uhuru kwa ukamilifu, na kupangwa vyema kiasi kwamba mabega yataweza kuhimili uzito wake (usimvalishe manguo mazito au hata kuweka kitu kizito kwenye nywele). [MH 382.2; HU Aya ya 15]

Katika baadhi ya nchi kuna desturi ya kuacha mabega wazi na viungo vya watoto wadogo vilivyo mbali na damu yaani mikono, miguu au kichwa. Desturi hii inapaswa kushutumiwa vikali sana. Viungo vikiwa mbali na kitovu cha mzunguko yaani moyo, vinahitaji ulinzi mkubwa kuliko sehemu zingine za mwili. Mishipa ambayo hupeleka damu safi toka kwenye moyo hadi mwisho wa mwili yaani miguu, mikono na kichwa, ikipeleka kiasi cha kutosha cha damu ili kuwezesha joto na lishe vifike kwenye sehemu hizo. Lakini wakati viungo vinapoachwa bila ulinzi wa nguo au vikiwa vimevalishwa kwa mavazi

yasiyotosha, mishipa ya kupelekea damu safi yaani oksijeni na mishipa ya kurudisha damu safi yaani kaboni-daoxide husinyaa, kisha sehemu nyeti za mwili huingia baridi, na hivyo mzunguko wa damu unazuiwa. [MH 382.3; HU Aya ya 16]

Kwa watoto ambao wanakua, nguvu zote za asili zinahitaji kunufaishwa ili ziwawezeshe kukamilisha umbo lenye afya la mwili. Ikiwa miguu, na mikono haijalindwa vya kutosha, watoto wasikae nje ya nyumba, na haswa wasichana, isipokuwa hali ya hewa ni ya joto la kawaida, yaani siyo baridi (angalau kipima joto kiwe 20 centigrade). Wakiwa ndani, kunakuwa hakuna hofu ya kupata magonjwa ya baridi kama vile kikohozi, mafua, pneuomia, mafundofundo nk. Ikiwa watoto wamevalishwa vizuri, watanufaika kufanya mazoezi kwa uhuru katika hewa iliyo wazi nje, katika majira ya joto au baridi (kutoka nje ni muhimu kila siku, ila watoto wavishwe vizuri). [MH 382.4; HU Aya ya 17]

Akina mama wanaotamani watoto wao wa kike na wa kiume wawe na nguvu za kiafya wanapaswa kuwavalisha ipasavyo na kuwatia moyo kuwa nje, katika hali zote za hewa. Huenda juhudi ikahitajika kuachana na minyororo ya desturi, au mapokeo katika kuwavisha watoto, ila mzazi elimisha watoto wako kuzingatia afya; na matokeo yatalipa juhudi zako za kufanya mambo kwa usahihi. [MH 382.5; HU Aya ya 18]

Mlo wa Mtoto

Chakula bora kwa mtoto mchanga ni chakula ambacho asili hutoa. Mtoto asinyimwe chakula hiki bila sababu. Ni jambo la ukatili kwa mama, kwa ajili ya kurahisisha maisha yake au kujipatia starehe ya kijamii, kutafuta kuepa jukumu la ofisi yake nyororo ya kumnyonyesha mtoto wake mdogo. [MH 383.1; HU Aya ya 19]

Mama anayemruhusu mtoto wake kulishwa chakula na mtu mwingine anapaswa kuzingatia vizuri matokeo yanayoweza kuja kutokana na mtindo wake huu wa maisha (mindset iliyopotoka). Kwa kiwango kikubwa au kidogo yule anayemnyonyesha mtoto humpa hulka, haiba na tabia yake mwenyewe mtoto anayenyonyesha. [MH 383.2; HU Aya ya 20]

Umuhimu wa kuwafundisha watoto tabia sahihi za lishe hauwezi kuvaliwa njuga kwa kiasi cha kutosha. Watoto wadogo wanahitaji kujifunza kwamba wanakula ili kuishi, na sio kuishi ili wale chakula. Mafunzo yanapaswa kuanza mwanadamu anapokuwa mtoto mchanga mikononi mwa mama yake anaponyonya. Mtoto anapaswa kupewa chakula kwa vipindi, na kwa kufuata muda, na siyo ale siku nzima, weka muda kati ya mlo na mlo (kama masaa matatu hivi akiwa mdogo sana), na kwa kadri anavyokua ongeza masaa kati ya

mlo (kwa watu wazima ni masaa matano mpaka sita, milo inapungua kadri wanavyokua wakubwa). Usimpe mtoto pipi, au chakula cha watu wazima, ambacho hakiwezi kumeng'enywa na mfumo wake. Matunzo na utaratibu katika kuwalisha watoto wachanga hautahamasisha afya yao tu, bali pia huwafanya kuwa watulivu, wenye subira na wenye hulka nzuri, pia itaweka msingi wa tabia ambazo zitakuwa baraka kwao katika miaka ya baadaye. [MH 383.3; HU Aya ya 21]

Watoto wanapoacha utoto uchanga, umakini mkubwa bado uwekwe katika kuelimisha ladha na hamu yao ya chakula. Mara nyingi wazazi ndiyo huruhusu watoto kula kile wanachochagua na wakati wanaochagua, bila hata ya kuzingatia afya. Maumivu na pesa wazazi wanazozitoa mara kwa mara kwenye tafrija zisizofaa huwaongoza vijana kufikiria kwamba hicho ndiyo kitu cha juu zaidi maishani, na kisha wanahitimisha kuwa kile ambacho huleta furaha kubwa zaidi maishani ni kufurahisha tamaa au uchu wa chakula. Matokeo ya mafunzo haya ni ulafi, na kisha magonjwa huja, ambayo kwa kawaida hufuatiliwa na dozi za dawa zenye sumu ili kuondoa matunda ya ulafi wa chakula. [MH 384.1; HU Aya ya 22]

Wazazi wanapaswa kuzoeza hamu chakula ya watoto wao kwa njia ambayo ni nzuri kwa afya ya kiroho, kimwili na kiakili na wasiruhusu matumizi ya vyakula visivyofaa. Lakini katika jitihada za kudhibiti mlo, tunapaswa kuwa waangalifu ili tusifanye makosa katika kuwalazimisha watoto wale chakula kisichopendeza, au kula chakula zaidi ya kile kinachohitajika. Watoto wana haki zao fulani kama wanadamu wote, wanakuwa na uchaguzi wa chakula, na wakati kile wanachopenda kula ni cha busara, basi, uchaguzi wao unapaswa uheshimiwe. [MH 384.2; HU Aya ya 23]

Muda maalumu wa chakula unapaswa kuzingatiwa kwa umakini. Hakuna kitu kinachopaswa kuliwa katikati ya milo, hakuna vitu vitamu kama keki, maandazi, bajia, vitumbua, peremende, pipimpira au jojo (confectioneries), karanga, matunda, au chakula cha aina yoyote kinapaswa kupita kooni. Ukiukwaji wa kula huharibu afya bora ya viungo vya tumbo vinavyomeng'enya chakula, na kudhuru afya na hata kuondoa uchangamfu. Na watoto wakija mezani kula baada ya kula vitafunwa siku nzima, huwa hawapendi chakula kizuri chenye afya ambacho hakijasindikwa wala kukobolewa; hamu yao ya chakula inawavuta kwa nguvu kwenye vile vitu vya vinavyowadhuru. [MH 384.3; HU Aya ya 24]

Akina mama wanaokidhi matamanio ya watoto wao ya chakula kwa gharama ya afya na hulka yenye furaha, wanapanda mbegu za uovu ambazo hakika zitachipuka na kuzaa matunda. Kujiendekeza na kujifurahisha kutakuwa kunaongezeka kwa kadri mtoto mdogo anavyokua, na nguvu zote za akili na

mwili hutolewa dhabihu. Hawa wakina mama wanaofanya kazi hii ya kuendekeza uchu wa chakula wa watoto, huvuna kwa uchungu mbegu waliyoipanda. Wanawaona watoto wao wakikua pasipo akili za kufaa na tabia ya utendaji bora kwenye nafasi yao katika jamii au nyumbani. Nguvu za kiroho, kiakili na kimwili zinapata mateso chini ya ushawishi wa chakula kisichofaa. Dhamiri inakuwa ngumu kuaminishwa dhambi, na uwezekano wa hisia na maoni mazuri huharibika kabisa. [MH 384.4; HU Aya ya 25]

Wakati watoto wanapaswa kufundishwa kutawala hamu ya kula na kula kwa kuzingatia afya; hebu ifahamike wazi kwa wazazi na watoto kwamba wanajikana nafsi zao tu, kwa yale yatakayowadhuru. Wanaacha mambo yanayowaumiza afya kwa kitu kilicho bora zaidi. Hebu meza ya chakula ifanywe kuwa ya kuvutia katika kumkaribisha mtu anayekaa mezani tayari kwa kula, kwa vile imejaa vitu vizuri ambavyo Mungu ametujalia kwa ukarimu. Hebu wakati wa chakula uwe wa furaha na uchangamfu. Tunapoendelea kufurahia zawadi za Mungu, hebu na tutoe mwitikio wa sifa na shukrani kwa kumtukuza Mpaji. [MH 385.1; HU Aya ya 26]

Utunzaji wa Watoto Wanapokuwa Wagonjwa

Mara nyingi mambo yanapofuatiliwa, itakutwa kuwa ugonjwa wa watoto umetokana na makosa katika usimamizi mbovu. Ukiukwaji wa masaa ya kula, yaana kula-kula ovyo hovyo, mavazi machache na yasiyoleta joto wakati wa jioni yenye baridi, kuukosesha mazoezi ya nguvu mwili ili kuweka damu katika mzunguko wa afya, au ukosefu wa hewa nyingi ya nje, inayozunguka vizuri na hivyo kuifanya iwe safi, inaweza kuwa sababu ya shida. Hebu wazazi wajifunze kuhusu shida mtoto aliyo nayo ili waweze kupata sababu au chanzo cha ugonjwa huo, na kisha kurekebisha hali mbaya kwa haraka iwezekanavyo. [MH 385.2; HU Aya ya 27]

Wazazi wote wana uwezo wa kujifunza mengi kuhusu matunzo, chanzo na uzuiaji wa ugonjwa, na hata tiba ya magonjwa. Mama ndiye haswa anayepaswa kujua nini cha kufanya katika kesi za kawaida za ugonjwa katika familia yake. Anapaswa kujua jinsi ya kumhudumia mtoto wake mgonjwa. Upendo, uelewa, na busara yake inapaswa kumpa stahiki ya kufanya huduma ambazo ingekuwa si vyema kumwamini mtu baki au mgeni amfanyie huduma hizi. [MH 385.3; HU Aya ya 28]

Fiziolojia

Wazazi wanapaswa kutafuta mapema namna ya kuwavutia watoto wao kwenye masomo ya fiziolojia na wanapaswa kuwafundisha kanuni zake rahisi.

Wafundishe namna bora ya kuhifadhi nguvu za kimwili, kiakili, na kiroho, na jinsi ya kutumia vipawa vyao ili maisha yao yaweze kuleta baraka kwa kila mmoja na heshima kwa Mungu. Ujuzi huu ni muhimu sana kwa vijana. Elimu ya mambo yanayohusu maisha, na afya ni muhimu zaidi kwao kuliko maarifa ya sayansi nyingi zinazofundishwa mashuleni. [MH 385.4; HU Aya ya 29]

Wazazi wanapaswa kuishi zaidi kwa ajili ya watoto wao, na kidogo kwa ajili ya jamii. Jifunze masomo ya afya, na utumie maarifa yako kwa vitendo. Wafundishe watoto wako sababu hadi athari. Wafundishe kwamba ikiwa wanataka afya na furaha, lazima watii sheria za asili. Ingawa unaweza usione ufanisi au maendeleo ya haraka kama unavyotamani, lakini usivunjike moyo, wewe endelea na kazi yako kwa subira na ustahimilivu. [MH 386.1; HU Aya ya 30]

Wafundishe watoto wako kutoka utotoni kujizoeza kujinyima, kujikana nafsi na kutawala nafsi. Wafundishe kufurahia uzuri wa asili na katika kazi muhimu zenye kumnufaisha mwanadamu na kufanya mazoezi kwa utaratibu kwa kuzishughulisha nguvu zote za mwili na akili. Walee ili wawe na katiba nzuri ya mwili nzuri na maadili mema, wawe na uchangamfu na hulka yenye kupendeza. Kazia katika akili zao nyororo ukweli wa kwamba Mungu hakupanga wanadamu waishi ili kujifurahisha au kujiridhisha wenyewe tu, bali kwaajili ya hatima nzuri ya mwisho. Wafundishe kwamba kujisalimisha kwenye majaribu ni udhaifu na uovu; waambie wayapinge majaribu, wawe waungwana, na watu bora, na kuwa watu wenye utu, ushujaa na tabia njema. Masomo haya yatakuwa kama mbegu iliyopandwa katika udongo mzuri, na yatazaa matunda ambayo yataifurahisha mioyo yenu. [MH 386.2; HU Aya ya 31]

Zaidi ya mambo mengine yote, hebu wazazi wawazunguke watoto wao kwa hali ya uchangamfu, adabu, uungwana, kujistahi na upendo. Nyumba ambayo upendo hukaa, na mahali ambapo hili huonyeshwa kwenye sura au mwonekano, maneno, na hata kwa vitendo, ni mahali ambapo malaika hufurahi kudhihirisha uwepo wao. [MH 386.3; HU Aya ya 32]

Wazazi, hebu mwanga wa jua wa upendo, uchangamfu, na kuridhika kwa furaha uingie mioyoni mwenu wenyewe, na acha ushawishi wake mtamu na wenye kupendeza, unaoshangilia kwa kuwatia watu wa nyumbani moyo, uenee kila mahali nyumbani kwenu. Onyesha roho ya upole, uvumilivu; na watie moyo watoto wako vivyo hivyo, wote mkiendelea kukuza neema zote zitakazofanya maisha ya nyumbani yang'ae. Angahewa itakayoundwa hivi, itakuwa kwa watoto jinsi hewa na mwanga wa jua ulivyo kwenye ulimwengu wa mimea, ikihamasisha afya na nguvu ya akili na mwili. [MH 387.1; HU Aya ya 33]

SURA YA 33

USHAWISHI WA NYUMBANI NA ATHARI ZAKE

Nyumba inapaswa kuwa mahali pa kuvutia zaidi kwa watoto ulimwenguni, na uwepo wa mama unapaswa kuwa ndivyo kivutio chake kikuu. Watoto wana asili nyeti, zenye kupenda watu. Wanafurahishwa kwa urahisi na kukasirishwa kwa urahisi. Kwa nidhamu nyororo, kwa maneno na matendo ya upendo, wakina mama wanaweza kuwafunga watoto wao kwenye mioyo yao. [MH 388.1; HU Aya ya 1]

Watoto wadogo wanapenda kuwa na watu wengine, na ni mara chache sana wanaweza kufurahi wakiwa peke yao. Wanatamani huruma, ulaini wa tabia na upendo. Kile wanachokifurahia huwa wanafikiri kuwa kitampendeza mama pia, na ni kawaida yao kumwendea mama katika furaha na huzuni zao ndogo-ndogo. Mama asijeruhi mioyo yao nyeti kwa kuonyesha kutojali katika yale mambo wanayomweleza au kuleta kwake, ambayo, ingawa ni madogo kwake, kwao ni muhimu sana. Huruma ya mama, pamoja na kuonyesha ukubali wake wa kuchukuliana na mambo yao ni vitu vya thamani sana. Mtupo wa jicho wa kuonyesha unafurahishwa nao, na moyo wako unakithamini kile wanachokuelezea, neno la kutia-moyo au pongezi, vitakuwa kama mwanga wa jua ndani ya mioyo yao, na mara nyingi kutaifanya siku nzima kuwa yenye furaha. [MH 388.2; HU Aya ya 2]

Badala ya kuwaambia watoto wake wawe mbali naye ili asikasirishwe au kusumbuliwa na kelele zao au matakwa yao madogo-madogo, hebu mama apange burudani au kazi nyepesi ili kuishughulisha mikono na akili ambazo zina utendaji wenye shughuli nyingi. [MH 388.3; HU Aya ya 3]

Kwa kuingia katika hisia zao na kufanya usimamizi katika burudani zao na kazi wanazozifanya, mama atapata ujasiri/imani ya watoto wake, na hivyo anaweza kurekebisha kwa ufanisi pale tabia mbaya inapojitokeza kirahisi, au kuangalia maonyesho ya ubinafsi, uchoyo au tamaa mbaya. Neno la tahadhari au karipio linalosemwa kwa wakati ufaao litakuwa na thamani kubwa. Kwa umakini na upendo wenye subira, anaweza kugeuza akili za watoto kwenye mwelekeo ufaao, na kupalilia ndani yao sifa nzuri na zenye kuvutia kitabia. [MH 389.1; HU Aya ya 4]

Akina mama wanapaswa kujilinda dhidi ya kuwafundisha watoto wao kuwa tegemezi na kujifikiria wenyewe. Kamwe usiwaongoze watoto wako kufikiria

kuwa wao ndio kitovu cha kila kitu, kwamba kila kitu lazima kizunguke karibu nao, (kwamba wao ndiyo wafalme na watumikiwe, na kila mtu awe anaangalia maslahi yao). Kuna wazazi ambao hutumia muda mwingi na umakini katika kuwatumbuiza au kuwafurahisha watoto wao, lakini watoto wanapaswa kuzoezwa kujifurahisha wenyewe, na kutumia akili yao kwa ubunifu na ustadi wao wenyewe (watengeneze toys zao!). Ndivyo watakavyojifunza kuridhika na starehe sahili sana. Wanapaswa kufundishwa kuvumilia kwa ujasiri masikitiko na kukatishwa tamaa kwao katika majaribu yao madogo. Badala ya kuelekeza umakini wao kwenye kila umivu dogo-dogo au maudhi, geuza akili zao, na wafundishe kuvumilia kero hizi ndogo-ndogo au usumbufu mdogo kwa kupuuzia. Jifunze jinsi ya kuwapendekezea njia ambazo watoto hawa wanaweza kujifunza kuwafikiria watu wengine. [MH 389.2; HU Aya ya 5]

Lakini watoto wasipuuzwe. Wakina mama wakiwa wametindikiwa na masumbufu mengi ya maisha haya, nyakati fulani, wanahisi kwamba hawawezi kuchukua muda, na kwa subira wawafundishe watoto wao wadogo na kuwaonyesha au kuwapa upendo na huruma. Lakini wazazi hawa wanapaswa kukumbuka kwamba, ikiwa watoto hawatapata umakini kutoka wazazi wao na nyumbani mwao kile ambacho kitatosheleza matamanio yao ya kupata huruma na urafiki, wataviangalia vyanzo vingine kwingine, mahali ambapo akili na tabia vinaweza kuwa hatarini. [MH 389.3; HU Aya ya 6]

Kwa kukosa wakati na mawazo, wakina mama wengi huwanyima watoto wao furaha isiyoambatana na uovu wowote au dhamira yenye hatia, alimradi vidole vya huyu mama vinaendelea na shughuli nyingi za kudarizi au kushona urembo, na kuchosha macho katika kujishughulisha kwa bidii na kazi ya kuwa disaina wa mapambo tu, jambo ambalo, kuwa ubora zaidi, litaelekea tu, kutumika katika kuhimiza ubatili na ubaradhifu kwenye mioyo ya watoto. Watoto wanapoukaribia utu uzima, masomo haya ya ubatili na ubaradhifu toka kwa wazazi wanaokazania urembo na mambo ya kuridhisha tamaa za mwili, yatazaa matunda ya kiburi na ukosefu wa maadili. Mama ataanza kuhuzunika kwaajili ya makosa ya watoto wake, lakini anakuwa hatambui kwamba mavuno anayovuna sasa yametokana na mbegu aliyoipanda mwenyewe. [MH 389.4; HU Aya ya 7]

Baadhi ya akina mama hawana msawaziko/balansi katika kushughulika na watoto wao. Nyakati fulani wanaendekeza mambo yanayoleta majeraha kwa watoto wao, na huku wakati mwingine wanakataa kabisa kuwaridhisha na kitu ambacho hakika hakina hatia kabisa, kile ambacho kingeufanya moyo wao wa kitoto uwe na furaha sana. Katika jambo hili hawamwigi Kristo; Yeye Aliwapenda watoto; Alizielewa hisia zao na akawahurumia katika raha zao, majaribu yao, na mitihani yao. [MH 390.1; HU Aya ya 8]

Wajibu wa Baba

Mume na baba ndiye kichwa cha familia. Mke humtazama yeye ili kupata upendo na huruma, na kwa msaada katika mafunzo ya watoto; na jambo hili ni sahihi kabisa. Watoto ni wake baba, na mama vilevile , baba anapendezwa na ustawi watoto kama vile mama. Watoto wanamtegemea baba yao kwa msaada na mwongozo; anahitaji kuwa na dhana sahihi ya maisha, mivuto na mahusiano ambayo inavyopaswa kuizunguka familia yake; zaidi ya yote, anapaswa kutawaliwa na upendo na hofu ya Mungu na mafundisho ya Neno Lake, ili aweze kuiongoza miguu ya watoto wake katika njia iliyo sahihi. [MH 390.2; HU Aya ya 9]

Baba ndiye mtunzi wa sheria za nyumbani; na, kama Ibrahimu, anapaswa kuifanya sheria ya Mungu itawale nyumba yake. Mungu alisema hivi juu ya Ibrahimu, "Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana…." Mwanzo 18:19. Hakutakuwa na dhambi ya kutozuia maovu ya watoto, wala udhaifu, na ubaguzi usio na busara; au kusalimisha wajibu wake kwa madai ya mapenzi potofu. Abrahamu hangetoa tu mafundisho sahihi, bali angedumisha mamlaka ya sheria za haki na uadilifu. Mungu ametoa sheria ili ziwe mwongozo wetu. Watoto wasiachwe tu kumangamanga mbali na njia salama iliyoainishwa katika Neno la Mungu, na kuingia katika njia za hatari, ambazo ziko wazi kila upande. Kwa fadhili, lakini kwa uthabiti, pamoja na bidii isiyochoka katika sala, shauku zao mbaya zapaswa kuzuiwa, mielekeo yao mibaya inapaswa kukataliwa au kupingwa. [MH 390.3; HU Aya ya 10]

Baba anapaswa kukazia katika familia yake sifa bora na zenye uwezo wa kushinda taabu na changamoto—nguvu, uadilifu, uaminifu, subira, ujasiri, bidii, na manufaa ya kivitendo. Na yale anayohitaji kutoka kwa watoto wake yeye mwenyewe anapaswa kuyaishi, akionyesha sifa hizi katika kuzibeba kwake mwenyewe kiume-kwa ushujaa. [MH 391.1; HU Aya ya 11]

Lakini, wakina baba, wasiwakatishe tamaa watoto wao. Changanya mapenzi na mamlaka, fadhili na huruma pamoja na kujizuia kwa uthabiti. Wape watoto wako baadhi ya masaa yako ya burudani; wafahamu watoto wako; na shirikiana nao katika kazi zao na katika michezo yao, na upate imani/ujasiri wao. Sitawisha urafiki pamoja nao, hasa na watoto wako wa kiume. Kwa njia hii utakuwa na ushawishi mkubwa kwa wema. [MH 391.2; HU Aya ya 12]

Baba anapaswa kufanya sehemu yake katika safari ya kufanya nyumba iwe mahali pa furaha. Haijalishi ana mashaka au masumbufu na matatizo katika shughuli, taaluma au biashara yake, haya hayapaswi kuruhusiwa kuifunika

familia yake kwa kivuli cha huzuni; baba anapaswa aingie nyumbani mwake akiwa na tabasamu na maneno ya kupendeza. [MH 392.1; HU Aya ya 13]

Baba ndiye kuhani wa nyumba yake, yeye ndiye anayeiweka familia yake juu ya madhabahu asubuhi na jioni (ibada). Lakini mke na watoto wanapaswa kuungana katika sala na kujiunga katika wimbo wa sifa. Asubuhi kabla ya kuondoka nyumbani kwa ajili ya kazi yake ya kila siku, hebu baba awakusanye watoto wake karibu naye, kisha kwa kuinama mbele za Mungu, awaweke chini ya uangalizi wa Baba aliye mbinguni. Masumbuko ya siku yanapopita, hebu familia iungane katika kutoa sala ya shukrani na kuinua wimbo wa sifa, kwa kutambua utunzaji wa Bwana wakati wa mchana. [MH 392.2; HU Aya ya 14]

Akina baba na akina mama, hata kama umesongwa na shughuli au pilikapilika za biashara zingine, usikose kuikusanya familia yako karibu na madhabahu ya Mungu. Omba ulinzi wa Malaika watakatifu nyumbani mwako. Kumbuka kwamba wapendwa wako wanaanikwa kwenye majaribu kila kukicha. Kero na masumbufu kila siku huzingira njia ya vijana na wazee. Wale ambao wangeishi maisha ya subira, upendo na uchangamfu, ni lazima wasali. Ni kwa kupokea tu msaada endelevu kutoka kwa Mungu ndiyo tunaweza kupata ushindi dhidi ya nafsi zetu wenyewe, yaani ushindi dhidi ya ubinafsi. [MH 393.1; HU Aya ya 15]

Nyumbani panapaswa kuwa mahali ambapo uchangamfu, adabu, nidhamu, kujistahi na upendo hukaa; na pale neema hizi zinapotamalaki, patakuwa na furaha na amani. Shida zinaweza kutuvamia, lakini hili ni fungu la ubinadamu baada ya maanguko yetu dhambini. Hebu subira, shukrani, na upendo viweke jua moyoni mwetu, na ingawa siku inaweza kuwa na mawingu sana (huzuni na mengineyo). Bado katika nyumba kama hizo malaika wa Mungu hukaa. [MH 393.2; HU Aya ya 16]

Hebu mume na mke wajifunze furaha ya kila mmoja wao, bila kushindwa katika kuonyesha adabu, uungwana na ukarimu mdogo-mdogo na vitendo vidogo vya fadhili ambavyo huchangamsha na kufanya maisha yang'ae. Ujasiri kamili unapaswa kuwepo kati ya mume na mke (kuaminiana, kuaminiwa na kuamini nk). Kwa pamoja hawa wanapaswa kuzingatia wajibu wao. Kwa pamoja wanapaswa kufanya kazi kwa manufaa ya juu zaidi ya watoto wao. Kamwe hawapaswi kukosoana mbele ya watoto, kuhusiana mipango ya kila mmoja wao au kuhoji maamuzi ya kila mmoja. Hebu mke awe mwangalifu kwa kutofanya kazi ya mume kwa watoto kuwa ngumu zaidi. Hebu mume aitegemeze mikono ya mke wake na kuiinua, akimpa ushauri wa hekima na kumtia moyo kwa upendo. [MH 393.3; HU Aya ya 17]

Hakuna kizuizi cha ubaridi na kujihifadhi kinachonapaswa kuruhusiwa kutokea na kuonyeshwa kati ya wazazi na watoto (mioyo ikunjuke kwa kila mmoja, kusiwe na ukavu-kavu). Hebu wazazi wachukue muda kuwafahamu watoto wao, wakitafuta kuelewa ladha zao, kile wanachopendelea na mielekeo yao, kwa kuingia katika hisia zao, na kutoa nje kile kilicho mioyoni mwao. [MH 394.1; HU Aya ya 18]

Wazazi, acheni watoto wenu waone kwamba mnawapenda na kwamba ninyi mtafanya yote mnayoweza ili kuwafanya wawe na furaha. Ukifanya hivyo, makatazo yanayohitajika, ambayo ni muhimu yatakuwa na uzito mkubwa zaidi katika akili zao changa. Uwatawale watoto wako kwa upole, ulaini na huruma, ukikumbuka kwamba “malaika wao sikuzote huutazama uso wa Baba Yangu/yao aliye mbinguni.” Mathayo 18:10. Ikiwa unatamani malaika wawafanyie watoto wako kazi waliyopewa na Mungu, shirikiana nao kwa kufanya sehemu yako. [MH 394.2; HU Aya ya 19]

Watoto wakilelewa chini ya mwongozo wenye hekima na upendo wa nyumba ya Kweli, watoto hawatakuwa na tamaa ya kutanga-tanga ili kutafuta raha/starehe na marafiki au wenzi wengine. Uovu hautawavutia. Roho inayotawala nyumbani itafinyanga tabia zao; watajenga tabia na kanuni ambazo zitakuwa ulinzi mkali dhidi ya majaribu wakati watakapoondoka kwenye makazi ya nyumbani na kuchukua nafasi yao katika ulimwengu. [MH 394.3; HU Aya ya 20]

Watoto na wazazi wana majukumu muhimu nyumbani. Wanapaswa kufundishwa kuwa wao ni sehemu ya taasisi ya nyumbani. Wanalishwa na kuvikwa na kupendwa na kutunzwa, na wanapaswa kutoa mwitikio kwa rehema hizi nyingi kwa kubeba sehemu yao ya mizigo ya nyumbani na kuleta furaha yote inayowezekana kupataikana katika familia ambayo wao ni washiriki. [MH 394.4; HU Aya ya 21]

Wakati fulani watoto wanashawishika kukasirika wanapokuwa chini ya makatazo au zuio fulani; lakini katika maisha ya baadaye watawabariki wazazi wao kwa ajili ya matunzo yenye uaminifu na uangalizi mkali ambao uliwalinda na kuwaongoza katika miaka yao ya kutokuwa na uzoefu. [MH 394.5; HU Aya ya 22]

SURA YA 34

ELIMU YA KWELI, MAFUNZO YA UMISHONARI

Elimu ya kweli ni mafunzo ya umishenari. Kila mwana na binti wa Mungu ameitwa kuwa mmishenari; tumeitwa kumtumikia Mungu na wanadamu wenzetu; na lengo kuu la elimu ni kutufanya tufae (stahiki) kwa ajili ya huduma hii. [MH 395.1; HU Aya ya 1]

Mafunzo kwa ajili ya Kutumika

Kusudi hili daima linapaswa kuzingatiwa na wazazi na walimu Wakristo. Hatujui watoto wetu watatumika katika nyanja au taaluma ipi. Wanaweza kutumia maisha yao katika mazingira ya nyumbani; wanaweza kushiriki katika miito ya kawaida ya maisha kupitia tasnia mbalimbali, au kwenda kama waalimu wa injili katika nchi za kipagani; lakini wote wameitwa kwa namna ile ile kuwa wamishenari kwa ajili ya Mungu, wakiwa wabeba rehema kwa ulimwengu. [MH 395.2; HU Aya ya 2]

Watoto na vijana, wakiwa na talanta zao halisi, nguvu, na ujasiri, utambuzi wao kwa vyepesi, ni wapendwa wa Mungu, na Yeye atamani kuwaleta katika kupatana na mawakala wa Kiungu. Hawana budi kupata elimu ambayo itawasaidia kusimama upande wa Kristo katika utumishi usio na ubinafsi. [MH 395.3; HU Aya ya 3]

Kwa watoto Wake wote hadi mwisho wa wakati, Bwana anasema nao kwa uzito ule ule alioutoa kwa wanafunzi wa kwanza, Kristo alisema, “Kama vile ulivyonituma Mimi ulimwenguni, vivyo hivyo na Mimi niliwatuma wao ulimwenguni” (Yohana 17:18) kuwa wawakilishi wa Mungu, kumfunua Roho Wake, kudhihirisha tabia Yake, na kufanya kazi Yake. [MH 395.4; HU Aya ya 4]

Watoto wetu wanasimama, kana kwamba, wapo kwenye njia panda. Katika kila upande, vishawishi vya ulimwengu katika kujitafutia maslahi yao

wenyewe na kujipendeza wenyewe tu vinawatoa katika njia iliyowekwa kwa ajili ya waliokombolewa na Bwana. Kwamba maisha yao yatakuwa baraka au laana, hutegemea uchaguzi waufanyao. Wakiwa wamejawa nguvu, wenye shauku ya kuupima uwezo wao ambao haujajaribiwa, lazima wagundue fursa kwa ajili ya maisha yao yaliyojawa tele. Watakuwa imara ama kwa wema au kwa ubaya. [MH 396.1; HU Aya ya 5]

Neno la Mungu halizuii utendaji wa kujishughulisha, bali huongoza huo utendaji kwa kutoa maelekezo kwa jinsi ipasavyo. Mungu hawaagizi vijana kuwa na matamanio madogo. Vipengele vya tabia ambavyo humfanya mwanadamu kufanikiwa na kuheshimiwa kikweli miongoni mwa wanadamu—shauku isiyozuilika kwa ajili ya jambo fulani kuu, nia isiyoshindika, matumizi ya uwezo huu kwa bidii, uvumilivu usiochoshwa—hivi vipengele havipaswi kuwekewa vikwazo. Kwa neema ya Mungu vijana waelekezwe kupata vitu vilivyo juu zaidi kuliko ubinafsi na maslahi ya kidunia kama vile mbingu zilivyo juu kuliko dunia. [MH 396.2; HU Aya ya 6]

Kwa sisi kama wazazi na kama Wakristo zoezi linalobakia kwetu ni kuwapa watoto wetu maongozi sahihi. Watoto wanapaswa kuongozwa kwa uangalifu, kwa hekima, kwa upole katika njia za huduma kama ya Kristo. Tu chini ya agano takatifu na Mungu kuwalea watoto wetu kwa ajili ya utumishi Wake. Kuwazunguka kwa mivuto ambayo itawaongoza kuchagua maisha ya utumishi, na kuwapa mafunzo yanayohitajika, huu ndio wajibu wetu wa kwanza. [MH 396.3; HU Aya ya 7]

“Mungu alipenda sana, ... hata akatoa,” “akamtoa Mwanawe pekee,” ili tusiangamie, bali tuwe na uzima wa milele. "Kristo ... alitupenda, akajitoa kwa ajili yetu.” Na sisi tukipenda tutatoa. “Sio kuhudumiwa, bali kuhudumu” ndilo somo kuu ambalo tunapaswa kujifunza na kulifundisha. Yohana 3:16; Waefeso 5:2; Mathayo 20:28. [MH 396.4; HU Aya ya 8]

Hebu vijana wavutiwe na wazo kwamba wao hawajimiliki wenyewe. Wao ni mali ya Kristo. Wamenunuliwa kwa damu Yake Mwenyewe, dai la upendo Wake. Wanaishi kwa sababu Yeye huwahifadhi kwa uwezo Wake. Muda wao, nguvu zao, uwezo wao ni Wake Yeye, kwa kukuzwa, kufunzwa, na kutumika kwa ajili Yake. [MH 396.5; HU Aya ya 9]

Baada ya malaika, familia ya wanadamu, iliyoumbwa kwa mfano wa Mungu, tu kazi bora zaidi ya uumbaji Wake. Mungu atamani wanadamu wawe kila kitu ambacho Yeye amewawezesha kuwa, na kufanya vyema kwa kadiri wawezavyo kwa uwezo ambao Yeye amewapa. [MH 397.1; HU Aya ya 10]

Maisha ni fumbo na ni matakatifu. Ni udhihirisho wa Mungu Mwenyewe, Chanzo cha uhai wote. Fursa zake zina thamani, na zinapaswa kuboreshwa kwa dhati. Pale fursa zinapopotea, hukoma milele. [MH 397.2; HU Aya ya 11]

Mbele yetu Mungu ameweka umilele, pamoja na uhalisia wake mkuu, na huu hutupatia sisi ufahamu juu ya mada zisizoweza kufa, zisizoweza kuharibika. Yeye huwasilisha ukweli wa thamani, unaoboresha, ili tuweze kusonga mbele katika njia salama na ya hakika, katika kujishughulisha na kusudi linalostahili uhusika wetu kwa dhati wa uwezo wetu wote. [MH 397.3; HU Aya ya 12]

Mungu hutazama ndani ya mbegu ndogo ambayo Yeye Mwenyewe ameiumba, na anaona ndani yake kukiwa na ua zuri, kichaka, au mti mrefu unaotapakaa kwenye eneo kubwa. Vivyo hivyo Anaona mambo yanayowezekana katika kila mwanadamu. Tu hapa duniani kwa kusudi fulani. Mungu ametupa mpango Wake kwa ajili ya maisha yetu, Naye atamani tufikie kiwango cha juu zaidi cha maendeleo. [MH 397.4; HU Aya ya 13]

Atamani kwamba tuzidi kukua katika utakatifu, katika furaha, katika kuwa na manufaa. Wote wana uwezo, naam, vipaji ambavyo ni lazima wafundishwe kuvichukulia kama karama takatifu, kuvithamini kama zawadi za Bwana, na kuvitumia ifaaavyo. Atamani vijana kusitawisha kila nguvu ya nafsi zao, na kuleta kila uwezo katika mazoezi ya vitendo. Atamani wafurahie yote yenye manufaa na ya thamani katika maisha haya, wawe wema na watende mema, wakijiwekea hazina yao mbinguni kwa ajili ya maisha yajayo. [MH 398.1; HU Aya ya 14]

Inapaswa iwe malengo yao kufaulu katika mambo yote yasiyo na ubinafsi, ya juu, na adhimu. Na wamtazame Kristo kama kielelezo ambacho kwa hicho wanapaswa kutengenezwa vyema. Matamanio matakatifu ambayo aliyafunua katika maisha Yake, wanadamu wanapaswa kuyathamini—yaani nia ya kufanya ulimwengu kuwa mahali bora pa kuishi ndani yake. Hii ndiyo kazi wanayoitiwa. [MH 398.2; HU Aya ya 15]

Msingi Wenye Kina

Sayansi kuu kupita sayansi zote, ni sayansi ya kuokoa roho. Kazi kubwa zaidi ambayo wanadamu wanaweza kuweka matamanio yao, ni kazi ya kuwaleta wanadamu kutoka dhambini hadi kwenye utakatifu. Ili kutimiza kazi hii, msingi mpana lazima uwekwe. Elimu ya kina inahitajika—elimu ambayo itadai kutoka kwa wazazi na walimu mawazo na jitihada za juu na kubwa, hii ni zaidi ya mafundisho tu yanayotolewa katika sayansi ambayo wanadamu hufundisha na kusoma leo mashuleni. Kuna kitu kingine kinachohitajika zaidi ya utamaduni wa akili tu. Elimu haikamiliki isipokuwa mwili, akili, na moyo vimeelimishwa kwa usawa. Tabia lazima ipokee nidhamu ifaayo kwa

maendeleo yake kamili na ya juu zaidi. Uwezo wote wa akili na mwili vinapaswa kukuzwa na kufunzwa ifaavyo. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kusitawisha, kupalilia na kutumia kila uwezo ambao utatufanya kuwa watendakazi wenye ufanisi zaidi kwa ajili ya Mungu. [MH 398.3; HU Aya ya 16]

Elimu ya kweli inajumuisha kila kitu kihusucho mwanadamu. Inafundisha matumizi sahihi binafsi. Inatuwezesha kutumia vyema ubongo, mifupa, na misuli, mwili, akili, na moyo. Uwezo wa akili, ambao ndio nguvu ya juu kwenye mwili wa mwanadamu, hauna budi kutawala ufalme wote wa mwili. Hamu na matamanio asili ya mwilini sharti yawe chini ya udhibiti wa dhamiri na mapenzi ya kiroho. Kristo asimama kama kichwa cha ubinadamu, na ni kusudi Lake kutuongoza, katika huduma Yake, katika njia kuu na takatifu. Kwa utendaji ajabu wa neema Yake, hatuna budi kukamilishwa katika Yeye. [MH 398.4; HU Aya ya 17]

Yesu alijipatia elimu Yake akiwa nyumbani. Mama yake alikuwa mwalimu Wake wa kwanza wa kibinadamu. Kutoka kwa midomo yake, na kutoka katika magombo ya manabii, alijifunza mambo ya mbinguni. Aliishi katika nyumba ya wakulima maskini na kwa uaminifu na furaha alitenda sehemu Yake katika kubeba mizigo ya nyumbani. Yeye aliyekuwa Amiri wa jeshi la mbinguni, alikuwa mtumishi aliyekuwa tayari kutii, Mwana Mtiifu na Mwenye upendo. Alijifunza tasnia ya ufundi na kwa mikono Yake Mwenyewe alifanya kazi katika karakana ya seremala pamoja na Yusufu. Akiwa amevalia mavazi ya mfanyakazi wa kawaida alitembea barabara za mji mdogo, akienda na kurudi kutoka kwenye kazi Yake isiyotaka makuu. [MH 399.1; HU Aya ya 18]

Kwa watu wa zama hizo, thamani ya vitu ilikadiriwa kwa mwonekano wa nje. Kwa kuwa moto au nguvu ya dini ilikuwa imeshuka, ufahari ulikuwa umeongezeka (kujigamba). Waelimishaji wa wakati huo walitafuta kulazimisha heshima kwa maonyesho na majivuno. Kwa haya yote watu hawa waliyoyafanya, maisha ya Yesu yalionyesha kuwa na tofauti kubwa. Maisha Yake yalionyesha mambo yao wanadamu kutokuwa na thamani, mambo waliyoyaona kuwa ni ya muhimu sana maishani mwao. Shule za wakati Wake, zilizokuwa zinakuza vitu vidogo visivyo na maana na kuvidharau vitu vikubwa na vya maana, Yeye hakujishughulisha nazo wakati wa kutafuta elimu yake humu duniani. Elimu yake ilipatikana kutoka kwa vyanzo vilivyowekwa na Mbingu, kutoka kwenye kazi inayonufaisha *(Msisitizo: kujionyesha kwa watu hakunufaishi)*, kutokana na kujifunza Maandiko, kutoka kwenye asili au uumbaji, na uzoefu wa maisha— ambapo hivi vyote ndivyo vitabu vya kiada vya Mungu, vilivyosheheni mafundisho kwa wale wote wanaoletea mikono yenye utayari, jicho lenye kuona, na moyo wenye ufahamu. [MH 400.1; HU Aya ya 19]

“Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake” Luka 2:40. [MH 400.2; HU Aya ya 20]

Akiwa amejitayarisha hivyo, alitoka na kwenda kwenye utume Wake, katika kila wasaa wa kukutana na wanadamu, akitafuta kuwabariki, kuwabadilisha, kwa jinsi ambayo ulimwengu huu haujawahi kushuhudia kamwe. [MH 400.3; HU Aya ya 21]

Shule ya kwanza ya mtoto ni nyumbani, na ni hapa ndipo msingi unapaswa kuwekwa kwa maisha ya huduma. Kanuni zake zinapaswa kufundishwa si kwa nadharia tu. Bali zinapaswa kuumba mafunzo ya maisha yote. [MH 400.4; HU Aya ya 22]

Mapema sana somo la kuwa msaada kwa wengine linapaswa kufundishwa kwa mtoto (kusaidia wenye mahitaji). Mara tu nguvu na uwezo wa kufikiri vinapokuzwa vya kutosha, mtoto anapaswa kupewa majukumu ya kufanya nyumbani. Anapaswa kuhimizwa katika kumsaidia baba na mama, akihimizwa kujikana nafsi yake na kujinyima, kutanguliza furaha na urahisi wa maisha kwa wengine kabla ya yeye, kutafuta fursa za kuwaburudisha na kuwasaidia kaka na dada na wenzake anaocheza nao, na kuonyesha wema kwa wazee, wagonjwa, na watu waliopatwa na maafa. Kadiri roho halisi ya utumishi inavyoenea nyumbani, ndivyo itakavyokuzwa katika maisha ya mtoto kikamilifu. Watoto watajifunza kupata furaha katika utumishi na kujitoa kwa ajili ya manufaa ya wengine. [MH 401.1; HU Aya ya 23]

Kazi ya Shule

Mafunzo ya nyumbani yanapaswa kujalizwa na mafunzo ya shule. Ukuaji wa mwanadamu katika mambo yote, kimwili, kiakili, na kiroho, na mafundisho ya utumishi na kujitoa, yapaswa kuzingatiwa daima. [MH 401.2; HU Aya ya 24]

Zaidi ya njia nyingine yo yote, utumishi kwa ajili ya Kristo katika mambo madogo ya maisha ya kila siku ina uwezo wa kufinyanga tabia na kuyaelekeza maisha katika njia za utumishi usio na ubinafsi. Kuamsha roho hii, kuihamasisha na kuielekeza ipasavyo, ni kazi ya wazazi na ya mwalimu. Hakuna kazi muhimu zaidi ambayo hawa watu wazima wanaweza kupewa ulimwenguni kuliko hiyo. Roho ya kutumika ni roho ya mbinguni, na kwa kila juhudi mwanadamu anayofanya ili kuikuza na kuihimiza roho hii, malaika watashirikiana na mtu huyo. [MH 401.3; HU Aya ya 25]

Elimu kama hiyo lazima ijengwe katika Neno la Mungu. Ni humu tu ambamo kanuni zake zimetolewa kwa ukamilifu wake. Biblia inapaswa kufanywa kuwa msingi wa mafunzo yote na msingi wa kufundishia. Ujuzi muhimu ni ujuzi wa Mungu na wa Yeye ambaye amemtuma. [MH 401.4; HU Aya ya 26]

Kila mtoto na kila kijana apaswa kuwa na ujuzi unaomhusu yeye mwenyewe. Apaswa kuelewa mwili wake ambao Mungu amempa, na sheria ambazo kwa hizo, mwili huu unaweza kutunzwa katika afya. Wote wanapaswa kujengwa imara katika matawi ya kawaida ya elimu (Lugha, Hisabati, Sayansi, Historia n.k). Na wanapaswa wawe na mafunzo ya tasnia, stadi, ufundi, na taaluma ambayo yatawafanya kuwa wanaume na wanawake wenye uwezo kiutendaji, watu wanaofaa kwa ajili ya majukumu ya maisha ya kila siku. Kwa haya yote kunapaswa kuongezwa mafunzo na uzoefu wa vitendo katika nyanja mbalimbali za jitihada za kimishenari. [MH 402.1; HU Aya ya 27]

Kujifunza Huku Ukielimisha

Vijana na wasonge mbele kwa haraka na kadiri wawezavyo katika kupata maarifa. Uwanja wao wa masomo na uwe mpana kadiri uwezo wao unavyoweza kuhifadhi. Na, wanapojifunza, wapate nafasi ya kutoa huu ujuzi kwa wengine. Ni kwa namna hiyo ndiyo kwamba akili zao zitapata nidhamu na nguvu. Ni yale matumizi wanayofanya ya maarifa waliyopokea, ndiyo ambayo huamua thamani ya elimu yao. Kutumia muda mrefu katika kujifunza, bila jitihada yoyote ya kutoa kile kilichopatikana akilini kwa vitendo, mara nyingi huthibitisha kuwa kikwazo badala ya msaada katika maendeleo halisi. Nyumbani na shuleni yapasa kuwa jitihada ya mwanafunzi kujifunza jinsi ya kusoma na jinsi ya kutoa ujuzi huo. Kwa vyo vyote mwito wake unavyoweza kuwa, apaswa kuwa mwanafunzi na mwalimu maadamu maisha haya yanadumu *(Msisitizo: kila mtu anapaswa kuwa mwalimu kwa namna moja au nyingine)*. Kwa hivyo aweza kusonga mbele daima, akimfanya Mungu kuwa tumaini lake, akishikamana na Yeye aliye na hekima isiyo na kikomo, awezaye kufichua siri zilizofichwa kwa zama nyingi, Yeye awezaye kutatua matatizo magumu zaidi kwa ajili yawote wanaomwamini. [MH 402.2; HU Aya ya 28]

Neno la Mungu hukazia sana ushawishi wa uhusiano katika jamii, si kwa watoto tu bali hata juu ya wanaume na wanawake. Ni kwa ukubwa kiasi gani Neno la Mungu lilivyo na nguvu katika akili na tabia zinazokua za vijana na watoto. Marafiki wanaokaa nao, kanuni wanazoziiga, mazoea wanayojenga, vitaamua suala la manufaa yao hapa duniani na mapenzi yao ya baadaye, ya milele. [MH 402.3; HU Aya ya 29]

Ni ukweli wa kutisha, na ambao unapaswa kufanya mioyo ya wazazi kutetemeka, kwamba katika shule na vyuo vingi ambavyo vijana hupelekwa ili kupata maarifa na nidhamu, kuna mvuto ambao huharibu tabia, na hugeuza akili kutoka kwenye malengo halisi ya maisha, na kushusha chini maadili. Kwa kuingiliana na watu wasio na dini, wapenda anasa, na wapotovu, vijana wengi hupoteza uhalisi na ukamilifu, na imani katika Mungu, na roho ya kujitoa

ambayo baba na mama Wakristo wameithamini na kuilinda kwa mafundisho makini na maombi ya dhati. [MH 403.1; HU Aya ya 30]

Wengi wanaoingia shuleni wakiwa na nia ya kujistahilisha kwa ajili ya huduma fulani isiyo na ubinafsi wanakuwa wametekwa na masomo ya ulimwengu (secular studies). Matamanio ya ukuu yanaamshwa katika kufanya vizuri kwenye masomo, ili wapate kufadhiliwa (scholarship) na kisha wapate nafasi na heshima duniani. Kusudi lao waliloingia nalo shuleni hapo awali, hupotea, na maisha yanaelekezwa kwenye ubinafsi na shughuli za kidunia. Na mara nyingi mazoea hutengenezwa ambayo huharibu maisha ya ulimwengu huu na kisha ya ulimwengu ujao pia. [MH 403.2; HU Aya ya 31]

Kwa kawaida, wanaume na wanawake wenye mawazo mapana, madhumuni yasiyo ya ubinafsi, na matamanio bora, ni wale ambao sifa hizi zilikuzwa toka katika mahusiano yao ya miaka ya awali. Katika kushughulika kote kwa Mungu na Israeli, Mungu alisisitiza kwao umuhimu wa kulinda mahusiano waliyo nayo, yaani watu ambao watoto wao wanashirikiana nao. Mipango yote ya maisha ya kiraia, kidini, na kijamii ilifanywa kwa kuzingatia kuwahifadhi watoto dhidi ya mahusiano yenye madhara na kuwafahamisha kanuni, maagizo na sheria za Mungu tangu miaka yao ya awali. Somo lililo kielelezo, lililotolewa wakati wa kuzaliwa kwa taifa na lilikuwa na asili ya kuvutia mioyo yote. Kabla ya hukumu ya mwisho ya kutisha kuwajia Wamisri kwa kifo cha wazaliwa wa kwanza, Mungu aliamuru watu Wake wakusanye watoto wao katika nyumba zao wenyewe. Miimo ya mlango wa kila nyumba vilitiwa alama ya damu, na kupitia ulinzi uliohakikishwa na ishara hii, watu wote walipaswa kutii. Ndivyo ilivyo hata hivi leo, wazazi wanaompenda na kumcha Mungu awana budi kuwaweka watoto wao chini ya “kifungo cha agano”—ndani ya ulinzi wa mivuto ile mitakatifu iliyofanywa kuwezekana kupitia damu ya Kristo yenye ikomboayo. [MH 403.3; HU Aya ya 32]

Kuhusu wanafunzi Wake Kristo alisema, “Mimi nimewapa neno lako... kwa kuwa wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu..” Yohana 17:14. [MH 404.1; HU Aya ya 33]

“Msiifuatishe namna ya dunia hii,” Mungu anatuagiza; “bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu.” Warumi 12:2. [MH 404.2; HU Aya ya 34]

“Msifungiwe nira pamoja na watu wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana ushirika gani kati ya nuru na giza?... Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? kwa maana sisi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, Nitakaa ndani yao, na ndani yao nitatembea; Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu. Kwa hiyo... [MH 404.3; HU Aya ya 35]

“Tokeni kati yao, mkatengwe nao, ...

Wala msiguse kitu kilicho najisi; ...

Nami nitawakaribisha,

Nami nitakuwa Baba kwenu,

Nanyi mtakuwa Wanangu wa kiume na wa kike,

asema Bwana Mwenyezi.” 2 Wakorintho 6:14-18. [MH 404.4; HU Aya ya 36]

“Kusanyeni watoto.” “Wajulishe amri za Mungu, na sheria Zake.” Yoeli 2:16; Kutoka 18:16. [MH 404.5; HU Aya ya 37]

“Wekeni Jina lLngu juu ya wana wa Israeli; Nami nitawabariki.” Hesabu 6:27. [MH 404.6; HU Aya ya 38]

“Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa Jina la Yehova, nao watakuwa na hofu kwako.” Kumbukumbu la Torati 28:10, ARV [MH 404.7; HU Aya ya 39]

“Na hayo mabaki ya Yakobo yatakuwa kati ya kabila nyingi mfano wa umande utokao kwa Bwana,

mfano wa manyunyu katika manyasi;

yasiyomngojea mtu,

wala kuwakawilia wanadamu.” Mika 5:7. [MH 404.8; HU Aya ya 40]

Twahesabiwa pamoja na Israeli. Maagizo yote yaliyotolewa kwa Waisraeli wa kale kuhusu malezi na mafunzo ya watoto wao, na ahadi zote za baraka kupitia utii, ni kwa ajili yetu. [MH 405.1; HU Aya ya 41]

Neno la Mungu kwetu ni, “Nitakubariki, ... nawe utakuwa baraka.” Mwanzo 12:2. [MH 405.2; HU Aya ya 42]

Kuhusu wanafunzi wa kwanza na wale wote wanaopaswa kumwamini siku za usoni kupitia neno lao, Kristo alisema, “Utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama Sisi tulivyo umoja; Mimi ndani yao, Nawe ndani Yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa Ndiwe uliyenituma, na ukawapenda wao kama ulivyonipenda Mimi.” Yohana 17:22, 23. [MH 405.3; HU Aya ya 43]

Maneno ya ajabu, ajabu kuu, karibu kupita uwezo wa kuikamata imani! Muumba wa ulimwengu wote, anawapenda wale wanaojitoa kwa ajili ya utumishi Wake, kama vile Yeye anavyompenda Mwanawe. Hata hapa na sasa, neema Yake yenye ukarimu, imetunukiwa kwetu, kwa kiwango hiki cha ajabu.

Ametupatia Nuru na Ukuu wa mbinguni, na pamoja Naye ametoa hazina yote ya mbinguni. Ijapokuwa ametuahidi sana kwa ajili ya maisha yajayo, Yeye hutoa zawadi za kifalme katika maisha haya tunayoishi sasa. Tukiwa ni raia wa neema Yake, Yeye atamani tufurahie kila kitu ambacho kitaboresha, kitapanua, na kuinua tabia zetu. Yeye Anangoja kuwahuisha na kuwatia moyo vijana kwa uwezo utokao juu, ili waweze kusimama chini ya bendera ya Kristo iliyotiwa doa na damu Yake, kufanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi kuongoza roho katika njia salama, kusimika miguu ya wengi juu ya Mwamba wa Kale. [MH 405.4; HU Aya ya 44]

Wote wanaotafuta kufanya kazi kwa kupatana na mpango wa Mungu wa elimu watadumishwa na neema Yake endelevu, uwepo Wake wa daima na nguvu Zake za utunzaji. Kwa kila mtu, asema: [MH 405.5; HU Aya ya 45]

“Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa BWANA, Mungu wako, Yu pamoja nawe kila uendako.” “Sitakupungukia wala sitakuacha.” Yoshua 1:9, 5. [MH 405.6; HU Aya ya 46]

“Maana kama vile mvua ishukavyo, na theluji kutoka mbinguni,

wala hairudi huko,

bali huinywesha nchi, na kuifanya izae na kuchipua,

ikampa mtu apandaye mbegu, na mtu alaye chakula;

ndivyo litakavyokuwa Neno Langu, litokalo katika kinywa Changu;

halitanirudia bure,

bali litatimiza mapenzi Yangu,

nayo litafanikiwa katika mambo yale niliyoituma.

Kwa maana mtatoka kwa furaha,

Mtaongozwa kwa amani:

Mbele yenu milima na vilima vitatoa

nyimbo,

na miti yote ya makondeni itapiga makofi.

Badala ya michongoma utamea msonobari, na badala ya mibigili mhadesi’ Jambo hili litakuwa la kumpatia Bwana Jina, litakuwa ishara ya milele isiyokataliwa; Isaya 55:10-13. [MH 406. ; HU Aya ya 47]

Ulimwenguni kote, jamii iko katika machafuko, na mabadiliko ya kina yanahitajika. Elimu itolewayo kwa vijana inapaswa kufanya matengenezo ya jamii nzima. [MH 406.2; HU Aya ya 48]

"Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa,

watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani,

wataitengeneza miji iliyoharibiwa,

mahali palipoachwa ukiwa kizazi baada ya kizazi."

Bali ninyi mtaitwa makuhani wa Bwana watu watawaita "wahudumu wa Mungu wetu....

Furaha yao itakuwa ya milele.

Maana Mimi, Yehova, naipenda hukumu ya haki." [MH 406.3; HU Aya ya 49]

"Nitaiongoza kazi yao katika kweli,

Nami nitafanya nao agano la milele."

"Na kizazi chao kitajulikana kati ya mataifa,

Na uzao wao katika kabila za watu;

Wote wawaonao watakiri ya kuwa wao ni kizazi kilichobarikiwa na Bwana....

Maana kama vile nchi itoavyo machipuko yake,

Na kama bustani ioteshavyo vitu vilivyopanda ndani yake,

ndivyo Bwana MUNGU atakavyootesha wokovu;

Na haki na sifa mbele ya mataifa yote." Isaya 61:4, 6-8; 61:8; 61:9, 11. [MH 406.4; HU Aya ya 50]

SEHEMU YA 7—MAARIFA MUHIMU

“Nuru ya ujuzi wa utukufu wa Mungu.”

SURA YA 35

MAARIFA HALISI YA KUMJUA MUNGU-ELIMU YA KWELI

Kama ilivyo kwa Mwokozi wetu, tu katika ulimwengu huu kumtumikia Mungu. Tu hapa duniani ili tabia zetu ziweze kufanana na tabia ya Mungu, na kwa maisha ya utumishi, kumfunua Yeye kwa ulimwengu. Ili kuwa watendakazi-wenza pamoja na Mungu, ili tufanane Naye na kufunua tabia Yake, ni sharti tumjue kwa usahihi. Ni lazima tumjue Yeye jinsi anavyojifunua Yeye Mwenyewe *(Msisitizo: si nadharia zetu za kufikirika kuhusu Mungu ni nani)*. [MH 409.1; HU Aya ya 1]

Maarifa katika kumjua Mungu ndio msingi wa elimu yote ya kweli na utumishi wo wote wa dhati. Hii ndiyo kinga pekee ya kweli dhidi ya majaribu. Ni hii pekee iwezayo kutufanya tufanane na Mungu katika tabia. [MH 409.2; HU Aya ya 2]

Huu ndio ujuzi unaohitajika kwa wote wanaofanya kazi kwa ajili ya kuwainua wanadamu wenzao. Mabadiliko ya tabia, ukamilifu wa maisha, ufanisi katika utumishi, kuzingatia kanuni mujarabu, yote yanategemea

maarifa sahihi ya kumjua Mungu. Maarifa haya ni maandalizi muhimu kwa maisha haya na yale yajayo. [MH 409.3; HU Aya ya 3]

"Na kumjua Mtakatifu ni ufahamu." Mithali 9:10. [MH 409.4; HU Aya ya 4]

Kupitia kumjua Yeye, ametukirimia “vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa.” 2 Petro 1:3. [MH 409.5; HU Aya ya 5]

“Uzima wa milele ndio huu,” amesema Yesu, “wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” Yohana 17:3. [MH 410.1; HU Aya ya 6]

“Mwenyezi Mungu asema hivi,

Mwenye hekima asijisifu kwasababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijififu kwasababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake

Bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu Mimi, na kunijua, ya kuwa Mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu na haki katika nchi; kwa maana napendezwa na mambo hayo, asema Bwana.” Yeremia 9:23, 24. [MH 410.2; HU Aya ya 7]

Twahitaji kujifunza mafunuo yamhusuyo Yeye Mwenyewe, ambayo Mungu Mwenyewe amekwisha kutoa. [MH 410.3; HU Aya ya 8]

“Mjue sana Mungu,

ili uwe na amani;

Ndivyo mema yatakavyokujia.

Uyapokee, tafadhali, mafunzo yatokayo katika kinywa Chake,

Na Maneno Yake yaweke moyoni mwako....

Naye Mwenyezi atakuwa hazina yako.... [MH 410.4; HU Aya ya 9]

“23 Ukimrudia Mwenyezi, utajengwa; Ukiuondoa udhalimu mbali na hema yako.

24 Nawe hazina zako ziweke mchangani, Na dhahabu ya Ofiri iweke kati ya mawe ya vijito;

25 Naye Mwenyezi atakuwa hazina yako, Atakuwa ni fedha ya thamani kwako.

26 Kwani ndipo utakapojifurahisha katika Mwenyezi, Na kuinua uso wako kumwelekea Mungu.

27 Utamwomba Yeye Naye atakusikia; Nawe utazitimiliza nadhiri Zake." Ayubu 22:21-29, [MH 410.5; HU Aya ya 10]

"Kwasababu mambo Yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana wazi, na kufahamika kwa kazi Zake; yaani, uweza Wake wa milele na Uungu Wake, hata wasiwe na udhuru" Warumi 1:20. [MH 410.6; HU Aya ya 11]

Mambo ya asili tunayoyaona sasa, yanatupa muonjo au dhana hafifu wa utukufu wa Edeni. Dhambi imeharibu uzuri wa dunia; kwenye mambo yote duniani kunaonekana viashiria vya utendaji wa uovu. Hata hivyo bado kuna mengi mazuri ambayo yamebakia. Maumbile yashuhudia kwamba Mmoja asiye na kikomo katika uweza, mkuu wa wema, rehema, na upendo, aliumba dunia, na kuijaza uhai na furaha. Hata katika hali yake ya kuharibiwa baada ya dhambi, mambo yote yanaonyesha kazi ya mikono ya Stadi Mkuu. Popote tunapogeuka, twaweza kusikia sauti ya Mungu, na kuona ushahidi wa wema Wake. [MH 411.1; HU Aya ya 12]

Toka kwenye sauti kuu ya ngurumo ya radi yenye kina na mngurumo usiokoma wa mawimbi ya bahari kuu ya kale, hadi nyimbo za furaha zinazofanya misitu irindime kwa sauti nzuri, sauti elfu kumi za asili zikinena sifa Zake Mungu. Katika ardhi na bahari na anga, pamoja na rangi zake za kustaajabisha, zikitofautiana kwa uzuri kwa kulinganisha au zikichanganyika kwa pamoja kwa kupatana, twauona utukufu Wake. Milima kamili yatuambia uweza Wake. Miti inayopeperusha bendera zake za kijani kwenye mwanga wa jua, na maua katika uzuri wayo maridadi, huelekeza kwa Muumba wake. Kijani kilicho hai kinachoifunika ardhi ya kahawia kama zulia, kinaeleza juu ya utunzaji wa Mungu kwa viumbe vyake vilivyo vinyenyekevu zaidi. Mapango ya bahari na vilindi vya ardhi vyadhihirisha hazina Zake. Yeye aliyeweka lulu katika bahari na amethisto na krisoliti katikati ya miamba, ni mpenzi wa uzuri. Jua linapochomoza angani humwakilisha Yeye ambaye ni uzima na nuru ya vyote alivyoviumba. Uangavu na uzuri wote unaopamba dunia na kuangaza anga lote, hunena juu ya Mungu. [MH 411.2; HU Aya ya 13]

"Utukufu Wake ukazifunika mbingu."

"Nayo dunia ikajaa sifa Yake." [MH 412.1; HU Aya ya 14]

"Mchana husemezana na mchana,

usiku hutolea usiku maarifa.

Hakuna lugha wala maneno,

sauti yako haisikilikani.

Sauti yao imeenea duniani mwote,

Na maneno yao hata miisho ya ulimwengu." Habakuki 3:3; Zaburi 104:24; Zaburi 19:2-4, pambizo. [MH 412.2; HU Aya ya 15]

Mambo yote hunena juu ya pendo Lake, utunzaji Wake kama Baba na matamanio Yake ya kuwafurahisha watoto Wake. [MH 412.3; HU Aya ya 16]

Nguvu kuu ifanyayo kazi kupitia maumbile yote na kudumisha vitu vyote siyo tu kuwa ni kanuni iliyoenea, nguvu ifanyayo kazi, kama wanasayansi wanavyofafanua. La! Mungu ni Roho; na bado Yeye ni Nafsi; kwani ndivyo alivyojidhihirisha Yeye Mwenyewe kwetu: [MH 413.1; HU Aya ya 17]

"BWANA Ndiye Mungu wa Kweli,

Yeye Ndiye Mungu aliye hai, na Mfalme wa milele: ...

Miungu hiyo isiyofanya mbingu na nchi,

hiyo itaangamia katika nchi, nayo itatoweka chini ya mbingu. [MH 413.2; HU Aya ya 18]

"Fungu la Yakobo siye kama hawa;

maana Yeye Ndiye Aliyeviumba vitu vyote." [MH 413.3; HU Aya ya 19]

"Ameiumba dunia kwa uweza Wake,

ameuthibitisha ulimwengu kwa hekima Yake,

na kwa fahamu Wake amezitandika mbingu." Yeremia 10:10, 11, 16, 12. [MH 413.4; HU Aya ya 20]

Viumbe Asili Sio Mungu

(Maumbile kama Milima, Jua, Anga, Bahari, Mimea au Wanyama sio Mungu)

Kazi ya mikono ya Mungu katika viumbe asili si Mungu Mwenyewe katika viumbe hivyo asili. Viumbe vya asili ni udhihirisho wa tabia na uweza wa Mungu *(Msisitizo: ni maelezo yenye ujumbe usio wa maneno ambayo mwanadamu anaweza kuyaelewa)*; lakini hatupaswi kuichukulia asili kwamba ndiyo Mungu Mwenyewe. Stadi za sanaa za wanadamu hutengeneza vitu kwa kutumia ufundi mzuri sana, vitu vinavyopendeza macho, na sanaa hizi au vitu hivi vyatuonyesha wazo la mbunifu; lakini kile kitu kilichotengenezwa na huyu fundi stadi, siyo fundi mwenyewe! Si ile kazi ya sanaa ndiyo inastahili heshima, la! bali yule aliyeifanya ile kazi ya sanaa, ndiye anayehesabiwa kuwa anastahili heshima. Hivyo, ikiwa asili ni onyesho linaloelezea wazo la Mungu, sio asili ambayo

inapaswa kuinuliwa, bali ni Mungu wa asili Ndiye apaswa kuinuliwa *(Msisitizo: vinyago, majengo au picha zilizochorwa ni kazi za msanii, ila hatusifu zile kazi za vinyago au picha au majengo, bali tunampongeza msanii)*. [MH 413.5; HU Aya ya 21]

"Njoni tuabudu, tusujudu;

Tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba."

“Mkononi Mwake zimo bonde za dunia;

hata vilele vya milima ni Vyake.

Bahari ni Yake, na Ndiye aliyeifanya;

Na mikono Yake iliumba nchi kavu.” Zaburi 95:6 ; 95:4, 5, [MH 413.6; HU Aya ya 22]

“Mtafuteni Yeye afanyaye Kilimia na Orioni,

na kukigeuza kivuli cha mauti kuwa asubuhi,

na kuufanya mchana kuwa giza kwa usiku;

"Yeye aifanyizaye milima, na kuuumba upepo,

na kumwambia mwanadamu mawazo yake;"

“Yeye avijengaye vyumba Vyake mbinguni,

Na kuweka misingi ya kuba yake juu ya nchi;

“Yeye Ndiye ayaitaye maji ya bahari,

na kuyamwaga juu ya uso wa nchi;

Yehova ndilo Jina Lake.” Amosi 5:8; Amosi 4:13; Amosi 9:6, ukingo; Amosi 9:6, [MH 414.1; HU Aya ya 23]

Kuumbwa Kwa Dunia

Kazi ya uumbaji haiwezi kuelezewa na sayansi. Ni sayansi gani inayoweza kueleza siri na fumbo la maisha? [MH 414.2; HU Aya ya 24]

“Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri. Waebrania 11:3. [MH 414.3; HU Aya ya 25]

“Mimi naiumba nuru, na kulihuluku giza: ...

Mimi, Bwana, niyatendaye hayo yote....

Mimi nimeiumba dunia,

na kumuumba mwanadamu juu yake;

Mimi, naam, kwa mikono Yangu Mimi, nimezitandaza mbingu,

na jeshi lake lote nimeliamuru.

“Niziitapo husimama pamoja.” Isaya 45:7-12; 48:13. [MH 414.4; HU Aya ya 26]

Katika uumbaji wa dunia, Mungu hahitaji malighafi au maada iliyokuwapo hapo awali, aliumba bila ya kutumia kitu chochote. “Akanena, ikawa; ... Akaamuru, ikasimama.” Zaburi 33:9. Vitu vyote, vya kimwili au vya kiroho, vilisimama mbele za Bwana Yehova kwa sauti Yake na viliumbwa kwa kusudi Lake Mwenyewe. Mbingu na jeshi lake lote, nchi na vyote vilivyomo ndani yake, vilitokea kwa pumzi ya kinywa Chake. [MH 414.5; HU Aya ya 27]

Katika uumbaji wa mwanadamu kulidhihirika namna Mungu alivyo. Mungu alipomfanya mwanadamu kwa mfano Wake, umbo la mwanadamu lilikuwa kamilifu katika mpangilio wake wote, lakini lilikuwa halina uhai. Ndipo Mungu wa nafsi hai, aliyekuwepo Mwenyewe bila ya kuumbwa (self-existent), akapulizia ndani ya umbo hilo pumzi ya uhai, na mwanadamu akawa kiumbe hai, mwenye akili. Sehemu zote za kiumbe huyu ziliwekwa katika utendaji. Iwe ni moyo, mishipa ya kusafirisha damu safi (ateri), mishipa ya kusafirisha damu yenye taka (veini), ulimi, mikono, miguu, milango ya utambuzi, uwezo wa akili, vyote vilianza kazi yake, na vyote viliwekwa chini ya sheria. Mwanadamu akawa nafsi hai. Kupitia Kristo ambaye ni Neno, Mungu mwenyewe alimwumba mwanadamu na kumpa akili na uwezo. [MH 415.1; HU Aya ya 28]

Sehemu zote zinazotengeneza mwili wetu Yeye aliviona vyote tukiwa tumeumbwa tumesitiriwa; Macho Yake yaliona kila sehemu ya mwili, tukiwa bado si wakamilifu, na katika kitabu Chake vipande vya mwili wetu vyote viliandikwa, japokuwa vilikuwa havipo, viliandikwa kabla havijakuwepo bado. [MH 415.2; HU Aya ya 29]

Ukilinganisha na viumbe wengine wo wote walioumbwa ambao ni wa chini, Mungu alikusudia kwamba mwanadamu, ambaye ndiye kazi kuu ya uumbaji Wake, adhihirishe kueleza Yake Mungu na kufunua utukufu Wake. Lakini mwanadamu hatakiwi kujiinua kana kwamba yeye ni Mungu. [MH 415.3; HU Aya ya 30]

“Mfanyieni Bwana kelele za shangwe....

Mtumikieni Bwana kwa furaha:

Njoni mbele Zake kwa kuimba.

Jueni ya kuwa Bwana Ndiye Mungu;

Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu Wake; na kondoo wa malisho Yake.

Ingieni malangoni Mwake kwa kushukuru,

nyuani Mwake kwa kusifu;

mshukuruni, lihimidini Jina Lake."

"Mtukuzeni Bwana, Mungu wetu,

Sujuduni mlima Wake mtakatifu;

Kwa maana BWANA Mungu wetu Ndiye mtakatifu." Zaburi 100:1-4; Zaburi 99:9. [MH 415.4; HU Aya ya 31]

Mungu daima anashughulika katika kutegemeza na kuutumia uumbaji kama watumishi Wake aliowaumba. Yeye hutenda kazi kupitia sheria za asili, akizitumia kama vyombo Vyake. Hivi vyombo Vyake havijiendeshi vyenyewe tu (siyo roboti au automatiki). Asili katika kazi yake inashuhudia uwepo mwerevu na njia hai ya Yeye ambaye hutenda kazi katika mambo yote kulingana na mapenzi Yake. [MH 416.1; HU Aya ya 32]

"Ee Bwana,

Neno Lako lasimama imara mbinguni hata milele.

Uaminifu Wako upo kizazi baada ya kizazi

Umeiweka nchi, nayo inakaa.

Kwa hukumu Zako vimesimama imara hata leo; maana vitu vyote ni watumishi Wako

"Bwana amefanya kila lililompendeza katika mbingu na katika Mbingu na katika nchi, katika bahari na katika vilindi vyote."

"Kwa maana aliamuru, vikaumbwa.

Amevithibithisha milele hata milele,

Ametoa amri wala haitapita." Zaburi 119:89-91; 135:6; 148:5, 6. [MH 416.2; HU Aya ya 33]

Si kwa uwezo asili kwamba mwaka baada ya mwaka dunia hutoa matunda yake ya ukarimu na kuendelea kulizunguka jua katika mwendo wake. Mkono

wa Yule Asiye na ukomo unafanya kazi daima kuiongoza sayari yetu hii. Ni nguvu za Mungu zinazotumiwa daima ambazo huiweka dunia katika nafasi yake ili iweze kuzunguka kwa jinsi inavyotakiwa. Ni Mungu anayelifanya jua litoke mbinguni. Yeye hufungua madirisha ya mbinguni na kutoa mvua. [MH 416.3; HU Aya ya 34]

"Ndiye atoaye theluji kama sufu;

Huimwaga barafu yake kama majivu." [MH 416.4; HU Aya ya 35]

"Atoapo sauti Yake, pana wingi wa maji mbinguni,

Naye hupandisha mawingu toka ncha za nchi

Huifanyia mvua umeme,

huutoa upepo katika hazina zake." Zaburi 147:16; Yeremia 10:13. [MH 416.5; HU Aya ya 36]

Ni kwa uweza Wake ndiyo mimea husitawi na kunawiri, kwamba kila jani huchipua, kila ua huchanua, na kila tunda hukua. [MH 416.6; HU Aya ya 37]

Utaratibu wa mwili wa mwanadamu unavyojiendesha hauwezi kueleweka kikamilifu; unawasilisha mafumbo yanayowashangaza watu wenye akili nyingi zaidi. Sio matokeo ya mchakato, ambao ulishawekwa hapo awali, kwamba ndio unaodumu kutenda kazi. Katika Mungu twaishi na kutembea na kuwa na uhai wetu. Moyo unaodunda, mapigo katika mapafu, kila neva na msuli katika mwanadamu aliye hai, huamriwa katika utaratibu na utendaji kwa nguvu ya Yule Aliyepo daima. [MH 417.1; HU Aya ya 38]

Biblia hutuonyesha Mungu katika mahali Pake pa juu na Patakatifu, si katika hali ya utulivu pasipo utendaji, si katika ukimya na upweke, bali amezungukwa na elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu ya viumbe watakatifu, yaani malaika, wote wakingojea kutekeleza matakwa Yake. Kupitia wajumbe hawa Yeye Yuko katika mawasiliano yaliyo hai na yenye bidii na kila sehemu ya milki Yake. Kwa Roho Wake, Yeye Yuko kila mahali. Kwa njia ya Roho Wake na malaika Zake huwahudumia watoto wa wanadamu. [MH 417.2; HU Aya ya 39]

Juu ya machafuko na masumbufu ya dunia, Yeye ameketi kwenye kiti cha enzi; vitu vyote viko wazi kwa uchunguzi Wake wa Kiungu; na kutoka katika umilele Wake mkuu na tulivu, Yeye huamuru yale ambayo majaliwa Yake huyaona kuwa ni bora zaidi. [MH 417.3; HU Aya ya 40]

"Njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake;

kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu." [MH 417.4; HU Aya ya 41]

"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote....

Katika njia zako zote mkiri Yeye,

Naye atayanyosha mapito yako." [MH 417.5; HU Aya ya 42]

"Tazama Jicho la Bwana li kwao wamchao,

Wazingojeao fadhili Zake;

Ili kuziokoa nafsi zao na mauti,

Na kuwahamisha katika njaa." [MH 417.6; HU Aya ya 43]

"Ee Mungu, jinsi zilivyo na thamani fadhili Zako! Wanadamu huukimbilia uvuli wa mbawa Zako.....

Wana wa binadamu hukimbilia chini ya uvuli

wa mbawa zako."

"Heri ambaye Mungu wa Yakobo ni msaada wake,

Ambaye tumaini lake ni kwa Bwana, Mungu wake. [MH 417.7; HU Aya ya 44]

"Ee Yehova, nchi imejaa fadhili Zako zenye upendo."

Huzipenda "haki na hukumu."

Wewe "uliye tumaini la miisho yote ya dunia,

Na la bahari iliyo mbali sana

wautuliza uvumi wa bahari, ...

na ghasia ya mataifa." [MH 418.1; HU Aya ya 45]

"Milango ya asubuhi na jioni waifurahisha."

"Umeuvika mwaka taji ya wema Wako;

Mapito Yako yadondoza unono." [MH 418.2; HU Aya ya 46]

"Bwana huwategemeza wote waangukao,

huwainua wote walioinama chini.

Macho ya wote yakuelekea Wewe;

Nawe unawapa chakula chao kwa wakati wake.

Waufumbua mkono Wako,

wakishibisha kila kilicho hai matakwa yake.”

Yeremia 10:23; Mithali 3:5, 6; Zaburi 33:18, 19; Zaburi 36:7; Zaburi 146:5; Zaburi 119:64; Zaburi 33:5; Zaburi 65:5-7; Zaburi 65:8, 11; Zaburi 145:14-16. [MH 418.3; HU Aya ya 47]

Nafsi ya Mungu Imefunuliwa katika Kristo

Kama Nafsi Hai, Mungu amejifunua Mwenyewe kupitia Mwanawe. Mng’ao wa utukufu wa Baba, "na sura kamili ya Nafsi Yake," Yesu, kama Mwokozi, alikuja ulimwenguni. Kama Mwokozi, alipaa juu. Kama Mwokozi hufanya maombezi katika nyua za mbinguni *(Msisitizo: huokoa mtu mmoja mmoja—personal saviour; haokoi kundi)*. Mbele ya kiti cha enzi cha Mungu kwa niaba yetu huhudumu “Mmoja kama Mwana wa Adamu.” Waebrania 1:3; Ufunuo 1:13. [MH 418.4; HU Aya ya 48]

Kristo, Nuru ya ulimwengu, alifunika utukufu ung'aao wa Uungu Wake na akaja kuishi kama mwanadamu kati ya wanadamu, ili bila kuangamizwa kwa utukufu Wake, waweze kumfahamu Muumba wao (Ebrania 12:29). Kwa kuwa dhambi ilileta utengano kati ya mwanadamu na Muumba wake, hakuna mwanadamu ambaye amemwona Mungu wakati wowote, isipokuwa kama anavyofunuliwa kupitia Kristo. [MH 419.1; HU Aya ya 49]

“Mimi na Baba Yangu tu umoja,” Kristo alisema. “Hakuna amjuaye Mwana ila Baba; wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana, na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia.” Yohana 10:30; Mathayo 11:27. [MH 419.2; HU Aya ya 50]

Kristo alikuja kuwafundisha wanadamu kile ambacho Mungu anataka wakijue. Mbinguni juu, katika dunia, katika ulimwengu wa maji, twaona kazi ya mikono ya Mungu. Viumbe vyote vyashuhudia uweza Wake, hekima Yake, na upendo Wake. Hata hivyo sio kutoka kwenye nyota au bahari au penye maporomoko ya maji kwamba ndiyo twaweza kujifunza juu ya Nafsi ya Mungu bali kama ilivyofunuliwa katika Kristo. [MH 419.3; HU Aya ya 51]

Mungu aliona kwamba ufunuo ulio wazi zaidi kuliko asili ulihitajika ili kuonyesha Nafsi Yake na tabia Yake. Yeye Alimtuma Mwanawe ulimwenguni ili kwa kadiri inavyoweza kuvumilika kwa macho ya wanadamu kuutazama utukufu Wake, adhihirishwe kwa watu asili na sifa za Mungu asiyeonekana kwa macho ya mwanadamu. [MH 419.4; HU Aya ya 52]

Kristo amefunuliwa kwa Wanafunzi

Tujifunze maneno ambayo Kristo aliyanena katika chumba cha juu usiku ule kabla ya kusulubiwa Kwake. Alikuwa akikaribia saa Yake ya kujaribiwa, na

alitafuta kuwafariji wanafunzi Wake, ambao haikuwa budi kwao kutahiniwa na kujaribiwa vikali. [MH 419.5; HU Aya ya 53]

“Msifadhaike mioyoni mwenu,” akasema “Mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi pia. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia. Naenda kuwaandalia mahali... [MH 419.6; HU Aya ya 54]

“Tomaso akamwambia, Bwana, sisi hatujui uendako; nasi twaijuaje njia? Yesu akamwambia, Mimi Ndimi njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi. Kama mngalinijua Mimi, mngalimjua na Baba Yangu; na tangu sasa mnamjua, tena mmemwona.... [MH 419.7; HU Aya ya 55]

Filipo akamwambia “Bwana, utuonyeshe Baba,” “yatutosha.” Yesu akamwambia, Mimi nimekuwa pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona Mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, utuonyeshe Baba? Husadiki ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani Yu ndani Yangu? Hayo Maneno niwaambiayo Mimi siyasemi kwa shauri Langu, bali Baba akaaye ndani Yangu huzifanya kazi Zake.” [MH 420.1; HU Aya ya 56]

Wanafunzi bado walikuwa hawajaelewa maneno ya Kristo kuhusu uhusiano Wake na Mungu. Mengi ya mafundisho Yake yalikuwa bado giza kwao. Kristo alitamani wawe na maarifa yaliyo wazi zaidi, na yaliyo tofauti zaidi juu ya Mungu. [MH 420.2; HU Aya ya 57]

“Hayo nimesema nanyi kwa mithali,” Alisema; “lakini saa yaja ambapo sitasema nanyi tena kwa mithali, bali nitawapa waziwazi habari ya Baba.” Yohana 16:25. [MH 420.3; HU Aya ya 58]

Wakati wa Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu alipomiminwa juu ya wanafunzi, hawa walielewa kwa ukamilifu zaidi kweli ambazo Kristo alikuwa amesema kwa mifano. Mengi ya mafundisho yaliyokuwa fumbo kwao yaliwekwa wazi. Lakini hata wakati huo wanafunzi hawakupokea kutimizwa kamili kwa ahadi ya Kristo. Walikuwa wamepokea maarifa yote ya kumjua Mungu ambayo wangeweza kustahimili, lakini utimizo kamili wa ahadi ambayo Kristo angewaonyesha waziwazi juu ya Baba ulikuwa bado haujawadia. Ndivyo ilivyo hata leo. Maarifa yetu ya kumjua Mungu ni sehemu tu, yaani nusu-nusu na sio makamilifu. Pale pambano litakapokwisha, na Mwana wa Adamu, Kristo Yesu akiwakiri watendakazi Wake waaminifu mbele za Baba, ambao katika ulimwengu wa dhambi wametoa ushuhuda wa kweli kwa ajili Yake, wataelewa waziwazi yale ambayo sasa ni mafumbo kwao. [MH 420.4; HU Aya ya 59]

Kristo aliuchukua pamoja Naye hadi kwenye nyua za mbinguni ubinadamu Wake uliotukuzwa. Kwa wale wanaompokea huwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu, ili hatimaye Mungu awapokee kama wana Wake, na wakae

Naye milele zote. Ikiwa katika maisha haya watakuwa waaminifu kwa Mungu, hatimaye “watamwona uso Wake; na Jina Lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao.” Ufunuo 22:4. Na furaha ya mbinguni ni nini basi isipokuwa kumwona Mungu? Je, ni furaha gani kubwa zaidi inayoweza kuja kwa mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema ya Kristo zaidi ya kuutazama uso wa Mungu na kumjua Yeye kama Baba? [MH 421.1; HU Aya ya 60]

Maandiko yanaonyesha wazi uhusiano kati ya Mungu na Kristo, na yanaleta ufahamu wazi wa Nafsi ya kila mmoja wao, na upekee wao mmoja mmoja (Uungu). [MH 421.2; HU Aya ya 61]

“Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema nasi katika Mwanawe; ... kwa kuwa Yeye ni mng’ao wa utukufu Wake na chapa ya Nafsi Yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza Wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; amefanyika kuwa bora zaidi kupita malaika, kwa kadiri Jina alilorithi lilivyo tukufu kuliko lao. Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wowote, Ndiwe Mwanangu…[MH 421.3

“Ndiwe Mwanangu,

Mimi leo nimekuzaa? [MH 421.4; HU Aya ya 62]

Na tena, [MH 421.5; HU Aya ya 63]

Mimi Nitakuwa Kwake Baba,

Naye atakuwa Kwangu Mwana?” Waebrania 1:1-5. [MH 421.6; HU Aya ya 64]

Nafsi ya Baba na Mwana, pia umoja uliopo kati Yao, umeonyeshwa katika sura ya kumi na saba ya Yohana, katika sala ya Kristo kwa ajili ya wanafunzi Wake: [MH 421.7; HU Aya ya 65]

“Wala si hao tu ninaowaombea, lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao; wote wawe na umoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami ndani Yako, hao nao wawe ndani Yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba Wewe Ndiwe uliyenituma.” Yohana 17:20, 21. [MH 421.8; HU Aya ya 66]

Umoja uliopo kati ya Kristo na wanafunzi Wake hauondoi ubainifu wa nafsi zao (kati ya nafsi ya Kristo na nafsi ya wanafunzi). Wao ni wamoja katika kusudi, fikra/mawazo, katika maumbile ya tabia, lakini si katika Nafsi. Ni kwa jinsi hiyo ambapo Mungu na Kristo ni wamoja. [MH 422.1; HU Aya ya 67]

Tabia ya Mungu Iliyofunuliwa katika Kristo

Akijivika ubinadamu, Kristo alikuja kuwa mmoja pamoja na ulimwengu wa mwanadamu, na wakati huo huo kumfunua Baba yetu wa mbinguni kwa wanadamu wenye dhambi. Yeye aliyekuwa katika uwepo wa Baba tangu mwanzo, Yeye aliyekuwa Mfano (udhihirisho) wa Mungu asiyeonekana (Kolosai 1:15-17), Ndiye pekee aliyeweza kufunua tabia ya Uungu kwa wanadamu. Alifananishwa na ndugu Zake katika mambo yote. Alifanyika mwili kama sisi. Alikuwa na njaa na kiu na uchovu. Alidumishwa kwa chakula na kuburudishwa na usingizi. Alishiriki mengi yaliyo fungu la wanadamu; hata hivyo alikuwa Mwana wa Mungu asiye na lawama (asiye na hatia). Alikuwa mgeni na mpitaji katika dunia—ulimwenguni, lakini hakuwa wa ulimwengu; alijaribiwa na kutahiniwa kama wanaume na wanawake leo wanavyotahiniwa na kujaribiwa, lakini bado angali akiishi maisha yasiyo na dhambi. Mpole, Mwenye huruma, Mwenye sikitiko kwa wanadamu, Mwenye kujali wengine daima, aliifunua tabia ya Mungu, na daima alijishughulisha katika kutumika kwa ajili ya Mungu na mwanadamu. [MH 422.2; HU Aya ya 68]

"BWANA amenitia mafuta," Yeye alisema,

"Niwahubiri maskini/wanyenyekevu habari njema;

Amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo,

amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao,"

"Na vipofu kupata kuona tena;

"kuwaacha huru waliosetwa; ...

Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa …

Kuwafariji wote waliao." Isaya 61:1; Luka 4:18; Isaya 61:2, [MH 423.1; HU Aya ya 69]

Atuagiza, "Lakini Mimi Nawaambia, wapendeni adui zenu, wabarikini wale wanaowalaani, watendeeni mema wale wanaowachukia ninyi, waombeeni wanaowadhulumu na kuwaudhi; ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; "Kwa kuwa Yeye ni mwema kwa wasiomshukuru na waovu." "Huwaangazia jua Lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki au wadhalimu." "Basi iweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma." Mathayo 5:44, 45; Luka 6:35; Mathayo 5:45; Luka 6:36. [MH 423.2; HU Aya ya 70]

"Kwa rehema za Mungu wetu; ...

Asubuhi itokayo juu imetujia,

Ili kuwaangazia waketio katika giza na uvuli wa mauti, na kuiongoza miguu yetu katika njia ya amani." Luka 1:78, 79. [MH 423.3; HU Aya ya 71]

Utukufu wa Msalaba

Ufunuo wa upendo wa Mungu kwa mwanadamu kiini chake ni katika msalaba. Umaana wake kamili hauwezi kutamkika kwa maneno ya kibinadamu, kalamu haiwezi kufafanua, akili ya mwanadamu haiwezi kuelewa. Kwa kuutazama msalaba wa Kalwari, twaweza tu kusema, "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16. [MH 423.4

Kristo aliyesulubiwa kwa ajili ya dhambi zetu, Kristo aliyefufuka toka katika wafu, Kristo aliyepaa kwenda juu mbinguni, ni sayansi ya wokovu ambayo hatuna budi kujifunza wenyewe na kuwafundisha wengine. [MH 424.1; HU Aya ya 72]

Alikuwa ni Kristo

"Ambaye Yeye mwanzo alikuwa Yuna namna ya Mungu, Naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; Naye alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza, akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." Wafilipi 2:6-8, [MH 424.2; HU Aya ya 73]

"Kristo Ndiye aliyekufa, naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, Naye Yuko mkono wa kuume wa Mungu; Tena Ndiye anayetuombea." "Kwa sababu hii, Yeye aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa Yeye; maana Yu hai sikuzote ili awaombee. Warumi 8:34; Waebrania 7:25. [MH 424.3; HU Aya ya 74]

"Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali Yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi." Waebrania 4:15, [MH 424.4; HU Aya ya 75]

Ni kwa njia ya Kristo kuwa zawadi yetu ndipo tunapokea kila baraka. Kupitia karama (zawadi) hiyo siku baada ya siku hutujia bubujiko la daima la wema wa Yehova. Kila ua, pamoja na rangi zake maridadi, pamoja na harufu yake nzuri, hutolewa kwa ajili yetu ili tuweze kufurahia kupitia kipawa hicho kimoja (Zawadi hiyo ya Kristo). Jua na mwezi viliumbwa na Yeye. Hakuna nyota inayopamba mbingu kwa uzuri ambayo Yeye hakuiumba. Kila tone la mvua linaloanguka, kila mwale wa nuru inayoangazia ulimwengu wetu usio na shukrani, yashuhudia upendo wa Mungu katika Kristo. Kila kitu hutolewa kwetu kupitia Kipawa Kimoja tusichoweza kukieleza ipasavyo, Mwana,

Mzaliwa-pekee wa Mungu. Alisulubishwa msalabani ili neema hizi zote ziweze kutiririka (kububujika) kwenye kazi ya Mungu (utendakazi wa Mungu) (2 Wakorintho 9:15). [MH 424.5; HU Aya ya 76] *[Katika kifungu hiki, maneno zawadi, kipawa na karama yametumika kwa mbadilishano kumaanisha Zawadi]*

"Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu." 1 Yohana 3:1. [MH 425.1; HU Aya ya 77]

"Watu hawakusikia, wala kufahamu kwa masikio, wala jicho halikuona Mungu ila Wewe, Atendaye mambo kwa ajili yake amngojaye." Isaya 64:4, [MH 425.2; HU Aya ya 78]

Maarifa Yabadilishayo

Maarifa ya kumjua Mungu kama yalivyofunuliwa katika Kristo ni elimu ambayo wote wanaookolewa lazima wawe nayo. Ni maarifa ambayo hufanya mabadiliko ya tabia zetu. Maarifa haya, yakipokelewa, yataiumba upya nafsi katika sura ya Mungu. Na yatatoa kwa kila kiungo cha mwanadamu nguvu ya kiroho ambayo ni ya kiungu. [MH 425.3; HU Aya ya 79]

"Sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana kama katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho." 2 Wakorintho 3:18. [MH 425.4; HU Aya ya 80]

Kuhusiana na maisha Yake Mwenyewe Mwokozi alisema, "Nimezishika amri za Baba Yangu." Yohana 15:10. "Baba hakuniacha peke Yangu; kwa maana siku zote nafanya yale yampendezayo Yeye." Yohana 8:29. Vile Yesu alivyokuwa katika asili ya mwanadamu, ndivyo Mungu anavyomaanisha wafuasi Wake kuwa. Katika nguvu Zake hatunabudi kuishi maisha ya ukamilifu na wema ambayo Mwokozi aliyaishi. [MH 426.1; HU Aya ya 81]

"Kwa sababu hiyo," Paulo asema, "nampigia Baba magoti mbele za Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa Jina Lake Ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa, awajalieni kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake. Kufanywa imara kwa nguvu na Roho Wake katika utu wa ndani; ili Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani; mkiwa na shina na msingi katika upendo, ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wa Kristo upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu." Waefeso 3:14-19. [MH 426.2; HU Aya ya 82]

Ha—"tuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu ili mjazwe maarifa ya mapenzi Yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; mwenende kama

ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda katika kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu; mkiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu Wake, mpate saburi yote na uvumilivu pamoja na furaha.” Wakolosai 1:9-11. [MH 426.3; HU Aya ya 83]

Haya ndiyo maarifa, elimu ambayo Mungu anatualika kuyapokea, na mengine yote mbali na haya ni ubatili na si kitu. [MH 426.4; HU Aya ya 84]

SURA YA 36

HATARI KATIKA UJUZI WA KUDHANIA

Mojawapo ya maovu makubwa zaidi yanayoambatana na utafutaji wa maarifa, uchunguzi wa sayansi, ni mwelekeo wa kuinua fikira ya kibinadamu

kuvuka mpaka wake halisi na eneo lake stahiki. Wengi hujaribu kufanya maamuzi kuhusu Muumba na kazi Zake kwa ujuzi wao wenyewe wa sayansi usio na kamilifu. Hujitahidi kubainisha asili na sifa Zake Mungu na haki Zake pekee za kifalme, na wanaendekeza nadharia za kubahatisha-bahatisha au za kubuni, kuhusu Yule Asiye na ukomo. Wale wanaojihusisha na njia hii ya utafiti wanakanyaga ardhi ambayo hawajapewa ruhusa kutembea juu yake. Utafiti wao hautatoa matokeo yo yote muhimu na unaweza tu kuiongoza roho kwenye hatari kubwa. [MH 427.1; HU Aya ya 1]

Wazazi wetu wa kwanza waliongozwa dhambini, kwa kujiingiza katika tamaa ya maarifa ambayo Mungu alikuwa amewazuilia. Katika kutafuta kupata maarifa haya, walipoteza kila kitu ambacho mwanadamu alipewa stahiki ya kuwa nacho. Endapo Adamu na Hawa wasingaliugusa kamwe mti waliokatazwa, Mungu angaliwapa ujuzi—maarifa ambayo yasingalikuwa na laana ya dhambi, maarifa ambayo yangaliwaletea furaha ya milele. Yote waliyopata kwa kumsikiliza mjaribu yalikuwa ni kujua dhambi na matokeo yake. Kwa kutotii kwao, wanadamu walitengwa na Mungu na dunia ikatengwa na mbingu. [MH 427.2; HU Aya ya 2]

Somo hili ni kwa ajili yetu. Mazingira ambayo Shetani aliwaongoza wazazi wetu wa kwanza ndiyo hayo-hayo ambayo anawavutia wanadamu leo. Anaugharikisha ulimwengu kwa maneno ya uongo ya kupendeza na yanayofurahisha watu. Kwa kila hila iliyo kwenye mamlaka yake hujaribu kuitumia kwa watu kukisia na kubuni mambo kuhusu Mungu. Hivyo ndivyo anavyotafuta kuwazuia wasipate ujuzi huo wa Mungu uuelekeao wokovu. [MH 428.1; HU Aya ya 3]

Nadharia za Pantheismu

[Pantheism ni imani kwamba viumbe asili ***(ambavyo Mungu aliviumba)*** *vina uungu ndani yake; kwamba ulimwengu wote na vyote vilivyomo ni mungu; kwamba hakuna mungu bali jumla ya vitu vyote, nguvu zote zilizopo ulimwenguni]*

Leo hivi katika taasisi za elimu na katika makanisa kila mahali yanakujia mafundisho ya kiroho ambayo yanadhoofisha imani katika Mungu na katika Neno Lake. Nadharia ya kwamba Mungu ni asili au uwezo unaoenea katika maumbile yote, inapokelewa na wengi wanaodai kuamini Maandiko; lakini, licha ya nadharia hiyo kuvikwa na uzuri, nadharia hii ni udanganyifu ulio hatari zaidi. Inamfunua Mungu isivyo na inafedhehesha ukuu wa enzi na utukufu Wake. Na hakika haielekei kupotosha tu, bali kuwadhalilisha

wanadamu kwa kuwashusha chini kabisa. Giza ndiyo kipengele chake kikuu, tamaa za mwilini ndiyo mazingira yake haswa. Matokeo ya kuikubali ni kutengwa na Mungu. Na kwa asili ya mwanadamu iliyoanguka hii inamaanisha uharibifu *(Msisitizo: imani kwamba Mungu si nafsi ila nguvu inayoenea katika maumbile yote, ambayo Dk. John Harvey Kellogg aliiunga mkono na kuandika kitabu—soma Shuhuda Gombo la 8. Nadharia kwamba Mungu Yuko kihalisi katika kila kitu (literaly). Kwa hivyo ikiwa Mungu yuko automatiki katika kila kitu, hiyo inajumuisha mimi na wewe, na wanadamu wote, hata kama hatujampa Yeye mioyo yetu. Hivyo watu walioikubali nadharia hii waliamini kwamba wanaweza kufanya ngono nje ya ndoa kwa sababu "mungu yu ndani yao)"* [MH 428.2; HU Aya ya 4]

Hali yetu tulipopitia dhambini sio ya kawaida (siyo ya juu juu tu), na hivyo ni lazima nguvu isiyo ya kawaida iturejeshe tena, vinginevyo nguvu nyingine yo yote haitaweza. Kuna nguvu moja tu ambayo inaweza kuvunja mhimili wa dhambi kutoka katika mioyo ya wanadamu, na hiyo ni nguvu ya Mungu katika Yesu Kristo. Ni kwa damu ya Yule Aliyesulubiwa tu ndimo kuna utakaso kutoka kwenye dhambi. Neema Yake pekee yaweza kutuwezesha kupinga na kutiisha mielekeo ya utu wetu wa kale. Nadharia za mambo ya rohoni zinazomhusu Mungu huifanya neema Yake kuwa isiyo na matokeo. Ikiwa Mungu ni nguvu/asili inayoenea kwa maumbile yote, basi akaa ndani ya wanadamu wote; na ili kuufikia utakatifu, mwanadamu anapaswa tu kukuza uwezo ndani yake (panrheism). [MH 428.3; HU Aya ya 5]

Nadharia hizi, zikifuatiwa na hitimisho lazo la kimantiki, hufagilia mbali utajiri wa elimu yote ya Kikristo. Hazizingatii sharti la mwanadamu kupatanishwa na Mungu bali kumfanya mwanadamu kuwa awezaye kujiokoa yeye mwenyewe. Nadharia hizi kuhusu Mungu hulifanya Neno Lake kutokuwa na matokeo yo yote, na wale wanaozikubali nadharia hizi wako katika hatari kubwa ya kuongozwa hatimaye kuitazama Biblia nzima kama habari za kubuniwa. Waweza kuona wema kuwa ni bora kuliko uovu; lakini, wakiwa wamemfungia Mungu nje ya nafasi Yake ya mamlaka anayostahili, wanaweka tegemeo lao juu ya nguvu za kibinadamu, ambazo hizo bila Mungu, ni bure. Dhamiri ya mwanadamu isiyoongozwa haina nguvu halisi ya kupinga na kuushinda uovu. Silaha za ulinzi wa roho huvunjwa. Mwanadamu hana kizuizi dhidi ya dhambi. Pale vizuizi vya Neno la Mungu na Roho Wake vinapokataliwa,

hatujui kiasi gani mtu aweza kuzama kwenye kina kirefu. [MH 428.4; HU Aya ya 6]

“Kila Neno la Mwenyezi Mungu ni safi na limehakikishwa,

Yeye ni ngao kwa wale wanaomtegemea.

Usiongeze Neno katika Maneno Yake,

Asije akakulaumu, ukaonekana kuwa mwongo.” [MH 429.1; HU Aya ya 7]

“Maovu yake yeye mwenyewe yatampata mtu mwovu,

Naye atashikwa kwa kamba za dhambi zake.” Mithali 30:5, 6; 5:22. [MH 429.2; HU Aya ya 8]

Kuchunguza Katika Mafumbo ya Bwana

“Mambo ya siri ni ya Bwana, Mungu wetu; lakini yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele.” Kumbukumbu la Torati 29:29. Ufunuo wa Yeye mwenyewe, ambao Mungu ameutoa katika Neno Lake, ni kwa ajili yetu kujifunza. Ufunuo huu tutafute kuuelewa. Lakini tusivuke mpaka zaidi ya hapa. Akili ya hali ya juu zaidi inaweza kujihenyesha yenyewe mpaka inachoka katika madhanio kuhusiana na uelewa wa asili ya Mungu, lakini juhudi hiyo haitazaa matunda. Tatizo hili sisi wanadamu hatujapewa kulitatua. Hakuna akili ya mwanadamu inayoweza kumwelewa Mungu. Hakuna anayepaswa kujiingiza katika madhanio kuhusu asili Yake Mungu. Kuwa kimya katika eneo hili ni ufasaha. Mwenyezi Mungu Yupo juu ya mijadala ya mwanadamu. [MH 429.3; HU Aya ya 9]

Hata malaika hawakuruhusiwa kushiriki mashauri kati ya Baba na Mwana wakati mpango wa wokovu ulipokuwa ukiwekwa. Na wanadamu pia hawatakiwi kuingilia mafumbo ya Yeye Aliye Juu. Sisi ni wajinga kuhusu Mungu, kwani hatumjui kama watoto wadogo wasivyomjua; lakini, kama watoto wadogo, twaweza kumpenda na kumtii. Badala ya kudhania au kukisia-kisia mambo kuhusiana na asili Yake ama stahiki Zake za kifalme, hebu tuzingatie Maneno Yeye Aliyosema: [MH 429.4; HU Aya ya 10]

“Je, kwa kutafuta-tafuta waweza kumpata Mungu?

Je, waweza kumpata Mwenyezi kwa ukamilifu?

Ni juu kama mbinguni; unaweza kufanya nini?

Kina zaidi kuliko kuzimu; unaweza kujua nini?

Kipimo chake ni kirefu kuliko dunia,

Na ni pana kuliko bahari.”

“Hekima itapatikana wapi?

Je! Wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu? (Je, kwa kutafuta-tafuta waweza kumpata Mungu?) Waweza kuufikilia upeo wa huyo Mwenyezi? Ni juu mno kama mbingu; waweza kufanya nini wewe? Ni wenye kina kuliko kuzimuni; waweza kujua nini wewe? Cheo Chake ni kirefu kuliko dunia, Ni kipana zaidi ya bahari. Ayubu 11:7-9

“Bali hekima itapatikana wapi? Na mahali pa ufahamu ni wapi?

Mwanadamu hajui thamani yake, Wala haionekani katika nchi ya

walio hai. Vilindi vyasema, Haimo ndani yangu; Na bahari yasema,

Haiko kwangu. Haipatikani kwa dhahabu, Wala fedha

haitapimwa iwe thamani yake. Haiwezi kutiwa thamani kwa

dhahabu ya Ofiri, Wala kwa shohamu ya thamani nyingi, wala kwa

yakuti ya samawi. Dhahabu na vioo haviwezi kulinganishwa nayo;

Wala kubadili kwake hakutakuwa kwa vyombo vya dhahabu safi.

Havitatajwa fedhaluka wala bilauri; Naam, kima cha hekima chapita marijani. Yakuti ya rangi ya manjano ya Kushi haitasawazishwa

nayo, Wala haitatiwa kima kwa dhahabu safi. Basi hekima yatoka

wapi? Na mahali pa ufahamu ni wapi? Kwa kuwa imefichwa mbali

na macho ya wote walio hai, Na kusitirika na ndege wa angani.

Uharibifu na Mauti husema, Tumesikia habari zake kwa masikio

yetu. Mungu ndiye aijuaye njia yake, Naye anajua mahali pake.

Maana anatazama hata miisho ya nchi, Na kuona chini ya mbingu

nzima. Apate kuufanyia upepo uzito wake; Naam, anayapima maji

kwa kipimo. Hapo alipoiwekea mvua amri, Na njia kwa umeme wa

radi. Ndipo alipoiona na kuitangaza; Aliithibitisha, naam, na

kuichunguza. Kisha akamwambia mwanadamu, Tazama,

kumcha Bwana ndiyo hekima, Na kujitenga na uovu ndio ufahamu.”

Ayubu 28:12-28; Ayubu 11:7-9; 28:12-28. [MH 430.1; HU Aya ya 11]

Hekima haipatikani kwa kupekua katika maficho ya duniani wala kwa jitihada za kazi bure za kuchunguza siri (mafumbo) zinazohusu nafsi ya Mungu.

Badala yake, inapatikana katika kupokea kwa unyenyekevu ufunuo ambao Yeye Mwenyewe amependezwa kuutoa, na katika kuyapatanisha maisha yetu wanadamu na mapenzi Yake. [MH 431.1; HU Aya ya 12]

Watu wenye akili mahiri zaidi, hawawezi kuelewa siri na mafumbo ya Yehova jinsi yanavyofunuliwa katika maumbile ya asili. Uvuvio wa Mungu katika Maandiko Matakatifu yana maswali mengi ambayo mwanazuoni mwenye akili za juu zaidi hawezi kuyajibu. Maswali haya hayakuulizwa ili tutafute majibu, bali ili kuuvuta usikivu wetu kwenye siri na mafumbo ya kina ya Mungu na kutufundisha kwamba hekima yetu wanadamu ina mipaka; kwamba katika mazingira ya maisha yetu ya kila siku kuna mambo mengi ambayo yanapita uelewa wetu, sisi viumbe wenye ukomo. [MH 431.2; HU Aya ya 13]

Watu wenye kumtilia mashaka Mungu, wanakataa kuamini katika Mungu kwa sababu hawawezi kuelewa uwezo usio na kikomo ambao Yeye anajifunua Mwenyewe kwetu. Lakini Mungu anastahili kutambuliwa Ukuu wake kwa yale ambayo hajatufunulia kuhusu Yeye kama ilivyo kwa yale ambayo yako wazi ambayo amejifunua kuhusu Yeye Mwenyewe, kwa ufahamu wetu mdogo. Katika ufunuo wa Mungu na katika asili, Mungu ametoa siri na mafumbo ili kuiongoza imani yetu. Hii lazima liwe hivyo. Tunaweza kuwa tunachunguza, tunatafuta, tunajifunza na kuuliza kila wakati, lakini bado kuna vitu ambavyo vipo juu sana ya uwezo wetu kuvijua. [MH 431.3; HU Aya ya 14]

“Ni nani aliyeyapima maji kwa konzi ya mkono wake, na kuzikadiri

mbingu kwa shubiri, na kuyashika mavumbi ya dunia katika pishi,

na kuipima milima kwa uzani, na vilima kama kwa mizani? Ni nani

aliyemwongoza roho ya Bwana, na kumfundisha kwa kuwa

mshauri wake? Alifanya shauri na nani, ni nani aliyemwelimisha na

kumfunza njia ya hukumu, na kumfunza maarifa, na kumwonyesha

njia ya fahamu? Tazama, mataifa ni kama tone la maji katika ndoo, huhesabiwa kuwa kama mavumbi membamba katika mizani; tazama, yeye huvinyanyua visiwa kama ni kitu kidogo sana. Lebanoni nayo

hautoshi kwa kuni, wala wanyama wake hawatoshi kwa kafara.

Mataifa yote huwa kama si kitu mbele zake; huhesabiwa kwake

kuwa duni ya si kitu, na ubatili. [MH 431.4; HU Aya ya 15]

Basi, mtamlinganisha Mungu na nani? Au mtamfananisha na mfano wa namna gani? Sanamu fundi mmoja huiyeyusha, na mfua dhahabu huifunika dhahabu, huifulia mikufu ya fedha.Yeye aliye maskini sana hata hawezi kutoa

sadaka ya namna hii, huchagua mti usiooza, hujitafutia fundi mstadi wa kusimamisha sanamu ya kuchonga isiyoweza kutikisika. Je! Hamkujua? Hamkusikia? Hamkuambiwa tokea mwanzo? Hamkufahamu tangu kuwekwa misingi ya dunia? Yeye Ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia, na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi; Yeye Ndiye azitandazaye mbingu kama pazia na kuzikunjua kama hema ya kukaliwa; Ndiye awatanguaye wakuu, na kuwabatilisha waamuzi wa dunia. Naam, hawakupandwa; hawakutiwa katika ardhi kama mbegu; naam, shina lao halikutia mizizi katika ardhi; tena awapuzia tu, wakanyauka, upepo wa kisulisuli wawaondoa kama mabua makavu. Mtanifananisha na nani, basi, nipate kuwa sawa naye? Asema Yeye aliye Mtakatifu. Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi; aletaye nje jeshi lao kwa hesabu; aziita zote kwa majina; kwa ukuu wa uweza Wake, na kwa kuwa Yeye ni hodari kwa nguvu Zake; hapana moja isiyokuwapo mahali pake. [MH 432.1; HU Aya ya 16]

"Mbona unasema, Ee Yakobo, mbona unanena, Ee Israeli, Njia yangu

imefichwa, Bwana asiione, na hukumu yangu imempita Mungu

wangu asiiangalie? Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; akili Zake hazichunguziki." Isaya 40:12-28, [MH 432.2; HU Aya ya 17]

Kutokana na uwakilishi uliotolewa na Roho Mtakatifu kwa manabii Wake, hebu na tujifunze ukuu wa Mungu wetu. Nabii Isaya anaandika hivi: [MH 432.3; HU Aya ya 18]

"Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana

ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na

pindo za vazi Lake zikalijaza hekalu. Juu yake walisimama

maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika

uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.

Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu,

Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa

utukufu Wake. Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya

sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi. [MH 432.4; HU Aya ya 19]

"Ndipo niliposema, Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo

michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa majeshi.”; [MH 433.1; HU Aya ya 20]

“Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu; akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa.” Isaya 6:1-7. [MH 433.2; HU Aya ya 21]

“Hapana hata mmoja aliye kama Wewe, Ee Bwana; Wewe Ndiwe

uliye mkuu, na Jina Lako ni kuu katika uweza. Ni nani asiyekucha Wewe, Ee mfalme wa mataifa? Maana hii ni sifa Yako Wewe; kwa kuwa miongoni mwa wenye hekima wote wa mataifa, na katika hali yao ya enzi yote pia, hapana hata mmoja kama Wewe.”

*Ee Bwana, umenichunguza na kunijua. Wewe wajua kuketi

kwangu na kuondoka kwangu; Umelifahamu wazo langu tokea

mbali. Umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu, Umeelewa

na njia zangu zote.Maana hamna neno ulimini mwangu Usilolijua kabisa, Bwana. Umenizingira nyuma na mbele, Ukaniwekea mkono Wako. Maarifa hayo ni ya ajabu, yanishinda mimi, Hayadirikiki, siwezi

kuyafikia.” “Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu, Akili zake hazina mpaka.” Yeremia 10:6, 7; Zaburi 139:1-6. [MH 433.3; HU Aya ya 22]

“Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu, Akili Zake hazina

mpaka.” Zaburi 147:5. [MH 433.4; HU Aya ya 23]

“Kwa maana njia za mwanadamu zi mbele za macho ya

Bwana, Na mienendo yake yote huitafakari.” Mithali 5:21. [MH 433.5; HU Aya ya 24]

“Yeye hufunua mambo ya fumbo na ya siri; huyajua yaliyo

gizani, na nuru hukaa Naye.” Danieli 2:22. [MH 433.6; HU Aya ya 25]

“Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, akiwapa

Roho Mtakatifu vile vile kama alivyotupa sisi”

“Maana ni nani aliyeijua nia ya Bwana? Au ni nani aliyekuwa

mshauri wake? Au ni nani aliyempa Yeye kitu kwanza, Naye

atalipwa tena? Kwa kuwa vitu vyote vyatoka Kwake, viko kwa uweza Wake, tena vinarejea Kwake. Utukufu una Yeye milele. Amina." Matendo 15:18; Warumi 11:34-36. [MH 433.7; HU Aya ya 26]

Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake, na iwe heshima na utukufu milele na milele. Amina."

"Ambaye Yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una Yeye hata milele. Amina." 1 Timotheo 1:17; 6:16. [MH 434.1; HU Aya ya 27]

"Je! Huo ukuu Wake hautawatia hofu, Na utisho Wake hautawaangukia?"

"Je! Mungu hayuko mbinguni juu? Tena tazama umbali wa nyota, jinsi zilivyo juu!

"Je! Majeshi Yake yahesabika? Ni nani asiyetokewa na mwanga Wake?" Ayubu 13:11, 22:12, 25:3,

"Mungu hunguruma kwa kustaajabisha kwa sauti Yake; Hufanya mambo makuu, ambayo hatuwezi kuelewa nayo.

Kwani huiambia theluji, Anguka juu ya nchi; Na vivyo manyonyota ya mvua, Na hayo maji ya mvua yake kubwa.

Huufunga mkono wa kila binadamu; Ili watu wote aliowaumba wajue.

Hapo wanyama huingia mafichoni, Na kukaa katika mapango yao.

Dhoruba hutoka katika vyumba vyake; Na baridi ghalani mwake.

Barafu huletwa kwa pumzi za Mungu; Na upana wa maji huganda.

Naam, huyatweka mawingu mazito mzigo wa maji; Hulitandika wingu la umeme Wake; Nalo hugeuzwa huku na huku kwa uongozi wake, Ili yafanye yote atakayoyaagiza Juu ya uso wa dunia hii ikaayo watu; kama ni kwa kuonya, au kama ni kwa nchi yake, Au kama ni kwa rehema, ndiye aletaye.

Sikiliza neno hili, Ee Ayubu; Simama kimya, uzifikiri kazi za Mungu za ajabu.

Je! Wajua wewe jinsi Mungu anavyoziagiza, Na kuumulikisha umeme wa wingu lake?

*Je! Wajua jinsi mawingu yalivyowekwa sawasawa, Hizo kazi za ajabu za huyo mkamilifu wa maarifa? Jinsi nguo zako zilivyo na moto, Hapo nchi ituliapo kwa sababu ya upepo wa kusini? Je! Waweza kuzitandaza mbingu pamoja naye, Ambazo zina nguvu kama kioo cha kuyeyushwa?**Utufundishe ni maneno gani tutakayomwambia; Kwa maana hamwezi kuyatengeza kwa sababu ya giza.*

Je! Aambiwe kwamba nataka kunena? Au mtu angetamani kumezwa? Na sasa watu hawawezi kuutazama mwanga ung'aao mbinguni; Lakini upepo ukipita huzitakasa. Kaskazini hutokea umemetufu wa dhahabu; Mungu huvikwa ukuu utishao.

Yeye Mwenyezi hamwezi kumwona; Yeye ni mkuu mwenye uweza; Tena mwenye hukumu, na mwingi wa haki, hataonea.

*Kwa hiyo watu humwogopa; Yeye hawaangalii walio na hekima mioyoni." [MH 434.2; HU Aya ya 28]

"Ni nani aliye kama Bwana, Mungu wetu, akaaye juu, ambaye hujinyenyekeza ili atazame mambo yaliyo mbinguni na duniani!" [MH 435.1; HU Aya ya 29]

"Bwana ana njia yake katika tufani na tufani,

Na mawingu ni mavumbi ya miguu yake.” [MH 435.2; HU Aya ya 30]

“Bwana ni mkuu mwenye kusifiwa sana;

Na ukuu wake hautafutikani.

Kizazi kimoja kitayasifu matendo yako kwa kizazi,

Na kuyasimulia matendo yako makuu.

Nitasema juu ya utukufu wa utukufu wa utukufu wako,

Na kazi zako za ajabu.

Na watu watasema juu ya uwezo wa matendo yako ya kutisha,

nami nitatangaza ukuu wako.

Watatangaza kwa wingi ukumbusho wa

wema wako mkuu,

Nao wataimba juu ya haki yako.... [MH 435.3; HU Aya ya 31]

“Matendo yako yote yatakusifu, Ee Bwana;

Na watakatifu wako watakubariki.

Wataunena utukufu wa ufalme wako,

na kuunena uweza wako;

Kuwajulisha wanadamu matendo yake makuu,

Na fahari ya utukufu wa ufalme wake.

Ufalme wako ni ufalme wa milele,

Na mamlaka yako yadumu vizazi hata vizazi....

Kinywa changu kitazinena sifa za Bwana:

Na wote wenye mwili na walihimidi jina lake takatifu milele na milele.” Ayubu 13:11; 22:12; Ayubu 25:3; 37:5-24, ARV, ukingo; Zaburi 113:5, 6; Nahumu 1:3; Zaburi 145:3-21. [MH 435.4; HU Aya ya 32]

Tunapojifunza zaidi na zaidi jinsi Mungu alivyo, na jinsi sisi wenyewe tulivyo machoni Pake, hakika tutaogopa na kutetemeka mbele Zake. Hebu watu wa siku hizi wachukue onyo kutokana na hatima ya wale ambao katika nyakati za kale walidhania kuwa huru na kile ambacho Mungu alikuwa ametangaza kuwa kitakatifu. Waisraeli walipojitosa kufungua sanduku waliporudi kutoka katika

nchi ya Wafilisti, kuthubutu kwao kulikokuwa hakuna kicho kuliadhibiwa kwa njia isiyo ya kawaida. [MH 435.5; HU Aya ya 33]

Tena, fikiria hukumu iliyompata Uza. Kama ilivyoelezwa katika utawala wa Daudi sanduku lilipokuwa likipelekwa Yerusalemu, Uza alinyoosha mkono wake ili kuliweka imara. Kwa kuwaza kwa dhanio, na kugusa ishara ya uwepo wa Mungu, alipigwa na kifo cha papo hapo. MH 436.1; HU Aya ya 34]

Katika kile kijiti kilichowaka moto, Musa, akiwa hatambui uwepo wa Mungu, alipogeuka kando ili kutazama kwa udadisi maono ya ajabu, amri hii ilitolewa na Mungu: [MH 436.2; HU Aya ya 35]

“Usikaribie hapa: vua viatu vyako miguuni mwako, kwa maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu.... Musa akauficha uso wake; kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu.” Kutoka 3:5, 6. [MH 436.3; HU Aya ya 36]

“Yakobo akatoka Beer-sheba, akaelekea Harani. Akafika mahali fulani, akakaa huko kwa sababu jua lilikuwa limetua; akatwaa baadhi ya mawe ya mahali pale, akayaweka chini ya mto wake, na akalala mahali pale.” [MH 436.4; HU Aya ya 37]

“Akaota ndoto, na tazama, ngazi imesimamishwa juu ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni; na tazama, malaika wa Mungu wakipanda na kushuka juu yake. Na tazama, Bwana akasimama juu yake, akasema, [MH 436:5; HU Aya ya 38]

“Mimi ni Bwana, Mungu wa Ibrahimu, baba yako, na Mungu wa Isaka; nchi hii unayolala nitakupa wewe na uzao wako.... Na tazama, Mimi ni pamoja nawe, Nami nitakulinda, kila mahali uendako, Nami nitakuleta tena katika nchi hii; kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia. [MH 436.6; HU Aya ya 39]

“Yakobo akaamka katika usingizi wake, akasema, Hakika Bwana Yupo mahali hapa; na sikujua. Akaogopa, akasema, Mahali hapa panatisha kama nini! Bila shaka hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo lango la mbinguni.” Mwanzo 28:10-17. [MH 436.7; HU Aya ya 40]

Katika Patakatifu pa hema la kukutania la jangwani na hekalu ambavyo vilikuwa ni alama za kidunia za makao ya Mungu, sehemu ya pili ilikuwa Patakatifu pa Patakatifu pa uwepo Wake. Pazia lililofunika mwonekano wa makerubi kwenye sehemu yake ya kuingilia halikupaswa kuinuliwa kwa mkono wowote isipokuwa mtu

mmoja. Kuinua pazia hilo, na kujiingiza bila idhini katika fumbo takatifu la Patakatifu pa Patakatifu, ilikuwa ni kifo. Kwani juu ya kiti cha Rehema kulikaa utukufu wa Patakatifu (mwanga wa Shekina)—utukufu ambao hakuna mtu angeweza kuutazama akadumu kuishi. Katika siku moja ya mwaka iliyowekwa kwa ajili ya huduma katika Patakatifu pa Patakatifu, kuhani mkuu akiwa anatetemeka aliingia mbele za Mungu, huku mawingu ya uvumba yakifunika utukufu ili kuhani asiuone. Katika nyua zote za hekalu kila sauti ilinyamazishwa. Hakuna makuhani waliohudumu kwenye madhabahu. Kundi la waabudu, wakiwa wameinama kwa kicho kimya-kimya, walitoa maombi yao ya rehema ya Mungu. [MH 437.1; HU Aya ya 41]

"Mambo hayo yaliwapata wao kwa mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya dunia." 1 Wakorintho 10:11. [MH 438.1; HU Aya ya 42]

"Lakini Bwana yumo ndani ya hekalu Lake takatifu; dunia yote na inyamaze kimya mbele Zake." [MH 438.2; HU Aya ya 43]

"Bwana ametamalaki, mataifa wanatetemeka; Ameketi juu ya makerubi, nchi inatikisika. Bwana katika Sayuni ni mkuu, Naye ametukuka juu ya mataifa yote. Na walishukuru jina lake kuu la kuhofiwa; Ndiye mtakatifu." [MH 438.3; HU Aya ya 44]

"Bwana Yu katika hekalu Lake takatifu. Bwana ambaye kiti Chake kiko mbinguni, Macho Yake yanaangalia; Kope Zake zinawajaribu wanadamu."

"Maana ametazama toka patakatifu pake pa juu, Toka mbinguni Bwana ameiangalia nchi"

"Toka mahali Pake aketipo Huwaangalia wote wakaao duniani.

Yeye aiumbaye mioyo yao wote Huzifikiri kazi zao zote”

“*Nchi yote na imwogope Bwana, Wote wakaao

duniani na wamche.” Habakuki 2:20; Zaburi 99:1-3; 11:4; 102:19; 33:14, 15, 8. [MH 438.4; HU Aya ya 45]

Kwa kuchunguza-chunguza mwanadamu hawezi kumjua Mungu. Mtu yeyote asitafute kwa mkono wa kiburi kuinua pazia linaloficha utukufu Wake. “Hukumu Zake hazichunguziki, na njia Zake hazichunguziki.” Warumi 11:33. Ni uthibitisho wa uwepo wa rehema Yake kwamba uweza Wake umefichwa; kwani kufungua pazia linalositiri uwepo wa Mungu hatima yake ni mauti. Hakuna akili ya mwanadamu inayoweza kupenya usiri ambamo Mungu Mwenye Nguvu anakaa na kufanya kazi. Ni yale tu anayoona yanafaa kuyafunua, ndiyo tunaweza kufahamu kuhusu Yeye. Hekima ni lazima itambue mamlaka iliyo kuu kuliko yenyewe. Moyo na akili lazima vimwinamie Mkuu, aitwaye MIMI NIKO. [MH 438.5; HU Aya ya 46]

SURA YA 37

ELIMU YA UONGO NA ELIMU YA KWELI

Mwasisi na Gwiji aliye mjanja mkuu kupita wote katika muungano wa maovu anafanya kazi daima ili kuweka mbali na macho yetu Maneno ya Mungu, na kuleta maoni ya wanadamu. Mipango yake ina umakini haswa katika kututaka sisi wanadamu tusiisikie sauti ya Mungu, ikisema, “Njia ndiyo hii, ifuateni.” Isaya 30:21. Kupitia michakato iliyopotoshwa/iliyopindishwa ya elimu anafanya yote awezayo kuificha nuru ya mbinguni. [MH 439.1; HU Aya ya 1]

Dhana za kukisia-kisia za falsafa na utafiti wa kisayansi ambao ndani yake Mungu hatambuliwi zinazalisha na kuongeza maelfu ya idadi ya watu wenye mashaka (kumtilia Mungu mashaka). Katika mashule ya leo, mahitimisho yale ambayo wanadamu walio wasomi wamefikia kama matokeo ya uchunguzi wao wa kisayansi, yanafundishwa kwa uangalifu na kufafanuliwa kwa upana kwa wanafunzi; na kisha maoni hutolewa waziwazi na watu wengi kwamba ikiwa watu hao wenye elimu wako sahihi kwa mahitimisho yao haya, basi Biblia haiwezi kuwa sahihi. Kwa asili, mashaka huvutia akili ya mwanadamu. Vijana wanaona ndani yake uhuru unaovutia mawazo na ubunifu, na kisha wanadanganyika. Shetani anakuwa ameshinda. Anaipa lishe kila mbegu ya shaka iliyopandwa katika mioyo michanga. Kisha anaifanya ikue na kuzaa matunda, na punde mavuno mengi ya ukafiri yanavunwa. *(Mashaka Ukweli,

Biblia, misingi ya imani, Uwepo wa Mungu, Injili nk- Skepticism) [MH 439.2; HU Aya ya 2]

Kwa sababu moyo wa mwanadamu una mwelekeo wa kutenda maovu, ni hatari sana kupanda mbegu za mashaka katika akili za vijana. Chochote kinachodhoofisha imani katika Mungu huinyang'anya nafsi uwezo wa kuyapinga majaribu. Mashaka yanaondoa ulinzi pekee wa Kweli dhidi ya dhambi. Twahitaji shule ambamo vijana watafundishwa kwamba ukuu wa mtu ni kumheshimu Mungu tu kwa kudhihirisha tabia Yake katika maisha yetu ya kila siku. Kupitia Neno Lake na kazi Zake twahitaji kujifunza kutoka kwa Mungu, ili maisha yetu yaweze kutimiza kusudi Lake. [MH 440.1; HU Aya ya 3]

Waandishi Wakana-Mungu au Makafiri

Ili kupata elimu, wengi wanafikiri ni jambo la muhimu kuyasoma maandishi ya watunzi wa vitabu walio makafiri, kwa sababu kazi hizi zina mawazo mengi ambayo watu hufikiri waandishi hawa makafiri wana vito angavu. Lakini ni nani kweli aliyekuwa mwanzilishi wa vito hivi vya mawazo? Ilikuwa ni Mungu, na Mungu pekee yake. Yeye Ndiye chanzo cha nuru yote. Kwa nini basi tupitie rundo la takataka za uozo wa makosa yaliyomo katika kazi za makafiri kwa ajili tu ya Kweli chache za kiakili, wakati Ukweli wote uko chini ya amri yetu? (Maandiko Matakatifu ndiyo Kweli Yote, na Ukweli Mtupu, Usiokosea, na Usiobahatisha) [MH 440.2; HU Aya ya 4]

Inakuwaje basi, kwamba watu wanaopigana vita na serikali ya Mungu hufikia nafasi ya kumiliki hekima ambayo huionyesha nyakati fulani? Shetani mwenyewe alielimishwa katika nyua za mbinguni, naye ana ujuzi wa mema na mabaya. Yeye huchanganya vitu vya thamani na sumu/uozo, na hii ndiyo inayompa uwezo wa kudanganya watu. Je, kwa sababu Shetani amejivika joho angavu la mbinguni, sisi sasa tumpokee yeye kama malaika wa nuru? Mjaribu ana mawakala wake, walioelimishwa kulingana na mbinu zake, wakiongozwa na roho yake, na kuzoezwa kazi yake. Je, tushirikiane na mawakala wake? Je, tutapokea kazi za mawakala wake kama ndiyo mafunzo muhimu kwetu katika safari yetu ya kujipatia elimu? [MH 440.3; HU Aya ya 5]

Ikiwa wakati na juhudi inayotumiwa katika kutafuta kuyaelewa mawazo angavu ya makafiri ingetolewa kwa kusoma mambo ya thamani ya Neno la Mungu, maelfu ambao sasa wameketi katika giza na uvuli wa mauti wangekuwa wanashangilia katika utukufu wa Nuru ya Uzima. [MH 440.4; HU Aya ya 6]

Hekaya, Mafunzo na Mapokeo ya Kihistoria na Kitheolojia

Kama matayarisho ya kazi ya Kikristo, wengi wanafikiri ni muhimu kupata ujuzi wa kina wa maandishi ya kihistoria na ya kitheolojia. Wanadhani kwamba ujuzi huu utakuwa msaada kwao katika kufundisha injili. Lakini kujifunza kwao kwa bidii maoni ya wanadamu hutoa mwelekeo wa kuidhoofisha tu huduma yao, badala ya kuiimarisha. Ninapoona maktaba zilizosheheni vitabu vingi vya kihistoria na kitheolojia, moyoni mwangu huwa nafikiri, Kwa nini nitumie pesa zangu kwa kile ambacho si chakula au mkate/ugali? Sura ya sita ya Yohana inatuambia mengi zaidi ya yale yanayoweza kupatikana katika maandishi au kazi hizo (au Video). Kristo anasema: “Mimi Ndimi Mkate wa Uzima: yeye ajaye Kwangu hataona njaa kamwe; naye aniaminiye Mimi, hataona kiu kamwe.” “Mimi Ndimi Mkate uzima ulioshuka kutoka mbinguni; mtu ye yote akila mkate huu, ataishi milele.” “Yeye aniaminiye yuna uzima wa milele.” “Maneno hayo ninayowaambia ni roho, tena ni uzima.” Yohana 6:35, 51, 47, 63. [MH 441.1; HU Aya ya 7]

Kuna utafiti na ujifunzaji wa historia ambao haupaswi kuhukumiwa. Historia takatifu ilikuwa mojawapo ya masomo katika shule za manabii. Katika kumbukumbu zilizoandikwa kwenye uvuvio na Mungu, na kushughulika Kwake na mataifa watu wanaweza kuona nyayo za Yehova humo. Nasi leo tunapaswa kuzingatia kushughulika kwa Mungu na mataifa ya dunia. Inatupasa kuona katika historia kutimizwa kwa unabii, kujifunza utendaji wa Mungu katika harakati kuu za Matengenezo, na kuelewa maendeleo ya matukio katika kuyapanga mataifa tayari katika mkao wa pambano la mwisho la mgogoro mkuu. [MH 441.2; HU Aya ya 8]

Utafiti na mafunzo kama hayo utatoa maoni mapana, na ya kina ya maisha. Vitatusaidia kuelewa jambo fulani kuhusu mahusiano na vitegemezi vyake, jinsi tulivyofungwa pamoja kwa namna ya ajabu katika udugu mkubwa wa jamii na mataifa, na ni kwa ukubwa gani basi, ukandamizaji na udhalilishaji wa mwanachama mmoja unavyomaanisha hasara kwa wote. [MH 442.1; HU Aya ya 9]

Lakini historia, kwa kawaida kama inavyosomwa, inahusisha mafanikio aliyojipatia mwanadamu, ushindi wake katika vita, mafanikio yake katika kupata mamlaka, nguvu na ukuu. Wakala wa Mungu katika mambo ya wanadamu umepotezwa machoni pa watu. Wachache tu, ndiyo hujifunza utendaji kazi wa Mungu, na kusudi Lake katika kuinuka na kuanguka kwa mataifa. [MH 442.2; HU Aya ya 10]

Na, kwa kiasi kikubwa, theolojia, kama inavyosomwa na kufundishwa, ni rekodi tu ya makisio na dhana za ubunifu wa mwanadamu, ambayo hutumika tu katika “kutia mashauri giza kwa maneno yasiyo na maarifa.” (Ayubu 38:2-

11). Mara nyingi nia ya kuvikusanya vitabu hivi vingi haipo sana katika matamanio ya kupata chakula cha kiakili na kiroho, bali ni shauku ya kufahamiana na wanafalsafa na wanatheolojia, shauku ya kuwasilisha Ukristo kwa watu kwa maneno ya kisomi na kutoa mapendekezo kwa watu. [MH 442.3; HU Aya ya 11]

Vitabu vyote vilivyoandikwa na wanadamu haviwezi kutumika katika kushughulikia kusudi la maisha matakatifu. “Jifunzeni Kwangu,” anasema Mwalimu Mkuu,” “jitieni nira Yangu, jifunzeni upole na unyenyekevu Wangu.” Kiburi chako cha kiakili hakitakusaidia katika kuwasiliana na roho zinazoangamia kwa kukosa mkate wa uzima. Unapojifunza na kufanya utafiti na vitabu hivi, unakuwa umeviruhusu kuwa mbadala wa masomo ya vitendo ambayo unapaswa kujifunza kutoka kwa Kristo (unaviruhusu kuchukua nafasi ya mafundisho ya vitendo kutoka kwa Mungu Mwenyewe). Matokeo ya utafiti huu kamwe hayawapi watu lishe. Ni sehemu ndogo tu ya utafiti huu, ambao unaiochosha akili ndiyo unatoa yale ambayo yatamsaidia mtu kuwa mtendakazi anayefanikiwa kwa ajili ya kuongoa nafsi za wati. [MH 442.4; HU Aya ya 12]

Mwokozi alikuja “kuhubiri injili kwa maskini.” Luka 4:18. Katika mafundisho Yake alitumia Maneno sahili na alama zilizo wazi kabisa. Na imesemwa kwamba “watu wa kawaida walimsikia kwa furaha.” Marko 12:37. Wale wanaotafuta kufanya kazi Yake Mungu kwa wakati huu wanahitaji jicho lenye kina zaidi katika masomo Yeye Aliyoyatoa. [MH 443.1; HU Aya ya 13]

Maneno ya Mungu aliye hai ndiyo elimu ya juu zaidi kuliko elimu zote duniani na mbinguni. Wale wanaohudumia watu wanahitaji kula mkate wa uzima. Mkate huu, utawapa nguvu za kiroho; kisha watakuwa tayari kuhudumia tabaka zote za watu. [MH 443.2; HU Aya ya 14]

Classics-Vitabu vinavyoitwa Klassik-Vitabu vya Kale na Maarufu

Katika taasisi na vyuo vikuu, maelfu ya vijana hutumia sehemu kubwa ya miaka bora ya maisha yao, kusoma Kigiriki na Kilatini. Na wakati wanajishughulisha na masomo haya, akili na tabia hufinyangwa na hisia mbovu za fasihi, filamu au machapisho ya kipagani*, ambayo kwa ujumla usomaji wake unachukuliwa kuwa sehemu muhimu ya ujifunzaji na uchunguzi wa lugha hizi. (*Vitabu vya Classic-Kwa ufupi, ni vitabu ambavyo vimestahimili mtihani wa wakati kwa sababu watu wameviona ni vizuri na vimependwa sana kusomwa. Hivi vina hadithi au hekaya za kusisimua ambazo zimeundwa kwa ustadi. Kuna idadi ya viungo muhimu vinavyofanya vitabu hiki kuwa maarufu na kuitwa Klasik. Mfano kwenye Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki, hadithi hizi zitakuwa ni visa vya sungura mjanja, au kobe aliyekimbia polepole

na akamshinda Sungura au simba mfalme wa wanyama nk. Kwenye ulimwengu wa Kingereza vitakuwa Harry Porter, hadithi za Esopo, Bibi Tarabushi, Alice in Wonderland, Alibaba na wezi arobaini, na kwa hakika vitabu hivi vingi pamoja na filamu zake, vina mambo ya uchawi au umizimu, la sivyo haviuziki, soma zaidi kuhusu filamu na vitabu vinavyouzika sokoni na Holywood). [MH 443.3; HU Aya ya 15]

Wale wanaojua kusoma vitabu ambavyo vimekuwa maarufu kwa miaka mingi au (Klasik) huhitimisha kwa kusema kwamba “matukio ya kutisha kwenye hekaya za Kigiriki yamejaa ngono chafu kama vile ndugu wa karibu kujamiiana kingono, mauaji au ukatili, na wanadamu kutolewa kafara kwa miungu yenye tamaa ya ngono, kuna tamaa zingine mbaya za mwili, pamoja na kulipiza kisasi.” Ingekuwa bora kabisa, kwa ulimwengu kama elimu inayopatikana kutoka katika vyanzo hivyo ingetupiliwa mbali au kufutwa kabisa kwenye ulimwengu wetu wa leo. Je! mtu aweza kukanyaga makaa ya moto, na nyayo zake zisiungue? Mithali 6:28. “Ni nani awezaye kutoa kitu kilicho safi katika kitu kisicho safi? Hakuna hata mtu mmoja.” Ayubu 14:4. Je, tunaweza basi kutarajia vijana kukuza tabia ya Kikristo huku elimu yao inafinyangwa na mafundisho ya wale wanaopinga kanuni za sheria ya Mungu? [MH 443.4; HU Aya ya 16]

Katika kutupilia mbali vizuizi na kutumbukia katika pumbao la kizembe au maburudisho, upotovu, na uovu, wanafunzi wanaiga yale ambayo huwekwa mbele ya akili zao kutoka katika masomo haya. Hakika kuna wakati fulani watu wanaitwa kwa njia maalumu, nao wanahitaji kuwa na ujuzi wa Kigiriki na Kilatini. Kwa maneno mengine ni lazima fulani wasomee lugha hizi. Lakini huu ujuzi muhimu kwao wa hizi lugha kwaajili ya matumizi ya vitendo kila siku, unaweza kupatikana bila kusoma machapisho haya ya hovyo ambayo yanakosa uadilifu, kwa kuwa na udanganyifu, uchafu na uovu. [MH 444.1; HU Aya ya 17]

Hata hivyo ujuzi wa Kigiriki na Kilatini hauhitajiki kwa wengi. Mafunzo ya lugha zilizokufa* yanapaswa kufanywa kuwa namba mbili kwa masomo yale yanayofundisha matumizi sahihi ya nguvu zote za mwili na akili. Ni upumbavu kwa wanafunzi kutoa muda wake katika kujipatia ujuzi wa lugha mfu (iliyokufa, au isiyozungumzwa na mtu ye yote duniani leo) au hata maarifa ya kitabu cha mada yoyote, kwa kupuuzia mafunzo ya majukumu ya kivitendo katika maisha. [MH 444.2; HU Aya ya 18]

Wanafunzi hubeba nini wanapotoka shuleni? Je, wanakwenda wapi? Je, wafanye nini? Je, wana ujuzi utakaowawezesha kuwafundisha wengine? Je, wameelimishwa kuwa baba na mama wakweli kwenye familia zao siku za usoni? Je, wanaweza kusimama kama kichwa cha familia wakiwa wakufunzi

wenye hekima? Elimu pekee yenye stahiki ya jina hilo ‘elimu’ ni ile inayowaongoza vijana wa kiume na wa kike kuwa kama Kristo (emulate), elimu ambayo inawastahilisha kubeba majukumu ya maisha, na kuwapa sifa ya kusimama kama vichwa vya familia zao. Elimu kama hiyo haipatikani kwa kusoma vitabu maarufu vya kale na vya kipagani (classic books). [MH 444.3; HU Aya ya 19]

Fasihi za Kusisimua, Zikiwemo Video

Machapisho mengi maarufu ya siku hizi yamejawa na hadithi za kusisimua ambazo zinawaelimisha vijana katika uovu na kuwaongoza katika njia ya upotevu. Watoto ambao bado ni wadogo tu kwa miaka, tayari wameshakuwa na ujuzi wa uhalifu. Wanachochewa kutenda maovu kwa hadithi wanazozisoma. Katika fikra za ubunifu, hawa wanafanya yale matendo yaliyoonyeshwa kwenye hekaya (au video) hizo, hadi matamanio yao yanaamshwa kuona ni nini wanaweza kutenda au kuigiza katika uhalifu huo wa kitabuni na kisha kukwepa adhabu wanayostahili. [MH 444.4; HU Aya ya 20]

Kwa akili zenye utendaji hai za watoto na vijana, matukio yanayoonyeshwa katika mafunuo ya kufikirika ya siku zijazo ni hali halisi (hadithi na video wao wanafikiri ni mambo halisi kabisa). Wakati mapinduzi yanapotabiriwa na aina zote za mifano zinaelezewa humo na waandishi hao kwa namna ambayo kuna uvunjaji wa vizuizi vya sheria na kutojizuia nafsi, wengi mioyo yao huidaka roho hii kama ilivyowakilishwa. Nao wanaongozwa kutenda uhalifu ulio mbaya zaidi kuliko video au maandishi ya kusisimua ya makafiri hawa kwa kadri wanavyoweza. Kupitia ushawishi kama huu, jamii inazidi kudhoofika. Mbegu za uasi wa sheria husambazwa na kuambukiza wengine. Hakuna anayepaswa kushtuka kwamba mavuno ya uhalifu ndiyo matokeo ya fasihi hizi maarufu. (watoto hawa wanabobea uovu huu na kisha wanakuwa na ubunifu mkubwa zaidi na kuwapita hawa makafiri na kuovateki/kuwapiku stadi yao!) [MH 444.5; HU Aya ya 21]

Vitabu vya mapenzi, hadithi zisizo na maana za futuhi, na za kusisimua, kwa kiasi kikubwa ni laana tu kwa msomaji. Mwandishi anaweza kudai kufundisha somo la maadili, na katika uandishi wake wote anaweza kuunganisha hisia za kidini; lakini mara nyingi hizo hutumikia tu kuficha upumbavu na ubatili uliosheheni chini. [MH 445.1; HU Aya ya 22]

Ulimwengu umejaa vitabu vilivyojaa makosa ya vinavyovutia mioyo ya watu. Vijana hupokea machapisho haya kama ndiyo Ukweli, kwa yale ambayo Biblia hushutumu kuwa ni uongo, nao huyapenda na kisha hung’ang’ania udanganyifu huu unaomaanisha uharibifu wa roho ya mtu. [MH 445.2; HU Aya ya 23]

Kuna vitabu vya riwaya (novels) ambavyo viliandikwa kwa madhumuni ya kufundisha Ukweli au kufichua uovu fulani mkubwa. Baadhi ya kazi hizi zimetimiza mema. Hata hivyo pia, bado zimetenda madhara makubwa sana. Maandishi yake yana kauli zinazotoa picha kichwani zinazosisimua kwa kupitiliza kwenye fikra za watu na kisha kutoa msururu wa mawazo ambao umejaa hatari, hasa kwa vijana. Matukio yaliyoelezewa humo yanaishi tena na tena katika mawazo yao (hasa video). Usomaji kama huo haufai katika kuinuafaisha akili, na pia huiondolea akili sifa ya kujizoeza mambo yenye mionjo ya kiroho. Inaondoa shauku ya kuipenda Biblia (mtu hatamani kuisoma Biblia baada ya maandishi au video hizi). Mambo ya mbinguni hupata nafasi ndogo tu katika mawazo ya watu. Wakati akili inakaa kwenye mandhari ya uchafu inayoonyeshwa, tamaa za mwili huamshwa, na mwisho wake, ni utendaji tu wa dhambi. [MH 445.3; HU Aya ya 24]

Hata hadithi za uongo au riwaya ambazo hazina pendekezo la uchafu, na ambazo zinaweza kukusudiwa kufundisha kanuni bora, zina madhara yake pia. Hizi zinahamasisha tabia ya kusoma kwa haraka-haraka na kwa juu juu tu kwa ajili ya kufurahia hadithi tu. Kwa njia hiyo inaelekea kwenye kuharibu nguvu ya mawazo yaliyounganishwa na yenye nguvu; na hivyo huifanya roho ya mtu ikose sifa ya kutafakari matatizo makubwa yahusuyo wajibu wa mtu na hatima yake. [MH 445.4; HU Aya ya 25]

Kwa kukuza roho ya kupenda kujifurahisha tu, usomaji wa tamthiliya huumba ladha mbaya kwa majukumu ya kivitendo ya maisha (watoto hawataki kulima, kudeki, kuheshimu watu n.k). Kupitia nguvu za vitabu hivi vinavyosisimua watu, na kuleta uraibu katika kuvisoma, jambo hili limekuwa sababu ya ugonjwa wa akili na mwili mara nyingi. Nyumba nyingi zenye huzuni, ambazo watu wamepuuza majukumu yao, na mahali ambapo watu wamekuwa walemavu maishani, na hata kuishi kama wagonjwa kwenye nyumba za wagonjwa wa maradhi ya akili (mental health institutions), wamekuwa hivyo kupitia tabia ya kusoma riwaya hizo (novels). [MH 446.1; HU Aya ya 26]

Mara nyingi inashauriwa kwamba, ili kuwatoa vijana kutoka katika usomaji wa fasihi za kusisimua au vitabu visivyo na thamani, tunapaswa kuwapa riwaya au vitabu vingine vya uongo ambavyo ni bora zaidi. Hii ni kama kujaribu kumponya mlevi anayekunywa gongo au konyagi au whiski kwa kumpa vileo visivyo kali, kama vile mvinyo, bia, au mbege. Matumizi ya hivi vileo ambavyo si vikali sana, yataendelea tu kukuza hamu ya vichocheo vikali zaidi, hatimaye. Huu ndiyo usalama pekee kwa mlevi, na pia ulinzi pekee wa mtu mwenye kiasi, wote wanapaswa kujizuia kwa kutotumia kabisa kileo cha aina yoyote, hata kama kina asilimia ndogo ya kileo. Kwa mpenda riwaya au

hadithi za uongo, sheria hiyo hiyo ina ukweli na inahusika. Hebu mtu ajizuie kabisa kusoma riwaya ya aina yoyote, na huu ndio usalama wake pekee. [MH 446.2; HU Aya ya 27]

Hadithi au Hekaya za Kufikirika na kutoka kwenye tamaduni mbalimbali

Katika elimu ya watoto na vijana, hekaya za kufikirika, hadithi za mapokeo ya tamaduni mbalimbali, na hadithi za uongo au riwaya, sasa zinapewa nafasi kubwa. Vitabu husika vya aina hii vinatumika mashuleni, na vinapatikana katika nyumba nyingi. Wazazi Wakristo wanawezaje kuwaruhusu watoto wao kutumia vitabu vilivyojaa uongo kiasi hicho? Watoto wanapouliza maana ya hadithi hizi za waandishi makafiri zilizo kinyume na mafundisho ya wazazi wao, wanajibiwa kwamba hadithi hizo si za kweli; lakini jibu hili haliondoi matokeo mabaya ya matumizi yake. Mawazo yaliyotolewa katika vitabu hivi huwapotosha watoto. Vinatoa maoni ya uongo juu ya maisha, na vinazalisha na kupalilia matamanio yasiyo na uhalisi (havina ukweli na watu wanatamani mambo ya kufikirika na siyo maisha ya kivitendo yale muhimu kwa mwanadamu kama mpango wa Mungu ulivyo, mfano kula vyakula feki vya watu wengine, kuigiza nguo na misemo n.k). [MH 446.3; HU Aya ya 28]

Matumizi yaliyoenea ya vitabu hivi wakati huu ni mojawapo ya mbinu za hila za Shetani. Adui huyu anatafuta kugeuza akili za wazee na vijana kutoka kwenye kazi kuu ya kujenga tabia. Anataka watoto na vijana wetu wafagiliwe mbali na madanganyo yanayoangamiza roho na ambayo kwayo anaujaza ulimwengu nayo. Na ndivyo anavyotafuta kukengeusha akili zao kutoka kwenye Neno la Mungu na hatimaye kuwazuia wasipate ujuzi wa zile Kweli ambazo zingekuwa ulinzi wao. [MH 447.1; HU Aya ya 29]

Kamwe vitabu hivi vyenye kupotosha Ukweli, visiwekwe mikononi mwa watoto au vijana. Katika mchakato wenyewe wa kujipatia elimu, hebu watoto wetu wasipate mawazo ambayo yatathibitika kuwa mbegu za dhambi. Ikiwa wale walio na akili zilizokomaa hawakujihusisha huko nyuma na vitabu vya namna hiyo, basi, wao wenyewe wangekuwa salama zaidi, na kielelezo chao na mvuto wao upande ulio sahihi ungefanya kuwalinda vijana dhidi ya vishawishi lisiwe jambo gumu. [MH 447.2; HU Aya ya 30]

Tuna wingi wa vile ambavyo ni halisi, kutoka kwa kile ambacho ni cha Mungu. Wale walio na kiu ya maarifa, hawahitaji kwenda kwenye chemchemi zenye uchafuzi. Bwana asema: [MH 447.3; HU Aya ya 31]

“Tega sikio lako, uyasikie maneno ya wenye hekima,

ukaelekeza moyo wako katika maarifa yangu....

Ili tumaini lako liwe kwa Bwana,

nimekujulisha wewe leo, naam, wewe.

Je! sikukuandikia mambo makuu ya mashauri na maarifa,

Ili nikujulishe hakika ya maneno ya Kweli;

Upate kujibu Maneno ya Kweli kwao wakutumao?"

“Aliweka ushuhuda katika Yakobo,

Na kuweka sheria katika Israeli, [MH 447:4; HU Aya ya 32]

Aliyowaamuru baba zetu,

Ya kwamba wawajulishe watoto wao;

“Nakionyesha kizazi kijacho sifa za Bwana,

Na nguvu Zake, na ajabu Zake alizozifanya.”

“Ili kizazi kijacho kipate kuyajua,

Hata watoto watakaozaliwa;

Ambao watainuka na kuwahubiri watoto wao,

ili wamtumaini Mungu. [MH 448.1; HU Aya ya 33]

“Baraka ya Bwana hutajirisha,

Wala hachanganyi huzuni nayo.” Mithali 22:17-21; Zaburi 78:5, 4, 6, 7; Mithali 10:22. [MH 448.2; HU Aya ya 34]

Mafundisho ya Kristo

Hivi ndivyo Kristo aliwasilisha kanuni za Ukweli katika injili pia. Katika mafundisho Yake tunaweza kunywa kwenye vijito safi, maji yanayotiririka kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Kristo angeweza kuwapa wanadamu ujuzi ambao ungepita ufunuo wowote waliopewa watu huko nyuma wakati alipokuwa akiishi hapa duniani, na kuwafanya watu wanyuma huko wawe na aina ya uvumbuzi mwingine kutoka Kwake. Yeye Angeweza kufunua siri na fumbo baada ya fumbo, na angeweza kuzingatia mafunuo ya ajabu yaliyo na mawazo yenye utendaji hai na ya dhati ya vizazi vilivyofuatana hadi mwisho wa wakati. Lakini asingeweza kutunza muda wa hata dakika moja ya kufundisha sayansi ya wokovu. Muda Wake, uwezo Wake, na maisha Yake vilikuwa vya thamani, Naye alitumia tu hivi, kama njia ya kufanyia kazi wokovu wa roho za wanadamu. Yeye alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea, na asingewa kugeuzwa kutoka katika kusudi Lake. Yeye

hakuruhusu chochote kumkengeusha au kumpindisha kutoka katika kusudi Lake. [MH 448.3; HU Aya ya 35]

Kristo alitoa ujuzi ule ambao tu ungeweza kutumika. Maelekezo na mafunzo Yake kwa watu yalikuwa yameshikamana na mahitaji ya hali yao wenyewe katika maisha ya kivitendo. Udadisi uliowafanya watu waje Kwake na maswali ya kuchunguza maisha Yake kwa umbeya tu, Yeye hakuuhamasisha. Kwa maswali yote ya aina hiyo, Yeye alitoa nafasi ya maombi mazito ya dhati, na kutoa miito muhimu kwa watu. Kwa wale ambao walikuwa na shauku kubwa ya kuchuma mazao kutoka kwenye mti wa ujuzi, Yeye Aliwapa tunda la mti wa uzima. Walikuta kila njia imefungwa isipokuwa ile njia iendayo kwa Mungu. Kila chemchemi ilizibwa, isipokuwa chemchemi ya uzima wa milele ndiyo ilikuwa wazi. [MH 448.4; HU Aya ya 36]

Mwokozi wetu hakumtia moyo mtu yeyote kuhudhuria shule za marabi wa siku Zake, kwa sababu akili zao zingepotoshwa na kurudiwa-rudiwa tena kwa maneno haya, “Watu wanasema,” au, “Imesemwa.” Kwa nini, basi, tukubali maneno yasiyo na uimara ya wanadamu kuwa ndiyo hekima iliyotukuka, wakati hekima kubwa zaidi, iliyo ya uhakika, ipo kwenye mamlaka na ufikiaji wetu? [MH 449.1; HU Aya ya 37]

Yale ambayo nimeona kuhusu mambo ya milele, na yale ambayo nimeona kuhusiana na udhaifu wa ubinadamu, yamevutia sana akili yangu na kuathiri kazi yangu ya maisha. Sioni chochote ambacho mwanadamu anapaswa kusifiwa au kutukuzwa. Sioni sababu ya maoni ya watu wenye hekima ya kilimwengu na wale wanaoitwa watu wakuu, yanapaswa kuaminiwa na kuinuliwa. Je, wale ambao hawana nuru ya Bwana watawezaje basi kuwa na mawazo sahihi ya mipango na njia za Mungu? Ama wanamkana Yeye kabisa na kupuuza uwepo Wake, au wanapiga-piga chenga kuhusiana na nguvu na uwezo Wake, kwa kuzipenda dhana zao zenye ukomo. [MH 449.2; HU Aya ya 38]

Hebu sisi tuchague kufundishwa na Yeye aliyeziumba mbingu na nchi, na Yeye aliyeziweka nyota katika anga katika mpangilio wake na akaliweka jua na mwezi kufanya kazi yake. [MH 449.3; HU Aya ya 39]

Ni jambo sahihi kwa vijana kuhisi kwamba lazima wafikie maendeleo ya juu zaidi ya nguvu zao za akili. Sisi hatuweki mipaka elimu ambayo Mungu hajaiwekea kikomo. Lakini mafanikio yetu hayafai kitu kama hayatatumika kwa ajili ya utukufu wa Mungu na wema kwa wanadamu. [MH 449.4; HU Aya ya 40]

Si vizuri kuijaza akili na masomo ambayo yanahitaji kazi kubwa kuyaweka kwenye vitendo, lakini shughulika na yale ambayo yanatumika katika maisha ya vitendo. Kwa kuwa elimu hiyo isiyohusisha maisha halisi ya mwanadamu,

itakuwa hasara kwa mwanafunzi (Haihusishi kumjua Mungu au kujua stadi za kujikimu maisha, bali ni uhamasisha ukafiri tu). Kwani masomo haya yanapunguza hamu na mwelekeo wa mtu kwa masomo ambayo yangemfaa kwa kumnufaisha, na kumwezesha kutimiza wajibu wake kama mwanadamu. Mafunzo ya vitendo ni ya thamani zaidi ya rundo la kiasi chochote cha nadharia tu (practical training). Haitoshi kuwa tu na maarifa. Ni lazima tuwe na uwezo wa kutumia huo ujuzi ipasavyo. [MH 449.5; HU Aya ya 41]

Wakati, fedha, na masomo ambavyo watu wengi huvitumia kwa ajili ya elimu isiyo na maana kwa kulingana na baraka hizo, watu hawa watu wangeshughulika na muda na mali katika kujipatia elimu ambayo ingewafanya wanaume na wanawake wenye elimu iliyowekwa kwenye vitendo halisi vya maisha na siyo nadharia tu, wangekuwa watu wanaofaa kubeba majukumu ya maisha. Elimu kama hiyo itakuwa ya thamani kubwa zaidi. [MH 450.1; HU Aya ya 42]

Tunachohitaji ni maarifa ambayo yataimarisha akili na roho, na kutufanya kuwa wanaume na wanawake bora. Elimu ya moyo ni muhimu zaidi kuliko kujifunza kutoka kwenye vitabu tu (nadharia). Ni jambo zuri na muhimu, kuwa nayo maarifa yanayohusu ulimwengu tunaoishi; lakini tukiacha umilele nje ya mahesabu yetu, tutafeli kwa jinsi ambayo hatuwezi kuponyeka. [MH 450.2; HU Aya ya 43]

Mwanafunzi anaweza kutumia nguvu zake zote kupata maarifa; lakini asipokuwa na maarifa ya Mungu, na asipozitii sheria zinazoongoza nafsi yake, basi atajiangamiza mwenyewe. Kwa mazoea mabaya, anapoteza uwezo wa kujithamini mwenyewe; anapoteza uwezo wa kutawala nafsi au kujizuia kwa kuwa na kiasi. Hawezi kudadavua mambo yamhusuyo kwa usahihi. Mtu wa namna hii atakuwa ni lofa tu asiyejali maisha yake na mtu asiyekuwa na akili katika kuitendea akili na mwili wake kwa jinsi inayofaa. Kupitia uzembe wake katika kupalilia kanuni zinazofaa, anaharibiwa kwa ulimwengu huu na kisha kwa ulimwengu ujao. [MH 450.3; HU Aya ya 44]

Ikiwa vijana wangeelewa udhaifu wao wenyewe, basi, wangejipatia kutoka kwa Mungu nguvu zao. Wanapotafuta kufundishwa na Bwana, watakuwa watu wenye hekima katika hekima Yake, na maisha yao yatakuwa yanazaa baraka kwa ulimwengu. Lakini wakiziachia akili zao kwenye masomo ya kidunia tu, ambayo ni ya kudhania-dhania au kubahatisha-bahatisha tu, ndivyo kujitenga na Mungu kutakapotokea, nao watakuwa wamepoteza kila kitu kinachorutubisha uhai. [MH 450.4; HU Aya ya 45]

SURA YA 38

UMUHIMU WA KUTAFUTA UJUZI WA KWELI

Twahitaji kuelewa masuala yanayohusika katika mgogoro mkubwa ambao tunahusika kwa uwazi zaidi kuliko tunavyofahamu sasa. Twahitaji kuelewa

kwa ukamilifu zaidi thamani ya kweli au Neno la Mungu na hatari ya kuziruhusu akili zetu kukengeushwa kutoka kwenye hizi Kweli na yule mdanganyifu mkuu. [MH 451.1; HU Aya ya 1]

Thamani isiyo na kikomo ya dhabihu iliyohitajika kwa ajili ya ukombozi wetu inadhihirisha uhalisia kwamba dhambi ni uovu mkuu. Kupitia dhambi mwanadamu mzima amepata wenda wazimu, na nia imeharibikiwa. Dhambi imeshusha nguvu ya roho. Vishawishi kutoka nje hupata mwitikio au kibwagizo ndani ya moyo, na miguu hugeukia uovuni taratibu na kwa njia nyeti ambayo mtu hawezi kugundua au hata kuweza kusimulia. [MH 451.2; HU Aya ya 2]

Kama vile dhabihu iliyotolewa kwa niaba yetu ilivyokamilika, vivyo hivyo urejeshwaji wetu kutoka kwenye unajisi wa dhambi unapaswa kukamilika. Hakuna tendo lolote hai la uovu au lisilo na uadilifu ambalo sheria ya Mungu italitolea udhuru; hakuna udhalimu unaoweza kuepuka hukumu Yake. Maadili ya injili hayakubali kiwango chochote isipokuwa ukamilifu wa tabia ya Kiungu. Maisha ya Kristo yalikuwa utimilifu kamili wa kila agizo la sheria. Yeye Alisema, “Nimezishika amri za Baba Yangu.” Maisha Yake ni mfano wetu; wa utii, huduma au utumishi. Mungu pekee Ndiye anayeweza kuuumba upya moyo.” Kwa maana Mungu Ndiye atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema.” Lakini tunaambiwa, “Utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka.” Yohana 15:10; Wafilipi 2:13, 12. [MH 451.3; HU Aya ya 3]

Kazi Inayohitaji Fikra Zetu

Makosa tuliyoyatenda hayawezi kurekebishwa, wala matengenezo katika mwenendo hayawezi kufanywa na juhudi chache dhaifu, za hapa na pale. Ujenzi wa tabia sio kazi ya siku moja, wala ya mwaka mmoja, bali ya maisha yote. Mapambano ya ushindi juu ya nafsi, kwa ajili ya utakatifu na mbingu, ni vita vya maisha yote. Bila juhudi endelevu na utendaji wa kudumu, hapawezi kuwa na kusonga mbele katika maisha ya Kiungu/utakatifu, hakuna kujipatia taji ya mshindi. [MH 452.1; HU Aya ya 4]

Ushahidi wenye hoja ya nguvu zaidi wa kuanguka kwetu wanadamu kutoka katika hali ya juu ni Ukweli kwamba inagharimu sana kurudi pale alipokuwa kwanza. Njia ya kurudi inaweza kupatikana tu kwa kupigana kwa bidii, sentimita kwa sentimita, saa kwa saa, na ndani ya muda mfupi ambao ni pungufu ya nukta moja, kwa tendo la haraka-haraka, linalofanywa bila ulinzi, au umakini, hilo linaweza kutuweka kwenye nguvu za uovu; lakini inahitajika zaidi ya nukta moja ili kuvunja pingu za uovu na kufikia maisha matakatifu zaidi. Kusudi linaweza kuundwa, na kazi kuanzwa; lakini kutimizwa kwake

kutahitaji kuhenyeka, muda, ustahimilivu, subira, kujikana nafsi na dhabihu. [MH 452.2; HU Aya ya 5]

Hatuwezi kujiruhusu kutenda kutokana na msukumo au mihemko. Hatuwezi kuwa nje ya kituo chetu cha ulinzi hata kwa nukta moja (tujilinde). Tunakabiliwa na majaribu yasiyo na idadi, ni lazima tuyapinge haya kwa uthabiti au tushindwe. Endapo tutafikia mwisho wa maisha yetu na kazi yetu haijafanywa, tutakuwa tumepata hasara ya milele. [MH 452.3; HU Aya ya 6]

Maisha ya mtume Paulo yalikuwa ni migogoro ya daima na nafsi. Alisema, “Mimi hufa kila siku.” 1 Wakorintho 15:31. Mapenzi yake na matamanio yake kila siku yalipingana na wajibu na mapenzi ya Mungu. Badala ya kufuata mielekeo, yeye alifanya mapenzi ya Mungu, haikujalisha ukali uliotumika katika kusulubisha asili yake. [MH 452.4; HU Aya ya 7]

Mwishoni mwa maisha yake ya mapambano, alipotazama nyuma na kuona mapambano na ushindi alioupata, aliweza kusema, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; tangu sasa nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, Mwamuzi Mwenye haki, atanipa siku ile.” 2 Timotheo 4:7, 8. [MH 453.1; HU Aya ya 8]

Maisha ya Kikristo ni pambano na gwaride. Katika vita hivi hakuna kuachiwa huru; juhudi lazima ziwe endelevu na za kudumu. Ni kwa jitihada zisizokoma ndipo tunadumisha ushindi dhidi ya majaribu ya Shetani. Uadilifu wa Kikristo lazima usakwe kwa nishati isiyoweza kupingwa na kudumishwa kwa uthabiti wenye wa kusudi/lengo. [MH 453.2; HU Aya ya 9]

Hakuna mtu atakayechukuliwa juu bila juhudi kali, na zenye kudumu kwa niaba yake mwenyewe. Wote lazima wajihusishe katika hii vita peke yao; hakuna mtu mwingine anayeweza kupigana vita kwa niaba ya mtu mwingine. Tuna wajibu binafsi katika masuala ya mapambano; ingawa Nuhu, Ayubu, na Danieli walikuwa katika nchi hawakuweza kumwokoa mwana wala binti kwa uadilifu wao. [MH 453.3; HU Aya ya 10]

Sayansi Tunayopaswa kuwa na Weledi Nayo

Kuna sayansi ya Ukristo inayopaswa kueleweka kwa kina na kuwekwa kwenye vitendo kwa weledi—sayansi iliyo ya kina zaidi, pana, na ya juu zaidi kuliko sayansi yoyote ya wanadamu, kama vile mbingu zilivyo juu zaidi kuliko dunia. Nia inapaswa kunidhamishwa, kuelimishwa, kuzoezwa na kufunzwa; kwa maana tunapaswa kumfanyia Mungu huduma kwa njia zisizopatana na mwelekeo tuliozaliwa nao. Ni Lazima tuishinde mielekeo tuliyoirithi, tuliyoikuza na tuliyoipalilia katika uovu. Mara nyingi elimu na mafunzo tuliyopata katika maisha yote lazima vitupiliwe mbali, ili mtu aweze kuwa

mwanafunzi katika shule ya Kristo. Mioyo yetu lazima ielimishwe kuwa imara katika Mungu. Tunapaswa kutengeneza mazoea ya kufikiri yale ambayo yatatuwezesha kushinda majaribu. Lazima tujifunze kutazama juu daima. Kanuni za Neno la Mungu—kanuni ambazo ziko juu kama mbingu, na zinazozunguka dira ya umilele—tunapaswa kuelewa jinsi zinavyohusika katika maisha yetu ya kila siku. Kila tendo, kila neno, kila wazo, linapaswa kupatana na kanuni hizi. Yote haya lazima yaletwe katika upatanifu na Kristo, na kusalimishwa kwa Kristo. [MH 453.4; HU Aya ya 11]

Neema za thamani za Roho Mtakatifu haziendelezwi au kukuzwa kwa dakika moja. Ujasiri, ustahimilivu, upole, imani, kumtegemea Mungu pasipo kuterereka katika nguvu ya Mungu inayookoa, hizi hupatikana kwa uzoefu wa miaka kadhaa. Kwa maisha ya juhudi takatifu na kushikamana kwa uthabiti na haki, watoto wa Mungu wanapaswa kutia muhuri hatima yao. [MH 454.1; HU Aya ya 12]

Hakuna Wakati wa Kupoteza

Hatuna muda wa kupoteza. Hatujui ni karibu kiasi gani, mlango wetu wa rehema unaweza kufungwa. Kwa muda mrefu, tumekuwa na maisha mafupi tu hapa duniani, nasi hatujui ni wakati gani mshale wa mauti utaichoma mioyo yetu. Hatujui ni muda gani tunaweza kuitwa kuuacha ulimwengu huu na matamanio au maslahi yake yote. Umilele umejifunua mbele yetu. Pazia linakaribia kufunguliwa. Ni miaka michache tu imebakia kwa kila mtu ambaye sasa yumo katika hesabu ya wale walio hai, atasikia tangazo lenye mamlaka likitolewa: [MH 454.2; HU Aya ya 13]

“Mwenye kushudulumu na azidi kudhulumu; ... na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa.” Ufunuo 22:11. [MH 454.3; HU Aya ya 14]

Je, tumejiandaa kweli? Je, tumefahamiana na Mungu, Gavana wa mbinguni, Mtoaji wa Sheria, na Yesu Kristo ambaye Mungu alimtuma ulimwenguni akiwa mwakilishi Wake? Wakati kazi yetu katika maisha haya ya duniani itakapokamilika, je, tutaweza kusema, kama alivyofanya Kristo Mfano wetu: [MH 454.4; HU Aya ya 15]

“Nimekutukuza duniani, nimemaliza kazi uliyonipa niifanye.... Nimelidhihirisha Jina Lako”? Yohana 17:4-6. [MH 454.5; HU Aya ya 16]

Malaika wa Mungu wanatafuta kutuvutia tutoke kwenye kujifikiria sisi wenyewe tu, na kisha tutoke kwenye vitu vya kidunia. Hebu hawa malaika wasifanye kazi bure. [MH 454.6; HU Aya ya 17]

Akili ambazo zimejidhabihu kwenye mawazo legelege, yasiyo na mashiko zinahitaji kubadilika. “Vifungeni viuno vya nia zenu, muwe na kiasi, mkitumainia kabisa ile neema mtakayoletewa katika ufunuo Wake Yesu Kristo; kama watoto wa kutii, msijifananishe na tamaa zenu za kwanza za ujinga wenu; bali kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa sababu imeandikwa, Iweni watakatifu; kwa maana Mimi ni mtakatifu.” 1 Petro 1:13-16. [MH 455.1; HU Aya ya 18]

Mawazo lazima yaelekezwe kwa Mungu, na yakite Kwake. Ni lazima tuweke juhudi za dhati kushinda mielekeo yenye uovu wa moyo wa asili au mtu wa kale. Juhudi zetu katika kujikana nafsi kwetu na ustahimilivu, lazima vilingane kabisa na ile thamani isiyo na kikomo ya kitu ambacho tunakifuata au kukiwinda. Ni kwa kushinda tu kama Kristo alivyoshinda ndipo tutajipatia taji ya ushindi na uzima. [MH 455.2; HU Aya ya 19]

Haja ya Kujinyima

Hatari kubwa ya mwanadamu ni kujidanganya mwenyewe, kuendekeza dhana ya kujitosheleza mwenyewe, na hivyo kujitenga na Mungu, Chanzo cha nguvu zake. Mielekeo yetu ya asili, isiporekebishwa na Roho Mtakatifu wa Mungu, ina mbegu za kifo cha maadili ndani yake. Pasipokuwa katika uhusiano mkubwa na Mungu, hatutaweza kupinga matokeo yasiyo matakatifu ya kujifurahisha wenyewe kwa anasa, uovu, kujipenda wenyewe, na majaribu ya kutenda dhambi. [MH 455.3; HU Aya ya 20]

Ili kupokea msaada kutoka kwa Kristo, ni lazima tutambue hitaji letu. Lazima tuwe na ujuzi wa kweli kuhusu nafsi zetu wenyewe. Ni yule tu anayejielewa mwenyewe kuwa ni mwenye dhambi, ndiye ambaye Kristo anaweza kumwokoa. Ni pale tu tunapoona hali yetu ya kutoweza kabisa na kuacha kujiamini wenyewe, ndipo tutakaposhikilia nguvu za Mungu. [MH 455.4; HU Aya ya 21]

Sio tu mwanzoni mwa maisha ya Kikristo ndiyo huku kujikana nafsi kunapaswa kufanywa. Katika kila hatua tunayopiga kwenda mbele kuelekea mbinguni inatupasa kuirudia hatua hiyo upya tena. Matendo yetu yote mema yanategemea nguvu iliyo nje ya sisi wenyewe; kwa hiyo twahitajika kuendelea kuufikia moyo wa Mungu, kuendelea kuungama dhambi kwa dhati na bidii na kunyenyekesha roho zetu mbele Zake. Hatari zinatuzunguka pande zote; nasi tuko salama pale tu tunapohisi udhaifu wetu na kumng’ang’ania Mkombozi wetu na mshiko wenye mng’ang’anio wa imani kwa Mwokozi wetu mkuu. [MH 455.5; HU Aya ya 22]

Kristo Chemchemi ya Maarifa ya Kweli

Ni lazima tugeuze akili zetu mbali na mada zingine elfu moja zinazovutia umakini wetu. Kuna mambo ambayo yanatafuna muda wetu na kuamsha uchunguzi na maswali akilini mwetu, ila yanaishia kwenye sifuri tu. Masilahi ya juu zaidi yanahitaji usikivu wetu wa karibu na nishati ambayo mara nyingi tunaitoa kwenye vitu visivyokuwa na maana. [MH 456.1; HU Aya ya 23]

Kukubali nadharia mpya yenyewe tu kama ilivyo, haileti maisha mapya kwenye roho zetu. Hata ile kufahamiana na mambo yaliyo halisi au yenye uhakika na nadharia muhimu yenyewe tu kama ilivyo haifai kitu isipokuwa itawekwa kwenye utendaji halisi (vitendo). Twahitaji kutambua wajibu wetu wa kuzipa nafsi zetu chakula ambacho kitarutubisha kwa lishe na kuchochea maisha ya kiroho. [MH 456.2; HU Aya ya 24]

“Mwanangu, kama ukiyakubali maneno yangu, Na kuyaweka akiba maagizo yangu; Hata ukatega sikio lako kusikia hekima, Ukauelekeza moyo wako upate kufahamu; Naam, ukiita busara, Na kupaza sauti yako upate ufahamu; Ukiutafuta kama fedha, Na kuutafutia kama hazina iliyositirika; Ndipo utakapofahamu kumcha Bwana, Na kupata kumjua Mungu.Kwa kuwa Bwana huwapa watu hekima; Kinywani Mwake hutoka maarifa na ufahamu;Huwawekea wanyofu akiba ya hekima kamili; Yeye ni ngao kwao waendao kwa ukamilifu; Apate kuyalinda mapito ya hukumu, Na kuhifadhi njia ya watakatifu wake. Ndipo utakapofahamu haki na hukumu, Na adili, na kila njia njema. Maana hekima itaingia moyoni mwako, Na maarifa yatakupendeza nafsi yako; Busara itakulinda; Ufahamu utakuhifadhi.Yeye ni mti wa uzima kwao wamshikao sana; Ana heri kila mtu ashikamanaye Naye.” Mithali 2:2-11; 3:18. [MH 456.3; HU Aya ya 25]

Swali la sisi kujifunza ni, “Ukweli ni nini—Ukweli unaopaswa kuthaminiwa, kupendwa, kuheshimiwa, na kutiiwa?” Wadau/wakereketwa wa sayansi wameshindwa na wamekatishwa tamaa katika jitihada zao za kumjua Mungu. Wanachohitaji kuuliza kwa wakati huu ni, “Ni Ukweli gani utakaotuwezesha kupata wokovu wa roho zetu?” [MH 456.4; HU Aya ya 26]

“Mnaonaje juu ya Kristo?”—hili ndilo swali muhimu sana. Je, unampokea kama Mwokozi wako binafsi? Wote wanaompokea, Yeye huwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu. [MH 457.1; HU Aya ya 27]

Kristo alimfunua Mungu kwa wanafunzi Wake kwa namna ambayo kazi ya pekee ilifanyika mioyoni mwao, kama ile Yeye anayotamani kuifanya mioyoni mwetu leo. Kuna wengi ambao, kwa kukaa sana juu ya nadharia, wamepoteza kuona nguvu hai ya mfano wa Mwokozi. Kristo kama Mtendakazi anayejikana nafsi, anayejinyima na mnyenyekevu amepotea machoni mwao. Wanachohitaji ni kumtazama Yesu. Kila siku twahitaji ufunuo mpya wa uwepo

Wake. Twahitaji kufuata kwa ukaribu zaidi mfano Wake wa kujinyima na kujitoa Kwake kama dhabihu. [MH 457.2; HU Aya ya 28]

Twahitaji uzoefu ambao Paulo alikuwa nao alipoandika: “Nimesulibiwa pamoja na Kristo; wala si mimi, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi Yake kwa ajili yangu.” Wagalatia 2:20. [MH 457.3; HU Aya ya 29]

Maarifa ya Mungu na ya Yesu Kristo yanaoonekana katika tabia yanapaswa kuinuliwa juu ya kila kitu kingine kinachoheshimiwa duniani au mbinguni. Ni elimu ya juu kupita elimu zote. Ni ufunguo unaofungua malango ya jiji la mbinguni. Ni kusudi la Mungu kwamba wote wanaomvaa Kristo wataumiliki ujuzi huu. [MH 457.4; HU Aya ya 30]

SURA YA 39

MAARIFA YANAYOPATIKANA KUPOKELEWA KUPITIA NENO LA MUNGU

Biblia nzima ni ufunuo wa utukufu wa Mungu katika Kristo. Kuipokea, kuiamini, na kuitii Biblia ndiyo nyenzo kuu katika mabadiliko ya tabia kwa kila mwanadamu. Biblia ndiyo kichocheo kikuu, na msukumo unaobidisha, ambao huhuisha nguvu za kimwili, kiakili, na kiroho, na kuelekeza maisha kwenye njia sahihi. [MH 458.1; HU Aya ya 1]

Sababu inayopelekea vijana, na hata wale walio katika umri wa ukomavu na kujitambua, kuongozwa kwa urahisi sana katika majaribu na dhambi, ni kwamba hawazielekezi akili zao na kulitafakari inavyopaswa. Wanakosa nguvu ya nia iliyo thabiti, imara na iliyoazimiwa, na ambayo inaonekana kwa udhahiri katika maisha na tabia, ni matokeo ya kupuuzia maagizo matakatifu ya Neno la Mungu. Hawazielekezi akili zao kwa dhati na bidii kwa yale ambayo yangevuvia mawazo safi, na matakatifu na kuyageuza kutoka kwa yale ambayo ni machafu na yasiyo ya kweli au halisi. Kuna wachache wanaochagua fungu lililo jema zaidi, hawa ni wale wanaoketi miguuni pa Yesu, kama alivyofanya Mariamu, ili kujifunza kutoka kwa Mwalimu wa mbinguni/Kiungu. Ni wachache wanaothamini Maneno Yake mioyoni mwao na kuyatenda maishani mwao. [MH 458.2; HU Aya ya 2]

Kweli za Biblia, zikipokelewa, zitaiinua akili na nafsi. Ikiwa Neno la Mungu lingekubaliwa, lingependwa na kuthaminiwa jinsi inavyopaswa, vijana kwa wazee wangekuwa na unyoofu wa maadili na mawazo, na nguvu ya kanuni, ambayo ingewawezesha kuyapinga majaribu. [MH 459.1; HU Aya ya 3]

Hebu watu wafundishe na kuandika mambo ya thamani yaliyo katika Maandiko Matakatifu. Hebu fikra, karama, talanta, tasnia, na mazoezi yenye umakini ya nguvu za ubongo, vishughulishwe katika kujifunza mawazo ya Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Usijifunze au hata kusoma falsafa za dhana za ubunifu wa mwanadamu, bali soma falsafa ya Yeye aliye Kweli. Hakuna fasihi au machapisho mengine yoyote, ambayo yanaweza kulinganishwa na Maandiko Matakatifu kwa thamani. [MH 459.2; HU Aya ya 4]

Akili yenye udunia haifurahii kutafuta muda wa kulitafakari Neno la Mungu; lakini ubongo na nia vilivyofanywa upya na Roho Mtakatifu, uzuri wa Mungu na nuru ya mbinguni huangaza na kung'aa kutoka kwenye kurasa zake takatifu. Kile ambacho kwa akili ya dunia kilikuwa ni jangwa tupu, kwa akili yenye mionjo ya kiroho kinakuwa ardhi yenye vijito hai. [MH 460.1; HU Aya ya 5]

Maarifa ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika Neno Lake ndiyo maarifa tu yanayopaswa kutolewa kuwapatia watoto wetu. Tangu pale wanapoanza kupata fununu ya uelewa wa mambo kwenye akili zao, watoto wanapaswa kufahamishwa na kupewa utambuzi/uelewa wa Jina na maisha ya Yesu. Masomo yao ya kwanza yanapaswa kuwafundisha kwamba Mungu ni Baba yao. Funzo lao la kwanza linapaswa kuwa utii wenye upendo. Kwa kicho na upole, hebu Neno la Mungu lisomwe na kurudiwa kwao katika vipengele vinavyoendana na uelewa wao na kurekebishwa kulingana ili kuamsha shauku yao. Na zaidi ya yote, waache watoto wajifunze juu ya upendo wa Mungu uliofunuliwa katika Kristo, na somo Lake kuu: [MH 460.2; HU Aya ya 6]

“Ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa nasi kupendana sisi kwa sisi.” 1 Yohana 4:11. [MH 460.3; HU Aya ya 7]

Hebu vijana walifanye Neno la Mungu kuwa chakula cha akili na roho zao. Hebu msalaba wa Kristo ufanywe kuwa sayansi ya elimu yote, kitovu cha mafundisho na kufundishia masomo yote. Hebu masomo ya msalaba yaletwe katika uzoefu wa kila siku na katika maisha ya utendaji/vitendo vya kila siku. Hivyo Mwokozi atakuwa mwenzi na rafiki wa kila siku kwa vijana . Kila fikra itatekwa nyara ili ipate kumtii Kristo. Pamoja na mtume Paulo wataweza kusema: [MH 460.4; HU Aya ya 8]

“Lakini mimi hashanisione fahari juu ya kitu chochote isipokuwa msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulubishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu.” Wagalatia 6:14. [MH 460.5; HU Aya ya 9]

Hivyo kwa njia ya imani wanafika mahali pa kumjua Mungu kwa maarifa yenye vitendo. Wamejithibitishia wenyewe Ukweli wa Neno Lake Mungu, Ukweli wa ahadi Zake. Wameonja, wameona na kujua ya kuwa Bwana ni mwema. [MH 461.1; HU Aya ya 10]

Yohana mwanafunzi mpendwa alikuwa na ujuzi uliopatikana kupitia uzoefu wake mwenyewe. Huyu Aliweza kushuhudia Maneno haya: [MH 461.2; HU Aya ya 11]

“Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu kulishika, kwa habari ya Neno la uzima; (kwa maana uzima huo ulidhihirika, nasi tumeuona, na twashuhudia na kuwaonyesha ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, na ukadhihirishwa kwetu;) hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri ninyi; ili ninyi nanyi mpate kushirikiana nasi; na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwanawe Yesu Kristo.” 1 Yohana 1:1-3. [MH 461.3; HU Aya ya 12]

Hivyo kila mtu anaweza, kupitia uzoefu wake mwenyewe, “kutia muhuri wake hivi, ya kwamba Mungu ni Kweli.” Yohana 3:33, Anaweza kushuhudia yale ambayo yeye mwenyewe ameyaona na kuyasikia na kuyahisi, kuyajua, kuhusu uweza na nguvu za Kristo. Anaweza kushuhudia: [MH 461.4; HU Aya ya 13]

“Nilihitaji msaada, na niliupata kwa Yesu. Kila hitaji langu lilitimizwa, njaa ya nafsi yangu ilishibishwa; Biblia kwangu ni ufunuo wa Kristo. Ninamwamini Yesu kwa sababu Yeye kwangu ni Mungu na Mwokozi (Mwokozi wa Kiungu). Ninaamini Biblia kwa sababu nimegundua kuwa ni sauti ya Mungu kwa nafsi yangu.” [MH 461.5; HU Aya ya 14]

Yule ambaye amepata maarifa ya Mungu na Neno Lake kupitia uzoefu wake binafsi, ameandaliwa kujihusisha na masomo ya sayansi ya asili (hawezi kujichanganya mwenyewe au kuchanganywa na watu). Kuhusu Kristo imeandikwa, “Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima; na huo uzima ulikuwa nuru ya watu.” Yohana 1:4. Kabla ya kuingia dhambini, Adamu na Hawa wakiwa katika bustani ya Edeni, walikuwa wamezungukwa na mwanga ulio wazi na mzuri, nuru ya Mungu. Nuru hii ilimulika kila kitu walichokikaribia. Hakukuwa na kitu chochote kilichoficha mtazamo au utambuzi wa tabia au kazi za Mungu. Lakini walipokubali kujisalimisha kwa mjaribu, nuru hiyo ilitoweka kwao. Kwa kupoteza mavazi ya utakatifu, walipoteza nuru iliyokuwa imeimulikia asili (ili waweze kuona vizuri Uumbaji, yaani mimea, wanyama, watu, milima, mabonde, bahari nk katika mtazamo wake halisi). Hivyo hawakuweza tena kuisoma asili ipasavyo. Hawakuweza kutambua tabia ya Mungu katika kazi Zake. Ndivyo ilivyo hata leo kwa mwanadamu, yeye hawezi mwenyewe kusoma kwa usahihi mafundisho au masomo ya asili (nature lessons). Isipokuwa kwa kuongozwa na hekima ya Mungu, watu huinua asili na sheria za asili juu ya Mungu wa asili. Hii ndiyo sababu mawazo ya kibinadamu peke yake kuhusu sayansi mara nyingi yanapingana na mafundisho ya Neno la Mungu. Lakini kwa wale wanaopokea nuru ya maisha ya Kristo, asili inaangazwa tena. Katika nuru inayoangaza kutoka msalabani, tunaweza kutafsiri na kufafanua kwa usahihi mafundisho ya asili. [MH 461.6; HU Aya ya 15]

Yeye aliye na maarifa ya Mungu na Neno Lake, kupitia uzoefu binafsi, ana imani iliyotulia ndani ya Uungu wa Maandiko Matakatifu. Amethibitisha kwamba Neno la Mungu ni Kweli, na anajua kwamba Kweli haiwezi kujipinga yenyewe. Yeye haipimi Biblia kwa mawazo ya wanadamu ya sayansi; bali anayaleta haya mawazo ya mwanadamu kwa kuyapima katika kipimo cha kiwango sahihi kisichokosea. Anajua kwamba katika sayansi ya Kweli hakuwezi kuwa na chochote kile ambacho ni kinyume na mafundisho ya Neno la Mungu;

kwa kuwa vyote viwili, yaani asili (nature) au Uumbaji wa Mungu na Maandiko, vina Mmiliki mmoja Yule-Yule, ufahamu sahihi wa hivi viwili utathibitisha uelewa kuwa vyote vinapatana kabisa kwani Mwasisi Wake ni mmoja. Chochote katika kile kinachoitwa mafundisho ya kisayansi kinachopingana na ushuhuda wa Neno la Mungu ni ubunifu tu, au kazi ya makisio ya mwanadamu (guesswork). [MH 462.1; HU Aya ya 16]

Kwa mwanafunzi kama huyo, utafiti wa kisayansi utafungua nyanja kubwa za mawazo na habari. Na kadri anavyotafakari mambo ya asili, mtazamo mpya wa Ukweli humjia. Kitabu cha asili (book of nature) na Neno lililo kwenye Maandishi (The Bible), vinaangaziana nuru kuhusiana kila mmoja (asili hutoa mwanga kuhusu Maandiko, na Maandiko yanatoa mwanga kuhusu maumbile). Vyote viwili vinamfanya mwanadamu amfahamu Mungu vizuri zaidi kwa kumfundisha tabia Yake na sheria anazofanya kazi kwazo. [MH 462.2; HU Aya ya 17]

Uzoefu wa mwandishi wa-Zaburi ni uzoefu ambao wote wanaweza kuupata kwa kupokea Neno la Mungu kupitia asili na kupitia ufunuo. Anasema hivi: [MH 462.3; HU Aya ya 18]

“Wewe, Bwana, umenifurahisha kwa kazi Yako;

nitashangilia kwa kazi ya mikono Yako.

“Ee Bwana, rehema Zako zi juu mbinguni;

Na uaminifu Wako unafika mawinguni.

Haki Yako ni kama milima mikubwa;

Hukumu Zako ni za kina kirefu.... [MH 463.1; HU Aya ya 19]

“Ee Mungu, jinsi zilivyo bora fadhili Zako!

“Wanadamu hujikinga chini ya

uvuli wa mbawa Zako....

Nawe utawanywesha mto wa

furaha Zako.

Maana Kwako iko chemchemi ya uzima;

Katika nuru Yako tutaona nuru.” [MH 463.2; HU Aya ya 20]

“Heri walio wanyofu katika njia,

Waendao katika sheria ya BWANA.

Heri wazishikao shuhuda Zake,

wamtafutao kwa moyo wote.” [MH 463.3; HU Aya ya 21]

“Kwa jinsi gani kijana aisafishe njia Yake?

Ni kwa kutii, akilifuana Neno Lako.”

“Nimeichagua njia ya uaminifu;

nimeweka amri Zako mbele yangu.”

Moyoni mwangu nimeliweka Neno Lako,

Nisije nikakutenda dhambi.

“Nami nitakwenda katika uhuru;

Maana nimeyatafuta mausia Yako.” [MH 463.4; HU Aya ya 22]

“Ufumbue macho yangu niyatazame

Maajabu yatokayo katika sheria Yako.”

“Shuhuda Zako nazo ni furaha yangu,

Na washauri wangu.”

“Sheria ya kinywa Chako ni bora kwangu,

Kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.” [MH 463.5; HU Aya ya 23]

“Sheria yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa.”

“Shuhuda Zako ni za ajabu;

Kwa hiyo nafsi yangu inawalinda.”

“Sheria Zako zimekuwa nyimbo zangu

katika nyumba ya hija yangu.” [MH 463.6; HU Aya ya 2; HU Aya ya 24]

“Neno Lako ni safi sana;

Kwa hiyo mtumishi Wako analipenda.” [MH 463.7; HU Aya ya 25]

“Jumla ya Neno Lako ni Kweli;

Na kila hukumu Yako ya haki ni ya milele.” [MH 464.1; HU Aya ya 26]

“Nafsi yangu na iishi, itakusifu;

Na hukumu Zako zinisaidie.”

“Wana amani nyingi waipendao sheria Yako;

wala hawana la kuwakwaza. [MH 464.2; HU Aya ya 27]

“Ee BWANA, nimeutumainia wokovu Wako,

nami nimeyafanya maagizo Yako.

Nafsi yangu imezishika shuhuda Zako;

Na nimezipenda sana.” [MH 464.3; HU Aya ya 28]

“Kufafanusha kwa Maneno Yako kwatia nuru;

Huwapa ufahamu wajinga.”

“Maagizo Yako hunitia hekima kuliko adui zangu; Kwa maana ninayo siku zote.

Nina ufahamu zaidi kuliko waalimu wangu wote;

Maana shuhuda Zako ndizo kutafakari kwangu.

Ninao ufahamu kuliko wazee,

Kwa kuwa nimeyashika mausia Yako.”

“Kwa mausia Yako najipatia ufahamu;

Kwa hiyo naichukia kila njia ya uongo.”

“Shuhuda Zako nimezifanya kuwa urithi milele;

Kwa maana hizo ndizo furaha ya moyo wangu.” Zaburi 92:4; 36:5-7; 36:7-9, ARV; 119:1, 2, 9, 30, ARV, ukingo; 119:11, 45, 18, 24, 72, 97, 129, 54, 140, 160, 175, 165-167, 130, 98-100, 104, 4, 6 ARV1; HU Aya ya 29]

Ufunuo Wazi Zaidi wa Mungu

Ni fursa yetu kufika juu na bado juu zaidi ili kupata ufunuo wazi zaidi wa tabia ya Mungu. Musa alipoomba, “Nakusihi, unionyeshe utukufu Wako,” Bwana hakumkemea, bali alilikubali ombi Lake. Mungu alimwambia mtumishi Wake, “Nitapitisha wema Wangu wote mbele Yako, Nami nitalitangaza Jina la BWANA mbele yako.” Kutoka 33:18, 19. [MH 464.5; HU Aya ya 30]

Dhambi, ndiyo itiayo giza akili zetu na kuhafifisha mitazamo na utambuzi ya bongo zetu. Dhambi inaposafishwa na kuondolewa kabisa mioyoni mwetu, nuru ya ujuzi wa utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo, ikimulika ndani ya Neno Lake na kuakisiwa kutoka katika uso wa asili, watu wengi zaidi na zaidi watatangaza kuwa Yeye ni “Mwenye rehema, mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na Kweli.” Kutoka 34:6. [MH 464.6; HU Aya ya 31]

Katika nuru Yake tutaona nuru, mpaka akili na moyo na roho vitakapogeuzwa kuwa mfano wa utakatifu Wake. [MH 465.1; HU Aya ya 32]

Kwa wale ambao hushikilia uhakikisho wa Mungu wa Neno Lake, ndani yake kuna uwezekano wa ajabu. Mbele yao kuna vipengele vikubwa vya Ukweli, rasilimali nyingi za nguvu. Mambo matukufu yatafunuliwa. Mapendeleo, fursa na majukumu ambayo hata wao hawajawahi kufikiria kuwa yamo katika Biblia yatadhihirishwa kwao. Wote wanaotembea katika njia ya utii mnyenyekevu, wakitimiza kusudi Lake Mungu, watajua zaidi na zaidi Maneno ya Mungu. [MH 465.2; HU Aya ya 33]

Hebu mwanafunzi aichukue Biblia kama mwongozo wake na asimame imara kwenye kanuni, naye anaweza kuyaweka matamanio yake juu ili kufikia kilele chochote. Falsafa zote zenye asili ya mwanadamu zimesababisha kuchanganyikiwa na aibu, wakati Mungu hajatambuliwa kuwa yote katika yote. Lakini imani ya thamani iliyovuviwa na Mungu inatia nguvu na kuleta ubora wa tabia. Kadiri tunavyodumu katika wema Wake, rehema Zake, na upendo Wake, uelewa wa Ukweli utakuwa wazi zaidi na zaidi; utakuwa wa juu, na mtakatifu zaidi, matamanio ya usafi (ukamilifu) wa moyo na mawazo yaliyo wazi, yote hayo yatakuwa ya juu kabisa. Nafsi inayokaa katika angahewa safi ya mawazo matakatifu inabadilishwa kwa kuungana kwenye mahusiano na Mungu, kwa njia ya kujifunza Neno Lake. Ukweli ni mkubwa sana, unasambaa na kwenda mbali sana, ni wa kina kiendacho chini sana, na mpana sana, kiasi kwamba ubinafsi unatokomea/unapotezwa. Moyo unalainishwa na kutiishwa katika unyenyekevu, wema, na upendo. [MH 465.3; HU Aya ya 34]

Na nguvu zote za asili za mwanadamu zinakuzwa kwa sababu ya utii wake mtakatifu. Kutoka kwenye somo la Neno la uzima, wanafunzi wanaweza kuja na akili zilizotanuka, zilizoinuliwa, na zilizoboreshwa. Ikiwa wao ni kama Danieli, yaani wasikilizaji na watendaji wa Neno la Mungu, wanaweza kusonga mbele kama yeye alivyofanya katika matawi yote ya elimu au mafunzo. Wakiwa na nia safi, watakuwa na nia thabiti. Kila kitivo cha kiakili kitahuishwa. Wanaweza kujielimisha na kujinidhamisha kiasi kwamba wote walio ndani ya uwanja wa ushawishi wao, nao wataona jinsi mwanadamu

anavyoweza kuwa, na kile anachoweza kufanya, akiunganishwa na Mungu Mwenye hekima na nguvu zisizo na ukomo. [MH 466.1; HU Aya ya 35]

Elimu katika Uzima wa Milele

Kazi yetu ya maisha hapa duniani, ni maandalizi ya uzima wa milele. Elimu iliyoanza hapa haitakamilika katika maisha haya; itakuwa ikiendelezwa milele zote—ni endelevu daima, kamwe haikamiliki. Hekima na upendo wa Mungu katika mpango wa ukombozi vitafunuliwa zaidi na zaidi. Mwokozi, anapowaongoza watoto Wake kwenye chemchemi za maji ya uzima, atawapa ghala nyingi za maarifa. Na siku baada ya siku kazi za ajabu za Mungu, uthibitisho wa nguvu Zake katika Uumbaji na kutegemeza sayari zote zisizo na idadi (universe), zitafunuliwa mbele ya akili zao katika uzuri mpya. Katika nuru inayong'aa kutoka kwenye kiti cha enzi, mafumbo yatatoweka, na nafsi itajawa na mshangao kwa usahili wa mambo ambayo hayakuwahi kueleweka kabla. [MH 466.2; HU Aya ya 36]

Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana. Kwa maana sasa tunaona taswira kama kwa kioo, lakini wakati huo tutaona wazi. Sasa nafahamu kwa sehemu, wakati huo nitafahamu kikamilifu, kama vile mimi ninavyofahamika kikamilifu. [MH 466.3; HU Aya ya 37]

SEHEMU YA 8—HITAJI LA MTENDAKAZI

SURA YA 40

KUFAANA KATIKA MAISHA YA KILA SIKU

Kuna kielelezo chenye nguvu zaidi kuliko kielelezo cha maneno katika maisha yenye utulivu daima, na thabiti, cha Mkristo mkamilifu, wa kweli. Mtu alivyo huwa na mvuto zaidi ya kile anachosema (demeanor). [MH 469.1; HU Aya ya 1]

Wale maofisa waliotumwa kwa Yesu walirudi na taarifa kwamba hakuna mwanadamu aliyenena kama Yeye alivyonena. Lakini sababu yake ilikuwa kwamba, kamwe mwanadamu hajawahi kuishi kama Yeye alivyoishi. Lau maisha Yake yangekuwa tofauti na yalivyokuwa, basi, hangeweza kuzungumza kama alivyonena. Maneno Yake yalibeba nguvu ya kumsadikisha mtu, kwa sababu yalitoka katika moyo safi na mtakatifu, uliojaa upendo na huruma, ukarimu na Ukweli. [MH 469.2; HU Aya ya 2]

Ni tabia na uzoefu wetu wenyewe, ndio ambao huamua ushawishi wetu juu ya watu wengine. Ili kuwashawishi wengine juu ya uwezo wa neema ya Kristo, ni lazima tujue nguvu Zake katika mioyo na maisha yetu wenyewe. Injili tunayowasilisha kwa ajili ya kuokoa roho za watu wengine, ni lazima iwe injili ambayo kwayo nafsi zetu wenyewe zinaokolewa. Ni kwa kupitia imani iliyo hai katika Kristo kama Mwokozi wetu binafsi peke yake, ndiyo kunakuwepo na uwezekano wa mvuto wetu kuhisiwa katika ulimwengu wenye mashaka (watu wenye nadharia za mashaka au wakana-Mungu). Ikiwa tunataka kuwavuta wenye dhambi kutoka katika mkondo wa maji uendao kasi, miguu yetu wenyewe lazima isimikwe kwa uimara juu ya Mwamba, Kristo Yesu. [MH 469.3; HU Aya ya 3]

Beji ya Ukristo si ishara ya nje, sio kuvaa msalaba au taji, bali ni kule kudhihirisha muungano wa mwanadamu pamoja Mungu. Kwa nguvu ya neema Yake inayodhihirishwa katika mabadiliko ya tabia zetu waamini, ndiyo ulimwengu utajiweka katika mkao wa kushawishiwa kwamba Mungu amemtuma Mwanawe kama Mkombozi wake. Hakuna mvuto mwingine

unaoweza kuzingira nafsi ya mwanadamu ambao una nguvu kama uvutano wa maisha yasiyo na ubinafsi. Hoja yenye nguvu zaidi katika kupendelea injili ni Mkristo mwenye upendo na anayependeka. [MH 470.1; HU Aya ya 4]

Nidhamu ya Majaribu

Kuishi maisha kama hayo, kushinikiza ushawishi kama huo, kunagharimu kila hatua ichukuliwayo, kwa kujitoa mhanga na, nidhamu. Ni kwa sababu watu hawaelewi jambo hili ndiyo maana wengi hukatishwa tamaa kwa urahisi katika maisha yao ya Ukristo. Watu wengi wanaoyaweka maisha yao wakfu kwa dhati kwa ajili ya utumishi wa Mungu, wanashangaa na kukatishwa tamaa wanapojikuta wakikabiliwa na vikwazo na tishio la shida au hata kuingia kwenye majaribu na fadhaa kuliko wakati mwingine wowote wa maisha yao, hata walipokuwa siyo waamini. Wanaomba kwa Mungu ili waweze na tabia inayofanana na Kristo, ili waweze kufaa kwa kazi ya Bwana, na wanawekwa katika mazingira ambayo yanaonekana kupunyua uovu wote ulio ndani ya asili yao na kuutoa nje. Makosa yanafichuliwa ambayo hata wao wenyewe hawakushuku au kuwa na fununu ya kuwepo kwake ndani yao. Kama Israeli wa kale watu hawa hujiliza, “Ikiwa Mungu anatuongoza kweli, kwa nini mambo haya yote yanatupata?” [MH 470.2; HU Aya ya 5]

Ni kwa sababu Mungu anawaongoza ndiyo maana mambo haya yanawajia. Majaribio na vikwazo ni njia zilizochaguliwa na Bwana za kunidhamisha na mikakati Yake aliyoweka ili kufikia mafanikio. Yeye Anayesoma nyoyo za watu anazijua tabia zao kuliko wao wenyewe wanavyozijua. Anaona kwamba wengine wana uwezo na mwelekeo au ushawishi ambao endapo utaelekezwa kwa usahihi, basi unaweza ukatumika katika kuendeleza kazi Yake. Katika majaliwa au mipango Yake, Yeye Anawaleta watu hawa katika nafasi tofauti-tofauti na hali anuwai ili waweze kugundua katika tabia zao kasoro ambazo zimefichwa hata kwenye uelewa wao wenyewe. Anawapa watu hawa nafasi ya kurekebisha kasoro hizi na kujistahilisha kwa ajili ya utumishi Wake. Mara nyingi Yeye uruhusu moto wa mateso uwashambulie watu hawa, ili wapate kutakasika. MH 471.1; HU Aya ya 6]

Ukweli kwamba sisi tunaitwa kuvumilia majaribu huonyesha kwamba Bwana Yesu anaona ndani yetu kitu cha thamani ambacho anatamani kusitawisha/kukipalilia. Ikiwa hakuona kitu chochote ndani yetu ambacho kingeweza kulitukuza Jina Lake, basi, asingetumia muda wetu kutusafisha. Yeye hana kawaida ya kuyatupa mawe yasiyofaa katika tanuru Lake la moto (kabuli). Ni madini ya thamani, ndiyo ambayo Yeye huyasafisha. Mhunzi huweka chuma (steel) na chuma cha pua (iron) ndani ya moto ili ajue madini au chuma cha aina gani. Bwana anaruhusu wateule Wake kuwekwa katika tanuru la mateso ili kuthibitisha hulka waliyo nayo na kama wanaweza

kutengenezwa au kuchongwa vizuri kwaajili ya kufaa katika kazi Yake. [MH 471.2; HU Aya ya 7]

Mfinyanzi huchukua udongo na kuufinyanga kulingana na mapenzi yake. Anaukandakanda na kuufanyia kazi. Anaunyumbua-nyumbua na kutoa vipande vingine na kuubonyeza wote kwa pamoja. Anauloweshа na kisha anaukausha. Anauacha ukae chini kwa muda bila kuugusa. Wakati udongo unapofikia hali ya kunyumbulika kikamilifu, hapo ndipo anaendelea na kazi ya kukitengeneza chombo. Anakitengeneza katika umbo la chombo anachotaka akitumia gurudumu linalozunguka, ambalo linapunguza sehemu zisizotakiwa, linalainisha chombo na kuking'arisha. Anakausha udongo huu ulio kwenye umbo la chombo kwenye jua na kisha anauoka katika tanuru la moto lijukanalo kama kabuli (oveni). Na ndivyo kinavyokuwa chombo kinachofaa kwa matumizi. Hivyo ndivyo Mungu, Mfanyakazi Mkuu anavyotamani kutufinyanga na kutuunda/kutuumba sisi wanadamu (tabia, hulka, haiba, mazoea). Na kama vile udongo ulivyo mikononi mwa mfinyanzi, ndivyo tunavyopaswa kuwa mikononi Mwake. Sisi wanadamu hatupaswi kujaribu kufanya kazi ya mfinyanzi. Sehemu yetu ni kujitoa ili kufinyangwa na Mtendakazi Mkuu. [MH 471.3; HU Aya ya 8]

“Wapenzi, msione ajabu juu ya majaribu makali yanayowapata ninyi, kana kwamba ni jambo lisilo la kawaida ambalo limewapata; ili utukufu Wake utakapofunuliwa, nanyi mfurahi kwa furaha tele." 1 Petro 4:12, 13. [MH 472.1; HU Aya ya 9]

Katika mwanga kamili wa mchana, na katika kusikia muziki wa sauti nyingine, ndege aliyefungiwa kwenye banda lake dogo aliloletengenezewa, hataweza kuimba wimbo ambao bwana wake anataka kumfundisha. Anajifunza kunyakua sauti hii, kuimba kidogo noti hii, kidogo ile, lakini kamwe haimbi melodi yote au melodi tofauti. Lakini bwana wake huendelea kumzoeza na kumfundisha kwa kufunika banda lake dogo alilomtengenezea, na kuliweka mahali ambapo ndege atasikiliza wimbo mmoja tu anaopaswa kuimba ili asijichanganye au kukanganyikiwa. Katika giza, ndege anajaribu na kujaribu tena kuimba wimbo huo mpaka wimbo unajifunzwa kwa uzuri wake, naye anaanza tena kuimba kwa sauti nzuri kabisa- yaani kwa ukamilifu. Kisha huyu ndege analetwa kutoka kwenye giza, na baada ya muda anaweza kuimba wimbo huo kwenye nuru. Hivyo ndivyo Mungu hushughulika na watoto Wake. Yeye Ana wimbo wa kutufundisha, na wakati tumejifunza katikati ya vivuli vya mateso tunaweza kuuimba milele baadaye. [MH 472.2; HU Aya ya 10]

Wengi hawajaridhika na kazi zao za maisha. Huenda mazingira yao siyo rafiki; wakati wao unatumika kufanya kazi za kawaida, kazi zisizopendeza au zisizo na wadhifa za nyumbani, wakati ambapo wao wenyewe wanafikiria

kwamba wana uwezo wa kushika majukumu ya juu; mara nyingi jitihada zao machoni pao zinaonekana kuwa hazithaminiwi au zisizo na matunda; mustakabali wao wa siku zijazo unakuwa haujulikani. [MH 472.3; HU Aya ya 11]

Tukumbuke kwamba ingawa kazi tunazopaswa kuzifanya zinaweza kuwa si za chaguzi zetu, inapaswa kukubaliwa kwamba hili ndilo chaguo la Mungu kwetu. Iwe zinapendeza au hazipendezi, sisi tunapaswa kufanya wajibu ulio karibu zaidi. “Lolote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako; kwa maana hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe.” Mhubiri 9:10. [MH 472.4; HU Aya ya 12]

Ikiwa Bwana anatutaka tupeleke ujumbe nchi ya Ninawi, haitampendeza kama sisi tutakwenda Yafa au Kapernaumu. Yeye Ana sababu za kutupeleka mahali ambapo miguu yetu imeelekezwa. Mahali hapo panaweza kuwa na mtu anayehitaji msaada ambao sisi tunaweza kuutoa. Yeye aliyemtuma Filipo kwa towashi wa Ethiopia, Petro kwa akida Mrumi, na yule msichana mdogo Mwisraeli kuwa msaada kwa Naamani, kapteni wa Shamu, hata hivi leo anawatuma wanaume na wanawake na vijana kama wawakilishi Wake kwa wale wanaohitaji msaada na mwongozo wa Bwana/mbinguni. [MH 473.1; HU Aya ya 13]

Mungu Anapanga Kwa Ubora kuliko Yoyote Yule

Mipango yetu sio mipango ya Mungu kila wakati. Anaweza kuona kwamba ni bora kwetu na kwa kusudi Lake kuikataa hata kunia kwetu kuzuri kabisa, kama alivyofanya katika kisa cha Daudi (2 Sam 7). Lakini sisi tunaweza kuwa na uhakikisho katika jambo moja, Yeye atabariki na kuwatumia katika kuendeleza kazi Yake watu wanaojitoa kwa dhati wenyewe na vyote waliyo navyo kwa utukufu Wake. Akiona ni bora asiwatimizie matamanio yao, Yeye atasawazisha mambo vizuri kuhusiana na lile katazo alilowapa, kwa kuwapa ishara za upendo Wake na kuwakabidhi utumishi mwingine. [MH 473.2; HU Aya ya 14]

Katika utunzaji Wake, uliyojaa upendo na maslahi kwetu, mara nyingi Yeye ambaye anatuelewa vizuri zaidi kuliko sisi tunavyojielewa wenyewe, hukataa kuturuhusu tujiingize kwenye ubinafsi wa kutafuta kutosheleza tamaa zetu wenyewe za ukuu (ambition). Yeye haturuhusu sisi tuzipite kando, kazi za nyumbani ambazo tunaziona kwamba ni kazi duni na nyenyekevu, au hazilingani na wadhifa wetu, kwani zinachosha tu, ila kazi hizi za nyumbani zilizo karibu nasi ni kazi takatifu. Mara nyingi majukumu haya yanatupa mazoezi na mafunzo muhimu sana katika kututayarisha kwa kazi za juu zaidi. Mara nyingi mipango yetu hushindwa ili mipango ya Mungu kwetu ifanikiwe. [MH 473.3; HU Aya ya 15]

Kamwe hatuitwi kutoa dhabihu ya kweli kwa ajili ya Mungu. Mambo mengi yale ambayo Yeye anatuomba tuyasalimishe Kwake, lakini kwa kufanya hivi tunasalimisha tu yale ambayo yanaziba njia katika safari yetu ya kuelekea mbinguni. Hata wakati ambapo tunaombwa kusalimisha vile vitu ambavyo ndani yake ni vyema tu, tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu anatufanyia jambo jema la juu zaidi. [MH 473.4; HU Aya ya 16]

Katika maisha yajayo mafumbo ambayo hapa duniani yametuudhi, yametusumbua na kutukatisha tamaa yatawekwa wazi. Tutaona kwamba maombi yetu yanayoonekana kutojibiwa na matumaini yaliyokatishwa tamaa yamekuwa miongoni mwa mibaraka yetu mikubwa. [MH 474.1; HU Aya ya 17]

Tunapaswa kulitazama kila jukumu kuwa ni takatifu, kwa sababu ni sehemu ya utumishi wa Mungu, hata liwe la unyenyekevu kwa kiasi gani. Maombi yetu ya kila siku yanapaswa kuwa, “Bwana, nisaidie kufanya vizuri zaidi. Nifundishe jinsi ya kufanya kazi kuwa ubora zaidi. Nipe nguvu na uchangamfu. Nisaidie kuleta katika huduma yangu huduma ya upendo ya Mwokozi.” [MH 474.2; HU Aya ya 18]

Somo Kutoka katika Maisha ya Musa

Fikiria juu ya uzoefu wa Musa. Elimu aliyopata huko Misri akiwa kama mjukuu wa mfalme na mrithi mtarajiwa wa kiti cha ufalme ilikuwa ya kina mno. Hakuna kitu kilichopuuzwa ambacho kilifikiriwa kumfanya kuwa mtu mwenye hekima, vile Wamisri walivyokuwa wanaielewa hekima. Alipata mafunzo makuu zaidi ya kiraia na kijeshi. Alihisi kuwa alikuwa amejitayarisha kikamilifu kwa kazi ya kuwakomboa Israeli kutoka katika utumwa. Lakini Mungu alipima vinginevyo kabisa. Majaliwa Yake yalimwamria Musa miaka arobaini ya mafunzo nyikani kama mchunga kondoo. [MH 474.3; HU Aya ya 19]

Elimu ambayo Musa alikuwa amepata huko Misri ilimfaa kwake katika mambo mengi; bali maandalizi ya thamani zaidi kwa kazi yake ya maisha yote yalikuwa yale aliyoyapata akiwa kama mchunga kondoo. Kwa kawaida Musa alikuwa na roho ya harara. Huko Misri, akiwa kiongozi wa kijeshi aliyefanikiwa, na kipenzi cha mfalme na taifa, alikuwa amezoea kupokea sifa na kujishaua. Aliwavutia sana watu. Alitumaini kuitimiza kwa nguvu zake mwenyewe kazi ya kuwakomboa Israeli. Mambo ambayo alipaswa kujifunza akiwa mwakilishi wa Mungu yalikuwa tofauti kabisa. Alipokuwa akiongoza kundi lake la kondoo katika pori la milima na katika kijani kibichi cha mabondeni, alijifunza imani na upole, subira, unyenyekevu, na kutojijali mwenyewe tu. Alijifunza kuwajali wanyonge, kuwalea wagonjwa, kutafuta waliotanga mbali, kuchukuliana na wakaidi, kuchunga wana-kondoo, na kulea wazee na wasiojiweza. [MH 474.4; HU Aya ya 20]

Katika kazi hii Musa alikuwa akivutwa karibu na Mchungaji Mkuu. Alipata kuunganiswa karibu na Mtakatifu wa Israeli. Hakuwa na mpango tena wa kufanya kazi kubwa. Alijitahidi kufanya kwa uaminifu kazi hiyo kama kazi aliyokabidhiwa na Mungu. Alitambua uwepo wa Mungu katika maali alipokuwa. Maumbile asili yalizungumza naye juu ya Asiyeonekana. Alimjua Mungu kama Mungu wake, na, katika kutafakari juu ya tabia Yake alifahamu zaidi na zaidi maana ya uwepo Wake. Alipata kimbilio katika mikono ya milele. [MH 475.1; HU Aya ya 21]

Baada ya uzoefu huu, Musa alisikia mwito kutoka mbinguni kubadilisha bakora ya kichungaji kuwa fimbo ya mamlaka; kuacha kundi lake la kondoo na kuiongoza Israeli. Amri ya kiungu ilimkuta mtu asiyejiamini mwenyewe, asiye na maneno mengi, na mwenye woga. Alizidiwa na hisia ya kutokuwa na uwezo wa kuwa msemaji wa Mungu. Lakini alikubali kazi hiyo, akiweka tumaini lake lote katika Bwana. Ukuu wa utume wake ulimtaka kutumia vyema nguvu za akili yake. Mungu alibariki utii wake wa utayari, naye akawa mwenye uwezo wa kuongea kwa ufasaha, mwenye tumaini, mwenye kujiamini, aliyefaa kwa ajili ya kazi kubwa kuliko zote ambazo amewahi kupewa mwanadamu. Imeandikwa juu yake: “Wala hajainuka tena katika Israeli nabii kama Musa, ambaye Bwana alimjua uso kwa uso.” Kumbukumbu la Torati 34:10, [MH 475.2; HU Aya ya 22]

Hebu wale wanaohisi kwamba kazi yao haithaminiwi, na wanaotamani nafasi ya wajibu mkubwa zaidi, wajifunze kwamba “Maana siko mashariki wala magharibi wala nyikani itokako heshima. Bali Mungu ndiye ahukumuye: Humdhili huyu na kumwinua huyu.” Zaburi 75:6, 7. Kila mtu ana nafasi yake katika mpango wa milele wa mbinguni. Ikiwa tutashika nafasi hiyo inategemea uaminifu wetu katika kushirikiana na Mungu. [MH 476.1; HU Aya ya 23]

Twahitaji kujihadhari na kujihurumia. Usijitie kamwe hisia kwamba hauheshimiwi jinsi unavyopaswa kuheshimiwa, kwamba jitihada zako hazithaminiwi, kwamba kazi yako ni ngumu sana. Hebu kumbukumbu ya yale ambayo Kristo amevumilia kwa ajili yetu inyamazishe kila wazo la manung'uniko. Tunatendewa vyema zaidi kuliko vile alivyotendewa Bwana wetu. “Je, unajitafutia mambo makuu? usiyatafute.” Yeremia 45:5. Bwana hana nafasi katika kazi yake kwa wale ambao wana hamu kubwa ya kushinda taji kuliko kubeba msalaba. Anataka watu ambao wamedhamiria zaidi kufanya wajibu wao kuliko kupokea thawabu yao—watu wanaotafuta msingi zaidi kuliko heshima. [MH 476.2; HU Aya ya 24]

Wale walio wanyenyekevu, na wanaofanya kazi yao kama ambayo wamepewa na Mungu, wanaweza wasifanye maonyesho makubwa kama wanavyofanya wale waliojawa na kiherehere na kujiona kuwa muhimu; lakini

kazi yao (waliojishusha) ni kubwa zaidi. Mara nyingi wale wanaofanya gwaride kubwa huita watu wajisikie wenyewe, wakiingilia kati ya watu na Mungu, na kazi yao huthibitisha kushindwa. “Bora hekima, basi jipatie hekima; Naam, kwa mapato yako yote jipatie ufahamu. Umtukuze, naye atakutukuza; Atakupatia heshima ukimkumbatia.” Mithali 4:7, 8. [MH 477.1; HU Aya ya 25]

Kwa kuwa hawana azimio la kujishika mkono wenyewe na kufanya matengenezo, wengi hufikiriwa kuwa katika njia mbaya ya utendaji. Lakini haipaswi kuwa hivi. Wanaweza kukuza uwezo wao wa kufanya aina bora za huduma, na kisha watakuwa katika kuhitajika kila wakati. Watathaminiwa kwa yote wanayostahili. [MH 477.2; HU Aya ya 26]

Ikiwa wo wote wanastahili kwa nafasi ya juu zaidi, Bwana ataweka mzigo, si kwao tu, bali juu ya wale ambao wamewapima, ambao wanajua kustahili kwao, na ambao wanaweza wakawahimiza kusonga mbele. Ni wale wanaofanya kwa uaminifu kazi yao waliyopewa ya kila siku siku, ambao kwa wakati wa Mungu mwenyewe watasikia mwito Wake, “Pandeni juu zaidi.” [MH 477.3; HU Aya ya 27]

Wakati wachungaji walipokuwa wakichunga mifugo yao kwenye vilima vya Bethlehemu, malaika kutoka mbinguni waliwatembelea. Hivyo, leo, wakati mtenda kazi mnyenyekevu wa Mungu anapofanya kazi yake ya maisha, malaika wa Mungu husimama kando yake, wakisikiliza maneno yake, wakiona jinsi kazi yake inavyofanywa, ili kuona ikiwa majukumu makubwa zaidi yanaweza kukabidhiwa mikononi mwake. [MH 477.4; HU Aya ya 28]

Si kwa mali zao, elimu yao, au vyeo vyao wenyewe ndiyo kwamba Mungu huwakadiria wanadamu (au kuwadadavua). Yeye anawakadiria kwa usafi wao wa nia na uzuri wa tabia zao. Yeye anatazama ili aone ni kiasi gani cha Roho Wake wanachomiliki na jinsi maisha yao yanavyofichua mfano Wake. Kuwa mkuu katika ufalme wa Mungu ni kuwa kama mtoto mdogo katika unyenyekevu, katika usahili wa imani, na katika Upendo ulio safi [MH 477.5; HU Aya ya 29]

“Mwajua,” Kristo alisema, “ya kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu atakaye kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu.” Mathayo 20:25, 26, [MH 478.1; HU Aya ya 30]

Kati ya vipawa vyote ambavyo mbingu inaweza kuwatunukia wanadamu, ushirika na Kristo katika mateso Yake ndiyo dhamana nzito na heshima kubwa kupita zote. Siyo Henoka, aliyechukuliwa na kwenda mbinguni, wala si Eliya, aliyepanda katika gari la moto, ndiyo walikuwa wakuu au wenye kuheshimiwa kuliko Yohana Mbatizaji, ambaye aliangamia peke yake kwenye gereza la

shimoni. “Ninyi mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, bali na kuteswa kwa ajili Yake.” Wafilipi 1:29. [MH 478.2; HU Aya ya 31]

Mipango ya Baadaye

Wengi hawawezi kufanya mipango hususani ya siku zijazo. Maisha yao hayajatulia, yamesheheni pilikapilika. Hawawezi kutambua matokeo ya masuala mbalimbali, na hii mara nyingi huwajaza wengi tashwishwi na machafuko. Tukumbuke kuwa maisha ya watoto wa Mungu hapa duniani ni maisha ya hija (tupo safarini). Sisi hatuna hekima ya kupanga maisha yetu wenyewe. Sio fungu letu kutengeneza mustakabali wa maisha yetu. “Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka, asijue alikokwenda. Waebrania 11:8. [MH 478.3; HU Aya ya 32]

Kristo katika maisha yake hapa duniani hakujiwekea mipango kwa ajili Yake Mwenyewe. Alikubali mipango ya Mungu Kwake, na siku baada ya siku Baba alifunua mikakati Yake. Vivyo hivyo nasi tunapaswa kumtegemea Mungu, ili maisha yetu yawe utimizo sahili wa mapenzi Yake Mungu. Tunapoziweka njia zetu Kwake, Yeye ataelekeza hatua zetu. [MH 479.1; HU Aya ya 33]

Watu wengi sana katika mkakati wa kupanga kwa ajili ya siku zijazo nzuri, hufeli kabisa. Acha Mungu akupangie wewe. Kama mtoto mdogo, utumainie mwongozo wa Yeye ambaye “ataiweka sawa miguu ya watakatifu Wake.” 1 Samweli 2:9. Mungu kamwe hawaongozi watoto Wake vinginevyo kuliko vile ambavyo wangechagua kuongozwa, kama wangeweza kuona mwisho kutokea mwanzo na kutambua utukufu wa kusudi ambalo wanalitimiza kama watenda kazi pamoja Naye. [MH 479.2; HU Aya ya 34]

Malipo au Mshahara

Kristo alipowaita wanafunzi Wake wamfuate, hakuwapa matazamio yenye udangayifu kuhusu maisha haya (hakutia chumvi kuhusu uzuri). Hakuwapa wanafunzi Wake ahadi za kujipatia faida au heshima ya kidunia, wala hakutoa ahadi yoyote ya kile watakachopata au kulipwa. Mathayo alipokuwa ameketi kwenye ofisi ya kutoza ushuru, Mwokozi alisema, “Nifuate. Akaacha yote, akainuka, akamfuata.” Luka 5:27, 28. Mathayo hakungoja kudai au kupokea mshara fulani kabla ya kutoa huduma, unaolingana na kiasi alichopokea katika kazi yake ya awali. Bila kuhoji wala kusita Mathayo alimfuata Yesu. Ilitosha kwake kuwa na Mwokozi, ili aweze kusikia Maneno Yake na kuungana Naye katika kazi Yake. [MH 479.3; HU Aya ya 35]

Ndivyo ilivyokuwa kwa wale wanafunzi walioitwa hapo awali. Yesu alipowaambia Petro na waandamani wake wamfuate, mara hiyo-hiyo waliacha

mashua na nyavu zao na wakamfuata. Baadhi ya wanafunzi hawa walikuwa na marafiki wanaowategemea kwa msaada; lakini walipopokea mwaliko wa Mwokozi hawakusita na kuuliza, “Nitaishi vipi na kuitegemeza familia yangu kwa njia gani?” Walikuwa watiifu kwa wito waliopewa; na baadaye Yesu akawauliza, “Je, hapo nilipowatuma hamna mfuko, na mkoba, na viatu, mlipungukiwa na kitu? waliweza kujibu, “La! Hakuna cho chote.” Luka 22:35. [MH 480.1; HU Aya ya 36]

Leo Mwokozi anatuita, kama alivyowaita Mathayo na Yohana na Petro, kwa kazi Yake. Ikiwa mioyo yetu itaguswa na upendo Wake, swali la fidia halitakuwa na kipaumbele cha juu zaidi katika akili zetu. Sisi tutafurahi kuwa watenda kazi tu pamoja na Kristo, na hatutaogopa kutumaini utunzaji Wake. Tukimfanya Mungu kuwa nguvu yetu tutakuwa na mitazamo wazi ya wajibu wetu, na matarajio yasiyo na ubinafsi; maisha yetu yatachochewa na kusudi bora ambalo litatuinua juu ya nia zote chafu. [MH 480.2; HU Aya ya 37]

Bwana Atatoa/Atatupatia

Wengi wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wana mioyo inayohangaika, ni wenye wasiwasi kwa sababu wanaogopa kujitoa kwa Mungu na kujitumainia wenyewe Kwake Mungu (wanaogopa kujidondosha Kwake kwani hawaamini kwamba Yeye atawadaka). Hawajisalimishi Kwake kikamilifu, kwa kuwa wanajiepusha na matokeo ambayo kujisalimisha huko kunaweza kuhusisha. Isipokuwa watajisalimisha, wao hawawezi kupata amani. [MH 480.3; HU Aya ya 38]

Kuna wengi ambao mioyo yao inaumia chini ya mzigo wa masumbufu ya maisha haya kwasababu wanatafuta kufikia kiwango cha ulimwengu (world standard). Wamechagua huduma Yake, wamekubali mahangaiko yake, na wameasili desturi zake. Hivyo tabia zao zinaharibiwa na maisha yao yanachoshwa au kuchakazwa. Wasiwasi unaoendelea maishani mwao unachosha nguvu za maisha. Mola wetu anawataka waiweke kando nira hii ya utumwa. Yeye Anawaalika waikubali nira Yake; Anasema, “Nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi.” Wasiwasi ina upofu na haiwezi kuelewa chochote kuhusu siku zijazo; lakini Yesu anaona mwisho tangu mwanzo. Katika kila shida, Yeye ana njia Yake iliyoandaliwa kuleta afueni. "Yeye hatawanyima jambo lolote jema wale wote waendao kwa unyofu." Mathayo 11:30; Zaburi 84:11. [MH 481.1; HU Aya ya 39]

Baba yetu wa mbinguni ana njia elfu moja za kutupatia mahitaji ambayo hatujui chochote kuhusiana nayo. Wale wote wanaokubali kanuni moja ya kufanya utumishi wa Mungu kuwa jambo kuu na lenye kipaumbele zaidi ya

yote, watapata matata yanayeyuka na njia iliyo wazi mbele ya nyayo zao. [MH 481.2; HU Aya ya 40]

Utekelezaji wenye uaminifu wa majukumu ya leo ndiyo maandalizi bora zaidi ya majaribu ya kesho. Usikusanye pamoja dhima na masumbufu yote ya kesho na kuyaongeza kwenye mzigo wako wa leo. "Yatosha kwa siku maovu yake." Mathayo 6:34. [MH 481.3; HU Aya ya 41]

Hebu tuwe na matumaini na ujasiri. Kukata tamaa katika utumishi wa Mungu ni dhambi na kutotumia busara. Yeye Anajua kila hitaji letu. Mwenyezi Mungu, Mfalme wa wafalme na Mungu wetu anayeshika maagano anaunganisha ulaini, upole na utunzaji wa mchungaji mwororo. Nguvu Zake ni kamilifu, na zisizo na ukomo nazo ni ahadi ya utimilifu wa hakika wa ahadi Zake kwa wote wanaomtumaini. Yeye Ana njia za kuondoa kila ugumu, ili wale wanaomtumikia na kuheshimu njia Anazotumia wapate kutegemezwa. Upendo Wake uko juu sana kuliko upendo mwingine wowote, kama vile mbingu zilivyo juu ya dunia. Yeye Anawaangalia watoto Wake kwa upendo wa milele na usio na kipimo. [MH 481.4; HU Aya ya 42]

Katika siku za maisha yetu zilizo na giza zaidi, wakati mwonekano ni ule unaotupigia marufuku au kutukataza zaidi, hebu tuwe na imani katika Mungu. Yeye Anatenda kazi ili kutimiza mapenzi Yake, akifanya mambo yote vizuri kwa niaba ya watu Wake. Nguvu za wale wanaompenda na kumtumikia Yeye zitafanywa upya siku baada ya siku. [MH 482.1; HU Aya ya 43]

Yeye, Anawezana, Naye Yuko tayari kuwapa waja Wake msaada wote wanaouhitaji. Yeye Atawapa watu hekima inayodaiwa kwa mahitaji yao mbalimbali. [MH 482.2; HU Aya ya 44]

Mtume Paulo aliyejaribiwa alisema hivi: "Akaniambia, Neema Yangu yakutosha; Kwa hiyo afadhali nitajisifu katika udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na matukano, na misiba, na adha, na taabu, kwa ajili ya Kristo; 2 Wakorintho 12:9, 10. [MH 482.3; HU Aya ya 45]

SURA YA 41

KUWASILIANA NA WENGINE

Kila uhusiano katika maisha haya huhitaji zoezi la kujitawala nafsi/kujidhibiti, ustahimilivu, na huruma. Tunatofautiana sana katika tabia, hulka, mazoea, na elimu, ambapo njia zetu za kutazama mambo hutofautiana. Tunahukumu mambo kwa njia tofauti. Uelewa wetu wa ukweli, na mawazo yetu kuhusiana na namna ya kuendesha maisha haya au mitindo ya maisha, si sawa katika mambo yote. Hakuna watu wawili ambao uzoefu wao unafanana katika kila kitu. Majaribu ya mtu mmoja sio si majaribu ya mtu mwingine. Majukumu ambayo mtu mmoja hugundua mwangaza ndani yake, kwa mwingine na mambo magumu na yaletayo fadhaa. [MH 483.1; HU Aya ya 1]

Asili ya mwanadamu ni dhaifu sana, yenye ujinga mwingi, na ni rahisi yeye kuwa na dhana potofu, hivi kwamba kila mmoja anapaswa kuwa mwangalifu katika makadirio anayoweka juu ya mwingine. Tunajua kwa udogo tu jinsi matendo yetu yanavyoathiri uzoefu wa wengine. Tunachofanya au kusema kinaweza kuonekana kwetu kuwa ni cha kitambo kidogo, wakati, macho yetu yangeweza kufunguliwa, tungeweza kuona kwamba juu ya jambo hilo yalibebwa matokeo muhimu zaidi kwa uzuri au kwa uovu, au hata kwa umilele. [MH 483.2; HU Aya ya 2]

Cha kuzingatia kwa wabeba mizigo.

Wengi wamebeba mizigo michache sana, mioyo yao imejua uchungu halisi kidogo sana, wamehisi mkanganyiko na mifadhaiko kidogo sana kwa niaba ya wengine , hawawezi kuelewa kazi ya mbeba mizigo wa kweli. Hawana uwezo wa kuthamini mizigo ya mtu kuliko ambavyo mtoto mdogo anavyoelewa masumbufu, wajibu na taabu ya baba yake anayelemewa na mzigo mzito. Mtoto anaweza kushangazwa na hofu na mashaka ya baba yake. Haya yanaonekana kutohitajika kwake. Lakini miaka ya uzoefu inapoongezeka katika maisha yake, wakati ule ambao yeye mwenyewe atakapofikia mahali pa kujitwika mizigo yake, atatazama nyuma katika maisha ya babaye na kuelewa kile ambacho hapo awali kilikuwa hakieleweki. Uzoefu wenye uchungu sasa umempa maarifa. [MH 483.3; HU Aya ya 3]

Kazi ya mbeba mizigo haieleweki kwa wengi, kazi zake hazithaminiwi, hadi kifo kimweke chini. Wengine wanapoipokea mizigo aliyoiweka chini, na kukabiliana na magumu aliyokumbana nayo, hapo ndipo wanaweza kuelewa jinsi imani na ujasiri wake vilivyojaribiwa. Mara nyingi makosa ambayo watu hawa walikuwa wepesi katika kuyakemea au kukosoa, hupotea machoni pao sasa. Uzoefu huwafundisha huruma. Mungu anaruhusu watu kuwekwa katika nafasi za kuwajibika. Watu hawa wanapokosea, Yeye ana uwezo wa kuwarekebisha au kuwaondoa. Tunapaswa kuwa waangalifu na kutochukua mikononi mwetu kazi ya kuhukumu wengine, ambayo kiuhalisia ni ya Mungu. [MH 484.1; HU Aya ya 4]

Mwenendo wa Daudi katika kumtendea Sauli una somo. Kwa amri ya Mungu, Sauli alikuwa ametiwa mafuta kuwa mfalme wa Israeli. Kwa sababu ya kutotii kwake, Bwana alitangaza kwamba ufalme unapaswa kuondolewa kwake; na bado mwenendo wa Daudi kwa Sauli ulikuwa wenye adabu, ustahimilivu na upole/mwororo kwake! Katika kutafuta uhai wa Daudi, Sauli alifika nyikani na, akiwa bila ulinzi, kisha akaiingia ndani ya pango lile-lile ambalo Daudi na watu wake wa vita walikuwa wamejificha. “Watu wa Daudi wakamwambia, Tazama, siku ile Bwana aliyokuambia, ... Nitamtia adui yako mkononi mwako, nawe umtendee kama utakavyoona vema...Akawaambia watu wake, Bwana apishe mbali, nisimtendee bwana wangu neno hili, masihi wa Bwana, kunyosha mkono wangu dhidi yake, kwa kuwa yeye ni masihi wa Bwana. Mwokozi anatuagiza, “Msihukumu, msije mkahukumiwa. Kwa maana hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimacho, ndicho mtakachopimiwa.” Kumbuka kwamba hivi karibuni kumbukumbu yako ya maisha itapitiwa upya mbele za Mungu (video ya maisha itapita mwanzo mpaka mwisho!). Kumbuka, pia, kwamba Yeye amesema, “Kwa hiyo, wewe mtu uwaye yote uhukumuye, huna udhuru; kwa maana katika hayo

umhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale.:... 1 Samweli 24:4-6; Mathayo 7:1, 2; Warumi 2:1. [MH 484.2; HU Aya ya 5]

Uvumilivu Tunapokosewa

Hatuwezi kuruhusu roho zetu kuchukizwa na uovu wowote ambao sisi tumetendewa kweli au tunaofikiria kwamba tumetendewa. Ubinafsi ni adui tunayehitaji sana kumwogopa. Hakuna aina ya uovu ambayo ina athari mbaya zaidi juu ya tabia kama ilivyo hasira ya binadamu isiyo chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu. Hakuna ushindi mwingine tunaoweza kupata ambao utakuwa wa thamani zaidi kama ushindi unaopatikana juu ya nafsi zetu sisi wenyewe. [MH 485.1; HU Aya ya 6]

Hatupaswi kuruhusu hisia zetu kujeruhiwa kwa urahisi. Tunapaswa kuishi ili tuokoe roho za watu na siyo kuzilinda hisia, hadhi au jina letu. Tunapovutiwa na wokovu wa roho za watu, tutaacha kuweka moyoni tofauti ndogo-ndogo ambazo mara nyingi hutokea katika mahusiano yetu na watu wengine. Chochote ambacho wengine wanaweza kufikiria kutuhusu au kutufanyia, hakipaswi kuuvuruga umoja wetu na Kristo, ushirika wa Roho. “Kwa maana ni sifa gani kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makofi? Lakini kustahimili, mtendapo mema na kupata mateso, huu ndio wema hasa mbele za Mungu.” 1 Petro 2:20. [MH 485.2; HU Aya ya 7]

Usilipize kisasi au kumjibisha mtu anaposema mabaya kwako. Kwa kadiri uwezavyo kwa upande wako, fagilia mbali sababu zote za kutoelewana au kushuku mabaya kuhusu wengine. Epuka mwonekano wa uovu. Fanya yote yaliyo katika uwezo wako, bila kuvunja kanuni za Mungu, kuoatana wengine. “Ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako; iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako; upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako.” Mathayo 5:23, 24. [MH 485.3; HU Aya ya 8]

Ikiwa maneno ya kukosa subira au jazba yamenenwa kwako, basi wewe usijibu kamwe kwa roho ile ile. Kumbuka kwamba “jibu la upole hugeuza hasira.” Mithali 15:1 . Na kuna nguvu ya ajabu katika kukaa kimya. Maneno yanayosemwa kwa kumjibu mtu aliyekasirika nyakati fulani huchochea hasira yake tu. Lakini hasira inapokutana na ukimya, katika roho ya nyororo, yenye uvumilivu, na upole, hufa kwa haraka. [MH 486.1; HU Aya ya 9]

Unapokuwa chini ya dhoruba ya maneno yanayoumiza moyo, na maneno ya kutafuta makosa ya watu wengine, wewe iweke akili yako katika neno la Mungu. Hebu akili na moyo wako vihifadhiwe na ahadi za Mungu. Ikiwa umetendewa vibaya au umeshtakiwa isivyo haki, badala ya wewe kurudisha

jibu la hasira, zirudie ahadi za Mungu zenye thamani kwako mwenyewe, yaani jizungumzie ahadi za Mungu, tena na tena: [MH 486.2; HU Aya ya 10]

“Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema.” Warumi 12:21. [MH 486.3; HU Aya ya 11]

“Umkabidhi Bwana njia yako; mtumaini pia; Naye atalitimiza. Naye ataidhihirisha haki yako kama nuru, na hukumu yako kama adhuhuri.” Zaburi 37:5, 6. [MH 486.4; HU Aya ya 12]

“Hakuna neno lililofunikwa, ambalo halitafunuliwa; wala lililofichwa, ambalo halitajulikana.” Luka 12:2. [MH 486.5; HU Aya ya 13]

“Uliwaruhusu watu watukalie vichwani, tulipita kwenye moto na kwenye maji, lakini ulituleta kwenye nchi iliyojaa utajiri tele.” Zaburi 66:12. [MH 486.6; HU Aya ya 14]

Tuna mwelekeo wa kutazamia kupata huruma na matumaini kutoka kwa wanadamu wenzetu, badala ya kumwangalia Yesu. Katika rehema na uaminifu Wake, mara nyingi Mungu huwaruhusu wale tunaowatumaini watuangushe, ili tupate kujifunza upumbavu wa kumtegemea mwanadamu, na kumfanya mwanadamu kuwa ulinzi na kinga yetu. Hebu na tumtegemee Mungu kikamilifu, kwa unyenyekevu, na bila ubinafsi. Yeye anajua huzuni ya kina tunayohisi hadi ndani ya nafsi zetu, lakini ambayo hatuwezi kuielezea. Wakati ambapo mambo yote yanaonekana kuwa giza na yasiyoelezeka, kumbuka Maneno ya Kristo, “Nifanyalo wewe hujui sasa; lakini utajua baadaye.” Yohana 13:7. [MH 486.7; HU Aya ya 15]

Jifunze historia ya Yusufu na ya Danieli. Bwana hakuzuia njama za wanadamu waliotaka kuwadhuru; lakini alizifanya mbinu hizi zote kufanya kazi kwa wema kwa watumishi Wake ambao katikati ya majaribu na migogoro hii, bado watu hawa waliitunza imani na uadilifu wao. [MH 487.1; HU Aya ya 16]

Kadri ambavyo tuko ulimwenguni, tutakumbana na mivutano mibaya. Kutakuwa na uchokozi wa makusudi kabisa, utakaojaribu hulka na hasira zetu; na ni kwa kukutana na matukio haya katika roho sahihi ndipo neema za Kikristo zinastawishwa/zinapaliliwa. Ikiwa Kristo anakaa ndani yetu, tutakuwa wavumilivu, wenye fadhili, wastahimilivu, wachangamfu katikati ya masumbufu na maudhi. Siku baada ya siku na mwaka baada ya mwaka tutaushinda ubinafsi/umimi, na kukua, na hata kuwa mashujaa bora. Hii ndiyo kazi yetu tuliyopewa; lakini kazi hii haiwezi kukamilishwa au kutimizwa bila ya msaada kutoka kwa Yesu, uamuzi thabiti, kusudi kusudi lisiloyunba, kudumu katika kukesha, na maombi yasiyokoma. Kila mmoja ana vita binafsi

vya kupigana. Hata Mungu Mwenyewe hawezi kuzifanya tabia zetu kuwa bora au maisha yetu kuwa ya manufaa, isipokuwa tumekuwa watenda kazi pamoja Naye. Wale wanaokataa mapambano haya, hupoteza nguvu na furaha ya ushindi. [MH 487.2; HU Aya ya 17]

Hatuhitaji kuweka rekodi yetu wenyewe ya majaribu na matatizo, huzuni, na sikitiko. Haya yote yameandikwa katika vitabu tayari, na mbingu itayashughulikia. Tunapohesabu mambo yanayotuchukiza, au tusiyoyakubali au mabaya, mambo mengi ambayo ni ya kupendeza na ambayo tungepaswa kuyatafakari yanatokomea kutoka kwenye kumbukumbu zetu, kama vile fadhili na rehema za Mungu zinazotuzunguka kila wakati na upendo wa Mungu kwa wanadamu ambao malaika wanaushangaa, kwamba Mungu alimtoa Mwana Wake afe kwa ajili yetu. Ikiwa kama Mtendakazi wa Kristo unahisi kwamba umekuwa na masumbufu na majaribu makubwa zaidi kuliko yale ambayo yamewaangukia wanadamu wengine, basi, kumbuka kwamba kwako kuna amani ipitayo akili ambayo wale wanaoepuka mizigo hii ya kazi ya Mungu, hawajajaliwa bado kuwa nayo. Kuna faraja na furaha katika huduma ya Kristo. Hebu na ulimwengu uone kuwa maisha pamoja Naye Kristo, hakika sio kufeli/kushindwa. [MH 487.3; HU Aya ya 18]

Ikiwa moyo wako hauchangamki au kuwa na furaha, usizungumze juu ya hisia zako. Usitupe kivuli juu ya maisha ya wengine. Dini iliyo na ubaridi, na isiyo na jua, kamwe haizivuti roho kwa Kristo. Bali huwafukuza kutoka Kwake hadi kwenye nyavu ambazo Shetani amezitandaza kwa ajili ya miguu ya wale waliopotea na wanaotangatanga mbali naye. Badala ya kufikiria kuhusu moyo wako uliovunjika, hebu fikiria juu ya nguvu ambayo unaweza kudai katika Jina la Kristo. Acha mawazo yako yashike kwa nguvu yale mambo yasiyoonekana. Hebu fikra zako zielekezwe kwenye ushahidi wa upendo mkuu wa Mungu kwako. Imani ina uwezo wa kustahimili majaribu, kupinga majaribu, na kustahimili kuvunjika moyo. Yesu anaishi kama mtetezi wetu. Vyote vile ambavyo upatanishi Wake umevipata ni vyetu sisi. [MH 488.1; HU Aya ya 19]

Je, hufikiri kwamba Kristo anawathamini wale wanaoishi kikamilifu kwa ajili Yake? Je, hujui kwamba Yeye huwatembelea wale ambao, kama Yohana mpendwa aliyekuwa uhamishoni, wako kwa ajili Yake katika maeneo magumu na yenye majaribu makali (mitihani mizito)? Mungu hatamwacha hata mmoja wa watenda kazi Wake wenye moyo wa kweli aachwe peke yake kupigana katika hali ngumu na kushindwa. Yeye anawahifadhi watu hao kama kito cha thamani, na kila mtu ambaye maisha yake yamefichwa pamoja na Kristo ndani Yake. Kristo Anasema hivi kuhusu kila mtu kama huyo: “Nitakufanya kuwa muhuri; kwa maana nimekuchagua wewe.” Hagai 2:23. [MH 488.2; HU Aya ya 20]

Basi zungumza juu ya ahadi za Mungu; zungumza juu ya utayari wa Yesu kubariki. Yeye hatusahau hata kwa muda mfupi . Haijalishi tuko katika wakati wa hali ngumu au mazingira ya kuchukiza kiasi gani, sisi tutapumzika Naye kwa siri na tumaini katika upendo Wake, na kujifungia ndani pamoja Naye, hisia ya uwepo Wake itatia msukumo wa furaha ya kina, na yenye utulivu. Kristo alisema hivi kuhusu Yeye Mwenyewe: “Sifanyi neno kwa nafsi Yangu; lakini kama Baba alivyonifundisha, ndivyo ninavyosema. Naye aliyenipeleka Yu pamoja Nami; kwa maana siku zote nafanya yale yampendezayo.” Yohana 8:28, 29. [MH 488.3; HU Aya ya 21]

Uwepo wa Baba ulimzunguka Kristo, na hakuna kitu kilichomfikia isipokuwa kile ambacho ule upendo usio na kikomo ulikiruhusu kuwa baraka ya ulimwengu. Hapa ndipo palikuwa chanzo Chake cha faraja, na ni kwaajiliyetu pia. Yeye aliyejazwa Roho wa Kristo, hukaa ndani ya Kristo. Chochote kinachomjia kinatoka kwa Mwokozi, ambaye anamzunguka kwa uwepo Wake. Hakuna kinachoweza kumgusa isipokuwa kwa idhini ya Bwana. Mateso na huzuni zetu zote, majaribu na mitihani yetu yote, masikitiko na huzuni zetu zote, mateso yetu yote na hali ngumu ya ufukara, kwa kifupi, mambo yote hufanya kazi pamoja kwa faida yetu. Uzoefu wote na hali zote ni watenda kazi wa Mungu katika maisha yetu, ambao hufanya mema yaletwe kwetu. [MH 488.4; HU Aya ya 22]

Ikiwa tuna hisia ya ustahimilivu wa Mungu kwetu sisi, hatutakutwa tukiwa tunawahukumu au kuwashtaki wengine. Wakati Kristo alipokuwa akiishi duniani, wenzake alioishi Naye wangemshangaa kwa kiasi gani, ikiwa, baada ya kufahamiana Naye, wangemsikia akinena neno moja la mashtaka, neno la kutafuta makosa ya watu, au kukosa subira. Kamwe tusisahau kwamba, wale wanaompenda Mungu wanapaswa kumwakilisha Yeye kwa tabia zao. [MH 489.1; HU Aya ya 23]

“Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu.” “msilipe ovu kwa ovu, wala laumu kwa laumu; mkijua ya kuwa ndiko mlioitiwa ili mrithi baraka.” Warumi 12:10; 1 Petro 3:9. [MH 489.2; HU Aya ya 24]

Bwana Yesu anatutaka sisi kutambua haki za kila mtu. Haki za kijamii za wanadamu, na haki zao kama Wakristo zinapaswa kuzingatiwa/kutiliwa maanani. Watu wote wanapaswa kutendewa kwa usafi na umakimi, kama wana na binti za Mungu. [MH 489.3; HU Aya ya 25]

Ukristo utamfanya mtu kuwa muungwana. Kristo alikuwa mwenye adabu/nidhamu/kujistahi, hata kwa watesi Wake; na wafuasi Wake wa kweli watadhihirisha roho hiyo hiyo pia. Mtazame Paulo alipoletwa mbele ya

watawala. Hotuba yake mbele ya Agripa ni kielelezo cha uungwana na adabu ya kweli pamoja na ufasaha wenye ushawishi wa kuongea. Injili haihamasishi mioyo ya watu kuwa na adabu na isiyotoka moyoni kama ulimwengu unavyofanya (adabu feki), adabu ya kutimiza wajibu tu, bali adabu inayotokana na wema halisi wa moyo. [MH 489.4; HU Aya ya 26]

Ukuzaji makini zaidi wa sifa za nje za maisha hautoshi kufungia nje jazba, au hasira zote , kuhukumu watu kwa ukali, na kuwa na maneno yasiyofaa. Usafi wa kweli hautaonekana mradi ubinafsi unaendelea kuzingatiwa kama kitu cha juu zaidi. Upendo lazima ukae moyoni. Mkristo mkamilifu hupata nia ya utendaji wake kutoka katika upendo wake wa kina kwa Bwana wake. Kupitia mizizi ya upendo wake kwa Kristo, yanaibuka maslahi yasiyo na ubinafsi kwa ndugu zake. Upendo humpa yule alio nao neema, stahiki, na uzuri wa tabia kwa mwonekano wa nje, na ndani. Unaangazia uso na kuitiisha sauti; husafisha na kuinua mtu mzima. [MH 490.1; HU Aya ya 27]

Maisha hayajumuishi dhabihu kubwa na mafanikio ya kushangaza, bali mambo madogo-madogo. Mara nyingi ni kupitia vitu vidogo-vidogo, ambavyo vinaonekana kutostahili kutambuliwa kwamba wema au uovu mkubwa huletwa katika maisha yetu. Ni kwa kushindwa kwetu kustahimili majaribu yanayotujia katika mambo madogo-madogo, ambapo mazoea yanaumbwa, na tabia inaharibiwa; na kisha mitihani mikubwa ikija inatukuta tukiwa hatuko tayari. Ni kwa kutenda kwa kanuni kwenye majaribio ya maisha ya kila siku, ndiyo tunaweza kupata uwezo wa kusimama imara na kwa uaminifu katika nafasi zenye hatari na ngumu zaidi. [MH 490.2; HU Aya ya 28]

Hatuko peke yetu kamwe. Iwe tunamchagua Yeye au la, sisi tuna Mwenzi. Kumbuka mahali popote pale ulipo, chochote kile unachofanya, Mungu Yupo. Hakuna kile kinachosemwa au kufanywa au kufikiriwa ambacho kinaweza kutoroka usikivu Wake. Kwa kila neno au tendo, wewe una shahidi—Mungu mtakatifu, anayechukia dhambi. Kabla hujazungumza au kutenda, fikiria jambo hili kila wakati. Wewe kama Mkristo, ni mshiriki wa familia ya kifalme, mtoto wa Mfalme wa mbinguni. Usiseme neno, usifanye tendo lolote, litakaloleta aibu juu ya “Jina lile zuri mliloitiwa.” Yakobo 2:7. [MH 490.3; HU Aya ya 29]

Jifunze kwa makini tabia ya Mungu-na mara kwa mara endelea kujiuliza swali hili, “Je, Yesu angefanya nini kama Angekuwa katika nafasi yangu?” Hiki ndicho kinapaswa kuwa kipimo cha wajibu wetu. Usijiweke bila sababu katika jamii ya wale ambao kwa sanaa au stadi zao wanaweza kudhoofisha kusudi lako la kufanya mema, au kuleta doa juu ya dhamiri yako. Usifanye chochote kati ya wageni, mitaani, kwenye magari, au nyumbani, ambacho kingekuwa na muonekano hata mdogo wa uovu. Fanya kitu fulani kila siku ili kuboresha,

kupendezesha, na kuyatukuza maisha ambayo Kristo ameyanunua kwa damu Yake Mwenyewe. [MH 491.1; HU Aya ya 30]

Daima tenda kwa msimamo wa kanuni, na kamwe usitende kwa misukumo au mihemko. Punguza msukumo wa asili wa jazba au kuhamaki kwa kuwa na uungwana, upole na ulaini wa tabia. Usiendekeze tabia ya kutokuwa makini, na kuchukulia vitu kwa urahisi au hata kuendekeza mambo madogo madogo yaliyo ya kipuuzi tu. Hebu kejeli za ovyo, matusi na tabia za maadili ya chini zisiruhusiwe kupita katika midomo yako. Hata mawazo yako yasiruhusiwe kukimbia huku na kule, ovyo ovyo. Yanapaswa kudhibitiwa, iteke nyara kila fikira yako ili ipate kumtii Kristo (2 Wakorintho 10:5). Hebu mawazo yako yawekwe juu ya mambo matakatifu. Kisha, kwa neema ya Kristo, yatakuwa safi na ya kweli (Wafilipi 4:8). [MH 491.2; HU Aya ya 31]

Tunahitaji utambuzi endelevu na wenye nguvu, unaoboresha mawazo yetu ili yawe safi. Usalama pekee kwa roho ya mtu ye yote ni fikra sahihi. Kama vile mtu “anavyowaza moyoni mwake, ndivyo alivyo.” Mithali 23:7. Nguvu ya kuizuia na kuidhibiti nafsi huimarishwa kwa mazoezi/kujizoesha. Kile ambacho mwanzoni kinaonekana kuwa kigumu, kwa kukirudia-rudia mara kwa mara kinakuwa rahisi, mpaka mawazo na matendo sahihi yanakuwa mazoea ya mtu. Ikiwa tuna tutaazimia, basi tunaweza kujiepusha na yale yote ambayo ni ya ovyo, kipumbavu na duni, na kupanda kufikia kiwango cha juu; tunaweza kuheshimiwa na wanadamu na kuwa wapendwa wa Mungu. [MH 491.3; HU Aya ya 32]

Jenga mazoea ya kusema mambo mazuri juu ya wengine. Zingatia sifa nzuri za wale unaoshirikiana nao, kisha uangalie kwa udogo sana kwa kadri iwezekanavyo, makosa na mapungufu yao. Unapojaribiwa kulalamika juu ya yale ambayo mtu amesema au kufanya, toa sifa kuhusu jambo fulani katika maisha au tabia ya mtu huyo. Palilia moyo wa shukrani. Msifu Mungu kwa upendo Wake wa ajabu katika kumtoa Kristo afe kwa ajili yetu. Haifai kamwe kukaa na kufikiria malalamiko au mang’uniko tuliyo nayo. Mungu anatuita tufikirie rehema Zake na upendo Wake usio na kifani, ili tuweze kuongozwa na Roho katika kutoa sifa. [MH 492.1; HU Aya ya 33]

Wafanyakazi wanaofanya kazi kwa bidii na dhati, hawana wakati wa kutafakari makosa ya wengine. Hatuwezi kuthubutu kuishi kwa kuangalia pumba za makosa au kasoro za watu wengine. Kuzungumza maovu ni laana yenye sehemu mbili, ambayo, inamwangukia mzungumzaji kwa uzito zaidi kuliko msikilizaji. Anayetawanya mbegu za mafarakano na ugomvi huvuna nafsini mwake matunda ya kufisha. Kitendo kile chenyewe cha kutafuta ubaya ndani ya watu wengine hupalilia uovu kwa watazamaji. Kwa kukaa kwenye makosa ya wengine, tunabadilishwa kuwa katika sura hiyo hiyo. Lakini kwa

kumtazama Yesu, na kuzungumzia kuhusu upendo Wake, na ukamilifu wa tabia Yake, sisi tunabadilishwa na kuwa na sura/taswira Yake. Kwa kutafakari ubora wa hali ya juu alioweka mbele yetu, tutainuliwa hadi katika angahewa lililo safi na takatifu, yaani kwenye uwepo wa Mungu Mwenyewe. Tukidumu kaa hapa, kuna nuru ambayo itatoka kwetu na kuwaangazia wote waliounganishwa nasi. [MH 492.2; HU Aya ya 34]

Badala ya kuwakosoa na kuwahukumu wanadamu wengine, wewe sema, “Lazima nitimize wokovu wangu mwenyewe. Ikiwa nitashirikiana na Yule anayetaka kuokoa roho yangu, basi ni lazima nikeshe na kujichunga mwenyewe kwa bidii. Lazima niondoe kila uovu kutoka katika maisha yangu. Lazima nishinde kila dhambi na kosa. Lazima nifanywe kuwa kiumbe kipya katika Kristo. Kisha, badala ya kuwadhoofisha na kuwakatisha tamaa wale wanaojitahidi kupigana dhidi ya uovu, mimi ninaweza kuwatia nguvu kwa maneno ya kutia moyo.” Sisi hatujaliani wenyewe kwa wenyewe. Mara nyingi twasahau kwamba watendakazi wenzetu wanahitaji nguvu na furaha. Uwe mwangalifu katika kuwahakikishia kwamba unajali maslahi yao na kuwaonyesha huruma. Wasaidie watu hawa kwa maombi yako, na wajulishe kwamba unafanya hivyo. [MH 492.3; HU Aya ya 35]

Sio wote wanaodai kuwa watenda kazi wa Kristo ni wanafunzi na wafuasi wa Kweli wa Mungu. Miongoni mwa wale wanaobeba Jina Lake, na ambao hata wamehesabiwa pamoja na watenda kazi Wake, wamo wengine ambao hawamwakilishi Yeye katika tabia zao. Hawaongozwi kwa kanuni Zake. Watu hawa mara nyingi ndiyo sababu ya kuchanganyikiwa, mifadhaiko na kukatishwa tamaa kwa watendakazi wenzao ambao ni vijana katika uzoefu wao wa Kikristo; ila hakuna haja ya mtu hata mmoja kupotoshwa miongoni mwetu. Kristo ametupa kielelezo kilicho kamili. Yeye Ametuamuru tumfuate. [MH 493.1; HU Aya ya 36]

Mpaka mwisho wa wakati kutakuwa na magugu kati ya ngano. Wakati watumishi wa tajiri mwenye shamba walipoomba ruhusa ya kung’oa magugu kwa shauku ya kumheshimu, bwana wao alisema: “La; msije mkakusanya magugu, na mkang'oa na ngano pamoja nayo. Viacheni vyote vikue pamoja mpaka wakati wa mavuno.” Mathayo 13:29, 30. [MH 493.2; HU Aya ya 37]

Katika rehema na subira Yake, Mungu huvumilia kwa ustahimilivu watu wapotovu, wadanganyifu na wasio waaminifu. Miongoni mwa mitume wateule wa Kristo alikuwemo Yuda msaliti. Je, sisi ndiyo tuwe na sababu ya kushangaa au kukatishwa tamaa kwamba tuna watu waongo au hata wasio waaminifu miongoni mwa watendakazi Wake hivi leo? Ikiwa Yeye awezaye kuusoma moyo aliweza kumstahimili yule ambaye alijua kuwa atakuwa msaliti Wake, sisi

tunapaswa kuvumilia kwa subira kubwa kiasi gani, wale walio na makosa. [MH 493.3; HU Aya ya 38]

Na hakika sio wote, hata miongoni mwa wanaoonekana waovu, walio kama Yuda. Petro, mtu mwenye hulka ya pupa, mwenye kiherehere, mwenye haraka katika kufanya mambo, na mwenye kujiamini, huyu mara nyingi alionekana kutokuwa na manufaa na hatakuleta hasara kubwa zaidi kuliko Yuda. Mara nyingi alikaripiwa na Mwokozi. Lakini maisha yake ya utumishi na kujikana nafsi yalikuwa ya thamani kubwa kiasi gani! Mtume huyu anatupa ushuhuda wa ajabu kiasi gani, wa uwezo wa neema ya Mungu! Kwa kadiri tuwezavyo, sisi tunapaswa kuwa kwa wengine kama Yesu alivyokuwa kwa wanafunzi Wake alipotembea na kuzungumza nao hapa duniani. [MH 493.4; HU Aya ya 39]

Jichukulieni na kuishi kama wamishenari, kwanza kabisa, miongoni mwa watendakazi wenzenu. Aghalabu twahitaji muda mwingi na kazi kubwa ili kuleta roho moja kwa Kristo. Na mtu anapogeuka kutoka katika dhambi na kuelekea katika haki, kuna furaha mbele ya malaika. Je, unafikiri kwamba roho za malaika hawa wahudumiaji, wanaozilinda nafsi hizi wanafurahi kweli kuona jinsi watu hawa wanavyotendewa bila kujali, na baadhi ya watu wanaodai kuwa ni Wakristo? Ikiwa Yesu angeshughulika nasi kama tunavyoshughulikiana sisi kwa sisi mara kwa mara, ni nani kati yetu kweli ambaye angeweza kuokolewa? [MH 493.5; HU Aya ya 40]

Kumbuka kwamba wewe huwezi kusoma mioyo. Huijui nia ambayo ilisababisha vitendo ambavyo kwako vinaonekana vibaya. Kuna wengi ambao hawajapata elimu sahihi; tabia na mazoea yao vimepotoka, wao ni wagumu na wenye mikunjo na mafundo-fundo na wanaonekana kupotoka katika kila njia. Lakini neema ya Kristo inaweza kuwabadilisha. Kamwe usiwatupe watu hawa kando, usiwafukuze kamwe na kuwafanya waende zao wakiwa wamevunjika mioyo au kukata tamaa, kwa wewe kusema kwamba; “Umenivunja moyo, na sitajaribu kukusaidia.” Maneno machache yanayosemwa kwa jazba wakati mtu anapochokozwa—maneno yale tu ambayo sisi tunafikiria kwamba kwa hakika wanayastahili—huenda yakakata kamba za mvuto au ushawishi, ambazo zingeifunga mioyo yao kwa mioyo yetu. [MH 494.1; HU Aya ya 41]

Maisha yenye uthabiti; yasiyotangatanga huku na kule, na yenye ustahimilivu wenye subira, roho isiyohisi kuvurugwa inapochokozwa, daima ni hoja thabiti na yenye ushawishi mkubwa. Ikiwa umekuwa na fursa na manufaa ambayo hayajawaangukia wengine bado, fikiria hili, na kisha uwe mwalimu mwenye hekima daima, mwangalifu na mpole kila wakati. [MH 494.2; HU Aya ya 42]

Ili kujipatia umbo la picha ya muhuri kwenye nta, na kisha umbo hilo lionekane wazi na liwe na chapa yenye ushawishi zaidi, huweki muhuri juu ya nta kwa haraka na kwa jeuri; unatengeneza picha ya muhuri kwa taratibu; unaweka muhuri kwa uangalifu kwenye nta ambayo ni kama plastiki mbichi na laini, na kwa utulivu, unakandamiza muhuri wako chini kwa taratibu kwenye nta, hadi muhuri na nta inakaukiana na kuwa ngumu. Vivyo hivyo ndivyo unavyopaswa kushughulika na roho za wanadamu. Uendelevu wa mvuto wa Kikristo ndiyo siri ya nguvu zake, na hii inategemea uthabiti wako katika kuidhihirisha tabia ya Kristo. Wasaidie wale ambao wamekosea, kwa kuwaambia uzoefu wako. Onyesha namna ambavyo ulipofanya makosa makubwa, subira, fadhili, na msaada kutoka kwa watendakazi wenzako ulikupa ujasiri na tumaini. [MH 494.3; HU Aya ya 43]

Ni mpaka katika hukumu, Kamwe hautajua mvuto wa ukarimu, kuwajali wasioeleweka, wasio na maana, na wasiostahili. Tunapokutana na moyo wa kutokuwa na shukrani na usaliti wa (amana takatifu), tunaamshwa kuonyesha dharau, chuki au hasira yetu. Mambo haya hakika wale watu wenye hatia wanayatarajia; wanakuwa wamejiandaa kwa mkao huo. Lakini uvumilivu uliochanganyika na fadhili huwashangaza, na mara nyingi huamsha misukumo yao bora na kuwasha moyoni mwao shauku ya maisha bora. [MH 495.1; HU Aya ya 44]

“Ndugu, mtu akighafilika katika kosa lo lote, ninyi mlio wa Roho, mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole; ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe. Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.” Wagalatia 6:1, 2. [MH 495.2; HU Aya ya 45]

Wote wanaodai kuwa watoto wa Mungu wanapaswa kukumbuka kwamba kama wamishenari, watakutana na makundi yote ya akili. Kuna wale waliosafishwa, kuna wale wakorofi, wanyenyekevu na wenye kiburi, wale wapenda dini na pia watu wenye mashaka, wasomi na wajinga, matajiri na masikini. Akili hizi mbalimbali haziwezi kutendewa sawa; ila watu wote wanahitaji kutendewa wema na kuonyeshwa huruma. Kwa kuwasiliana na kila mmoja wa watu hawa, akili zetu zinapaswa kupigwa msasa ili zing’ae, zisafishwe na kuboreshwa. Sisi wanadamu tunategemeana, tukiwa tumeunganishwa kwa ukaribu na vifungo vya undugu wa kibinadamu. [MH 495.3; HU Aya ya 46]

“Mbingu ziliumba kila mmoja kwa mwingine, wote wanategemeana,

bwana mkubwa au mtumishi au rafiki,

Huitana kila mmoja kwa mwenzake ili kuomba msaada,

Mpaka udhaifu wa mtu mmoja unapaliliwa na kuwa nguvu za wote.” [MH 496.1; HU Aya ya 47]

Ni kwa kupitia mahusiano ya kijamii ambapo Ukristo unaletwa katika uhusiano na ulimwengu. Kila mwanamume au mwanamke ambaye amepokea nuru ya kiungu, anapaswa kuangaza nuru katika njia ya giza ya wale ambao hawajaifahamu njia iliyo bora zaidi. Nguvu ya kijamii, iliyotakaswa na Roho wa Kristo, lazima iboreshwe katika kuzileta roho kwa Mwokozi. Kristo hatakiwi kufichwa moyoni kama hazina ya kichoyo, takatifu na tamu, ya kufurahiwa na yule tu aliye nayo peke yake. Tunapaswa tuwe na Kristo ndani yetu kama kisima cha maji, yanayobubujikia kwenye uzima wa milele, yakiwaburudisha na kuwafanya upya wote wanaokutana nasi. [MH 496.2; HU Aya ya 48]

SURA YA 42

MAENDELEO NA HUDUMA

Maisha ya Kikristo ni zaidi ya ambavyo wengi wanavyoyafikiria kuwa. Hayajumuishi tu uungwana, subira, upole, na wema. Hakika neema hizi ni za muhimu sana; lakini pia kuna haja ya kuwa na ujasiri, moyo mkuu, nguvu, msukumo, na uvumilivu. Njia ambayo Kristo anaiwekea alama, ni njia nyembamba, yenye kujikana nafsi. Kuingia kwenye njia hiyo na kusonga mbele katika magumu na kukatishwa tamaa kunahitaji watu ambao wana zaidi ya

tabia ya unyonge (hawana tabia dhaifu, wana myo mkuu). [MH 497.1; HU Aya ya 1]

Nguvu ya Tabia

Wanatafutwa watu wenye nguvu/stamina, wanaume na wanawake ambao hawatangoja njia yao ilainishwe na kila kizuizi kiondolewe, watu ambao wataleta jotojoto lenye ari mpya kwenye jitihada zinazolegalega za watendakazi waliokata tamaa, watu ambao mioyo yao imechangamka kwa joto la upendo wa Kikristo na ambao mikono yao ina nguvu ya kufanya kazi ya Mwalimu wao. [MH 497.2; HU Aya ya 2]

Baadhi ya wanaoshiriki katika huduma ya umishenari ni dhaifu, hawana ujasiri, wanavunjika moyo kirahisi. Wanakosa msukumo. Hawana sifa chanya za tabia zinazowapa uwezo wa kufanya jambo fulani—hawana roho na nishati inayotia joto matamanio yao. Wale ambao wangejitwalia mafanikio, ni lazima wawe na ujasiri na matumaini. Hawa wanapaswa kustawisha sio tu sifa tulivu zisizoonekana au zisizo na sauti, bali pia sifa za utendaji hai. Ingawa wanapaswa kutoa jibu laini ambalo hugeuza hasira, lakini ni lazima pia wawe na ujasiri wa shujaa unaosaidia kuupinga uovu. Wakiwa tayari na upendo unaostahimili mambo yote, wanahitaji msukumo wa tabia ambao utafanya mvuto wao kuwa na nguvu chanya. [MH 497.3; HU Aya ya 3]

Wengine hawana uimara wa tabia. Mipango na madhumuni yao haina umbo na uthabiti. Utendaji wao halisi ulio na manufaa kwa ulimwengu ni mdogo sana. Tunapaswa kupata ushindi kutoka kwenye udhaifu huu wa kutokuwa na maamuzi, na uzembe. Katika tabia ya Kikristo ya kweli kuna hali ya ujasiri ya kufanya tusiweze kushindwa ambayo haiwezi kufinyangwa au kutawaliwa na mazingira magumu au mabaya. Ni lazima tuwe na uti wa mgongo wa maadili, uadilifu ambao hauwezi kubembelezwa, kusifiwa kwa kupakwa mafuta kwa chupa ya mgongo, kuhongwa, au kutishwa. [MH 498.1; HU Aya ya 4]

Mungu anatamani sisi tutumie kila fursa kwa ajili ya kujipatia maandalizi ya kazi Yake. Yeye Anatutarajia sisi tuweke nguvu zetu zote katika utendaji wa hii kazi na kuweka mioyo yetu hai kwa utakatifu wake na majukumu yake ya kuogopesha. [MH 498.2; HU Aya ya 5]

Wengi wenye stahiki za kufanya kazi bora hutimiza machache kwa sababu wanadiriki machache tu. Maelfu hupita katika safari ya maisha kana kwamba hawana kitu kikubwa cha kuishi kwacho, hawana kiwango cha juu cha kufikia. Sababu moja ya jambo hili, ni kuwa wamejiwekea makadirio binafsi, ya chini. Kristo alilipa bei isiyo na kikomo kwa ajili yetu, na kulingana na bei ambayo Yeye aliilipa, anatamani kwamba na sisi tutajithamini wenyewe. [MH 498.3; HU Aya ya 6]

Usiridhike kukifikia kiwango kilicho chini kabisa. Sisi hatujafikia vile tunavyoweza kuwa, au vile ambavyo tunapaswa kuwa kutokana na mapenzi ya Mungu. Mungu ametupa sisi uwezo wa kufikiri, nawe usikae bila kujishughulisha au utendaji fulani, au kupotoshwa kwa shughuli za kidunia na zenye maadili machafu na kuchukiza, ila uwezo wetu wa kufikiri uweze kuendelezwa kwa kiwango cha juu kabisa, kilichosafishwa, kilichotakaswa, kilichoboreshwa, na kutumika katika kuendeleza maslahi ya ufalme Wake Mungu. [MH 498.4; HU Aya ya 7]

Hakuna anayepaswa kukubali kuwa mashine tu, inayoendeshwa na akili ya mtu mwingine. Mungu ametupa uwezo, wa kufikiri na kutenda, na ni kwa kutenda kwa uangalifu, tukimtazama Yeye kwaajili ya hekima ndipo tutaweza kubeba mizigo. Simama katika haiba/hulka yako uliyopewa na Mungu. Usiwe kivuli cha mtu mwingine. Tarajia kwamba Bwana atafanya kazi ndani yako, kwako wewe na kupitia kwako. [MH 498.5; HU Aya ya 8]

Kamwe usifikiri kwamba umejifunza vya kutosha, na kwamba sasa unaweza kupumzisha juhudi zako (usibweteke). Akili iliyokuzwa na kupaliliwa ndiyo kipimo cha mtu. Elimu yako inapaswa kuwa endelevu wakati wa maisha yako; kila siku unapaswa kujifunza na kutumia kwa vitendo ujuzi uliopatikana. [MH 499.1; HU Aya ya 9]

Kumbuka kwamba katika nafasi yoyote ambayo unaweza kutumika unadhihirisha nia yako, na kukuza tabia. Haijalishi kazi yako ni ipi,wewe ifanye kwa usahihi na kwa bidii; ondokana na mwelekeo wa kutafuta kazi rahisi. [MH 499.2; HU Aya ya 10]

Roho na kanuni sawa ambazo mtu huleta katika kazi ya kila siku zitaletwa katika maisha yote. Wale wanaotamani kufanya kipande fulani cha kazi kilichomegwa, na kiasi fulani cha mshahara, na wanaotaka kuthibitisha kuwa wanafaa kabisa bila kupitia shida ya kuchukuliana na hali, au kujirekebisha au mafunzo, sio wale ambao Mungu anawaita kufanya kazi katika kusudi Lake. Wale ambao wanajifunza jinsi ya kutoa au kufanya kwa kiasi kidogo tu cha uwezo wao wa kimwili, kiakili, na kimaadili kwa kadri iwezekanavyo, hao sio watendakazi ambao Yeye anaweza kuwamiminia baraka tele. Mfano wao unaambukiza wengine. Maslahi binafsi ndio dhamira kuu inayotawala mioyoni mwao. Wale ambao wanahitaji kusimamiwa na kuangaliwa saa yote na bado hufanya tu jukumu lile ambalo limebainishwa walifanye, sio wale ambao watatangazwa kuwa watumishi wema na waaminifu. Watendakazi wanahitajika wanaodhihirisha nguvu, uadilifu, na bidii, wale ambao wako tayari kufanya chochote kinachohitajika kufanywa. [MH 499.3; HU Aya ya 11]

Wengi wanakuwa hawana ufanisi kwasababu wanakwepa majukumu kwa kuogopa kushindwa. Hivyo wanashindwa kupata elimu hiyo inayotokana na uzoefu, na ambayo kusoma/kisomo na kujifunza na faida zote zinazopatikana vinginevyo haziwezi kuwapa. [MH 500.1; HU Aya ya 12]

Mwanadamu anaweza kuumba hali (kushepu mazingira), lakini mazingira hayapaswi kumuumba mtu. Tunapaswa kuchukua hali iliyopo kama vyombo vya kufanyia kazi. Tunapaswa kutawala hali, na wala tusiruhusu hali au mazingira kututawala sisi. [MH 500.2; HU Aya ya 13]

Watu wenye nguvu ni wale ambao wamepingwa, wamechanganyikiwa, na kuzuiwa. Kwa kuziita nguvu zao na kuziwekeza katika utendaji, vizuizi wanavyokutana navyo vinawathibitishia baraka chanya. Wanapata uwezo wa kujitegemea. Migogoro na mifadhaiko huimarisha misuli ya imani, yaani kumtumaini Mungu na uthabiti huo unaokuza uwezo wa mtu. [MH 500.3; HU Aya ya 14]

Kristo hakutoa huduma yoyote yenye ubahili au yenye upungufu. Hakuipima kazi Yake kwa kutumia saa. Wakati Wake, moyo Wake, nafsi Yake na nguvu, vilitolewa kufanya kazi kwa manufaa ya wanadamu. Katika siku za uchovu alihenyeka/alijitaabisha, na kwa usiku mrefu aliinama katika maombi kwa ajili ya neema na uvumilivu ili afanye kazi kubwa zaidi. Kwa vilio vikali na machozi, Alituma maombi Yake mbinguni, ili asili Yake ya ubinadamu iweze kuimarishwa, ili Awezeshwe kustahimili anapokutana na adui mjanja katika matendo yake yote ya udanganyifu, na kuimarishwa kutimiza utume Wake wa kuuinua ubinadamu. Kwa watenda kazi Wake anasema, “Nimewapa kielelezo, ili nanyi mfanye kama Mimi nilivyofanya.” Yohana 13:15. [MH 500.4; HU Aya ya 15]

“Upendo wa Kristo,” asema Paulo, “hutubidisha.” 2 Wakorintho 5:14. Hii ndiyo ilikuwa kanuni inayotumika katika utendaji Wake; ilikuwa nia Yake ya nguvu. Endapo wakati wowote ule bidii yake katika njia ya wajibu ililegalega kwa pungufu ya nukta moja, mtupo mmoja wa jicho kwenye msalaba ulimfanya ajifunge upya viuno vya akili yake na kusonga mbele katika njia ya kujikana nafsi. Katika kazi yake kwa ajili ya ndugu zake alitegemea sana udhihirisho wa upendo usio na kikomo wa dhabihu ya Kristo, pamoja na nguvu yake ya kutiisha, na kubidisha. [MH 500.5; HU Aya ya 16]

Wito wake ni wa dhati kwa kiasi kikubwa, na una mguso mkubwa: “Mnaijua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini Wake. 2 Wakorintho 8:9. Je, tunajua urefu Kristo alioshuka chini, na kina cha urefu cha unyonge alichoshuka. Miguu Yake iliingia kwenye njia ya dhabihu na

haikugeuka kando mpaka alipoutoa uhai Wake. Hakukuwa na pumziko Kwake kati ya kiti cha enzi mbinguni hadi msalabani. Upendo Wake kwa mwanadamu ulimpelekea kukaribisha kila dharau na kujipatia kila teso na dhuluma. [MH 501.1; HU Aya ya 17]

Paulo anatuhimiza 'tusiangalie kila mtu mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine. Anatuagiza tuwe na nia "iliyokuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye Yeye mwanzo alikuwa Yuna namna ya Mungu, Naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; akawa ana mfano wa wanadamu, Naye alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza, akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." Wafilipi 2:4-8. [MH 501.2; HU Aya ya 18]

Paulo alikuwa na shauku kubwa kwamba kufedheheshwa kwa Kristo kunapaswa kuonekana na wanadamu na kutambuliwa. Alikuwa na hakika kwamba ikiwa wanadamu wangeweza kuongozwa kufikiria dhabihu ya kushangaza iliyotolewa na Mkuu wa mbinguni, ubinafsi ungeondolewa mioyoni mwao. Mtume anatembea taratibu toka kipengele baada ya kipengele, ili kwamba kwa kiasi fulani tuweze kupata uelewa wa kujishusha chini kwa ajabu kwa Mwokozi kwa ajili ya wenye dhambi. Anaelekeza akili zetu kwanza kwenye nafasi ambayo Kristo alikuwa nayo mbinguni katika kifua cha Baba Yake; baadaye anamdhihirisha Yeye kama Yule aliyeweka kando utukufu Wake, kwa hiari Yake Mwenyewe, akijiweka chini, hata kufikia hali duni ya maisha ya mwanadamu, akichukua majukumu ya mtumwa, na kuwa mtiifu hadi kifo, na kwamba kile ambacho ni aibu na cha kuchukiza zaidi, kifo cha mateso zaidi kimwili na kiakili--- Kifo cha msalaba. Je, tunaweza kweli kutafakari tukio hili la ajabu la upendo wa Mungu bila kuwa na shukrani na upendo moyoni, kuwa na hisia ya kina ya uhalisia kwamba sisi si mali yetu wenyewe? Bwana kama huyo hapaswi kutumikiwa kwa nia yenye kinyongo, uchoyo au ubinafsi. [MH 501.3; HU Aya ya 19]

"Mnajua," asema Petro, "mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha na dhahabu." 1 Petro 1:18. Lo!, ikiwa hizi fedha na dhahabu zingetosha kununua wokovu wa mwanadamu, basi ingekuwa ni rahisi kiasi gani Kwa Yesu kutimiza jambo hilo la kafara, kwa maana Yeye asema, "Fedha ni Yangu, na dhahabu ni Yangu"! Hagai 2:8. Lakini mwenye dhambi angeweza kukombolewa tu kwa damu ya thamani ya Mwana wa Mungu. Wale ambao, wanakosa kuithamini dhabihu hii ya kushangaza, wanajizuia wenyewe kufanya utumishi wa Kristo, nao wataangamia katika ubinafsi wao. [MH 502.1; HU Aya ya 20]

Kusudi Moja

Katika maisha ya Kristo, kila kitu kilifanywa kuwa chini ya kazi Yake kuu ya ukombozi ambayo alikuja kuikamilisha. Na kujitolea kule kule, kujinyima kule kule na kujidhabihu kule kule, na utii ule-ule kwa madai ya Neno la Mungu, unapaswa kudhihirika/kuonekana kwa wanafunzi Wake. [MH 502.2; HU Aya ya 21]

Kila mtu anayemkubali Kristo kuwa Mwokozi wake binafsi atatamani fursa ya kumtumikia Mungu. Akitafakari kile ambacho mbingu imemfanyia, moyo wake unakuwa unasukumwa kwa upendo usio na kikomo na shukrani ya kumwabudu Mungu. Ana hamu ya kuonyesha shukrani kwa kutumia uwezo wake katika utumishi wa Mungu. Anatamani sana kuonyesha upendo wake kwa Kristo na mali Yake aliyoinunua. Anatamani taabu, shida, na kujidhabihu. [MH 502.3; HU Aya ya 22]

Mfanyakazi wa kweli wa Mungu atafanya yote awezayo, kwa sababu kwa kufanya hivyo anaweza kumtukuza Bwana wake. Atafanya mambo yote kwa usahihi na uadilifu ili kutimiza matakwa ya Mungu. Atajitahidi kuboresha vitivyo vyake vyote, yaani kuboresha kila uwezo wake. Atafanya kila wajibu kama kwa Mwenyezi Mungu. Tamanio lake kuu ni kwamba Kristo apokee heshima, ibada na huduma kamilifu. [MH 502.4; HU Aya ya 23]

Kuna picha inayowakilisha fahali aliyesimama kati ya jembe la plau na madhabahu, yenye maandishi, “Tayari kwa lolote,” Fahali huyu akiwa tayari kufanya kazi katika tuta shambani au kutolewa kwenye madhabahu kwa dhabihu. Huu ndio msimamo wa mtoto wa kweli wa Mungu—aliye tayari kwenda mahali ambapo wajibu unamwita, kujikana nafsi, kujitolea kwa ajili ya kazi ya Mkombozi. [MH 502.5; HU Aya ya 24]

SURA YA 43

UZOEFU WA VIWANGO VYA JUU

Kila mara twahitaji ufunuo mpya na mzuri wa Kristo, uzoefu unaopatana na mafundisho Yake kila siku. Mafanikio ya juu na matakatifu yanapatikana

karibu yetu (mambo yaliyo ndani ya uwezo wetu kufikia). Ujuzi wa daima na ulio endelevu na wema ni kusudi la Mungu kwetu. Sheria Yake ni mwangwi wa sauti Yake Mwenyewe, ikialika wote, “Pandeni juu zaidi. Iweni watakatifu, na mwenye haki na azidi kufanya haki.” Kila siku twaweza kuzidi katika ukamilifu wa tabia ya Kikristo. [MH 503.1; HU Aya ya 1]

Wale wanaojishughulisha katika utumishi kwa Bwana wanahitaji uzoefu wa juu zaidi, wenye kina zaidi, na mpana zaidi, kuliko ambavyo watu wengi bado hawajafikiria kuwa nao. Wengi ambao tayari ni washiriki wa familia kuu ya Mungu wanajua kwa udogo sana, maana ya kuutazama utukufu Wake na kubadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu. Wengi wanao mtazamo hafifu tu wa ubora wa Kristo, na mioyo yao husisimka kwa furaha. Hutamani utambuzi kamili na wa kina zaidi wa upendo wa Mwokozi. Hebu na wathamini kila shauku ya nafsi yenye mwelekeo kwa Mungu. Roho Mtakatifu hufanya kazi pamoja na wale ambao watafanyiwa kazi, Naye huwaumba/ huwafinyanga wale walio tayari kuumbwa, huwatengeneza wale ambao wapo tayari kutengenezwa. Jipeni utamaduni/elimu ya mawazo ya kiroho na ushirika mtakatifu. Ninyi mmeona miale tu ile ya kwanza ya mapambazuko ya utukufu Wake. Na mnapoendelea kumjua Bwana, mtajua kwamba “njia ya mwenye haki ni kama nuru ya mapambazuko, inayozidi kung’aa hadi mchana mkamilifu.” Mithali 4:18. [MH 503.2; HU Aya ya 2]

“Hayo nimewaambia,” Kristo alisema, “ili furaha Yangu ikae ndani yenu, na furaha yenu iwe kamili.” Yohana 15:11. [MH 504.1; HU Aya ya 3]

Kristo daima aliona mbele Zake matokeo ya utume Wake. Maisha Yake ya duniani, yaliyojaa taabu na kujitoa nafsi kikamilifu, yalishangiliwa na wazo kwamba, Yeye hangetoka bure kwa kupitia taabu hii yote. Kwa kutoa maisha Yake kwa ajili ya maisha ya wanadamu, Angerejesha kwenye ubinadamu sura ya Mungu. Angetuinua kutoka mavumbini, akifinyanga upya tabia inayopatana na kielelezo cha tabia Yake Mwenyewe, na kuifanya kuwa nzuri kwa utukufu Wake Mwenyewe. [MH 504.2; HU Aya ya 4]

Kristo aliona taabu ya nafsi Yake na akaridhika. Alitazama anga pana la umilele na kuona furaha ya wale ambao kupitia unyonge Wake wangeweza kupokea msamaha na uzima wa milele. Alijeruhiwa kwa makosa yao/yetu, alichubuliwa kwa maovu yao/yetu. Adhabu ya amani yao/yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake wanadamu sote tumeponywa. Alisikia kelele za waliokombolewa. Aliwasikia wale waliokombolewa wakiimba wimbo wa Musa na Mwana-Kondoo. Ingawa ubatizo wa damu ulikuwa ni lazima upokelewe kwanza, ingawa dhambi za ulimwengu zingeilemea nafsi Yake isiyo na hatia, ingawa kivuli cha janga lisiloneneka kilikuwa juu Yake; lakini kwa ajili ya

furaha iliyowekwa mbele Yake, Yeye alichagua kustahimili msalaba na kuidharau aibu. [MH 504.3; HU Aya ya 5]

Furaha hii, wafuasi Wake wote, wanapaswa kuishiriki. Haijalishi jinsi ukubwa wa utukufu utakavyokuwa baada ya hapa, thawabu yetu haijaifadhiwa kwaajili tu, ya wakati wa ukombozi wa mwisho. Hata hapa tulipo sasa, kwa imani tunapaswa kuingia katika furaha ya Mwokozi. Kama ilivyokuwa kwenye uzoefu wa Musa, sisi nasi pia, tunapaswa kustahimili kama wale wamwonao Yeye Asiyeonekana (Ebra 11:27). [MH 504.4; HU Aya ya 6]

Sasa kanisa liko vitani, likipigana. Sasa tunakabiliwa na ulimwengu ulio gizani, ni karibu ujitolee kabisa kwa ibada ya sanamu. Lakini siku inakuja ambapo vita vitakuwa vimepiganwa, na ushindi kupatikana (washindi watakuwa wameshinda). Mapenzi ya Mungu yatatimizwa hapa duniani kama vile yanavyotimizwa huko mbinguni. Mataifa ya waliookolewa hawatajua sheria nyingine isipokuwa sheria ya mbinguni. Wote watakuwa familia yenye furaha na umoja, watavikwa mavazi ya sifa na shukrani—joho la haki ya Kristo. Asili yote, katika uzuri wake upitao kiasi, itamtolea Mungu maneno ya sifa na ibada. Ulimwengu utaoshwa/utaogeshwa kwa maji na nuru ya mbinguni. Nuru ya mwezi itakuwa kama nuru ya jua, na nuru ya jua itakuwa kubwa mara saba kuliko ilivyo sasa. Miaka itasonga mbele kwa furaha. Juu ya tukio hilo, nyota za asubuhi zitaimba pamoja, na wana wa Mungu watapiga kelele kwa shangwe, huku Mungu na Kristo wakiungana pamoja katika kutangaza, “Hakutakuwa na dhambi tena, wala mauti haitakuwapo tena.” [MH 504.5; HU Aya ya 7]

Maono haya ya utukufu ujao, matukio yanayoonyeshwa na mkono wa Mungu, yanapaswa kupendwa na watoto Wake. [MH 506.1; HU Aya ya 8]

Simama kwenye kizingiti cha umilele na usikie makaribisho ya neema yanayotolewa kwa wale ambao katika maisha haya wameshirikiana na Kristo, wakiona kuwa ni upendeleo na heshima kuteseka kwa ajili Yake. Wakishirikiana na malaika, wanatupa taji zao miguuni pa Mkombozi, wakisema, “Anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa kuupokea uweza, na utajiri, na hekima, na nguvu, na heshima, na utukufu, na baraka.... Heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo hata milele na milele.” Ufunuo 5:12, 13. [MH 506.2; HU Aya ya 9]

Huko wale waliokombolewa watawasalimia wale waliowaelekeza kwa Mwokozi aliyeinuliwa. Wanaungana katika kumsifu Yeye aliyekufa ili wanadamu wapate uzima unaolingana na maisha ya Mungu (umilele). Pambano kuu limekwisha. Dhiki na migogoro yote imefikia mwisho wake. Nyimbo za ushindi zinaijaza mbingu yote, wakati wale waliokombolewa wanamesimama kukizunguka kiti cha enzi cha Mungu. Wote wanachukua

chombo chao cha muziki cha nyuzi kwa furaha-yaani kinubi na kuimba, “Anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa” na ametukomboa kwa Mungu. [MH 506.3; HU Aya ya 10]

“Nikatazama, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa mataifa yote, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele ya Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, na mitende katika mikono yao. mikono; wakilia kwa sauti kuu, wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye juu ya kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo. Ufunuo 7:9, 10. [MH 507.1; HU Aya ya 11]

“Hawa ndio wanaotoka katika dhiki iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake; Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena; wala jua halitawapiga, wala hari yoyote. Kwa maana Mwana-Kondoo aliye katikati ya kiti cha enzi atawalisha, Naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uzima, na Mungu atafuta kila chozi katika macho yao.” “Wala mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.” Ufunuo 7:14-17; Ufunuo 21:4. [MH 507.2; HU Aya ya 12]

Twahitaji kuweka mbele yetu daima maono haya ya mambo yasiyoonekana. Ni kwa njia hiyo, ndiyo kwamba tutaweza kuweka thamani ifaayo juu ya mambo ya umilele kwa kulinganisha na mambo ya muda mfupi. Ni kwa kufanya hivi, ndiyo tutapata uwezo wa kuwashawishi wengine kuhusiana na maisha ya juu zaidi. [MH 508.1; HU Aya ya 13]

Kwenye Mlima Pamoja na Mungu

“Njooni Kwangu mlimani,” Mungu anatuamuru. Kwa Musa, kabla hajawa chombo cha Mungu katika kuwakomboa Israeli, aliteuliwa kwa miaka arobaini kuwa na ushirika Naye katika maeneo ya upweke mlimani. Kabla ya kupeleka ujumbe wa Mungu kwa Farao, alizungumza na malaika katika kichaka kilichokuwa kinawaka moto. Kabla ya kupokea sheria ya Mungu kama mwakilishi wa watu Wake, aliitwa mlimani, na kuuona utukufu Wake. Kabla ya kutekeleza haki juu ya waabudu sanamu, alikuwa amefichwa katika ufa wa mwamba, na Bwana akasema, “Nitalitangaza Jina la BWANA mbele yako,” ni “Mwingi wa huruma na fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema. na kweli; ... na hilo halitawaondolea hatia kwa vyovyote.” Kutoka 33:19; 34:6, 7, Kabla hajalala usingizi wa mauti, na maisha yake kumalizika na mzigo wake kwa Israeli kuisha, Mungu alimwita Musa hadi kilele cha Pisga na kuupitisha mbele yake utukufu wa Nchi ya Ahadi. [MH 508.2; HU Aya ya 14]

Kabla wanafunzi hawajaenda kwenye utume wao, waliitwa wapande mlimani pamoja na Yesu. Kabla ya nguvu na utukufu wa Pentekoste kuwasili, ulikuja usiku wa ushirika na Mwokozi, walikutana juu ya mlima katika Galilaya, walikuwa na tukio la kuagana juu ya mlima wa Mizeituni, pamoja na ahadi ya malaika, na siku za maombi na ushirika katika chumba cha juu. [MH 508.3; HU Aya ya 15]

Yesu, alipokuwa akijiandaa kwa ajili ya jaribu kubwa au kazi fulani muhimu, angelikimbilia mahali palipo na upweke wa milima na kulala usiku kucha katika sala kwa Baba Yake. Usiku wa maombi ulitangulia matukio yafuatayo, kuwekwa wakfu kwa mitume na Mahubiri ya Mlimani, kugeuka sura kwa mng'ao, uchungu katika jumba la hukumu na msalaba, na utukufu wa ufufuo. [MH 509.1; HU Aya ya 16]

Upendeleo wa Maombi

Sisi pia, lazima tuwe na nyakati zilizotengwa kwa ajili ya kutafakari na sala na kupokea upya wa roho (burudiko la kiroho). Sisi hatuthamini nguvu na ufanisi wa maombi jinsi tunavyopaswa. Sala na imani zitafanya kile ambacho hakuna mamlaka duniani inaweza kutimiza. Kwa nadra sana sisi tunawekwa katika nafasi inayofanana mara mbili (tukio lenye mfanano mara mbili). Daima tunakuwa na matukio mapya na majaribu mapya tunayopitia, ambayo uzoefu wa zamani hauwezi kutupatia mwongozo wa kutosha. Ni lazima tuwe na nuru endelevu kutoka kwa Mungu. [MH 509.2; HU Aya ya 17]

Daima Kristo anawatumia watu wanaoisikiliza sauti Yake jumbe. Katika ule usiku wa uchungu wa Gethsemane, wanafunzi waliolala hawakuisikia sauti ya Yesu. Walikuwa na hisia ndogo tu ya uwepo wa malaika, hivyo walipoteza nguvu na utukufu wa tukio hilo. Kwa sababu ya kusinzia na kulala kwao walishindwa kupokea uthibithisho ambao ungezitia nguvu na uimara roho zao kwa matukio ya kutisha mbele yao. Ndivyo ilivyo leo kwetu, watu walewale ambao wanahitaji sana mafundisho ya Bwana, ndiyo mara nyingi hushindwa kuyapokea, kwa sababu hawajiweki katika ushirika na mbingu. [MH 509.3; HU Aya ya 18]

Majaribu ambayo tunaanikwa kwayo kila siku hufanya maombi kuwa jambo la lazima na muhimu. Hatari huzunguka kila njia. Wale wanaotafuta kuwaokoa wengine kutokana na uovu na uharibifu unaowakabili, hawa ndio wanaokabiliwa haswa na majaribu. Katika kugusana mara kwa mara na uovu, hawa wanahitaji kumshikilia Mungu kwa nguvu ili wao wenyewe wasije kupotoshwa. Hatua fupi na zilizoamuliwa, ndizo ambazo huwaongoza watu chini kutoka juu, wanatoka kwenye eneo takatifu na kushuka hadi ngazi ya chini. Kwa muda mfupi mtu anaweza kufanya maamuzi ambayo huweka

hatima ya mtu milele. Kushindwa mara moja tu katika mapambano ya kuishinda dhambi huiacha nafsi bila ulinzi. Tabia moja mbaya, ikiwa haitapingwa kwa nguvu, itaimarika na kuwa na nguvu ya minyororo ya chuma, na kisha itamfunga mtu mzima (mwili wote utafungwa). [MH 509.4; HU Aya ya 19]

Sababu ya watu wengi kuachwa peke yao katika maeneo ya majaribu ni kwa vile hawamweki Bwana mbele yao daima. Tunaporuhusu ushirika wetu na Mungu kuvunjwa, ulinzi wetu unaondoka kwetu. Sio makusudi yako yote mazuri na nia njema, ndiyo yanayokuwezesha wewe kustahimili uovu. Lazima uwe mwanaume na mwanamke wa maombi. Maombi yako hayapaswi kuwa ya hafifu, yanayozimia, ya hapa na pale, yasiyo thabiti, bali ya dhati, yenye uvumilivu, na ya kudumu. Sio lazima upige magoti kila wakati ili kuomba. Jenga mazoea ya kuzungumza na Mwokozi unapokuwa peke yako, unapotembea, na unapokuwa na shughuli nyingi na katika kazi zako za kila siku. Hebu moyo uinuliwe katika maombi kimyakimya, ukiwa katika kuomba msaada, nuru, nguvu, na ujuzi. Hebu kila pumzi yako iwe maombi. [MH 510.1; HU Aya ya 20]

Kama watenda kazi wa Mungu ni lazima tuwafikie wanadamu pale walipo, watu wamezungukwa na giza, wamezama katika uovu, na wametiwa madoa ya uharibifu. Lakini tunapoziweka akili zetu Kwake Yeye ambaye ni Jua letu na Ngao yetu, uovu unaotuzunguka hautaleta doa hata moja kwenye mavazi yetu. Tunapofanya kazi ya kuokoa roho zilizo tayari kuangamia, hatutaaibishwa ikiwa tutamfanya Mungu kuwa tumaini letu. Kristo moyoni, Kristo maishani, huu ndio usalama wetu. Anga hewa la uwepo Wake itazijaza nafsi zetu chuki kwa yote ambayo ni maovu. Roho yetu itaweza kujitambulisha na Yake kwa ukaribu sana, hivi kwamba katika mawazo na lengo, sisi tutakuwa kitu kimoja Na Yeye. [MH 511.1; HU Aya ya 21]

Ilikuwa ni kwa njia ya imani na maombi kwamba Yakobo, alitoka kwenye hatua ya kuwa mtu dhaifu na mwenye dhambi, na kuwa mkuu na Mungu. Hivyo ndiyo jinsi wewe unavyoweza kuwa mwanaume na mwanamke wa kusudi la juu na takatifu, na lenye maisha ya utukufu, mwanaume na mwanamke ambaye kwa namna yoyote ile hautapindishwa au kuyumbishwa kutoka kwenye Ukweli, haki na uadilifu. Kila mtu anabanwa na mambo ya dharura, mizigo, na majukumu, lakini kwa kadiri nafasi yako inavyozidi kuwa ngumu zaidi na jinsi mizigo yako inavyozidi kuwa mizito zaidi, ndivyo jinsi unavyomhitaji Yesu zaidi. [MH 511.2; HU Aya ya 22]

Ni kosa zito kupuuzia ibada ya hadhara ya Mungu. Upendeleo wa kushiriki katika Ibada Kuu katika utumishi wa Bwana haupaswi kuchukuliwa kwa urahisi (Divine service). Wale wanaowahudumia wagonjwa mara nyingi hawawezi

kuwa katika nafasi ya kujipatia manufaa binafsi ya fursa hii, lakini watu hawa wanapaswa kuwa waangalifu ili wasikosekane katika nyumba ya ibada kwa namna isivyo lazima (kila nyuki ana mzinga, watajua kwamba sisi ni Wakristo kwa mahusiano ya upendo kati yetu). [MH 511.3; HU Aya ya 23]

Katika kuwahudumia wagonjwa, ukilinganisha na shughuli nyingine yoyote ya kidunia, mafanikio yanategemea na roho ya kujiweka wakfu na kujidhabihu kikamilifu katika kufanya kazi hiyo. Wale wanaobeba majukumu wanahitaji kujiweka mahali ambapo watavutiwa sana na Roho wa Mungu. Unapaswa kuwa na tashwishwi kubwa zaidi kuliko watu wengine kuhusiana na msaada wa Roho Mtakatifu na kwa ajili ya maarifa ya Mungu kama nafasi yako, ambayo ni amana, wewe unawajibika zaidi katika nafasi hiyo kuliko zile amana za wengine. [MH 511.4; HU Aya ya 24]

Hakuna kitu kinachohitajika zaidi katika kazi yetu kuliko matokeo ya utendaji yenye ushirika na Mungu. Tunapaswa kuonyesha kwa mitindo ya maisha yetu ya kila siku kwamba tuna amani na pumziko ndani ya Mwokozi. Amani Yake inapokuwa mioyoni mwetu, itang'aa usoni. Nayo itaipa sauti nguvu ya ushawishi. Ushirika na Mungu utainua tabia na maisha. Wanadamu watatufahamu, kama walivyowafahamu wanafunzi wa kwanza, kwamba tumekuwa pamoja na Yesu. Hii itampa mfanyakazi nguvu ambayo hakuna kitu kingine kinachoweza kuiondoa. Uwezo huu, mtu hapaswi kabisa kujiruhusu kupungukiwa nao. [MH 512.1; HU Aya ya 25]

Ni lazima tuishi maisha ya pande mbili—maisha ya fikra, yaani kutumia akili zetu na maisha ya utendaji, na sala ya kimya na ufanyaji kazi wa dhati na bidii. Nguvu inayopatikana kwa njia ya ushirika na Mungu, ikiunganishwa na juhudi ya dhati katika kuzoeza akili iweze yenye kufikiri na kujali wengine, humtayarisha mtu kwa ajili ya majukumu ya kila siku na kuiweka roho katika hali ya amani chini ya hali zote, licha ya changamoto. [MH 512.2; HU Aya ya 26]

Mshauri wa Kimungu/Mbinguni

Wakati wa shida, watu wengi hufikiri kwamba ni lazima wamwite rafiki yao fulani aliye hapa duniani, na kisha wamweleze matatizo yao, na kisha mwamwombe msaada. Katika hali ngumu, kutoamini huijaza mioyo yao, na njia huonekana ina giza. Na wakati huu wote, karibu yao hapo pembeni, amesimama Mshauri mkuu wa zama zote, akiwaalika kuweka tumaini lao Kwake. Yesu, Mbebaji mizigo mkuu, anasema, “Njooni Kwangu, Nami nitawapumzisha.” Je, tugeuke kutoka Kwake na kuwaendea wanadamu wasio na uhakika, na ambao nao wanamtegemea Mungu kama sisi wenyewe tunavyofanya? [MH 512.3; HU Aya ya 27]

Unaweza kuhisi mapungufu ya tabia yako na uwezo wako mdogo, ukilinganisha na ukubwa wa kazi. Lakini hata kama ungekuwa na akili kubwa zaidi kuwahi kutolewa kwa mwanadamu, bado isingetosha kwa kazi yako. “Bila Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote,” asema Bwana na Mwokozi wetu. Yohana 15:5 . Matokeo ya yote tunayofanya yapo mikononi mwa Mungu. Haijalishi kile kinachotokea, wewe mshikilie Yeye kwa ujasiri thabiti na wa kudumu. [MH 513.1; HU Aya ya 28]

Katika biashara yako, katika ushirika na wengine kwenye saa zako za kustarehe, na katika muungano wa maisha, acha mahusiano yoyote unayounda yaingizwe katika maombi ya dhati, na ya unyenyekevu. Kwa njia hiyo utaonyesha kuwa unamheshimu Mungu, Naye Mungu atakuheshimu. Omba ukiwa umekata tamaa. Unapokuwa umekata tamaa, usifungue midomo yako kwa watu; usiweke kivuli kwenye njia ya wengine (kuwapa huzuni au shida); bali umwambie Yesu yote. Inua mikono yako, ili upate msaada. Katika udhaifu wako, ishikilie kwa nguvu ile nguvu isiyokuwa na kikomo. Omba unyenyekevu, hekima, ujasiri, na kuongezewa imani, ili uweze kuona mwanga katika nuru ya Mungu na kufurahia Pendo Lake. [MH 513.2; HU Aya ya 29]

Kuwekwa wakfu; Amini

Tunapokuwa wanyenyekevu na wenye toba moyoni, tunasimama pale ambapo Mungu anaweza kujidhihirisha kwetu, Naye atajidhihirisha kwetu. Yeye Anafurahishwa sana tunapoonyesha matamanio yetu yanayokita Kwake na kusisitiza rehema na baraka Zake kama sababu ya Yeye kutupa baraka kubwa zaidi. Yeye Atawatimizia kwa kuwajibu wote hata kuzidi matarajio yao, watu wale wanaomtumaini Yeye kikamilifu. Bwana Yesu anajua kile ambacho watoto Wake wanahitaji, Je, basi ni kiasi gani cha nguvu hizo na baraka, sisi tutawekeza katika kuwabariki wanadamu wengine; Kwani Naye hutupa sisi sote ili tutumie katika kuwabariki wengine na kuziboresha nafsi zetu. [MH 513.3; HU Aya ya 30]

Ni lazima tuamini kwa udogo tu, kile ambacho sisi wenyewe tunaweza kukifanya, na kuamini zaidi, kile ambacho Bwana anaweza kufanya kwa ajili yetu na kupitia kwetu. Wewe hufanyi shughuli yako mwenyewe; bali unafanya kazi ya Mungu. Salimisha mapenzi yako na njia yako Kwake Bwana. Usijibakize, hata katika nyanja moja, usifanye ridhiano hata moja na nafsi yako mwenyewe, au hata katika kitu kimoja kingine. Elewa ni nini maana ya kuwa huru katika Kristo. [MH 513.4; HU Aya ya 31]

Usikilizaji tu wa mahubiri Sabato baada ya Sabato, usomaji wa Biblia mwanzo mpaka mwisho tena na tena, au maelezo ya ufafanuzi wake mstari kwa mstari, hautatunufaisha sisi, au hata wale wanaotusikia, isipokuwa

tutazileta Kweli hizi za Biblia katika uzoefu wetu binafsi. Ufahamu, nia, na mapenzi, lazima vikabidhiwe kwenye udhibiti wa Neno la Mungu. Kisha kupitia kazi ya Roho Mtakatifu kanuni za Neno la Mungu, zitakuwa kanuni za maisha yetu ya kila siku. [MH 514.1; HU Aya ya 32]

Unapomwomba Bwana akusaidie, mheshimu Mwokozi wako kwa kuamini kwamba unapokea mibaraka Yake. Nguvu zote, hekima yote, ziko chini ya amri yetu. Sisi tunachopaswa kufanya ni kuomba tu. [MH 514.2; HU Aya ya 33]

Tembea daima katika nuru ya Mungu. Tafakari mchana na usiku juu ya tabia Yake. Kisha utaona uzuri Wake na kufurahia wema Wake. Moyo wako utawaka kwenye hisia za upendo Wake. Utainuliwa kana kwamba umebebwa na mikono ya umilele. Kwa nguvu na nuru ambayo Mungu hutoa, unaweza kuelewa zaidi na kutimiza zaidi kuliko vile ulivyowahi kudhani kuwa inawezekana. [MH 514.3; HU Aya ya 34]

“Kaeni ndani Yangu”

Kristo anatuagiza hivi: “Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; hamwezi tena, msipokaa ndani Yangu.... Akaaye ndani Yangu Nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.... Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lolote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba Yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi Wangu.” [MH 514.4; HU Aya ya 35]

“Kama vile Baba alivyonipenda Mimi, Nami nilivyowapenda ninyi; kaeni katika pendo Langu.... [MH 514.5; HU Aya ya 36]

“Si ninyi mlionichagua Mimi, bali ni Mimi niliyewachagua ninyi; Nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mwombalo Baba kwa Jina Langu awapeni.” Yohana 15:4-16. [MH 514.6; HU Aya ya 37]

“Tazama, Mimi nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia Kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.” Ufunuo 3:20. [MH 516.1; HU Aya ya 38]

“Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, Nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya hilo jiwe limeandikwa jina jipya asilolijua mtu ila yeye anayelipokea. Ufunuo 2:17. [MH 516.2; HU Aya ya 39]

“Yeye ashindaye, ... nitampa Nyota ya Asubuhi,” “Nami nitaandika juu yake Jina la Mungu Wangu, na jina la mji wa Mungu Wangu: ... Nami nitaandika juu yake Jina Langu jina jipya.” Mistari ya 26-28; 3:12. [MH 516.3; HU Aya ya 40]

“Jambo Hili Moja Ninafanya”

Yeye ambaye tumaini lake liko kwa Mungu atakuwa anaenda sambamba pamoja na Paulo katika kusema, “Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.” Wafilipi 4:13. Haijalishi makosa au kushindwa kulikotokea wakati uliopita, tunaweza, kwa msaada wa Mungu, kuyashinda yote. Pamoja na mtume, isis tunaweza kusema: [MH 516.4; HU Aya ya 41]

“Natenda neno hili moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. Wafilipi 3:13, 14. [MH 516.5; HU Aya ya 42]

Ufanisi Wa Kazi Ya Umishonari Wa Matibabu Ni Kuwaelekeza Watu Kwa Yesu

Bonasi Ya Jumbe Kutoka Loma Linda

(Loma Linda Messages)

Mipango ya Kazi ya Umishonari ya Kitabibu

Vijana walio na ujuzi wa kivitendo wa jinsi ya kuwatibu wagonjwa, sasa watatumwa kufanya kazi ya umishenari wa tiba ya injili, kuhusiana na wahudumu wenye uzoefu zaidi wa injili. Ikiwa vijana hawa watajitolea kujifunza Neno, watakuwa wainjilisti wenye mafanikio. Wahudumu ambao hawa vijana wanafanya kazi pamoja nao wanapaswa kuwapa nafasi ileile ya kujifunza ambayo Eliya alimpa Elisha. Wanapaswa kuwaonyesha jinsi ya kuwafundisha wengine Kweli. Inapowezekana vijana hawa wanapaswa kutembelea hospitali, na katika kesi zingine wanaweza kuungana nao kwa muda, wakifanya kazi bila kujali. Mfano safi kabisa wa kutokuwa na ubinafsi sasa unapaswa kuonyeshwa na wahudumu wetu wa umishenari wa tiba. Kwa ujuzi na uzoefu unaopatikana kwa kazi ya vitendo, wanapaswa kwenda kuwatibu wagonjwa. Wanapoenda nyumba kwa nyumba, watapata ufikiaji wa mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao vinginevyo hawangesikia ujumbe wa injili. LLM 69.3

Mengi mazuri yanaweza kufanywa na wale ambao hawana masomo ya udaktari, na walioidhinishwa kikamilifu. Wengine wanapaswa kuwa tayari kufanya kazi kama madaktari wenye uwezo. Wengi, wakifanya kazi chini ya maelekezo ya watu kama hao, wanaweza kufanya kazi zinazokubalika bila kutumia muda mrefu sana katika kujifunza kama ilivyofikiriwa kuwa ni lazima kutumia hapo awali. LLM 69.4

Wengi wataenda kufanya kazi kama Mwalimu ambaye hawajaweza kuchukua kozi ya kawaida ya masomo shuleni (untrained teacher). Mungu atawasaidia watendakazi hawa. Watapata maarifa kutoka kwa shule ya upili, nao watafaa kuchukua nafasi zao katika safu na faili za wafanyikazi kama wauguzi. Mmishenari mkuu wa tiba anaona kila juhudi inayofanywa kupata ufikiaji wa roho kwa kuwasilisha kanuni za matengenezo ya afya. LLM 69.5

Mabadiliko yaliyoamuliwa yanafanyika katika ulimwengu wetu. Bwana ametangaza kwamba atageuka na kupindua. Wanaume wanyenyekevu, ambao hadi sasa wamekuwa katika giza, lazima sasa wapewe nafasi ya kuwa wafanyakazi. LLM 70.1

Kwa wale wanaotoka kufanya kazi ya umishonari wa tiba, ningesema, Mtumikie Bwana Yesu kwa ufahamu uliotakaswa, kuhusiana na wahudumu wa

injili na Mwalimu mkuu. Yeye ambaye amekupa utume wako atakupa ujuzi na ufahamu unapojiweka wakfu kwa utumishi Wake, ukijishughulisha kwa bidii katika kazi na masomo, ukifanya yote uwezayo kuleta kitulizo kwa wagonjwa na wanaoteseka. LLM 70.2

Kwa wale ambao wamechoshwa na maisha ya dhambi, lakini ambao hawajui wapi pa kugeukia ili kupata kitulizo/afueni, mwasilishe Mwokozi mwenye huruma, aliyejaa upendo na huruma kwao, akitamani kuwapokea wale wanaomjia kwa mioyo iliyovunjika na roho iliyotubu. Wachukue kwa mkono, wainue, sema nao maneno ya matumaini na ujasiri. Wasaidie kuushika mkono Wake Yeye aliyesema, “Na azishike nguvu Zangu, apate kufanya amani Nami, naam afanye amani nami.” LLM 70.3

“Tazama,” Kristo atangaza, “Naja upesi; na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo." Mungu anatuita sisi kutamka Maneno, “Amina! Njoo Bwana Yesu.” Mungu atafanya mengi zaidi kwa watu Wake ikiwa watakuwa na imani Kwake. Ukafiri unanyemelea nje ya nchi kupitia ardhini. Shetani ameweka mipango yake ya kudhoofisha imani yetu katika historia na kusudi la kazi ya Mungu. Niko makini sana ninapoandika haya. Shetani anafanya kazi na watu walio katika vyeo maarufu ili kufagilia mbali misingi ya imani yetu. Je, turuhusu hili lifanyike, ndugu? LLM 70.4

Nafsi yangu imesisimka ndani yangu. Nitamtumaini Mungu kwa moyo na roho. Nitatangaza ujumbe ambao amenipa niutangaze. Ninashuhudia katika Bwana kwamba vijana wetu wasihimizwe kwenda Battle Creek kufanywa kuwa makafiri. Mungu atatusaidia tuone ni nini kifanyike ili kuzuia hili. Sasa tunapaswa kufanya kazi kwa bidii na akili, katika kuwaokoa vijana wetu dhidi ya kuchukuliwa mateka na adui. LLM 70.5

*****

Ndipo wataweza kuona kwa macho ya upako wa Roho mtakatifu, jinsi kazi ya umishenari wa tiba inavyounganishwa kwa ukaribu na utangazaji wa ujumbe wa wakati huu. LLM 70.6

Bwana amewasilisha mbele yangu hatari zinazowatishia watu Wake walio na kazi takatifu ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu kwa uwazi na udhahiri. Watu wa Mungu wanapaswa kujihadhari wasije wakanaswa na mapendekezo yasiyotakaswa. Vijana wetu hawapaswi kuwekwa mahali ambapo watapotoshwa na hisia zisizo sahihi. Ukweli sio wa kufumbiwa macho. Ujumbe wa siku hizi za mwisho haupaswi kutolewa kwa maneno yasiyo wazi. LLM 70.7

*****

Kazi ya Umishenari wa tiba ingali changa. Maana ya kazi halisi ya umishenari wa tiba inajulikana na watu wachache. Kwa nini?—Kwa sababu pesa za Mungu zimetumiwa vibaya. Kazi za vitendo vya uinjilisti inafanywa. Wanaume na wanawake ambao wanapaswa kuwa shambani kama wamisionari wa tiba ili kusaidia wale wanaoshughulika na huduma ya injili, wanakusanywa hapo Battle Creek, wakisimamia mpango ule ule ambao umetekelezwa hapo awali, wakifunga majeshi, na kuwafunga. katika sehemu moja. Mungu amesema dhidi ya hili kwa kutuma hukumu Zake kwenye taasisi katika Battle Creek. Lakini kila harakati kwa upande wa wale wanaotii maonyo, ili wabadili mpangilio wa mambo, imefanywa kuwa ngumu sana na maoni potofu ya wengine kuhusu njia ambayo kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuendelezwa. LLM 71.2

Mungu hajatupa kazi ya kujenga nyumba kubwa za sanitarium ili zitumike kama vituo vya afya kwa wote wanaokuja. Wala si kusudi Lake kwamba wamishenari wa tiba watumie muda mrefu chuoni kabla hawajaingia shambani. Wacha vijana wa kiume na wa kike wanaoijua kweli waende kazini, si mahali ambapo Kweli imetangazwa tayari, bali mahali ambapo hawajasikia ujumbe, na watu hawa wafanye kazi kama wahubiri na wainjilisti. Waalimu wa vijana hawa wawaondoe mahali ambapo Mungu ameonyesha kwa hukumu Zake kwamba hawapaswi kuwa... LLM 71.3

Wanaume na wanawake wengi watakuja (kwenye Sanitarium mpya mjini Battle Creek) ambao si wagonjwa kabisa. Wafanyakazi watahitajika kuwahudumia. Lakini hii sio kazi ambayo Mungu amewapa wamishenari Wake wa tiba. Jukumu letu limetolewa kwetu na Mmshenari mkuu wa tiba ambaye ulimwengu huu umepata kumwona. Akiwa amesimama hatua chache tu kutoka kwenye kiti cha enzi cha Baba Yake, Kristo aliwaambia wanafunzi wake, LLM 71.4

“Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.” Hakuwaambia waanzishe seminari huko Yerusalemu, na wakusanye pamoja wanafunzi kufundishwakatika darasa la juu zaidi. “Enendeni ulimwenguni mwote,” Alisema, “mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe,” “na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” LLM 71.5

Msiwakusanye pamoja wale ambao Mungu amewapa utume huu, na kuwafanya waamini kwamba inawapasa kukaa miaka mingi chuoni ili kupata mafunzo kwa ajili ya kazi ya Bwana. Kuwapo kwa Kristo kuna thamani zaidi kuliko miaka ya mafunzo. Hebu vijana wetu wawe chini ya nira ya Kristo, na kwa imani waende mbele kama wamisionari wa tiba wa injili, wakichukua

pamoja nao ahadi, “Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Waende wawili wawili, wakimtegemea Mungu, si mwanadamu, kwa hekima yao na mafanikio yao. Acha wayachunguze Maandiko, na kisha watoe Kweli za Neno la Mungu kwa wengine. Waongozwe na kanuni ambazo Mungu ameweka. LLM 72.1

Hebu wahudumu wetu ambao wamepata uzoefu katika kuhubiri Neno wajifunze jinsi ya kutoa tiba sahili, na kisha waende kama wainjilisti wamishenari wa tiba. LLM 72.2

Wafanyakazi,—wamishenari wa tiba wa injili—wanahitajika sasa. Hatuwezi kumudu kutumia miaka mingi katika maandalizi. Hivi karibuni milango iliyofunguliwa kwa Ukweli itafungwa milele. Beba ujumbe sasa. Usisubiri, kuruhusu adui kuchukua milki ya mashamba yaliyo sasa wazi mbele yako. Acha vikundi vidogo viende kufanya kazi ambayo Kristo aliwateua wanafunzi Wake. Acheni wafanye kazi kwa bidii kama waeneza-injili, wakitawanya machapisho yetu, kuzungumza juu ya Kweli na wale wanaokutana nao, wakiwaombea wagonjwa, na ikihitajika, wawatibu, si kwa dawa za kulevya au za famasia, bali kwa tiba za asili. Watenda kazi wakumbuke daima kwamba wanamtegemea Mungu. Wasiwategemee wanadamu ili wapate hekima, bali wamtumaini Yeye asemaye, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.” Hivyo tulifanya kazi katika historia ya mapema ya ujumbe.” LLM 72.3

*****

Kutokana na nuru ambayo nimepewa, kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili havipaswi kutenganishwa kamwe. Zinapaswa kuunganishwa pamoja kama kazi moja. Kristo Ndiye Kichwa cha mwili—Kanisa, na tunapaswa kufanya kazi kwa umoja pamoja Naye. Akirejelea uhusiano wetu Naye, mtume anasema, “Sisi tu watendakazi kazi pamoja na Mungu.” LLM 72.4

Katika siku za Kristo hapakuwa na nyumba za sanitarium katika Nchi takatifu ya Israeli. Lakini popote alipokwenda, Yeye Mwenyewe alikuwa sanitarium. Tabibu Mkuu alibeba pamoja Naye uwezo wa uponyaji ambao ulikuwa ni tiba ya kila ugonjwa, wa kiroho na kimwili. Aliwapa afueni wale waliokuwa chini ya nguvu za adui, akawaponya magonjwa na udhaifu wao.... LLM 72A.1

Katika kufanya kazi ya umishenari wa tiba tutakutana na upinzani uleule ambao Kristo alikutana nao. Anatangaza hivi: “Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; Watakapowaudhi katika mji huu, kimbilieni mwingine; kwa maana, amin, nawaambia, Hamtaimaliza miji ya Israeli, hata ajapo Mwana wa Adamu. LLM 72A.2

Tunapaswa kuwafundisha wengine jinsi ya kupata uzima wa milele. Na tunapaswa kukumbuka daima kwamba ufanisi wa kazi ya umishenari wa tiba ni katika kuwaelekeza wanaume na wanawake wagonjwa kwa Yesu. Tunapaswa kuwaita "wamtazame Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." LLM 72A.3

Maisha ya Kristo na huduma Yake kwa watu wanaoteseka yanaunganishwa bila kutenganishwa. Na leo Yeye ni Tabibu Yule Yule Mwenye huruma. Tunapaswa kuwaruhusu wote wanaoteseka waelewe kwamba ndani Yake mna zeri ya uponyaji kwa kila ugonjwa, kurejesha nguvu kwa kila udhaifu. LLM 72A.4

Ulimwengu umejitenga mbali na kanuni za Kweli za urejesho na afya. Tamaa iliyopotoka na shauku za kuelekea chini zimechukua udhibiti wa akili za wengi. Mara nyingi mwelekeo wa kukasirika huimarishwa na kupaliliwa. Hasira mbaya, kuthaminiwa, huharibu mitazamo dhaifu, safi, takatifu ya roho. Shetani anatamani kutufanya tuhangaike na kunyanyaswa kwa mambo madogo tu, ili tusahau mambo mazito yanayohusu ustawi wetu wa milele. LLM 72A.5

Bwana anatamani kila mtu afanye sehemu yake kwa ubora. Unaweza kufikiri kwamba unaweza kufanya kidogo sana; lakini kumbuka kwamba katika mfano wa talanta, Kristo hakuwakilisha watumishi wote kupokea kiasi kile kile. Mtumishi mmoja alipewa talanta tano; kwa mwingine, wawili, na kwa mwingine, mmoja. Ikiwa una talanta moja tu, itumie kwa busara, ukiongeza kwa kuipeleka kwa wabadilishanaji. Fanya uwezavyo kurudisha nyuma wimbi la magonjwa na mateso ambalo linaenea katika ulimwengu wetu. Njooni kwa msaada wa Bwana, kwa msaada wa Bwana dhidi ya nguvu kuu za giza-Waamuzi 5:23. LLM 72A.6

Kazi hii ya zahanati ya tiba ambayo Ndugu Sadler ametueleza, ni sawa na kazi tuliyofanya huko Australia. Tulipokuwa Cooranbong, hapakuwa na tabibu kwa umbali wa maili nyingi kutoka kwetu; na muuguzi wangu, mwanamke mwenye uzoefu katika kutibu wagonjwa, alitenda nafasi ya daktari katika jumuiya yetu. Aliitikia miito mingi, akisafiri kutoka mahali hadi mahali na kufanya kazi ambayo Mungu anataka wengine wengi wafanye. Katika kazi hii, wengine hawawezi kufanya mengi kama wengine, lakini kila mmoja anapaswa kufanya awezavyo ili kuondoa mateso. Mungu anataka kila mmoja wa watoto Wake awe na akili na maarifa, ili kwa nguvu utukufu Wake udhihirishwe katika ulimwengu wetu kwa wazi kabisa. LLM 72B.1

*****

Katika kazi ya umishenari wa tiba lazima kuwe na matamanio zaidi ya roho za watu. Shauku hii ndiy iliyojaza mioyo ya wale walioanzisha taasisi yetu ya

kwanza ya tiba. Kristo anapaswa kuwepo katika chumba cha wagonjwa, akiujaza moyo wa daktari harufu ya upendo Wake. Wakati maisha yake yanapokuwa hivi kwamba Kristo anaweza kwenda pamoja naye kwenye kando ya kitanda cha wagonjwa, kutawajia usadikisho kwamba Yeye, Mwokozi Mwenye huruma, Yuko, na usadikisho huo utafanya mengi kuwarudishia afya zao. LLM 72B.2

Kwa maneno na vitendo waganga na wauguzi katika taasisi zetu za tiba wanapaswa kusema, kwa uwazi sana, kiasi kwamba haiwezi kueleweka vibaya, "Mungu Yuko mahali hapa," kuokoa, sio kuharibu. Kristo anawaalika waganga wetu kumfahamu. Wanapoitikia mwaliko Wake, watajua kwamba wanapokea mambo wanayoomba. Akili zao zitaangazwa na hekima itokayo juu. Wakimtazama Mwokozi mara kwa mara, watafanana kama Yeye zaidi na zaidi, hadi mwishowe inaweza kusemwa juu yao katika nyua za mbinguni, “Ninyi mmetimilika katika Yeye.” Kristo amejitolea kuwapa wanafunzi Wake kile wanachoomba kwa Jina Lake. Wanapofanya kazi kwa kupatana Naye, wanaweza kumwomba Yeye kuwasaidia katika kila wakati wa hitaji. LLM 72B.3

*****

Soma sura ya nane ya Mathayo, na ujifunze kutoka kwayo jinsi Kristo alivyounganisha huduma ya Neno na kazi ya umishenari wa tiba. Jifunze mbinu za Mponyaji mkuu, na fanya kazi kama alivyofanya kazi. LLM 73.1

*****

Wale wanaodai kuwa wamishenari wa tiba wanapaswa kuwekwa wakfu, wakifanya kazi kwa ajili ya maslahi ya ulimwengu, lakini hawajanaswa na hila za ulimwengu. Bwana anataka uwe chombo cha heshima... LLM 73.2

Maneno yafuatayo yanaeleza kwa muhtasari kazi ya Kweli ya umishenari wa injili,—kazi ambayo wote watashiriki wale ambao wameongoka kikweli: (Ona MS. kwa Maandiko mengi.) LLM 73.3

*****

Wafanyakazi wa kimishenari wa tiba wanahitajika katika uwanja wa Kusini mwa nchi, ambao wanaweza kushiriki katika kazi ya Sanitarium. Sanitarium zinahitajika, ambazo mafanikio ya kazi ya tiba na upasuaji inaweza kufanyika. Taasisi hizi, zinazoendeshwa kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu, zingeondoa ubaguzi, na kufanya kazi yetu ionekane vizuri. Lengo kuu la watendakazi katika taasisi hizi ni kuwa na afya ya kiroho ya wagonjwa. Kazi ya uinjilisti yenye mafanikio inaweza kufanywa kuhusiana na kazi ya umishenari wa tiba.

Ni jinsi mistari hii ya kazi inavyounganishwa ndipo tunaweza kutarajia kukusanya tunda la thamani zaidi kwa Bwana. LLM 73.4

Kutokana na maagizo ambayo Bwana amenipa mara kwa mara, ninajua kwamba kunapaswa kuwa na watendakazi wanaofanya safari za uinjilisti wa tiba kati ya miji na vijiji. Wale wanaofanya kazi hii watakusanya mavuno mengi ya roho, kutoka kwenye tabaka za juu na za chini. Njia ya kazi hii imeandaliwa vyema zaidi na juhudi za mwinjilisti wa vitabu. LLM 73.5

Wengi wataitwa shambani kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba, kusoma Biblia, na kusali pamoja na wale wanaopendezwa. LLM 73.6

Ni muhimu sana kuwepo na maelewano katika taasisi zetu. Afadhali kazi ilemae kuliko watendakazi ambao hawajajitolea kikamilifu kuajiriwa. Ni wale ambao hawajawekwa wakfu, ambao hawajaokoka ambao wamekuwa wakiharibu kazi ya Mungu. Bwana hana matumizi yoyote kwa watu ambao hawajajiweka wakfu kabisa kwa utumishi Wake. LLM 73.7

Mioyo na maslahi ya watenda kazi wa Mungu yanapaswa kuwa kitu kimoja. Watenda kazi wanapaswa kufungwa pamoja na Kristo, na kuheshimiana wao kwa wao ni jambo la juu kwa ajili ya kazi yao… LLM 73.8

*****

Kazi iliyoamuliwa zaidi inahitaji kufanywa katika makanisa yetu huko Michigan. Kumekuwa na ukosefu wa ushirikiano na vitendo vyenye upatanifu, lakini ikiwa nyote mtafuata kwa uthabiti mistari ya Biblia, badiliko litafanyika katika makanisa..... LLM 74.1

Ninatumaini kwamba sasa, kuliko wakati mwingine wowote, ninyi nyote,—wahudumu na washiriki wa kanisa—mtakuja kwa msaada wa Bwana, kwa msaada wa Bwana dhidi ya nguvu kuu za giza (Waamuzi 5:26). Lakini nimeandika mambo mengi sana kwamba sihitaji kuwaandikia kwa sehemu kubwa. Nitauliza kwa nini baadhi ya ndugu zetu wachungaji wako nyuma sana katika kutangaza mada iliyotukuka ya kiasi (temperance)? Kwa nini, nia kubwa zaidi haionyeshwi katika matengenezo ya afya? Kuna wengi wanaolisha na kuiweka hai chuki ya mara kwa mara dhidi ya Dk. Kellogg. Daktari huyu anafanya kazi kubwa. Kwanini watu hawa wasijaze nafasi zao katika huduma pia, kwa bidii kama vile yeye anajaza nafasi yake? Kwa nini wahudumu wa makanisa yetu hawafanyi kazi ile ile ambayo ilipaswa kufanywa miaka mingi iliyopita? Ninafurahi kwamba mtu fulani amechukua kazi ambayo imepuuzwa sana. LLM 74.2

Malalamiko yanakuja kwa viongozi kwamba Dk. Kellogg amekusanya vijana wote anaoweza kupata, na kwa hiyo sisi hatuna watendakazi. Lakini hili ndilo

jambo bora zaidi ambalo lingeweza kufanywa kwa vijana na kazi. (Wakati huo, kama 1898, nadhani.) Hebu tuchunguze tarehe kama hizo kwa uangalifu, ili tusichanganywe na Shetani. Muda mfupi baada ya habari hizo hapo juu kuandikwa, Dada White aliona ni muhimu kutoa shauri dhidi ya kuwapeleka vijana Battle Creek kwa sababu kazi ilikuwa kubwa sana na Dakt. Kellogg alifundisha makosa mengi yaliyochanganyika na mwanga mwingi (pantheismu nk).— Copyist, ERP) LLM 74.3

Kwako, (maneno hayapo kwenye ukurasa) kama Mwenyekiti wa General Konferensi, na kwa Ndugu Evans, Rais wa Jumuiya ya Konferensi Kuu, na kwa Ndugu Durland, kama Rais wa Kongamano la Michigan, ningesema, Endelea kufanya kazi kwa busara na kwa hekima. Pata baadhi ya hawa vijana wa kiume na wa kike kufanya kazi makanisani. Unganisha kazi ya umishenari wa tiba na tangazo la ujumbe wa malaika wa tatu. Fanya juhudi za mara kwa mara, zilizopangwa ili kuyainua makanisa kutoka katika kiwango kilichokufa ambacho yamekuwa humo kwa miaka mingi. Tuma wahudumu wa makanisa ambao wataweka kanuni za matengenezo ya afya mbele kwa kila kanisa huko Michigan. Utaona jinsi pumzi ya uhai itakavyoingia katika makanisa haya. LLM 74.4

Kipengele kipya kinahitaji kuletwa kwenye kazi. Watu wa Mungu lazima wapokee maonyo, na kufanyia kazi roho pale walipo; kwa maana watu hawatambui hitaji lao kuu na hatari. Kristo aliwatafuta watu mahali walipo, na kuweka mbele yao Kweli kuu kuhusu ufalme Wake. Alipoenda kutoka mahali hadi mahali, Aliwabariki na kuwafariji walioteseka, na kuwaponya wagonjwa. Hii ni kazi yetu. Mungu angetaka tuwasaidie wasio na mahitaji. Sababu ya kwamba Bwana haonyeshi uwezo Wake kwa kudhamiria zaidi ni kwa sababu kuna hali ya kiroho ndogo sana miongoni mwa wale wanaodai kuuamini Ukweli. LLM 74.5

Katika ulimwengu wetu kuna wafanyakazi wengi Wakristo ambao bado hawajasikia Kweli kuu na za ajabu ambazo zimetujia. Hawa wanafanya kazi nzuri, kwa mujibu wa nuru waliyo nayo, na wengi wao wameendelea zaidi katika elimu, na kazi ya vitendo kuliko wale ambao wamekuwa na nuru kubwa na fursa kubwa. LLM 75.1

Kutojali miongoni mwa wahudumu wetu kuhusiana na matengenezo ya afya na kazi ya umishenari wa tiba , inashangaza. Hata wale ambao ambao hawadai kuwa Wakristo wanalitendea somo hilo kwa heshima kubwa kuliko baadhi ya watu wetu wenyewe, na wanatangulia mbele yetu. Neno nililopewa kwa ajili yako ni, “Nenda mbele.” “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; na

kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari....” LLM 75.2

Ndugu. Irwin, shikilia kazi ya mageuzi ya afya. Ikiwa yeyote kati ya wahudumu ana wazo kwamba kazi ya umishenari wa tiba inazidi kuwa ngumu, acha wachukue wanaume ambao wamekuwa wakifanya kazi katika safu hizi pamoja nao kwenye nyanja zao za kazi, wawili hapa na wawili pale. Hebu wahudumu wawapokee wamishenari hawa wa tiba kama wangempokea Kristo, na kuona ni kazi gani wanaweza kufanya. Sidhani kama watawaona vijana katika uzoefu wa kidini kama waliokuwa nao. Angalia kama kwa njia hii, huwezi kuleta baadhi ya mkondo muhimu wa mbinguni kwenye makanisa. Angalia kama hakuna tabaka ambalo litashika elimu wanayohitaji sana, na uone kama hawatatoa ushuhuda, “Lakini Mungu, ambaye ni mwingi wa rehema, kwa upendo Wake mkuu aliotupenda sisi, hata tulipokuwa wafu katika dhambi, alituhuisha pamoja na Kristo, (si mbali na Kristo), (mmeokolewa kwa neema) akatufufua pamoja Naye, akatuketisha pamoja (si katika atomi za kujitegemea) katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu. ” LLM 75.3

*****

Katika kazi yetu ya Washington, madaktari wenye busara, wenye uwezo, wasimamizi bora, na wauguzi walio na sifa bora zaidi watahitajika. Vijana wenye bidii, waliojitolea pia watahitajika, kuingia kazini kama wauguzi. Vijana hawa wa kiume na wa kike wataongezeka uwezo wanapotumia kwa uangalifu ujuzi wanaopata, na watakuwa bora na wenye kustahili kuwa mkono wa msaada wa Bwana. Wanaweza kuwa wamishenari waliofaulu, wakielekeza roho kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu, na ambaye ufanisi Wake wa uponyaji unaweza kuokoa roho na mwili. LLM 75.4

Bwana anataka wanaume na wanawake wenye hekima, wakitenda kazi kama wauguzi, kuwafariji na kuwasaidia wagonjwa na wanaoteseka. Kupitia huduma za wauguzi hawa, wale ambao hapo awali hawajapendezwa na mambo ya kidini wataongozwa kuuliza, “Nifanye nini ili nipate kuokolewa?” Wagonjwa wataongozwa kwa Kristo kwa usikivu na subira za wauguzi wanaohudumia mahitaji yao, na ambao huinama kwa sala na kumwomba Mmishenari mkuu wa tiba umtazame mgonjwa kwa huruma, na kuruhusu mvuto wa neema Yake usikike na kurejesha nguvu kutekelezwa. Laiti wote walio wagonjwa na wanaoteseka wangeweza kuhudumiwa na matabibu na wauguzi wanaofanana na Kristo, ambao wangewasaidia kuiweka miili yao iliyochoka, na yenye maumivu makali chini ya uangalizi wa Mponyaji mkuu, kwa imani wakimtazamia kwa urejeshwaji. LLM 75.5

Woga wa neva za wagonjwa utashindwa wanapofahamishwa na shauku kubwa ambayo Mwokozi anayo kwa wanadamu wote wanaoteseka. Ee, Ni kina cha upendo mkubwa kiasi gani, alicho nacho Kristo! Ili kutukomboa kutoka kwa kifo, alikufa msalabani wa Kalvari. LLM 76.1

Hebu waganga wetu na wauguzi daima wakumbuke Maneno, “Sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu.” Hebu kila daktari na kila muuguzi ajifunze jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya kupunguza mateso ya kiakili na kimwili. Kwa wakati huu, wakati dhambi imeenea sana na kufunuliwa kwa ukali sana, ni muhimu jinsi gani kwamba huduma zetu za sanitarium zifanywe kwa njia ambayo zitatimiza kiasi kikubwa cha wema. Ni muhimu sana kwamba watendakazi wote katika taasisi hizi wajue jinsi ya kunena neno kwa wakati kwa wale waliochoka na wagonjwa. LLM 76.2

Madaktari na wauguzi wanapaswa kuwa wenye fadhili na furaha, wakiondoa huzuni na sikitiko zote. Hebu imani ishike mkono wa Kristo kwa mguso Wake wa uponyaji... LLM 76.3

Wauguzi wetu wanapowahudumia wagonjwa wa mwili na roho kwa subira, wamuombe Mungu awafanyie kazi wanaoteseka, wapate kuongozwa kumjua Kristo, na waamini kwamba maombi yao yatajibiwa. Katika yote yanayofanyika, upendo wa Kristo na udhihirishwe. LLM 76.4

Kila Mkristo mwaminifu huinama kwa Yesu kama daktari wa kweli wa roho. Atakaposimama kando ya kitanda cha walioteseka, kutakuwa na wengi, sio tu walioongoka, bali ambao wameponywa, Yeye aliyetangaza, “Mimi Ndimi Njia, na Kweli, na Uzima,” atakuwa pamoja na matabibu na wauguzi wake waaminifu wakiwa wanajitahidi kushirikiana Naye. Ikiwa kwa njia ya huduma ya busara mgonjwa anaongozwa kutoa roho yake kwa Kristo, na kuleta mawazo yake katika utii wa mapenzi ya Mungu, ushindi mkubwa hupatikana. LLM 76.5

*****

B 29 '05 (Imenakiliwa Januari 1, '05)

Lo! jinsi ninavyotamani kuona kazi ikienda kwa nguvu katika miji ya New Bedford na Fairhaven, na katika maeneo mengine mengi tu yaliyo na uhitaji mkubwa wa Ukweli kama vile maeneo haya. Tunatumai kwamba wakati fulani kituo cha sanitarium kinaweza kuanzishwa New Bedford. Wafanyakazi Wamishenari wa tiba wanahitajika katika miji kama hiyo. Lakini, dada mpendwa, inahitajika talanta isiyo na uwezo wa kawaida kusimamia huduma za sanitarium. Wanaume wenye uzoefu, waliojaribiwa na kutahiniwa lazima washikilie kazi hiyo. Kwamba sehemu ya watendakazi wanaojitolea kuanzisha

taasisi hiyo wana uzoefu na sifa, haitoshi. Kwaajili yao wenyewe, kwa ajili ya taasisi, na kwa ajili ya kusudi kwa ujumla, ni muhimu kwamba idadi kamili ya wanaume na wanawake waliohitimu vizuri ipatikane kuingia kwenye kazi. Jicho la Bwana liko juu ya shamba zima, na wakati umefika wa taasisi kuanzishwa katika uwanja fulani, Yeye anaweza kugeukia mahali hapo akili za wanaume na wanawake zilizoandaliwa vyema kuingia kwenye taasisi hiyo. LLM 76.6

Kuna mistari mingi ya kazi inayopaswa kuendelezwa. Kuna fursa kwa wauguzi waliozoezwa vizuri kwenda miongoni mwa familia na kuamsha shauku ya kupendezwa katika familia. Kuna hitaji la dharura la wainjilisti wengi na watendakazi wanaoendele darasa la Biblia katika miji kama vile Boston na New Bedford. Wafanyakazi hao wangepata fursa nyingi za kupanda mbegu nzuri. Kuna kazi kwa kila mtendakazi mwenye juhudi makini na mwenye bidii. Mafundisho ya Kristo, Kweli rahisi zinazofundishwa na mifano Yake, zinahitajika sana leo kama zilivyokuwa wakati alipokuwa ulimwenguni ana kwa ana. LLM 77.1

*****

O, -55 '05 (Imenakiliwa Januari 30, '05)

Bwana alinipa mwanga mkubwa juu ya matengenezo ya afya. Kuhusiana na mume wangu nilipaswa kuwa mfanyakazi wa kimishenari wa tiba. Nilipaswa kuweka mfano kwa kanisa kwa kuwapeleka wagonjwa nyumbani kwangu na kuwatunza. Hii nimefanya, mimi mwenyewe kwa kuwapa wanawake na watoto tiba zenye nguvu zaidi. Pia nilipaswa kuzungumza juu ya somo la kiasi cha Kikristo, kama mjumbe aliyeteuliwa na Bwana. Nilijishughulisha kwa moyo wote katika kazi hii, na nilizungumza na mkutano mkubwa juu ya kiasi kwa maana yake pana na ya kweli... LLM 77.2

Tulipokuwa Australia tulifanya kazi kama wamishenari wa tiba katika kila maana ya neno hili. Nyakati fulani nilijenga nyumba yangu huko Cooranbong, kama makao ya wagonjwa, na walioteseka. Katibu muhtasi wangu, ambaye alikuwa amepata mafunzo huko Battle Creek Sanitarium, alisimama kando yangu, na kufanya kazi ya mmishenari muuguzi. Hakuna malipo yoyote yaliyotolewa kwa ajili ya huduma yake, nasi tulipata ujasiri wa watu kwani walipendezwa na tulisaidia wagonjwa na wanaoteseka. Baada ya muda Retreat ya Afya huko Cooranbong ilijengwa, na kisha tukaondolewa mzigo huu. LLM 77.3

*****

B. 59 '05 (Imenakiliwa Feb. 4 '05) LB 38, p. 173.

Wauguzi wanaohusishwa na taasisi hizi wanapaswa kuwa tayari kutoa ushawishi wa kuokoa roho. Wale wasio na mizizi na msingi katika Ukweli hawapaswi kuajiriwa. Waache kwanza wathibitishwe katika Kweli. Basi na wajifunze kuwa macho siku zote, wakitafuta daima kutoa maoni yanayofaa katika akili za wagonjwa... LLM 77.4

Wauguzi wanapaswa kuonyesha kupendezwa na kuwa wachangamfu kila wakati, na wanapaswa kuonyesha kufikiria wenzao. Wanapaswa daima kujitahidi kufanya kazi yao kwa hekima na vizuri, wakitambua kwamba wanamtumikia Bwana, na kwamba katika kutekeleza wajibu wao wanapaswa kuishi mbele ya wasioamini imani yao katika Ukweli kwa wakati huu. LLM 78.1

Uangalifu mkubwa unapaswa kuonyeshwa katika kuchagua vijana wa kuungana na sanitariums zetu. Wale ambao hawana upendo na Ukweli katika nafsi hawapaswi kuchaguliwa. Wagonjwa wanahitaji kuambiwa maneno ya busara. Mvuto wa kila mfanyakazi unapaswa kuibua akilini kupenda dini ya Kristo. Nuru imetolewa kwangu kwamba vijana waliochaguliwa kuungana na nyumba zetu za usafi wanapaswa kuwa wale ambao wana ushahidi kwamba wamekuwa wanafunzi wanaofaa katika shule ya Kristo... LLM 78.2

Wauguzi wanapaswa kuwa na mafundisho ya Biblia ya kawaida, ili waweze kuzungumza na wagonjwa maneno ambayo yatawaelimisha na kuwasaidia. Malaika wa Mungu wako katika vyumba ambamo watu wanaoteseka wanapaswa kutibiwa, na hali inayozunguka roho ya yule anayetoa matibabu inapaswa kuwa safi na yenye harufu nzuri. Katika maisha ya waganga na wauguzi wema wa Kristo unapaswa kuonekana. Kanuni Zake ni za watu kuishi. Kisha, kwa kile wanachofanya na kusema, wagonjwa watavutwa kwa Mwokozi… LLM 78.3

Ni kuokoa roho, na pia kuponya miili ya wanaume na wanawake, kwamba huduma zetu za sanitarium zimeanzishwa kwa gharama kubwa. Mungu anakusudia kwamba kupitia kwao, matajiri na maskini, walio juu na chini, watapata mkate kutoka mbinguni na maji ya uzima… LLM 78.4

Muuguzi Mkristo mwenye uzoefu katika chumba cha wagonjwa atatumia tiba bora zaidi anazojua ili kumrudishia mgonjwa afya yake. Naye atamvuta kwa furaha na kwa mafanikio yule ambaye anamfanyia kazi kwa Kristo, Mponyaji wa roho na mwili pia. Masomo yaliyotolewa, mstari juu ya mstari, hapa kidogo na pale kidogo, yatakuwa na ushawishi wao. Wauguzi wakubwa, wawe wanaume au wanawake, wasipoteze nafasi yoyote ya kuita usikivu wa wagonjwa kwa Kristo. Wale wanaowatunza wagonjwa wanapaswa kuwa tayari kuchanganya uponyaji wa kiroho na uponyaji wa kimwili. Wauguzi katika vyumba vyetu vya sanitarium waonyeshe kwamba katika kazi nzito ya kutunza

wagonjwa, hawategemei dawa za kulevya, bali nguvu za Kristo, na matumizi ya tiba rahisi ambazo ametoa, - matumizi ya maji moto na baridi na chakula sahili, chenye lishe, bila kileo cha aina yoyote, pamoja na mazoezi ya busara, na kuachana na mazoea yote mabaya. Katika matibabu kama haya kuna afya kwa wagonjwa. LLM 78.5

NINI KAZI YA MMISHENARI WA TIBA?—**Kufungua Milango Ya Injili Kwa Kuonyesha Upendo Wa Mungu Kwa Watu**

Upendo Kwa Vitendo Au Upendo Kwa Utendaji

Jambo kuu juu ya kazi ya umishenari wa tiba ni kuwaandaa watu kwa SIKU YA HUKUMU! Ni daraja au ngazi ya kuwasaidia watu Ili wapatikane TAYARI, SIKU YA HUKUMU! Soma Ufunuo 14:6-12 Injili ya milele, ikisema mche na MUNGU na kumtukuza maana saa ya hukumu imefika, Kuwa na ibada ya Kweli, na Binadamu wasipokuwa na ibada ya kweli wanapewa onyo, na baadaye hukumu (adhabu au thawabu) Kazi ya umishenari wa tiba rahisi ni mlango ambao jiwe la kuvukia mto au mlango wa kufikia nyumba nyingi katika miji. —

Umishenari wa kumsaidia mtu katika mahitaji yake ambayo yanamsibu, mahitaji ya kiroho, kijamii, kiuchumi, au kimwili, mfano anahitaji ushauri, anahitaji kusafishiwa mazingira yake, ana kidonda, anaumwa homa, mke wake amemkimbia, anahitaji ada, hana chakula, anahitaji mume au mke, anahitaji kusaidiwa masomo yake au kazi za nyumbani, anahitaji kukata nywele zake n.k (**Soma zaidi Counsel on Health, 556).**

Mkono wa kulia unatumika kufungua mlango ili mwili uweze kupata mpenyo au nafasi ya kupita. Hii ndio sehemu ya kazi ya umishonari wa matibabu/tiba MWT (Mmishenari wa Tiba) sio kazi ya kusomea masomo ya mitishamba (herbology) au Kanuni Nane za Afya, au unesi au udaktari au tiba rahisi tu, ILA

ni Kuandaa watu kwaajili ya hukumu ya MWISHO wa DUNIA hii kumlaki BWANA mawinguni wakiwa washindi na kuishi na MUNGU wetu MILELE NA MILELE NENO mmishenari wa tiba lilianza kutumiwa mnamo 1893 kwa neno “Upendo usiojifikiria au usio na uchoyo ukivutia kwake (disinterested BENEVOLENCE in kingereza. KINDNESS (WEMA) NOT JUST I LOVE YOU, but ACTION.) UPENDO KWA VITENDO), Si kusema nakupenda ila vitendo hamna, bali kusiwepo kujisaidia na kujifikiria mwenyewe tu!

Kazi ya Umishenari wa Tiba. Watendakazi wa tiba na Injili "wamefungwa pamoja na uhusiano usioweza kufunjika au kuyeyuka" MAJUKUMU YA NYUMBANI 1955 KAZI YA UMISHONARI WA MATIBABU YA OKTOBA Kazi ya umishenari wa tiba ni kazi ya mstari wa mbele kwa injili, Mlango wa awali wa kuingia kwenye nyumba na mioyo ya watu kwa wakati huu ikitumiwa itatuingiza kwenye nyumba nyingi. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wamishenari wa kweli wa tiba; kwani wanapaswa kujifunza kuhudumia mahitaji ya roho na mwili. Upendo na kujali watu kusiko na ubinafsi kabisa kunapaswa kuonyeshwa na watendakazi wetu. Kwa hayo maarifa na uzoefu uliopatikana kwa kazi ya vitendo, wanaenda kutoa matibabu kwa wagonjwa. Wanapoenda nyumba kwa nyumba watapata ufikiaji wa mioyo mingi. Wengi watafikiwa ambao isingekuwa hivyo kamwe wasingesikia ujumbe wa injili ya milele na kupata kuwepo mbinguni. Maonyesho ya kanuni za matengenezo ya afya hufanya mengi kuelekea, kuondoa ubaguzi dhidi ya kazi yetu ya injili. Daktari Mkuu ni MUNGU Mwenyewe, Mwanzilishi wa kazi ya umishenari wa tiba, atawabariki wote ambao kwa hivyo wanatafuta kutoa Ukweli kwa wakati huu.

Uponyaji wa mwili umefungwa na utume wa injili. Wakati Kristo alipowatuma wanafunzi Wake katika safari yao ya kwanza ya umishenari, aliwaambia, "Mnapoenda, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Ponyeni wagonjwa, toeni ukoma, toeni wafu, toeni pepo kwa hiari. Mmepokea, toeni bure. " Mt. 10: 7, 8. Na wakati wa mwisho wa huduma Yake ya kidunia aliwapa agizo lao, Akisema, "Ishara hizi zitafuata wale waaminio; Kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; na wakinywa kitu cha mauti, hakitawaumiza; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. " Marko 16:17, 18. . . MFANO WA KRISTO Tume ya Bwana haihitaji marekebisho. Njia ya Kristo ya kuwasilisha Ukweli haiwezi kuboreshwa. Mwokozi aliwapa wanafunzi masomo ya vitendo, aliwafundisha jinsi ya kufanya kazi kwa njia ambayo itafurahisha roho kuingia katika Ukweli. Aliwahurumia waliochoka, wenye kulemewa, walioonewa. Aliwalisha wenye njaa na akawaponya wagonjwa. Daima Alizunguka-zunguka akitenda mema. Kwa mema aliyotimiza, kwa maneno Yake ya upendo na matendo mema, Alifasiri na kufanunua injili kwa wanadamu. Kwa kifupi kama ilivyokuwa

kipindi cha huduma Yake ya umma, Alitimiza kazi aliyokuja kuifanya. Kweli alizofundisha zilivutia sana! Jinsi kazi Yake ilivyokuwa na maisha kamilifu aliyoishi! Ni chakula gani cha kiroho alichotoa kila siku alipowasilisha mkate wa uzima kwa maelfu ya roho zenye njaa! Maisha Yake yalikuwa huduma hai ya Neno. Hakuahidi chochote ambacho hakufanya. Maneno ya maisha yaliwasilishwa kwa urahisi kiasi kwamba mtoto angeweza kuyaelewa. Wanaume, wanawake, na watoto walivutiwa sana na njia Yake ya kuelezea Maandiko hivi kwamba wangeweza kuisikia Yake, wakaweka maneno yao sawa na yake, na kuiga ishara Zake. Vijana waliambukizwa na roho Yake ya huduma, na wakatafuta kuiga njia Zake za neema kwa kutafuta kuwasaidia wale ambao waliona wanahitaji msaada.

Kama viletunavyofuatilia njia ya kijito cha maji kwa kuangalia kijani kibichi kando yake, ndivyo Kristo angeweza kuonekana katika matendo ya rehema yaliyoashiria njia Yake kila hatua. Popote alipokwenda, afya ilikuboreshwa (afya ilikuwa hapo), na furaha ilifuata popote alipopita. Vipofu na viziwi walifurahi mbele Zake. Maneno Yake kwa wajinga yaliwafungulia chemchemi ya uzima. Alitoa baraka Zake kwa wingi na mfululizo/mpigo. Alikuwa na hazina za umilele zilizokusanywa, zilizotolewa kwa watu, yaani zawadi ya Bwana kwa mtu. Kazi ya Kristo kwa niaba ya mwanadamu haijakamilika. Inaendelea hata hivi leo. Vivyo hivyo mabalozi Wake wanapaswa kuhubiri injili na kufunua upendo Wake wa huruma kwa roho zilizopotea na zinazoangamia. Kwa shauku isiyo na ubinafsi kwa wale wanaohitaji msaada, wanapaswa kutoa onyesho la Ukweli wa injili. Kazi hii inahitaji zaidi ya mahubiri. Uinjilishaji wa ulimwengu ni kazi ambayo Mungu amewapa wale wanaokwenda kwa Jina Lake.

UFUNDISHAJI NA UPONYAJI

Haja ya ulimwengu ya kufundisha na uponyaji haijawahi kuwa kubwa kuliko ilivyo leo. Ulimwengu umejaa wale ambao wanahitaji kuhudumiwa, - wanyonge, dhaifu, wasio na ufahamu, wagonjwa. Ukiukaji wa sheria za afya wa mwanadamu mara kwa mara kwa karibu miaka elfu sita umeleta magonjwa, maumivu, na kifo kama matunda yake. Umati wa watu unaangamia kwa kukosa maarifa. Wakati wahudumu wa Mungu wanapoona matokeo mabaya ya dhambi iliyoendelea kwa muda mrefu, mioyo yao imeguswa na ole ya ulimwengu, na wanajitahidi kufanya kazi kama Mfanyikazi Mkuu na wanafunzi Wake walivyofanya kazi. Kuunganishwa na Mponyaji wa Mbinguni, kutasaidia kwenda kwa nguvu za uweza Wake kufundisha na kuponya. Wanatambua kwamba injili ndiyo dawa pekee ya dhambi, na kwamba kama mashahidi wa Kristo wanapaswa kutoa ushuhuda juu ya nguvu Zake. Wanapowaelekeza wake waliotaabika kwa Mwana-Kondoo wa Mungu,

ambaye huondoa dhambi ya ulimwengu, neema Yake inayobadilisha na nguvu ya kufanya miujiza inasababisha wengi kukubali ujumbe wa Ukweli unaobebwa. Nguvu Yake ya uponyaji, iliyounganishwa na ujumbe wa injili, inaleta mafanikio katika dharura. Roho Mtakatifu anafanya kazi juu ya mioyo, na wokovu wa Mungu unafunuliwa. Wahubiri, WAGANGA, NA WAUGUZI wanapaswa KUUNGANISHA KAZI ZAO. Lakini hitaji la ulimwengu leo haliwezi kutimizwa kikamilifu na huduma ya watumishi wa Mungu ambao wameitwa kuhubiri injili ya milele kwa kila kiumbe. Ingawa ni vizuri, kwa kadiri inavyowezekana, kwa wafanyikazi wa kiinjili kujifunza jinsi ya kuhudumia mahitaji ya mwili na roho, kwa hivyo kufuata mfano wa Kristo, lakini hawawezi kutumia wakati wao wote na nguvu katika kuwasaidia wakihitaji msaada. Bwana ameamuru kwamba pamoja na wale wanaohubiri Neno watahusishwa pia watendakazi Wake wa kimishenari wa tiba, Waganga na wauguzi wa Kikristo, ambao wamepata mafunzo maalum katika uponyaji wa magonjwa na katika kuzileta roho kwa Kristo. Wamishenari wa tiba na watendakazi katika huduma ya injili wanapaswa kufungwa pamoja na mahusiano yasiyofutwa. Kazi yao inapaswa kufanywa kwa upya na nguvu. Kwa juhudi zao za pamoja, ulimwengu unapaswa kuwa tayari kwa ujio wa pili wa Kristo. Kupitia kazi yao ya pamoja Jua la Haki litachomoza, likiwa na uponyaji katika mabawa Yake, na kupeperusha kwenye maeneo yasiyo na nuru ya dunia, ambapo watu wameishi kwa muda mrefu katika giza kuu. Wengi ambao sasa wanaishi katika uvuli wa dhambi na mauti, wanapoona kwa watumishi waaminifu wa Mungu mwangaza wa Nuru ya ulimwengu, watatambua kuwa wana tumaini la wokovu, na watafungua mioyo yao kupokea mihimili ya uponyaji, na sisi tutakuwa wachukuaji wa nuru kwa wengine bado katika giza.

Sanitariamu (Nyumba za kusaidia wagonjwa kwa tiba rahisi za asili) Kristo hayupo tena hapa ulimwenguni kimwili, lakini ametuamuru kuendeleza kazi ya umishonari wa tiba aliyoanza; na katika kazi hii tunapaswa kufanya bidii yetu yote. Kwa maendeleo ya kazi hii taasisi za utunzaji wa wagonjwa zinapaswa kuanzishwa, ambapo wanaume na wanawake wanaougua magonjwa wanaweza kuwekwa chini ya uangalizi wa matabibu na wauguzi wanaomcha Mungu. ' Bwana ameamuru kwamba vituo vya sanitariamu vianzishwe mahali pengi kusimama kama kumbukizi ya kazi Yesu aliyoifanya akiwa duniani. Hii ni mojawapo ya njia Zake teule za kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu, yaani injili ya milele ya kutayarisha watu kusimama katika hukumu wakiwa bila mawaa au hatia. Kwa njia hii ukweli utawafikia wengi ambao wangekuwa wazito kusikia Habari njema ya Msalaba. Lakini kwa mashirika mengine yaliyo na injili kavu peke yake, kamwe hawataangazwa na mwangaza wa ujumbe wa injili ila tu kwa njia ya kujali afya yao kwa njia rahisi. Katika uwasilishaji wa Ukweli, wengine watavutiwa na awamu moja ya ujumbe wa injili na wengine

na njia nyingine. Tumeagizwa na Bwana kufanya kazi kwa njia ambayo madaraja yote yatafikiwa. Ujumbe lazima uende kwa ulimwengu wote, hata ule wa Kiswahili

Kazi yetu ya Sanitarium, usafi na afya ni kusaidia kuongeza idadi ya watu wa Mungu. Kupitia safu hii ya juhudi za kimishenari makafiri watageuzwa na kuwa wacha Mungu. Kwa urejeshwaji mzuri unaofanyika katika nyumba zetu za Sanitarium wengi wataongozwa kumtazama Kristo kama mponyaji wa roho na mwili.

Watendakazi wa kujitolea, ambao wana imani kamili kwa Mungu, wanapaswa kuchaguliwa kuchukua jukumu la taasisi hizi. Wanaume na wanawake wenye busara, wanaofanya kazi kama wauguzi, wanapaswa kuwafariji na kuwasaidia wagonjwa na wanaoteseka. Usafi wetu unapaswa kuwa kama taa inayoangaza mahali penye giza, kwa sababu waganga, wauguzi, na wasaidizi wanaonyesha mwangaza wa jua wa haki ya Kristo.

Nyumba za usafi zinapaswa kuanzishwa na kuendeshwa hivi kwamba zitakuwa zenye kuelimisha kwa tabia. Wanapaswa kuuonyesha ulimwengu wema wa mbinguni. Ingawa uwepo wa Kristo hauonekani, lakini watendakazi wanaweza kudai ahadi hii, "Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa ulimwengu." Amewahakikishia wafuasi Wake kwamba kwa wale wanaompenda na kumcha Yeye atawapa nguvu ya kuendelea na kazi aliyoianza. Alizunguka-zunguka akitenda mema, akiwafundisha wasiojua, na kuponya wagonjwa. Kazi Yake haikuacha na maonyesho ya nguvu Zake juu ya magonjwa (miujiza). Alifanya kila kazi ya uponyaji, tukio la kuingiza ndani ya moyo kanuni za Mungu za upendo na ukarimu. Kwa hivyo wafuasi Wake wanapaswa kufanya kazi. . . ……

Mungu amewahitimisha watu Wake kuangaza ulimwengu. Amewapa wanaume vitivo vinavyowabadilisha ili kupanua bidii zao na kukamilisha kazi ambayo italinda ulimwengu.

Kumbuka:

- Mashauri juu ya Afya, ukurasa wa 497-499.
- Mashauri kwa Wazazi na Walimu, uk. 467-469.
- The Review and Herald, Mei 2, 1912.

MAENDELEO YA UMISHONARI WA KITABIBU

Kristo hayupo tena hapa ulimwenguni kwa binafsi, lakini ametuamuru kuendeleza kazi ya umishonari ya matibabu aliyoanza; na katika kazi hii tunapaswa kufanya bidii yetu yote. Kwa maendeleo ya kazi hii ya kutunza

wagonjwa ili wanadamu wanaougua magonjwa wanaweza kuwekwa chini ya uangalizi wa matabibu na wauguzi wanaomcha Mungu. '

Ni vyema kwetu kwamba tuna vituo vya tiba rahisi yaani Sanitarium na migahawa ya chakula cha afya (Hygeine restaurant). Hii ni moja wapo ya njia za Mungu teule za kutangaza ujumbe wa malaika watatu. Kwa njia hii Ukweli utawafikia wengi ambao, wasingepata ujumbe wa injili, na hivyo makundi yote yaweze kufikiwa. Kupitia tiba rahisi makafiri watageuzwa nao wataongozwa kumtazama Kristo kama mponyaji wa roho na mwili. Wauguzi wa nyumbani au kwenye taasisi, wanapaswa kuwafariji na kuwasaidia wagonjwa na watu wanaoteseka. Huduma yetu ya tiba inapaswa kuwa kama taa inayoangaza mahali penye giza, kwa sababu madakatari, wauguzi, na wasaidizi wanaonyesha mwangaza wa jua wa haki ya Kristo na wema wa mbinguni. Ingawa uwepo wa Kristo hauonekani, lakini wafanyikazi wanaweza kudai ahadi hii, "Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa ulimwengu." Bwana amewahakikishia wafuasi Wake kwamba kwa wale wanaompenda na kumcha Yeye atawapa nguvu ya kuendelea na kazi aliyoanza. Alizunguka-zunguka akitenda mema, akiwafundisha wasiojua/wajinga, na kuponya wagonjwa. Kazi Yake haikukoma na maonyesho ya nguvu Zake juu ya magonjwa. Mungu amewastahilisha watu Wake kuangaza ulimwenguni. Amewapa watu vitivo vinavyowabadilisha ili kupanua bidii zao na kukamilisha kazi ambayo italinda ulimwengu. '

*Wale wote wanaompenda Mungu ni vyema wajue kwamba kuna njia nyingi za Tiba ambazo haziendani na imani yetu, na kuna mstari mwembamba wa kuzitofautisha wakati mwingine. Hapa amezungumza njia ya tiba ya maji waliyotumia ambayo ilikuwa na mambo ya giza. Hivyo anashauri kufungua vituo vya tiba rahisi kwa kutumia vitu kama maji hayo hayo, ila wajielekeze kwenye mambo ya Mungu wa mbinguni maana Ndiye Mponyaji, na Tabibu Mkuu (tiba zingine ambazo Wakristo hawapaswi kutumia ni kama hyponotism, reiki, yoga, ramli, kusoma mikono, uaguzi nk). Hapa ndiyo walianza vituo vyao vya tiba rahisi –(Sanitarium-Hygienic Institute), pia kulikuwa na migahawa ya afya (Hygeneic restaurants). Ukisoma zaidi hata Dr Kellog tabibu alikuja na nadharia ya Patheismu ambayo inapingana na Maandiko, kwamba Mungu si Nafsi hai, ila ni uwepo tu kwenye miti, mimea na kila kitu. Japo alikuwa muumini, alikataa kushauriwa, mchungaji wa mke wake alimwambukiza nadharia hii. Hakuna binadamu aliye na elimu yote, ushauri na maonyo ni muhimu na kuomba Mungu atusaidie maamuzi wakati wa dhiki ya ugonjwa au muafaka ili tusiingie gizani.

Njia mbali mbali za giza ambazo tusizifuate kwetu Afrika ni kama kwenda kwa wachawi au waganga wa kienyeji, kusoma mikono, kubashiri, kupiga

ramli, wanajimu, kuzungumza na mizimu ili kupata suluhu za mambo, frenology, mesmerism, New Age, yoga, Ayuverdic n.k. Watu wengi wa Mashariki yaani bara la Asia wameingia kwetu Afrika, nao wamekuja na tamaduni zingine nzuri za tiba za miti/mimea au maji, ila wana zingine ambazo haziendani na imani yetu. Muumini anapaswa kuchunguza na kupata habari zaidi kutoka kwa Biblia au viongozi wake, Madaktari waumini, au walei ambao wana elimu ya jambo hili.

Soma zaidi Kumbukumbu la Torati 18:9-12. Neno la MUNGU linasema mtu akifa hana kumbukumbu tena, ni kama usingizi mzito, hivyo umizimu au kutumia nguvu za giza ili kujaribu kuungana na wale waliokufa ni kinyume cha Neno la MUNGU.

Dondoo la msaada katika kuchagua tiba rahisi: Kuna njia nyingi za kufanya sanaa ya uponyaji; lakini kuna njia moja tu ambayo Mbingu zinaithibithisha na kuikubali. Uponyaji/ tiba ya Mungu ni namna rahisi ya asili, ambayo haitakugharimu wala kudhoofisha mwili kupitia nguvu Mungu alizoziweka. Hewa safi na maji, usafi, lishe bora/sahihi, maisha safi, na imani thabiti kwa Mungu, ni tiba wengi wanaokufa wanaihitaji, na bahati mbaya tiba hizi zinaonekana kupitwa na wakati kwa sababu matumizi yake yanahitaji ustadi na kazi ambayo watu wengi hawaithamini kuifanya. Hewa safi, mazoezi, maji safi na salama, mazingira safi ya kuishi wengi wanaweza kuvimudu, kwa gharama kidogo pengine; lakini dawa za hospitali zina gharama za ina zote, katika utengenezaji na kuzinunua, na kwa athari zinazozalishwa kwenye mfumo kwa kuzitumia. — Ushuhuda wa Kanisa 5: 443, 1885 CD 301.2

Hapa ni vyema kujua kwamba wakati wa dharura mtu aende hospitalini haraka, kama vile kuvunjika mguu, presha au sukari iliyopanda au kushuka. Ila hali itakapokuwa na afueni atafute watalaamu wa kujifunza kutibu hivi vitu kwa njia rahisi, za mtindo wa maisha, ambazo huondoa ugonjwa kabisa mara nyingi, ili apunguze mzigo wa kutumia dawa maishani mwote, japo kutibu huku kunakofuata mtindo wa maisha, kunahitaji nidhamu kubwa!. Tafadhali, yote haya uyafanye kwa kushauriana na Daktari wako, mwenye leseni ya kutibu.

Madaktari na wahudumu wanapaswa kuungana katika jitihada ya kuwaongoza wanaume na wanawake kutii amri za Mungu.”— The Review and Herald, Aprili 21, 1906.

“Kazi mliyokuwa mkiifanya mijini inapata kibali cha mbingu... Mlichofanya kinadhihirisha kwamba ikiwa matabibu wetu na wahudumu wetu wanaweza kushirikiana katika uwasilishaji wa Ukweli kwa wananchi, mengi zaidi

yanaweza kufikiwa kuliko kushawishiwa. Na mchungaji anayefanya kazi peke yake.”—Medical Ministry, p. 263.

“Mungu anawaita vijana wa kiume na wa kike ambao tayari wamepata ujuzi wa vitendo wa jinsi ya kuwatendea wagonjwa, kufanya kazi kama wamisionari wa tiba wa injili, kuhusiana na wahudumu wa injili wenye uzoefu.”— Counsels to Parents and Teachers, p. 469.

"Hakuna matabibu wacha Mungu walio wengi wanaoweza kuhudumu katika taaluma yao. Kuna kazi nyingi ya kufanywa na wachungaji na madaktari, na hawa wanapaswa kufanya kazi kwa umoja kamili. ....

“Wahudumu na matabibu wanapaswa kufanya kazi kwa upatanifu na kwa bidii ili kuokoa roho.”—Testimonies, gombo la 1. 6, uk. 233.

“Madaktari wetu wanapaswa kuungana na kazi ya wahudumu wa injili. . . .

"Kazi ya umishonari wa tiba haiwezi kufanya bila huduma ya injili. Bwana amebainisha kwamba mawili hayo yatakuwa na uhusiano wa karibu kama mkono ulivyo na mwili. Bila muungano huu hakuna sehemu ya kazi itakuwa imekamilika. Mmishenai wa tiba ni mtenda kazi wa injili katika kielelezo, katika matendo.”—Ibid., uk. 240, 241.

"Kwa waganga wetu na wahudumu ninatuma ujumbe: Shikilia kazi ya Bwana kana kwamba unaamini ile Kweli ya wakati huu. Wahudumu wamishenari wa tiba na wafanyakazi katika huduma ya injili wanapaswa kufungwa pamoja na mahusiano yasiyoweza kuvunjika." - Ibid., juzuu ya 8, uk. 46.

“Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuunganishwa kwa ukaribu na kazi ya kuhubiri.”—Ibid., ukurasa wa 521, 522.

"Wamishenari wa tiba wanaofanya kazi katika safu za uinjilisti wanafanya kazi ya daraja la juu kama wafanya kazi wenzao walio katika huduma ya kichungaji. Aina hii ya kazi ya tiba au matibabu, pamoja na kazi ya huduma, haipaswi kuzuiwa kwa tabaka maskini zaidi tu...

"Daktari mwaminifu na mhudumu wanahusika katika kazi moja.Wao Wanapaswa kufanya kazi kwa upatanifu kamili. Wanapaswa kushauriana pamoja." - Ibid., p. 546.

"Ningependa kuzungumza juu ya uhusiano uliopo kati ya kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili. Imewasilishwa kwangu kwamba kila idara ya kazi inapaswa kuunganishwa katika umoja mkubwa…..... ili kusimama imara katika ile siku kuu ya mwisho, ni lazima kazi yetu isiwe ile iliyogawanyika.

"Pasiwe na mgawanyiko kati ya huduma na kazi ya tiba. Tabibu anapaswa kufanya kazi kwa usawa na mchungaji, na kwa bidii na uangalifu mwingi kwa wokovu wa roho, na pia kwa urekebishaji na matengenezo ya mwili.

"Inapounganishwa na njia zingine za juhudi za injili, kazi ya umishenari ya tiba ni chombo chenye ufanisi zaidi ambacho udongo hutayarishwa kwa ajili ya kupanda mbegu za Ukweli, na chombo ambacho kwa hicho mavuno huvunwa. Kazi ya umishenari wa tiba ni kusaidia, ni mkono wa huduma ya injili..... Bwana ameagiza kwamba madaktari wa Kikristo na wauguzi wafanye kazi katika uhusiano na wale wanaohubiri Neno.

“Wahudumu wa injili wanapaswa kuungana na kazi ya umishenari wa tiba, ambayo imewahi kuwasilishwa kwangu kama kazi ambayo huvunja chuki iliyopo miongoni mwa watu au kushuku. . . .

“Matabibu wanapoungana na wahudumu katika kutangaza injili katika miji mikubwa ya nchi, kazi yao iliyounganishwa itasababisha kushawishi akili nyingi kupenda Ukweli kwa wakati huu. . . .

“Watumishi waliowekwa wakfu peke yao hawatoshi katika kuifanya kazi ya Bwana. Mungu hawaiti wahudumu peke yao tu, bali pia matabibu, wauguzi, waombezi, wafanyakazi wa Biblia, na walei wengine waliojiweka wakfu, wenye vipaji mbalimbali ila ambao wana ujuzi wa Ukweli wa sasa, wafikirie mahitaji ya miji ambayo haijaonywa.

"Hakuna mstari ambao unapaswa kuwekwa kwenye kazi ya umishenari wa kweli kati ya tiba na huduma ya injili. Hivi viwili lazima vichanganywe pamoja. Havipaswi kusimama kando kama safu tofauti za kazi. Zinapaswa kuunganishwa katika muungano usioweza kutenganishwa, kama vile ambavyo mkono na mwili haviwezi kutenganishwa……

"Hakuna hata neno moja lililosemwa sana katika kuhalalisha na kusifu kazi halisi ya umishenari wa tiba.... Ikiwa kazi ya umishonari wa tiba itatenda kama mkono wa usaidizi wa huduma ya injili, wagonjwa wangerudishwa kwenye afya, na roho nyingi zingeongozwa, kwenye nuru ....

"Injili ya Kristo inapaswa kuunganishwa na kazi ya umishonari wa tiba, na kazi ya umishonari wa tiba inapaswa kuunganishwa na huduma ya injili. Ulimwengu unahitaji juhudi za wamisionari wa tiba ambao wamefungamanishwa na ujumbe wa injili. . . . [wahudumu wa injili] wanapaswa kuiona kama mkono wa kusaidia wa injili, wakiichukulia na kuithamini kwa hali ya juu na kutayarisha mioyo kwa ajili ya kupanda mbegu ya ile Kweli, na kuwaleta wengi kwa Kristo.”— Yoh. Medical Ministry, ukurasa wa 237

253.

“Bwana ameagiza kwamba wamishenari wa tiba washirikiswe pamoja na wale wanaohubiri Neno,—madaktari na wauguzi Wakristo, ambao wamepata mafunzo maalum katika uponyaji wa magonjwa na katika kuzileta roho kwa Kristo.

"Wamisionari wa tiba na watenda kazi katika huduma ya injili wanapaswa kuunganishwa pamoja na mahusiano yasiyoweza kuvunjika. Kazi yao inapaswa kufanywa kwa upya na kwa nguvu. Kwa juhudi zao za pamoja ulimwengu unapaswa kutayarishwa kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo. Kupitia kazi zao za umoja. Jua la Haki litachomoza, likiwa na uponyaji katika mbawa Zake.”—Counsels to Teachers, p. 468.

"Kazi ya uinjilisti yenye mafanikio inaweza kufanywa kuhusiana na kazi ya umishenari wa tiba. Ni pale ambapo safu hizi za kazi zinavyounganishwa pamoja, ndipo tunaweza kutazamia kukusanya tunda la thamani zaidi kwa ajili ya Bwana." - Medical Ministry, uk. 26, 27.

"Ikiwa wakati wowote Bwana amesema kupitia mimi, Yeye hunena ninaposema kwamba watenda kazi wanaojishughulisha na masuala ya elimu, katika safu za huduma na katika safu za umishenari wa lazima lazima wasimame kama kitengo kimoja, wote wakifanya kazi chini ya usimamizi wa Mungu, mmoja akimsaidia mwingine. kila mmoja akibariki mwingine.”—Testimonies, vol. 9, ukurasa wa 169, 170.

"Ndugu zangu, Bwana anaita umoja, kusimama pamoja. Twapaswa kuwa kitu kimoja katika imani. Nataka kuwaambia kwamba wahudumu wa injili na wahudumu wa umishenari wa tiba wanapokosa umoja, uovu mbaya zaidi unawekwa kwenye makanisa yetu, jambo ambalo lisingelikuwapo.”—Medical Ministry, p. 241.

"Kristo, Mmisionari mkuu wa tiba, Ndiye kielelezo chetu. ... Yeye Aliponya wagonjwa na kuhubiri injili. Katika huduma Yake, uponyaji na mafundisho yaliunganishwa kwa ukaribu. Leo havipaswi kutenganishwa." - Testimonies, vol. 9, ukurasa wa 170, 171.

"Maisha ya Kristo na huduma Yake kwa wanaoteseka yameunganishwa kwa njia isiyoweza kutenganishwa. Kutoka kwa nuru ambayo nimepewa, najua kwamba uhusiano wa karibu unapaswa kuwepo kati ya kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili. Hivi vimefungwa pamoja katika muungano mtakatifu kama kazi moja, na kamwe havipaswi kuachanishwa.Kanuni za mbinguni zinapaswa kuchukuliwa na kutekelezwa na wale wanaodai kutembea katika nyayo za Mwokozi. Kwa mfano Wake Yeye ametuonyesha kwamba kazi ya

umishenari wa tiba haipaswi kuchukua nafasi ya mahubiri ya injili, lakini inapaswa kuunganishwa nayo.”—Counsels on Health, p. 528.

"Mungu hufikia mioyo kupitia kutulizwa kwa mateso ya kimwili ... Mungu anafanya kazi leo kufikia mioyo kwa njia ile ile aliyofanya wakati Kristo alipokuwa katika dunia hii. Katika kusoma Neno la Mungu, tunaona kwamba Kristo alileta kazi ya umishenari wa tiba katika kufanya huduma Yake. Je, macho yetu hayawezi kufunguliwa ili kutambua mbinu za Kristo? Je, hatuwezi kuelewa agizo alilolitoa kwa wanafunzi Wake na kwetu sisi?”—Medical Ministry, p. 246.

"Kama kazi ya umishenari wa tiba inafanywa kama sehemu ya injili, walimwengu wataona wema unaofanywa; nao watasadikishwa hatiani na ile Kweli Yake nao wataiunga mkono." - Testimonies, vol. 6, uk. 292.

"Mwokozi alifanya kila kazi ya kuponya watu kuwa nafasi ya kupandikiza kanuni za Kiungu/mbinguni katika akili na nafsi Yake. Hili ndilo lilikuwa kusudi la kazi Yake. Alitoa baraka za kidunia, ili Aweze kuelekeza mioyo ya wanadamu kupokea injili ya neema Yake." - Wizara ya Uponyaji, uk. 20.

“Kuna baraka za thamani na uzoefu mzuri wa kupata ikiwa wahudumu watachanganya uwasilishaji wa suala la afya na kazi zao zote makanisani.”—Counsels on Health, p. 431.

“Katika kazi ya Mungu, mafundisho na uponyaji haviwezi kutenganishwa kamwe.”—Testimonies, vol. 8, uk. 165.

"Huduma ya injili inahitajika ili kutoa udumishaji na uthabiti kwa kazi ya umishenari wa tiba; na huduma inahitaji kazi ya umishenari ya tiba ili kuonyesha kazi katika vitendo kwenye injili. Hakuna sehemu yoyote ya kazi iliyokamilika bila nyingine. ....

"Katika Neno Lake Mungu ameunganisha mistari hii miwili ya kazi, na hakuna mtu anayepaswa kuiacha." - Counsels on Health, uk. 514, 515.

KUMBUKUMBU ZA NYUMBANI 1955 OKTOBA "TABIBU NA WACHUNGAJI TUUNGANE"

Madaktari na wahudumu wanapaswa kuungana katika jitihada ya kuwaongoza wanaume na wanawake kutii amri za Mungu.”— The Review and Herald, Aprili 21, 1906.

“Kazi mliyokuwa mkiifanya mijini inapata kibali cha mbingu... Mlichofanya kinadhihirisha kwamba ikiwa madaktari wetu na wachungaji wetu wanaweza kushirikiana katika uwasilishaji wa Ukweli kwa wananchi, basi mengi zaidi

yanaweza kutimizwa kuliko ushawishi wa mchungaji anayefanya kazi peke yake.”—Medical Ministry, p. 263.

“Mungu anawaita vijana wa kiume na wa kike ambao tayari wamepata ujuzi wa vitendo wa jinsi ya kuwasaidia kwa vitendo wagonjwa, kufanya kazi kama wamishenari wa tiba wa injili kwa kuhusiana na wahudumu wa injili wenye uzoefu.”— Counsels to Parents and Teachers, p. 469.

"Hatuna matabibu wacha Mungu wengi ambao wamebobea katika taaluma yao. Kuna kazi nyingi ya kufanywa, ambayo wachungaji na madaktari wanapaswa kufanya kazi hii, kwa umoja kamili. ....

“Wahudumu/wachungaji na matabibu wanapaswa kufanya kazi kwa upatanifu na kwa bidii ili kuokoa roho.”—Testimonies, gombo la 1. 6, uk. 233.

“Madaktari wetu wanapaswa kuungana na kazi ya wahudumu wa injili. . . .

"Kazi ya umishenari wa tiba haiwezi kuachwa mbali kutoka kwenye huduma ya injili. Bwana amebainisha kwamba hivi viwili vitakuwa na uhusiano wa karibu kama mkono ulivyo na mwili. Bila muungano huu hakuna sehemu ya kazi itakuwa imekamilika. Kazi ya mmishenari wa tiba ni ya kazi ya injili katika kielelezo yaani injili kwa vitendo.”—Ibid., uk. 240, 241.

"Ninatuma agizo la huduma kwa madaktari na wahudumu wetu: Shikilia kazi ya Bwana kana kwamba unaamini Ukweli wa wakati huu. Wahudumu wamishenari wa tiba na wafanyakazi katika huduma ya injili wanapaswa kufungwa pamoja na mahusiano yasiyoweza kuvunjika." - Ibid., juzuu ya 8, uk. 46.

“Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuunganishwa kwa ukaribu na kazi ya kuhubiri.”—Ibid., ukurasa wa 521, 522.

"Wamishenari wa tiba wanaofanya kazi katika safu za uinjilisti wanafanya kazi ya daraja la juu kama ile kazi ya wenzao kwenye idara ya huduma ya kichungaji. Aina hii ya kazi ya tiba, pamoja na kazi ya huduma, haipaswi kufanywa kwa tabaka maskini zaidi tu bali kwa matajiri na watu wa kati, yaani watu wote……..

"Daktari mwaminifu na mchungaji wanahusika katika kazi moja. Wao Wanapaswa kufanya kazi kwa upatanifu kamili. Wanapaswa kushauriana pamoja." - Ibid., p. 546.

"Ningependa kuzungumza juu ya uhusiano uliopo kati ya kazi ya umishenari wa tiba na huduma ya injili. Imewasilishwa kwangu kwamba kila idara ya kazi inapaswa kuunganishwa katika umoja mkubwa ……. ili watu waweze kusimama

imara katika siku kuu ya mwisho ya hukumu, yabidi kusiwe na kazi iliyogawanyika.

"Pasiwe na mgawanyiko kati ya huduma na kazi ya tiba. Tabibu anapaswa kufanya kazi kwa usawa, pamoja na mhudumu, na kwa bidii na uangalifu mwingi kwa wokovu wa roho, na pia katika urekebishaji na matengenezo ya mwili.

"Inapounganishwa na njia zingine za juhudi za injili, kazi ya umishenari wa tiba ni chombo chenye ufanisi zaidi ambacho udongo hutayarishwa kwa ajili ya kupanda mbegu za Ukweli, na chombo ambacho kwa hicho mavuno huvunwa. Kazi ya umishenari wa tiba ni kusaidia, kwani ni mkono wa kulia wa huduma ya injili.... Bwana ameagiza kwamba waganga wa Kikristo na wauguzi wafanye kazi katika uhusiano na wale wanaolihubiri Neno.

“Wahudumu wa injili wanapaswa kuungana na kazi ya umishenari wa tiba, ambayo imewahi kuwasilishwa kwangu kama kazi ambayo inasaidia kuvunja chuki iliyopo miongoni mwa watu wasio waumini ….

“Matabibu wanapoungana na wahudumu katika kutangaza injili katika miji mikubwa ya nchi, kazi yao iliyounganishwa na wamishenari wa tiba, itasababisha kushawishiwa kwa akili nyingi kuupenda Ukweli wa wakati huu...

“Watumishi waliowekwa wakfu peke yao hawatakuwa sawa katika kuifanya kazi ya injili peke yao. Mungu anawaita si wachungaji au wahudumu wa injili tu, bali pia matabibu, wauguzi, watu wa maombezi, wafanyakazi wa Biblia, na walei wengine waliojiweka wakfu, wenye vipaji mbalimbali ambao wana ujuzi wa Ukweli wa sasa, wachekecheke vichwa vyao na kuona mahitaji ya miji ambayo haijaonywa.

"Hakuna mstari utakaowekwa kati ya kazi ya umishenari ya Kweli ya tiba na huduma ya injili. Hizi mbili lazima zichanganywe pamoja. Hazipaswi kusimama kando kama safu tofauti za kazi. Zinapaswa kuunganishwa katika muungano usioweza kutenganishwa, kama vile mkono usivyoweza kutenganishwa na mwili

"Hakuna hata neno moja lililosemwa sana katika kuhalalisha na kusifu kazi halisi ya umishenari wa tiba..... Kwa kuwa kazi ya umishenari wa tiba ikitenda kama mkono wa msaada, katika kusaidia huduma ya injili, wagonjwa watarudishwa kwenye afya, na roho nyingi zingeongozwa kwenye nuru ya Mwenyezi Mungu ....

"Injili ya Kristo inapaswa kuunganishwa na kazi ya umishenari wa tiba, na kazi ya umishenari ya matibabu inapaswa kuunganishwa na huduma ya injili. Ulimwengu unahitaji juhudi za wamishenari wa tiba ambao

wamefungamanishwa na ujumbe wa injili. . . . [wahudumu wa injili] wanapaswa kuiona kazi ya umishenari wa tiba kama mkono wa kusaidia injili, mkono wa kufungua mlango, wakiichukulia kwa kuithamini kwa ukubwa kama ndiyo fursa ya kutayarisha mioyo kwa ajili ya kupanda mbegu ya Kweli, na kuwaleta wengi kwa Kristo.”— Yoh. Medical Ministry, ukurasa wa 237

“Bwana ameagiza kwamba pamoja na wale wanaohubiri Neno, washirikishwe wahudumu Wake wa kimishenari wa tiba,—madaktari na wauguzi Wakristo, ambao wamepata mafunzo maalum katika uponyaji wa magonjwa na katika kuleta roho kwa Bwana.

"Wamishenari wa tiba na watenda kazi katika huduma ya injili wanapaswa kuunganishwa pamoja na mahusiano yasiyoweza kuvunjika. Kazi yao inapaswa kufanywa kwa upya na kwa nguvu. Kwa juhudi zao za pamoja ulimwengu unapaswa kutayarishwa kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo. Kupitia kazi zao za mshikamano wenye umoja. Jua la Haki litachomoza, likiwa na uponyaji katika mbawa Zake.”—Counsels to Teachers, p. 468.

"Kazi ya uinjilisti yenye mafanikio inaweza kufanywa kwa kuhusiana na kazi ya umishenari wa tiba. Ni kwa pale safu hizi za kazi zinavyounganishwa ndipo twaweza kutazamia kukusanya matunda ya thamani zaidi kwa ajili ya Bwana-yaani roho za watu waliojitoa kwa Mwenyezi Mungu." - Medical Ministry, uk. 26, 27.

"Ikiwa wakati wowote Bwana amesema kupitia mimi, Yeye hunena ninaposema kwamba watenda kazi wanaojishughulisha na masuala ya elimu, katika safu za huduma na katika safu za umishenari wa tiba lazima wasimame kama kitengo, wote wakifanya kazi chini ya usimamizi wa Mungu, mmoja akimsaidia mwingine. kila mmoja akibariki kila mmoja.”—Testimonies, vol. 9, ukurasa wa 169, 170.

"Ndugu zangu, Bwana anaita umoja, mfanye kazi kwa pamoja. Twapaswa kuwa kitu kimoja katika imani. Nataka kuwaambia kwamba wahudumu wa injili na wahudumu wamishenari wa tiba wanapokosa umoja, kunawekwa kwenye makanisa yetu uovu mbaya zaidi hapo.”—Medical Ministry, p. 241.

"Kristo, Mmishenari mkuu wa tiba, Ndiye kielelezo chetu…….. Aliponya wagonjwa na kuhubiri injili. Katika huduma Yake, uponyaji na mafundisho yaliunganishwa kwa karibu. Leo hawapaswi kutenganishwa." - Testimonies, vol. 9, ukurasa wa 170, 171.

"Maisha ya Kristo na huduma Yake kwa wanaoteseka yameunganishwa kwa njia isiyoweza kutenganishwa. Kutoka kwa nuru ambayo nimepewa, najua kwamba uhusiano wa karibu unapaswa kuwepo kati ya kazi ya umishenari wa

tiba na huduma ya injili. vimefungwa pamoja katika muungano mtakatifu. kama kazi moja, na kamwe havipaswi kuachana. Kanuni za mbinguni zinapaswa kuchukuliwa na kutekelezwa na wale wanaodai kutembea katika nyayo za Mwokozi. Kwa mfano Wake ametuonyesha kwamba kazi ya umishenari wa tiba haipaswi kuchukua nafasi ya mahubiri ya injili, lakini inapaswa kuunganishwa nayo."—Counsels on Health, p. 528.

"Mungu hufikia mioyo kupitia kitulizo cha mateso ya kimwili ... Mungu anafanya kazi leo kufikia mioyo kwa njia ile ile aliyofanya wakati Kristo alipokuwa juu ya dunia hii. Katika kusoma Neno la Mungu, tunaona kwamba Kristo alileta kazi ya umishenari wa tiba katika kufanya kazi ya huduma Yake. Je, macho yetu hayawezi kufunguliwa ili kutambua mbinu za Kristo? Je, hatuwezi kuelewa agizo alilotoa kwa wanafunzi Wake na kwetu sisi?"—Medical Ministry, p. 246.

"Kama kazi ya umishenari wa tiba inafanywa kama sehemu ya injili, walimwengu wataona wema unaofanywa; nao dhamira zao zitasadikishwa naile Kweli ya Mungu na kisha wataiunga mkono." - Testimonies, vol. 6, uk. 292.

"Mwokozi alifanya kila kazi ya kuponya kuwa nafasi ya kupandikiza kanuni Zake katika akili na nafsi za watu. Hili ndilo lilikuwa kusudi la kazi Yake. Yeye Alitoa baraka za kidunia, ili Aweze kuielekeza mioyo ya wanadamu kupokea injili ya neema Yake." - Huduma ya Uponyaji, uk. 20.

"Kuna baraka za thamani na uzoefu mzuri utakaopatikana kama wahudumu watachanganya uwasilishaji wa ujumbe wa afya na kazi zao zote makanisani."—Counsels on Health, p. 431.

"Katika kazi ya Mungu, mafundisho na uponyaji haviwezi kutenganishwa kamwe."—Testimonies, vol. 8, uk. 165.

"Huduma ya injili inahitajika ili kutoa uendelevu na uthabiti kwa kazi ya umisionari ya tiba; na huduma inahitaji kazi ya umishenari wa tiba ili kuonyesha utendaji au vitendo vya injili. Hakuna sehemu yoyote ya kazi iliyokamilika bila nyingine. ....

"Katika Neno Lake Mungu ameunganisha mistari hii miwili ya kazi, na hakuna mtu anayepaswa kuviachanisha." - Counsels on Health, uk. 514, 515.

451. Kuna njia nyingi za kushughulika na stadi ya uponyaji/tiba; lakini kuna njia moja tu ambayo Mbingu huidhinisha. Dawa za Mungu ni wakala rahisi wa asili, ambao hautatoza ushuru mwili au kudhoofisha mfumo kupitia silika yake yenye nguvu. Hewa safi na maji, usafi, mlo ufaao, usafi wa maisha, na imani thabiti katika Mungu, ni tiba inayohitajika kwa maelfu ambao wanakufa; na

bado tiba hizi hazitumiwi na hivyo kusahauliwa kwa sababu utumiaji wake unahitaji weledi/stadi na kazi nyingi ambayo watu hawathamini kuifanya. Hewa safi, mazoezi, maji safi, na mapumziko, lishe bora, kiasi, hewa bora, yanaweza kufikiwa na wote, kwa gharama ndogo tu; lakini madawa ya kulevya ni ghali, katika matumizi ya fedha, na matokeo yanayoletwa kwenye mfumo wa mwili wa mwanadamu.— Testimonies for the Church 5:443, 1885

451. There are many ways of practicing the healing art; but there is only one way that Heaven approves. God's remedies are the simple agencies of nature, that will not tax or debilitate the system through their powerful properties. Pure air and water, cleanliness, a proper diet, purity of life, and a firm trust in God, are remedies for the want of which thousands are dying; yet these remedies are going out of date because their skillful use requires work that the people do not appreciate. Fresh air, exercise, pure water, and clean, sweet premises, are within the reach of all, with but little expense; but drugs are expensive, both in the outlay of means, and the effect produced upon the system.—Testimonies for the Church 5:443, 1885

AU!

451. Kuna njia nyingi za kufanya zoezi la stadi ya uponyaji; lakini kuna njia moja tu ambayo ndiyo mbingu huiidhinisha. Tiba za uponyaji za Mungu ni wakala sahili wa asili, ambao hautatoza ushuru au kudhoofisha mfumo kupitia sifa zake zenye ukali au nguvu nzito kwenye mwili. Hewa safi na maji, usafi, mlo ufaao, usafi wa maisha, na imani thabiti katika Mungu, ni tiba ambazo maelfu wanazihitaji na kwa kuwa hawazipati, wanakufa; bado dawa hizi zinaendelea kupitwa na wakati mawazoni mwa watu wengi, yaani watu hawazitumii kwasababu utumiaji wake, na ustadi wake unahitaji kazi ambayo watu wengi hawaithamini kwani zinachukua muda ukilinganisha na kubugia dawa. Hewa safi, mazoezi, maji safi, na majengo safi, yenye utulivu na uzuri sahili, na hivi vinaweza kufikiwa na wote, kwa gharama ndogo tu; lakini madawa ya kulevya ni ghali, katika matumizi ya fedha, na matokeo yanayoletwa kwenye mfumo wa mwili ni ya gharama pia.— Testimonies for the Church 5:443, 1885

452. Hewa safi, mwanga wa jua, kiasi, pumziko, mazoezi, mlo ufaao, matumizi ya maji, kumtumaini Mungu —haya ndiyo tiba ya kweli. Kila mtu anapaswa kuwa na ujuzi wa mawakala wa asili wanaouhisika na kurekebisha na jinsi ya kuyatumia. Ni muhimu pia kuelewa kanuni zinazohusika katika tiba ya wagonjwa na kuwa na mazoezi ya kivitendo ambayo yatamwezesha mtu kutumia ujuzi huo kwa njia ifaayo.

Matumizi ya tiba asili yanahitaji kiasi cha huduma na jitihada ambazo wengi hawako tayari kutoa. Mchakato wa asili wa uponyaji na kujenga ni wa polepole, na kwa wale wasio na subira inaonekana polepole. Kujisalimisha kwa msamaha wa dhambi kunahitaji dhabihu. Lakini mwishowe itapatikana kwamba asili, bila ya kupunguzwa, hufanya kazi yake kwa busara na vizuri. Wale wanaodumu katika kutii sheria zake watapata thawabu katika afya ya mwili na akili.— The Ministry of Healing, 127, 1905

453. Madaktari mara nyingi hushauri wagonjwa kutembelea nchi za kigeni na meli (cruise), kwenda kwenye chemchemi ya madini, au kuvuka bahari, ili kupata afya tena; wakati, katika visa tisa kati ya kumi, ikiwa wangekula kwa kiasi, na kufanya mazoezi yenye afya wakiwa na roho ya uchangamfu, wangepata afya tena na kuokoa wakati na pesa. Mazoezi, na matumizi mengi ya bure ya hewa na mwanga wa jua—baraka ambazo mbingu imewapa wote—katika hali nyingi zingewapa uzima na nguvu wale waliodhoofika.—Christian Temperance and Bible Hygiene, 160, 1890

Baadhi ya Mambo Tunayoweza Kujifanyia Wenyewe

454. Kuhusiana na yale tunayoweza kujifanyia sisi wenyewe, kuna jambo ambalo linahitaji mazingatio makini na akili zenye akili.

Ni lazima nijitambue, lazima niwe mtu wa kujifunza siku zote jinsi ya kutunza jengo hili, yaani mwili ambao Mungu amenipa, ili niuhifadhi katika hali bora kabisa ya afya. Ni lazima nile vile vitu ambavyo vitanisaidia vyema kimwili, na lazima nichukue uangalifu wa pekee kuwa na mavazi yangu kwa ubora, na kwa jinsi ambavyo yatachangia mzunguko wa damu wenye afya. Sipaswi kujinyima mazoezi na hewa. Lazima nipate mwanga wote wa jua ambao inawezekana kwangu kuupata. Lazima niwe na hekima ya kuwa mlinzi mwaminifu wa mwili wangu.

Kuingia katika chumba chenye baridi nikiwa katika jasho ni jambo lisilo na hekima; Ninapaswa kuonyesha kwamba ninasimia kwa busara hili, ili kujiruhusu kukaa kwenye mkutano, na hivyo kujiweka wazi ili kupata baridi. Sio busara kukaa mkao wa kuacha miguu baridi na viungo vilivyo mbali na moyo kama mikono, miguu na kichwa, na hivyo kufanya kurudishwa damu kutoka kwenye ncha za mwili yaani miguu na mikono hadi kwenye ubongo au viungo vya ndani kuwa vigumu. Ninapaswa kuilinda miguu yangu kila wakati wakati wa hali ya hewa yenye unyevunyevu. Ninapaswa kula kwa kawaida, kwa kiasi, chakula chenye afya zaidi ambacho kitafanya damu iwe bora zaidi, na sipaswi kufanya kazi kwa kupitiliza kiasi ikiwa ni katika uwezo wangu kuepuka kufanya hivyo. Na ninapokiuka sheria ambazo Mungu aliweka katika nafsi yangu, ninapaswa kutubu na kurekebisha hali hiyo, na kujiweka katika

hali nzuri zaidi chini ya madaktari sahili ambao Mungu ametupa kwa uponyaji, matabibu hao ni —hewa safi, lishe bora, maji safi, mazoezi, kumtumaini Mungu, kupumzika, kuwa na kiasi au kutawala na nafsi, uponyaji, mwanga wa jua wenye thamani.

NUKUU za RYU AFYA

Mchanganyiko wa nukuu za afya: IMETOLEWA NA DKT CALVIN DENCE NA GRACE MOMADI-MASAKA

1. Ikiwa tunashinda hamu ya kula tunaweza kushinda juu ya yote. CD145
2. Soma waandishi bora juu ya sheria za maisha, uzima na afya. Kisha utii hoja yako. GW 242
3. Edeni ilipotea kwa hamu ya kula, na itarejeshwa kwa kushinda hamu ya kula. 161
4. Wale wanaotenda dhambi dhidi ya maarifa ya afya, na kutegemea dawa watapoteza maisha. MM224
5. Dawa za famasia zimefanya madhara zaidi na kuua zaidi ya zilivyosaidia. MM 27
6. Dawa za famasia nyingi zinapaswa kutupwa. MS 162
7. Ushawishi wa Roho Mtakatifu ni dawa bora kabisa kwa wagonjwa. MM 12
8. Vitu vya asili ni bora kwa afya kuliko dawa zote ulimwenguni. CH 169
9. Dawa ni dutu ya kigeni na yenye asili ya sumu. 134
10. Ugonjwa ni adhabu ya kukiuka sheria za asili. CH 347
11. Zuia magonjwa kwa usafi na kutii sheria za afya. 4 SG 140

12. Magonjwa ni juhudi ya mwili na maumbile kuondoa uchafu wa mwili. CH 61
13. Kufanya vizuri ni dawa bora ya magonjwa. HH 447
14. Ugonjwa hauji kamwe bila sababu. 469.
15. Kusoma Biblia na kufanya kazi ni tiba bora kwa miili na akili za wagonjwa. 2T 325
16. Kufunga siku moja au mbili ni bora kuliko dawa za Famakia. CH 477
17. Kuacha kula kwa muda mfupi, au kuacha kabisa pombe na sigara ndiyo njia ya kuelekea kwenye afya 310
18. Pika kidogo na kula matunda mengi katika hali ya asili. 134
19. Imani katika Kristo na utii ni sayansi ya kweli ya uponyaji. CH 346
20. Tutakapochukua mpango wa asili wa bustani ya Edeni mapema, afya yetu itarejeshwa mapema. CH 174
21. Kwa kutii sheria za maisha TUNAHAKIKISHA AFYA YETU kuwa bora. CH 49
22. Maisha ya nje ya nyumba, hurejesha afya. 231
23. Imani ya mtu mgonjwa imekufa isipokuwa ikiwa yuko tayari kubadilisha tabia zake. MM 262
24, Ikiwa una afya mbaya, wasaidie wengine na utajikuta unaanza kupona. 442
25. Panda juu katika Matengenezo ya Afya tunapokaribia mwisho. CH 467
26. Chochote kinachopunguza nguvu ya mwili, hufanya akili iwe dhaifu. KOL 346

27. Bila Matengenezo ya Afya matumaini yote ya mbinguni ni bure. CH 574-9
28. Tutakutana mbinguni na wale ambao tumewafanyia kazi katika Matengenezo ya afya. KOL 373
29. Hakuna usalama katika bidhaa za wanyama au samaki. CD1 411
30. Hakuna chakula kimoja kinachopaswa kupita kati ya midomo kati ya chakula CH 408
30. Hakuna chakula kimoja kinachopaswa kupita kati ya midomo kati ya chakula CH 408
31. Kula chakula ganzi ubongo na husababisha njaa ya uwongo. 2T 212-3
32. Sukari huziba mifumo na inazuia mitambo. CH 149
33. Ikiwa wagonjwa wangeelimishwa kutumia mimea, hawatakufa kama vile dawa za kulevya. 308
34. Kuelewa utumiaji sahihi wa mimea na mizizi inamaanisha hakuna haja ya daktari. 306
35. Matumizi ya mimea huafikiana na zoezi la imani.HL 305
36. Njia ya kweli ya kuponya wagonjwa ni kutumia mimea (herbs). HL 310
38. Chakula cha nyama na samaki, huunda magonjwa. KK 1: 1112
38. Wale walioongoka nusu-nusu kwenye ulaji wa nyama wataliacha kanisa. Ch 575
39. Dhima ya magonjwa ni mara 10 zaidi kwa wale wanaokula nyama, HL 62
40, kula nyama ni sababu ya moja kwa moja ya magonjwa. 2 SM 418-9

41. Wafanyakazi wa kimishenari wa tiba wanatoa wito wa mwisho. UT 71
42. Ufahamu wa kutenda haki ni dawa bora kwa mgonjwa. 502
43. Vitu vya maumbile ni matabibu wa MUNGU; walio bora kwa afya kuliko dawa za mfamasia. CH 169-170
44. Kutii sheria za asili ni njia ya moja kwa moja kwenda mbinguni CH
45. Kuna silika ya uponyaji katika zeri za mpaini, mierezi na miti ya miberoshi. 7T 77
46, Waganga wanashughulikia dawa na mgonjwa anauawa. SM 441
47. Daktari mwenye busara ataweza kugundua ugonjwa kwa kuchunguza mzizi au sababu yake. HL269
48. Mishipa ya fahamu bora, inaweza kupatikana tu kwa njia ya kujikana nafsi, na kuwa na kiasi. KK 3: 1165
49. Tiba ya maji huleta matokeo mazuri ya asili (hydrotherapia). KK 7: 938
50. Lazima tuwe na afya kamilifu au hatuwezi kumpendeza MUNGU. KK 1: 1102
51. Huzuni hupunguza nguvu muhimu na mishipa ya fahamu. KK 3: 1146
52. Mazoezi ya asubuhi katika hewa safi ni kinga dhidi ya magonjwa yote. MLT
53. Masaa yasiyo ya kawaida ya kula na kunywa hupunguza nguvu za ubongo. YT 5/3/9
54. Wengi hufa kutokana na magonjwa ambayo ni ya kufikirika kabisa. HH 171

55. MUNGU aliiondoa nyama na akawapa mana ili kuamsha nguvu za akili. KK 1: 1113
56. Kuhusu matengenezo ya afya, zezeta hawawajibiki. MM 289
57. Wokovu hauwezekani bila Matengenezo ya Afya. 137
58. Madaktari wa Kikristo hawawezi kutoza bei kubwa kama vile waganga wa kidunia. MM 125
59. Dawa za BWANA mwenyewe ni hewa, maji na jua. 228
60. Amani ya ndani, na upendo kwa MUNGU vitaimarisha akili. 2T 327

SOP Distillation of health quotations: COMPILED BY DR CALVIN DENCE and Grace Momadi-Masaka

1.If we overcome on appetite we can overcome on all else. CDF 145

2.Read the best authors on the laws of life and health. Then obey your reasoning. Gw 242

3. Eden was lost by appetite, it will be regained by overcoming on appetite. 3T 161

4. Those who sin against knowledge and rely on drugs will lose hold on life. MM224

5. Drugs have done more harm and killed more than they have helped. MM 27

6. Drug medication is to be discarded. MS 162

7. The influence of the Holy Spirit is the very best medicine for the sick. MM 12

8. The things of nature are better for health than all the drug in the world. CH 169

9.A drug is a foreign substance of a poisonous nature. SC 134

10. Disease is the penalty of violating nature's laws. CH 347

11.Prevent diseases by cleanliness and obeying the laws health. 4 SG 140

12. Diseases is an effort of nature to free the body of impurities. CH 61

13. Doing good is an excellent remedy for disease. AH 447

14. Disease never comes without a cause. 2SM 469

15. Reading the Bible and work are the best remedies for diseased bodies and minds. 2T 325

16. Fasting one or two days is better than medicine. CH 477

17. A short period of complete abstinence is he road to health. CDF 310

18. Do less cooking and eat more fruit in the natural state. 7T 134

19. Faith in Christ and obedience is the true science of healing. CH 346

20. The sooner we adopt the original plan of gardening, the sooner health will be recovered. CH 174

21. By obeying the laws of life we INSURE OUR HEALTH. CH 49

22. Outdoor life restores health. MM 231

23. The sick man's faith is dead unless he is willing to change his habits. MM 262

24, If you are in poor health, help others. AH 442

25.Rise higher in Health Reform as we near the end. CH 467

26.Anything that lessens the physical strength, enfeebles the mind. COL 346

27.Without Health Reform all hope of heaven is vain. CH 574-9

28. We will meet in heaven those for whom we have labored in health Reform. COL 373

29.There is no safety in animal products. CDF 411

30.Not one morsel of food should pass between lips between meals CH 408

31.Overeating numbs the brain and causes false hunger. 2T 212-3

32. Sugar clogs the systems and hinders the machinery. CH 149

33. If the sick were educated to use herbs, they would not die as with drugs. HL 308

34. Understanding the right use of herbs and roots means no need of doctor. HL 306

35. The use of herbs is in harmony with the exercise of faith.HL 305

36. The true method of healing the sick is to tell them about herbs. HL 310

37.A flesh diet creates diseases. BC 1:1112

38. Those half converted on meat eating will leave the church. Ch 575

39. The liability of diseases is 10 times greater by meat eaters, HL 62

40,Meat eating is a direct cause of disease. 2 SM 418-9

41. Medical missionary workers are giving the last call. UT 71

42. The consciousness of right doing is the best medicine for the sick. IT 502

43. The things of nature are GOD's physicians; better for health than drugs. CH 169-170

44.Obedience to the laws nature is a direct path to heaven CH

45. There are healing properties in the balsam of pine, cedar and fir trees. 7T 77

46, Physicians deal out drugs and the patient is murdered. SM 441

47.An intelligent physician will be able to track disease and its cause. HL 269

48.Sound nerves can only can secured through temperance. BC 3:1165

49.Water treatment bring super natural results. BC 7:938

50. We must be in perfect soundness of health or we can not please GOD. BC 1:1102

51. Grief saps the vital forces and nerves. BC 3:1146

52. Morning excercise in the fresh air is a safeguard against all disease. MLT

53. irregular hours of eating and drinking sap the brain forces. YT 5/3/9

54. Many die from disease that is wholly imaginary. HH 171

55. GOD took away flesh and gave manna in order o activate the powers of the mind. BC 1:1113

56. As for health reform, idiots are not held responsible. MM 289

57. Salvation impossible without Health Reform. 7T 137

58. Christian Physicians can not charge high prices as do the worldly physicians. MM 125

59.The LORD's own remedies are air, water and sun. MM 228

60. Inner peace and love to GOD will envigorate the intellect. 2T 327

OP Distillation of health quotations: COMPILED BY DR CALVIN DENCE and Grace Momadi-Masaka

1.If we overcome on appetite we can overcome on all else. CDF 145

2.Read the best authors on the laws of life and health. Then obey your reasoning. Gw 242

3. Eden was lost by appetite, it will be regained by overcoming on appetite. 3T 161

4. Those who sin against knowledge and rely on drugs will lose hold on life. MM224

5. Drugs have done more harm and killed more than they have helped. MM 27

6. Drug medication is to be discarded. MS 162

7. The influence of the Holy Spirit is the very best medicine for the sick. MM 12

8. The things of nature are better for health than all the drug in the world. CH 169

9.A drug is a foreign substance of a poisonous nature. SC 134

10. Disease is the penalty of violating nature's laws. CH 347

11.Prevent diseases by cleanliness and obeying the laws health. 4 SG 140

12. Diseases is an effort of nature to free the body of impurities. CH 61

13. Doing good is an excellent remedy for disease. AH 447

14. Disease never comes without a cause. 2SM 469

15. Reading the Bible and work are the best remedies for diseased bodies and minds. 2T 325

16. Fasting one or two days is better than medicine. CH 477

17. A short period of complete abstinence is he road to health. CDF 310

18. Do less cooking and eat more fruit in the natural state. 7T 134

19. Faith in Christ and obedience is the true science of healing. CH 346

20. The sooner we adopt the original plan of gardening, the sooner health will be recovered. CH 174

21. By obeying the laws of life we INSURE OUR HEALTH. CH 49

22. Outdoor life restores health. MM 231

23. The sick man's faith is dead unless he is willing to change his habits. MM 262

24, If you are in poor health, help others. AH 442

25.Rise higher in Health Reform as we near the end. CH 467

26.Anything that lessens the physical strength, enfeebles the mind. COL 346

27.Without Health Reform all hope of heaven is vain. CH 574-9

28. We will meet in heaven those for whom we have labored in health Reform. COL 373

29.There is no safety in animal products. CDF 411

30.Not one morsel of food should pass between lips between meals CH 408

31.Overeating numbs the brain and causes false hunger. 2T 212-3

32. Sugar clogs the systems and hinders the machinery. CH 149

33. If the sick were educated to use herbs, they would not die as with drugs. HL 308

34. Understanding the right use of herbs and roots means no need of doctor. HL 306

35. The use of herbs is in harmony with the exercise of faith.HL 305

36. The true method of healing the sick is to tell them about herbs. HL 310

37.A flesh diet creates diseases. BC 1:1112

38. Those half converted on meat eating will leave the church. Ch 575

39. The liability of diseases is 10 times greater by meat eaters, HL 62

40,Meat eating is a direct cause of disease. 2 SM 418-9

41. Medical missionary workers are giving the last call. UT 71

42. The consciousness of right doing is the best medicine for the sick. IT 502

43. The things of nature are GOD's physicians; better for health than drugs. CH 169-170

44.Obedience to the laws nature is a direct path to heaven CH

45. There are healing properties in the balsam of pine, cedar and fir trees. 7T 77

46, Physicians deal out drugs and the patient is murdered. SM 441

47.An intelligent physician will be able to track disease and its cause. HL 269

48.Sound nerves can only can secured through temperance. BC 3:1165

49.Water treatment bring super natural results. BC 7:938

50. We must be in perfect soundness of health or we can not please GOD. BC 1:1102

51. Grief saps the vital forces and nerves. BC 3:1146

52. Morning excercise in the fresh air is a safeguard against all disease. MLT

53. irregular hours of eating and drinking sap the brain forces. YT 5/3/9

54. Many die from disease that is wholly imaginary. HH 171

55. GOD took away flesh and gave manna in order o activate the powers of the mind. BC 1:1113

56. As for health reform, idiots are not held responsible. MM 289

57. Salvation impossible without Health Reform. 7T 137

58. Christian Physicians can not charge high prices as do the worldly physicians. MM 125

59.The LORD's own remedies are air, water and sun. MM 228

60. Inner peace and love to GOD will envigorate the intellect. 2T 327